KANISA LA MNAZARETI

# KITABU CHA MWONGOZO
## TOLEO LA

2017 – 2021

•

HISTORIA

KATIBA

UONGOZI WA KANISA

SAKRAMENTI NA MIPAKA

•

ANP
Africa Nazarene Publications

**S. L. P. 44, Florida 1710**
**Afrika Kusini**

Copyright © 2019
Church of the Nazarene, Inc.

**KISWAHILI VERSION**

Kimechapichwa na mamlaka ya
Kikao Kikuu wa Ishirini na tisa cha Kimataifa
kilichofanyika katika Orlando, Florida, U.S.A
Juni 25 –Juni 29 2017

**KAMATI YA WAHARIRI WA KIINGEREZA**
**DEAN G. BLEVINS**
**CHARLES D. CROW**
**DAVID E. DOWNS**
**PAUL W. THORNHILL**
**DAVID P. WILSON**

**KAMATI YA WATAFSIRI WA KISWAHILI**
KENNEDY NGULWA
EDSON MWANDETELE
NICHOLAS BARASA

ISBN 978-0-7977-1529-5

Kitabu hiki kilichapishwa kwa lugha ya Kingereza kwenye mada:
Manual 2017-2021, Church of the Nazarene
Hakimiliki © 2017
Hati zote Zimehifadhiwa

Toleo hili limechapishwa na Shirika la Uchapishaji la Mnazareti Afrika
Copyright © 2019
Haki zote zimehifadhiwa.

Kituo cha Idara ya Vitabu
S. L. P. O. 20025-00200
Nairobi
Kenya – Afrika Mashariki

**KATIBA YA KANISA NA AGANO LA MAADILI YA KIKRISTO**

**(Mfuatano wa 1 - 99)**

**UONGOZI WA KANISA LA MTAA**

**(Mfuatano wa 100)**

**UONGOZI WA WILAYA**

**(Mfuatano wa 200)**

**UONGOZI WA KIKAO KIKUU**

**( Mfuatano wa 300)**

**ELIMU YA JUU**

**(Mfuatano wa 400)**

**HUDUMA NA UTUMISHI WA KIKRISTO**

**(Mfuatano wa 500)**

**UTARATIBU WA UTEKELEZAJI WA NIDHAMU**

**(Mfuatano wa 600)**

**SAKRAMENTI NA UTARATIBU WA IBADA**

**(Mfuatano wa 700)**

**MIPANGO YA MKATABA NA HUDUMA ZA KATIBA/SHERIA ZA,**

**CHAMA CHA VIJANA ULIMWENGUNI,**

**MISHENI YA MNAZARETI ULIMWENGUNI NA,**

**HUDUMA ZA SHULE YA JUMAPILI ULIMWENGUNI**

**(Mfuatano wa 800)**

**MIUNDO**

**(Mfuatano wa 800)**

**NYONGEZA**

**(Mfuatano wa 900)**

# D I B A J I

"*Taarifa ya Utume* wa Kanisa la Mnazareti ni kuwafanya wanafunzi kuwa kama Kristo katika mataifa.

*Thamani Kuu* za Kanisa la Mnazareti ni kwamba sisi ni Kikristo, Utakatifu na Umisheni.

*Sifa* saba za Kanisa la Mnazareti ni Ibada yenye Maana, Mwambatano wa Thiolojia, Uinjilisti wa Moyo wa Bidii, Uanafunzi wa Kimataifa, Ujenzi wa Kanisa, Uongozi wa Mabadiliko, na Huruma yenye Madhumuni.

"Lengo la kimsingi la Kanisa la Mnazareti ni kuendeleza ufalme wa Mungu kwa kuhubiri na kufundisha utakatifu wa Kikristo kama ulivyoonyeshwa katika Maandiko Matakatifu."

"Shabaha muhimu za Kanisa la Mnazareti ni ushirika mtakatifu wa Kikristo, kuokolewa kwa wenye dhambi, utakaso kamili wa waumini, kuimarishwa kwao katika utakatifu, unyofu na nguvu za kiroho zilizodhihirika katika Kanisa la awali la Agano Jipya, pamoja na kuhubiriwa injili kwa kila kiumbe.'"(19)

Kanisa la Mnazareti linadumu kama chombo cha kuendeleza ufalme wa Mungu kwa kuhubiri na kufundisha Injili ulimwenguni kote. Utume wetu uliofafanuliwa kikamilifu ni kuhifadhi na kueneza utakatifu wa Kikristo kama ulivyoonyeshwa katika Maandiko Matakatifu, kwa kuokolewa kwa wenye dhambi, kurejeshwa kwa waliorudi nyuma, na utakaso kamili wa waumini.

Shabaha yetu ni ya kiroho, ambayo ni kufanya uinjilisti kwa kuitikia Utume Mkuu wa Bwana wetu anatuagiza "tuenende tukawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi" (Mathayo 28:19, Yohana 20:21, Marko 16:15). Tunaamini kwamba lengo au shabaha hii inaweza kufikiwa kupitia kwa mwongozo na utaratibu uliokubaliwa, kama vile mafundisho ya imani yetu, na maisha ya uadilifu na usafi, ambayo yamedhibitishwa na wakati kuwa yanafaa kwa Mkristo.

Toleo hili la *Kitabu cha Mwongozo* la 2017-2021 lina taarifa fupi ya kihistoria ya kanisa, Katiba ya kanisa inayofafanua Kanuni za Imani yetu, ufahamu wetu wa kanisa, Agano la Maadili ya Kikristo ya kuishi kitakatifu, na utaratibu wa uratibishaji na uongozi; na Agano la Maadili ya Kikristo linaloeleza mambo muhimu kuhusu jamii ya kisasa; na maongozi ya usimamizi wa kanisa la mtaa, wilaya na kuratibiwa kwa kanisa lote.

Kikao Kikuu ndicho chenye mamlaka na uwezo wa juu zaidi wa kutunga sheria na mafundisho ya imani katika Kanisa la Mnazareti. Toleo hili la Mwongozo lina maamuzi na hukumu za makasisi na wajumbe

waumini wa Kikao Kikuu cha 29, kilichokutana mjini Indianapolis, katika jimbo la Indiana nchini Marekani, tarehe 25-29, mwezi wa sita, mwaka wa 2017, na kwa hivyo lina mamlaka kama mwongozo wa kufuatwa kwa kuchukua hatua. Kwa sababu ni taarifa rasmi ya imani na mwenendo wa kanisa na unaambatana na mafundisho ya Maandiko, tunatarajia watu wetu kila mahali walipo kukubali mafundisho ya imani na miongozo na misaada ya kuishi kitakatifu iliyomo ndani. Kukosa kufanya hivyo, baada ya kukubali kuweka nadhiri za Ushirika wa Kanisa la Mnazareti, kutaharibu ushuhuda na sifa za kanisa letu, na kudhuru ushirika wa watu wanaoitwa Wanazareni.

Uongozi wa Kanisa la Mnazareti ni wa kipekee. Kiutawala, kanisa hufuata mfumo wa uwakilishi-uongozi usio wa maaskofu wala waumini peke yao. Kwa sababu waumini na makasisi wana mamlaka sawa katika majadiliano na kutunga sheria za kanisa, kuna uwezo unaohitajika kwa pande zote mbili wa kusimamia shughuli za kanisa. Tunaliona jambo hili si kama nafasi tu ya kushiriki na kuhudumu katika kanisa, bali pia kama wajibu kwa waumini na wahudumu wote.

Kujitoa na kuwa na kusudi lililo dhahiri ni muhimu. Watu werevu na wenye ufahamu, wakifuata mwenendo na utaratibu waliokubaliana, hueneza Ufalme wa Mungu haraka, na kuimarisha ushuhuda wao kwa Kristo. Kwa hivyo, ni jambo muhimu kwa washirika wetu kujifahamisha na mambo yaliyomo katika kitabu hiki cha mwongozo - yaani historia ya kanisa, mafundisho yetu, pamoja na maadili na mwenendo wa uadilifu wa Mnazareni halisi. Watakaoshika maagizo yaliyomo katika kitabu hiki watakuza utiifu na uaminifu wao kwa Mungu na kwa kanisa; na wataongeza na kuimarisha juhudi zetu za kiroho.

Tukiwa na Biblia kama Mwongozo wetu mkuu, tukiangaziwa na Roho Mtakatifu na kitabu hiki cha Mwongozo rasmi wa imani yetu, mwenendo, na uongozi, tunatazamia kuingia katika kipindi kingine kipya cha miaka minne tukiwa na furaha na imani thabiti katika Yesu Kristo.

***Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu***

EUGÉNIO R. DUARTE — GUSTAVO A. CROCKER
DAVID W. GRAVES — FILIMÃO M. CHAMBO
DAVID A. BUSIC — CARLA D. SUNBERG

# Y A L I Y O M O

**Dibaji** 4

## SEHEMU YA KWANZA

Taarifa ya Kihistoria 12

## SEHEMU YA PILI
## KATIBA YA KANISA

**Utangulizi** 21
Kanuni za Imani 21
Kanisa 29
Kanuni za Uratibishaji na Uongozi 32
Marekebisho 35

## SEHEMU YA TATU
## AGANO LA MAADILI YA KIKRISTO

A. Maisha ya Kikristo 37
B. Utakaso wa Uhai wa Binadamu 41
C. Maumbile ya Kiume na Kike na Ndoa 44
D. Uwakili wa Kikristo 48
E. Viongozi wa Kanisa 50
F. Kanuni za Utengemano 51
G. Kurekebisha Agano la Maadili ya Kikristo 51

## SEHEMU YA NNE
## UONGOZI WA KANISA

**Utangulizi** 53
**I. UONGOZI WA MTAA** 54
A. Utaratibu wa Kanisa la Mtaa, Jina, Usajili, Mali, Vizuizi, Miungano, Kubatilishwa kwa Kuratibiwa 54
B. Ushirika wa Kanisa la Mtaa 59
C. Kamati ya Kanisa la Mtaa ya Uinjilisti na Ushirika 61
D. Uhamisho wa Mshirika wa Kanisa la Mtaa 62
E. Kukatiza Ushirika wa Kanisa la Mtaa 62

F. Mikutano ya Kanisa la Mtaa 63
G. Mwaka wa Kanisa la Mtaa 66
H. Kumwita Mchungaji 66
I. Uhusiano wa Mchungaji na Kanisa 70
J. Kuchunguza Upya Uhusiano Kati ya Kanisa la Mtaa na Mchungaji 71
K. Halmashauri ya Kanisa la Mtaa 74
L. Mawakili wa Kanisa la Mtaa 81
M. Wadhamini wa Kanisa la Mtaa 82
N. Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uinjilisti za Kimataifa 82
O. Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya Kanisa la Mtaa 88
P. Shule za Malezi (Chekechea) (Kuanzishwa kupitia Shule ya Upili) ya Kanisa la Mtaa 89
Q. Misheni ya Kanisa la Mnazareti ya Kimataifa 89
R. Kizuizi cha Kuomba Pesa za Kanisa la Mtaa 90
S. Kutumiwa kwa Jina la Kanisa la Mtaa 90
T. Mashirika Yanayodhaminiwa na Kanisa 91
U. Wasaidizi katika Kanisa la Mtaa 91

**II. KIKAO CHA WILAYA**

A. Mipaka na Jina ya Wilaya 94
B. Ushirika na Wakati wa Mkutano ya Wilaya 98
C. Shughuli za Kikao cha Wilaya 99
D. Kitabu cha Matukio ya Kikao cha Wilaya 105
E. Msimamizi wa Wilaya 106
F. Katibu wa Wilaya 112
G. Mtunza Hazina wa Wilaya 113
H. Halmashauri ya Wilaya 114
I. Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu 118
J. Halmashauri ya Wilaya ya Mafunzo ya Wahudumu 120
K. Halmashauri ya Wilaya ya Uinjilisti au Mkurugenzi wa Uinjilisti 122
L. Halmashauri ya Wilaya ya Mali ya Kanisa 123
M. Kamati ya Fedha ya Kikao cha Wilaya 124
N. Kamati ya Ushauri ya Wilaya 124
O. Mkurugenzi wa Wilaya wa Huduma kwa Jeshi na Gereza 124

P. Halmashauri ya Wilaya ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa 124
Q. Huduma ya Vijana wa Wilaya ya Kimataifa 127
R. Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa ya Wilaya 128
S. Wasaidizi wa Kulipwa na Wilaya 128
T. Kubatilishwa Kuratibiwa kwa Wilaya 129

**III. KIKAO KIKUU**
A. Kazi na Uratibishaji wa Kikao Kikuu 130
B. Ushirika wa Kikao Kikuu 130
C. Mahali na Wakati wa Mkutano wa Kikao Kikuu 132
D. Vikao Maalum vya Kikao Kikuu 132
E. Kamati ya Matayarisho ya Kikao Kikuu 132
F. Shughuli za Kikao Kikuu 133
G. Wasimamizi Wakuu 134
H. Wasimamizi Wakuu Waliotunukiwa Heshima na Waliostaafu 136
I. Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu 136
J. Katibu Mkuu 138
K. Mweka Hazina Mkuu 140
L. Halmashauri Kuu 141
M. Mipango ya Malipo ya Kustaafu 148
N. Wasaidizi Wadogo wa Kanisa la Mnazareti, Wanaohusishwa 148
O. Shirika la Uchapishaji la Mnazareti 149
P. Kamati Kuu ya Hatua za Kikristo 150
Q. Kamati ya Maslahi ya Muinjilisti Aliyeitwa na Mungu 150
R. Kamati ya Halmashauri ya Masomo ya Kitaifa 151
S. Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa 151
T. Baraza la Ulimwenguni la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa Ulimwenguni 153
U. Halmashauri za Kitaifa 154
V. Jimbo 154

## SEHEMU YA TANO
## ELIMU YA JUU


I. Kanisa na Chuo/Chuo Kikuu 159
II. Shirika la Elimu ya Mnazareti Ulimwenguni 160
III. Halmashauri ya Elimu ya Kimataifa 160


## SEHEMU YA SITA
## HUDUMA NA UTUMISHI WA KIKRISTO


**I.** Mwito na Kuhitimu kwa Mhudumu 163
**II.** Namna za Huduma 164
A. Huduma ya Kiongozi-msimamizi 164
B. Huduma ya Mtumishi 166
III. Majukumu ya Huduma Huduma 166
IV. Elimu kwa Wahudumu 175
A. Misingi ya Elimu kwa Mhudumu Aliyewekwa Wakfu 175
B. Marekebisho ya Kitamaduni ya Misingi ya Elimu kwa Huduma ya Kuwekwa Wakfu 178

**V. HATI ZA KUHITIMU NA TARATIBU ZA KIHUDUMA** 179
A. Mhudumu wa Mtaa 179
B. Mhudumu Aliyepewa Hati 180
C. Shemasi 184
D. Kasisi 185
E. Kutambuliwa kwa Hati za Kuhitimu 186
F. Mhudumu Aliyestaafu 187
G. Kuhama kwa Wahudumu 188
H. Maagizo ya Jumla 189
I. Kuhifadhi, Kusimamishwa, Kujiuzulu, au Kubatilishwa kwa Hati za Kihuduma 195
J. Kurudishwa kwa Wahudumu katika Ushirika na msimamo wa kanisa 198


## SEHEMU YA SABA
## UTARATIBU WA KUTEKELEZA NIDHAMU


I. Uchunguzi wa Uwezekano wa kuwepo kwa Tendo Baya na Nidhamu ya Kanisa 205

II. Kuchukua Hatua kunapokuwa na Uwezakano wa Tendo Baya 205
III. Kuchukua Hatua kwa Tendo Baya la Mtu Mwenye Mamlaka au Wadhifa wa Kuaminiwa 206
IV. Nidhamu Yenye Ubishi ya Muumini 208
V. Nidhamu Yenye Ubishi ya Mhudumu 209
VI. Kanuni za Utaratibu 213
VII. Mahakama ya Wilaya ya Rufani 213
VIII. Mahakama Kuu ya Rufani 213
IX. Mahakama ya Jimbo ya Rufani 214
**X.** Hakikisho la Haki 214

**SEHEMU YA NANE**
**SAKRAMENTI NA MIPAKA**

I. Sakramenti 218
A. Meza ya Bwana
B. Ubatizo wa Waumini 218
C. Ubatizo wa Watoto Wachanga au Wadogo 221

II. Utaratibu 223
**A.** Kuwekwa Wakfu kwa Watoto Wachanga au Wadogo 225
B. Kupokea Rasmi Washirika wa Kanisa 225
C. Ndoa 227
D. Ibada ya Mazishi 231
E. Kutawazwa kwa Viongozi wa Kanisa 241
F. Uratibishaji wa Kanisa la Mtaa 245
G. Kuweka Kanisa Wakfu 248

**SEHEMU YA TISA**
**KATIBA ZA MAKUNDI YA KANISA**

I. Huduma ya Vijana wa Mnazareti wa Kimataifa 251
II Misheni yaMnazareti ya Kimataifa 296
III Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa 317

## SEHEMU YA KUMI
## HATI

I. Kanisa la Mtaa 330
II. Kikao Cha Wilaya 333
III. Hati za Mashtaka 334

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
## NYONGEZA

I. Viongozi Wakuu 336
II. Halmashauri na Mabaraza ya Usimamizi, na Vyuo vya Elimu 337
III. Maelekezo ya Usimamizi 342
IV. Mambo ya Kisasa ya Uadilifu na Vitendo vya Jumla 345

Faharisi Maalum ya Upitiaji tena 356
Faharisi ya Vifungo Vilivyo Wazi 359
Faharisi ya Kitabu cha Mwongozo 360

## SEHEMU YA KWANZA

# TAARIFA YA KIHISTORIA

Kanisa la Mnazareti linakiri lenyewe kuwa ni tawi la lile Kanisa la Kikristo "moja, takatifu, la kimitume ulimwenguni," likikumbatia historia ya watu wa Mungu walioandikwa katika Agano la Kale na Agano Jipya kuwa yake na kuwakumbatia watu wa Mungu wa kizazi chote, katika kudhihirisha kanisa la Kristo. Dhehebu letu linapokea imani ya karne tano za kwanza za Kikristo kama dhihirisho la imani yake. Tunatambuliwa pamoja na kanisa la kihistoria katika kuhubiri Neno, kuadhimisha sakramenti, kudumisha huduma ya imani ya kimitume na matendo na kufundisha nidhamu ya maisha na huduma inayofanana na Kristo. Dhehebu letu linatii mwito wa Kibiblia wa kuishi kitakatifu na kujitoa kamili kwa Mungu, ambapo tunatangaza kupitia thiolojia ya utakaso kamili.

Urithi wetu wa Kikristo ulipatanishwa kupitia uhuisho wa Wesley wa Mabadiliko ya Kiingereza katika karne ya kumi na sita na karne ya kumi na nane. Kupitia mahubiri ya John na Charles Wesley, watu katika Uingereza, Scotland, Jamhuri ya Ireland, na Wales waliacha dhambi na kutiwa nguvu za huduma ya Kikristo. Uhuisho huu ulibainishwa na mahubiri ya ushirika, ushuhuda, nidhamu, na makundi ya wanafunzi waaminifu inayojulikana kama "jumuiya," "madarasa" na "bendi." Alama za uhuisho wa thiolojia ya Wesley zilikuwa: Kuhesabiwa haki kwa neema kupitia imani; utakaso, na ukamilifu wa Kikristo, vivyo hivyo neema kupitia imani; na ushaidi wa Roho kwa hakikisho la neema. Mchango wa kipekee wa John Wesley ulikuwa pamoja na mkazo wa utakaso kamili kama kitendo cha Mungu cha neema kwa maisha ya Mkristo. Mikazo hii ilienezwa katika ulimwengu wote. Katika nchi ya Amerika ya Kaskazini, Kanisa la Kimethodisti la maaskofu liliratibiwa mwaka 1784 kubadilisha Bara, na kueneza Utakatifu wa kimaandiko katika Nchi hizi zote."

Mkazo wa utakaso wa Kikristo ulikuzwa katika karne ya kumi na tisa. Timothy Merritt wa Boston, Massachusetts, kule Marekani, alionyesha moyo kama mhariri wa *Mwongozo wa Ukristo Ukamilifu*. Phoebe Palmer wa Mji wa New York, katika jiji la New, York, Marekani, aliongoza Mkutano wa Jumanne wa Kuendeleza Utakatifu na akawa Mnenaji, mwandishi, na mhariri wa kutafutwa. Mwaka wa 1867 wahudumu wa Kimethodisti, John A. Wood, John Inskip na wengine, wakiwa Vineland, New Jersey, Marekani, waliratibisha mikutano ya kwanza ambayo iliendeleza utakatifu wa Kiwesley ulimwenguni kote. Kanisa la

Kimethodisti la Kiwesley, Free Methodist, Jeshi la Wokovu, Ancertain Mennonites, Brethren, na Quakers wote walitilia mkazo utakatifu wa Kikristo. Wainjilisti waliendeleza kazi hii hadi Ujerumani, Uingereza, Scandinavia, India, na Australia. Makanisa mapya ya utakatifu yaliibuka, ikiwemo Kanisa la Mungu la (Anderson), Indiana, Marekani. Makanisa ya kitakatifu, misheni za miji mikuu, na ushirikiano wa kimishenari ilikua katika njia hii. Kanisa la Mnazareti lilizaliwa kutokana na mvuto wa kuunganisha mengi ya haya madhehebu katika kanisa moja takatifu.

## Umoja katika Utakatifu

Fred Hillery aliweka wakfu Kanisa la Kiinjilisti la (Providence, Rhode Island, Marekani) katika mwaka 1887. Kanisa la Misheni (Lynn, Massachusetts, Marekani) lilifuata katika mwaka 1888. Katika mwaka wa 1890, wao pamoja na kongamano zingine nane za Uingereza Mpya walianzisha Jumuiya ya Mtakatifu wa Kiinjilisti la Central. Anna S. Hanscome aliwekwa wakfu mwaka wa 1892, mhudumu mwanamke wa kwanza kuwekwa wakfu katika ukoo wa Mnazareni. kati ya miaka ya 1894-1895, William Howard Hoople aliratibu kongamano tatu ya utakatifu katika Brooklyn, New York, Marekani, ambayo yalianzisha Jumuiya ya Makanisa ya Kipentekoste ya Marekani. Neno "Pentekoste" lilikuwa kisawe cha "Utakatifu" kwa watu hawa na waanzilishi wengine wa Mnazareti. Vikundi vya Hillery na Hoople viliungana katika mwaka wa 1896, na kuanzisha kazi katika nchi ya India mwaka wa (1899) na Cape Verde mwaka wa (1901), na mtendaji mkuu wa misheni Hiram Reynolds aliratibu kongamano katika nchi ya Canada mwaka wa (1902). Kundi hili lilifika Nova Scotia, Canada hadi Iowa, Marekani kufikia mwaka wa 1907.

Robert Lee Harris aliratibu Kanisa la Kristo la Agano Jipya huko Milan, Tennessee, Marekani katika mwaka wa 1894. Mary Lee Cagle, mjane wake, alilieneza hadi magharibi mwa Texas, Marekani, katika mwaka wa 1895. C. B. Jernigan aliratibu kanisa la kwanza la Independent Holiness Church katika Van Alstyne, Texas, Marekani, katika mwaka 1901. Makanisa haya yaliungana katika Rising Star, huko Texas, Marekani mwaka wa (1904), yakiunda Kanisa la Kristo la Utakatifu Kufikia mwaka wa 1908, kanisa lilienea kutoka Georgia, Marekani, hadi New Mexico, Marekani, likihudumia waliokataliwa na wenye mahitaji, likiwasaidia mayatima na wamama waliokosa ndoa, na na wafanyakazi wa nchi za India na Japan.

Phineas F. Bresse na Joseph P. Widney, pamoja na wengine 100, waliratibu Kanisa la Mnazareti la Los Angele, California, Marekani katika

mwaka wa 1895. Walitia mkazo kwamba Wakristo waliotakaswa kwa imani walistahili kufuata mfano wa Kristo na kuhubiri injili kwa maskini. Waliamini kwamba wakati na fedha zao zilifaa zilitolewa kwenye huduma zilizo na mfano wa Kristo kwa ajili ya wokovu wa nafsi za watu na kuwa tulizo la wahitaji. Kanisa la Mnazareti lilienea pembeni mwa ufukoni mwa magharibi ya Marekani, pamoja na kongamano zingine zikienea mashariki mwa Milima ya Rocky hadi Illinois, Marekani. Walisaidia umisheni kwa wenyeji wa Calcutta, India.

Katika mwezi wa Oktoba, mwaka wa 1907, Jumuiya ya Makanisa ya Kipentekoste ya Marekani na Kanisa la Mnazareti walikutana Chicago, Illinois, Marekani, kuanzisha utawala wa kanisa ambao uliweka sawa usimamizi pamoja na haki za kongamano. Wasimamizi walitakiwa kulea na kulinda makanisa yaliyoanzishwa, yaratibiwe na kuhimiza makanisa mapya, bali si kuingilia matendo ya uhuru ya kanisa lililoratibiwa. Wajumbe wa Kanisa Takatifu la Kristo walihusika. Mkutano Mkuu wa kwanza ulipata jina lake kutoka kwa makundi yote: Kanisa la Mnazareti la Kipentekoste. Bresee na Reynolds walichaguliwa kuwa wasimamizi wakuu.

Septemba 1908, kongamao la Pennsyvenia la Kanisa la Kikristo la Utakatifu, chini ya uongozi wa H.G Trumbaur liliungana na kanisa la Pentekoste la Mnazareti.

Katika mwezi wa Oktoba, Mkutano Mkuu wa Pili ulikutana Pilot Point, huko Texas, Marekani, pamoja na Baraza Kuu la Kanisa Takatifu la Kristo. Jumanne asubuhi, tarehe 13 Oktoba, R. B. Mitchum alipendekeza na C. W. Ruth aliunga mkono uamuzi huo: “Kwamba muungano wa makanisa mawili kwa sasa ukamilishwe.” Bresee alishinikiza juhudi ya kuendelea juu ya matokeo haya, na saa 10:40 asubuhi.., katikati ya shauku kuu, mswada wa kuunga ulikubaliwa kwa kura za pamoja.

Misheni ya Pentekoste ilianza katika Nashville, Tennessee, Marekani mwaka 1898, ikiongozwa na J.O McClurkan, ikiwaunganisha watu watakatifu kutoka Tennessee na miji inayokaribiana ya Amerika. Waliwatuma wachungaji na walimu huko Cuba, Guatemala, Mexico, na India. Katika mwaka wa 1906, George Sharpe aliondolewa kwa lazima kutoka kwa Kongamano la Kanisa la Parkhead katika Glasgow, Scotland, kwa kuhubiri imani ya Wesley ya utakatifu wa Kikristo. Kanisa la Pentekoste la Parkhead lilianzishwa, kongamano zingine yaliratibiwa, na Kanisa la Pentekoste la Scotland lilianzishwa mwaka wa 1909. Misheni ya Pentekoste na Kanisa la Pentekoste la Scotland liliungana na Kanisa la Kipentekoste la Mnazareti katika mwaka wa 1915.

Mkutano Mkuu wa Tano wa mwaka wa (1919) ulibadilisha jina rasmi la dhehebu kuwa Kanisa la Mnazareti kwa sababu maana mpya ilikuwa imeshirikiana na neno “Pentekoste.”

## Kanisa la Kimataifa

Sifa muhimu ya Kanisa la Mnazareti iliundwa na makanisa mama ambayo yaliungana kufikia mwaka wa 1915. Kulikuwa na mwelekeo mkuu kwa sifa hii. Dhehebu lilisaidia makanisa yaliyoratibiwa katika Jamhuri ya Amerika, India, Cape Verde, Cuba, Canada, Mexico, Guatemala, Japan, Argentina, Uingereza, Swaziland, China, na Peru. Kufikia mwaka wa 1930, kanisa lilifika Afrika Kusini, Syria, Palestine, Msumbiji, Barbados, na Trinidad. Viongozi wa mataifa walikuwa wa muhimu sana kwa hatua hii, kama vile wasimamizi wa wilaya V. G. Santin (Mexico), Hiroshi Kitagawa (Japan), na Samwul Bhujbal (India). Sifa hii ya kimataifa iliwekwa mkazo zaidi kupitia namna mpya.

Katika mwaka wa 1922, J. G Morrison aliwaongoza wafanyakazi wa Jumuiya ya Waumini wa Utakatifu na zaidi ya washirika 1,000 katika Dakota, Marekani, Minnesota, Amerika na Montana, Marekani, ndani ya kanisa. Robert Chung aliongoza umoja wa wachungaji wa Korea na kongamano katika Kanisa la Mnazareti mwaka wa 1930. Makanisa katika Australia chini ya uongozi wa A. A. E. Berg yaliungana mwaka wa 1945. Alfredo del Rosso aliyaongoza makanisa ya Kiitaliano katika dhehebu la Mnazareti mwaka wa 1948. Kazi ya Jumuiya ya Wamishenari wa Imani ya Hephzibah pamoja na kituo chake katika Tabor, Iowa, Marekani, iliungana na Kanisa la Mnazareti karibu mwaka wa 1950.

Misheni Takatifu ya Kimataifa, liliyoanzishwa jijini London, kule England, na David Thomas mwaka 1907, ilianzisha kazi kubwa katika nchi za kusini mwa Afrika chini ya David Jones. Katika mwaka wa 1952, Makanisa ya Misheni Takatifu ya Kimataifa huko Uingereza chini ya J. B. Maclagan na kazi katika Afrika yaliungana na Wanazareti. Mwaka wa 1955. Kanisa la Wafanyakazi wa Injili, lililoratibiwa na Frank Goff katika Ontario, Canada, mwaka wa 1918, lilijiunga na Kanisa la Mnazareti mwaka wa 1958. Watu wa Nigeria walianzisha Kanisa la Mnazareti la wenyeji katika miaka ya 1940 ikiwa chini ya uongozi wa Jeremiah U. Ekaidem, walijiunga na mwili wa kimataifa katika mwaka wa 1988.

Kanisa la Mnazareti limeendeleza mtindo wa kanisa ambao unatofautiana na hali ya Kiprotestanti. Katika mwaka wa 1976, agizo la uchunguzi lilitolewa la kuchunguza ujenzi wa baadaye wa dhehebu. Katika ripoti ya mwaka wa 1980, agizo hilo lilipendekeza kanisa *kufanywa la*

*kimataifa* kulingana na kanuni mbili. Kwanza, ilitambua kwamba makanisa ya Mnazareti na wilaya ulimwenguni yalijumuisha "ushirika wa waumini wa kimataifa ambao ulikuwa na kukubaliwa kamili ndani ya muktadha wao wa kitamaduni." Pili, agizo hili lilitambua kujitoa ambako ni sawa kwa "misheni ya kipekee ya Kanisa la Mnazareti," kwa ajil ya "kueneza utakatifu wa kimaandiko . . . [kama] kiini kikuu cha maadili yasiyopingwa ambayo yanawakilisha kutambuliwa kwa Nazareni."

Mkutano Mkuu wa mwaka wa 1980 ulikumbatia "mfanano wa thiolojia wa kimataifa" wa Kanuni za Imani, ulithibitisha umuhimu wa mafunzo ya thiolojia kwa wahudumu wote, na kuita msaada wa kutosha wa vyuo vya elimu ya thiolojia katika kila sehemu ya dunia. Uliwaonya Wanazareti juu ya ukomavu kama ushirika mtakatifu wa kimataifa miongoni mwa kazi moja ya muungano ambayo mawazo ya ukoloni ambayo iliwachunguza watu na mataifa kulingana na "nguvu na udhaifu, udhamini na upokeaji" ulitoa njia kwa "mawazo ambayo yalikubali njia mpya ya kuangalia ulimwengu: njia ambayo inatambua nguvu na usawa wa washirika wote."

**TAZAMA:** Jarida la Mkutano Mkuu wa Ishirini, Kanisa la Mnazareti, (1980): 232. Franklin Cook, Eneo la Kimataifa (1984): 49.

Kanisa la Mnazareti linao muundo wa ukuaji ambao ni wa kipekee miongoni mwa Waprotestanti. Kufikia mwaka wa 1998, nusu ya Wanazareni hawakuishi tena Marekani na Canada, na asilimia arobaini ya wajumbe katika Mkutano Mkuu wa 2001 walisema kwa lugha ya Kiingereza kama lugha yao ya pili au hawakuizungumza kabisa. Mwafrika, Eugenio Duarte kutoka nchi ya Cape Verde, alichaguliwa kama mmoja wa wasimamizi wakuu mwaka wa 2009. Katika mwaka wa 2013, Gustavo Croker kutoka Guatemala, Amerika ya Kati, alichaguliwa kama msimamizi mkuu. Katika mwaka 2017, Mwafrika mwingine, Filimao Chambo, mzaliwa wa Msumbiji, alichaguliwa kama msimamizi mkuu, na, kwa mara ya kwanza, nusu ya washirika wa Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu walikuwa watu waliozaliwa na kulelewa nje ya Marekani Kaskazini.

Kufikia mwaka wa 2017, kanisa ilikuwa na washirika milioni mbili na nusu katika wilaya 471 na zaidi ya maeneo 160 dunia nzima. Karibu asilimia 28 ya Wanazareni walikuwa Waafrika, asilimia 29 waliishi katika Latin Amerika na Caribberan, na karibu robo walishi katika Jamhuri ya Amerika na Kanada. Wilaya za Uropa za kanisa ambazo zilianzishwa zilisaidia katika njia mpya ya kuwafikia watu katika Uropa ya Mashariki, na kanisa katika Asia lilienea nje ya tamaduni na kuingia katika nchi za Korea, Japan, na India, hadi Kusini-Mashariki mwa Asia, miongoni mwa

sehemu zingine. Kufikia 2017, wilaya tatu kubwa za Mnazareti zilikuwa Asia na Afrika, na kongamano tatu kubwa zaidi katika mahudhurio ya ibada yalikuwa katika Marekani ya Kusini na Caribbean.

### Huduma za Kipekee za Mataifa

Huduma za mikakati za Nazareni zimeangazia kihistoria sehemu za uinjilisti, huduma za jumuiya, na elimu. Huduma hizi zimestawi kupitia ushirikiano wa kirafiki wa tamaduni mbalimbali za kimishenari na maelfu ya wahudumu wa mtaa na wafanyakazi wa kanisa, ambao wamefanya kanuni za Kiwesley kuwa za wenyeji miongoni mwa tamaduni zao.

*Uinjilisti.* Hiram F. Reynolds alikuwa na sifa ya kuweka mikakati katika kuanzisha huduma za tamaduni mbalimbali za Mnazareti. Wakati wa robo ya karne kama msimamizi mkuu, utetezi wake wa mara kwa mara ulisaidia kuinua misheni kuwa kipaumbele cha dhehebu. Tangu mwaka wa 1915, Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa (ambayo kabla ilijulikana kama Ushirika wa Wamama Wamishenari) imekusanya fedha na kuendeleza elimu ya umisheni katika makongamano ulimwenguni kote. Misheni za nyumbani zilikuwa sehemu muhimu ya uinjilisti wa Marekani ya Kaskazini, ambapo wamishenari wa kitaifa John Diaz (Cape Verde), Santos Elizondo (Mexico), Samuel Krikorian (Palestine), J. I. Nagamatsu (Japan), na Robert Chung (Korea) walikuwa viongozi waanzilishi. Vita vya Karne ya Kati vya Nafsi viliekeza nguvu mpya kwa uinjilisti wa dunia baada ya Vita vya pili vya Dunia. Misheni za nyumbani zilienea katika Marekani ya Kaskazini. Maeneo mapya yalifunguliwa kwenye mabara mengine. Uinjilisti wa mjini ulilazimisha kanisa kutambua tena mji mikuu kama sehemu ya msingi ya huduma katika mwaka wa 1970. Aina mpya za huduma za mjini zilianzishwa, na kanisa likachukua himizo la "Msukumo wa Miji" wa kimataifa mwaka wa 1980. Kanisa liliingia Mashariki mwa Uropa mwaka wa 1990. Wanazareni wanahusika katika uhuisho wa Afrika Mashariki na huduma kwa mataifa hadi Bangladesh, ambao tarehe 24 Machi 2010, wazee wa kanisa 193 waliwekwa wakfu kwa huduma ya ibaba moja-tukio la ajabu katika historia ya Kikristo.

*Huruma*. Wanazareni wa kwanza walishuhudia neema ya Mungu kwa kusaidia janga la njaa katika nchi ya India, na kuanzisha makao ya watoto yatima, nyumba ya wamama ya uzazi kwa mabinti na wanawake, na misheni ya mjini ambayo iliwahudumia watu wa madawa ya kulevya na wasio na makao. Katika miaka 1920, vipaumbele vya huduma ya jamii vya kanisa vilibadilishwa hadi kwa tembe, hospitali zilijengwa katika nchi za China na Swaziland, na baadaye katika nchi za India na Papua New

Guinea. Wasomi wa matibabu wa Mnazareti waliwajali wagonjwa, wakafanya upasuaji, wakawafundisha wauguzi, na kufadhili zahanati zinazo enda sehemu tofauti miongoni mwa watu maskini mno wa ulimwengu. Zahanati maalum zilianzishwa, kama vile zahanati za ugonjwa wa ukoma katika nchi za Afrika. Kuanzishwa kwa Huduma za Huruma za Mnazareti katika miaka ya 1980 kuliruhusu kiwango kikubwa cha huduma ya jamii ambayo inadumu hadi sasa, ikiwa pamoja na ufadhili, msaada wa majanga, elimu ya UKIMWI, msaada wa yatima, miradi ya maji, na ugawaji wa vyakula.


*Elimu*. Shule za Jumapili za Mnazareti na mafunzo ya Biblia mara kwa mara zimekuwa sehemu ya maisha ya kongamano na kutekeleza jukumu muhimu katika kuwafanya wanafunzi kama Kristo. Kanisa limepata hifadhi katika elimu ya msingi na lugha tangu miaka ya kwanza ya Shule ya Tumaini kwa Wasichana mjini Calcutta, iliyoanzishwa mwaka 1905. Shule za Mnazareti zinawatayarisha watu ulimwenguni kote kwa kuhusika kamili katika maisha ya jamii, uchumi na ya kidini. Vingi vya vyuo vya Mnazareti katika Jamhuri ya Amerika vilikuwa na shule za msingi na shule za sekondari hadi wakati wa karne ya 20. Waanzilishi wa Mnazareti waliwekeza umuhimu wao katika elimu ya juu, wakiamini katika mafundisho ya wachungaji na wafanyakazi wengine wa Kikristo na kuwafundisha washirika. Halmashauri ya Elimu ya Kimataifa ina orodha ya vyuo 53 vya Mnazareti vya elimu ya juu ulimwenguni kote, vikiwemo vyuo vya usanii na vyuo vikuu katika bara la Afrika, Canada, Korea, Swaziland, Trinidad, na Marekani ya Kusini, vyuo 30 vya Biblia na vyuo vya masomo mengine, shule za wauguzi katika nchi za India na Papua New Guinea, na shule za wahitimu wa thiolojia katika nchi za Australia, Costa Rica, England, Ufilipino, na Jamhuri ya Amerika.

Kanisa la Mnazareti limeenea zaidi kutoka kwa kanisa lililo na uwepo wa kitaifa hadi jamii ya waumini wa kimataifa. Kwa kufuata tamaduni ya Kiwesley, Wanazareni wanajielewa wenyewe kuwa watu ambao ni wa Misheni Takatifu ya Kikristo, na kauli mbiu ya umisheni yenye manano: "Kuwa wanafunzi walio kama Kristo katika mataifa yote."

# RAMANI YA URATIBISHAJI NA UONGOZI WA KANISA

*(Pamoja na maelezo)*

• Kanisa la Mnazareti la Kimataifa • Katiba na kanuni za Uratibishaji – Kitabu cha Mwongozo Kifungu cha 22-27 •



SEHEMU YA PILI

# KATIBA YA KANISA

## Utangulizi

## Kanuni za Imani

## Kanisa

## Kanuni za Uratibishaji na Uongozi

## Marekebisho

# UTANGULIZI KWA KATIBA YA KANISA

Ili tuweze kuhifadhi ule urithi tuliopewa na Mungu, imani ile waliopewa watakatifu, hasa mafundisho ya imani na ujuzi wa utakaso kamili kama kazi ya pili ya neema, na pia ili tuweze kushirikiana na matawi mengine ya Kanisa la Yesu Kristo kwa njia inayofaa kuendeleza ufalme wa Mungu, sisi makasisi na waumini washirika wa Kanisa la Mnazareti, kulingana na kanuni za katiba iliyotungwa na kuwekwa kati yetu kisheria, tunakubali na kuagiza yafuatayo kuwa sheria ya msingi au Katiba ya Kanisa la Mnazareti inayohusu Kanuni za Imani, Agano la Maadili ya Kikristo na Kanuni za Uratibishaji na Uongozi, kama ifuatavyo:

# KANUNI ZA IMANI

**KUMBUKA**: Maandiko yanaunga mkono Kanuni ya Imani na kuwekwa hapa kulingana na tendo la Mkutano Mkuu wa mwaka wa 1976 lakini hayo maandiko hayachukuliwi kama sehemu ya maandishi ya katiba.

## I. Mungu wa Utatu

**1.** Tunamwamini Mungu mmoja aishiye milele, Mungu asiye na kikomo, Mwenye Enzi wa ulimwengu; na kwamba Yeye pekee ndiye Mungu, muumbaji na kiongozi-msimamizi, mtakatifu kwa asili, sifa na tabia na kwa kusudi. Mungu aliye wa upendo mtakatifu na nuru ni Mungu wa Utatu katika hali yake halisi, anayedhihirika kama Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.

(Mwanzo 1; Mambo ya Walawi 19:2; Kumbukumbu la Torati 6:4-5; Isaya 5:16; 6:1-7; 40:18-31; Mathayo 3:16-17; 28:19-20, Yohana 14:6-27; 1 Wakorintho 8:6; 2 Wakorintho 13:14, Wagalatia 4:4-6; Waefeso 2:13-18; 1 Yohana 1:5; 4:8)

## II. Yesu Kristo

**2.** Tunamwamini Yesu Kristo, Nafsi ya Pili katika Utatu wa Uungu; na kwamba Yeye amekuwa daima mmoja na Baba; na kwamba alichukua asili na mwili wa mwanadamu kwa uwezo wa Roho Mtakatifu na akazaliwa na Bikira Mariamu ili asili mbili timilifu na kamilifu, yaani Uungu na ubinadamu ziunganishwe ziwe Nafsi moja yenye asili ya Mungu na asili ya mwanadamu, yaani Mungu-mtu.

Tunaamini kwamba Yesu Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, na kwamba kweli alifufuka kutoka kwa wafu na akachukua mwili Wake tena,

pamoja na vitu vyote vinavyohusika na kukamilishwa kwa asili ya mwanadamu, na alipaa mbinguni na yuko huko sasa akituombea.

(Mathayo 1:20-25; 16:15-16; Luka 1:26-35; Yohana 1:1-18; Matendo ya Mitume 2:22-36; Warumi 8:3, 32-34; Wagalatia 4:4-5; Wafilipi 2:5-11; Wakolosai 1:12-22; 1 Timotheo 6:14-16; Waebrania 1:1-5; 7:22-28; 9:24-28; 1 Yohana 1:1-3; 4:2-3, 15)

## III. Roho Mtakatifu

**3.** Tunamwamini Roho Mtakatifu, Nafsi ya Tatu katika Utatu wa Uungu, kwamba Yeye yuko daima akitenda kazi ndani ya kanisa na pia pamoja na Kanisa la Kristo, akiushawishi ulimwengu kuhusu dhambi, na kuhuisha wale wanaotubu na kuamini, akitakasa waumini, na kuwaongoza katika kweli yote kama ilivyo katika Yesu Kristo.

(Yohana 7:39; 14:15-18, 26; 16:7-15; Matendo ya Mitume 2:33; 15:8-9; Warumi 8:1-27; Wagalatia 3:1-14; 4:6; Waefeso 3:14-21; 1 Wathesalonike 4:7-8; 2 Wathesalonike 2:13; 1 Petro 1:2; 1 Yohana 3:24; 4:13)

## IV. Maandiko Matakatifu

**4.** Tunaamini kwamba maandiko matakatifu yana pumzi ya Mungu, ambayo kwayo tunaelewa vitabu 66 vya Agano Jipya na Agano la Kale, vilivyoandikwa kwa uongozi wa Roho Mtakatifu, ambavyo vinaonyesha bila makosa, mapenzi ya Mungu kwetu sisi yanayohusu mambo yote ambayo yanapasa wokovu wetu, ili chochote ambacho hakiko ndani ya Maandiko Matakatifu kisiweze kunakiliwa kama sehemu ya kanuni ya imani yetu.

(Luka 24:44-47; Yohana 10:35; 1 Wakorintho 15:3-4; 2 Timotheo 3:15-17; 1 Petro 1:10-12; 2 Petro 1:20-21)

## V. Dhambi ya Asili na Binafsi

**5.** Tunaamini kwamba dhambi iliingia ulimwenguni kupitia kuasi kwa wazazi wetu wa kwanza, na kwa ajili ya dhambi mauti ikatokea. Tunaamini kwamba kuna aina mbili za dhambi; dhambi ya asili au upotovu, na dhambi anayotenda mtu binafsi.

**5.1.** Tunaamini kwamba dhambi ya asili, au upotovu, ni kule kuharibiwa na kuchafuliwa kwa maumbile ya kizazi cha Adamu kwa sababu ambayo kila mmoja ameenda mbali na ile haki ya asili au usafi halisi waliokuwa nao wazazi wa kwanza wakati waliumbwa, hampendezi Mungu, hana uzima wa kiroho, na mwenye nia ambayo inamwelekeza kwenye uovu kila mara. Pia tunaamini kwamba dhambi ya asili huendelea kuwapo katika

maisha mapya ya mtu aliyezaliwa upya, hadi roho inapotakaswa kabisa kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu.

**5.2.** Tunaamini kwamba dhambi ya asili ni tofauti na dhambi ya kitendo kwa vile inahusu mvuto uliorithiwa kwa dhambi yenyewe kwa kuwa hakuna mtu anayewajibika au kulaumiwa hadi suluhisho takatifu limepuuzwa au kukataliwa.

**5.3.** Tunaamini kwamba dhambi ya kweli au dhambi anayotenda mtu binafsi ni tendo la hiari la linalovunja sheria ya Mungu na mtu mwenye ufahamu wa mema na mabaya. Kwa hivyo tendo hilo la hiari la kuvunja amri ya Mungu halipaswi kuchukuliwa kuwa sawa na makosa yasiyokuwa ya hiari na upungufu usioweza kuepukwa, udhaifu, au kasoro kutoka kwa viwango vya mwenendo mkamilifu ambayo ni matokeo ya dhambi ya asili. Hata hivyo, utendaji huo wa mambo bila kujua hauhusishi nia au kuitikia mambo yaliyo kinyume cha roho wa Kristo, ambayo kwa usahihi yanapaswa kuitwa dhambi za roho. Tunaamini kwamba dhambi anayotenda mtu binafsi hasa ni kuvunja amri ya upendo; na kwamba kuhusiana na Kristo dhambi inaweza kufafanuliwa kama kutaoamini.

(Dhambi ya Asili: Mwanzo 3; 6:5 Ayubu 15:14; Zaburi 51:5; Yeremia 17:9-10; Marko 7:21-23; Warumi 1:18-25; 5:12-14; 7:1-8:9; 1 Wakorintho 3:1-4; Wagalatia 5:16-25; 1 Yohana 1:7-8)

(Dhambi ya Binafsi: Mathayo 22:36-40 (pamoja na 1 Yohana 3:4); Yohana 8:34-36; 16:8-9; Warumi 3:23; 6:15-23; 8:18-24; 14:23; 1 Yohana 1:9-2:4; 3:7-10)

## VI. Upatanisho

**6.** Tunaamini kwamba Yesu Kristo, kwa mateso yake, kwa kuimwaga damu Yake, na kwa kifo chake Msalabani, alifanya upatanisho kamili kwa ajili ya kila dhambi ya mwanadamu, na kwamba upatanisho huu ndio msingi wa pekee wa wokovu, na unatosha kwa wokovu wa kila mmoja aliye wa uzao wa Adamu. Upatanisho huu unafanya kazi kwa njia ya neema kwa wokovu wa wale wasioweza kuwajibika kwa matendo yao, na kwa watoto wasiojua mema na mabaya, lakini unafanya kazi kwa wokovu wa wale waliofikia umri wa kuwajibika wakati tu wanapotubu na kuamini.

(Isaya 53:5-6,11; Marko 10:45; Luka 24:46-48; Yohana 1:29; 3:14-17; Matendo ya Mitume 4:10-12; Warumi 3:21-26; 4:17-25; 5:6-21; 1 Wakorintho 6:20; 2 Wakorintho 5:14-21; Wagalatia 1:3-4; 3:13-14; Wakolosai 1:19-23; 1 Timotheo 2:3-6; Tito 2:11-14; Waebrania 2:9; 9:11-14; 13:12; 1 Petro 1:18-21; 2:19-25; 1 Yohana 2:1-2)

## VII. Neema Tangulizi

**7.** Tunaamini kwamba neema ya Mungu kupitia Yesu Kristo imewekwa kwa watu wote bure, ikiwawezesha wale wote watakaotubu dhambi na kuwa haki, kumwamini Yesu Kristo kwa ajili ya kusamehewa na kusafishwa kutoka kwa dhambi, na kufuata matendo mema yanayopendeza na kukubalika mbele Zake. Tunaamini kwamba kuumbwa kwa wanadamu kwa mfano wa Mungu kulihusisha uwezo wa kuchagua kati ya mema na mabaya, na kwa hivyo wanadamu walifanywa viumbe wanaowajibika kimaadili; kwamba kupitia kuanguka kwa Adamu, mwanadamu aliingia katika upotovu hivyo hawawezi kugeuka na kujitayarisha wenyewe kwa nguvu zao za asili na kazi ya neema na mwito wa Mungu.

(Uungu na kuwajibika kimaadili: Mwanzo 1:26-27; 2:16-17; Kumbukumbu la Torati 28:1-2; 30:19; Yoshua 24:15; Zaburi 8:3-5; Isaya 1:8-10; Yeremia 31:29-30; Ezekieli 18:1-4; Mika 6:8; Warumi 1:19-20; 2:1-16; 14:7-12; Wagalatia 6:7-8)

(Kutoweza kwa kiasili: Ayubu 14:4; 15:14; Zaburi 14:1-4; 51:5; Yohana 3:6a; Warumi 3:10-12; 5:12-14,20a; 7:14-25)

(Neema ya bure na matendo ya imani: Ezekieli 18:25-26; Yohana 1:12-13; 3:6b; Matendo ya Mitume 5:31; Warumi 5:6-8, 18; 6:15-16, 23; 10:6-8; 11:22; 1 Wakorintho 2:9-14; 10:1-12; 2 Wakorintho 5:18-19; Wagalatia 5:6; Waefeso 2:8-10; Wafilipi 2:12-13; Wakolosai 1:21-23; 2 Timotheo 4:10a; Tito 2:11-14; Waebrania 2:1-3; 3:12-15; 6:4-6; 10:26-31; Yakobo 2:18-22; 2 Petro 1:10-11; 2:20-22)

## VIII. Toba

**8.** Tunaamini kwamba Roho wa Mungu huwapatia msaada wote wanaotubu, kwa neema, na majuto ya moyo na tumaini la rehema ili waweze kuamini, kunakoleta msamaha na maisha ya kiroho. Toba, ambayo ni mabadiliko halisi ya nia kuhusu dhambi, inayohusisha hisia ya hatia ya mtu binafsi na kugeuka kwa hiari kutoka dhambini, inadaiwa kutoka kwa watu wote ambao kwa tendo au kusudio wamekuwa wenye dhambi kinyume na Mungu. Toba, ambayo ni badiliko la dhati na halisi la nia kuhusu dhambi, linalohusisha hisia ya hatia ya mtu binafsi na kugeuka kwa hiari kutoka dhambini, inadaiwa kutoka kwa watu wote, ambao kwa tendo au kusudio wamekuwa wenye dhambi kinyume cha Mungu.

Tunaamini kwamba watu wote wanaweza kuanguka kutoka kwa neema na utume na, wasipotubu dhambi zao, wanakosa tumaini na kupotea milele. Tunaamini kwamba watu wanaohuishwa hawafai kurudi kwa dhambi lakini wanaweza kuishi katika uhusiano na Mungu usiovunjika kupitia

nguvu za Roho Mtakatifu anayeishi ndani ambaye anashuhudia pamoja na roho zetu kwamba sisi ni watoto wa Mungu.

(2 Mambo ya Nyakati 7:14; Zaburi 32:5-6; 51:1-17; Isaya 55:6-7; Yeremia 3:12-14; Ezekieli 18:30-32; 33:14-16; Marko 1:14-15; Luka 3:1-14; 13:1-5; 18:9-14; Matendo ya Mitume 2:38; 3:19; 5:31; 17:30-31; 26:16-18; Warumi 2:4; 2 Wakorintho 7:8-11; 1 Wathesalonike 1:9; 2 Petro 3:9)

## IX. Kuhesabiwa Haki, Kuhuishwa, na Kupokelewa

**9.** Tunaamini kwamba kuhesabiwa haki ni tendo la Mungu la neema na haki ambalo kwalo Mungu huwapa msamaha kamili wa hatia zote na kuwekwa huru kutokana na hukumu ya dhambi zilizotendwa, na kukubaliwa kama wenye haki, kwa wote wanaomwamini Yesu Kristo na kumpokea kama Bwana na Mwokozi wao.

**9.1.** Tunaamini kwamba kuhuishwa kiroho, au kuzaliwa upya ni ile kazi ya Mungu ya neema ambayo kwayo dhamiri au hali ya kimaadili ya muumini aliyetubu uhuishwa na kupewa uzima dhahiri wa kiroho, wenye uwezo wa kuwa na imani, upendo na utiifu.

**9.2.** Tunaamini kwamba kukubaliwa kama wana ni lile tendo la Mungu la neema ambalo kwalo muumini aliyehesabiwa haki na kuhuishwa hufanywa kuwa mtoto wa Mungu.

**9.3.** Tunaamini kwamba kuhesabiwa haki, kuhuishwa kiroho, na kufanywa wana hutendeka wakati mmoja katika ujuzi wa wale wanaomtafuta Mungu na wanapokelewa kwa imani, ikitanguliwa na toba; na kwamba kwa kazi hii na hali ya neema hushuhudiwa na Roho Mtakatifu.

(Luka 18:14; Yohana 1:12-13; 3:3-8; 5:24; Matendo ya Mitume 13:39; Warumi 1:17; 3:21-26, 28; 4:5-9, 17-25; 5:1,16-19; 6:4; 7:6; 8:1, 15-17; 1 Wakorintho 1:30; 6:11; 2 Wakorintho 5:17-21; Wagalatia 2:16-21; 3:1-14,26; 4:4-7; Waefeso 1:6-7; 2:1,4-5; Wafilipi 3:3-9; Wakolosai 2:13; Tito 3:4-7; 1 Petro 1:23; 1 Yohana 1:9; 3:1-2,9; 4;7; 5:1, 9-13,18)

## X. *Ukristo Mtakatifu* na Utakaso Timilifu

**10.** Tunaamini kwamba utakaso kamili ni ile kazi ya Mungu, ambayo hubadili waumini kuwa mfano wa Kristo. Imetiwa mfuo na Neema ya Mungu kuptia kwa Roho Mtakatifu katika utakaso wa mwanzo, au kuhuishwa (iliyo sawa na kuhesabiwa haki), utakaso kamili, na kazi kamilifu inayoendelea ya Roho Mtakatifu akifikia kilele cha utukufu. Katika utukufu tunabadilishwa kuwa mfano wa Mwana.

Tunaamini kwamba utakaso kamili ni kile kitendo cha Mungu kinachofuatia kuhuishwa, ambapo waumini wanafanywa huru kutoka kwa

dhambi ya asili, au upotovu, na kuletwa katika hali ya kujitoa kikamilifu kwa Mungu, na kuwa na utiifu mtakatifu unaotokana na pendo lililokamilika.

Utakaso kamili hutokana na kubatizwa na kujazwa na Roho Mtakatifu, inaeleweka kwamba katika tukio moja hilo kuna kutakaswa kwa moyo kutokana na dhambi, na kukaliwa ndani yake na uwepo unaodumu wa Roho Mtakatifu, ambao humtia muumini nguvu kwa maisha na utumishi. Utakaso kamili huwezeshwa kuwepo na damu ya Yesu, na hutokea papo hapo kwa imani, na hutanguliwa na kujitoa kikamilifu; na kazi hii na hali hii ya neema hushuhudiwa na Roho Mtakatifu.

Ujuzi huu pia unajulikana kwa majina mengine yanayoeleza sehemu zake tofauti, kama vile “Ukamilifu wa Mkristo”, “upendo mkamilifu”, “usafi wa moyo”, “ubatizo na au kujazwa kwa Roho Mtakatifu”, “utimilifu wa baraka”, na “Utakatifu wa Kikristo”.

**10.1.** Tunaamini kwamba kuna tofauti dhahiri kati ya moyo safi na tabia iliyokomaa. Usafi wa moyo unapatikana papo hapo, kama tokeo la utakaso kamili; kukomaa kwa tabia ni tokeo la kukua na kuimarika katika neema.

Tunaamini kwamba neema ya utakaso kamili huwa pamoja na mvuto au msukumo wa kukua katika neema kama wanafunzi wanaofanana na Kristo. Hata hivyo, mvuto huu ni lazima ukuzwe kwa ufahamu, na mahitaji na jinsi ya kukua kiroho yashughulikiwe kwa makini pamoja kustawishwa kwa tabia na utu wetu ili tuwe kama Kristo. Bila kusudi na juhudi kama hiyo, ushuhuda wa mtu unaweza kuharibika au kudhoofika na neema yenyewe kutatizwa na hatimaye kupotea.

(Yeremia 31:31-34; Ezekieli 36:25-27; Malaki 3:2-3; Mathayo 3:11-12; Luka 3:16-17; Yohana 7:37-39, 14:15-23; 17:6-20; Matendo ya Mitume 1:5; 2:1-4; 15:8-9; Warumi 6:11-13, 19; 8:1-4, 8-14; 12:1-2; 2 Wakorintho 6:14-7:1; Wagalatia 2:20, 5:16-25; Waefeso 3:14-21, 5:17-18, 25-27; Wafilipi 3:10-15; Wakolosai 3:1-17; 1 Wathesalonike 5:23-24; Waebrania 4:9-11, 10:10-17, 12:1-2, 13:12; 1 Yohana 1:7,9)

(“Ukamilifu wa Kikristo” na “Pendo kamilifu”: Kumbukumbu la Torati 30:6; Mathayo 5:43-48, 22:37-40; Warumi 12:9-21; 13:8-10; 1 Wakorintho 13; Wafilipi 3:10-15; Waebrania 6:1; 1 Yohana 4:17-18)

(“Usafi wa Moyo”: Mathayo 5:8; Matendo ya Mitume 15:8-9; 1 Petro 1:22; 1 Yohana 3:3)

(“Ubatizo wa Roho Mtakatifu”: Yeremia 31:31-34; Ezekieli 36:25-27; Malaki 3:2-3; Mathayo 3:11-12; Luka 3:16-17; Matendo ya Mitume 1:5,2:1-4, 15:8-9)

(“Utimilifu wa Baraka”: Warumi 15:29)

(“Utakatifu wa Mkristo”: Mathayo 5:1-7:29; Yohana 15:1-11; Warumi 12:1-15:3; 2 Wakorintho 7:1; Waefeso 4:17-5:20; Wafilipi 1:9-11; 3:12-15; Wakolosai 2:20-3:17; Wathesalonike 3:13, 4:7-8, 5:23; 2 Timotheo 2:19-222; Waebrania 10:19-25, 12:14; 13:20-21; 1 Petro 1:15-16; 2 Petro 1:1-11, 3:18; Yuda 20-21)

## XI. Kanisa

**11.** Tunaamini katika Kanisa, jamii ya wale wanaomkiri Yesu Kristo kuwa Bwana, watu wa Mungu kwa agano waliofanywa upya katika Kristo, Mwili wa Kristo uliyoitwa pamoja na Roho Mtakatifu kupitia kwa Neno.

Mungu huliita Kanisa lidhihirishe maisha yake katika umoja na ushirika wa Roho Mtakatifu; katika kuabudu kupitia kwa kuhubiriwa kwa Neno, kuadhimisha sakramenti, na huduma katika jina Lake; kwa kumtii Kristo, kuishi maisha matakatifu, na kuwajibika mmoja kwa mwingine.

Utume wa Kanisa duniani ni kuendeleza kazi ya ukombozi na kupatanisha huduma ya Kristo katika nguvu za Roho. Kanisa linatimiza utume wake kwa kuwafanya wanafunzi kupitia uinjilisti, elimu, kuonyesha huruma, na kutekeleza haki, na kuwa shahidi wa ufalme wa Mungu.

Kanisa ni ukweli halisi katika historia ambalo linajiratibu lenyewe kulingana na hali za utamaduni zinazofaa, linadumu kama kongamano la mtaa na kama mwili wa Kristo ulimwenguni, na pia hutenga watu walioitwa na Mungu kwa huduma maalum. Mungu analiita Kanisa kukaa chini ya utawala wake likitarajia kukamilishwa kwa mambo yote wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo.

(Kutoka 19:3; Yeremia 31:33; Mathayo 8:11, 10:7, 16:13-19, 24; 18:15-20; 28:19-20; Yohana 17:14-26, 20:21-23; Matendo ya Mitume 1:7-8, 2:32-47, 6:1-2, 13:1, 14:23; Warumi 2:28-29; 4:16; 10:9-15; 11:13-32; 12:1-8; 15:1-3; 1 Wakorintho 3:5-9; 7:17; 11:1; 17-33; 12:3; 12-31; 14:26-40; 2 Wakorintho 5:11-6:1; Wagalatia 5:6; 13-14; 6:1-5, 15; Waefeso 4:1-17; 5:25-27; Wafilipi 2:1-16; 1 Wathesalonike 4:1-12, 1 Timotheo 4:13; Waebrania 10:19-25; 1 Petro 1:1-2,13; 2:4-12, 21; 4:1-2, 10-11; 1 Yohana 4:17; Yuda 24; Ufunuo 5:9-10)

## XII. Ubatizo

**12.** Tunaamini kwamba ubatizo wa Kikristo, ambao umeamriwa na Bwana wetu, ni sakramenti ambayo ni ishara ya kukubali manufaa ya upatanisho na kushirikishwa katika mwili wa Kristo. Ubatizo ni njia ya neema inayotangaza imani katika Yesu Kristo kuwa Mwokozi. Ubatizo unafanyiwa kwa waumini kudhihirisha kusudio lao kamili ya utiifu katika utakatifu na haki. Kama wahusika katika agano jipya, watoto wadogo na wale wasio na hatia wanaweza kubatizwa kwa ombi kutoka kwa wazazi wao au wasimamizi. Kanisa linaweza kutoa hakikisho la mafunzo ya

Kikristo. Ubatizo unazaweza kufanywa kwa kunyunyiziwa, kumwagiwa maji au kuzamishwa ndani ya maji.

(Mathayo 3:1-7; 28:16-20; Matendo ya Mitume 2:37-41; 8:35-39; 10:44-48; 16:29-34; 19:1-6; Warumi 6:3-4; Wagalatia 3:26-28; Wakolosai 2:12; 1 Petro 3:18-22)

## XIII. Meza ya Bwana

**13.** Tunaamini kwamba Chakula cha Ushirika kilichoanzishwa na Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo ni sakramenti, inayotangaza maisha Yake, mateso, kifo cha dhabihu, ufufuo, na tumaini la kuja Kwake kwa mara ya pili. Meza ya Bwana ni njia ya neema ambapo Kristo anawakilishwa na Roho. Watu wote wamealikwa kushiriki kwa imani katika Kristo na kufanywa upya katika maisha, wokovu, na umoja kama Kanisa. Watu wote wanastahili kuja kwa shukrani za heshima za umuhimu wake, na hivyo kuonyesha kifo cha Bwana hadi atakaporudi. Wale walio na imani katika Kristo na upendo kwa wateule wamealikwa na Kristo kushiriki mara kwa mara kama vile inavyowezekana.

(Kutoka 12:1-14; Mathayo 26:26-29; Marko 14:22-25; Luka 22:17-20; Yohana 6:28-58; 1 Wakorintho 10:14-21, 11:23-32)

## XIV. Uponyaji wa Kimungu

**14.** Tunaamini katika mafundisho ya kibiblia ya uponyaji wa kimungu na kuwahimiza watu wetu kutoa maombi ya imani kwa uponyaji wa walio wagonjwa. Pia tunaamini kwamba Mungu anaponya kwa njia ya matibabu ya kisasa.

(2 Wafalme 5:1-19; Zaburi 103:1-5; Mathayo 4:23-24; 9:18-35; Yohana 4:46-54; Matendo ya Matendo 5:12-16; 9:32-42; 14:8-15; 1 Wakorintho 12:4-11; 2 Wakorintho 12:7-10; Yakobo 5:13-16)

## XV. Kuja kwa Pili kwa Kristo

**15.** Tunaamini kwamba Bwana Yesu Kristo atarudi tena; na kwamba sisi tulio hai wakati wa kuja Kwake hatutawatangulia wale waliolala katika Kristo Yesu; lakini ikiwa tutakuwa tunakaa ndani ya Kristo, tutanyakuliwa pamoja na watakatifu watakaokuwa wamefufuliwa ili kumlaki Bwana angani, na hivyo tutakaa pamoja na Bwana milele.

(Mathayo 25:31-46; Yohana 14:1-3; Matendo ya Mitume 1:9-11; Wafilipi 3:20-21; 1 Wathesalonike 4:13-18; Tito 2:11-14; Waebrania 9:26-28; 2 Petro 3:3-15; Ufunuo 1:7-8; 22:7-20)

### XVI. Ufufuo, Hukumu, na Kiama

**16.** Tunaamini katika ufufuo wa wafu, kwamba miili ya wenye haki na wasio haki itafufuliwa na kuunganishwa na roho zao- "wale waliofanya mema, kwa ufufuo wa uzima; na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu."

**16.1.** Tunaamini katika hukumu ya siku zijazo ambapo kila mtu atasimama mbele za Mungu ili ahukumiwe kulingana na matendo yake wakati wa uhai huu.

**16.2.** Tunaamini kwamba maisha ya utukufu na uzima wa milele yamehakikishiwa wote ambao wanamwamini kwa wokovu, na kumfuata kwa utiifu, Yesu Kristo Bwana wetu; na kwamba mwishoni wale wasiotubu dhambi zao watateseka milele jehanamu.

(Mwanzo 18:25; 1 Samweli 2:10; Zaburi 50:6; Isaya 26:19; Danieli 12:2-3; Mathayo 25:31-46; Marko 9:43-48; Luka 16:19-31; 20:27-38; Yohana 3:16-18; 5:25-29; 11:21-27 Matendo ya Matendo 17:30-31; Warumi 2:1-16; 14:7-12; 1 Wakorintho 15:12-58; 2 Wakorintho 5:10; 2 Wathesalonike 1:5-10; Ufunuo 20:11-15; 22:1-15)

## KANISA

### I. Kanisa la Waumini Wote

**17**. Kanisa la Mungu linajumuisha wote waliohuishwa kiroho ambao majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima mbinguni.

### II. Makanisa Moja Moja

**18.** Makanisa moja moja yanajumlisha watu waliohuishwa kiroho kama kwa ruhusa ya kiuungu, kwa maongozi ya Roho Mtakatifu, ambao hukutana pamoja kwa ushirika na huduma takatifu.

### III. Kanisa la Mnazareti

**19.** Kanisa la Mnazareti linajumlisha watu wale ambao kwa hiari yao wenyewe hujijumuisha pamoja kulingana na mafundisho na maongozi ya kanisa hilo, na ambao hutafuta ushirika mtakatifu wa Kikristo, kuokolewa kwa wenye dhambi, utakaso kamili wa waumini, kujengwa kwao katika utakatifu, unyoofu na nguvu zilizodhihirika katika Kanisa la kale la Agano Jipya, pamoja na kuhubiriwa Injili kwa kila kiumbe.

### IV. Taarifa Iliyokubaliwa ya Imani

**20.** Kwa kutambua kwamba haki na manufaa ya watu kuwa katika ushirika wa kanisa kunategemea kuhuishwa kwao, tutakachohitaji ni watu

kukiri imani inayolingana na ujuzi wa Kikristo tu. Kwa hivyo, tunaamini katika taarifa fupi zifuatazo kuwa zinatosha. Tunaamini:

**20.1.** Katika Mungu mmoja-Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

**20.2.** Tunaamini kwamba Maandiko ya Agano la Kale na Agano Jipya, yaliandikwa kwa pumzi kamili ya Mungu, yana ukweli wote unaohitajika kwa imani na maisha ya Kikristo.

**20.3.** Tunaamini kwamba wanadamu wanazaliwa wakiwa na asili ya dhambi, na kwa hiyo, wana mvuto unaomwelekeza kwenye uovu.

**20.4.** Tunaamini kwamba wale waliokataa kutubu mwisho wao ni kupotea milele bila tumaini.

**20.5.** Tunaamini kwamba upatanisho kupitia kwa Yesu Kristo ni kwa wanadamu wote; na kwamba yeyote anayetubu na kumwamini Bwana Yesu Kristo anahesabiwa haki na kuhuishwa kiroho na kuokolewa kutoka katika utawala wa dhambi.

**20.6.** Tunaamini kwamba waumini wanapaswa kutakaswa kikamilifu, kufuatia kuhuishwa kiroho, kupitia imani katika Bwana Yesu Kristo.

**20.7.** Tunaamini kwamba Roho Mtakatifu hushuhudia kuzaliwa upya na pia utakaso kamili wa waumini.

**20.8**. Tunaamini kwamba Bwana wetu Yesu Kristo atarudi, wafu watafufuliwa, na hukumu ya mwisho itafanyika.

## V. Kanuni za Kawaida

**21.** Kutambuliwa kama sehemu ya Kanisa linaloonekana ni manufaa ya baraka na jukumu takatifu la wote ambao wameokolewa kutoka kwa dhambi zao na wanatafuta ukamilifu katika Kristo Yesu. Inahitajika kwa wote wanaotaka kujiunga na Kanisa la Mnazareti, na kwa njia hiyo waenende katika ushirika nasi, kwamba waonyeshe ushahidi wa wokovu kutoka katika dhambi zao kwa kuenenda kitakatifu na kuishi maisha masafi; na kwamba watakuwa na, au wanajitahidi kupata utakaso kutoka katika kila dhambi inayokaa ndani yao. Watadhihirisha kujitoa kwao kwa Mungu:

**21.1** KWANZA. Kwa kutenda yale yanayohitajika katika Neno la Mungu, ambalo ndio sheria yetu ya imani na matendo, hii ikiwa ni pamoja na:

(1) Kumpenda Mungu kwa moyo wote, nafsi yote, nia yote, na kwa nguvu zote, na kumpenda jirani yako kama nafsi yako. (Kutoka 20:3-6; Mambo ya Walawi 19:17-18; Kumbukumbu la Torati 5:7-10; 6:4-5; Marko 12:28-31; Warumi 13:8-10)

(2) Kuwajulisha wale ambao hawajaokoka madai ya Injili, kuwaalika katika nyumba ya Bwana, na kujaribu kuwaongoza wafikie wokovu.

(Mathayo 28:19-20; Matendo ya Mitume 1:8; Warumi 1:14-16; 2 Wakorintho 5:18-20)

(3) Kuwaheshimu na kuwastahi watu wote. (Waefeso 4:32; Tito 3:2; 1 Petro 2:17; 1 Yohana 3:18)

(4) Kuwasaidia waumini wengine ambao ni wa imani hii, na kuvumiliana katika upendo. (Warumi 12:13; Wagalatia 6:2, 10; Wakolosai 3:12-14)

(5) Kujitahidi kutenda mema kwa miili na nafsi za watu; kuwalisha wenye njaa, kuwavika walio uchi, kuwatembelea wagonjwa na walio gerezani, na kuwahudumia wahitaji, kadiri ya nafasi na uwezo tunaopewa. (Mathayo 25:35-36; 2 Wakorintho 9:8-10; Wagalatia 2:10; Yakobo 2:15-16; 1 Yohana 3:17-18)

(6) Kuchangia katika kusaidia huduma na kanisa pamoja na kazi zake katika fungu la kumi na sadaka. (Malaki 3:10; Luka 6:38; 1 Wakorintho 9:14; 16:2; 2 Wakorintho 9:6-10; Wafilipi 4:15-19)

(7) Kutekeleza maagizo yote ya Mungu kwa uaminifu, na yale yapasayo neema, hii ikiwa ni pamoja na kumwabudu Mungu hadharani, (Waebrania 10:25), huduma ya Neno (Matendo ya Mitume 2:42), sakramenti ya Meza ya Bwana (1 Wakorintho 11:23-30); kuchunguza na kutafakari Maandiko (Matendo ya Mitume 17:11; 2 Timotheo 2:15; 3:14-16); kuwa na maombi na jamaa yako na maombi ya kibinafsi. (Kumbukumbu la Torati 6:6-7; Mathayo 6:6).

**21.2.** PILI. Kwa kujiepusha na uovu wa kila namna, hii ikiwa pamoja na:

(1) Kulitaja bure jina la Bwana Mungu wako. (Kutoka 20:7; Mambo ya Walawi 19:12; Yakobo 5:12.)

(2) Kukufuru au kutoheshimu siku ya Bwana kwa kufanya kazi za kawaida zisizo za lazima, na kwa njia hiyo kushiriki katika mazoea yanayokana utakatifu wake. (Kutoka 20:8-11; Isaya 58:13-14; Marko 2:27-28; Matendo ya Mitume 20:7; Ufunuo wa Yohana 1:10)

(3) Uzinzi na uasherati, kama vile kufanya mapenzi nje ya ndoa au kufanya mapenzi kabla ya kuoa au kuolewa, ulawiti au na ufiraji, au ukahaba na mwenendo au tabia inayoweza kusisimua mapenzi kwa njia isiyostahili. (Mwanzo 19:4-11; Kutoka 20:14; Mambo ya Walawi 18:22; 20:13; Mathayo 5:27-32; Warumi 1:26-27; 1 Wakorintho 6:9-11; Wagalatia 5:19; 1 Wathesalonike 4:3-7 1 Timotheo 1:10)

(4) Tabia au mazoea yanayojulikana kuwa yanaharibu au kudhuru mwili na akili. Wakristo wanapaswa kujichukua kama hekalu la Roho Mtakatifu. (Mithali 20:1; 23:1-3; 1 Wakorintho 6:17-20; 2 Wakorintho 7-1; Waefeso 5:18)

(5) Kugombana, kulipa ovu kwa ovu, kusengenya, kusingizia na kueneza uvumi unaochafua majina au sifa za watu wengine. (2 Wakorintho 12:20; Wagalatia 5:15; Waefeso 4:30-32; Yakobo 3:5-18; 1 Petro 3:9-10)

(6) Kutokuwa mwaminifu, ulaghai, udanganyifu katika ununuzi na uuzaji, ushahidi wa uwongo, na matendo mengine kama hayo ya giza. (Mambo ya Walawi 19:10-11; Warumi 12:17; 1 Wakorintho 6:7-10)

(7) Kiburi kwa ajili ya mavazi au tabia. Wafuasi wetu wanapaswa kujipamba au kuvaa mavazi ya heshima kama iwapasavyo wale wanaoukiri uchaji wa Mungu. (Mithali 29:23; 1 Timotheo 2:8-10; Yakobo 4:6; 1 Petro 3-4; 1 Yohana 2:15-17)

(8) Muziki, vitabu na magazeti, pamoja na starehe zisizoleta heshima kwa Mungu; (1 Wakorintho 10:31; 2 Wakorintho 6:14-17; Yakobo 4:4)

**21.3.** TATU. Kuwa na ushirika mwema na kanisa, bila kuwa na kinyume bali kujitoa kikamilifu kushika na kutekeleza mafundisho yake, na kujihusisha na kazi za kanisa, kama vile ushuhuda, na kuwafikia wengine. (Waefeso 2:18-22; 4:1-3, 11-16; Wafilipi 2:1-8; 1 Petro 2:9-10).

********

## KANUNI ZA URATIBISHAJI NA UONGOZI

### Kanuni ya I. Mfumo wa Uongozi

**22**. Kanisa la Mnazareti lina mfumo wa uongozi wa uwakilishi.

**22.1.** Tumekubaliana kwamba kuna vitengo vitatu vya usimamizi katika Kanisa la Mnazareti: mtaa, wilaya, makao kuu. Majimbo yanatumika kama vitengo vya usimamizi wa mikakati ya misheni na utekelezaji.

**22.2.** Tumekubaliana kwamba kuhusu umuhimu wa mamlaka ya wasimamizi ambayo yatakamilisha na kusaidia kanisa la mtaa katika kutimiza misheni yake na malengo. Usimamizi utajenga msisimko, kupeana motisha, na kutoa usimamizi na mtindo wa msaada, na kuongoza na kuhimiza uongozi wa makanisa mapya na misheni kila mahali.

**22.3.** Tumekubaliana kwamba mamlaka wanayopewa wasimamizi hayataingiliana na kitendo cha binasfi cha kanisa lililoratibiwa. Kila kanisa litafurahia haki ya kuchagua mchungaji wao, baada ya kukubaliwa kama Kikao Kikuu kitaona likiwa jambo la hekima kuanzisha. Kila kanisa pia litawachagua wajume katika mikutano mbalimbali, wasimamie fedha zao,

na kuwa na uongozi wa shughuli zote zinazohusiana na maisha na kazi yake ya mtaa.

### Kanuni ya II. Makanisa ya Mtaa

**23.** Ushirika wa kanisa la mtaa utakuwa kwa wale wote ambao wameratibiwa kuwa kanisa na viongozi wenye mamlaka ya kufanya hivyo na ambao wamepokelewa hadharani katika kanisa na wenye mamlaka ya kufanya hivyo, baada ya kukiri ujuzi wao wa wokovu, kuamini kwao kwa mafundisho yetu, na kutaka kwao kujitoa au kutii uongozi wetu. (100-107)

### Kanuni ya III. Vikao vya Wilaya

**24.** Kikao Kikuu kitaratibisha ushirika wa kanisa kuwa vikao vya wilaya, na kuruhusu uwakilishi wa idadi ya wajumbe wahudumu na waumini kama kitakavyoona kuwa ni sawa na haki, na kitaamua kuhitimu kunakohitajika kwa wawakilishi hao, mradi makasisi wote wanaohudumu watakuwa washirika wa kikao hicho.

Kikao Kikuu pia kitaamua uwezo na majukumu ya vikao vya wilaya. (200-207.6)

### Kanuni ya IV. Kikao Kikuu

**25. Jinsi Kinavyoundwa.** Kikao Kikuu kitajumuisha idadi sawa ya wajumbe wahudumu na waumini waliochaguliwa na Vikao vya Wilaya vya Kanisa la Mnazareti; wajumbe wenye ujuzi au vyeo fulani watakaochaguliwa kama Kikao Kikuu kitakavyoagiza; na wajumbe hao kama itakavyohitajika na Kikao Kikuu.

**25.1. Kuchaguliwa kwa Wajumbe.** Katika kikao cha wilaya kati ya miezi 16 ya mkutano wa Kikao Kikuu au miezi 24 katika sehemu ambazo hati za usafiri (viza) matayarisho mengine yasiyo ya kawaida yanahitajika, idadi sawa ya wahudumu na waumini kwenye Kikao Kikuu itachaguliwa kwa kura za wingi, mradi kwamba wajumbe wawe ni makasisi wanaohudumu wa Kanisa la Mnazareti. Kila wilaya ya kiwango cha tatu itakuwa na haki ya mhudumu mmoja na muumini mmoja, na wajumbe wengine wa ziada kadiri ya idadi ya washirika wake itakavyoruhusu kulingana na idadi ya wawakilishi iliyowekwa na Kikao Kikuu. Kila kikao cha wilaya kitachagua wajumbe wa kubadilishana wasiozidi idadi ya wajumbe wawili waliochaguliwa. Katika hali ambazo hati za usafiri zitakuwa tatizo, kikao cha wilaya kinaweza kuruhusu Baraza la Halmashauri ya Wilaya kuchagua wajumbe wa kubadilishana. (205.23, 301- 301.1)

**25.2. Hati za Wajumbe.** Katibu wa kila wilaya atatoa hati za kuthibitisha kuchaguliwa kwa wajumbe wawakilishi na wale wa kubadilishana mmoja mmoja waliochaguliwa kuwa wajumbe katika Kikao Kikuu, pia atatuma hati za uchaguzi huo kwa katibu mkuu wa Kanisa la Mnazareti mara tu baada ya kumalizika kwa mkutano wa kikao cha wilaya.

**25.3. Idadi ya Wanaohitajika Mkutanoni.** Idadi itakayokuwa katika Kikao chochote Kikuu kitakuwa wengi wa wajumbe waliopiga kura ambao wameandikishwa wakati wa mkutano wa Kikao Kikuu na Kamati ya Uteuzi wa Hati wa Kikao Kikuu. Baada ya idadi inayohitajika ya wajumbe kupatikana, idadi ndogo inaweza kuidhinisha maazimio ambayo yatakuwa bado hayajaidhinishwa na kufunga mkutano.

**25.4. Wasimamizi Wakuu.** Kikao Kikuu kitachagua kwa kura itakayopigwa kwa siri kutoka kati ya makasisi wa Kanisa la Mnazareti wasimamizi wakuu sita, ambao wataunda Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu. Ikiwa kutatokea nafasi yoyote katika ofisi ya msimamizi mkuu kabla ya mkutano ujao wa kikao kikuu, nafasi itachukuliwa na msimamizi mwingine atakayechaguliwa kwa theluthi mbili ya kura za Halmashauri Kuu ya Kanisa la Mnazareti. (305.2, 316)

**25.5. Viongozi Wasimamizi.** Msimamizi mkuu aliyeteuliwa na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu ndiye atakayesimamia mikutano ya kila siku ya Kikao Kikuu. Lakini ikiwa hakuna msimamizi mkuu aliyeteuliwa, au akikosa kuwepo, Kikao Kikuu kitachagua mmoja wa wajumbe wake awe msimamizi wa muda wa mikutano ya Kikao Kikuu. (300.1)

**25.6. Kanuni za Utengemano**. Kikao Kikuu kitaidhinisha kanuni za utengemano zitakazotumiwa katika usimamizi na uongozi wake, utaratibu, kamati zake na mambo mengine yote yanayohusu kutekelezwa kwa njia inayofaa kwa shughuli zake. Kikao Kikuu kitakuwa mwamuzi wa uchaguzi na kuhitimu kwa washirika wake. (300.2-300-3)

**25.7. Mahakama Kuu ya Rufani.** Kikao Kikuu kitachagua kutoka kati ya washirika wa Kanisa la Mnazareti watu waliohitimu kuendesha kazi ya Mahakama Kuu ya Rufani, na kitafafanua mamlaka na uwezo wa mahakama hiyo. (305.7)

**25.8. Mamlaka na Mipaka ya Kikao Kikuu.**

(1) Kikao Kikuu kitakuwa na uwezo na mamlaka ya kutunga sheria kwa Kanisa la Mnazareti, na kutayarisha kanuni na mwongozo kwa idara zote zinazohusiana na kanisa kwa njia yoyote, lakini kanuni na mwongozo huo usiwe unahitilafiana na katiba hii. (300, 305-305-8)

(2) Hakuna kanisa la mtaa litakalonyimwa haki ya kumwita au kumchagua mchungaji wake, mradi tu kanuni na utaratibu uliowekwa na Kikao Kikuu unazingatiwa. (115)

(3) Makanisa yote ya mtaa, viongozi wa kanisa, wahudumu, na waumini watakuwa na haki wakati wote ya kufanyiwa hukumu au uamuzi wa haki, na wasiporidhika wanaweza kukata rufani.

## MAREKEBISHO

**26.** Vifungu vya Katiba hii vinaweza kubadilishwa au kurekebishwa ikiwa theluthi mbili ya washirika wote wa Kikao Kikuu watakubali pendekezo hilo kwa kupiga kura, na likikubaliwa na theluthi mbili au zaidi ya wilaya zote za kiwango cha pili na cha tatu za Kanisa la Mnazareti. Theluthi mbili ya kupiga kura inahitajika kwa kila marekebisho ya kikao cha wilaya yoyote ya Kiwango cha Tatu au Kiwango cha Pili. Pengine Kikao Kikuu au Kiwango chochote cha tatu au Kiwango cha pili cha kikao cha wilaya kinaweza kuchukua hatua ya kupendekeza mabadiliko haya. Baada ya mabadiliko haya kukubalika kulingana na utaratibu uliowekwa, matokeo ya kura ilioyaidhinisha yatatangazwa na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu, na baada ya hapo mabadiliko au marekebisho hayo yatakuwa na nguvu na uwezo kamili.

**27**. Azimio za kubadilisha Kanuni ya Imani (vifungu vya 1-16.2) zitarejelewa na Kikao Kikuu kwa Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu kwa kurudiwa na kamati ya masomo, ikiwa ni pamoja na wanathiolojia na wahudumu waliowekwa wakfu, ambao wameteuliwa na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu ambao wanaonyesha hali ya Kanisa la ulimwengu. Kamati itatoa ripoti, na mapendekezo yoyote au azimio, kwa Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu, ambao watatoa ripoti kwa Kikao Kikuu kitakachofuata.

**SEHEMU YA TATU**

# AGANO LA MAADILI YA KIKRISTO

## MAISHA YA KIKRISTO

## UTAKATIFU WA MAISHA YA BINADAMU

## MAUMBILE YA MWANAUME NA MWANAMKE NA NDOA

## UWAKILI WA KIKRISTO

## VIONGOZI WA KANISA

## SHERIA ZA UTENGAMANO

## KUREKEBISHA AGANO LA MAADILI YA KIKRISTO

# A. Maisha ya Kikristo

**28.** Kanisa hutangaza kwa furaha habari njema kwamba watu wote waweze kukombolewa kutoka kwa dhambi na kuwa na maisha mapya katika Kristo. Kwa neema ya Mungu, sisi Wakristo tunapaswa "kuvua utu wa kale" - tabia na matendo ya kale pamoja na nia ya mwili - na "tuvae utu mpya"- yaani mwenendo mpya na mtakatifu wa maisha pamoja na nia ya Kristo. (Waefeso 4:17-24)

**28.1.** Kanisa la Mnazareti linakusudia kueleza kanuni za kibiblia kwa jamii ya kisasa njia ambayo mafundisho na kanuni za kanisa zitajulikana na kueleweka katika nchi nyingi na katika tamaduni tofauti. Tunashikilia kwamba Amri Kumi, kama zilivyothibitishwa katika mafundisho ya Agano Jipya ya Yesu Kristo, zilidhihirishwa vikamilifu na kwa kifupi katika Amri Kuu na kwamba Hotuba za Mlimani zina msingi wa elimu ya maadili ya Kikristo.

**28.2.** Pia imetambuliwa kwamba kuna uthabiti katika kuwa na nia au wazo la pamoja kuhusu dhamiri ya Kikristo kama inavyodhihirishwa na kuongozwa na Roho Mtakatifu. Kanisa la Mnazareti, kama dhihirisho la kimataifa la Mwili wa Kristo, linakubali wajibu wake wa kutafuta njia za kuonyesha wazi ushahidi wa maisha ya Kikristo ili kufikia maadili ya utakatifu. Viwango vya kihistoria vya maadili ya kanisa vimeelezwa kwa ufupi katika vifungu vifuatavyo. Maelezo hayo yanapaswa kufuatwa kwa makini kama mwongozo na msaada wa kuishi maisha ya utakatifu. Wale ambao huaribu dhamiri ya kanisa hufanya hivyo kwa uangamivu wao wenyewe na kwa kuharibu ushuhuda wa kanisa. Marekebisho ya kuambatana na utamaduni wa watu wanaohudumiwa na kanisa yatahitaji kupelekwa na kuidhinishwa na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu.

**28.3.** Kanisa la Mnazareti linaamini njia hii mpya na takatifu inahusisha mambo ya kuepukwa na matendo ya ukombozi ya upendo yatimizwe kwa sababu ya roho, akili na mwili wa majirani wetu. Uwanja mmoja wa ukombozi wa upendo unahusisha uhusiano maalum ambao Yesu alikuwa nao, na kuwaamuru wanafunzi wake kuwa nao, na maskini wa dunia hii; kwamba Kanisa Lake, linapaswa, mwanzo, kuwa kanisa nyepesi na huru kutokana na mkazo wa mali na utumiaji wa vitu kupita kiasi na, kujitoa katika kuwalinda, kuwalisha, kuvisha, kuwapa makao maskini na waliotengwa. Katika Biblia yote na katika maisha na mfano wa Yesu, Mungu anajitambulisha na kuwasaidia maskini, walidhulumiwa, na wale katika jamii ambao hawawezi kujitetea. Katika hali hiyo, nasi pia, tumeitwa katika kujitambulisha na kuingia katika umoja na maskini.

Tunatambua kwamba huduma ya huruma kwa maskini inajumlisha vitendo vya fadhili na vile vile kupambana na kutoa nafasi, usawa, na haki kwa maskini. Pia tunaamini jukumu la Mkristo kwa maskini ni jambo muhimu la maisha ya kila muumini ambaye anatafuta imani inayofanya kazi kupitia upendo. Tunaamini kwamba utakatifu wa Kikristo haufai kutenganishwa na huduma kwa maskini kwa vile inamwelekeza Mkristo kwenda zaidi ya ukamilifu wa mtu binafsi na kumweka katika jamii na ulimwengu wa haki na usawa zaidi. Kando na kuwaweka waumini mbali na mahitaji ya uchumi mbaya wa watu katika ulimwengu huu, utakatifu unatutia moyo kuweka fedha zetu katika huduma ya kuinua mahitaji kama haya na kubadilisha haja zetu kulingana na mahitaji ya wengine.

(Kutoka 23:11' Kumbukumbu la Torati 15:7; Zaburi 41:1; 82:3; Mithali 19:17; 21:13; 22:9; Yeremia 22:16; Mathayo 19:21; Luka 12:33; Matendo ya Mitume 20:35; 2 Wakorintho 9:6; Wagalatia 2:10)

**28.4.** Katika kuorodhesha mambo yanayopaswa kuepukwa, tunatambua kwamba hakuna orodha ambayo, kwa vyovyote vile, inaweza kujumuisha aina zote za uovu duniani. Kwa hivyo, ni jambo la muhimu sana kwa wafuasi wetu kutafuta kwa bidii msaada wa Roho katika kuhisi na kutambua uovu unaozidi barua ya kawaida ya sheria; tukikumbuka maonyo: "Jaribuni mambo yote; lishikeni lililo jema; na jitengeni na ubaya wa kila namna."

(1 Wathesalonike 5:21-22)

**28.5.** Viongozi wetu na wachungaji wanatarajiwa kutilia mkazo sana katika vipindi vyetu maalum kutoka kwa madhabahu yetu watafute ukweli wa kibiblia unaohitajika ambao utaimarisha ufahamu na umuhimu wa kutenganisha mema na mabaya.

**28.6.** Elimu ni muhimu sana kwa ustawi wa jamii na kiroho katika jamii. Mashirika ya elimu ya Mnazareti na vyuo, kama vile Shule za Jumapili, shule (shule za kawaida), vituo vya malezi ya watoto, vituo vya kutunza watu wazima, vyuo vya Biblia na seminari, vinatarajiwa kuwafunza watoto, vijana, na watu wazima kanuni za kibiblia na maadili yanayotakiwa katika njia ambayo mafundisho yetu yanaweza kujulikana. Utaratibu huu utakuwa badala au wa kuongezea ule unaotumika katika shule za umma. Elimu kutoka shule za umma inapaswa kuandamana na mafunzo ya utakatifu nyumbani. Wakristo wanapaswa pia kutiwa moyo

kufanya kazi katika mashirika ya umma wayashuhudie na kuyaelekeza mashirika haya kwa ufalme wa Mungu. (Mathayo 5:13-14)

**29.** Tunasisitiza kwamba mambo yafuatayo ni lazima yaepukwe:

**29.1. Starehe ambazo ni haribifu kwa maadili ya Kikristo**. Watu wetu, wote kama Wakristo binafsi na sehemu za familia za Kikristo wanatakiwa kujitawala kwa kanuni tatu. Kanuni ya kwanza ni uwakili wa Kikristo kwa wakati wa starehe. Kanuni ya pili ni kutambua wajibu wa kila Mkristo kwa kudumisha kiwango cha juu cha uadilifu katika maisha ya Kikristo. Kwa sababu tunaishi nyakati za kuchanganyikiwa na mambo ya uadilifu, jambo linalotufanya kukabiliwa na tishio la maovu ya nyakati hizi kuingia katika nyumba zetu kupitia kwa magazeti, vitabu, redio na runinga na kompyuta, ni muhimu kuchukua hatua thabiti kujikinga na mambo hayo ili kufanya nyumba zetu zisiwe za kidunia. Hata hivyo, tunasisitiza kwamba starehe zinazokubali na kuhimiza maisha matakatifu, ambayo yanathibitisha thamani za kimaandiko, na ambazo zinaendeleza utukufu wa agano la ndoa na heshima ya kipekee ya agano la ndoa, zinaweza kuthibitishwa na kuhimizwa. Hasa tunawahimiza vijana wetu kutumia vipawa vyao katika mtandao na usanii kushawishi kwa wema sehemu iliyopotoka ya tamaduni. Kanuni ya tatu ni wajibu wa kushuhudia kinyume cha fujo ya kijamii zinazomchukiza au kumkufuru Mungu, na vile vile maovu ya kijamii kama vile, vita, picha na maneno yenye matusi, ukatili, matendo ya ushirikina kama vile yalivyoonyeshwa kupitia matangazo ya kibiashara kwa njia nyingi na kusababisha kuangamiza tamasha na mambo mengine ambayo ni chukizo kwa Mungu, kama yanavyodhihirishwa na kutangazwa kwa njia nyingi katika juhudi inayojulikana kuwa inasambaza au kueneza mambo hayo. Hii inaweza kuwa ni pamoja na kujiepusha na starehe zote mbaya na mahali zinapofanyiwa na vyombo vya habari vinavyotangaza au kuinua mambo ya fujo, anasa maneno au picha za matusi pamoja na mambo ya kukufuru na uchawi, au zile zinaonyesha au kuvutia filosofia za kidunia na utafutaji wa mali kwa njia ambazo zinashusha kiwango cha Mungu cha utakatifu wa roho na maisha. Mambo hayo hudhuru kiwango cha Mungu cha utakatifu wa moyo na maisha.

Jambo linalazimisha mafundisho ya mahubiri ya viwango hivi vya maadili ya maisha ya Kikristo, na kwamba watu wetu wafundishwe kutumia ufahamu wa maombi katika kuendelea kuchagua “njia ya juu” ya kuishi kitakatifu. Kwa hivyo tunawahimiza viongozi na wachungaji wetu kutilia mkazo katika magazeti yetu na kutoka kwa mahubiri yetu kwa ukweli huu muhimu kwa vile utaendeleza kanuni ya utambuzi kati ya maovu na mema katika kupatika na kwenye mtandao.

Tunapendekeza kwamba kiwango cha maisha alichopewa John Wesley na mama yake, ambacho ni “chochote kidhoofishacho uwezo wako wa kutambua mema na mabaya, kinachodhuru dhamira yako, kinazuia hisia zako kwa Mungu, au kuondoa upendo wako wa mambo ya kiroho, chochote kinachoongeza utawala wa mwili wako juu ya mawazo yako, kitu hicho kwako ni dhambi,” kiwe ndicho ushauri wa msingi fundisho la kutambua mema na mabaya. (28.2-28.4, 926-931)

(Warumi 14:7-13;1 Wakorintho 10:31-33, Waefeso 5:1-18, Wafilipi 4:8-9; 1 Petro 1:13-17; 2 Petro 1:3-11)

**29.2. Bahati nasibu na aina nyingine za kamari, ziwe halali au zisizokuwa halali.** Kanisa linazingatia kwamba matokeo ya mwisho ya kushiriki katika aina yoyote ya kamari yanadhuru mtu binafsi na jamii kwa jumla.

(Mathayo 6:24-34; 2 Wathesalonike 3:6-13; 1 Timotheo 6:6-11; Waebrania 13:5-6; 1 Yohana 2:15-17)

**29.3. Ushirika katika makundi yaliyofungamanishwa na siri za kiapo au jamii zinazojumlishwa zinahusishwa na Chama cha siri.** Hali duni ya kidini ya makundi hayo ya siri inapunguza uzito wa umuhimu wa kujitoa kikamilifu wa Mkristo, na shughuli zake za siri huzuia ushuhuda wa Mkristo unaopaswa kuwa wazi na dhahiri. Mambo haya yatazingatiwa kulingana na aya ya 112.1 inayohusu ushirika wa kanisa.

(1 Wakorintho 1:26-31, 2 Wakorintho 6:14-7:1; Waefeso 5:11-16; Yakobo 4:4, 1 Yohana 2:15-17)

**29.4. Uchezaji dansi zinazoharibu ukuaji wa kiroho na kuvunja tabia ya uadilifu na staha inayopaswa kudumishwa.**

(Mathayo 22:36-39, Warumi 12:1-2, 1 Wakorintho 10:31-33, Wafilipi 1:9-11, Wakolosai 3:1-17)

**29.5. Utumiaji wa pombe kama kinywaji, au kupinga uuzaji wake; kushawishi, au kupigia kura, kuidhinishwa kwa sehemu za kuuzia pombe; utumiaji wa madwa ya kulevya au usafirishaji wake; utumiaji wa tumbaku katika aina yake yoyote, au usafirishaji wake.**

Katika kuangazia Maandiko Matakatifu na ujuzi wa kibinadamu juu ya matokeo ya uharibifu wa utumiaji wa pombe kama kinywaji, na katika utambuzi wa matibabu ya kisayansi kuhusu madhara makubwa ya pombe

na tumbaku kwa mwili na akili, kama jamii ya imani iliyojitoa kutafuta maisha matakatifu, msimamo wetu na mazoea ni uzuiaji kuliko kiasi. Maandiko Matakatifu yanafundisha kwamba mwili wetu ni hekalu la Roho Mtakatifu. Kwa upendo mkuu kwetu na kwa wengine, tunawasihi watu wajizuie kabisa na vileo vyote.

Zaidi ya yote, jukumu letu la Kikristo kwa kijamii linatuhimiza kutumia aina yoyote iliyo halali na inayokubalika ya kupunguza kuwepo kwa vinywaji vya pombe na tumbaku kwa matumizi mengine. Hali kubwa ya kuenea kwa matumizi mabaya ya vileo katika ulimwengu wetu inahitaji kwamba tuweke msimamo unaokuwa kama ushahidi kwa wengine. (929-931)

(Mithali 20:1; 23:29-24:2; Habakuki 2:5; 1 Wakorintho 6:9-12:19-20; Wagalatia 5:21, Waefeso 5:18)

(Ni divai usiyotiwa chachu tu unaopaswa kutumiwa katika sakramenti wakati wa Meza ya Bwana.) (515.4, 532.7, 533.2, 534.1 700)

**29.6. Matumizi ya viburudisho, madawa ya kupunguza wasiwasi, vidonge vya kulevya na vileo vingine nje ya ushauri na usimamizi wa daktari.**

Katika kuangazia dhihirisho za madawa zinazotoa hatari za vifaa kama hivi, pamoja na maonyo ya kimaandiko kuwajibika kwa uongozi wa akili na mwili, haijalishi kuhalalishwa na kuwepo kwa vifaa kama hivyo.

(Mathayo 22:37-39, 27:34, Warumi 12:1-2, 1 Wakorintho 6:19-20; 9:24-27)

## B. Utakaso wa Uhai wa Mwanadamu

**30.** Kanisa la Mnazareti linaamini katika utakatifu wa uhai wa binadamu na kujitahidi kulinda dhidi ya uaviaji wa mimba, utafiti wa wa chembechembe na shina za mbegu ya uzazi, kifo cha huruma kwa mgonjwa anayeteseka sana, na kuzuia ushauri wa madawa kwa mtu asiyejiweza au mzee.

**30.1 Utoaji Mimba kwa Kusudi.** Kanisa la Mnazareti linakubali utakatifu wa uhai wa mwanadamu kama ilivyoanzishwa na Mungu Muumbaaji na linaamini kwamba utakatifu huo unaenea mpaka kwa mtoto ambaye bado hajazaliwa. Uhai ni zawadi kutoka kwa Mungu. Uhai wote wa mwanadamu, ukiwa pamoja na uhai unaumbika ndani ya tumbo la uzazi, umeumbwa na Mungu katika mfano Wake na kwa hivyo, unapaswa kutunzwa, kuungwa mkono, na kulindwa. Kuanzia wakati wa utungaji mimba, mtoto ni mwanadamu pamoja na kila kiungu kinavyojiumba kwa

uhai wa mwanadamu, na uhai huu unaotegemea mama kwa ajili ya kukua kwake kunakoendelea. Kwa hivyo, tunaamini kwamba uhai wa mwanadamu ni lazima upewe heshima na kulindwa kuanzia wakati wa utungaji wa mimba. Tunapinga sheria zinazoruhusu utoaji wa mimba. Kwa kutambua kwamba kuna hali za matibabu ambazo ni chache, ambapo mama au mtoto ambaye hajazaliwa, au wote, hawawezi kuendelea na hali ya mimba, utoaji mimba unaweza tu kufanywa baada ya ushauri wa daktari na wa Kikristo.

Kupinga utoaji wa mimba kunakofaa ni kujitoa kwetu kuanzisha na kusaidia miradi ambayo itatoa misaada kwa kina mama na malezi kwa watoto. Tatizo la mimba isiyotakikana linahitaji jamii ya waumini (inayowakilishwa na wale tu wanaostahili kujua tatizo hilo) kujihusisha kwa kuonyesha upendo, maombi na kutoa ushauri. Katika hali kama hizo, usaidizi unaweza kuwa wa vituo vya kutoa mawaidha, makao ya kina mama wajaa wazito, na kuanzishwa au kutumiwa kwa huduma za Kikristo za kuwapokea watoto.

Kanisa la Mnazareti linatambua kwamba kufikiria kwa uharibifu wa mimba kama njia ya kukatiza mimba isiyotakikana mara nyingi hutokea kwa sababu viwango vya Kikristo vinavyohusu tabia na uhusiano wa kimapenzi kati ya mwanaume na mwanamke vinapuuzwa. Kwa hivyo kanisa linawataka watu kufuata kwa utiifu maadili ya Agano Jipya yanayohusu hali ya kimapenzi ya mwanadamu na kukabiliana na tatizo la kuharibu mimba kulingana na misingi ya Biblia inayotoa mwongozo wa kufanya maamuzi yanayohusu mambo ya uadilifu.

(Mwanzo 2:7, Kutoka 20:13; 21:12-16; 22:25; Mambo ya Walawi 18:21; Ayubu 31:15; Zaburi 22:9; 139:3-16; Isaaya 44:2, 24; 49:5; Yeremia 1:5; Luka 1:23-25; 36-45, Matendo ya Mitume 17:25; Warumi 12:1-2; 1 Wakorintho 6:16; 7:1ff; 1 Wathesolonike 4:3-6)

Kanisa la Mnazareti pia linatambua kwamba wengi wameathiriwa na mkasa wa kutoa mimba. Kila kongamano la mtaa na muumini anaombwa kutoa ujumbe wa msamaha kutoka kwa Mungu kwa kila mtu ambaye amepitia hali ya kutoa mimba. Kongamano zetu za mitaa zinapaswa kuwa jamii ya ukombozi na tumaini kwa wale wote wanaopitia machungu ya mwili, hisia, na kiroho kwa ajili ya kuangamiza mimba kwa makusudi.

(Warumi 3:22-24; Wagalatia 6:1)

**30.2. Kupandikiza na matibabu ya vinasaba.** Kanisa la Mnazareti linahimiza utumiaji wa uumbaji wa viumbe kwa njia zisizo za kimaumbile

ili kupata tiba ya vinasaba. Tunatambua kwamba tiba ya vinasaba inaweza kusaidia kuzuia na kutibu magonjwa, na kuzuia na kutibu elimumwili na kuchanganyikiwa kwa akili. Tunapinga matumizi ya uumbaji wa viumbe kwa njia zisizo za kimaumbile ambao unaendeleza dhuluma kwa jamii, kudharau hadhi ya watu, au ambayo inajaribu kutimiza ubaguzi wa jamii, utalaam, au ubora wa jamii juu wengine (udhibitihali). Tunapinga uanzishaji wa masomo ya DNA ambao matokeo yake yanaweza kuhimiza au kusaidia utoaji mimba wa mwanadamu kama njia nyingine ya kumaliza uzazi ulio hai. Katika hali zote, unyenyekevu, heshima kwa hadhi ya uhai wa mwanadamu isiyoweze kukiukwa, usawa wa mwanadamu mbele za Mungu, na kujitoa kwa rehema na haki vinafaa kusimamia uumbaji wa viumbe kwa njia zisizo za kimaumbile na tiba ya vinasaba.

**30.3. Uzazi wa Chupa/Jitihada za Kisayanzi zinazoharibu Uhai baada ya Kutungwa Mimba.** Kanisa la Mnazareti linahimiza jamii ya kisayansi kuweka jitihada ya kutafuta teknolojia ya uzazi wa chupa kutoka kwa watu wazima, misuli, kondo ya nyuma/njia ya uzazi, damu ya uzazi, vianzo vya wanyama, na viini vya uzazi visivyo vya kibinadamu. Hii ina mwisho mzuri wa kujaribu kuleta uponyaji kwa wengi, bila kwenda kinyume na utakatifu wa uhai wa binadamu. Msimamo wetu kuhusu utafiti wa uzazi wa chupa unatokana na uthibitisho kwamba kiinitete/mtoto mchanga ni mtu katika mfano wa Mungu. Kwa hivyo, tunapinga matumizi ya chembechembe za vyanzo vya uhai kutoka kwa binadamu kwa ajili ya utafiti, njia ya tiba au makusudi mengine.

Kwa kadiri ya maendeleo ya baadaye ya kisayansi yanavyoendeleza teknolojia mpya, tunaunga mkono utafiti huo ikiwa haukiuki utakatifu wa uhai wa binadamu au tabia njema, kanuni za kibiblia. Hata hivyo, tunapinga uharibifu wa viinitete vya binadamu kwa ajili ya kusudi lolote na aina yoyote ya utafiti inayoharibu uhai wa binadamu baada ya kutunga mimba. Kulingana na mtazamo huu, tunapinga matumizi ya misuli kwa kusudi lolote, kutokana na mimba iliyoharibiwa.

**30.4. Kubadilisha Maumbile.** Tunapinga ubadilishaji maumbile ya mwanadamu. Mwanadamu anathaminiwa na Mungu, ambaye alituumba kwa mfano Wake, na kubadilisha maumbile ya mwanadamu ni kumfanya awe kitu, hivyo inamnyima heshima na thamani tuliyopewa na Muumba wetu.

**30.5. Euthanasia (Pamoja na Uuaji wa Kitaalamu).** Tunaamini kwamba Euthanasia (kukatiza uhai wa mtu mahututi au mtu aliye taabani na ugonjwa usiotibika na sio tishio kwa maisha kwa kusudi la kuzima/kumaliza mateso) haiambatani na imani ya Kikristo. Hii inahusika wakati euthanasia imeombwa au imehalalishwa na mtu aliye mahututi

(euthanasia ya hiari) na wakati ambapo mtu aliye mahututi ana upungufu wa akili kutoa ombi la (euthanasia isiyo ya hiari). Tunaamini kwamba historia ya kupinga euthanasia na kanisa la Kikristo inathibitishwa na ushawishi wa Ukristo inayotoka kwa Biblia na ambayo ni kiini kwa ukiri wa Kanisa wa imani katikaYesu Kristo kama Bwana. Euthanasia inavunja ujasiri wa Mkristo ndani ya Mungu kama Bwana mtawala wa uhai na kujifanya mtawala wa uhai wake; inavunja jukumu letu kama wahudumu mbele za Mungu; inachangia mmomonyoko wa thamani ambayo Biblia inauweka juu ya uhai wa mwanadamu na jamii; inaegemeza umuhimu zaidi kwa kuhisi mateso; na inaangazia kiburi cha mwanadamu mbele ya Mungu wa neema na mtawala. Tunawahimiza watu wapinge jitihada zozote za kuhalalisha Euthanasia.

**30.6. Kuruhusu Kufa.** Wakati kifo ni dhahiri, tunaamini kwamba pengine kuondoa au kutokana na mashine kunaruhusiwa kufuatana na imani na mwenendo wa Kikristo. Msimamo huu unahusiana na watu ambao wako katika hatima na wale ambao kutumia njia za ziada za kuendeleza maisha haziwezi kurudisha afya. Tunaamini kwamba wakati kifo ni dhahiri hakuna njia katika imani ya Kikristo inayoweza kubuniwa ili kuahirisha kifo. Kama Wakristo tunaamini katika uaminifu wa Mungu na kuwa na kuwa tumaini la uzima wa milele. Hii inawawezesha Wakristo kukubaliana na kifo kama maelezo ya imani katika Kristo aliyeshinda kifo kwa niaba yetu na kukinyang'anya kifo ushindi wake.

## C. Maumbile ya Kiume na Kike na Ndoa

**31.** Kanisa la Mnazareti linachukua hisia za maumbile ya kiume na kike katika mwili wa mwanadamu kama dhihirisho la utakatifu na uzuri ambao Mungu Muumbaji alikusudia. Kwa sababu wanadamu waote wameumbwa kwa mfano wa Mungu, ni wa thamani na heshima ya juu. Kwa hivyo tunaamini kwamba maumbile ya kiume na kike yanastahili kuwa pamoja na tendo la hisia, na ni zawadi ambayo Mungu aliumba ili idhihirishe uumbaji wetu wote wa kimwili na uhusiano. Kama watu wa utakatifu, Kanisa la Mnazareti linakubali kwamba mwili wa mwanadamu una umuhimu kwa Mungu. Wakristo wameitwa na kuwezeshwa na kazi ya Roho Mtakatifu inayobadilisha na kutakasa ili kumtukuza Mungu ndani na pamoja na miili yetu. Hisia zetu, hisia za mume na mke, uwezo wetu wa kuona raha, na tamaa yetu ya kuungana na mwingine zinafanywa kulingana na sifa ya Mungu. Miili yetu ni nzuri, nzuri sana.

Tunathibitisha imani katika Mungu ambaye uumbaji ni tendo la upendo. Kuwa na ujuzi wa Mungu kama upendo mtakatifu. Tunaelewa Utatu kuwa upendo wa umoja kati ya Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Kwa hivyo,

tumeumbwa na hamu ya kuungana na wengine kwa ajili ya kuishi. Hamu hiyo inatimizwa kamili tunapoishi katika uhusiano wa maagano na Mungu, muumba, na kumpenda jirani yako kama unavyoipenda nafsi yako. Uumbaji wetu kama jamii inayoishi ni nzuri na ya urembo. Tunawakilisha mfano wa Mungu katika uwezo wetu wa kushirikiana na tamaa yetu ya kufanya hivyo. Watu wa Mungu wameumbwa kama kitu kimoja katika Kristo, jamii iliyojaa upendo na neema.

Ndani ya jamii, waumini wameitwa waishi kama washirika waaminifu wa mwili wa Kristo. Upweke miongoni mwa watu wa Mungu unastahili kuthaminiwa na kudumishwa na ushirika mkubwa wa kanisa na muungano wa watakatifu. Kuishi kama mtu peke yake ni kujihusisha, kama vile Yesu alifanya, katika uhusiano wa karibu sana wa jamii, iliyozingirwa na marafiki, ukiwakaribisha na kukaribishwa kwa meza, na kuthihirisha ushahidi wa uwaminifu.

Pia ndani ya jamii hii, tunathibitisha kwamba waumini wengine wameitwa kuolewa. Kama vile ilivyoelezewa katika Mwanzo, "mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja." (Mwanzo 2:24) Agano la ndoa, dhihirisho la agano kati ya Mungu na watu wa Mungu, sehemu ya kipekee uaminifu kati ya mume na mke, huduma isiyo na ubinafsi, na ushahidi wa kijamii. Mwanamke na mwanaume wanajitoa wazi mbele ya watu, mmoja kwa mwingine kama ushahidi kwa njia ambayo Mungu anapenda. Uhusiano wa ndani wa ndoa umekusudiwa kuthihirisha umoja wa Kristo na kanisa, kama neema ya muujiza. Pia ni kusudio la Mungu kwamba katika umoja huu mtakatifu mwanaume na mwanamke waweze kuhisi furaha na raha ya uhusiano wa ndani wa mapenzi na kutoka kwa tendo hili ya upendo wa ndani uhai mpya uweze kuingia katika ulimwengu na katika jamii ya maagano ya ulinzi. Nyumba inayotawaliwa na Kristo inafaa kuhudumu kama sehemu ya msingi wa ujenzi wa kiroho. Kanisa linapaswa kuchukua ulinzi mkubwa katika ujenzi ndoa kupitia ushauri kati ya wanajitayarisha kuoana na mafundisho ambayo yanaonyesha utakaso wa ndoa.

Hata hivyo, hadithi ya kimaandiko pia inajumlisha sura ya huzuni ya kuvunjika kwa tamaa ya mwanadamu katika Kuanguka, ikisababisha tabia ambayo inainua kiburi cha mtu vinafsi, maangamizo na kuwatumia wengine vibaya, na kuharibu njia ya tamaa ya mwanadamu. Kama wanadamu tulioanguka, tumeona uovu huu kwa kila kiwango kwa mtu binafsi na jumla. Utawala na nguvu za dunia zimetuchanganya na uongo juu ya maumbile ya kiume na kike. Tamaa yetu imetapeliwa na dhambi na tukabadilishwa kwa ndani. Tumechangia pia kwa kuvunjika kwa uumbaji

kupitia chaguo letu la kusudi la kuharibu upendo wa Mungu na kuishi kulingana na nia zetu mbali na Mungu.

Kuvunjika kwetu katika sehemu za maumbile ya kiume na kike kunachukua njia nyingi, zingine kwa sababu uchaguzi wetu na zingine kuletwa katika maisha yetu kupitia ulimwengu uliovunjika. Hata hivyo, neema ya Mungu inatosha katika udhaifu wetu, kiasi cha kutuletea ushawishi, mabadiliko, na utakaso katika maisha yetu. Kwa hivyo, ili tushinde ongezeko la kuvunjika kwa dhambi na kuweza kushuhudia uzuri na upekee wa makusudio matakatifu ya Mungu kwa miili yetu, tunaamini washirika wa mwili wa Kristo, wanaowezeshwa na Roho, wanaweza na wanapaswa kujiepusha kutoka kwa:

- **Kujihusisha katika mapenzi nje ya ndoa na njia zingine zisizoheshimu muungano wa mapenzi.** Kwa sababu tunaamini kwaba ni kusudio la Mungu kwa maumbile yetu ya kiume na ya kike kuendelezwa katika umoja wa kimaagano kati ya mwanamke mmoja na mwanaume mmoja, tunaamini kwamba mazoea haya mara nyingi huelekeza kwa kumdhulumu mwingine katika husiano. Katika hali zote, mara nyingi yanaumiza uwezo wetu wa kuingia katika uzuri na utakatifu wa ndoa ya Kikristo kikamilifu.
- **Vitendo vya mapenzi kati ya watu walio na maumbile sawa ya kiume au ya kike.** Kwa sababu tunaamini kwamba ni kusudio la Mungu kwa maumbile yetu ya kiume au ya kike kuendeleza umoja wa kimaagano kati ya mwanamke na mwanaume, tunaamini matendo ya ndani ya mapenzi ya kati ya watu walio na jinsia sawa ya kiume au ya kike ni kinyume na mapenzi ya Mungu kwa jinsia ya mwanadamu ya kiume au ya kike. Wakati mvuto wa mtu wa msenge au mvuto wa jinsia mbili unaweza kuwa na uzito na asili zinazotofautiana, na athari za mwito huu wa usafi wa maumbile kuwa na gharama, tunaamini neema ya Mungu inatosa kwa mwito kama huo. Tunatambua jukumu la ushirikiano la mwili wa Kristo kuwa wa jamii ya kukaribisha, kusamehe, na kupenda ambapo huruma, himizo, mabadiliko, na kuwajibika vinapatikana kwa wote.
- **Mahusiano ya mapenzi nje ya ndoa.** Kwa sababu tunaamini tabia hii hukiuka maagano ambayo yalifanywa mbele ya Mungu na ndani ya mwili wa Kristo, uzinzi ni tendo la ubinafsi, chaguo linaloangamiza familia, na chukizo kwa Mungu ambaye ametupenda kwa usafi na kujitoa.
- **Talaka**. Kwa sababu ndoa imekusudiwa kuwa kujitoa kwa maisha marefu, kuvunjwa kwa agano la ndoa, iwe imeanzishwa na mtu

binafsi, au kwa chaguo la mwana ndoa mmoja, inapungukiwa na makusudio mema ya Mungu. Kanisa linapaswa kuwa angalifu katika kuhifadhi muungano wa ndoa ambapo ushauri wa hekima na unaowezekana kwa neema zinahitajika kwa wale walioathiriwa na talaka.

- **Matendo kama vile ndoa ya wake wengi.** Kwa sababu tunaamini kwamba uaminifu wa kimaagano na Mungu unathihirishwa katika kujitoa kwa ndoa ya mume na mke mmoja, matendo haya huondoa kusudio la pekee na lililotengwa la uaminifu wa ndoa.

Dhambi uzinzi na kuvunjika si jambo mtu binafsi lakini linaenea kwa utaratibu na ujenzi wa ulimwengu. Kwa hivyo, kanisa linaposhuhudia ukweli wa uzuri na upekee wa makusudi matakatifu ya Mungu tunaamini pia kanisa linapaswa kujiepusha kutoka kwa na kupinga:

- **Picha za uchi katika hali zote, ambazo zinaamsha tamaa.** Ni matumizi mabaya ya watu kwa sababu ya kujinufaisha kimapenzi kwa mtu binafsi. Mazoea haya uharibu uwezo wetu wa kupenda bila vipimo.
- **Mapenzi ya nguvu ya aina yoyote, ikiwemo pamoja na ubakaji, shambulio la mapenzi, kudhulumiwa kimapenzi, matamshi ya chukizo, dhuluma za ndoa, kujamiiana kwa ndugu wa karibu, biashara ya mapenzi, ndoa ya lazima, tohara ya wanawake, mapenzi ya kinyama, unyanyasaji wa kimapenzi, na kosa la kumwingilia kimwili msichana aliye chini ya umri unaokubalika kisheria na idadi nyingine ya watu dhaifu.** Watu wote na miundo ambayo inasababisha nguvu za kimapenzi wanavunja amri ya kumpenda na kumlinda jirani yetu. Mwili wa Kristo unafaa kila wakati kuwa sehemu ya haki, ulinzi, na uponyaji kwa wale ambao, wameathiriwa na wanaendelea kuathiriwa na nguvu za kimapnezi. Msichana wa umri wa chini anachukuliwa kama mwanadamu yeyote aliye chini ya umri wa miaka 18, isipokuwa umri wa wengi unapatikana baadaye chini ya sheria za nyumbani zilizotungwa na nchi au taifa.

Kwa hivyo tunathibitisha kwamba:

- **Mahali dhambi iko nyingi, neema inakuwa nyingi zaidi.** Ingawa madhara ya dhambi ni ya ulimwengu na jumla, umadhubuti wa neema pia ni wa ulimwengu na wa jumla. Katika Kristo, kupitia kwa Roho Mtakatifu, tunafanywa upya kwa mfano wa Mungu. Ya kale yamekwisha na mapya yakaingia. Ingawa kuundwa kwa maisha yetu kama kiumbe kipya kunaweza kuwa kwa hatua ya pole pole, uponyaji

wa Mungu ni wa kufaa katika kukabiliana na kuvunjika kwa mwanadamu katika sehemu za kimapenzi.

- **Mwili wa mwanadamu ni hekalu la Roho Mtakatifu.** Tunathibitisha hitaji la maumbile yetu ya kiume au ya kike kuambatana na mapenzi ya Mungu. Miili yetu si yetu bali imenunuliwa kwa gharama. Kwa hivyo, tumeitwa kumtukuza Mungu katika miili yetu kupitia maisha yaliyojitoa kwa utiifu.
- **Watu wa Mungu wanajulikana kwa upendo mtakatifu**. Tunathibitisha kwamba, juu ya uadilifu wote, watu wa Mungu wanapaswa kuwa na upendo. Watu wa Mungu mara nyingi wamewakaribisha watu waliovunjika katika mikutano yetu. Ukarimu kama huo wa Kikristo si jambo la uasi wa mtu binafsi au kukataa kuhusika kiukombozi katika kufahamu mizizi ya kuvunjika. Kurejesha wanadamu katika kufanana na Yesu kunahitaji kukiri, msamaha, matendo ya kuumbika, utakaso, na ushauri mtakatifu – lakini zaidi ya yote, inahusisha ukaribisho wa upendo ambao unamleta mtu aliyevunjika katika mviringo wa neema unaojulikana kama kanisa. Tukikosa kukabiliana na dhambi kwa uaminifu na moyo uliovunjika, hatujapenda. Tukikosa kupenda, hatuwezi kushiriki katika uponyaji wa Mungu wa kuvunjika.

Kanisa la kimataifa linapoendelea kupokea na kuhudumia watu wa ulimwengu wetu, kazi ya uaminifu ya maneno haya kama kongamano ni mazito na lazima yaelekezwe kwa uangalifu, unyenyekevu, ujasiri, na ufahamu.

## D. Uwakili wa Kikristo

**32. Maana ya Uwakili.** Maandiko yanafundisha kwamba Mungu ndiye anayemiliki watu wote na vitu vyote. Kwa hivyo, sisi ni mawakili Wake wa uhai na mali. Kumiliki kwa Mungu na uwakili wetu unapaswa kukiriwa, kwa vile tutawajibika binafsi mbele ya Mungu kwa kutoa hesabu ya uwakili wetu. Mungu, kama Mungu wa utaratibu na utengamano katika mambo yake yote, ameweka utaratibu wa kutoa ambao unakubali kumiliki Kwake juu ya mali ya mwanadamu na uhusiano. Hadi sasa watoto Wake wote wanapaswa kutoa zaka au sehemu ya kumi ya mapato yao pamoja na sadaka kwa uaminifu ili kutegemeza uenezaji wa injili. (140)

(Malaki 3:8-12; Mathayo 6:24-34; 25:31-46; Marko 10:17-31; Luka 12:13-24; 19:11-27; Yohana 15:1-17; Warumi 12:1-13; 1 Wakorintho 9:7-14; 2 Wakorintho 8:1-15; 9:6-15; 1 Timotheo 6:6-19; Waebrania 7:8; Yakobo 1:27; 1 Yohana 3:16-18)

**32.1. Kuleta Zaka Ghalani.** Kuleta zaka ghalani ni tendo lililoagizwa kimaandiko na kuaminifu na kila wakati kupeleka zaka kamili katika kanisa ambalo washirika wanashiriki. Kwa hivyo, fedha za kanisa zitakadiriwa kulingana na mpango wa kuleta zaka ghalani, na Kanisa la Mnazareti la mtaa ndilo litakalohesabiwa na watu wake wote kama ghala. Watu wote ambao ni sehemu ya Kanisa la Mnazareti wanasisitizwa kutoa kwa uaminifu sehemu ya kumi ya mapato yao yote kama kiwango cha chini cha wajibu wao kwa Bwana na sadaka za hiari kadiri Mungu anavyowafanikisha ili kutegemeza Kanisa kwa jumla, yaani kanisa la mtaa, wilaya, elimu, na Kanisa Kuu.

**32.2. Uchangishaji na Matumizi ya Fedha.** Kufuatana na mafundisho ya maandiko kuhusu kutoa zaka na sadaka za hiari ili kutegemeza uenezaji wa injili, na kwa kujenga majengo ya kanisa, hakuna kanisa lolote la Mnazareti linaloruhusiwa kujihusisha na aina yoyote ya kuchangisha pesa ambayo inaweza kupunguza umuhimu wa mafundisho haya, kutatanisha ujumbe wa injili, kuchafua jina la kanisa, kubagua maskini, au kuelekeza nguvu za watu wengine kinyume cha kuendeleza injili.

Katika kulipa ili kukutana na mahitaji ya kanisa la mtaa, elimu, na shughuli zote za Kanisa la Mnazareti, makanisa ya mtaa yanaombwa kukubali na kuwa na mpango wa makadirio ya fedha na kulipa kiwango walichowekewa kwa wilaya, jimbo na kanisa kuu kila mwezi. (130, 153, 154-154.2, 516.13)

**32.3. Kutegemeza Huduma**. “Vivyo hivyo Bwana ameamuru kwamba wale wanaohubiri injili wapate riziki zao kwa hiyo injili” (1 Wakorintho 9:14). Kanisa lina wajibu wa kusaidia wahudumu wake, ambao wameitwa na Mungu, na ambao, chini ya uongozi wa kanisa, wamejitoa kikamilifu kwa kazi ya kuhudumu. Kwa hivyo tunaomba kwamba washirika wa kanisa wajitoe kwa hiari katika kazi ya kuendeleza huduma kwa kukusanya fedha kila juma kugharamia kazi takatifu na kwamba msharaha wa mchungaji unapaswa kulipwa kila juma. (115.4, 115.6, 129.8)

**32.4. Zawadi za Mapato ya Urithi, Mapato Yaliyopangwa na ya Baadaye.** Ni muhimu katika kutekeleza wajibu wa uwakili wa Kikristo kwamba kufikiria kwa makini kutolewe kwa kile kitakachofanyika na mapato na mali ya mtu ambayo Bwana alimweka Mkristo kuwa wakili wakati wa uhai wake. Kanisa la Mnazareti, kwa kutambua hitaji la uwakili ulio mwaminifu katika maisha haya na maono yaliyotolewa na Mungu ya kuacha urithi wa maisha ya baadaye, limeanzisha Msingi wa Kanisa la Mnazareti wa kuongeza uwakili wa Kikristo kupitia mapato yaliyopangwa na ya baadaye. Sheria ya kiraia mara nyingi haitoi ugawaji wa makazi

katika hali ambayo inamtukuza Mungu. Kila Mkristo anapaswa kuweka umakini kwa matayarisho ya azimio na ushaidi katika hali ya uangalifu na ya kisheria, na Kanisa la Mnazareti kupitia huduma zake kadhaa za umisheni, uinjilisti, elimu, na uhisani-wa mtaa, wilaya, elimu, na kanisa kuu-unapendekezwa kwa ajili ya kujali.

**32.5. Kazi ya Kusaidiana kwa ajili ya Misheni ya Dhehebu.** Utawala wa Kanisa la Mnazareti unawakilishwa. Kila kongamano la mtaa linasaidia misheni yote ya kanisa kama vile ilivyoelezewa na Kikao Kikuu na kutekelezwa kupitia uongozi wa Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu katika ulimwengu wa uinjilisti, elimu, msaada wa huduma, na huduma za wilaya.

Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu na Halmashauri Kuu wamepewa mamlaka na uwezo wa kujenga, kurejelea, na kuhifadhi utaratibu wa kuchangisha fedha kupitia mradi wa Fedha za Uinjilisti wa Ulimwengu na kuweka malengo ya kifedha na majukumu ya makanisa ya mtaa kupitia mikutano ya wilaya.

Kulingana na aya ya 337.1, halmashauri za kitaifa na baraza la ushauri la eneo wamepewa mamlaka na uwezo wa kuanzisha mpango wa hifadhi ya kustaafu ya kuhudumu kwenye eneo lao. Ripoti ya mipango kama hiyo itatolewa katika aya ya 337.2. Kuweko kwa aya ya 32.5 hakutahusishwa kwa Halmashauri ya Kiinua mgongo na Faida Marekani.

Halmashauri ya kitaifa na baraza la ushauri la eneo pia wamepewa mamlaka na uwezo kuanzisha msaada wa vyuo vya elimu ya juu katika eneo lao.

Kila wilaya inapewa mamlaka na uwezo wa kuanzisha malengo ya fedha majukumu ya makanisa ya mtaa kwa ajili ya kuegemeza huduma ya wilaya kupitia Kamati ya Fedha ya Mkutano wa Wilaya. (238.1, 317.10, 345,346.3)

## E. Viongozi wa Kanisa

**33.** Tunaagiza makanisa yetu ya mtaa kuchagua kama viongozi wa kanisa watu ambao wanakiri ujuzi wa utakaso kamili na ambao maisha yao yanadhihirisha wazi ushahidi wa neema ya Mungu ambaye ametuita kwa uhai mtakatifu; ambao wanakubaliana na kanuni, utawala, na tabia za Kanisa la Mnazareti; na wanasaidia kanisa la mtaa kwa uwaminifu katika mahudhurio, ibada ya wazi, na zaka zao na sadaka. Viongozi wa Kanisa wanapaswa kujihusisha kikamilifu katika "kuwafanya wanafunzi kama Kristo katika taifa." (113.11, 127, 145-147)

## F. Kanuni za Utengamano

**34.** Kulingana na sheria inayotumika, Kanuni za Muungo na sheria za uongozi uliyoko katika kitabu cha Mwongozo, mikutano na shughuli za washirika wa Kanisa la Mnazareti katika mtaa, wilaya, na kanisa kuu na kamati za umoja zitaongozwa na kusimamiwa kulingana na (toleo la sasa) la *Kanuni za Utengamano za Robert lililoboreshwa* kwa ajili ya utaratibu wa Bunge. (113, 205, 300.3)

## G. Kurekebisha Agano la Maadili ya Kikristo

**35.** Kuwepo kwa Agano la Maadili ya Kikristo kunaweza kubatilishwa au kurekebishwa ikiwa jambo hilo litakubaliwa na theluthi mbili za kura za wajumbe ambao wako na kuza za Kikao Kikuu.

SEHEMU YA IV

# UONGOZI WA KANISA

## Utangulizi

## Uongozi wa Mtaa

## Uongozi  wa Wilaya

## Uongozi wa Kikao Kikuu

# UTANGULIZI KWA UONGOZI WA KANISA

Kazi ya Kanisa la Mnazareti ni kuwajulisha watu wote neema ya Mungu inayobadilisha kupitia msamaha wa dhambi na usafi wa roho katika Yesu Kristo. Utume wetu kwanza na zaidi ya yote, ni “kufanya wanafunzi kuwa kama Kristo katika mataifa,” kuwashirikisha waumini katika ushirika na ushirika wa kanisa (mkusanyiko), na kuwatayarisha (kuwafundisha) kwa ajili ya huduma wote watakaoitikia kwa imani. Lengo kuu la “jamii ya imani” ni kumleta kila mtu akiwa mtimilifu katika Kristo siku ile ya mwisho (Wakolosai 1:28).

Ni katika kanisa la mtaa ambapo wokovu, utimilifu, mafundisho na utume hufanyika. Kanisa la mtaa, ambalo ni Mwili wa Kristo, ndilo mwakilishi wa imani na utume wetu. Makanisa haya yameorodheshwa kiusimamizi katika makundi yanayounda wilaya na majimbo.

Misingi ya umoja katika Kanisa la Mnazareti ni imani yetu, uongozi wetu, maelezo, na utaratibu kama ilivyoelezwa katika *Kitabu cha mwongozo wa Kanisa la Mnazareti.*

Kiini cha umoja huu kimetajwa katika Kanuni za Imani katika *Kitabu cha Mwongozo.* Tunalitia moyo kanisa katika majimbo yote na lugha zote watafsiri na kusambaza kwa wingi, na kufundisha kanuni hizi za imani kwa waumini wetu. Huu ndiyo uzi wa dhahabu ambao unafunganisha mambo yote tufanyayo na jinsi tulivyo kama Wanazareni.

Mfano unaoonekana wa umoja huu unawakilishwa na Kikao Kikuu, ambacho ndicho chenye “uwezo wa juu zaidi wa kutunga mafundisho ya imani, sheria za kanisa, na mamlaka ya uchaguzi katika Kanisa la Mnazareti.” Mfano wa pili unaoonekana ni Halmashauri Kuu ya kimataifa ambayo inawakilisha kanisa lote.

Mfano wa tatu ni Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu, ambao wanaweza kufafanua *Kitabu cha Mwongozo*, kuidhinisha mabadiliko yatokanayo na utamaduni, na kuweka wakfu wahudumu.

Uongozi wa Kanisa la Mnazareti ni wa uwakilishi, na kwa hivyo unaepuka matatizo ya uongozi unaosimamiwa na maaskofu pekee, na ule usio na mipaka wa waumini wa kanisa.

Katika majimbo ya ulimwengu yanayohudumiwa na kanisa ambako tofauti za utamaduni na siasa zitalazimu, mabadiliko ya utaratibu wa uongozi wa kanisa la mtaa, wilaya, na jimbo ulioko katika sehemu ya IV, aya ya 100, 200, 300, yanaweza kufanywa. Maombi ya kufanya mabadiliko hayo yanapaswa kuandikwa na kupelekwa kwa Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu ili yaidhinishwe.

## I. UONGOZI WA MTAA

# KANISA LA MTAA

### A. Utaratibu wa Kanisa la Mtaa, Jina, Usajili, Mali, Vizuizi, Miungano, na Kubatilishwa kwa Kuratibiwa

**100. Utaratibu.** Makanisa ya mtaa yanaweza kuratibiwa na msimamizi wa wilaya, au msimamizi mkuu anayehusika na eneo, au kasisi aliyeruhusiwa kufanya hivyo na mmoja wa wasimamizi hao. Ripoti rasmi za makanisa mapya yaliyoratibiwa zitahitajika kuwekwa ofisi ya Katibu Mkuu kupitia ofisi ya utawala inayohusika. (23, 107, 211.1, 538.15)

**100.1. Kanisa la Misheni ambalo Halijaratibiwa.** Kazi ya Kusanyiko jipya ambalo halijaratibiwa kulingana na aya ya 100 inaweza kuandikishwa na katibu mkuu kama misheni ya Kanisa ambalo halijaratibiwa, kwa kuthibitishwa na msimamizi wa wilaya mahali ambapo kazi mpya imewekwa. Mtumishi anayehudumu katika Kanisa la misheni ambalo halijaratibiwa kama mchungaji ama mshirika atachukuliwa kama mhudumu mfanyikazi kwa kuthibitishwa na msimamizi wa wilaya. Kanisa la misheni ambalo halijasajiliwa linaweza kujumlishwa katika aya ya 102 na kupokea na kutoa ripoti ya washirika. (100.2, 107.2, 138.1, 159, 211.6)

**100.2. Kanisa Lililo na Kusanyiko Zaidi ya Moja.** Makanisa ya mtaa yaliyoratibiwa yanaweza kupanua huduma zao kwa kuanzisha madarasa ya Biblia kwa lugha mbali mbali katika majengo ya makanisa yao. Madarasa hayo ya Biblia yanaweza kustawi na kuimarika hadi yawe kanisa ambalo halijaratibiwa au kanisa ambalo limeratibiwa. Jambo hilo linaweza kusababisha kuwepo kwa zaidi ya kusanyiko moja lililo chini ya jina moja la kanisa, kwa kuidhinishwa na msimamizi wa wilaya. Katika makanisa hayo yenye kusanyiko zaidi ya moja ambapo si mikusanyiko yote iliyoratibiwa kuwa makanisa rasmi, Baraza la Halmashauri ya Wilaya, kwa idhini ya msimamizi wa wilaya na msimamizi mkuu anayehusika, anaweza kuipa mikusanyiko hiyo, haki na manufaa ya kanisa la mtaa lililoratibiwa kwa masharti yafuatayo:

1. Mikusanyiko kama hiyo haiwezi kusajiliwa au kuungwa kama kanisa tofauti mbali na kanisa la mtaa lililoratibiwa.
2. Mikusanyiko hii haitaruhusiwa kuwa na hati ya kumiliki ardhi au mali tofauti na ile ya kanisa la mtaa liliooratibiwa.

3. Mikusanyiko hiyo haitaruhusiwa kuwa na madeni bila idhini ya msimamizi wa wilaya, halmashauri ya kanisa lililoratibiwa, na Baraza la Halmashauri ya Wilaya.
4. Hakuna kusanyiko kama hilo litakaloruhusiwa kujitenga kama kundi kutoka katika kanisa la mtaa lililoratibiwa au kuvunja uhusiano wake na kanisa hilo kwa njia yoyote bila idhini ya msimamizi wa wilaya akishauriana na mchungaji wa kanisa la mtaa. (100-100.1)

**101. Jina.** Jina la kanisa lililoratibiwa hivi karibuni litaamuliwa na kanisa lenyewe baada ya kushauriana na msimamizi wa wilaya na kwa idhini ya Baraza la Halmashauri ya Wilaya. (102.4)

**101.1. Kubadilishwa kwa Jina.** Kanisa la Mnazareti la mtaa linaweza kubadilisha jina kwa njia hii:

1. Halmashauri ya kanisa la mtaa itatoa pendekezo la kubadilisha jina kwa msimamizi wa ambaye atapata idhini iliyoandikwa ya Baraza la Halmashauri ya Wilaya;

2. Kura nyingi za siri katika mkutano wa mwaka au mkutano maalum wa ushirika wa kanisa;

3. Baraza la Halmashauri ya Wilaya litatoa ripoti za badiliko la kikao cha wilaya, na idhinisho la kura za kikao cha wilaya hiyo. (102.4)

**102. Ushirikishaji.** Katika sehemu zote ambazo sheria zitaruhusu, wadhamini watashirikisha kanisa la mtaa, na wadhamini hao na waandamizi wao watakuwa wadhamini wa ushirikishaji huo. Mahali ambapo utaratibu huo hauambatani na sheria, Kanuni za Kushirikishwa zitaunda uwezo wa shirika, na kuweka kwamba shirika hilo litawekwa chini ya mamlaka ya Kanisa la Mnazareti, na mara kwa mara kuidhinishwa na kutangazwa katika *Kitabu cha Mwongozo* na Kikao Kikuu cha kanisa. Mali yote ya shirika hilo itashughulikiwa na kusimamiwa na wadhamini hao kwa ruhusa au idhini ya kanisa hilo la mtaa.

**102.1.** Ikiwa ardhi itanunuliwa na kustawishwa na Baraza la Halmashauri ya Wilaya kwa niaba ya kanisa la mtaa au mahali ambapo kanisa jipya lilianzishwa, inapendekezwa kwamba Baraza la Halmashauri ya Wilaya litabadilisha hati ya kanisa la mtaa baada ya kanisa la mtaa kulipa pesa za kumiliki ardhi kwa Baraza la Halmashauri ya Wilaya.

**102.2.** Wakati kanisa la mtaa limeshirikishwa, mali yote itakayopatikana itaandikishwa moja kwa moja kwa jina la kanisa mara tu itakapowezekana kufanya hivyo. (102.6)

**102.3.** Mchungaji na katibu wa halmashauri ya kanisa ndio watakaokuwa mwenyekiti na katibu wa kanisa, likiwa limeshirikishwa au halijashirikishwa, na watatia sahihi na kutekeleza shughuli zote zinazohusiana na ardhi, amana, kurudishwa kwa amana, mikataba, na hati

nyingine za kisheria ambazo hazikutajwa katika *Kitabu cha Mwongozo* na kulingana na maagizo yaliyowekwa katika kifungu cha 104-104.3.

**102.4.** Kanuni za Usajili au Kushirikishwa za kila kanisa la mtaa zinapaswa kuwa na maelezo ya mambo yafuatayo:

1. Jina la shirika lililosajiliwa lazima liwe na maneno haya: "Kanisa la Mnazareti."
2. Sheria na utaratibu wa shirika hilo zitakuwa ni zile za *Kitabu cha Mwongozo cha Kanisa la Mnazareti.*
3. Kanuni za Usajili zisiwe na kifungu chochote ambacho kinaweza kulifanya kanisa la mtaa kukosa kuepushwa na kodi ambayo makanisa ya sehemu hiyo yameruhusiwa kutolipa kisheria.
4. Baada ya kuvunjwa, mali ya shirika lililosajiliwa itakabidhiwa Baraza la Halmashauri ya Wilaya kwa usimamizi.

Kanuni za Usajili zinaweza kuwa na vifungu vingine zaidi ikiwa inafaa kulingana na sheria za sehemu hiyo. Hata hivyo hakuna kifungu kitakachowekwa ambacho kinaweza kusababisha mali ya kanisa la mtaa kuepushwa kutoka kwa Kanisa la Mnazareti. (101-101.1, 104.3, 106.1-106.3]

**102.5.** Katika makanisa yenye kusanyiko zaidi ya moja, ambapo zaidi ya kanisa moja lililoratibiwa hutumia jengo moja, usajili unaweza kutimizwa mahali ambapo sheria za sehemu hiyo zitaruhusu.

**102.6.** Katika sehemu ambazo usajili hauwezekani, jina la kanisa litahusisha maneno "Kanisa la Mnazareti" katika hati zote za kisheria zikiwemo hati za ardhi na hati za ufadhili bila kuwekewa mipaka. (102.2)

**103. Ardhi/Mali**. Kanisa la mtaa linalokusudia kununua au kuuza ardhi, kujenga makanisa au majengo yanayohusiana na kanisa, kurekebisha majengo hayo, au kukodisha mali yake kwa sababu yoyote, litatoa pendekezo la kufanya hivyo kwa msimamizi wa wilaya na Halmashauri ya Wilaya ya Mali za Kanisa ili walifikirie, watoe ushauri na idhini. Hakuna deni litakaloruhusiwa, iwe kuna amana au hakuna, la kununua ardhi au jengo, kujenga aina yoyote ya nyumba, au kurekebisha majengo ya kanisa bila idhini iliyoandikwa ya msimamizi wa wilaya na Halmashauri ya Wilaya ya Mali za Kanisa. (236-237.5)

**103.1**. Ikiwa makubaliano hayawezi kufikiwa kati ya halmashauri ya kanisa na msimamizi wa wilaya na Halmashauri ya Wilaya ya Mali za Kanisa, jambo hilo linaweza kufikishwa kwa msimamizi mkuu anayesimamia eneo hilo kwa uamuzi kufanywa. Aidha kanisa au msimamizi wa wilaya anaweza kukata rufani kwa Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu dhidi ya uamuzi uliofikiwa kwa uamuzi wa mwisho. Rufani zote kama hizo, kukanushwa kwa rufani, au ubishi unaohusiana na

rufani, zikiwa ni kwa msimamizi mkuu anayesimamia au kwa Halmashauri ya Wasimamizi, yatafanyika kwa maandishi. Nakala ya rufani, kukanushwa kwa rufani, au ubishi unaohusiana na rufani na halmashauri ya kanisa au msimamizi wa wilaya atatumwa kwa wote wanaohusika. Taarifa ya halmashauri ya kanisa ya kukata rufani itakuwa pamoja na azimio la kukata rufani, sababu zinazoonyesha haja ya rufani hiyo, na matokeo ya kura zilizopigwa.

**104. Vizuizi**. Kanisa la mtaa halina uwezo wa kununua au kukodisha ardhi, au kuuza jengo, kuweka amana au kubadilisha mali iliyopewa kanisa kwa kusudi la kulipatia kanisa mapato, au kwa njia ingine kuzuia mali, au pengine kupeana ardhi bila idhini ya theluthi mbili ya washirika wanaohudhuria mkutano wa mwaka, au mkutano maalum uliotishwa kwa kusudi hilo. Ikiwa kanisa linalipa deni ambalo kanisa liko nayo, na matayarisho ya malipo hayaongezei deni la kanisa na deni hilo halitazuia ardhi ya kanisa, idhini ya malipo inaweza kukubaliwa na theluthi mbili ya kura za halmashauri, bila hitaji la kuchukua kura za kusanyiko juu ya suala hilo. Halmashauri ya kanisa itatoa idhini kwa theluthi mbili za kura za washirika wake wanaohuduria mkutano na kupiga kura, maandilizi ya mali iliyotolewa kwa sababu ya kusudi maalum kwa kutoa fedha kwa kanisa la mtaa. Vifaa vyote hapo juu vinahitaji idhini iliyoandikwa ya msimamizi wa wilaya na Halmashauri ya Wilaya ya Mali ya Kanisa. (113.2-113.4, 113.7-113.8, 237.3-237.4)

**104.1.** Ardhi ya kanisa la mtaa haitawekwa dhamana ili kugharamia matumizi ya kawaida.

**104.2.** Kanisa la mtaa ambalo litaweka rehani au kuuza ardhi yake, au kupokea malipo ya bima kutokana na ardhi, litatumia mapato hayo kununua ardhi ingine, au kustawisha ardhi, au kupunguza deni la ardhi lililopo. Ni kwa idhini ya msimamizi wa wilaya tu, na ya Halmashauri ya Wilaya ya Mali za Kanisa, ambapo mapato hayo yanaweza kutumiwa kwa kusudi lingine.

**104.3.** Wadhamini na kanisa la mtaa hawana mamlaka ya kuzuia Kanisa la Mnazareti kutumia mali ya kanisa. (113-113.1)

**104.4. Kujitenga kwa Makanisa.** Hakuna kanisa lolote la mtaa linaloweza kujitenga kutoka kwa Kanisa la Mnazareti, au kukata uhusiano nalo, isipokuwa kwa kwa utaratibu uliyowekwa na Kikao Kikuu, na kwa masharti na mipango iliyokubaliwa.

**105. Kuungana.** Makanisa mawili au zaidi yanaweza kuunganishwa kwa theluthi mbili ya washirika wake walioko na wanaruhusiwa kupiga kura kaktika mikutano maalum iliyoitishwa na makanisa yanayohusika, ikiwa: muungano huo utapendekezwa na kura nyingi kwa kupiga kura za

siri za washirika halali wa halmashauri za makanisa yanayohusika, na siri katika mikutano maalum iliyoitishwa rasmi na makanisa yanayohusika, ikiwa: Muungano huo utapendekezwa na zaidi ya nusu ya kura za washirika wa halmashauri za makanisa yanayohusika, na mkuungano huo utaidhinishwa katika maandiko na msimamizi wa wilaya, na Baraza la Halmashauri ya Wilaya, na msimamizi mkuu katika usimamizi.

Muungano huo utakamilishwa kwenye mkutano maalum wa kusanyiko hilo jipya kwa kusudi la kuwachagua viongozi na kupanga mipango ya uchungaji. Msimamizi wa wilaya, au kasisi aliyeteuliwa na msimamizi, atasimamia mkutano.

Muungano ulioundwa hivyo utashirikisha washirika wote wa makanisa ya zamani, washirika wa idara zote za makanisa hayo, na unaweza kuchukua sehemu ya, au mali zote za makanisa hayo, pamoja na madeni yaliyokuwa yanadaiwa, kwa idhini ya msimamizi wa wilaya, Baraza la Halmashauri ya Wilaya, na msimamizi mkuu wa eneo linalohusika. Muungano huo pia utaunganisha makadirio ya kikao kikuu, elimu, na wilaya.

Baada ya kujulishwa rasmi na msimamizi wa wilaya, katibu mkuu wa Kanisa la Mnazareti ameidhinishwa kuondoa majina ya makanisa hayo yaliyoungana katika orodha ya makanisa.

**106. Kutangaza Makanisa Yamebatilishwa au Hayajaratibiwa.** Makanisa yanaweza kutangazwa kuwa yamebatilishwa kwa kipindi cha mpito kwa hatua ya Baraza la Halmashauri ya Wilaya kabla ya kutangazwa kutoratibiwa kirasmi, kufanywa upya na kuratibiwa tena.

**106.1.** Kanisa la mtaa linaweza kuwa Halijaratibiwa kama ifuatavyo:

1. kwa pendekezo kutoka kwa msimamizi wa wilaya;
2. matokeo ya kuthibitishwa kutoka kwa msimamizi mkuu anayehusika; na
3. theluthi mbili ya kura za Baraza la Halmashauri ya Wilaya.

**106.2**. Ikiwa kanisa litakuwa limebatilishwa au kutoratibiwa, au katika hali ya kujiondoa au kujaribu kujiondoa kutoka kwa Kanisa la Mnazareti (kwa kuruhusiwa na Baraza la Halmashauri ya Wilaya), mali yoyote ya kanisa hilo itakayokuwepo, hairuhusiwi kutumiwa kwa kusudi lingine, bali hati za kuimiliki zitakabidhiwa Baraza la Halmashauri ya Wilaya anasimamia kama mwakilishi wa wilaya inayohusika ambapo hati hiyo imeshirikishwa, au wawakilishi wengine walioidhinishwa, kwa matumizi ya Kanisa la Mnazareti, kama vile kikao cha wilaya kitakavyoagiza. Wadhamini wa kanisa la mtaa wanaotunza mali ya kanisa ambalo kuratibiwa kwake kumebatilishwa, watauza au kuitumia kwa mamlaka na chini ya maagizo ya Baraza la Halmashauri ya Wilaya au wakili

aliyeteuliwa na kikao cha wilaya, kwa idhini iliyoandikwa ya Msimamizi Mkuu wa eneo hilo; aidha kuwasilisha mali hiyo au kuwasilisha matokeo ya mauzo kama vile ilivyoagizwa na kikao cha wilaya Baraza lake Halmashauri ya Wilaya. (104.4, 106, 225.23)

**106.3.** Hakuna mdhamini au wadhamini wa kanisa ambalo kuratibiwa kwake kumebatilishwa, au kanisa ambalo linajiondoa au kujaribu kujiondoa kutoka kwa Kanisa la Mnazareti, linaweza kuhamisha mali kwa kutotumiwa na Kanisa la Mnazareti. (104.4, 141-144, 225.23)

**106.4.** Ni makanisa yale tu ambayo kuratibiwa kwake kumebatishwa rasmi yanayoweza kuondolewa katika orodha ya katibu mkuu.

**106.5.** Kanisa la mtaa linapotangazwa kuwa limeondolewa katika orodha ya makanisa yalioratibiwa, wanaoweka sahihi hati na hundi za akaunti ya kanisa lazima wazipeleke hati au hundi zote kwa Baraza la Halmashauri ya Wilaya ili zihifadhiwe. Kukataa kufanya hivyo kunaipa mamlaka Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya kufunga akaunti zote na kuchukua jukumu la usimamizi wa mali yote ya kanisa hilo kwa kupitisha azimio la kufanya hivyo ikiwa sheria ya sehemu hiyo inaruhusu.

## B. Ushirika wa Kanisa la Mtaa

**107. Ushirika Kamili.** Ushirika kamili wa kanisa la mtaa utakuwa ni watu wote walioratibiwa kuunda kanisa la mtaa na wale waliopewa mamlaka ya kufanya hivyo, na wale wote waliopokelewa hadharani na mchungaji, msimamizi wa wilaya, au msimamizi mkuu, baada ya kukiri ujuzi wao wa wokovu, na kuamini kwao kwa mafundisho ya Kanisa la Mnazareti, na kukubali kwao kutii uongozi wake. Uongozi wa kanisa la mtaa utatafuta kumweka kila mshirika katika huduma ya utumishi na kipindi cha malezi na msaada. (23, 107.2, 111, 113.1, 516.1, 520, 532.8, 538.8 538.9)

**107.1.** Watu wakitaka kujiunga na kanisa, mchungaji atawaeleza manufaa na jukumu la ushirika katika kanisa, atawafundisha Kanuni za Imani, matakwa ya Agano la Maadili ya Kikiristo, na Agano la Tabia ya Kikristo, na makusudi na utume wa Kanisa la Mnazareti.

Baada ya kushauriana na Kamati ya Uinjilisti na Ushirika wa Kanisa, mchungaji atawapokea watu wanaostahili katika ushirika wa kanisa katika ibada ya hadharani, akitumia hati iliyokubaliwa ya kuwapokea watu kama washirika wa kanisa (21, 28-33, 110.4, 228, 704)

**107.2. Washirika wa Kanisa Ambalo Halijaratibiwa.** Mahali ambapo uongozi wa kanisa la mtaa haujathibitishwa, Utume wa kanisa ambalo

halijaratibiwa utawapokeka na kutoa ripoti ya washirika wa kanisa katika tarakimu za mwaka kulingana na aya ya 107 na 107.1.

**107.3. Kupiga kura na Kuwa kiongozi .** Ni wale watu walio washirika kamili na wanaohusika katika kanisa la mtaa, na wamefikisha umri wa miaka 15, wanaweza kuwa na ofisi katika kanisa ambalo sheria yao inaruhusu, watapiga kura katika mikutano ya mwaka na mikutano maalum ya kanisa, au wawakilishe kanisa kama wajumbe katika kikao cha wilaya.

**108. Washiriki Wasio Washirika Kamili.** Katika sehemu ambazo wilaya itaruhusu, kanisa la mtaa linaweza kuwa na washiriki wasio washirika kamili ambao watakuwa na haki zote za ushirika, isipokuwa haki ya kupiga kura na kuchaguliwa kwenye wadhifa wowote katika kanisa. (205.24)

**108.1**. Washirika wa aina hiyo wanaweza kupewa haki ya ushirika kamili au kutolewa katika ushirika wa kanisa wakati wowote, ikiwa mchungaji na Kamati ya Unjilisti na Ushirika wa Kanisa ina sababu ya kufanya hivyo.

**109. Washirika Wasioshiriki Kikamilifu.** Kanisa la mtaa linaweza kuweka washiriki katika orodha ya "washirika wasioshiriki kikamilifu" kwa sababu zilizotajwa katika aya ya 109.1 na 109.2. (112.3, 133)

**109.1.** Mshirika wa kanisa la mtaa ambaye amehamia sehemu nyingine na hawezi kushiriki kikamilifu katika kanisa ambalo yeye ni mshirika anapaswa kuhimizwa ahudhurie Kanisa la Mnazareti katika sehemu anayoishi na ahamishie ushirika wake katika kanisa hilo.

**109.2.** Ikiwa mshirika wa kanisa atakosa kuhudhuria ibada zote za kanisa kwa muda wa miezi sita mfululizo bila sababu inayokubalika na halmashauri ya kanisa, na juhudi zimefanywa za kumtia moyo ili ahudhurie ibada kadiri inavyowezekana, ushirika wa mtu huyo utahesabiwa kama mshirika asiyeshiriki kikamilifu kwa pendekezo la Kamati ya Uinjilisti na Kamati ya Ushirika wa Kanisa na hatua ya halmashauri ya kanisa. Mtu huyo atajulishwa jambo hilo kwa barua ya kumtia moyo kutoka kwa mchungaji, katika kipindi cha siku saba, baada ya hatua ya halmashauri ya kanisa. Baada ya hatua hiyo ya halmashauri ya kanisa, mchungaji atarekebisha orotha ya ushirika wa kanisa la mtaa kwa maneno haya pamoja na tarehe: "Amewekwa katika orodha ya Washirika wasioshiriki Kikamilifu na halmashauri ya kanisa."

**109.3.** Washirika wasioshiriki kikamilifu watajumlishwa pamoja na washirika kamili katika orodha ya washirika wote wa kanisa la mtaa. Ripoti ya Ushirika itatolewa kwa kikao cha wilaya katika idadi tofauti, kama vile (1) wanaoshiriki kikamilifu na (2) wasioshiriki kikamilifu.

**109.4.** Washirika wasioshiriki kikamilifu hawana haki ya kupiga kura katika mikutano ya mwaka au mikutano maalum ya kanisa, wala kushikilia wadhifa wowote katika kanisa.

**109.5**. Mshirika asiyeshiriki kikamilifu anaweza kuomba halmashauri ya kanisa kwa kuandika barua kurudisha jina lake katika orodha ya washirika kamili wa kanisa. Ombi hilo ni lazima liwe na hakikisho jipya la kutimiza ahadi za ushirika na kushiriki kikamilifu katika ibada za kanisa. Ushirika kamili unaweza kurudishiwa mtu huyo kwa pendekezo la Kamati ya Uinjilisti na Ushirika wa Kanisa na hatua kutoka kwa halmashauri ya kanisa.

## C. Kamati ya Uinjilisti na Ushirika wa Kanisa la Mtaa

**110.** Halmashauri ya kanisa itateua Kamati ya Uinjilisti na Ushirika wa Kanisa yenye watu wasiopungua watatu, itakayohusika katika kumshauri mchungaji, ambaye ndiye atakuwa mwenyekiti wake. Kazi ya kamati hiyo itakuwa ni:

**110.1.** Kuendeleza uinjilisti katika kanisa la mtaa na kujitahidi kuhifadhi matunda ya uinjilisti. (107-107.1, 129.24)

**110.2.** Kufanya utafiti na kutoa mapendekezo kwa halmashauri ya kanisa na idara zingine jinsi ya kusisitiza na kuendeleza uinjilisti katika shughuli zote za uhai wa kanisa.

**110.3.** Kutumika kama kamati ya kanisa ya kutekeleza ratiba na mipango ya dhehebu ya uinjilisti wilaya.

**110.4.** Kuwatia moyo waumini wapya wajitahidi kuhitimu kwa ushirika wa kanisa kwa kuishi maisha ya utakatifu, kujifunza Biblia na *Kitabu cha Mwongozo,* kibinafsi au kwa kushiriki katika darasa la mchungaji la mafundisho ya ushirika, wakikumbuka kwamba washirika wanaopokelewa kwa kukiri imani husaidia kuhifadhi matunda ya uinjilisti. (20-21)

**110.5.** Kujitahidi kuwaleta washirika wapya katika ushirika kamili na utumishi wa kanisa.

**110.6.** Kufanya kazi pamoja na mchungaji katika kustawisha ratiba ya kuendelea ya mwongozo wa kiroho kwa washirika wapya.

**110.7.** Kupendekeza kwa halmashauri ya kanisa, baada ya kuteuliwa na mchungaji, wainjilisti wa kuongoza mikutano ya uinjilisti. Inapendekezwa kwamba kuwe na angalau mkutano mmoja wa injili kila mwaka, utakaoongozwa na muinjilisti aliyesajiliwa au aliyetumwa.

**110.8.** Hakuna mtu atakayepokelewa katika ushirika kamili wa kanisa kabla mchungaji kushauriana na Kamati ya Uinjilisti na Ushirika wa Kanisa kuhusu kupokelewa kwa mtu huyo (107.1)

### D. Uhamisho wa Mshirika Wa Kanisa la Mtaa

**111. Kuhamisha.** Mchungaji, akiombwa na mshirika, anaweza kutoa hati ya kuhamisha ushirika kwa kanisa lingine lolote la Mnazareti litakalotajwa (tazama hati katika kifungu cha 817), hati kama hiyo ya uhamisho itakuwa halali kwa kipindi cha miezi mitatu pekee. Kupokelewa kwa mshirika huyo kukikubaliwa na kanisa alilohamia, ushirika wake katika kanisa alilotoka utakoma. (818)

**111.1. Kutambulishwa.** Mchungaji, akiombwa na mshirika, anaweza kutoa Hati ya Kumtambulisha mshirika (tazama hati katika kifungu cha 815) kwa kanisa lolote la Injili litakalotajwa, baadaye ushirika wa mtu huyo katika kanisa la mtaa unaotoa hati utakoma mara moja. (112.2, 539.5, 815)

## E. Kukatiza Ushirika katika Kanisa la Mtaa

**112. Wahudumu.** Mhudumu aliyepewa hati au aliyewekwa wakfu amejiunga na ushirika wa kanisa au huduma ya kanisa lingine mbali na Kanisa la Mnazareti, mchungaji wa kanisa la mtaa ambalo mhudumu huyo ni mshirika atajulisha Halmashauri ya Wilaya ya Hati za Kuhihitmu kwa jambo hilo mara moja. Halmashauri ya Wilaya ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu au Halmashauri ya Wahudumu ya Wilaya itachunguza na kudhibitisha hali ya ushirika wake kama mtumishi. Halmashauri hiyo au Halmashauri ya Wahudumu ya Wilaya ikiamua kwamba kasisi ataondolewa kutoka katika Orodha ya Wahudumu, mchungaji wa kanisa la mtaa ambalo mhudumu huyo ni mshirika pia ataondoa jina lake katika orodha ya ushirika wa kanisa na ataandika kando ya jina lake maneno haya: “Ametolewa kwa sababu ya kujiunga na dhehebu, au huduma ingine.” (532.9, 538.10. 538.13-538.14)

**112.1. Waumini.** Muumini mshirika wa kanisa la mtaa, akikubali ushirika, hati ya kuhubiri, au kuwekwa wakfu katika dhehebu au shirika lingine la dini, au akijishughulisha na kazi ya kanisa huru au umishenari wa kujitegemea, ushirika wake katika kanisa la mtaa utakoma mara moja kwa sababu ya hiyo. Lakini ushirika wake katika kanisa hilo utaendelea kuwa halali ikiwa alikuwa amepata idhini iliyoandikwa ya halmashauri ya kanisa ambalo yeye ni mshirika, na ya Halmashauri ya Wilaya ambayo kanisa hilo liko.

**112.2. Kuwekwa Huru Kutoka kwa Ushirika.** Mchungaji, akiombwa na mshirika, anaweza kutoa barua ya kumweka huru mshirika, (tazama hati katika kifungu cha 816), na kwa hivyo kukomesha ushirika wa mtu huyo mara moja. (111.1, 112)

**112.3**. Baada ya miaka miwili kutoka tarehe ambayo muumini alitangazwa kuwa mshiriki asiyeshiriki kikamilifu, jina lake linaweza kuondolewa katika orodha ya washirika wa kanisa kwa hatua ya halmashauri ya kanisa. Baada ya hatua hiyo ya halmashauri ya kanisa, mchungaji ataandika tarehe na maneno yafuatayo kando ya jina la mshirika huyo: "Ameondolewa na halmashauri ya kanisa." [109, 133]

## F. Mikutano ya Kanisa

**113.** Mkutano wa washirika wa kanisa la mtaa wa kujadiliana na kutekeleza shughuli na mipango ya kanisa utaitwa mkutano wa kanisa. Kufuatana na sheria inayotumika, Kanuni ya Kushirikishwa na Sheria za Uongozi katika Kitabu cha Mwongozo, mikutano na matukio ya washirika wa Kanisa la Mnazareti katika kanisa la mtaa, wilaya, na makao makuu pamoja na kamati zake itaendeshwa na kusimamiwa kulingana na utaratibu uliowekwa katika toleo la sasa la kitabu cha (Toleo la sasa) la *Kanuni za utengamano za Robert lililoboreshwa* kwa kutumiwa kwa utaratibu huo. (32, 104, 113.7-113.8, 115, 518)

**113.1.** Ni washirika kamili tu na ambao wametimiza umri wa miaka 15 au zaidi watakaoruhusiwa kupiga kura kwenye mikutano ya kanisa. (107.3, 109-109.4)

**113.2.** Hakuna nafasi kwa mtu asiyekuweko katika mkutano kupiga kwenye mikutano ya kanisa.

**113.3. Kutekelezwa kwa Shughuli**. Shughuli zote, zikiwa ni pamoja na uchaguzi, zikiambatana na roho na utaratibu wa kanisa, na ambazo utaratibu wake haujaelezwa, zinaweza kutekelezwa katika mkutano wowote wa kanisa.

**113.4. Kuzingatia Sheria ya Uraia.** Katika sehemu zote ambazo sheria ya uraia inataka utaratibu fulani ufuatwe wa kuitisha na kuendesha mikutano ya kanisa, utaratibu huo unapaswa kufuatwa kwa makini. (142)

**113.5. Kiongozi Msimamizi.** Mchungaji, ambaye ndiye msimamizi rasmi wa kanisa la mtaa, au msimamizi wa wilaya, au msimamizi mkuu wa eneo hilo, au mtu aliyechaguliwa na msimamizi wa wilaya au msimamizi mkuu, ndiye atakayesimamia mikutano ya mwaka au mikutano maalum ya kanisa. (213.1, 307.10, 516.15)

**113.6. Katibu.** Katibu wa halmashauri ya kanisa ndiye atakayekuwa katibu wa mikutano yote ya kanisa; na asipokuwepo, katibu wa muda atachaguliwa. (135.4)

**113.7. Mkutano wa Mwaka.** Mkutano wa mwaka wa kanisa utafanyika katika kipindi cha siku 90 kabla ya mkutano wa kikao cha wilaya. Tangazo

la hadhara kuhusu mkutano wa mwaka ni lazima litangazwe kwenye mimbari Jumapili mbili kabla ya mkutano huo. Mkutano huu wa mwaka unaweza kufanyika kwa zaidi ya siku moja ama katika ibada zaidi ya moja kwa idhini ya halmashauri ya kanisa.

**113.8. Taarifa Maalum.** Mikutano maalum ya kanisa inaweza kutangazwa wakati wowote na mchungaji, au halmashauri ya kanisa baada ya kupata idhini kutoka kwa mchungaji au msimamizi wa wilaya au msimamizi mkuu wa eneo hilo. Tangazo la hadhara la mikutano maalum ya kanisa litatangazwa kwenye mimbari katika ibada aghalau mbili zinazofuatana, au katika hali ambayo inakubaliana na sheria za nchi. (104, 113.1, 115-115.1, 123-123.7, 137, 139, 142.1, 144)

**113.9. Ripoti.** Ripoti zitatolewa kwenye mkutano wa kanisa wa mwaka na mchungaji, msimamizi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa (HSJUK), mwenyekiti wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti wa Kimataifa (HVMK), mwenyekiti wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa (MMK), mashemasi, wahudumu wa mtaa, katibu, na mweka hazina wa halmashauri ya kanisa. (135.2, 136.5, 146.6, 152.2, 508, 516.7. 531.1)

**113.10. Kamati ya Uteuzi.** Kamati ya Uteuzi itatumiwa kuteua viongozi, halmashauri, na wajumbe wa kikao cha wilaya ambao kuteuliwa kwao hakukuelezwa mahali pengine.

Kamati ya Uteuzi itakuwa na washirika wa kanisa wasiopungua watatu na wasiozidi saba, pamoja na mchungaji. Kamati ya Uteuzi itaundwa kulingana na vile halmashauri ya kanisa itakavyopendekeza. Mchungaji atakuwa mwenyekiti wa kamati ya uteuzi. Watu wote walioteuliwa na kamati hii wanapaswa kuwa wametimiza matakwa yote yanayohitajika kwa viongozi wa kanisa yaliyoelezwa katika kifungu cha 33.

**113.11. Uchaguzi.** Katika mkutano wa mwaka wa kanisa kutakuwako na uchaguzi, kwa kura ya siri; wa mawakili, wadhamini, msimamizi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa, na washirika wa Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa, watatumika kwa kipindi cha mwaka mmoja utakaofuata, na hadi waandamizi wao watakapochaguliwa na kuhitimishwa. Mahali sheria itaruhusu na kuidhinishwa na kura ya wingi ya washirika wote wa kanisa waliohudhuria mkutano, wale wote waliochaguliwa watahudumu kwa kipindi cha miaka miwili. Wale wote waliochaguliwa kuwa viongozi wa kanisa watakuwa washirika kamili wa hilo kanisa la mtaa la Mnazareti.

Tunaagiza makanisa yetu ya mtaa kuchagua kama viongozi wa kanisa washirika wanaoshiriki kikamilifu katika kanisa la mtaa na ambao wanadhihirisha wazi ujuzi wa utakaso kamili na wanaonyesha ushahidi wa

wazi kwa neema ya Mungu aliyetuita kwa maisha ya utakatifu; wanaokubaliana kikamilifu na mafundisho, uongozi na utaratibu wa Kanisa la Mnazareti; na ambao wanasaidia na kutegemeza kanisa la mtaa kwa maudhurio, kuhusika katika huduma, na zaka na sadaka kwa uaminifu. (33, 127, 137, 141, 142.1, 145-147)

**113.12.** Katika sehemu ambazo sheria zinaruhusu, na katika makanisa ambayo utaratibu huo na idadi ya wale watakaochaguliwa imeidhinishwa kwa wingi wa kura kura zilizopigwa na washirika wa kanisa walioko mkutanoni, halmashauri ya kanisa inaweza kuchaguliwa, na baadaye idadi inayostahili ya waliochaguliwa inaweza kutumika kama mawakili na wadhamini wa kanisa, kulingana na kifungu cha 137 na 141. Halmashauri ya kanisa ikichaguliwa kwa njia hiyo, halmashauri itajiratibu kujiunda katika kamati kadhaa zitakayoshughulikia kazi zilizokabidhiwa. Ikiwa kanisa limechagua kamati ya elimu kama sehemu ya halmashauri yake kulingana na kifungu cha 145, kamati hiyo ndiyo itakayokuwa Kamati ya Elimu ya halmashauri ya kanisa. Halmashauri ingine na muundo wa kamati inaweza kutumiwa na kanisa la mtaa katika kujiongoza kwa sababu ya tendo la huduma na la kimisheni, mradi iwe halmashauri hiyo tofauti imeidhinishwa katika maandishi na msimamizi wa wilaya na Baraza la Halmashauri ya Wilaya, na miundo kama hiyo inakubaliana na mahitaji ya nchi. (145-145.10)

**113.13.** Katika sehemu ambazo sheria zinaruhusu, na katika makanisa ambapo utaratibu kama huo umekubaliwa kwa wingi wa kura zilizopigwa na washirika wa kanisa walioko katika mkutano rasmi wa mwaka, baada ya kupata idhini ilioandikwa ya msimamizi wa wilaya, kanisa linaweza kuchagua nusu ya washirika wa halmashauri yake kutumika kwa kipindi cha miaka miwili, au theluthi moja ya washirika hao kutumika kwa kipindi cha miaka mitatu, kwa utaratibu wowote ule utakaotumiwa, kanisa litapaswa kuchagua idadi iliyo sawa na ile itakayotumika zaidi ya mwaka mmoja ambayo itachaguliwa kila mwaka. Halmashauri ya kanisa ikichaguliwa kwa njia hiyo, idadi ya wadhamini na mawakili wa kanisa ni lazima ilingane na kifungu cha 137 na 141.

**113.14.** Katika mkutano wa mwaka wa kanisa, kutakuwa na uchaguzi, kwa kura ya siri, wa wajumbe waumini watakaowakilisha kanisa katika kikao cha wilaya, au walioidhinishwa na wingi wa kura za ushirika wa kanisa katika mkutano wa mwaka, wajumbe wanaweza kupendekezwa na mchungaji na kuidhinishwa na halmashauri ya kanisa la mtaa kulingana na kuwakilishwa kulikowekwa na Kikao Kikuu kulingana na kifungu cha 201-201.2. Wale wote waliochaguliwa kama wajumbe watakuwa washirika kamili wa Kanisa hilo la Mnazareti la mtaa. (107.3, 113.11)

**113.15.** Wajumbe wa kikao cha Wilaya kutoka kwa Kanisa ambalo halijaratibiwa wanaweza kuchaguliwa na mchungaji kulingana na utaratibu katika vifungu vya 33, 201.1, na 201.2. Wajumbe wanaweza kutajwa na mchungaji wa kanisa ambalo halijasajiliwa kuhudhuria mikutano ya wilaya, kulingana na Mkataba wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti wa Kimataifa (MHVMK), Mkataba wa Kimataifa wa Misheni ya Mnazareti, na Sheria za Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa. (100.1, 810, 811, 812)

## G. Mwaka wa Kanisa la Mtaa

**114.** Mwaka wa usimamizi utaenda sambamba na mwaka wa tarakimu za kanisa la mtaa na utatambuliwa kama mwaka wa kanisa.

**114.1.** Mwaka wa tarakimu za kanisa utamalizika katika kipindi cha siku 90 kabla ya kufunguliwa kwa mkutano wa kikao cha wilaya; na mwaka mpya wa tarakimu utaanza siku itakayofuata kumalizika kwa mkutano. Tarehe yenyewe rasmi ya kuanza na kumalizika kwa mwaka wa tarakimu za kanisa la mtaa itawekwa na Halmashauri ya Wilaya. (225.1)

### H. Kumwita Mchungaji

**115**. Kasisi au mhudumu aliyepewa hati (alama ya kasisi) anaweza kuitwa kuwa mchungaji wa kanisa ikikubaliwa kwa theluthi mbili za kura iliyopigwa kwa siri na washirika wa kanisa waliotimiza umri wa kupiga kura katika mkutano rasmi wa mwaka au mkutano maalum wa kanisa, mradi tu:

1. Uteuzi utakuwa na idhini mbele ya msimamizi wa wilaya.
2. Uteuzi utakuwa umeidhinishwa na Halmashauri ya Baraza la halmashauri ya wilaya wakati mteuzi huyo atakuwa ameteuliwa ni mshirika wa kanisa hilo la mtaa, au anahudumu kama mshirika anayelipwa au halipwi wa kanisa hilo la mtaa; na
3. Mteuzi huyo atakuwa ameteuliwa kwa kanisa na halmashauri ya wilaya kwa theluthi mbili za kura ya siri ya washirika wote.

Kuitwa huko kutahitaji kuchunguzwa na kuendelezwa kama ilivyoelezwa katika vifungu vifuatavyo. (119, 122-125.5, 129.2, 159.8, 211.10, 225.16, 514, 532, 533.4, 534.3)

**115.1.** Kukubali mwito wa kuwa na uhusiano wa uchungaji kutajulishwa na mhudumu aliyeitwa katika kipindi cha siku 15 kutoka tarehe ambayo kanisa lilikutana na kupiga kura ya mwito.

**115.2.** Halmashauri ya kanisa na mchungaji wataeleza wazi wazi matarajio na shabaha walizo nazo kila mmoja wao kwa mwingine kwa maandishi. (122, 129.3-129.4)

**115.3.** Kwa haraka iwezekanavyo baada ya mchungaji kuanza huduma yake, mchungaji na waumini wanaweza kushiriki katika ibada ya kutawazwa au kushikamana. Kusudi la ibada hiyo ni kusherehekea umoja na mwelekeo wa mapenzi ya Mungu. Ikiwezekana, msimamizi wa wilaya atasimamia sherehe.

**115.4.** Baada ya kutoa mwito, kanisa la mtaa mshahara linalokusudia kumlipa mchungaji. Kiasi cha mshahara huo kitaamuliwa na halmashauri ya kanisa. Mapatano yakififikiwa kati ya kanisa au halmashauri ya kanisa na mchungaji, malipo ya mchungaji yatakayoamuliwa yatakuwa ni wajibu wa kanisa. Hata hivyo, ikiwa kanisa litashindwa kuendelea kulipa malipo ya mshahara uliokubaliwa, kukosa uwezo huo na kushindwa kulipa hakutachukuliwa kuwa sababu ya kutosha kumfanya mchungaji kuchukulia kanisa hatua za kisheria; na kwa hali yoyote kanisa au Baraza la Halmashauri ya Wilaya hawatakuwa na jukumu la kisheria la kumlipa mchungaji pesa zaidi ya zitakazopatikana wakati wa kipindi cha huduma yake kwa kanisa, na ambazo hazikupangiwa jambo hilo. Hatua za kisheria zikichukuliwa juu ya kanisa au kwa Baraza la Halmashauri ya Wilaya na mchungaji ambaye anahudumu kwa sasa au mchungaji aliyeondoka, wilaya inaweza kuchukua hatua za kuhifadhi hati za mhudumu na papo hapo kuondoa jina la mchungaji kutoka kwa Orodha ya Wahudumu.

Kanisa la mtaa pia litapaswa kufanya matayarisho ya kulipa gharama za usafiri na kuhama kwa mchungaji aliyeitwa. (32-32.3, 129.8-129.9)

**115.5.** Malipo ya mchungaji yataanza kuhesabiwa Jumatatu itakayotangulia Jumapili ya kwanza ya utumishi rasmi kwa kanisa.

**115.6.** Makanisa ya mtaa yanaweza kufikiria mipango tofauti ya msaada wa kiuchungaji yakishirikiana na wilaya zao. (32.3, 129.8)

**116**. Kuthibitisha thamani za familia na umuhimu wa mfano wa maisha ya amani na uadilifu ya wachungaji, makanisa ya mtaa yanapaswa kufikiria kuwapa wachungaji na wahudumu washirika likizo ya uzazi kwa mama na kwa baba. Wasimamizi wa wilaya wanastahili kuhimiza makanisa ya mtaa kutilia maanani sheria ya likizo ya uzazi kwa mama na kwa baba na kutoa msaada kwa sababu ya kuendelea kwao. Sheria kama hizo zinaweza kuwa na mambo yafuatayo:

1. Kuweka wakati na muda wa likizo ya uzazi kwa mama na kwa baba kunafaa kuamuliwa kwa makubaliano ya mchungaji na halmashauri ya kanisa ya kuzaliwa kwa mtoto au kupanga kupokelewa kwa mtoto.

2. Likizo ya uzazi kwa baba au mama inapaswa kuongezwa kuwa sehemu ya likizo ya kazi na kutengwa kutoka kwa likizo ya kazi.
3. Kanisa la mtaa litawasiliana na mchungaji na msimamizi wa wilaya kupanga mchungaji wa kuhudumu kwa muda wakati wa likizo ya uzazi ya baba au mama ya mchungaji wa kanisa hilo.
4. Wakati wa likizo ya uzazi kwa mama au baba, mshahara wote wa mchungaji na faida zingine utaendelea. Mipangilio ingine itawekwa kwa maandishi na kuweka saini na mchungaji, katibu wa halmashauri ya kanisa, na msimamizi wa wilaya.

**117.** Mchungaji wa kanisa ambalo limeratibiwa kwa kipindi cha chini ya miaka mitano, au lenye washirika chini 35 waliopiga kura kwenye mkutano uliopita wa mwaka wa kanisa, au linapokea msaada wa kifedha kutoka kwenye wilaya, anaweza kuteuliwa mara moja au zaidi na msimamizi wa wilaya, kwa ruhusa ya Halmashauri ya Wilaya. (211.17)

**117.1** Wakati kanisa linakuwa na washirika zaidi ya 35 au limeratibiwa angalau kwa miaka mitano, na mchungaji wake amehudumu kama mchungaji aliyeteuliwa aghalau kwa miaka miwili, hatua ya kubadilishwa kutoka kwa "hali ya kuteuliwa" inaweza kuanzishwa. Hatua hiyo ni lazima ihusishe kuchunguza upya kwa uhusiano wa kanisa na mchungaji, kura za wingi za washirika wa halmashauri ya kanisa walio kwenye mkutano, idhinisho la msimamizi wa wilaya, na idhinisho la Halmashauri ya Wilaya. Tarehe ya ukumbusho wa baadaye wa kipindi cha miaka minne ya kila mara ya uhusiano wa kanisa na mchungaji itakuwa tarehe ya idhinisho la mwisho.

**118.** Ikiwa kutakosa kuwa na makubaliano kati ya halmashauri ya kanisa na msimamizi wa wilaya kuhusu matayarisho ya uchungaji, halmashauri ya kanisa au msimamizi wa wilaya anaweza kupeleka jambo hilo kwa msimamizi mkuu wa eneo hilo ili afanye uamuzi wake. Kutoka kwa uamuzi huo aidha halmashauri ya kanisa au msimamizi wa wilaya anaweza kukata rufani kwa Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu. Rufani zote kama hizo, kukanushwa kwake, au ubishi unaohusu jambo hilo, ziwe ni kwa msimamizi mkuu au Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu, ni lazima ziwasilishwe kwa maandishi. Nakala ya rufani, kukanushwa kwa rufani, au ubishi unaohusu jambo hilo, aidha kutoka kwa halmashauri ya kanisa au msimamizi wa wilaya, itapaswa kutumwa kwa yule mhusika mwingine. Taarifa ya mkutano wa halmashauri ya kanisa uliokata rufani itakuwa na azimio la kukata rufani, sababu za kukata rufani, na matokeo ya kura zilizopigwa. Ikiwa mhudumu anayehusika atajiondoa, au ikiwa yule anayekusudiwa kuwa mchungaji hawezi kupatikana, utaratibu wa rufani

utakoma mara, na msimamizi wa wilaya na halmashauri ya kanisa wataendelea na matayarisho ya uchungaji.

**119.** Mwito wa mchungaji ambaye ni mhudumu aliyepewa hati (alama ya kasisi) itamalizika baada ya kumalizika kwa mkutano wa kikao cha wilaya, ikiwa mhudumu huyo atanyimwa hati mpya.

**120.** Mchungaji anayetaka kuacha kazi ya uchungaji:

1. Kwanza atashauriana na msimamizi wa wilaya;
2. Atatoa ilani iliyoandikwa kwa halmashauri ya kanisa aghalau siku 30 kabla ya kujiuzulu kwake kwa uchungaji; na
3. Atatuma nakala ya ilani kwa msimamizi wa wilaya.

Wakati kujiuzulu kumepokelewa na halmashauri ya wilaya na kuidhinishwa kwa maandishi na msimamizi wa wilaya, tarehe ya kusimamishwa itamalizika katika kipindi cha siku 30.

**120.1.** Mchungaji anayejiuzulu, akishirikiana na katibu wa halmashauri ya kanisa, atatayarisha orodha sahihi ya washirika wa kanisa pamoja na anwani zao. Orodha hiyo ni lazima ilingane kwa hesabu na ile iliyochapishwa katika taarifa ya mwisho ya mkutano wa wilaya, ikionyesha walioondolewa na walioongezeka katika mwaka unaoendelea.

**121.** Baada ya kupendekezwa na halmashauri ya kanisa na kuidhinishwa na msimamizi wa wilaya, kusanyiko linaweza kuchagua mchungaji msaidizi wa kuhudumu. Katika hali hiyo, masharti yafuatayo yatatumika:

1. Wasaidizi wa mchungaji watafanya kazi na halmashauri ya kanisa, chini ya uongozi wa msimamizi wa wilaya, kuunda mpango wa jukumu na mamlaka ya kushirikiana.
2. Wasaidizi wa mchungaji wanao usawa mmoja katika ofisi ya kichungaji. Ikiwa inatakikana na sheria, mtu mmoja atapewa kazi kirasmi na halmashauri ya kanisa kama kiongozi anayesimamia, akihudumu kama kiongozi wa ushirika na mwenyekiti wa halmashauri ya kanisa.
3. Hatua ya kuchunguza uhusiano wa kanisa na mchungaji utaendelezwa kulingana na kifungu cha 123.123-7.
4. Kanisa la mtaa ambalo mchungaji hajachaguliwa na ambaye amehudumu kwa aghalau kipindi cha miaka miwili linaweza kuongeza mhudumu mmoja au wahudumu zaidi kama wasaidizi wa wachungaji kwa kufuata kifungu 115 kwa hatua hii. Baada ya kuidhinishwa na msimamizi wa wilaya na theluthi mbili za kura za washirika wote wa halmashauri ya kanisa, kanisa litapiga kura ikiwa litaongeza msaidizi yeyote wa mchungaji. Msaidizi wa mchungaji ambaye ni mtahiniwa atahitaji kupokea theluthi mbili za kura za

kusanyiko ili kuidhinishwa kuhudumu kama msaidizi wa mchungaji wa kanisa hilo la mtaa.

5. Kama theluthi mbili za kura zinazohitaji zimepokelewe, kipindi cha miaka miwili kitaanza tarehe hiyo kwa kila mhudumu. Uchunguzi wa kila mara wa uhusiano wa kanisa na mchungaji utapangwa katika ya siku 60 za ukumbusho wa pili wa huduma ya kichungaji ya mchungaji msaidizi (115, 123-123.7)

**121.1.** Katika siku 60 za kujiuzulu au kuachishwa kwa msaidizi wa mchungaji, msimamizi wa wilaya, au mwakilishi aliyeteuliwa, ataendeleza uchunguzi wa mara kwa mara wa kanisa na mchungaji kama vile ilivyoangaziwa katika kifungu cha 123.123.7). Kama halmashauri ya kanisa itaamua kwamba haitaita tena msaidiizi wa mchungaji, uamuzi kama huo utahitaji idhini ya msimamizi wa wilaya na theluthi mbili za kura za washirika wa kanisa la mtaa.

## I. Uhusiano wa Mchungaji na Kanisa

**122.** Kila mwaka, mchungaji na halmashauri ya kanisa watasimamia kipindi cha mpango wa kufanya upya matarajio na malengo ya kanisa na mchungaji. Makubaliano ya malengo yaliyoandikwa, mipango na mikakati kati ya kanisa na mchungaji yatafanywa upya. Makubaliano kama hayo yaliyoandikwa yatajazwa na msimamizi wa wilaya. (115.2, 129.4)

**122.1.** Wachungaji na waumini wanapaswa kujitahidi kuelewa vizuri matarajio ya kila mmoja na kutatua tofauti ambazo ziko kwa kufuata kanuni za kibiblia zikiwa ni pamoja na zile zinazopatikana katika Mathayo 18:15-20 na Wagalatia 6:1-5. Katika moyo wa ushirikiano na mapatano katika kanisa,

1. Watu binafsi au washirika wa kusanyiko watahimizwa kusuluhisha tofauti kwa kwa kujadiliana uso kwa uso na mchungaji au kwa uangalifu na mshirika wa halmashauri ya kanisa.
2. Ikiwa majadiliano ya ana kwa ana yatashindwa kuleta suluhisho, mtu anayelalamika atatafuta usaidizi wa mtu mmoja au wawili katika kusuluhisha tofauti hizo.
3. Mtu anayehusika katika jitahadi za kundi dogo kama hilo atapeleka tofauti zilizoko kwa halmashauri ya kanisa ikiwa tu juhudi za majadiliano ya ana kwa ana na za kundi dogo zimeshindwa kusuluhisha tofauti hizo. Halmashauri ya kanisa ikihitajika, itatumika katika kusuluhisha tofauti katika moyo wa upendo, kukubaliana, na kusameheana, na kulingana na nidhamu ya kanisa. (123-126.2, 129.1)

## J. Kuchunguza Upya Uhusiano
### Kati ya Mchungaji na Kanisa la Mtaa

**123. Ukaguzi wa Kawaida wa Uhusiano wa Kanisa na Uchungaji**. Uhusiano kati ya kanisa na mchungaji utachunguzwa na halmashauri ya kanisa, ikikutana pamoja na msimamizi wa wilaya, au mhudumu aliyewekwa wakfu, au muumini aliyeteuliwa na msimamizi wa wilaya, katika kipindi cha siku 60 za mwaka wa pili wa huduma ya uchungaji, na kila baada ya kila miaka minne baadaye. Katika mkutano wa uchunguzi, swala la kuendelea kuwa uhusiano kati ya kanisa na mchungaji yatajadiliwa. Lengo ni kutafuta kuafikiana bila hitaji la kura rasmi za halmashauri ya kanisa.

**123.1.** Msimamizi wa wilaya, au mhudumu aliyewekwa wakfu au muumini aliychaguliwa na msimamizi wa wilaya, atasimamia kupanga na kuongoza mikutano ya uchunguzi na halmashauri ya kanisa. Msimamizi wa wilalya ataamua njia ya uchunguzi. Mikutano ya uchunguzi itapangwa kwa kushauriana na mchungaji. Mikutano hiyo itaendelezwa katika sehemu ya mamlaka (halmashauri ya wilaya, ikiwa ni pamoja na mchungaji). Katika uamuzi wa msimamizi wa wilaya, sehemu ya uchunguzi inaweza kuendelezwa wakati mchungaji hayupo. Ikiwa mke au mume wa mchungaji ni mshirika aliyechaguliwa wa halmashauri, yeye hatahusika katika uchunguzi. Zaidi ya yote, watu wa karibu wa familia ya mchungaji wataondolewa kwa uchunguzi, kwa kuombwa na msimamizi wa wilaya au mwakilishi aliyechaguliwa.

**123.2.** Tangazo la hadhara ambalo limechapishwa linaloeleza kusudi la mkutano wa halmashauri ya kanisa litepelekwa kwa kusanyiko la Jumapili kabla ya halmashauri ya kanisa na msimamizi wa wilaya kukutana kwa sababu ya uchunguzi wa kawaida wa uhusiano wa kanisa na mchungaji.

**123.3.** Ikiwa halmashauri ya kanisa haitapiga kura ya kuwakilisha swala la kuendelea kuwa na uhusiano wa kanisa na uchungaji kwa ushirika wa kanisa, uhusiano wa kanisa na uchungaji utaendelea.

**123.4.** Halmashauri ya kanisa inaweza kupiga kura ya kupeleka kwa washirika wa kanisa swala la kuendeleza mwito wa uchungaji. Kura ya halmashauri itapigwa kwa siri na kuhitaji theluthi mbili za kura ya washirika wote wa halmashauri ya kanisa walioko mkutanoni.

**123.5.** Ikiwa halmashauri ya kanisa itapiga kura ya kukubali swala la kuendeleza uhusiano wa uchungaji lipelekwe kwa washirika wa kanisa, jambo hilo litawasilishwa katika mkutano wa kanisa uliyoitishwa rasmi kwa kusudi hilo na utafanyika katika kipindi cha siku 30 baada ya hatua hiyo kuchukuliwa. Swali litaulizwa, “Je, uhusiano wa sasa kati ya

mchungaji na kanisa uendelee?" Kura itapigwa kwa siri na itahitajika iwe na wingi wa theluthi-mbili za kura zote zitakazopigwa ili ukubalike, isipokuwa katika nchi ambayo sheria inaagiza utaratibu tofauti kufuatwa.

**123.6.** Ikiwa kura za ushirika wa kanisa za kuamua uhusiano wa kanisa na uchungaji uendelee, uhusiano huo utaendelea kana kwamba kura hiyo haikupigwa; isipokuwa hivyo, uhusiano wa kanisa na uchungaji utamalizika tarehe iliyowekwa na msimamizi wa wilaya isiyo chini ya siku 30 wala zaidi ya siku 180 zitakazofuata kupigwa kwa kura. Ikiwa mchungaji atachagua kutoendelea na kura ya uamuzi wa washiriki au achague kukataa kura, atahitajika kutoa barua ya kujiuzulu kwake. Hatua kama hiyo ikichukuliwa, uhusiano wa kiuchungaji kati yake na kanisa utaisha tarehe ambayo itaamuliwa na msimamizi wa wilaya isio chini ya siku 30 wala zaidi ya siku 180 zitakazofuata baada ya uamuzi huo wa kutoendelea na kura ya uamuzi wa washiriki. (120)

**123.7.** Kama sehemu ya ukaguzi wa kawaida, taarifa au ripoti itapelekwa kwa msimamizi wa wilaya na mchungaji na halmashauri ya kanisa kuhusu maendeleo yaliofikiwa katika kutimiza kusudi, maono na maadili ya kimsingi ya kanisa.

**124.** Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wahesabu kura mwenyewe binafsi atamjulisha mchungaji matokeo ya kura ya uchungaji kabla ya tangazo lolote rasmi kutangazwa hadharani.

**125. Ukaguzi Maalum wa Uhusiano wa Kiuchungaji na Kanisa.** Kabla ya wakati wa ukaguzi wa kawaida kuwadia, mkutano wa halmashauri ya kanisa la mtaa utakuwa kikao maalum rasmi cha ukaguzi kwa kura za wingi peke yake za halmashauri yote ya kanisa iliyochaguliwa na msimamizi wa wilaya au kasisi aliyeteuliwa na msimamizi wa wilaya akiwepo na kutumika kama mwenyekiti.

**125.1.** Mkutano huu maalum wa ukaguzi wa uhusiano kati ya mchungaji na kanisa utaendelezwa katika sehemu ya ofisi mamlaka (halmashauri ya kanisa, ikiwemo pamoja na mchungaji). Kwa uamuzi wa msimamizi wa wilaya, sehemu ya ukaguzi inaweza kuendelezwa bila kuwepo kwa mchungaji. Katika hali ambayo mke au mume wa mchungaji ni mshirika aliyeteuliwa na halmashauri, huyo mke au mume hatahusika katika ukaguzi. Zaidi, msimamizi wa wilaya au mwakilishi aliyechaguliwa anaweza kuwaondoa washirika wa karibu wa familia ya mchungaji kutoka kwa ukaguzi.

**125.2.** Ikiwa msimamizi wa wilaya na halmashauri ya kanisa wataamua kwamba swala la kuendelea kwa uhusiano wa kiuchungaji na kanisa linapaswa kuwasilishwa kwa kanisa, msimamizi wa wilaya na halmashauri ya kanisa kwa theluthi mbili ya kura zitakazopigwa na washirika wote

walioko, ikiwa sheria za nchi hiyo haziagizi utaratibu tofauti kufuatwa, wanaweza kuagiza swala hilo lipigiwe kura kwenye mkutano maalum wa kanisa. Swali hilo litawasilishwa kama ifuatavyo: "Je, uhusiano wa sasa kati ya mchungaji na kanisa uendelee?"

**125.3.** Ikiwa kwa theluthi-mbili ya kura zilizopigwa kwa siri na washirika wa kanisa waliofikia umri wa kupiga kura, walioko mkutanoni na wanapiga kura, isipokuwa mahali ambapo sheria ya nchi ina utaratibu tofauti, kanisa litaamua kuendeleza uhusiano wa kiuchungaji na kanisa, kipindi cha ofisi cha mchungaji kitaendelea kana kwamba ukaguzi huo maalum haukufanyika.

**125.4.** Hata hivyo, ikiwa kanisa litakosa kuamua kwa kupiga kura kuendeleza uhusiano ulioko wa kiuchungaji na kanisa, kipindi cha huduma ya mchungaji kitamalizika tarehe itakayowekwa na msimamizi wa wilaya, siku zisizozidi 180 baada ya kura hiyo kupigwa.

**125.5.** Ikiwa mchungaji atachagua kukosa kuendelea na kura za waumini au achague kukosa kuzikubali kura hizo, atatoa barua ya kujiuzulu. Wakati huo, uhusiano wa kiuchungaji na kanisa utakamilika tarehe ambayo itawekwa na msimamizi wa wilaya, siku zisizozidia 30 au zaidi ya siku 180 kufuatana na uamuzi wa mchungaji wa kukosa kuendelea na kura za waumini au kukosa kuzikubali. (113.8, 123-124)

**126. Kanisa la Mtaa Lenye Mzozo.** Inapofahamika kwamba kanisa la mtaa linaelekea kukabiliwa na mzozo, msimamizi wa wilaya akiruhusiwa na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya, atakuwa na mamlaka ya kuteua kamati ya kuchunguza hali ilivyo na kutekeleza hatua zinazohitajika kuepuka mzozo huo. Kamati hiyo itakuwa na makasisi wawili na waumini wawili ambao ni washirika wa Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya pamoja na msimamizi wa wilaya, ambaye atatumika kama mwenyekiti wake. (211.3)

**126.1.** Ikiwa kwa maoni ya msimamizi wa wilaya na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya kanisa la mtaa linalokabiliwa na mzozo-matatizo ya pesa, maadili, kuvunjika moyo au ya aina nyingine yote na mzozo huo unatatiza uthabiti na hali ya baadaye ya kanisa hilo, (a) swala la kuendelezwa kwa uhusiano wa kiuchungaji na kanisa linaweza kuwasilishwa kwa waumini wa mtaa na msimamizi wa wilaya au mshirika wa Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya aliyeteuliwa na msimamizi wa wilaya kana kwamba halmashauri ya kanisa ilikuwa imeomba kura chini ya kifungu cha 123-123.7, au (b) kipindi cha huduma ya mchungaji na cha halmashauri ya kanisa kinaweza kukatizwa kwa idhini ya msimamizi mkuu wa eneo hilo, na kwa wingi wa kura za Halmashauri ya Wilaya. Msimamizi wa wilaya, kwa idhini ya msimamizi mkuu na Halmashauri ya Wilaya,

anaweza kuteua washirika wa halmashauri ya kanisa katika kanisa lolote ambalo limetangazwa kuwa katika mzozo. Tendo la taarifa ya Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya itapelekwa kwa msimamizi mkuu wa eneo hilo katika siku 30. (211.3)

**126.2.** Wakati wa maoni ya msimamizi wa wilaya, kanisa la mtaa linalotangwa kuwa katika mzozo kufuatana na kifungu cha 126.1 limetimiza kuingiliwa kati kulikotumiwa na liko tayari kurudi kwa huduma yake katika hali ya kawaida, kanisa la mtaa linaweza kutangazwa kuwa mzozo umekwisha kwa wingi wa kura za Halmashauri ya Wilaya. Msimamizi mkuu wa eneo hilo atajulishwa hatua ya Halmashauri ya Wilaya katika siku 30. (211.4)

## K. Halmashauri ya Kanisa Mtaa

**127. Ushirika.** Kila kanisa la mtaa litakuwa na halmashauri ya kanisa, ambayo iko na mchungaji, msimamizi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa, mwenyekiti wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, mwenyekiti wa Umisheni wa Mnazareti wa Kimataifa, mawakili, na wadhamini wa kanisa, na washirika wa Halmashauri ya Huduma ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa ikiwa wamechaguliwa kama Kamati ya Elimu ya halmashauri ya kanisa na mkutano wa mwaka wa kanisa. Ikiwa mwenyekiti wa umisheni ni mke au mume wa mchungaji, na ameamua kutotumika katika halmashauri ya kanisa, naibu wake anaweza kuhudumu; hata hivyo ikiwa mwenyekiti ni mke au mume wa mchungaji na amechagua kutumika kwa halmashauri, hatakuwa sehemu ya hatua ya ukaguzi ya uhusiano wa kanisa na kiuchungaji wa mchungaji.

Halmashauri ya kanisa hairuhisiwi kuwa na washirika zaidi ya 25 kwa wakati mmoja. Wahudumu waliowekwa wakfu na wenye hati za wilaya bila kuhusisha watu walioidhinishwa na mchungaji na msimamizi wa wilaya na wafanyakazi wa kulipwa wa kanisa la mtaa hawastahili kutumika katika halmashauri ya kanisa ya mtaa. Msimamizi wa wilaya kwa pendekezo la mchungaji na halmashauri ya wilaya, anaweza kutoa hati ya wahudumu wa wilaya ambao hawapewa na ambao ni wanafunzi wa Masomo ya Biblia au ni wanafunzi katika chuo cha Mnazareti cha elimu ya juu. Wahudumu hao wataondolewa kwa hatua ya halmashauri ya wilaya inayohusu pendekezo la wahudumu kwa kikao cha wilaya ili kufanya upya hati za kuhudumu za wilaya.

Tunaagiza makanisa yetu ya mtaa kuchagua kama viongozi wa kanisa watu ambao wanadhihirisha wazi ujuzi wa utakaso kamili na ambao maisha yao ni ushuhuda wa wazi wa neema ya Mungu inayotuhitaji kuishi maisha

ya utakatifu; wanaokubaliana kikamilifu na mafundisho, uongozi na utaratibu wa Kanisa la Mnazareti; na ambao wanasaidia na kutegemeza kanisa la mtaa kwa maudhurio, zaka au fungu la kumi na sadaka kwa uaminifu. Viongozi wa kanisa wanapaswa kuhusika kikamilifu katika "kuwafanya wanafunzi kama Mfano wa Kristo katika mataifa." (33, 113.11, 137, 141, 145-147, 152, 159.4)

**127.1.** Wakati mkutano wa wilaya wa kanisa la mtaa unakuweko katika kipindi cha kubadilishwa kwa uchungaji, kamati ya uteuzi ya mtaa, ikisimamiwa na msimamizi wa wilaya, kwa idhini ya msimamizi wa wilaya, itapeleka azimio kwenye kusanyiko, katika siku zisizozidi 30 kabla ya mkutano wa mwaka, kuhifadhi halmashauri ya kanisa ya wakati huu kwa ajili ya mwaka wa kanisa unaofuata. Mazimio hayo yanaweza kukubaliwa na wingi wa kura za siri za washirika wa kanisa wa umri wa kupiga kura walioko na kupiga kura katika mkutano maalum wa kanisa uliopangwa vizuri. Azimio hilo lisipo kubaliwa,, halmashauri ya kanisa itachaguliwa na mkutano wa mwaka kama ilivyo kawaida.

**128. Mikutano.** Halmashauri ya kanisa itaanza kazi yake mwanzo wa mwaka wa kanisa na itakuwa na mikutano ya kawaida katika kipindi cha siku 15 za kwanza za kila mwezi, na itakutana kwa mkutano maalum ukiitwa na mchungaji, msimamizi wa wilaya. Katibu wa halmashauri ya kanisa ataita mkutano maalum wa halmashauri kwa idhini ya mchungaji, au ya msimamizi wa wilaya mchungaji asipokuwepo. Mikutano ya halmashauri ya kanisa, ikiwa n pamoja na kupiga kura, inaweza kufanyika kwa njia ya elektroniki, mikutano kama hiyo na kura itakuwa na nguvu na matokeo sawa sawa na kura za mkutano wa washirika waliokusanyika katika chumba kimoja au sehemu moja. Katikati ya mkutano wa mwaka na mwanzo wa mwaka wa kanisa, halmashauri mpya ya kanisa iliyochaguliwa inaweza kukutana kwa kusudi la kujiandaa, na wakati wa mkutano huo itachagua katibu wa kanisa, mtunza hazina, na afisa mwingine ye yote ambaye itakuwa ni wajibu wake kuchagua, kama ilivyoelezwa hapa. [129.19-130]

**129. Shughuli. Shughuli za halmashauri ya kanisa** zitakuwa ni:

**129.1.** Kushughulikia maslahi na kazi za kanisa, ambazo hazikutajwa hapa, ikishirikiana na mchungaji. (155, 518)

**129.2.** Kuteua kwenye kanisa, baada ya kushauriana na msimamizi wa wilaya, kasisi au mhudumu yeyote aliyepewa hati (alama ya kasisi) ambaye anafaa kuwa mchungaji, mradi uteuzi huo umeidhinishwa kufuatana na kifungu cha 115. (159.8, 211.10, 225.16)

**129.3.** Kushirikiana na mchungaji mpya kutayarisha taarifa ya shabaha au lengo na matarajio ya kanisa na mchungaji. (115.2)

**129.4.** Kuongoza aghalau kwa mwaka mmoja, akiwa pamoja na mchungaji, sehemu ya mpangilio wa kusudi la kufanya upya ufahamu ulioandikwa wa matarajio, shabaha na mafanikio, shabaha na mafanikio. (122)

**129.5.** Kutayarisha jinsi ya kupata huduma ya uchungaji, baada ya kushauriana na msimamizi wa wilaya, hadi wakati ule mchungaji atakapopatikana na kuitwa na kanisa. (212. 524)

**129.6.** Kufanya matayarisho ya kuandaa na kukubaliwa kwa bajeti ya kanisa, Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa, Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa, shule yoyote ya malezi (iliyoanzishwa kupitia shule ya upili) yakionyesha mapato na matumzi yao.

**129.7.** Kuipa kamati ya halmashauri ya kanisa wajibu wa: (a) kuchunguza bajeti ya kanisa, (b) kuripoti kwa halmashauri ya kanisa hali ya pesa ilivyo na mahitaji ya kanisa.

**129.8.** Kuamua kiwango cha malipo ya mchungaji na faida zingine, zikiwemo faida za kustaafu, ambazo mchungaji atapokea, na kuyachunguza upya aghalau mara moja kwa mwaka. (32.3, 115.4, 115.6, 123-123.7)

**129.9.** Kupendekeza njia na namna za kumtegemeza mchungaji, huduma ya uchungaji, au wafanyakazi wengine wa kulipwa na kanisa; kutia moyo na kutegemeza kwa kupanga na makadirio ya fedha, hitaji la kuendeleza elimu ya mchungaji na wafanyakazi wengine wa kanisa wakati wote watakapokuwa hai. (115.4)

**129.10.** Ili kutia moyo kujifunza kwa mchungaji maishani mwake kuimarisha hali ya kiroho, halmashauri ya kanisa, ikishauriana na msimamizi wa wilaya, wanapaswa kufikiria kulipia gharama ya likizo (sabato) ya masomo kwa mchungaji katika mwaka wake wa saba mfululizo wa kulihudumia kanisa moja. Muda na wakati wa likizo ya sabato utamuliwa kwa kushauriana na mchungaji, halmashauri ya kanisa na msimamizi wa wilaya. Inahimizwa kwa bidii kwamba mshahara wa mchungaji uendelee kamili na halmashauri ya kanisa itatafuta mchungaji msaidizi wakati wa kipindi cha sabato cha mchungaji. Mada haya yatashughulikiwa na msimamizi wa wilaya kama sehemu ya hatua ya kuchunguza uhusiano wa kiuchungaji na kanisa ambao utakuwepo baada ya miaka miwili na tena katika miaka sita, mara tu uwezekano wa kuendeleza uhusiano umeanzishwa. Vifaa vitatengenezwa na kutolewa na ofisi ya Ujenzi ya Ulimwengu ya Kuhudumu ili kuongoza kusanyiko la mtaa katika kuanzisha na kutekeleza sera na utaratibu wa likizo ya sabato. Katika uamuzi wa halmashauri ya kanisa, utaratibu huo unaweza kutekelezwa kwa washirika wa ofisi ya kiuchungaji.

**129.11.** Ili kuamua kiasi cha pesa za kumtegemeza na kulipia nyumba ambacho muinjilisti anafaa kupokea na kumjulisha muinjilisti huyo kiasi hicho wakati wa kuitwa na halmashauri ya kanisa.

**129.12.** Kutoa hati au kuidhinisha kutolewa upya kwa hati, ikiona ni vyema, mtu yeyote ambaye amependekezwa na mchungaji kwa (a) mhudumu wa mtaa, au (b) muumini mhudumu. (503.3-503.5, 531.1-531.3, 813)

**129.13.** Kupendekeza kwa kikao cha wilaya, ikiona ni vyema, baada ya uteuzi wa mchungaji, mtu yeyote anayetaka kupata hati ya mojawapo ya huduma, hii ikiwa ni pamoja na waumini na wahudumu, wanaotaka kutambuliwa kwa huduma zinazotekelezwa nje ya mipaka ya kanisa la mtaa, ikiwa pendekezo hilo linahitajika na Manual.

**129.14.** Kupendekeza kwa kikao cha wilaya, ikiona ni vyema, baada ya uteuzi wa mchungaji, mtu ye yote anayetaka cheti cha kuthibitisha mhudumu aliyepewa hati, au anayetaka hati hiyo iidhinishwe upya. (531.5, 532.1)

**129.15.** Kupendekeza kwa kikao cha wilaya, ikiona ni vyema, baada ya uteuzi wa mchungaji, kutolewa upya kwa hati ya shemasi wa kike kulingana na kifungu cha 408.

**129.16.** Kuchagua, baada ya uteuzi wa Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa, kwa idhini ya mchungaji, mkurugenzi wa Huduma za Watoto na mkurugenzi wa Huduma za Watu Wazima. (145.6)

**129.17.** Kuidhinisha kiongozi wa vijana aliyechaguliwa na Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya kanisa la mtaa, kulingana na Mkataba wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.

**129.18.** Kuidhinisha kuchaguliwa kwa wasimamizi wa shule zinazomilikiwa na Kanisa la Mnazareti za malezi, (shule za kawaida). (151, 159.1, 211.13, 516.10)

**129.19.** Kuchagua katibu katika mkutano wa kwanza wa halmashauri mpya ya kanisa, kutokana na washirika wa kanisa, anayestahili kuwa kiongozi wa kanisa kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 33. Uchaguzi kama huo utafanywa katika mkutano wa kwanza wa halmashauri mpya. Mtu atakayechaguliwa atatumika hadi mwisho wa mwaka wa kanisa na hadi mwandamizi wake atakapochaguliwa na kuhitimishwa, na anazo faida za kura wakati ule amechaguliwa na halmashauri ya kanisa katika mkutano wa washirika ulioandaliwa vyema na kusanyiko. (33, 113.6-113.8, 113.11, 128, 135.1-135.7)

**129.20.** Kuchagua mtunza hazina kati ya washirika wa kanisa ambao wanatimiza sifa za viongozi wa kanisa kama vile ilivyoelezewa katika

kifungu cha 33. Uchaguzi kama huo utafanywa katika mkutano wa kwanza wa halmashauri mpya. Mtu huyo atakayechaguliwa atatumika hadi mwisho wa mwaka wa kanisa na hadi mwandamizi wake atakapochaguliwa na kuhitimishwa, na anazo haki za kupita kura wakati ule tu amechaguliwa kwa halmashauri ya kanisa kwa mkutano wa washirika wa kusanyiko kwa wakati unaofaa. Mshirika wa karibu wa familia ya mchungaji hatatumika kwa hazina ya kanisa la mtaa bila idhini ya msimamizi wa wilaya na Halmashauri ya Wilaya. Watu wa familia ya karibu ni pamoja na mke au mume wa mchungaji, watoto, ndugu au dada, au wazazi. (33, 113.7-113.8, 113.11, 128, 136.1-136.6)

**129.21.** Kuhakikisha kwamba hesabu ya pesa zote zinazopokelewa na kutumiwa na kanisa, zikiwa ni pamoja na zile za shule ya malezi (zile za shule ya upili) na Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa, Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa, zinaandikwa na kuhifadhiwa kwa uangalifu, na kutoa ripoti ya hesabu ya pesa hizo katika mikutano yake ya kila mwezi na katika mkutano wa mwaka wa kanisa. (136.3-136.5)

**129.22.** Kuunda kamati ya washirika wawili au zaidi ambao watahesabu na kuwajibika kwa pesa zote zinazopokelewa na kanisa.

**129.23.** Kuteua kamati ya ukaguzi au kamati binafsi ya watahini, au watu waliohitimu, ambao watakagua au kutahini, kwa aghalau kiwango kisichopungua kinachohitajika na taifa au sheria za nchi kama inakubalika, au shirika za viwango zinazotambuliwa, aghalau kila mwaka, rekodi za fedha za mweka hazina wa kanisa, Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa, shule za malezi, chekechea (kuanzishwa kupitia Shule ya Upili), na rekodi zingine zozote za fedha za kanisa. Mchungaji atakuwa na haki ya kutazama rekodi zote za kanisa la mtaa.

**129.24.** Kuunda Kamati ya Uinjilisti na Ushirika ya Kanisa yenye washirika wasiopungua watatu. [110]

**129.25.** Kufanya kazi, ikiwa ni vyema kama Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa katika makanisa ambayo hayana washirika zaidi ya 75. (145)

**129.26.** Kuteua kamati ya mashtaka yenye watu watano ikiwa kuna mashtaka yaliyoletwa dhidi ya mshirika wa kanisa kwa maandishi. (605)

**129.27.** Kuchagua, kwa idhini iliyoandikwa ya msimamizi wa wilaya, na baada ya uteuzi wa mchungaji, wasaidizi wa kulipwa kama itakavyohijika na kanisa la mtaa. (151, 159-159.1, 211.13)

**129.28.** Kuchagua mhudumu wa mtaa au mhudumu aliyepewa hati, awe msaidizi wa mchungaji asiyelipwa, mradi idhini itatolewe na msimamizi wa wilaya kila mwaka kwa maandishi. (115.6)

**129.29.** Kuunda kamati ya kupanga mipango ya muda mrefu ya kanisa ambayo mwenyekiti wake atakuwa ni mchungaji.

**129.30.** Kuandaa na kutekeleza mpango wa kupunguza hatari ambazo watu waliowekwa katika nafasi za mamlaka kanisani wanaweza kutumia nafasi hizo au mamlaka yao kufanya mambo yasiofaa. Mpango wa kila kanisa la mtaa ni lazima utilie maanani hali za kipekee za kanisa hilo zinaweza kusababisha kutokea kwa jambo hilo.

**130.** Halmashauri ya kanisa, pamoja na mchungaji, itafuata mipango iliyoandaliwa na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu na Halmashauri ya Kikao Kikuu ya kukusanya pesa za Hazina ya Uinjilisti wa Dunia na Fedha za Huduma za Wilaya katika kanisa la mtaa, na litatoa idadi ya pesa hizi kila mara kwa mweka hazina mkuu na mweka hazina wa wilaya, kwa wakati mmoja. (317.10, 335.7)

**131. Maana ya Uwakili.** Rejelea kifungu cha 32-32.5.

**132.** Halmashauri ya kanisa itafanya kazi ya Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili katika kanisa lililoratibiwa hivi karibuni hadi halmashauri hiyo itakapochaguliwa rasmi. (145)]

**132.1.** Halmashauri ya kanisa lililoratibiwa hivi karibuni pamoja na mchungaji wataamua wakati unaofaa wa kumchagua msimamizi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa. (129.25, 145, 146)

**133.** Halmashauri ya kanisa inaweza kuondoa katika orodha ya Ushirika wa kanisa jina la mshirika ambaye hashiriki kikamilifu baada ya kipindi cha miaka miwili kupita tangu tarehe ambayo jina hilo liliwekwa katika orodha ya washirika wasioshiriki kikamilifu. (109-109.4, 112.3)

**134.** Halmashauri ya kanisa inaweza kusimamisha kwa muda au kubatilisha hati ya mtu yeyote aliyeidhinishwa na kanisa la mtaa kuwa mhudumu.

**135. Katibu wa Kanisa. Kazi ya katibu wa halmashauri ya kanisa** itakuwa ni:

**135.1** Kuandika kwa usahihi na kuhifadhi kwa uaminifu muhtasari wa yaliyojadiliwa katika mikutano yote ya kanisa na mikutano ya halmashauri ya kanisa, na kufanya mambo mengine yanayohusiana na ofisi yake. Muhtasari wa halmashauri unafaa kutambua washirika wote wa halmashauri wa kupiga kura walioko na wale wasiokuwepo kwa kuweka idadi iliyo sawa ya maandishi. (120.1, 129.19)

**135.2.** Kuwasilisha kwa mkutano wa mwaka wa kanisa ripoti ya mwaka ya mambo muhimu yaliyotendeka katika kanisa la mtaa, hii ikiwa ni pamoja na tarakimu za ushirika wa kanisa. (113.9)

**135.3.** Kuhakikisha kwamba makaratasi rasmi, kumbukumbu, na hati za kisheria zinazohusu kanisa la mtaa, ikiwa ni pamoja na hati za kumiliki, mikataba ya bima, hati za mkopo, orodha za ushirika wa kanisa, rekodi za historia, muhtasari wa majadiliano ya halmashauri ya kanisa, na hati za kuungwa au kusajiliwa kwa kanisa kuwa shirika, zinahifadhiwa kwa udhamini mahali ambapo haziwezi kuteketea kwa moto au katika kasha la kuhifadhia vitu katika jengo la kanisa, au inapowezekana zihifadhiwe katika makasha ya benki au mashirika mengine kama hayo. Mchungaji na mtunza hazina daima watakuwa na haki ya kufikia hati na kumbukumbu hizo, na wajibu huo utakabidhiwa kwa mwandamizi wa katibu mara tu atakapochaguliwa.

**135.4**. Kuwa katibu ama karani katika mikutano yote ya mwaka na mikutano maalum ya kanisa; na mhifadhi wa kumbukumbu zote na muhtasari wa majadiliano ya mikutano hiyo ya kanisa. (113.6)

**135.5.** Kuthibitisha kwa msimamizi wa wilaya kwa maandishi matokeo ya kura ya kumwita mchungaji na kura ya kuendelezwa kwa uhusiano wa uchungaji. Thibitisho hilo litatolewa katika kipindi cha wiki moja baada ya kupigwa kwa kura hiyo.

**135.6** Kutuma kwa msimamizi wa wilaya nakala ya muhtasari wa majadiliano ya mikutano yote ya kanisa na mikutano ya halmashauri ya kanisa katika kipindi cha siku tatu baada ya mikutano hiyo kufanyika, ikiwa kanisa hilo halina mchungaji.

**135.7.** Kutia sahihi, pamoja na mchungaji, hati zote za majengo na viwanja vya kanisa, hati za amana, na kurudishwa kwa vitu vilivyowekwa rehani, mikataba na hati zingine za kisheria ambazo hazikutajwa katika Kitabu cha Mwongozo. (102.3, 103-104.2)

**136. Mtunza Hazina. Kazi ya mtunza hazina** wa halmashauri ya kanisa itakuwa ni:

**136.1.** Kupokea pesa zote ambazo hazikupangiwa kupokewa na mwingine na kuzitoa tu kwa amri ya halmashauri ya kanisa. (129.21)

**136.2.** Kulipa malipo ya kila mwezi kwa mtunza hazina wa wilaya, ya pesa zote zilizopangwa kwa wilaya na malipo yaliotengwa kwa kanisa kuu kwa mtunza hazina mkuu, isipokuwa kama imepangwa tofauti na hivyo. (516.9)

**136.3.** Kuweka kitabu cha rekodi/kumbukumbu sahihi ya pesa zote zilizopokewa na kutumiwa. (129.21)

**136.4.** Kutayarisha ripoti ya fedha kila mwezi yenye maelezo kamili ambayo itatolewa kwa halmashauri ya kanisa. (129.21)

**136.5.** Kuwasilisha ripoti ya mwaka ya fedha kwa mkutano wa mwaka wa kanisa. (113.9, 129.21)

**136.6.** Kukabidhi kwa halmashauri ya kanisa rekodi/kumbukumbu zote kamili za mtunza hazina wakati atakapoacha wadhifa wa mtunza hazina.

## L. Mawakili wa Kanisa la Mtaa

**137.** Mawakili wa kanisa hawatakuwa chini ya watatu wala zaidi ya 13 kwa idadi. Watachaguliwa kwa kura ya siri, wakati wa mkutano wa mwaka au mkutano maalum wa kanisa, kutumika kwa mwaka unaofuata wa kanisa, na hadi waandamizi wao watakapochaguliwa na kuhitimishwa. (33, 113.7, 113.11, 127)

**138. Kazi ya mawakili** itakuwa ni:

**138.1.** Kutumika kama kamati ya ustawi wa kanisa, ikiwa hakuna utartatibu mwingine uliowekwa, yenye wajibu wa kuwafikia wengine, uinjisti, na kusambaa kwa kanisa, hii ikiwa ni pamoja na kudhamini makanisa mapya na vituo vya kuhubiri, mchungaji akiwa ndiye mwenyekiti wake.

**138.2.** Kutoa msaada kwa, na kutegemeza wenye mahitaji na dhiki. Madaraka ya kibiblia ya viongozi waumini ni kuhudumu katika sehemu zinazohitaji utumishi unaotekelezwa (Warumi 12:6-8). Kwa hivyo mawakili wanapaswa kutoa wakati wao na vipawa vyao vya kiroho kuwahudumia au kuwatumikia wengine, kuongoza, kutia watu moyo, kurehemu, kutembelea na kufariji wenye huzuni, na huduma zingine kama hizo.

**138.3.** Kutumika kama Kamati ya Uinjilisti na Ushirika wa Kanisa, halmashauri ya kanisa ikiona ni vyema, kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 110-110.8.

**138.4.** Kusaidia mchungaji katika kutayarisha kanisa ili nafasi za utumishi wa Kikristo ziweze kupatikana na washirika wote. Kunapaswa kuwa na uangalifu maalum katika ustawishaji wa huduma kwa watu wa utamaduni mwingine tofauti wanaoishi karibu na kanisa.

**138.5.** Kutumika kama waunganishaji wa shughuli za Kikristo katika jamii na kwa makundi yanayotoa huduma au kutumikia watu.

**138.6.** Kumsaidia mchungaji wakati wa ibada ya hadhara na katika malezi ya Kikristo ya kuimarisha waumini katika kanisa la mtaa.

**138.7.** Kutayarisha vifaa vya Meza ya Bwana, na wakiulizwa na mchungaji, kusaidia kugawanya vifaa hivyo. (29.5, 515.4)

**139.** Kukitokea nafasi katika ofisi ya wakili, nafasi hiyo inaweza kujazwa na kanisa la mtaa kwenye mkutano rasmi wa kanisa. (113.8)

**140**. Mawakili watakuwa ni pamoja na Kamati ya Uwakili, ambayo kazi yake itakuwa ni kuendeleza hali ya uwakili wa Kikristo wa raslimali za maisha katika kanisa la mtaa kwa kushirikiana na mchungaji na ofisi ya Huduma za Uwakili. (32-32.5)

### M. Wadhamini wa Kanisa la Mtaa

**141.** Wadhamini wa kanisa hawatakuwa chini ya watatu wala zaidi ya tisa. Watachaguliwa kutoka katika washirika wa kanisa la mtaa kutumika kwa mwaka unaofuata wa kanisa na hadi waandamizi wao watakapochaguliwa na kuhitimishwa. (33, 113.11, 127)

**142.** Katika sehemu zote ambazo sheria ya nchi inahitaji utaratibu fulani ufuatwe katika uchaguzi wa wadhamini wa kanisa, utaratibu huo utafuatwa kikamilifu. (113.4)

**142.1.** Mahali ambapo hakuna utaratibu wa uchaguzi uliowekwa na sheria ya nchi wadhamini watachaguliwa kwa kura ya siri wakati wa mkutano wa mwaka wa kanisa la mtaa au wakati wa mkutano maalum ulioitishwa rasmi kwa kusudi hilo. (113.7, 113.11)

**143. Kazi ya wadhamini** ni:

**143.1.** Kutunza hati za mali ya kanisa na kuisimamia mali hiyo kama wadhamini wa kanisa la mtaa, mahali ambapo kanisa la mtaa halijaungwa au kusajiliwa kama shirika, au mahali ambapo sheria ya nchi inaagiza hivyo, au mahali ambapo msimamizi wa wilaya au Halmashauri ya Wilaya itaona ni bora zaidi kwa sababu fulani, chini ya mwongozo na mipaka iliyowekwa katika 102-104.4.

**143.2.** Kutoa mwongozo wa kustawisha majengo na viwanja vya kanisa pamoja na mipango ya kifedha, isipokuwa halmashauri ya kanisa iwe imefanya matayarisho mengine.

**144.** Nafasi katika ofisi ya mdhamini inaweza kujazwa na kanisa la mtaa wakati wa mkutano wa kanisa ulioitishwa rasmi. (113.8)

### N. Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa Kanisa la Mtaa

**145.** Kila kanisa la mtaa litaanzisha **Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa (HSJUK)**, au **Kamati ya Elimu** kama sehemu ya halmashauri ya kanisa, wakati wa mkutano wa mwaka wa kanisa, itakayosimamia huduma za elimu ya Kikristo katika kanisa. Katika makanisa yenye washirika 75, au wachache, wajibu huo unaweza kutekelezwa na halmashauri ya kanisa. Washirika watakuwa ni:

msimamizi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa; mchungaji; mwenyekiti wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa; mwenyekiti wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa; mkurugenzi wa Huduma za Watoto; mkurugenzi wa Huduma za Watu Wazima; na watu wengine watatu hadi tisa waliochaguliwa miongoni mwa washirika wa kanisa wakati wa mkutano wa mwaka wa kanisa. Washirika wanaweza kuchaguliwa kwa muda tofauti wa vipindi vya miaka miwili (2) na watatumika hadi mwisho wa mwaka unaofuata wa kanisa, na hadi waandamizi wao watakapochaguliwa na kuhitimishwa. Mshirika aliyechaguliwa akiacha kazi, nafasi yake inaweza kujazwa katika mkutano ulioitishwa rasmi na kanisa. Ikiwa kanisa litachagua kamati ya elimu kama sehemu ya halmashauri ya kanisa, lazima lifuate maagizo ya *Kitabu cha Mwongozo* yanayohusu idadi ya chini kabisa ya mawakili na wadhamini. Wafanyakazi wenye madaraka au ujuzi maalum watakuwa washirika wa kamati hiyo, ingawa wengine wao hawatakuwa washirika wa halmashauri ya kanisa.

Tunaagiza makanisa yetu ya mtaa kuhakikisha kwamba watu wanaochaguliwa kama viongozi wa kanisa ni wale tu wenye ujuzi wa utakaso kamili, na wanadhihirisha wazi maishani mwao neema ya Mungu inayotuhitaji kuishi maisha ya utakatifu; wanaokubaliana kikamilifu na mafundisho, uongozi na utaratibu wa Kanisa la Mnazareti; na ambao wanasaidia na kutegemeza kanisa la mtaa kwa mahudhurio, kuhusika kamili katika ibada, na kutoa sadaka na zaka au fungu la kumi kwa uaminifu. Viongozi wa kanisa wanafaa kuhusika kikamilifu katika "kuwafanya wanafunzi wa mataifa kuwa kama Kristo." (33. 137, 141, 146)

**Kazi na mamlaka ya Halmashauri ya Huduma ya Kimataifa ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi au Kamati ya Elimu** ni:

**145.1.** Kupanga, kutayarisha, kuendeleza na kutekeleza huduma ya elimu ya Kikristo kwa kanisa la mtaa. Mambo hayo yatafanyika chini ya uangalizi wa mchungaji, na uongozi wa msimamizi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa, na mwongozo wa halmashauri ya kanisa la mtaa, kulingana na shabaha na viwango vya kanisa letu vilivyowekwa na Halmashauri Kuu na kuendelezwa kupitia Kamati ya Misheni ya Ulimwengu na ofisi za Huduma za Watu Wazima (WW), Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, na Huduma za Watoto. Shule ya Jumapili ni pamoja na huduma zilizopangwa za watu wazima, vijana, na watoto. Shule ya Jumapili/Mafundisho ya Biblia/vikundi vidogo, vikiwa ni pamoja na huduma za mahubiri, hutoa kiini cha kujifunza Maandiko kwa kanisa na mafundisho ya imani. Malezi ya watoto/Shule

(kuanzishwa kupitia shule ya upili) na huduma maalum za mwaka na mafundisho, kama vile Karavani, Shule ya Biblia wakati wa Likizo (SBL), huduma kwa vijana na wale hawajaoa au kuolewa, hutoa nafasi ambazo mafundisho ya Biblia yanaweza kushirikishwa katika maisha ya waumini. (516.15)

**145.2.** Kuwafikia watu wengi iwezekanavyo wasiokuwa na kanisa na kuwaleta kwa Kristo na kanisani, kuwajumuisha katika ushirika, kufundisha Neno la Mungu kwa ufasaha, na kuwajulisha umuhimu wa wokovu, kuwafahamisha mafundisho ya imani ya Kikristo na umuhimu wa kustawisha tabia, nia na desturi ya Kristo; na kusaidia kuanzisha jamaa za Kikristo; kuwatayarisha waumini kwa Ushirika wa kanisa na kuwaandaa kwa huduma zinazowafaa za Kikristo.

**145.3.** Kuchunguza na kutayarisha utaratibu unaotumiwa katika kutoa huduma tofauti, na kuhakikisha kwamba kutumia vitabu vilivyochapishwa na Kanisa la Mnazareti kuunda msingi wa mafundisho yote ya Kibiblia ya tafsiri za imani.

**145.4.** Kupanga na kutayarisha huduma zote za Shule ya Jumapili katika kanisa la mtaa kulingana na Kanuni za Shule ya Jumapili. [812]

**145.5.** Kuteua mtu mmoja au zaidi, aliyeidhinishwa na mchungaji, atayechaguliwa wakati wa mkutano wa mwaka katika ofisi ya msimamizi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa. Uteuzi huo utafanywa kwenye mkutano ambao hautahudhuriwa na msimamizi wa Shule ya Jumapili anayeshikilia wadhifa huo.

**145.6.** Kuteua watu waliokubaliwa na mchungaji, kuwa wajumbe wa halmashauri ya kanisa, ili wachaguliwe kutumika kama wakurugenzi wa Huduma za Watoto na Huduma za Watu Wazima.

**145.7.** Kuchagua baraza la Huduma ya Watoto na la Watu Wazima kutoka kwa watu walioteuliwa na wakurugenzi wa Huduma za Watoto na Watu Wazima, kwa idhini ya mchungaji na msimamizi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa.

**145.8.** Kuchagua wasimamizi, walimu, na viongozi wa makundi yote ya rika ya Shule ya Jumapili/mafundisho ya Biblia/vikundi vidogo ambao ni Wakristo wanaoishi maisha yenye mfano mwema na wanaokubaliana na mafundisho pamoja na uongozi wa Kanisa la Mnazareti, watakaoteuliwa na mwenyekiti wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na wakurugenzi wa Huduma za Watoto na Watu Wazima. Watakaoteuliwa ni lazima waidhinishwe na mchungaji na msimamizi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa.

**145.9.** Kuchagua mkurugenzi wa Mafunzo ya Kuendelea ya Waumini katika kanisa, ambaye atatayarisha, kuendeleza na kusimamia nafasi za

mafundisho kwa wafanyakazi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa na washirika wote wa kanisa. Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa itakuwa na chaguo la kumruhusu mkurugenzi wa Mafunzo ya Kuendelea ya Waumini kuwa mshirika wa halmashauri hiyo kwa ajili ya wadhifa wake.

**145.10.** Kuwa na mikutano ya mara kwa mara, na kujiratibu, kwa kuchagua katibu na viongozi wengine wanaohitajika, mwanzo wa mwaka wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa, ambao utakuwa sawa na mwaka wa kanisa. Mchungaji au msimamizi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa anaweza kuitisha mikutano maalum. (114)

**146. Msimamizi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa.** Mkutano wa mwaka wa kanisa utachagua, kwa wingi wa kura zitakazopigwa kwa siri, kutoka katika washirika wake kamili, walioko na wanapiga kura, kutoka katika washirika wake kamili, msimamizi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa atakayetumika kwa mwaka mmoja, au hadi mwandamizi wake atakapochaguliwa. Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa, kwa idhini ya mchungaji, inaweza kupanga kwamba msimamizi anayeshikilia wadhifa huo achaguliwe kwa kura ya “Ndio” au “La”. Nafasi inayoachwa wazi itajazwa na kanisa la mtaa kwenye mkutano wa kanisa ulioitishwa rasmi. Msimamizi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa aliyechaguliwa upya, atakuwa mshirika, kwa ajili ya kazi yake, wa kikao cha wilaya, halmashauri ya kanisa na Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa.

Tunaagiza makanisa yetu ya mtaa kuhakikisha kwamba watu wanaochaguliwa kama viongozi wa kanisa ni wale tu wenye ujuzi wa utakaso kamili na wanadhihirisha wazi maishani mwao neema ya Mungu inayotuhitaji kuishi maisha ya utakatifu; wanaokubaliana kikamilifu na mafundisho, uongozi na utaratibu wa Kanisa la Mnazareti; na ambao wanasaidia na kutegemeza kanisa la mtaa kwa maudhurio, na kutoa sadaka na zaka au fungu la kumi kwa uaminifu. Viongozi wa kanisa wanaweza kuhusika kamili katika “kuwafanya mataifa kuwa wanafunzi wa Kristo.” (33, 113.11, 127, 145, 145.5, 201) **Kazi na mamlaka ya msimamizi wa Huduma ya Kimataifa ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi** ni:

**146.1.** Kuwa msimamizi mkuu wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa katika kanisa la mtaa.

**146.2.** Kusimamia Huduma za Kimataifa za Shule ya Jumapili na Uanafunzi kulingana na Kanuni za Shule ya Jumapili. (812).

**146.3.** Kuendeleza mipango na ratiba za kuongezeka kwa uandikishaji, maudhurio, na mafundisho ya uongozi.

**146.4.** Kusimamia na kuongoza mikutano ya kawaida ya Halmashauri ya Huduma za Kimataifa za Shule ya Jumapili na Uanafunzi, au Kamati ya Elimu ya halmashauri ya kanisa, na kuongoza Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa katika kutekeleza wajibu wake.

**146.5.** Kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa kwa halmashauri ya kanisa kila mwaka.

**146.6.** Kutoa ripoti kila mwezi kwa halmashauri ya kanisa, na kuwasilisha ripoti iliyoandikwa kwenye mkutano wa mwaka wa kanisa.

**147. Mabaraza na Wakurugenzi wa Huduma kwa Watoto na Watu Wazima.** Kazi ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa inafanyika vizuri zaidi ikipangwa kulingana na umri wa wale wanaohudumiwa: watoto, vijana na watu wazima. Kwa kila rika kunapaswa kuwa na baraza lenye wajibu wa kupanga na kutekeleza huduma hizo. Baraza kama hilo litaundwa na mkurugenzi wa kundi la rika hilo na wawakilishi kutoka kwa Shule ya Jumapili/mafundisho ya Biblia/vikundi vidogo na idara nyingine za kanisa zinazotoa huduma kwa rika hilo. Kazi ya baraza hilo itakuwa ni kufanya kazi pamoja na mkurugenzi wa kundi la rika kupanga huduma kwa kundi hilo, na kutayarisha jinsi ya kutekeleza huduma hizo. Kazi zote za baraza la kundi la rika zitahitaji idhini ya mkurugenzi wake na Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa.

**Kazi ya wakurugenzi wa makundi ya rika** ni:

**147.1.** Kuwa mwenyekiti wa baraza la kundi la rika analosimamia, na kuongoza baraza hilo katika kupanga, kuendeleza, na kuunganisha Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa kwa watu walioko katika kundi hilo.

**147.2.** Kutoa uongozi kwa tawi linalostahili la Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa kwa kuendeleza mipango ya kuongeza uandikishaji na mahudhurio kwa watoto, vijana au watu wazima katika kanisa la mtaa, akishirikiana na Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa.

**147.3.** Kutoa uongozi kwa huduma za ziada za Jumapili shule za malezi (kuanzishwa kupitia Shule ya upili), huduma maalum na za kila mwaka, uinjilisti na ushirika kwa kundi la rika analowakilisha.

**147.4.** Kuteua kwa Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa viongozi wa huduma mbalimbali zinazotekelezwa

na kundi lake, hii ikiwa ni pamoja na wasimamizi wa Shule ya Jumapili, waalimu na viongozi, bila kuhusisha Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ambayo itateua wasimamizi, walimu, na viongozi wa Shule ya Jumapili ya Vijana/Mafundisho ya Biblia/vikundi vidogo. Walioteuliwa sharti waidhinishwe na mchungaji na msimamizi wa Shule ya Jumapili. (33)

**147.5.** Kupata idhini ya Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa kabla ya kutumia utaratibu wa ziada wa mafundisho.

**147.6.** Kutoa mafundisho ya uongozi kwa wafanyakazi wa makundi ya rika akishirikiana na Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa na mkurugenzi wa Mafundisho ya Kuendelea kwa Waumini.

**147.7.** Kupeleka ombi la makadirio ya matumizi kwa Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa au kwa halmashauri ya kanisa, na kusimamia kutumiwa kwa pesa kulingana na makadirio yaliyoidhinishwa.

**147.8.** Kupokea ripoti zote za huduma tofauti zinazotolewa na matawi ya kundi la rika la kanisa la mtaa lililo chini ya uongozi wake. Ripoti ya kila mwezi ya Huduma za Uanafunzi (Shule ya Jumapili/Majukumu ya Huduma Iliyoongezeka/Uanafunzi/Mafundisho ya Biblia) zilizotolewa itapelekwa kwa msimamizi wa Huduma za Kimataifa za Shule ya Juampili na Uanafunzi.

**147.9.** Kuwasilisha ratiba ya kipindi cha miezi mitatu ya shughuli za kundi la rika analosimamia kwa Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa ili ziwekwe pamoja na huduma nyingine za Shule ya Jumapili ya kanisa la mtaa.

**148. Baraza la Huduma za Watoto.** Baraza la Huduma za Watoto litakuwa na wajibu wa kupanga Huduma zote za Kimataifa za Shule ya Jumapili kwa watoto wachanga hadi wa umri wa miaka 12 katika kanisa la mtaa. Baraza hilo litakuwa, kwa uchache, na mjumbe mmoja wa Shule ya Jumapili na wakurugenzi wa huduma nyingine yo yote kwa watoto inayotolewa na kanisa la mtaa, kama vile kanisa la watoto, Karavani, Shule ya Biblia Wakati wa Likizo, Maswali ya Biblia, Elimu ya Umisheni, na huduma zingine zinazohitajika. Ukubwa wa baraza hilo utategemea kiasi cha huduma zinazotolewa kwa watoto katika kanisa la mtaa, kadiri mahitaji yanavyotambuliwa na uongozi unavyopatikana.

**Kazi ya mkurugenzi wa Huduma za Watoto ni:**

**148.1.** Kufanya kazi zote za wakurugenzi wa makundi ya rika zilizoelezwa katika 147.1-147.9.

**148.2.** Kushirikiana na Kamati Kuu ya Umisheni wa Mnazareti wa Kimataifa ya kanisa la mtaa katika kuchagua mkurugenzi wa elimu ya umisheni kwa watoto. Atakayechaguliwa kufanya kazi hiyo atakuwa mshirika wa baraza la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa na baraza la Huduma za Watato. Watakaoteuliwa kwa kazi hiyo ni sharti waidhinishwe na mchungaji na msimamizi wa Shule ya Jumapili.

**149. Baraza la Huduma za Watu Wazima.** Baraza la Huduma za Watu Wazima litakuwa na wajibu wa kupanga huduma yote ya watu wazima katika kanisa la mtaa. Baraza hilo litakuwa na angalau mwakilishi mmoja wa Shule ya Jumapili/mafundisho ya Biblia/Vikundi vidogo na wakurugenzi wa huduma nyingine zozote zinazotolewa na kanisa, kama vile ndoa na maisha ya familia, huduma kwa wazee, huduma kwa watu wazima ambao hawajaolea au kuoa, huduma kwa waumini, huduma za wanawake na wanaume, na zingine zitakazohitajika. Ukubwa wa baraza utategemea hesabu ya huduma zinazotolewa katika kanisa la mtaa kwa watu wazima, na kadiri mahitaji yanavyotambuliwa na uongozi kupatikana.

**Kazi ya mkurugenzi wa baraza la huduma kwa watu wazima ni:**

**149.1.** Kufanya kazi zote zile za wakurugenzi wa makundi ya rika zilizoelezwa katika vifungu vya 147.1- 147.9.

## O. Huduma ya Vijana Mnazareti ya Kimataifa ya Kanisa Mtaa

**150.** Huduma ya vijana wa Mnazareti hutekelezwa katika kanisa la mtaa chini ya uangalizi na usaidizi Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa. Makundi ya mtaa ya vijana huendeshwa kwa utaratibu uliowekwa katika katiba ya Huduma ya Kimataifa ya Vijana kanisa la Mnazareti na chini ya mamlaka ya halmashauri ya kanisa la mtaa.

**150.1.** Huduma ya Vijana Wanazareti ya Kimataifa katika kanisa la mtaa kitaratibiwa kulingana na Mpango wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa (810.100-810.118), ambao unaweza kuambatanishwa na mahitaji ya huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa katika kanisa la mtaa, kulingana na katiba ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na *Kitabu cha Mwongozo cha Kanisa la Mnazareti*.

## P. Shule zinazomilikiwa na kanisa za Malezi (Kuanzishwa kupitia Shule ya Upili) za Kanisa la Mnazareti

**151.** Shule za Nazareni za malezi/chekechea, za msingi na za upili zinaweza kuanzishwa na kuratibiwa na halmashauri ya kanisa la mtaa, baada ya kupata ruhusa au idhini ya msimamizi wa wilaya na Halmashauri ya Wilaya, zikifuata utaratibu uliowekwa na Huduma za Watoto/ofisi ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa. Mkurugenzi na halmashauri ya shule zitakuwa chini ya usimamizi ya halmashauri ya kanisa. (129.18, 211.13-211.14, 225.14, 516.15, 517)

**151.1. Kufungwa kwa Shule.** Ikiwa kanisa la mtaa litaona kuwa kuna haja ya kusimamisha shughuli za shule ya malezi, za msingi na za upili), itaruhusiwa kufanya hivyo baada ya kushauriana na msimamizi wa wilaya na Halmashauri ya Wilaya na kutoa ripoti ya mapato na matumizi ya fedha za shule.

## Q. Umisheni wa Kanisa la Mnazareti wa Kimataifa

**152.** Baada ya kuruhusiwa na halmashauri ya kanisa, makundi ya Umisheni wa Mnazareti wa Kimataifa ya mtaa yanaweza kuundwa kanisani kwenye kundi lolote la rika kulingana na Katiba ya Umisheni wa Mnazareti wa Kimataifa na Kamati ya Misheni ya Dunia ya Halmashauri Kuu. (811)

**152.1.** Kundi la mtaa la Misheni ya Mnazareti la Kimataifa litakuwa sehemu ya kanisa la mtaa na litafanya kazi chini ya uangalizi na uongozi wa mchungaji na halmashauri ya kanisa. (516)

**152.2.** Kiongozi wa kundi la mtaa la Misheni ya Mnazareti la Kimataifa katika kanisa la mtaa atateuliwa na kamati ya washirika watatu hadi saba wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa walioteuliwa na mchungaji, ambaye atakuwa mwenyikiti wa kamati hiyo. Kamati hiyo itawasilisha jina moja au zaidi ya wale watakaochaguliwa kwa ofisi ya kiongozi, baada ya kuidhinishwa na halmashauri ya kanisa. Kiongozi wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa atachaguliwa kwa kura za wingi kwa siri na washirika kamili walioko mkutanoni na wanapiga kura (bila kuhusisha waumini). Kiongozi atakayechaguliwa atakuwa mshirika wa kanisa la mtaa ambalo linatumikiwa na Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa iliyomchagua, na pia mshirika wa halmashauri ya kanisa (au katika makanisa ambayo mwenyekiti ni mke au mume wa mchungaji, naibu wake atatumika katika halmashauri ya kanisa), na mshirika wa kikao cha wilaya kitakachokutana kabla ya kuanza kwa mwaka wa kipindi cha utumishi wake. Kiongozi atatoa ripoti katika mkutano wa mwaka wa kanisa la mtaa. (113.7, 114, 123, 127, 201)

**153.** Pesa zote zitakazochangishwa na kundi la mtaa la Misheni ya Mnazareti la Kimataifa kwa manufaa ya Kanisa la Mnazareti zitawekwa katika Hazina ya Uinjilisti wa Ulimwengu ya kanisa la mtaa, isipokuwa miradi maalum ya misheni ambayo imeidhinishwa na Asilimia Kumi ya Kamati.

**153.1.** Baada ya kufikiriwa kwanza kwa malipo kamili ya Hazina ya Uinjilisti wa Dunia, makanisa ya mtaa yanahimizwa kusaidia misheni ya dunia kufanya kazi kupitia matoleo maalum ya misheni yaliyoidhinishwa.

**154**. Pesa za kutegemeza shughuli zenye manufaa kwa kanisa zitachangishwa kwa njia hizi zifuatazo:

**154.1.** Kutoka kwa zawadi na matoleo yaliyotolewa kwa Hazina ya Uinjilisti wa Dunia na kwa manufaa ya kanisa.

**154.3.** Hakuna sehemu ya pesa hizo itakayotumiwa kwa matumizi ya kanisa la mtaa au wilaya au kwa kusudi la kufadhili watu.

## R. Kizuizi Cha Kuomba Pesa za Kanisa la Mtaa

**155.** Itakuwa kinyume cha sheria kwa kanisa la mtaa, viongozi wake au washirika, kutuma maombi kwa makanisa mengine ya mtaa, viongozi wake, au washirika, ya kuomba pesa au msaada wa kifedha kwa mahitaji ya kanisa lao au shughuli nyingine wanazotaka kutekeleza. Hata hivyo, inakubaliwa kutuma maombi kama hayo kwa washirika au makanisa ya mtaa yaliyoko katika wilaya ambayo kanisa hilo liko, lakini sharti yaidhinishwe na msimamizi wa wilaya na Halmashauri ya Wilaya.

**156.** Washirika wa Kanisa la Mnazareti ambao hawakuruhusiwa na Halmashauri Kuu au mojawapo ya idara zake, hawana haki ya kukusanya au kuomba pesa kwa shughuli za kimishenari kutoka katika makanisa au washirika wake, mbali na malipo ya Hazina ya Uinjilisti wa Dunia, kutoka kusanyiko la makanisa ya mtaa, au kutoka kwa washirika wa makanisa kama hayo.

## S. Kutumiwa Kwa Jina la Kanisa la Mtaa

**157.** Jina la Kanisa la Mnazareti, au la kanisa lolote la mtaa, au shirika lolote ambalo ni sehemu ama linahusika na Kanisa la Mnazareti kwa njia yoyote, au sehemu ya jina kama hilo, haliruhusiwi kutumiwa na washirika wowote wa Kanisa la Mnazareti, au shirika, jumuiya, muungano ama kundi lolote, kwa shughuli yoyote, (iwe ya kibiashara, kwa watu wote, kielimu, kufadhili watu, au ya aina nyingine yoyote) bila idhini iliyoandikwa ya Halmashauri Kuu ya Kanisa la Mnazareti na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu. Hata hivyo, kifungu hiki cha katiba hakitahusu shughuli za Kanisa

la Mnazareti ambazo zimeidhinishwa katika *Kitabu rasmi cha Mwongozo* wa Kanisa la Mnazareti.

### T. Mashirika Yanayodhaminiwa na Kanisa

**158.** Hakuna kanisa lolote la mtaa, halmashauri ya kanisa lolote, shirika la wilaya, Halmashauri ya Wilaya, ama washirika wawili au zaidi wa kanisa lolote, wenyewe binafsi au kupitia watu wengine watakaoruhusiwa kuunda au kuwa washirika wa jumuiya, kundi au muungano wowote ambao unaendeleza, kudhamini, au kutia moyo au kwa nia yoyote kujihusisha katika shughuli ya aina nyingine yoyote (iwe ya kibiashara, kijamii, kielimu, kufadhili watu au aina nyingine yoyote) ambayo washirika wa Kanisa la Mnazareti wataombwa au kuulizwa kwa njia yoyote kuwa wahusika, wateja, wapangaji nyumba, wateja wa biashara, washirika, au wasaidizi, au kwenye shughuli ya aina yoyote (iwe ya kibiashara, kijamii, kielimu, kufadhili au namna yoyote) inayoonekana kama kwamba inadhaminiwa au inaendeshwa kwa manufaa, au kuwatumikia washirika wa Kanisa la Mnazareti, bila idhini iliyoandikwa ya msimamizi wa wilaya, Halmashauri ya Wilaya, na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu.

### U. Wasaidizi Katika Kanisa la Mtaa.

**159.** Kunaweza kuwa na wale wanaohisi mwito wa kujitayarisha kwa utumishi fulani muhimu wa waumini katika kanisa, aidha wa muda fulani au wa kudumu. Kanisa linatambua kuwepo kwa nafasi za wafanyakazi kama hao, lakini kwa kawaida kazi kama hizo hufanywa na wale wanaojitoa kuzifanya katika kanisa, kwa kutumikia Mungu na wengine kulingana na uwezo wao. Wakati wasaidizi wa kulipwa watakapohitajika katika kanisa la mtaa, au katika tawi au shirika linalohusiana na kanisa la mtaa, wawe wahudumu au waumini, ili kuimarisha huduma inayotolewa, jambo hilo halipaswi kuwavunja watu moyo wa kujitolea kufanya kazi bila malipo, au kuwa mzigo wa kifedha kwa kanisa utakaotatiza kulipwa kwa makadirio ya pesa kanisa linalopaswa kulipa. Hata hivyo, ombi la kuchunguzwa upya kwa jambo kama hilo, na msimamizi wa wilaya na Halmashauri ya Wilaya, linaweza kuwasilishwa kwa maandishi ili lifanyiwe uamuzi unaofaa. (129.27)

**159.1.** Wasaidizi wote wa mtaa, wawe wa kulipwa au wakujitolea, kama vile wachungaji wasaidizi, wakurugenzi wa elimu ya Kikristo, kazi ya vijana, muziki na wakurugenzi wa shule za malezi (Kuanzishwa kupitia Shule ya Upili), watachaguliwa na halmashauri ya kanisa baada, ya kuteuliwa na mchungaji. Uteuzi wote ni lazima uwe na idhini iliyoandikwa

ya msimamizi wa wilaya, ambaye katika kipindi cha siku 15 baada ya kupokea ombi la kufanya hiyo. [159.4, 211.13)

**159.2.** Muda wa kuajiriwa kwa wasaidizi hao hautazidi mwaka mmoja, lakini unaweza kuongezwa kwa pendekezo la mchungaji akiwa na idhini iliyoandikwa ya msimamizi wa wilaya na kura ya kukubali ya halmashauri ya kanisa. Mchungaji, akishauriana na halmashauri ya kanisa, anaweza kutoa pendekezo la marekebisho ya maelezo ya kazi kama vile itakavyohitajika na ripoti ya ukaguzi. Kuachishwa kazi kwa wasaidizi hao kabla ya kumalizika kwa kipindi cha kuajiriwa kwao (mwisho wa mwaka wa kanisa) ni lazima kupendekezwe na mchungaji, kuidhinishwe na msimamizi wa wilaya, na kura za wingi za halmashauri ya kanisa. Taarifa ya kuachishwa au kukosa kufanya upya kwa ajira ni lazima kutolewa kwa maandishi katika siku zisizopungua 30 kabla ya kuachishwa kwa kazi (129.27).

**159.3.** Kazi na utumishi wa wasaidizi hao zitaamuliwa na kusimamiwa na mchungaji. Taarifa kamili iliyoandikwa ya maelezo ya kazi na wajibu wao itakabidhiwa kwa wasaidizi hao katika kipindi cha siku 30 baada ya kuanza kwa wajibu wao kwa kanisa.

**159.4.** Hakuna mfanyakazi yeyote wa kulipwa wa kanisa atakayestahili kuchaguliwa katika halmashauri ya kanisa. Mshirika yeyote wa halmashauri ya kanisa atakayekuwa mfanyakazi wa kulipwa wa kanisa, hataendelea kuwa mshirika wa halmashauri ya kanisa.

**159.5.** Mchungaji akijiuzulu, kustawi, umoja, na huduma zinazoendelea za kanisa la mtaa ni muhimu. Kwa hivyo, msimamzi wa wilaya (au mwakilishi aliyeteuliwa na msimamizi wa wilaya) atafanya kazi kwa karibu sana na halmashauri ya wilaya kuendeleza hatua zinazofuata ambazo (a) anaweza kuruhusu kanisa la mtaa kuhifadhi baadhi ya wafanyakazi au wafanyakazi wote aghalau kwa kipindi cha wakati wa mabadiliko; (b) bado ataruhusu mchungaji mpya kuwa ha uhuru wa kujenga kundi lake la wasaidizi, kama itahitajika; na (c) ataruhusu halmashauri na msimamizi wa wilaya kuamua kuwa wafanyakazi wapya malipo yanastahili ya kufanya mabadiliko ya kikazi yanayofaa. Kwanza baada ya kujiuzulu au kuachishwa kazi kwa mchungaji, msaidizi yeyote pia atapeana atatoa maombi ya kujiuzulu pamoja na mchungaji. Pili, halmashauri ya kanisa la mtaa inaweza kuomba kwamba msimamizi wa wilaya atoe idhini ya msaidizi wowote yeyote wa ya huduma kuendelea. Idhini hii, ikikubaliwa, inaweza kuendelea hadi siku 90 baada ya mchungaji mpya kuanza kazi au hadi mchungaji anayeingia ambaye atatteuwa wasaidizi wake wa kulipwa kwa mwaka huo kulinga na kifungu cha 159. Wakurugenzi wa shule ya malezi (Shule za Kawaida) watatoa

barua zao za kujiuzulu katika mwisho wa mwaka wa shule ambapo mchungaji mpya ataanza kazi za ofisi. Afisa mkuu shirika lolote la msaada mdogo au shirika lenye kushirikishwa atapeana barua yake ya kujiuzulu mwishoni mwa kipindi cha hati zake za kazi kuisha ambapo mchungaji mpya ataanza kazi za ofisi wakati huo. Mchungaji anayeingia anaweza kuwa na nafasi ya kupendekeza kuajiriwa kwa wafanyakazi wa ofisi ambao walikuweko hapo mwanzo.

**159.6.** Mawasiliano na wafanyakazi wa kanisa, halmashauri ya kanisa, na waumini kuhusu matokeo ya kifungu 159.5 kwa wafanyakazi wakati wa mabadiliko ya uchungaji itakuwa ni wajibu wa msimamizi wa wilaya. (211.13)

**159.7.** Mchungaji wa kusanyiko lililopata idhini ya kuendesha shughuli zake kama kanisa la mtaa kulingana ni kifungu 100.2 hatahesabiwa kama mfanyakazi wa kuajiriwa.

**159.8.** Mtu yeyote ambaye anatumika kama mfanyakazi wa kulipwa hawezi kuitwa kuwa mchungaji wa kanisa ambalo yeye ni mshirika bila idhini ya Halmashauri ya Wilaya na Halmashauri ya Wilaya. (115, 129.2, 211.10, 225.16)

# SURA YA PILI

# KIKAO CHA WILAYA

## A. Mipaka na Jina ya Wilaya

**200.** Kikao Kikuu kitaratibu ushirika wa Kanisa katika vikao vya wilaya.

Wilaya ni kitengo kilichoundwa cha makanisa ya mtaa yenye kutegemeana ambayo yameratibiwa kurahisisha misheni ya kila kanisa la mtaa kupitia msaada wa kuafikiana, kugawa kwa mali, na kushirikiana.

Mipaka na jina la wilaya itakuwa kama itakavyoagizwa na Kamati Kuu ya Mipaka na kuidhinishwa na wingi wa kura za vikao vya wilaya vinavyohusika, kwa idhini ya mwisho kutoka kwa msimamizi mkuu au wasimamizi wakuu wanaohusika na wilaya hiyo.

Mahali ambapo wilaya kutoka jimbo moja la elimu inaweza kufikiria kuunganishwa kuwa wilaya moja, Kamati Kuu ya Mipaka itaamua ni jimbo gani ambalo wilaya mpya itakuwa sehemu yake, kwa kushauriana na wasimamizi wakuu wa eneo husika. (24)

**200.1. Kuundwa Kwa Wilaya Mpya.** Wilaya mpya katika Kanisa la Mnazareti zinaweza kuanzishwa kwa:

1. Kugawanya wilaya moja kuwa wilaya mbili au zaidi (kunahijitaji theluthi mbili za kura za kikao cha wilaya);
2. Kuunganishwa kwa wilaya mbili au zaidi ili kuunda wilaya zingine zaidi;
3. Kuanzisha wilaya mpya katika eneo ambalo si sehemu ya mojawapo ya wilaya zilizoko; au
4. Kuunganishwa kwa wilaya mbili au zaidi; au
5. Pendekezo la kuanzisha wilaya mpya litapelekwa kwa msimamizi/wasimamizi wakuu wa eneo hilo. Msimamizi/wasimamizi wa wilaya na Halmashauri za Wilaya au halmashauri za kitaifa zinaweza kuidhinisha na kurejesha suala hilo kwa vikao vya wilaya kwa kupigwa kura kwa idhini ya wasimamizi wa kuu wa eneo hilo na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu. (24, 200, 200.4)

**200.2.** Kazi katika Kanisa la Mnazareti inaweza kuanzishwa kwa taasisi zingine mpya na kuelekeza kuanzishwa kwa wilaya mpya na mipaka mipya ya kikao cha wilaya. Wilaya zinaweza kufikia Kiwango cha 3 haraka iwezekenavyo kulingana na utaratibu ufuatao:

**Kiwango cha 1.** Wilaya ya kiwango cha 1 itaanzishwa wakati nafasi ya kuingia katika sehemu mpya itakapopatikana, kwa mwongozo wa ustawi na uinjilisti. Maombi ya kuingia sehemu mpya yanaweza kutumwa na mkurugenzi wa jimbo, au wilaya kupitia kwa Baraza la Ushauri la Jimbo, au msimamizi wa wilaya na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya kwa idhini ya mwisho kutoka kwa wasimamizi wakuu wa eneo hilo na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu.

Msimamizi wa wilaya ya kiwango cha 1 atapendekezwa na mkurugenzi wa jimbo, akishauriana na mkurugenzi wa idara ya Umisheni wa Dunia, kwa msimamizi mkuu wa eneo hilo ambaye ndiye atakayeteua. Jimbo litatoa mwongozo kwa wilaya ya kiwango cha 1 kuhusu raslimali zitakazopatikana kwa ustawi. Katika majimbo ambayo yako na wilaya zinazodhamini, msimamizi wa wilaya atateuliwa na msimamizi mkuu wa eneo baada ya kushauriana na msimamizi au wasimamizi wa wilaya na Halmashauri za wilaya zinazodhamini.

Ikiwa, kwa maoni ya mkurugenzi wa eneo na mkurugenzi wa jimbo, wilaya ya Kiwango cha 1 katika majimbo yanayohusiana na Idara ya Umisheni wa Dunia, inakabiliwa na mzozo-uwe wa kifedha, kimaadili-na mzozo huo unaweza kutatiza uthabiti na hali ya baadaye ya wilaya, wilaya inaweza kutangazwa kuwa katika hali ya mzozo kwa idhini ya msimamizi mkuu wa eneo hilo akishauriana na mkurugenzi wa Idara ya Umisheni wa Dunia. Mkurugenzi wa jimbo, akiwa na idhini kutoka kwa msimamizi mkuu, anaweza kuteua halmashauri ya muda mfupi kusimamia wilaya badala ya halmashauri zingine hadi wakati wa kikao rasmi cha wilaya kitakachofuata.

**Kiwango cha 2.** Wilaya ya kiwango cha 2 inaweza kuanzishwa wakati idadi ya kutosha ya makanisa yaliyoratibiwa na makasisi waliowekwa wakfu, na ufanisi au ustawi na mipangilio ya wilaya iliyoko imekomaa kiasi cha kutosha kupendekeza jambo hilo.

Jambo hilo lililoanzishwa litatekelezwa na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu kwa pendekezo la msimamizi mkuu wa eneo hilo baada ya kushauriana na mkurugenzi wa Misheni ya Dunia, mkurugenzi wa jimbo, na watu binafsi na halmashauri katika kuteuliwa kwa msimamizi wa wilaya. Msimamizi wa wilaya anaweza kuchaguliwa au kuteuliwa.

Mwongozo wa idadi inayoweza kukadiriwa utakuwa na kiasi cha makanisa 10 yalioratibiwa, washirika kamili 500, na makasisi 5 waliowekwa wakfu, na kiasi cha 50% cha matumizi ya usimamizi wa wilaya kitakuwa kinatolewa katika hazina ya huduma za wilaya wakati wa uchaguzi. Halmashauri ya Wilaya au halmashauri ya kitaifa inaweza

kumuomba msimamizi mkuu wa eneo kutohesabu au kutilia masharti hayo uzito.

Ikiwa, kwa maoni ya mkurugenzi wa eneo na mkurugenzi wa jimbo, wilaya ya Kiwango cha 2 iko katika mzozo-uwe wa kifedha, kimaadili, au mzozo mwingine-na mzozo huo huo unaweza kutatiza uthabiti na hali ya baadaye ya wilaya, wilaya inaweza kutangazwa kuwa katika hali ya mzozo kwa idhini ya msimamizi mkuu wa eneo hilo akishauriana na mkurugenzi wa Idara ya Umisheni wa Dunia. Mkurugenzi wa jimbo, akiwa na idhini kutoka kwa msimamizi mkuu, anaweza kuteua halmashauri ya muda mfupi kusimamia wilaya badala ya halmashauri zingine hadi wakati wa kikao rasmi cha wilaya kitakachofuata.

**Kiwango cha 3.** Wilaya ya kiwango cha 3 inaweza kutangazwa kuwa na idadi ya kutosha ya makanisa yaliyoratibiwa, makasisi waliowekwa wakfu, na washirika walioko kuruhusu chaguo hilo. Uongozi, ufanisi au ustawi na mipangilio, wajibu wa makadirio ya fedha, na uthabiti wa mafundisho ya imani ya kanisa ni lazima udhihirishwe. Wilaya ya kiwango cha 3 ni lazima iwe na uwezo wa kushughulikia mambo mazito na kushiriki katika changamoto za Utume Mkuu kwa kiwango cha ulimwengu cha kanisa la kimataifa.

Chaguo kama hilo litahitajika na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu kwa kupendekezwa na msimamizi mkuu wa eneo hilo baada ya kushauriana na mkurugenzi wa Misheni ya Dunia, mkurugenzi wa jimbo, na watu wengine binafsi na halmashauri inayohusika katika kuteuliwa kwa msimamizi wa wilaya. Msimamizi wa wilaya atachaguliwa kufuatana na mwelekeo wa *Kitabu cha Mwongozo*.

Utaratibu wa idadi itakayohitajika utakuwa ni pamoja na makanisa 20 yaliyoratibiwa, washirika kamili 1,000, na makasisi 10 waliowekwa wakfu.

Halmashauri ya wilaya au halmashauri ya kitaifa inaweza kumuomba msimamizi mkuu wa eneo kutohesabu au kutilia masharti hayo uzito.

Wilaya ya kiwango cha 3 ni lazima iwe inajitegemea kwa asilimia 100 katika matumizi yake ya usimamizi.

Wilaya za kiwango cha 3 zitakuwa sehemu ya jimbo zilizoko.

Ikiwa, kwa maoni ya msimamizi mkuu wa eneo, wilaya iko katika mzozo-uwe wa kifedha, kimaadili, au mzozo mwingine na mzozo huo unaweza kutatiza uthabiti na hali ya baadaye ya wilaya, wilaya inaweza kutangazwa kuwa katika hali ya mzozo kwa idhini ya Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu. Msimamizi mkuu wa eneo, akiwa na idhini kutoka kwa Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu anaweza kuchukua hatua moja kati ya zifuatazo au zaidi:

1. Kumwondoa msimamizi wa wilaya;

2. Kuteua halmashauri ya muda kwa kusimamia wilaya badala ya zile halmashauri zote ambazo ziko, hadi wakati wa kikao kingine cha wilaya kilichopangwa; na
3. Kuanzisha kuingilia kati kuliko maalum kama vile inavyotakikana kurejesha kikamilifu uhai na misheni ya wilaya. (200.1, 205.12, 206.2, 209.1, 307.9, 322)

**200.3. Masharti ya Kugawanya Wilaya au Kubadilisha Mpaka wa Wilaya.** Pendekezo la ustawi wa wilaya au la kubadilisha mpaka wa wilaya lililotayarishwa na ofisi ya jimbo, halmashauri ya kitaifa, au Halmashauri ya Wilaya litawasilishwa kwa msimamizi mkuu wa eneo. Mpango huo unapaswa kutilia maanani mambo yafuatayo:

1. Kuwa wilaya mpya zilizopendekezwa au wilaya zilizonyooshwa zinapaswa kuwa na sehemu zenye idadi ya kutosha ya watu ili kufanya kuanzishwa kwa wilaya hizo mpya kuwe kwa manufaa;
2. Kuwa vifaa vya mawasiliano na uchukuzi vinapatikana katika sehemu zilizopendekezwa kuanzishwa kwa wilaya mpya;
3. Kuwa idadi ya kutosha ya makasisi waliowekwa wakfu na waumini wako tayari kwa ajili ya kazi ya wilaya;
4. Kuwa wilaya zinazodhamini zitagawanywa mahali inawezekana, hazina inayotosha ya huduma za wilaya, ushirika wa kutosha na makanisa yaliyoratibiwa kuhakikisha kwamba zitaendelea kuwa za Kiwango cha 3 cha hali ya Wilaya

**200.4. Muungano.** Wilaya moja au zaidi za Kiwango cha 3 zinaweza kuunganishwa kwa theluthi-mbili za kura zilizopendekezwa na kila vikao vya wilaya vinavyohusika, mradi tu: muungano huo utapendekezwa na Halmashauri ya Wilaya inayohusika, (na halmashauri za kitaifa zikiwapo), na kuidhinishwa katika maandishi na wasimamizi wakuu wa eneo la wilaya zinazohusika.

Kuungana huko na mambo yote yanayohusika yatakamilishwa wakati na mahali patakapoamuliwa na wilaya zinazohusika pamoja na wasimamizi wakuu wa eneo hilo.

Wilaya zilizoundwa kwa njia hiyo zitajumuisha raslimali na madeni ya wilaya zilizoungana.

Wilaya za Kiwango cha 1 na Kiwango cha 2 zinaweza kuunganishwa kufuatana na masharti ya kuundwa kwa wilaya mpya kama vile ilivyo katika kifungu cha 200.2. (200.1)

**200.5.** Ikiwa kikao kimoja au vikao vyote vya wilaya vinavyohusika vitakosa kuchukua hatua, au ikiwa hatua za vikao kadha vya wilaya hazipatani, pendekezo la kuungana linaweza kuwasilishwa kwa Kikao Kikuu kitakachofuata ili hatua ichukuliwe, ikiwa Halmashauri ya Ushauri

ya Wilaya zinazohusika zitatuma ombi lililokubaliwa kwa theluthi-mbili ya kura.

**200.6.** Msimamizi wa wilaya anaweza kutumia warahisishaji au wakurugenzi wa umisheni wa eneo kusaidia:

1. Kujenga hali ya jamii na undugu kati ya wachungaji wa kata au eneo la misheni;
2. Kuendeleza hali ya Kristo kwa kutia moyo na kuunda mikakati ya kuendelea kihuduma, ukuaji wa kanisa, uinjilisti, kuanza na kujenga upya kwa makanisa
3. Kutekeleza majukumu maalum kwa niaba ya msimamizi wa wilaya na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya; na
4. Kutumika kama daraja la mawasiliano katika ya kusanyiko la mtaa na wilaya.

## B. Ushirika na Wakati wa Kikao cha Wilaya

**201. Ushirika.** Kikao cha wilaya kitajumuisha makasisi wote wanaohudumu; mashemasi wote wanaohudumu; wahudumu wote waliopewa vyeti na wanaohudumu; wahudumu waliostaafu wanaohudumu; katibu wa wilaya; mtunza hazina wa wilaya; wenyeviti wa kamati za wilaya watakaotoa ripoti kwenye kikao cha wilaya; muumini yeyote anayesimamia shirika lolote la Mnazareti la elimu ya juu, ambaye ushirika wake wa kanisa la mtaa uko katika wilaya hiyo; mwenyekiti wa Wilaya wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa; wakurugenzi wa huduma za makundi ya rika wa kimataifa (watoto na watu wazima); Halmashauri ya Wilaya ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa; mwenyekiti wa Wilaya wa Huduma ya Vijana ya Kimataifa; mwenyekiti wa Wilaya wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa; msimamizi aliyechaguliwa karibuni au naibu wa msimamizi wa kila halmashauri ya kanisa la mtaa ya Huduma ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi ya Kimataifa; mwenyekiti aliyechaguliwa karibuni wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti wa Kimataifa katika kanisa la mtaa; mwenyekiti aliyechaguliwa karibuni au naibu wa mwenyekiti wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa wa kanisa la mtaa; au mwakilishi aliyechaguliwa inavyostahili anaweza kuwakilisha makundi hayo katika kikao cha wilaya; wale wanaotumika katika nyadhifa za kukabidhiwa za huduma; waumini washirika wa Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya; waumini wamishenari ambao ushirika wao wa kanisa la mtaa uko kwenye wilaya; waumini wote wamishenari waliostaafu wanaohudumu ambao ushirika wao wa kanisa la mtaa uko katika wilaya hiyo ambao walikuwa wamishenari kamili wakati wa kustaafu; na waumini wajumbe kutoka katika kila kanisa la mtaa na kanisa

ambalo halijaratibiwa katika kikao cha wilaya. (24, 113.14-113.15, 146, 152.2, 201.1-201.2, 219.2, 222.2, 224.4, 242.2, 244.2, 505-528.1, 532.8, 533-533.4, 534-534.3, 535-535.1, 536-536.2, 538.9)

**201.1.** Makanisa ya mtaa na makanisa ambayo hayajaratibiwa katika wilaya zenye washirika kamili wanaopungua 5,000 yatakuwa na haki ya kuwakilishwa katika kikao cha wilaya kama ifuatavyo: wajumbe wawili waumini kutoka katika kila kanisa la mtaa au kanisa lisiloratibiwa lenye washirika kamili wasiozidi 50, na mjumbe mmoja zaidi muumini kwa kila ongezeko la washirika wengine kamili 50 na sehemu kubwa ya mwisho ya washirika kamili 50 wa kanisa. (24, 113.14-113.15, 201)

**201.2.** Makanisa ya mtaa na kanisa lisiloratibiwa katika wilaya zenye washirika kamili 5,000 au zaidi yatakuwa na haki ya kuwakilishwa katika kikao cha wilaya kama ifuatavyo: mjumbe mmoja muumini kutoka katika kila kanisa la mtaa au kanisa lisiloratibiwa lenye washirika kamili wasiozidi 50 au washirika kamili wachache, na mjumbe mmoja zaidi muumini kwa kila ongezeko la washirika kamili 50 na sehemu kubwa ya mwisho ya washirika kamili 50 wa kanisa. (24, 113.14-113.15, 201)

**202. Wakati.** Kikao cha wilaya kitakutana kila mwaka, wakati utakaopangwa na msimamizi mkuu aliye na mamlaka, na mahali palipochaguliwa na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya au mahali palipopangwa na msimamizi wa wilaya.

**203. Kamati ya Uteuzi.** Kabla ya kukutana kwa kikao cha wilaya, msimamizi wa wilaya akishauriana na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya anaweza kuteua kamati ya uteuzi itakayotumikia kikao cha wilaya. Kamati hii inaweza kutayarisha uteuzi wa kamati na nyadhifa za kawaida mapema kabla ya kukutana kwa kikao cha wilaya. (215.2)

**204.** Vitengo vyote vya wilaya vitaamrishwa kukutana kupitia njia ya kimtandao. Njia za kupiga kura zinaidhinishwa na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya. Mawasiliano yote na kupiga kura kunakohitajika kunaweza kuendelezwa kwa njia ya kimtandao.

### C. Shughuli za Kikao cha Wilaya

**205. Kanuni za Utengemano.** Kuambatana na sheria inayotumika, pamoja na kanuni za usajili na sheria za uongozi katika *Kitabu cha Mwongozo,* mikutano na utaratibu wa washirika wa Kanisa la Mnazareti (katika mtaa, wilaya, na kikao kikuu), na kamati za shirika itatekelezwa na kusimamiwa kulingana na toleo la sasa la kitabu cha kanuni na utaratibu wa bunge kiitwacho (Toleo la sasa) la *Kanuni za Utengamano za Robert lililoboreshwa* (34).

**205.1 Shughuli za kikao cha wilaya zitakuwa** ni**:**

**205.2.** Kusikia na kupokea ripoti ya mwaka kutoka kwa msimamizi wa wilaya ambayo inatoa mukhtasari wa huduma ya wilaya ikiwa ni pamoja na makanisa yaliyoratibiwa.

**205.3.** Kusikia na kupokea ripoti kutoka kwa makasisi na wahudumu wote waliopewa vyeti wanaotumika kama wachungaji au wainjilisti walioagizwa; na kujadili juu ya sifa na tabia za makasisi na mashemasi wote wa kiume na kike. Kwa kura za kikao cha wilaya kumbukumbu ya ripoti zilizoandikwa na kupokelewa na katibu zinaweza kukubaliwa badala ya ripoti za mdomo za makasisi na mashemasi wengine wote wa kiume na kike, na wahudumu waliopewa vyeti ambao hawako katika huduma rasmi, na wale wahudumu ambao wana hati za wilaya kwa majukumu yote ya huduma zilizoelezwa katika kifungu cha 505-528.2. (521,532.8, 538.9)

**205.4.** Kutoa leseni kama wahudumu waliopewa vyeti, baada ya kuwachunguza kwa makini, watu ambao wamependekezwa na halmashauri za makanisa au Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya na ambao wanaweza kuhesabiwa kuwa wameitwa katika huduma na kuvitoa upya kwa pendekezo la kukubali la Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya au Halmashauri ya Huduma ya Wilaya. (129.14, 531.5, 532.1, 532.3)

**205.5.** Kutoa upya vyeti vya mashemasi wa kike baada ya kuwachunguza kwa makini, watu waliopendekezwa na halmashauri za kanisa na ambao wanaweza kuhesabiwa kuwa wameitwa katika wadhifa wa ushemasi wa kike kwa pendekezo la kukubali la Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya au Halmashauri ya Huduma ya Wilaya. (129.15)

**205.6.** Kuchagua kulingana na matakwa ya kasisi, au matakwa ya shemasi, watu waliotimiza mahitaji yote ya matakwa hayo ya huduma kwa pendekezo la Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya au Halmashauri ya Hudma ya Wilaya. (533.3, 534.3)

**205.7.** Kutambua mwito wa huduma na kuhitimu kwa watu wanaokuja kutoka katika madhehebu mengine ambao wanaweza kuhesabiwa kuwa wamehitimu na inahitajika wapewe nafasi ya kuhudumu katika Kanisa la Mnazareti kwa pendekezo la kukubali la Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya au Halmashauri ya Wilaya ya Huduma. (532.2, 535-535.2)

**205.8**. Kupokea, kwa uhamisho kutoka wilaya nyingine watu waliokuja ambao wana hati za huduma, washirika wahudumu, na wale walioagizwa kwa nyadhifa za huduma, ikiwa ni pamoja na wale waliopata vibali vya muda vya uhamisho vilivyoidhinishwa na Halmashauri ya Ushauri ya

Wilaya, ambao wanaweza kuhesabiwa kuwa wanafaa kwa ushirika wa kikao cha wilaya kwa pendekezo la Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya au Halmashauri ya Huduma ya Wilaya. (231.9-231.10, 505, 508-511.1, 537-537.2)

**205.9.** Kutoa hati ya uhamisho kwa wahudumu wenye vyeti, na wale wenye majukumu yaliyoagizwa ya huduma, ikiwa ni pamoja na wale walio na hati za muda za uhamisho ambazo zimeidhinishwa na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya, wanaohitaji kuhamia katika wilaya nyingine kwa pendekezo lililokubaliwa na Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya au Halmashauri ya Huduma ya Wilaya (231.9-231.10, 505, 508-511.1, 537-537.2)

**205.10.** Kutoa tume au kusajili kwa mwaka mmoja watu waliohitimu kwa majukumu ya huduma yaliyotajwa na kuelezwa katika kifungu cha 505-528.2 kwa pendekezo lililokubaliwa na Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya au Halmashauri ya Huduma ya Wilaya.

**205.11.** Kuchagua, kwa theluthi-mbili ya kura zilizopigwa kwa siri, kasisi kwa wadhifa wa msimamizi wa wilaya, atakayetumika hadi siku 30 zinazofuatia kuahirishwa kwa kikao cha pili cha wilaya baada ya kuchaguliwa kwake, na hadi mwandamizi achaguliwe au ateuliwe na kuhitimishwa. Utaratibu wa kuchaguliwa kwa mara nyingine kwa msimamizi wa wilaya utakuwa kwa kura ya "Ndio" au "La" itakayopigwa kwa siri. Hakuna kasisi yeyote atakayestahili kuchaguliwa kwa ofisi hii ikiwa vyeti vyake vya kuhudumu vilishawahi kutwaliwa kwa sababu za kinidhamu. Hakuna msimamizi atakayetumika zaidi ya siku 30 kufuatia kikao cha wilaya baada ya yeye kutimiza umri wa miaka 70.

**205.12.** Baada ya msimamizi wa wilaya ya Kiwango cha 2 au cha 3 ameitumikia wilaya kwa miaka isiyopungua miwili, kikao cha wilaya kinaweza kumchagua tena msimamizi huyo kwa kipindi cha miaka minne kwa idhini ya msimamizi mkuu wa eneo hilo. Utaratibu wa kuchagua msimamizi wa wilaya kwa kipindi kirefu katika ofisi utakuwa kwa theluthi-mbili ya kura za "ndio" au "la" zilizopigwa kwa siri. (200.2)

**205.13.** Ikiwa msimamizi mkuu na Kamati ya Ushauri ya Wilaya, atakuwa na maono kwamba huduma za msimamizi wa wilaya zisiendelee zaidi ya mwaka unaoendelea, msimamizi mkuu wa eneo hilo na Kamati ya Ushauri ya Wilaya inaweza kuagiza hoja hiyo iwasilishwe kwa njia ifuatayo: "Je, msimamizi wa wilaya aliyeko wakati huu aendelee kuwa katika ofisi baada ya kikao hiki cha wilaya?"

Ikiwa kikao cha wilaya, kwa theluthi-mbili ya kura zilizopigwa kwa siri, kitaamua msimamizi wa wilaya aendelee kuwa katika ofisi, msimamizi huyo ataendelea kutumika kama kwamba hoja hiyo haikupigiwa kura.

Hata hivyo, ikiwa kikao cha wilaya kitakosa kuamua kwa kura kama hiyo kuendeleza huduma ya msimamizi wa wilaya, kipindi chake cha kuwa katika ofisi kitamalizika siku 30-180 kufuatia kumalizika kwa kikao hicho cha wilaya, kwa tarehe itakavyoamuliwa na msimamizi mkuu wa eneo akishauriana na Kamati ya Ushauri ya Wilaya. (206.2, 208, 239)

**205.14.** Kuchagua, kwa kura ya siri, makasisi watatu na waumini watatu ili wawe washirika wa Halmashauri ya Wilaya, watatumika kwa kipindi kisichozidi miaka minne, kama itakavyoamuliwa na kikao cha wilaya, na hadi waandamizi wao watakapochaguliwa na kuhitimishwa.

Hata hivyo, wakati wilaya itakapokuwa na zaidi ya jumla ya washirika 5,000, inaweza kuchagua kasisi mmoja na muumini mmoja zaidi kwa kila ongezeko la washirika 2,500 na sehemu kubwa ya mwisho ya washirika 2,500. (224)

**205.15.** Kuchagua Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya yenye washirika wasiopungua makasisi 5, ambapo wawili kati yao watakuwa msimamizi wa wilaya na katibu wa wilaya, ikiwa amewekwa wakfu, kuhudumu kwa miaka minne na hadi waandamizi wao watakapochaguliwa na kuhitimishwa. Katibu wa wilaya ambaye ni muumini atatumika kama mshirika asiyepiga kura wa halmashauri. Halmashauri hii itakutana kabla ya kikao cha wilaya kushughulikia mambo yote yaliyo chini ya mamlaka yake na kadiri inavyowezekana kukamilisha kazi yake kabla ya kikao cha wilaya. (229-231.10)

**205.16.** Kuchagua Halmashauri ya Wahudumu ya Mafunzo ya Wilaya yenye makasisi watano au zaidi, itakayotumika kwa miaka minne na hadi waandamizi wao watakapochaguliwa na kuhitimishwa. (232)

**205.17.** Ili kusimamia uwezo wake wa kutayarisha watahiniwa wa kuwekwa wakfu na kutoa msaada na nafasi za kuwajenga watumishi kwa ajili ya wahudumu wake, wilaya inaweza kuchagua idadi inayohitajika kutoka katika Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya na Halmashauri ya Mafunzo ya Wahudumu ya Wilaya watakaotumika kama Halmashauri ya Huduma ya Wilaya. Wahudumu waliochaguliwa watahudumu kwa miaka minne.

Halmashauri ya Huduma ya Wilaya, pamoja na msimamizi wa wilaya akiwa kama mwenyekiti kwa wadhifa wake anayesimamia ataratibu Halmashauri ya Huduma ya Wilaya kutekeleza kazi na majukumu yote ya Halmashauri ya Hati ya Kuhitimu kwa Wahudumu Wilaya na Halmashauri ya Elimu ya Wahudumu ya Wilaya. (216, 229-234.4)

**205.18**. Kuchagua Halmashauri ya Mali ya Kanisa ya Wilaya kuambatana na kifungu cha 236. (206.1)

**205.19.** Kuchagua ikiona ni vyema mojawapo au yote yafuatayo:

1. Halmashauri ya Uinjilisti ya Wilaya yenye washirika wasiopungua sita ikiwa ni pamoja na msimamizi wa wilaya;
2. Mkurugenzi wa wilaya wa uinjilisti.

Watu watakaochaguliwa watatumika hadi kuahirishwa kwa kikao cha wilaya kinachofuata na hadi waandamizi wao watakapochaguliwa na kuhitimishwa. (206.1, 215)

**205.20.** Kuchagua Halmashauri ya Wilaya ya Huduma za Kimataifa ya Shule ya Jumapili na Uinjilisti kulingana na utaratibu ulioelezwa katika kifungu cha 241, itakayotumika hadi waandamizi wao watakapochaguliwa na kuhitimishwa. (206.1, 215)

**205.21.** Kuchagua Kamati ya Fedha ya Kikao cha Wilaya, yenye idadi sawa ya wawakilishi wa makasisi na waumini kutumika kwa kipindi kisichozidi miaka minne, kama itakavyoamuliwa na kikao cha wilaya, na hadi waandamizi wao watakapochaguliwa na kuhitimishwa. Msimamizi wa wilaya na mweka hazina watakuwa washirika kwa wadhifa wao. (238-238.3)

**205.22.** Kuchagua Mahakama ya Rufani ya Wilaya yenye makasisi watatu, pamoja na msimamizi wa wilaya, itakayotumika kwa kipindi kisichozidi miaka minne na hadi waandimizi wao watakapochaguliwa na kuhitimishwa. (610)

**205.23.** Kuchagua, kwa kura ya siri, katika kikao kitakachofanyika miezi 16 kabla ya mkutano wa Kikao Kikuu, au miezi 24 katika sehemu ambazo hati za kusafiria nchi za nje au mipango mingine isiyo ya kawaida ya usafiri inahitajika, wajumbe wote waumini na wahudumu, isipokuwa mmoja ambaye atakuwa msimamizi wa wilaya. Kila kikao cha wilaya ya Kiwango cha 3 itakuwa na haki ya kuwakilishwa katika Kikao Kikuu na idadi sawa ya wahudumu na waumini. Msimamizi wa wilaya wakati wa Kikao Kikuu atakuwa mmoja wa wajumbe wahudumu, na wajumbe wengine wahudumu waliobaki watakuwa makasisi waliowekwa wakfu. Ikiwa msimamizi wa wilaya hataweza kuhudhuria, au ikiwa ofisi ya msimamizi wa wilaya ilikuwa wazi na mwingine hajateuliwa, mwakilishi aliyechaguliwa inavyostahili atakaa mahali pake. Kamati ya Uteuzi itawasilisha makaratasi ya kura ambayo yana idadi mara tatu ya hesabu ya wajumbe wanaohitajika kutoka wilaya hiyo, upande wa wahudumu na waumini. Kutoka katika watu hao walioteuliwa, idadi inayotakikana ya wajumbe na wabadilishanaji wao watachaguliwa kuambatana na kifungu cha 301.1-301.3. Kila kikao cha wilaya kinaweza kuchagua watu wengine

wasiozidi idadi ya wajumbe mara mbili. Katika hali ambapo hati za usafiri ni tatizo, kikao cha wilaya kinaweza kuagiza Halmashauri ya Wilaya kuchagua watu wengine badala yake. Wajumbe waliochaguliwa wanatakiwa kuhudhuria kwa uaminifu mikutano yote ya Kikao Kikuu kuanzia mwanzo hadi mwisho isipokuwa wawe wamezuiwa na jambo lisiloweza kuepukika. (25-25.2, 301.1-301.3, 303, 332.1)

**205.24.** Kuanzisha, ikiona ni vyema, utaratibu wa ushirika wa kushiriki kwa makanisa yao ya mtaa. (Washirika wa kushiriki hawapaswi kuhesabiwa kama washirika kamili kwa kusudi la uwakilishi.) (108)

**205.25.** Kufanya matayarisho ya kukaguliwa kwa vitabu vyote vya hesabu ya mweka hazina wa wilaya kila mwaka, aghalau kwa kiasi cha kiwango kinachohitajika na sheria ya kitaifa au sheria ya nchi kama inahitajika, au viwango vingine ambavyo vinatambuliwa na kuhitimu, aidha na Kamati ya Ukaguzi ya Wilaya, kamati ya watahiniwa binafsi, au na watu waliohitimu vizuri ambao wamechaguliwa na Halmashauri ya Wilaya. (225.24)

**205.26.** Kutuma kwa Kikao Kikuu, kupitia kwa katibu wa wilaya, kitabu rasmi cha mambo yaliyotendeka kwa kipindi cha miaka minne iliyopita, ili kiifadhiwe. (207.3-207.4, 220.7)

**205.27**. Kumpa mhudumu uhusiano wa kustaafu kwa pendekezo la Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya au Halmashauri ya Huduma ya Wilaya. Mabadiliko yoyote ya uhusiano huo ni lazima yaidhinishwe na kikao cha wilaya, kwa pendekezo la Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya au Halmashauri ya Huduma ya Wilaya. (231.8, 536)

**205.28.** Kujadili na kutunza kazi yote ya Kanisa la Mnazareti katika mipaka ya kikao cha wilaya.

**205.29.** Kutekeleza shughuli nyingine yoyote inayohusiana na kazi, ambayo maelezo yake hayapo katika kitabu hiki, kuambatana na moyo na kanuni za Kanisa la Mnazareti.

**206. Kanuni zingine zinazohusu Vikao vya Wilaya.** Kikao cha wilaya kinaweza kutoa mamlaka, mahali sheria za nchi zinaruhusu, kwa Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya isajiliwe. Baada ya kusajiliwa kama ilivyoelezwa hapo juu, Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya itakuwa na uwezo, kwa azimio lake yenyewe, kununua, kumiliki, kuuza, kubadilishana, kuweka amana, mkataba wa amana, kuweka rehani, kukodisha, na kutoa hati ya kumiliki mali yoyote, ya binafsi au viwanja na nyumba, kama itakavyohitajika au kuonekana kuwa inafaa kwa kusudi la shirika lililosajiliwa. (225.6)

**206.1.** Kadiri itakavyowezekana, ushirika wa halmashauri na kamati za wilaya utakuwa na idadi sawa ya wahudumu na waumini, isipokuwa kama imeelezwa tofauti katika *Kitabu cha Mwongozo.*

**206.2. Wasimamizi wa wilaya za Kiwango cha 1 na cha 2** watachaguliwa kulingana na kifungu 200.2 cha kitabu cha mwongozo. Wilaya ya kiwango cha pili inaweza kurejeshwa katika kiwango cha kwanza hadi itakapoweza kutimiza matakwa ya kiwango cha 2.

**206.3.** Ikiwa afisa msimamizi wa mkutano wa kikao cha wilaya ataona kwamba haiwezekani kuendelea na shughuli za kikao cha wilaya na kwa hivyo aahirishe, asitishe, au afunge kikao cha wilaya, msimamizi mkuu aliye na mamlaka, akishauriana na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu, atateua maafisa wote wa wilaya ambao walikuwa hawajachaguliwa kabla ya kuahirishwa kwa kikao cha wilaya, kutumika kwa kipindi cha mwaka mmoja.

## D. Jarida la Kikao cha Wilaya

**207.** Jarida la matukio litakuwa ni kumbukumbu la matukio ya mkutano wa kikao cha wilaya.

**207.1.** Jarida hili ni lazima liandaliwe katika muundo ulioruhusiwa na ofisi Kuu ya Katibu. Nakala za karatasi zitachapishwa nyumbani.

**207.2.** Habari tofauti za shughuli mbali mbali zitaandikwa katika vifungu tofauti katika kitabu hicho.

**207.3.** Kitabu hicho ni lazima kihaririwe kwa uangalifu kwa kusudi la kukaguliwa na Kikao Kikuu. (205.26, 220.7)

**207.4.** Kitabu kamili rasmi kwa kila kipindi cha miaka minne kitaifadhiwa katika kumbukumbu za kikao cha wilaya na Kikao Kikuu. (220.5, 220.7)

**207.5.** Kitabu hicho kitapangwa kadiri iwezekanavyo kulingana na orodha ya yaliyomo iliyotayarishwa na katibu mkuu akishauriana na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu. Orodha ya yaliyomo itakabidhiwa kwa katibu wa wilaya kabla ya mkutano wa kikao cha wilaya.

**207.6.** Kitabu hicho hakitakuwa tu na maelezo ya wachungaji wanaohudumu katika makanisa ya mtaa, bali pia shughuli zote za kawaida na shughuli maalum zilizokubaliwa kufanywa na washirika wahudumu na waumini wa kikao cha wilaya ambao wamepewa utumishi wowote wa dhehebu hili ambao unaweza kuwawezesha kufikiriwa wanapotuma maombi ya fadhili kutoka kwa Halmashauri ya Malipo ya Kustaafu inayoshughulikia malipo ya kustaafu na fadhili katika wilaya hiyo. (115)

### E. Msimamizi wa Wilaya

**208.** Kipindi cha kuanza kuwa katika ofisi cha msimamizi wa wilaya aliyechaguliwa katika kikao cha wilaya kitaanza siku 30 baada ya kikao cha wilaya kumalizika. Kipindi hicho kitaendelea kwa muda wa miaka miwili, na kitamalizika siku 30 baada ya kuhairishwa kwa kikao cha wilaya cha pili baada ya kuchaguliwa kwake. Wakati wa kikao hicho cha wilaya, msimamizi anaweza kuchaguliwa tena au mwandamizi wake anaweza kuchaguliwa au kuteuliwa na kuhitimishwa. Kipindi cha kuanza kuwa katika ofisi ya msimamizi wa wilaya ambaye ameteuliwa na msimamizi mkuu wa eneo hilo kitaanza wakati wa uteuzi huo, na kitakuwa ni pamoja na sehemu ya mwaka wa kanisa iliyosalia ambapo msimamizi huyo aliteuliwa, na kitaendelea kwa miaka miwili ifuatayo ya kanisa. Kipindi cha kuwa katika ofisi kitamalizika siku 30 baada ya kumalizika kwa kikao cha wilaya cha mwisho kufuatia utumishi wa miaka miwili. Katika kikao hicho, msimamizi huyo anaweza kuchaguliwa kwa kipindi kingine, au mwandamizi wake atachaguliwa au kuteuliwa na kuhitimishwa. Kasisi ambaye ameajiriwa na ofisi ya wilaya hataweza kuchaguliwa au kuteuliwa katika ofisi ya msimamizi wa wilaya kwenye wilaya ambayo wanatumika bila idhini ya Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya na ya idhini ya msimamizi mkuu wa eneo (kufuatana na kifungu cha 115). (2035.11-205.13).

**209.** Ikiwa kwa sababu yoyote kutatokea nafasi katika ofisi ya msimamizi wa wilaya kabla ya mkutano wa kikao cha wilaya, wasimamizi wakuu, kwa pamoja wanaweza kujaza nafasi hiyo, wakishauriana na Kamati ya Ushauri ya Wilaya. Mashauriano yatakuwa ni pamoja na mwaliko wa kamati, kwa jumla, kuwasilisha majina yatakayofikiriwa pamoja na yale majina yaliyoletwa na msimamizi mkuu wa eneo. (239. 307.7)

**209.1.** Ofisi ya msimamizi wa wilaya ya Kiwango cha 1 na Kiwango cha 2 inaweza kutangazwa kuwa na nafasi kwa jambo ambalo limependekezwa na msimamizi mkuu katika mamlaka. Ofisi ya msimamizi wa wilaya katika Kiwango cha 3 cha wilaya inaweza kutangazwa kuwa na nafasi baada ya theluthi mbili za kura za Kamati ya Ushauri ya Wilaya. (239, 321)

**209.2.** Iwapo kutatokea hali ya muda mfupi ya msimamizi wa wilaya anayehudumu kutoweza kufanya kazi, msimamizi mkuu wa eneo hilo, akishauriana na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya, anaweza kuteua kasisi aliyehitimu kutumika kama msimamizi wa wilaya wa muda. Swala hilo la kutowezeshwa kwa msimamizi wa wilaya, litaamuliwa na msimamizi mkuu wa eneo hilo akishirikiana na Halmashauri ya Wilaya. (307.8)

**209.3.** Baada ya kujiuzulu au kuachishwa kazi kwa msimamizi wa wilaya, wafanyakazi wa ofisi ya wilaya, msimamizi mkuu wa ofisi au msaada wowote wa chini au mashirika yenye kujumuishwa ya wilaya wanaolipwa au wasiolipwa, kama vile msaidizi wa msimamizi na katibu wa ofisi, wawasilisha barua zao za kujiuzulu zinazoambatana na tarehe ya mwisho ya usimamizi wa wilaya. Hata hivyo, mfanyikazi mmoja au wawili wanaweza kubaki kwa idhini iliyoandikwa ya msimamizi mkuu wa eneo hilo na Halmashauri ya Wilaya, lakini isizidi tarehe ya msimamizi mpya anayeanza kazi. (245.3)

**209.4.** Baada ya kushauriana na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya na kuidhinishwa na msimamizi mkuu wa eneo hilo, msimamizi mpya wa wilaya aliyechaguliwa au kuteuliwa anaweza kuwa na nafasi ya kupendekeza kuajiriwa kwa wafanyakazi waliokuwepo hapo awali. (245.3)

**210.** Kazi ya msimamizi wa wilaya ni kupeana mwelekeo na uongozi wa kiroho kwa wachungaji na mikusanyiko za wilaya kwa:

- Kuonyesha mfano wa maisha ya maombi na kujifunza Maandiko
- Kuendeleza thiolojia ya kibiblia ya kiuchungaji na utaratibu wake kati ya watumishi wa wilaya
- Kuendeleza thiolojia takatifu ya Kiwesley na utaratibu wake katika wilaya yote
- Kuwa maono ya uinjilisti na kuanzisha makanisa mapya ndani ya wilaya
- Kuwasaidia washirika wa wilaya kuendeleza mambo yanayohusu afya.

**211. Kazi ya msimamizi wa wilaya** ni:

**211.1.** Kuratibu, kutambua, na kusimamia makanisa ya mtaa yaliyo katika mipaka ya wilaya iliyo chini ya usimamizi wake, kwa idhini ya msimamizi mkuu aliye na mamlaka. (100, 538.15)

**211.2.** Kupatikana kwa makanisa ya mtaa katika wilaya yake kama atakavyohitajika, na kama itakavyohitajika, kukutana na halmashauri ya kanisa kushauriana kuhusu mambo ya kiroho, kifedha, na mambo ya uchungaji, akitoa ushauri na usaidizi unaohitajika kama atakavyoona kuwa ni vyema kwa kanisa.

**211.3.** Katika hali ambazo msimamizi wa wilaya ameona kuwa kanisa la mtaa lina shida, huduma yake inafifia, na kuendelea kwa hali hiyo ni tisho kwa uthabiti wa kanisa na huduma zake, msimamizi wa wilaya anaweza kuwasiliana na mchungaji au halmashauri ya kanisa kukadiria na kujadili hali hiyo na kutafuta suluhisho lake. Kila juhudi itafanywa ya

kushirikiana na mchungaji pamoja na halmashauri ya kanisa kutatua mizozo na matatizo yaliosababisha kuenda chini kwa misheni.

Ikiwa msimamizi wa wilaya, baada ya kufanya kazi na mchungaji pamoja na halmashauri ya kanisa, ataamua kuwa kuna haja ya kuchukua hatua zaidi, anaweza kuchukua hatua zinazofaa, ikikubaliwa na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya kutatua shida hiyo. Hatua hizo zinaweza kuwa ni pamoja na:

1. kuondolewa kwa mchungaji;
2. kuvunjwa kwa halmashauri ya kanisa;
3. kuanzishwa kwa utaratibu unaohitajika kurejesha uthabiti wa kanisa na kuimarisha huduma zake.

Mali ya kanisa lililoratibiwa itabaki chini ya uongozi wa kanisa la mtaa lililoshirikishwa, labda iwe kanisa hilo limetangazwa kuwa haliendelei kulingana na kifungu cha 106.5 au lisiloratibiwa kulingana na kifungu cha 106.1. Msimamizi mkuu wa eneo hilo atafahamishwa juu ya hatua zilizochukuliwa katika siku 30.

**211.4.** Wakati katika maoni ya msimamizi wa wilaya, kanisa la mtaa limetangazwa kuwa katika mzozo kufuatana na kifungu cha 126.1 limetimiza kushauriwa kulikotumiwa na liko tayari kurudi kwa huduma yake katika hali iliyo sawa, kanisa la mtaa linaweza kutangazwa kuwa halina mzozo tena kwa wingi wa kura za Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya. Msimamizi wa wilaya atafahamisha msimamizi mkuu wa eneo hili katika siku 30.

**211.5.** Kupanga na kutekeleza, pamoja na kila halmashauri ya kanisa la mtaa, ukaguzi wa kawaida wa uhusiano kati ya mchungaji na kanisa kulingana na kanuni za kifungu cha 123.-123.7. Msimamizi wa wilaya atatoa ripoti ya ukaguzi wa kawaida wa uhusiano kati ya mchungaji na kanisa iliongozwa na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya na msimamizi mkuu katika wa eneo hilo.

**211.6.** Kuwa na mamlaka maalum ya kusimamia na uongozi wa makanisa mapya au vituo vyote vya misheni vya Kanisa la Mnazareti vilivyoko katika wilaya anayosimamia.

**211.7.** Kuteua au kupendekeza kwa Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya, mtu atayejaza nafasi, iwapo kutatokea nafasi, katika ofisi ya katibu wa wilaya. (219.1)

**211.8.** Kuteua au kupendekeza kwa Halmashauri ya Wilaya, mtu atayejaza nafasi, iwapo kutatokea nafasi katika ofisi ya mtunza hazina wa wilaya. (222.1)

**211.9.** Kuteua mkurugenzi wa wilaya wa huduma zinazotekelezwa kwa jeshi na magereza ili kuendeleza uinjilisti na utakatifu kupitia kwa huduma za magereza. (240)

**211.10.** Kushauriana na halmashauri ya kanisa kuhusu uteuzi wa kasisi au mhudumu mwenye hati (alama ya kasisi) anayefaa kuwa mchungaji wa kanisa la mtaa na kuidhinisha au kukataa uteuzi kama huo, kwa idhini zaidi ya Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya kama vile inavyohitajika katika kifungu cha 115. (129.2, 159.8, 225.16)

**211.11.** Kupanga ukaguzi maalum wa uhusiano wa mchungaji na kanisa katika kipindi cha siku 90 baada ya halmashauri ya kanisa kutuma ombi la ukaguzi huo, kuhusu kuendelea kwa uhusiano wa kiuchungaji kati ya mchungaji na kanisa.

**211.12.** Kuidhinisha au kukataa kutolewa kwa hati ya kuhudumu kwa mshirika yeyote wa Kanisa la Mnazareti ambaye ataomba hati ya mhudumu wa mtaa au kutaka hati yake ya mhudumu wa mtaa ifanywe upya kutoka kwa halmashauri ya kanisa la mtaa ambalo halihudumiwi na kasisi kama mchungaji (531.1, 531.3)

**211.13.** Kuidhinisha au kukataa kutoa idhini kwa maandishi maombi kutoka kwa mchungaji na halmashauri ya kanisa la mtaa ya kuajiri wasaidizi wachungaji au wasaidizi wa mtaa wa kulipwa (kama vile, wasaidizi wa mchungaji, wahudumu au wakurugenzi wa elimu ya Kikristo; watoto, vijana, na watu wazima, wakurugenzi wa muziki, shule za kanisa, {za msingi na za upili}, n.k). Jambo la msingi litakalomuongoza msimamizi wa wilaya katika kufanya uamuzi wa kuidhinisha au kukataa kuajiriwa kwa wasaidizi wa kulipwa litakuwa ni uwezo na kupenda kwa kanisa la mtaa kutimiza matakwa yake katika kanisa lao la mtaa, wilaya, na kanisa kuu. Ni wajibu wa mchungaji kuchunguza na kuchagua wachungaji na wasaidizi wengine katika kanisa la mtaa. Hata hivyo, msimamizi wa wilaya atakuwa na haki ya kuidhinisha au kukataa mchungaji msaidizi aliyeteuliwa. (129.27, 159-159.8)

**211.14.** Kuidhinisha au kukataa, pamoja na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya, maombi kutoka kwa makanisa ya mtaa ya kuanzisha na kuendesha miradi ya shule za Kikristo. (151, 225.14, 517)

**211.15.** Kuweka sahihi na kutekeleza, pamoja na katibu wa Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya, hati zote za kisheria za wilaya. (225.6)

**211.16.** Kuteua kwa Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya na kusimamia wasaidizi wote wa kulipwa katika wilaya. (245)

**211.17.** Kuteua wachungaji kulingana na kifungu cha 117.

**211.18.** Msimamizi wa wilaya anaweza, ikikubaliwa na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya, kuteua washirika wa halmashauri ya kanisa (mawakili

na wadhamini), mwenyekiti wa Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa, na maafisa wengine wa kanisa (katibu, mtunza hazina), ikiwa kanisa limeratibiwa kwa kipindi cha chini ya miaka mitano, au lina washirika chini ya 35 waliopiga kura kwenye mkutano wa mwaka uliopita wa kanisa, au linapokea msaada wa kifedha mara kwa mara kutoka kwa wilaya, au limetangazwa kuwa kanisa linalokabiliwa na matatizo. Jumla ya idadi ya washirika wa halmashauri kama hiyo haitakuwa chini ya watu watatu. (117, 126)

**211.19.** Kuwezesha kuchunguzwa kwa mashtaka au makosa yaliyotolewa kwa maandishi dhidi ya mhudumu katika wilaya yake, kulingana na kifungu cha 606-606.3.

**211.20.** Kuteua katika kushaurina na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya mtumishi na muumini wa kutumika kama timu ya ukombozi iliyotayarishwa kutoa majibu kwa wakati na kiukombozi kwa mhudumu, mke au mume wake na familia, kanisa, na jumuiya wakati mtumishi amehusika kwa vitendo visivyofaa. Hali kama hiyo ikitokea, msimamizi wa wilaya ataeneza timu ya ukombozi mara moja inavyowezekana na kulingana na mpango wa wilaya. (225.5, 540.1)

**211.21.** Msimamizi wa wilaya atapanga na kutekeleza mahojiano ya kujikadiria, na kuchunguzwa upya kwa mwinjilisti aliyetimiza matakwa ya kanisa, akishauriana naye kulingana na kifungu cha 510.4.

**211.22.** Kuweka bidii ya kutia moyo, pamoja na uongozi wa wilaya, kila kanisa la mtaa kukutana na malengo yao ya fedha ya jumla, wilaya, na elimu.

**212.** Msimamizi wa wilaya, kwa ruhusa ya halmashauri ya kanisa, anaweza kuteua mtu atakayetoa huduma ya uchungaji kujaza nafasi iliyo wazi katika ofisi ya mchungaji hadi wakati wa mkutano utakaofuata wa kikao cha wilaya. Mtu aliyeteuliwa kwa huduma kama hiyo ya uchungaji anaweza kuondolewa katika huduma hiyo na msimamizi wa wilaya ikiwa huduma yake itakuwa si ya kuridhisha kwa halmashauri ya kanisa na kanisa la mtaa. (129.5, 524, 531.6)

**212.1.** Msimamizi wa wilaya, kwa ruhusa ya halmashauri ya kanisa na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya, anaweza kumteua mchungaji wa muda mfupi kujaza nafasi katika ofisi ya mchungaji, hadi mchungaji wa kudumu atakapoitwa. Msimamizi wa wilaya atapewa mamlaka ya kuongeza muda wa kutumika kwa mchungaji wa muda mfupi kama vile anavyohitajika kwa kushauriana na halmashauri ya kanisa. Mchungaji wa muda mfupi pia atatumika kama mjumbe kutoka katika kanisa lile anatumika kwa kikao cha wilaya kama mchungaji ana ushirika kwenye wilaya anayotumikia kwa muda mfupi.

Mchungaji kama huyo aliyepewa kazi ya muda mfupi yuko chini ya mamlaka ya msimamizi wa wilaya na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya wakati wote. Mchungaji huyo wa muda mfupi atakuwa tena na haki ya kuondolewa na msimamizi wa wilaya kwa kushaurianana na halmashauri ya kanisa. (526)

**213.** Msimamizi wa wilaya ana mamlaka ya kutekeleza shughuli zote za mchungaji kwa kanisa la mtaa lililo katika mipaka ya wilaya yake, ikiwa kanisa hilo halina mchungaji au mtu wa kutoa huduma ya uchungaji. (514)

**213.1.** Msimamizi wa wilaya anaweza kuongoza mkutano wa mwaka, au mkutano maalum wa kanisa la mtaa, au kuteua tu mwingine atakayefanya kazi hiyo kwa niaba yake. (113.5)

**214.** Ikiwa kwa sababu yoyote msimamizi mkuu wa eneo hilo atashindwa kuhudhuria au kuteua mwakilishi kuhudhuria mkutano wa kikao cha wilaya kwa niaba yake, msimamizi wa wilaya ataanzisha na kusimamia kikao hicho hadi uamuzi mwingine utakapofanywa na kikao cha wilaya. (307.4)

**215.** Msimamizi wa wilaya anaweza kujaza nafasi zilizo wazi katika kamati zifuatazo:

1. Kamati ya Fedha ya Kikao cha Wilaya
2. Kamati ya Wilaya ya Ukaguzi
3. Halmashauri ya Wahudumu ya Wilaya ya (au Halmashauri ya Hati za Kuhitimu na Masomo ya Wahudumu ya Wilaya)
4. Halmashauri ya Uinjilisti ya Wilaya au mkurugenzi wa uinjilisti wa wilaya
5. Halmashauri ya Wilaya ya Mali za Kanisa
6. Halmashauri ya Wilaya ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa.
7. Mahakama ya Rufani ya Wilaya
8. Halmashauri zingine za wilaya na kamati za kudumu ambazo kuteuliwa kwao hakukueleza katika *Kitabu cha Mwongozo* au kwa uamuzi wa kikao cha wilaya. (205.21, 205.25, 229.1, 232.1, 235, 236, 241, 610)

**215.1.** Msimamizi wa wilaya anaweza kuteua wenyeviti, makatibu na washirika wote wa halmashauri za wilaya na kamati za kudumu ambao kuteuliwa kwao hakukuelezwa katika *Kitabu cha Mwongozo* au kwa uamuzi wa kikao cha wilaya.

**215.2** Msimamizi wa wilaya, akishauriana na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya, atateua kamati ya uteuzi kutayarisha uteuzi wa kamati na ofisi za kawaida kabla ya mkutano wa kikao cha wilaya. (203)

**216.** Msimamizi wa wilaya atakuwa mwenyekiti wa Baraza la Ushauri la Wilaya na Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya na Halmashauri ya Wahudumu ya Wilaya. (224.2, 230.1)

**216.1.** Msimamizi wa wilaya atakuwa mshirika wa halmashauri na kamati zote zilizochaguliwa na zinazoendelea za wilaya anayohudumia kwa ajili ya wadhifa wake. (205.20-205.21, 237, 241,810, 811)

**217**. Msimamizi wa wilaya hatawajibika kwa fedha, kuhesabu pesa, au kugawa fedha za wilaya isipokuwa apewe na kuelekezwa na kura ya wingi za Halmashauri ya Wilaya; uamuzi kama huo, ikiwa utafanyika, utaandikwa vizuri na kuhifadhiwa kwenye taarifa ya Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya. Hakuna msimamizi wa wilaya au mshirika wa karibu wa familia yake ambaye ataruhusiwa kuwa na nafasi ya kufikia hazina ya fedha au mali ya wilaya bila uongozi wa ndani ulioelezwa na kuandikwa wazi ambao umeidhinishwa na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya. Watu wa karibu wa familia ya msimamizi wa wilaya watakuwa ni mke au mume, watoto, ndugu na dada, au wazazi. (218, 222-223.2)

**218.** Maamuzi yote rasmi ya msimamizi wa wilaya yatachunguzwa upya na kugeuzwa na kikao cha wilaya, na kukatiwa rufani.

**218.1.** Msimamizi wa wilaya wakati wote anapaswa kuheshimu ushauri wa msimamizi mkuu wa eneo lake na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu kuhusiana na mipango ya uchungaji na mambo mengine yanayohusu ofisi ya msimamizi wa wilaya.

## F. Katibu wa Wilaya

**219.** Katibu wa wilaya, aliyechaguliwa na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya, atatumika kwa kipindi cha kati ya mwaka mmoja hadi miaka mitatu, na hadi mwandamizi wake atakapochaguliwa na kuhitimishwa. (225.22)

**219.1.** Ikiwa katibu wa wilaya ataacha kuhudumu, kwa sababu yoyote, kabla ya mkutano wa kikao cha wilaya kitakachofuata, Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya itachagua mwandamizi wake atakayekuwa ameteuliwa na msimamizi wa wilaya kuchukua mahali pake. (211.7)

**219.2.** Katibu wa wilaya atakuwa mshirika wa kikao cha wilaya kwa wadhifa wake. (2010

**220. Kazi ya katibu wa wilaya itakuwa** ni:

**220.1.** Kuandika kwa usahihi na kuhifadhi kwa uaminifu mukhtasari wa kumbukumbu ya mambo yote yanayojadiliwa au kupitishwa katika kikao cha wilaya.

**220.2.** Kuandika kwa usahihi na kuhifadhi tarakimu zote za wilaya.

**220.3.** Kupeleka orodha zote za tarakimu kwa katibu mkuu ili zikaguliwe kabla ya kuchapishwa katika kitabu rasmi cha kanisa. (326.6)

**220.4.** Kuwa mtunzaji wa hati zote za kikao cha wilaya, na kuzikabidhi mara moja kwa mwandamizi wake.

**220.5.** Kuhifadhi kitabu rasmi cha kumbukumbu za wilaya kwa kila kipindi cha miaka minne. (207.4)

**220.6.** Kupeleka nakala za kutosha zilizochapishwa za muhtasari wa shughuli za kila kikao cha wilaya kwa Huduma ya Makao Makuu ili zigawanywe kwa maafisa wakuu wa Kanisa la Mnazareti.

**220.7.** Kupeleka kwa Kikao Kikuu, kwa niaba ya kikao cha wilaya, kitabu kamili rasmi cha shughuli za kikao cha wilaya kwa kipindi cha miaka minne iliyopita ili kihifadhiwe (205.26, 207.4-207.4)

**220.8.** Kufanya kazi nyingine yoyote ambayo inahusiana na ofisi yake.

**220.9.** Kupeleka mambo yote yanayohusiana na shughuli za wilaya ambayo yameletwa kwake katika kipindi cha mwaka huo kwa kamati inayostahili au halmashauri ya kudumu inayohusika.

**221.** Katibu wa wilaya anaweza kuwa na wasaidizi wengi kadiri kikao cha wilaya kitakavyochagua.

## G. Mtunza Hazina wa Wilaya

**222.** Mtunza hazina wa wilaya, aliyechaguliwa na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya, atahudumu kwa kipindi cha mwaka mmoja hadi mitatu na hadi mwandamizi wake atakapochaguliwa na kuhitimishwa. (225.21).

**222.1.** Ikiwa mtunza hazina wa wilaya ataacha kutumika, kwa sababu yoyote, kabla ya mkutano ufuatao wa kikao cha wilaya, Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya itachagua mwandamizi wake atakayeteuliwa na msimamizi wa wilaya. (211.8)

**222.2.** Mtunza hazina wa wilaya atakuwa mshirika wa kikao cha wilaya kwa ajili ya wadhifa wake. (201)

**223. Kazi ya mtunza hazina wa wilaya itakuwa** ni:

**223.1.** Kupokea pesa zote kutoka katika wilaya yake kama itakavyoagizwa na Kikao Kikuu, au na kikao cha wilaya, au na Halmashauri ya Wilaya, au kama mahitaji ya Kanisa la Mnazareti yatakavyokuwa. Matumizi yoyote ya pesa yatakuwa kulingana na maongozi na utaratibu wa kikao cha wilaya na Halmashauri ya Wilaya.

**223.2.** Kuhifadhi kumbukumbu sahihi ya pesa zote zilizopokewa na kutumiwa, na kutoa ripoti kila mwezi kwa msimamizi wa wilaya ili iwasilishwe kwa Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya na ripoti ya mwaka kwa kikao cha wilaya ambacho atakuwa chini yake.

## H. Halmashauri ya Wilaya

**224.** Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya itashirikisha msimamizi wa wilaya kwa ajili ya wadhifa wake na wahudumu watatu waliowekwa wakfu pamoja na waumini watatu ambao watachaguliwa kila mwaka kwa kura ya siri na kikao cha wilaya, au kwa kipindi kisichozidi miaka minne, kutumika hadi kuahirishwa kwa kikao cha wilaya kitakachofuata na hadi waandamizi wao watakapochaguliwa na kuhitimishwa. Hata hivyo, vipindi vya huduma yao vinaweza kuwa vya muda tofauti kwa kuchagua idadi fulani ya halmashauri hiyo kila mwaka.

Wakati idadi ya washirika katika wilaya itazidi 5,000, kikao cha wilaya kinaweza kuchagua mhudumu aliyewekwa wakfu mmoja zaidi na muumini mmoja kwa kila ongezeko la washirika 2,500 au sehemu kubwa ya mwisho ya washirika 2,500. (205.14)

**224.1.** Nafasi katika Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya inaweza kujazwa na washirika waliobaki wa halmashauri hiyo**.**

**224.2.** Msimamizi wa wilaya atakuwa mwenyekiti wa Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya kwa ajili ya wadhifa wake.

**224.3.** Halmashauri itachagua kutoka kwa ushirika wake katibu, ambaye ataweka taarifa yote ya hatua za halmashauri kwa umakini na kwa uangalifu kuzituma kwa mwandamizi wake.

**224.4.** Washirika waumini wa Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya watakuwa washirika wa kikao cha wilaya kwa ajili ya wadhifa wao, washirika wa Kongamano la Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa kwa ajili ya wadhifa wao, washirika wa Kongamano la Umisheni wa Mnazareti la Kimataifa kwa ajili ya wadhifa wao, na washirika wa Kongamano la Huduma ya Vijana ya Kimataifa kwa ajili ya wadhifa wao. (201, 224)

**225. Wajibu wa Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya** ni:

**225.1.** Kupanga tarehe ya kuanzia na kumalizia mwaka wa tarakimu za wilaya kulingana na kanuni za kifungu cha 114.1.

**225.2.** Kutoa habari kwa msimamizi wa wilaya na kushauriana naye kuhusu kuwaheshimu wahudumu na makanisa ya mtaa katika kikao cha wilaya. (115.6, 519)

**225.3.** Kuteua kamati ya uchunguzi itakayokuwa na wahudumu waliowekwa wakfu watatu au zaidi na waumini wasiopungua wawili kuchunguza mashtaka yaliyoletwa dhidi ya mtumishi. (606-606.3)

**225.4.** Kuchagua mahakama ya kusikiliza kesi ikiwa mashtaka yatatolewa dhidi ya mtumishi. (606.5-606.6)

**225.5.** Kujenga na kuchunguza kila mwaka mpango kamili ulioandikwa ambao unaambatana na maelekezo ya *Kitabu cha Mwongozo* ya kuongoza

jitihada katika kutoa majibu mwafaka kwa wakati unaofaa, nay a huruma kwa wahudumu wanaohusika mhudumu asiyefuata nidhamu, kwa familia, na kwa kongamano linalohusika. (538.20, 539-539.13)

**225.6.** Kujishirikisha, mahali ambapo sheria za nchi zinaruhusu na ikipewa mamlaka na kikao cha wilaya. Baada ya kusajiliwa, kama ilivyoelezwa hapo juu, Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya itakuwa na uwezo, kwa azimio lake, kununua, kumiliki, kuuza, kubadilishana, kuweka amana, kuweka hati kwa dhamana, kuweka rehani, kukodisha na kutoa haki ya kumiliki mali yoyote, na mali ya kibinafsi, kama itakavyohitajika au kuonekana kuwa inafaa kwa kusudi la usajili huo. Msimamizi wa wilaya na katibu wa Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya, au watu wengine waliopewa mamlaka na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya, iwe imesajiliwa au haijasajiliwa, watatekeleza na kutia sahihi kutolewa kwa hati zote za kumiliki viwanja na nyumba, kuweka amana, kurudishwa kwa amana, mikataba na hati nyingine za kisheria za Halmashauri ya wilaya. (206).

**225.7.** Wakati Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya itashirikisha, Kanuni za Kushirikishwa, sheria za Kitabu cha Mwongozo, au hati halali zinazolinganishwa zitaruhusu kwamba kushirikishwa kunaongozwa na kanuni za *Kitabu cha Mwongozo cha Kanisa la Mnazareti*. Hizi zitakuwa ni pamoja na kanuni kama vile itakavyopendekezwa na msimamizi mkuu wa eneo kuhakikisha kwamba kuondolewa au kujaribu kuacha Kanisa la Mnazareti, mali ya ushirika hayatahamishwa kutoka kwa Kanisa la Mnazareti. Kushirikishwa kwa wilaya kukishaidhinishwa na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu, baada ya kupendekezwa na msimamizi mkuu wa eneo hilo, Kanuni ya Kushirikishwa iliyopendekezwa itatumwa kwa ofisi ya Katibu Mkuu kwa kuchunguzwa na kuhifadhiwa na zitakuwa ni pamoja na kanuni sawa na zile za kifungu cha 102.4. (225.6)

**225.8.** Katika nchi ambazo sheria haziruhusu usajili kama huo, kikao cha wilaya kinaweza kuchagua Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya kuwa mdhamini wa wilaya mwenye uwezo, kwa azimio lake, ya kununua, kumiliki, kuuza, kubadilishana, kuweka amana, kuweka hati kwa dhamana, kuweka rehani, kukodisha na kutoa haki ya kumiliki mali yoyote, nyumba au viwanja na mali ya kibinafsi kama itakavyohitajika au kuonekana kuwa inafaa kwa kusudi la kutekeleza kazi yake katika wilaya. (102.6, 106.2, 225.6).

**225.9.** Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya, katika nchi ambazo inawezekana kwa makanisa ya mtaa kusajiliwa, inaweza, kwa ushauri wa mwanasheria anayestahili, kutoa mtindo wa fomu za muungo au usajili zitakazokubalika katika nchi ambayo wilaya iko. Mtindo huo wa fomu za

usajili unapaswa kila mara kushirikisha maelezo yote yaliyotolewa katika kifungu cha 102-102.5.

**225.10.** Kutumika kama mshauri kwa msimamizi wa wilaya katika usimamizi wake wa idara, halmashauri na kamati zote za wilaya.

**225.11.** Ili kuhimiza usimamizi bora na maisha ya bidii ya kiroho ya msimamizi wa wilaya, Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya, ikishirikiana na msimamizi mkuu wa eneo, inapaswa kupeana likizo ya sabato kwa msimamizi wa wilaya wakati wa kipindi cha kila mwaka wa saba mfululizo wa huduma kwa wilaya au baada ya kila mwaka wa saba. Wakati wa likizo ya sabato, mshahara wa msimamizi wa wilaya na faida zake utalipwa kamili. Msimamizi wa wilaya atafanya kazi na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya kutengeneza pendekezo la likizo ya sabato likiwa ni pamoja na muda, mpango wa kujijenga, na mpango wa endeleza jukumu wakati wa kipindi cha sabato.

**225.12**. Kuwasilisha kwa Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu mipango yoyote iliyopendekezwa ya kuanzishwa kwa kituo cha wilaya. Mipango kama hiyo itahitaji idhini iliyoandikwa ya Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu kabla haijatekelezwa. (319)

**225.13.** Kupendekeza kutolewa upya kwa hati ya mhudumu aliyepewa hati anayetumika kama mchungaji. (532.5)

**225.14.** Kukubali au kukataa maombi kutoka kwa makanisa ya mtaa ya kuendesha huduma za shule ya Kikristo ya malezi ya watoto (kuanzishwa kupitia Shule ya Upili) Msimamizi wa wilaya na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya wakiona ni vyema, Kamati ya Wilaya ya Shule za Kikristo a za malezi ya watoto (kuanzishwa kupitia Shule ya Upili) inaweza kuanzishwa. Kazi yake itakuwa kupendekeza maongozi, utaratibu na mambo yanayohusu elimu kwa Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya ili kutumiwa katika shule ya kanisa la mtaa ya malezi ya watoto (shule zinazopatikana kupitia sekondari), na kusaidia kuanzisha, kutegemeza na kuangalia shule hizo. (151, 211.14, 517)

**225.15.** Kuchagua Vituo vya Huduma ya Huruma (VHH) kila mwaka kulingana na maongozi ya jimbo yaliyoanzishwa. Ni vile tu Vituo vya Huduma ya Huruma ambavyo vimepewa idhini na wilaya ndivyo vitahitimu kama “misheni maalum iliyokubalika” kwa makusudi ya mchango kama ilivyo na kifungu 153.1.

**225.16**. Kukubali au kukataa ombi kutoka kwa halmashauri ya kanisa la mtaa la kuchagua kasisi aliyewekwa wakfu au mhudumu aliyepewa hati ya kuhudumu (alama ya kasisi) ya kuitwa mchungaji wakati mtu huyo pia ni mshirika wa kanisa la mtaa au anahudumu kama msaidizi wa kulipwa au

asiyelipwa wa kanisa la mtaa. Uamuzi huu utafanywa kwa kushauriana na msimamizi wa wilaya. (115, 129.2, 159.8, 211.10)

**225.17**. Kukubali au kukataa ombi kutoka kwa mtumishi la kila wakati la kuendesha shughuli za kanisa linalojitegemea ambazo haziko chini ya uongozi wa Kanisa la Mnazareti, au kuendeleza misheni inayojitegemea au shughuli za kanisa ambazo hazijaidhinishwa, au zinazohusiana na wafanyakazi waliko wa kanisa linalojitegemea au kundi lingine la kidini au dhehebu. Idhini ya ombi lolote kama hilo itahitajika kila mwaka. (528, 538.13)

**225.18**. Kuchagua au kuachisha kazi wasaidizi wowote wa kulipwa ambao wameajiriwa na wilaya. (245-245.1)

**225.19.** Kufanya kazi, kwa kushauriana na msimamizi wa wilaya, kama kamati ya fedha katikati ya vipindi vya kikao cha wilaya kwa mamlaka ya kurekebisha makadirio ya matumizi ya pesa za wilaya kama itakavyohitajika na kutoa ripoti yake kwa kikao cha wilaya. (223.1)

**225.20**. Kulinda mali yote ya wilaya, majengo au mali ya binafsi, ikiwa ni pamoja na hisa iliyo katika wilaya, ili isiweze kutumiwa kibinafsi au na shirika lolote mbali na Kanisa la Mnazareti. (102.4, 106.5, 206)

**225.21.** Kuchagua mtunza hazina wa wilaya, atayetumika kwa muda wa mwaka mmoja hadi miaka mitatu na hadi wakati ule mwandamizi wake atachaguliwa na kuhitimishwa. (222)

**225.22.** Kuchagua katibu wa wilaya, atakayetumika kwa muda wa mwaka mmoja hadi miaka mitatu na hadi mwandamizi wake atakapochaguliwa na kuhitimishwa. (219)

**225.23.** Kuthibitisha kuondolewa au majaribu ya kuondolewa kwa kanisa lolote la mtaa kutoka kwa Kanisa la Mnazareti kwa makusudi ya utekelezaji wa kuhamisha kwa hati za mali za wilaya kama ilivyopeanwa katika kifungu cha 106.2.

**225.24.** Ikiwa itahitajika, kufuatana na kifungu cha 205.25, kuchagua Kamati ya Ukaguzi ya Wilaya kutumika hadi mwisho wa kikao cha wilaya kitakachokuwepo. (205.25)

**225.25.** Kutoa ripoti ya mwaka kwa kikao cha wilaya iliyo na mukhtasari wa shughuli za kazi za halmashauri ikiwa ni pamoja na idadi ya mikutano iliyoitishwa.

**226.** Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya inaweza kutoa uhamisho wa ushirika kwa kasisi mhudumu wa wilaya, mhudumu wa elimu ya Kikristo, au shemasi wa kike, ambaye anataka kuhamia wilaya nyingine, kabla ya mkutano wa kikao cha wilaya ambayo ushirika wake uko. Uhamisho kama huo unaweza kukubaliwa na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya anayohamia, na kuwapa wale waliohamishwa haki kamili na manufaa

mengine ya ushirika katika wilaya wanayohamia. Kikao cha wilaya inayohamiwa kitatoa idhini ya mwisho ya kupokelewa kwa uhamisho kama huo na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya, baada ya pendekezo la kukubali la Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu. (205.8-205.9, 231.9-231.10, 508, 511, 537-537.2)

**226.1.** Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya, ikiombwa, inaweza kutoa Hati ya Sifa kwa mshirika wa kikao cha wilaya ambaye anataka kujiunga na dhehebu lingine. (815)

**227.** Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya, kwa idhini ya msimamizi wa wilaya, inaweza kumsimamisha kazi shemasi wa kike aliyepewa hati ikiwa itahitajika kwa manufaa ya kanisa, baada ya kujadiliana na halmashauri ya kanisa la mtaa ambalo shemasi huyo ni mshirika, na baada ya kusikiliza kesi yake kwa haki.

**228**. Iwapo mhudumu aliyewekwa wakfu au aliyepewa hati atawasilisha hati zake za kuhitimu kutoka kwa dhehebu lingine, kabla ya wakati wa kikao cha wilaya akiomba kujiunga na Kanisa la Mnazareti, hati hizo zitachunguzwa na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya. Itakuwa tu kwa pendekezo la kukubali la Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya ambapo mhudumu kama huyo atapokelewa katika ushirika wa kanisa la mtaa. (520, 532.2, 535)

## I. Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu

**229**. Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya itakuwa na makasisi wasiopungua 5 waliopewa kazi kama wahudumu waliowekwa wakfu, wawili wao watakuwa msimamizi wa wilaya na katibu wa wilaya, ikiwa wamewekwa wakfu. Katibu wa wilaya ambaye ni muumini anatumika kama mshirika wa halmashauri asiyepiga kura. Wale waliochaguliwa watatumika kwa kipindi cha miaka minne na hadi waandamizi wao watakapochaguliwa na kuhitimishwa. Hata hivyo, muda wa vipindi vya utumishi wao unaweza kuwa tofauti kwa kuchagua baadhi yao kila mwaka. (205.15)

**229.1.** Nafasi ikitokea katika Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya kabla ya kikao cha wilaya inaweza kujazwa kwa uteuzi utakaofanywa na msimamizi wa wilaya. (215)

**230**. Kufuatana na kuchaguliwa kwa Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya msimamizi wa wilaya ataitisha mkutano wa halmashauri hiyo kwa minajili ya uratibishaji kama ifuatavyo:

**230.1.** Msimamizi wa wilaya atatumika kama mwenyekiti wa halmashauri hiyo kwa ajili ya wadhifa wake; hata hivyo, kwa ombi lake, halmashauri hiyo inaweza kuchagua mwenyekiti mtendaji atakayetumika

katika wadhifa huo hadi mwisho wa kikao cha wilaya kitakachofuata kuchaguliwa kwake. (216)

**230.2.** Halmashauri hiyo itachagua kutoka kwa washirika wake katibu wa kudumu ambaye ataandaa utaratibu unaofaa wa kutayarisha na kuhifadhi kumbukumbu, ambazo zitakuwa mali ya wilaya kwa gharama ya kikao cha wilaya. Katibu huyo ataandika kwa uangalifu matukio ya halmashauri hiyo na atahifadhi kumbukumbu hizo kwa uaminifu pamoja na rekodi nyingine ambazo zinahusiana na kazi ya halmashauri hiyo na kuzikabidhi kwa mwandamizi wake bila kuchelewa.

**231. Wajibu wa Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu** ni:

**231.1.** Kuchunguza na kukagua kwa makini watu wote watakaokuwa wamewasilishwa kwenye kikao cha wilaya ili wachaguliwe katika wadhifa wa kasisi, shemasi, na mhudumu aliyepewa hati.

**231.2.** Kuchunguza na kukagua kwa makini watu wote wanaotaka kupata hati ya kutekeleza aina yoyote ya huduma, ikiwa pamoja na waumini na wahudumu wote wanaotaka kutambuliwa kwa huduma zinazopita kiwango cha kanisa la mtaa, na uhusiano mwingine wowote maalum ulioelezwa katika *Kitabu cha Mwongozo*.

**231.3.** Kumhoji kwa makini kila mtu anayetaka kuhudumu na kufanya uchunguzi mwingine wowote ambao utaonekana kuwa wa manufaa kuhusiana na ujuzi wake wa wokovu; ujuzi wa kibinafsi wa utakaso kamili kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu; ufahamu wa mafundisho ya Biblia; kukubaliana kikamilifu na mafundisho, Agano ya Sifa ya Kikristo na Agano ya Tabia ya Kikristo, na uongozi wa kanisa; thibitisho la neema, vipawa, utambuzi, uadilifu, na ufahamu wa kiroho, na kustahili kwake kwa huduma ambayo anahisi kuwa ameitwa.

**231.4.** Kuchunguza kwa makini tabia ya kila mtu anayetaka kutambua kama au la mtu huyo anahusika au yuko na sehemu ya tabia, ambayo akiendelea itakuwa kinyume na matakwa ya huduma anaomba kutekeleza.

**231.5.** Kuchunguza upya kwa kuidhinishwa kuteuliwa tena kwa mhudumu yeyote wa mtaa ambaye alikuwa ameteuliwa kama mchungaji wa muda ikiwa ataendelea na huduma hiyo baada ya kikao cha wilaya kufuatia kuteuliwa kwake. (531.6)

**231.6.** Kupeleleza na kuchunguza upya sababu za kushindwa kwa mhudumu aliyewekwa wakfu kutoa ripoti kwa kikao cha wilaya kwa miaka miwili mfululizo na kutoa pendekezo kwa kusanyiko la wilaya kuhusu kuendelea kuorodhesha jina lake katika Orodha zilizochapishwa za Wahudumu.

**231.7**. Kuchunguza ripoti kuhusu mhudumu aliyewekwa wakfu zinazoonyesha kwamba ameweka ushirika wake wa kanisa katika kanisa lingine lolote au amejiunga na huduma ya dhehebu au kundi lingine au anajihusisha na shughuli zingine za kibinafsi bila idhini iliyoruhusiwa rasmi, na kutoa pendekezo kwa kikao cha wilaya kuhusu kuondolewa kwake katika orodha ya makasisi (112, 538.13)

**231.8.** Kupendekeza kwa kikao cha wilaya uhusiano wa kustaafu kwa mhudumu anayeomba uhusiano kama huo na ambaye, kwa uamuzi wa halmashauri hiyo, hawezi kuendelea na utumishi wa huduma kwa sababu ya umri au ulemavu. (205.27, 536)

**231.9.** Kupendekeza kwa kikao cha wilaya wahudumu na wale waliopewa vyeti vya huduma, uhamisho kwa wilaya nyingine, hii ikiwa ni pamoja na uhamisho wa muda ambao umehidhinishwa na halmashauri ya wilaya. (205.9, 537-537.2)

**231.10.** Kupendekeza kwa kikao cha wilaya watu wenye hati za kuhitimu kwa mhudumu, wahudumu na wale waliopewa vyeti kwa huduma inayoendelea, kupokelewa kwa uhamisho wao kutoka kwa wilaya nyingine, hii ikiwa ni pamoja na uhamisho wa muda ulioidhinishwa na halmashauri ya wilaya. (205.8, 537-537.2)

## J. Halmashauri ya Wilaya ya Mafunzo ya Wahudumu

**232.** Halmashauri ya Mafunzo ya Wahudumu ya Wilaya itakuwa na wahudumu watano au zaidi waliowekwa wakfu, waliochaguliwa na kikao cha wilaya, kutumika kwa muda wa miaka minne na hadi waandamizi wao watakapochaguliwa na kuhitimishwa. Hata hivyo, muda wa vipindi vyao vya utumishi unaweza kutofautiana kwa kuchagua baadhi yao kila mwaka. (205.16)

**232.1.** Nafasi zinazotokea katika Halmashauri ya Mafunzo ya Wahudumu ya Wilaya kabla ya mkutano wa kikao cha wilaya zinaweza kujazwa kwa uteuzi utakaofanywa na msimamizi wa wilaya. (215)

**233.** Kabla ya kumalizika kwa kikao cha wilaya ambacho halmashauri hiyo ilichaguliwa, msimamizi wa wilaya au katibu wa wilaya ataitisha mkutano wa washirika wote wa halmashauri hiyo kwa uratibishaji na ugawaji wa kazi kama ifuatavyo:

**233.1**. Halmashauri hiyo itachagua mwenyekiti kutoka miongoni mwa washirika wake. Watachagua mhudumu aliyewekwa wakfu kuwa katibu wake, ambaye pamoja na washirika wengine, watakuwa na jukumu la kuwahoji na kuwaendeleza wanafunzi kupitia kwa Ratiba ya Mafundisho ya Kuongozwa ya Wahudumu hadi wakamilishe matakwa ya kuwekwa

wakfu. Watahifadhi kumbukumbu ya kudumu ya wanafunzi wote. (233.5, 529.1-529.3)

**233.2.** Mwenyekiti atagawia washirika wengine wa halmashauri hiyo kazi na usimamizi wa wanafunzi wote walioandikishwa katika ile ratiba ya masomo ya kuongozwa. Wajibu huo utaendelea kwa muda wote ambao wanafunzi watakuwa wanaendelea na mafundisho katika kipindi cha utumishi wa mwanakamati huyo isipokuwa kama kuna makubaliano mengine yaliyoafikiwa.

**233.3.** Mwenyekiti atahudhuria mikutano yote ya halmashauri hiyo, isipokuwa awe amezuiliwa na mambo yasiyoweza kuepukika, na atasimamia shughuli za halmashauri hiyo kila mwaka. Iwapo mwenyekiti hatakuwepo, katibu wa halmashauri hiyo atafanya kazi ya mwenyekiti kwa muda.

**233.4.** Katibu atatayarisha kitabu cha kumbukumbu cha mafundisho ya wahudumu kwa gharama ya kikao cha wilaya, ambacho kitakuwa mali ya kikao cha wilaya, na kitatumika kulingana na maagizo yaliyoko katika "*Kitabu cha Maelezo ya Ustawi wa Kihuduma."*

**233.5.** Washirika wengine wa halmashauri hiyo watahudhuria kwa uaminifu mikutano ya halmashauri hiyo na watasimamia wanafunzi waliowekwa chini yao kwa: (1) kuwatia moyo, kuwapa mawaidha, na kuwaongoza; na (2) kuwa mfano unaoweza kuigwa na wanafunzi wa vitendo na mazungumzo kuhusu uadilifu wa kasisi, mkazo ukiwekewa jinsi mhudumu anavyoweza kujiepusha na tabia ya uzinzi. (233.1)

**233.6.** Halmashauri hiyo itashirikiana na msimamizi wa wilaya na ofisi ya Utumishi kwa Wahudumu ya Ulimwengu kupitia Kamati ya Halmashauri ya Masomo ya Mbali mbali (KHMM) katika kutafuta njia za kuwatia moyo, kusaidia na kuelekeza wanafunzi wanaoendelea na masomo au taaluma mbali mbali katika vyuo vya Biblia, vyuo vikuu au seminari za kanisa la Mnazareti**.**

**234**. Halmashauri hiyo inaweza kuanzisha madarasa au semina ili kusaidia wahudumu waliopewa vyeti au wanafunzi wengine katika kuendelea na mafunzo mbali mbali, na kuanzisha, ikiwa wilaya itakubali kugharamia, maktaba za vitabu vyote vinavyohitajika vinavyoweza kuazimwa na wanafunzi ikihitajika.

**234.1.** Mwenyekiti na katibu wa Halmashauri ya Mafunzo ya Wahudumu wamepewa mamlaka ya kuandikisha mwanafunzi katika masomo ya wahudumu, wakishauriana na msimamizi wa wilaya. (233.1-233.2, 529.1-529.3)

**234.2**. Halmashauri hiyo itatekeleza wajibu wake kuambatana na muongozo ulioko katika Kitabu rasmi cha *Maelezo ya Ustawi wa Kihuduma*.

**234.3**. Halmashauri hiyo itaripoti mambo yote yanayohitajika kuhusu jinsi kila mwanafunzi anavyoendelea na elimu yake kwa Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya kwa wakati unaofaa kuiwezesha halmashauri hiyo ya kutoa hati za kuitimu kwa wahudumu kutayarisha mapendekezo yake kabla ya kikao cha wilaya. Halmashauri ya Mafunzo ya Wahudumu ya Wilaya itapendekeza kwa kikao cha wilaya wale wanaohitaji kuorodheshwa kwa masomo ya kihuduma, jinsi wale waliorodheshwa wanavyoendelea, na wale wanaokaribia kuhitimu kutoka katika masomo hayo ya wahudumu. Kuorodheshwa huko kwa wanafunzi, na jinsi wanavyoendelea au kuhitimu, kutapaswa kulingana na mwongozo uliowekwa na ofisi ya Utumishi kwa Wahudumu kupitia Kamati ya Halmashauri ya Masomo ya Mbalimbali.

**234.4**. Halmashauri ya Mafunzo ya Wahudumu ya Wilaya itakuwa na jukumu la kuendeleza elimu kwa wahudumu waliopewa vyeti na wahudumu wengine katika wilaya ikishirikiana rasmi na Chuo cha Biblia au chuo kikuu cha jimbo na ofisi ya Utumishi kwa Wahudumu ya Ulimwengu kupitia Kamati ya Halmashauri ya Masomo ya Mbalimbali, na chini ya uongozi wa msimamizi wa wilaya. Elimu ya kuendelea ya wahudumu itahusisha elimu ya maadili kwa makasisi inayotilia mkazo jinsi muhudumu anavyoweza kujiepusha na tabia ya uzinzi.

## K. Halmashauri ya Wilaya ya Uinjilisti, au Mkurugenzi wa Uinjilisti

**235**. Kikao cha wilaya kinaweza kuchagua Halmashauri ya Uinjilisti ya Wilaya au mkurugenzi wa uinjilisti wa wilaya. Watakaochaguliwa watatumika hadi mwisho wa kikao cha wilaya kitakachofuata kuchaguliwa kwao na hadi waandamizi wao watakapochaguliwa na kuhitimishwa. (205.19)

**235.1.** Katika ushirikiano na msimamizi wa wilaya, Halmashauri ya Uinjilisti ya Wilaya, au mkurugenzi wa uinjilisti wa wilaya, watatafuta njia za kuanzisha na kukuza uinjilisti na kusisitiza umuhimu wa uinjilisti wa utakatifu kwa kutoa nafasi za mafunzo, kwa kuendesha mikutano ya hadhara, kwa kutilia mkazo haja ya kuhuishwa kwa kanisa la mtaa na wainjilisti wenye mwito wa Mungu, na kwa kila njia nyingine inayojulikana, kuleta mageuzi katika wilaya katika kutimiza Tume Kuu ya Yesu Kristo kama wajibu wa kwanza wa utendaji kazi wa Mwili wa Kristo.

### L. Halmashauri ya Wilaya ya Mali ya Kanisa

**236.** Halmashauri ya Mali ya Kanisa ya Wilaya itakuwa na msimamizi wa wilaya kwa ajili ya wadhifa wake, wahudumu wasiopungua wawili na waumini wawili na wahudumu wasiopungua wawili na waumini wawili. Washirika wanaweza kuchaguliwa na kikao cha wilaya kutumika kwa kipindi cha miaka minne au hadi waandamizi wao watakapochaguliwa na kuhitimishwa. Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya inaweza kutumika kama Halmashauri ya Mali ya Kanisa ya Wilaya kwa kura ya kukubali ya kikao cha wilaya.

**237. Wajibu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mali ya Kanisa** ni:

**237.1.** Kuendeleza umuhimu wa kujengwa kwa majengo yanayohusiana na kanisa katika mipaka ya wilaya, wakishirikiana na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya.

**237.2** Kuhakikisha uhalisi na kutunza hati za mali ya kanisa la mtaa.

**237.3.** Kufikiria mapendekezo yaliyowasilishwa na makanisa ya mtaa kuhusu ununuzi au uuzaji wa viwanja, nyumba au ujenzi wa majengo ya kanisa au nyumba za wachungaji, na kuyashauri makanisa hayo kuhusu mapendekezo yaliyowasilishwa. (103-104)

**237.4.** Kuidhinisha au kutoidhinisha, kwa ushirikiano na msimamizi wa wilaya, maazimio yaliyowasilishwa na makanisa ya mtaa kuhusu mipango ya ujenzi wa kanisa na kuwa na madeni katika ununuzi wa viwanja, nyumba au ujenzi wa majengo. Halmashauri ya Mali ya Kanisa itatoa idhini ya kuongeza madeni chini ya mwongozo ufuatao:

1. Kanisa la mtaa linaloomba idhini ya kuongeza madeni liwe limelipa malipo yote ya pesa lililotengewa kwa kipindi cha miaka miwili iliyotangulia ombi hilo.
2. Jumla ya kiasi cha deni haitakuwa zaidi ya mara tatu ya wastani wa kiasi kilichotolewa kila mwaka katika kipindi cha miaka mitatu iliyotangulia.
3. Maelezo ya mipango ya kufanyia marekebisho au ujenzi uliopangwa yatapaswa kuwa yameidhinishwa na Halmashauri ya Mali ya Kanisa.
4. Kiasi cha deni na masharti ya kulipa deni hilo hayapaswi kuhatarisha hali ya maisha ya kiroho ya kanisa.

Halmashauri ya Mali ya Kanisa inaweza tu kuidhinisha maombi ambayo hayanatimiza masharti hayo kwa idhini ya msimamizi wa wilaya na Halmashauri ya Wilaya**.** (103-104)

**237.5.** Kufanya chochote kitakachoagizwa na kikao cha wilaya kuhusiana na mali ya kanisa katika wilaya.

## M. Kamati ya Fedha ya Kikao cha Wilaya

**238. Wajibu wa kamati ya fedha ya kikao cha wilaya** ni:

**238.1.** Kukutana kabla ya kikao cha wilaya na kutoa pendekezo kwa kikao cha wilaya kuhusu makadirio ya pesa zote za matumizi na jinsi makadirio hayo yatakavyogawanywa kwa makanisa ya mtaa. (32.5)

**238.2.** Kufanya jambo lingine lolote litakaloagizwa na kikao cha wilaya linalohusiana na pesa za wilaya. (205.21)

**238.3.** Kuchapisha katika jarida la wilaya njia zilizotumika na asilimia zilizowekwa kuamua msingi wa fedha ya sehemu zote za kifedha zilizogawa.

## N. Kamati ya Halmashauri ya Wilaya

**239.** Kamati ya Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya (KHUW) itakuwa na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya, mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa, mkurugenzi wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya, mkurugenzi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya, katibu wa wilaya, na mweka hazina wa wilaya. Kamati hii itakutana mara kwa mara inavyohitajika na itasimamiwa na msimamizi wa wilaya au msimamizi mkuu wa eneo au mteuliwa. (209)

## O. Mkurugenzi wa Wilaya wa Huduma za Majeshi au/na Magereza

**240**. Msimamizi wa wilaya anaweza kuchagua mkurugenzi wa wilaya wa huduma za nje ya kanisa. Akishirikiana na msimamizi wa wilaya, mkurugenzi wa wilaya wa huduma za nje ya kanisa atatafuta njia za kuendeleza na kustawisha uinjilisti wa utakatifu kupitia huduma maalum zinazotekelezwa nje ya kanisa. Mkurugenzi huyo ataendeleza na kutegemeza uinjilisti kupitia nafasi zinazopatikana za kuhudumu katika viwanda, mashirika, vyuo vya elimu, na katika vikosi vya jeshi. Mkurugenzi huyo pia atashughulikia kwa njia maalum wanajeshi wote wa Mnazareti na wanajeshi wengine ambao wanakaa katika makao hayo ya kijeshi, akichagua na kusaidia wachungaji walio karibu na makao hayo kuwahudumia wanajeshi wote na jamii zao ili wamjue Kristo na kushikamana na kanisa letu wanapoitumikia nchi yao. (211.9)

## P. Halmashauri ya Wilaya ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa

**241.** Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi ya Wilaya za Kimataifa itakuwa na msimamizi wa wilaya, mwenyekiti wa

Umisheni wa Mnazareti ya Kimataifa, mwenyekiti wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, na mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Huduma ya Shule ya Jumapili , ambao ndiyo watakaokuwa Kamati Kuu, na washirika wengine wasiopungua watatu. Washirika hao zaidi watachaguliwa na kikao cha wilaya au Kongamano la Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi la Wilaya kwa vipindi vinavyotofautiana vya miaka mitatu na hadi waandamizi wao watakapochaguliwa na kuhitimishwa. Baada ya kuratibiwa kwa Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi ya Wilaya, wale washirika watatu zaidi watachaguliwa kutoka katika wateule sita, mmoja wao atachaguliwa kwa kipindi cha miaka mitatu, mmoja kwa kipindi cha miaka miwili, na mmoja kwa kipindi cha mwaka mmoja kulingana na idadi ya kura kila mmoja wao atakazopata. Hata hivyo, ikiwa idadi ya washirika wa wilaya itazidi 5,000, idadi ya washirika watakaoteuliwa na kuchaguliwa inaweza kuwa maradufu, na ikiwezekana, kwa uchache watu wanne kati ya washirika 10 wa halmashauri hiyo watakuwa waumini. Nafasi zinazotokea katika Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili, kabla ya mkutano wa kikao cha wilaya, zinaweza kujazwa kwa uteuzi wa msimamizi wa wilaya. (215)

**Wajibu wa Halmashauri ya Wilaya ya Huduma za Shule ya Jumapili ni:**

**241.1.** Kukutana katika kipindi cha juma moja baada ya kuchaguliwa kwao na kujiratibu kwa kuchagua katibu, mtunza hazina, wakurugenzi wa wilaya wa Huduma za Watu Wazima, Huduma za Watoto, na Masomo ya Kuendelea ya Waumini, ambao watakuwa washirika wa Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa kwa ajili ya wadhifa wao. Wakurugenzi wengine wa wilaya, kama itakavyohitajika, wanaweza kuteuliwa na Kamati Kuu na kuchaguliwa na Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili.

**241.2.** Kutoa usimamizi kwa shughuli zote za Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa katika wilaya.

**241.3.** Kuchagua Baraza la Huduma za Watoto ambalo mwenyekiti wake atakuwa mkurugenzi wa wilaya wa huduma za watoto na ambalo washirika wake watakuwa wakurugenzi wa kambi za wavulana na wasichana, Karavani, Shule ya Biblia ya Likizo, (SBL) maswali ya Biblia, kanisa la watoto, wazazi wa watoto wachanga, na wengine watakaohitajika.

TAZAMA: Kwa maelezo zaidi kuhusu wajibu wa Baraza za Huduma za Watoto na Watu Wazima, tazama Kijitabu cha Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa

**241.4.** Kuchagua Baraza la Huduma za Watu Wazima ambalo mwenyekiti wake atakuwa mkurugenzi wa Huduma za Watu Wazima na ambalo washirika wake watakuwa wakurugenzi wa ndoa na maisha ya familia, huduma kwa wazee (waliostaafu), huduma ya watu ambao hawajaoa au kuolewa, mkutano wa faragha wa waumini, mafundisho ya Biblia ya makundi madogo, huduma za wanawake, huduma za wanaume na wengine watakaohitajika.

**241.5.** Kutayarisha mkutano au kongamano la mwaka la Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimaitafa katika wilaya. (241)

**241.6.** Kuamua, wakishauriana na msimamizi wa wilaya, ikiwa uchaguzi wa washirika na mwenyekiti wa Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa ya Wilaya utafanyika katika kikao cha wilaya au katika Kongamano la Wilaya la Huduma za Shule ya Jumapili.

**241.7.** Kuwatia moyo wenyeviti wote wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa, na huduma za makundi ya rika au wakurugenzi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, na wakurugenzi wa huduma za makundi ya rika katika makanisa ya mtaa kuhudhuria mkutano wa wilaya wa Huduma za Shule ya Jumapili na kushiriki kadiri nafasi itakavyopatikana.

**241.8.** Kuratibu wilaya katika kanda na kuwateuwa wenyeviti wa kanda hizo ambao watasaidia halmashauri hiyo chini ya maongozi yake kuendeleza kazi za Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa katika wilaya.

**241.9.** Kupanga na kutekeleza madarasa ya wilaya au kanda ya Masomo ya Kuendelea ya Waumini.

**241.10.** Kusaidia Tawi la Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa za Kanisa la Mnazareti, zikiwa ni pamoja na maelezo yanahusu habari za Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa za wilaya na za mtaa.

**241.11.** Kupendekeza kwa Kamati ya Wilaya ya Kikao Kikuu makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka ya Huduma za Wilaya za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa.

**241.12.** Kusimamia mkutano wa faragha wa waumini katika wilaya. Mkurugenzi wa wilaya wa huduma za watu wazima atakuwa mshirika wa Kamati ya Wilaya ya Mkutano wa Faragha wa Waumini, kwa ajili ya wadhifa wake.

**241.13.** Kuidhinisha ripoti ya mwenyekiti wake itakayowasilishwa kwenye Kikao cha wilaya**.**

**241.14.** Kukutana mara kwa mara kama itakavyohitajika na msimamizi wa wilaya au mwenyekiti wa Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa ya Wilaya kupanga na kutekeleza inavyohitajika shughuli za halmashauri hiyo.

**242**. **Mwenyekiti wa Wilaya wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa.** Kikao cha wilaya au Kongamano la Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa kitachagua mwenyekiti kutoka kwa Halmashauri ya Wilaya ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa atakayetumika kwa kipindi cha mwaka mmoja au miwili, kutoka kwa wateule wawili au zaidi waliowasilishwa na Kamati ya Uteuzi ya Wilaya. Mwenyekiti anayetumika anaweza kuchaguliwa kwa kura ya "ndio" au "la" ikiwa kura kama hiyo itapendekezwa na Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa ya Wilaya, kwa idhini ya msimamizi wa wilaya. Nafasi ikitokea kabla ya kikao cha wilaya inaweza kujazwa kulingana na kifungu cha 215. (241.6.)

Wajibu na mamlaka ya mwenyekiti wa wilaya wa huduma za Shule ya Jumapili **ni:**

**242.1.** Kutoa uongozi unaofaa kwa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa katika wilaya kwa:

1. Kuendeleza mipango ya ustawi katika uandikishaji na mahudhurio;
2. Kuunganisha mipango yote inayohusiana na Huduma za Watoto na Watu Wazima na;
3. Kufanya kazi akishirikiana na Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kusimamia Shule ya Jumapili kwa vijana/Mafunzo ya Biblia/makundi madogo.

**242.2.** Kuwa mshirika wa kikao cha wilaya na Halmashauri ya Wilaya Huduma za Shule za Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa kwa ajili ya wadhifa wake.

**242.3.** Kutayarisha ripoti kwa Wilaya ya Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa kwa kuchapishwa katika jarida rasmi la kikao cha wilaya.

## Q. Huduma ya Vijana wa Wilaya ya Kimataifa

**243.** Huduma ya vijana wa Mnazareti inaratibiwa chini ya uongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, chini ya Mkataba wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, na mamlaka ya msimamizi wa wilaya, Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya, na kikao cha wilaya. Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya Wilaya itashirikisha washirika na matawi ya mtaa ya Huduma ya Vijana Mnazareti ya Kimataifa ya wilaya inayohusika.

**243.1.** Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya Wilaya itajiratibu yenyewe kulingana na Mpango wa Wilaya wa Huduma kwa Vijana (810.200-810.219), ambao unaweza kutayarishwa kulingana na mahitaji ya vijana kuambatana na mkataba wa Huduma ya Vijana ya Kimataifa na *Kitabu cha Mwongozo cha Kanisa la Mnazareti.*

## R. Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa ya Wilaya

**244.** Jumuiya ya Wilaya ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa itashirikisha jumuiya za misheni za makanisa ya mtaa yaliyoko katika mipaka ya wilaya inayohusika. Jumuiya ya wilaya ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa itawakilisha Jumuiya Kuu ya Misheni ya Mnazareti Kimataifa (811).

**244.1.** Jumuiya ya Wilaya ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa itaongozwa na Katiba ya Wilaya ya Umisheni wa Mnazareti wa Kimataifa iliyoidhinishwa na Kamati ya Umisheni wa Dunia na na Halmashauri Kuu. Jumuiya hiyo itakuwa chini ya msimamizi wa wilaya, Halmashauri ya Wilaya, na Baraza la wilaya la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa. (811)

**244.2.** Kiongozi wa Wilaya wa Misheni wa Mnazareti wa Kimataifa atatumika bila mshahara na atakuwa mshirika wa kikao cha wilaya kwa ajili ya wadhifa wake. (201)

## S. Wasaidi wa Wilaya wa Kulipwa

**245.** Wakati kulipwa kwa wasaidizi kunahitajika kwa kuimarisha kazi ya usimamizi wa wilaya, watu kama hao, wakiwa wahudumu au waumini, watateuliwa na msimamizi wa wilaya, baada ya kupata idhini iliyoandikwa ya msimamizi mkuu wa eneo hilo. Watachaguliwa na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya. Kuajiriwa kwa wasaidizi kama hao hakutakuwa kwa muda wa zaidi ya mwaka mmoja, lakini muda wao unaweza kuongezwa kwa pendekezo la msimamizi wa wilaya na kwa wingi wa kura za Halmashauri ya Wilaya. (211.16)

**245.1.** Kuachishwa kazi kwa wasaidizi hao kabla ya kumalizika kwa muda wa kuajiriwa kwao ni lazima kupendekezwe na msimamizi wa wilaya na kukubaliwe kwa zaidi ya nusu ya kura za Halmashauri ya Wilaya. (225.16).

**245.2.** Wajibu na kazi za wasaidizi kama hao wa wilaya zitaamuliwa na kusimamiwa na msimamizi wa wilaya.

**245.3.** Katika muda wa kujiuzulu au kuachishwa kazi kwa msimamizi wa wilaya, muda wa kazi wa wasaidizi wa kulipwa utahesabiwa kuwa umekamilika, isipokuwa kama sheria za uajiri za nchi zinaeleza vingine. Hata hivyo, mshirika mmoja au washirika zaidi wa waajiriwa wanaweza

kubaki kwa idhini iliyoandikwa ya msimamizi mkuu wa eneo hilo na Halmashauri ya Wilaya, lakini isiyopungua tarehe ya kuchukuliwa kwa majukumu mpya ya msimamizi. (209.3-209.4)

**245.4** Utumishi kama msaidizi wa wilaya wa kulipwa hautamzuia mtu kutumika katika wadhifa mwingine wa kuchaguliwa au kuteuliwa katika wilaya kama vile katibu wa wilaya au mtunza hazina wa wilaya.

### T. Kubatilishwa kwa Kuratibiwa kwa Wilaya

**246.** Iwapo itaonekana dhahiri kwa Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu kwamba wilaya fulani haistahili kuwepo, kwa pendekezo lao, kuratibiwa kwa wilaya hiyo kunaweza kubatilishwa kwa theluthi mbili ya kura za kukubali zilizopigwa na Halmashauri Kuu ya Kanisa la Mnazareti na tangazo rasmi kuhusu jambo hilo kutolewa. (200)

**246.1**. Ikiwa kuratibiwa kwa wilaya kumebatilishwa rasmi, mali yoyote ya kanisa itakayokuwepo haitaelekezwa kwa kusudi lingine lolote, bali itabaki chini ya usimamizi wa Kanisa la Mnazareti, ikiwa imeshirikishwa, kwa matumizi ya dhehebu kwa upana, kama vile Kikao Kikuu kitakavyoagiza, na wadhamini wanaosimamia mali, au mashirika yaliyosajiliwa kusimamia mali, ya wilaya iliyobatilishwa itauza au kutolewa mali hiyo kwa amri na chini ya uongozi wa mjumbe aliyeteuliwa na Kanisa la Mnazareti, ikiwemo, na kukabidhi fedha kwa mjumbe huyo. (106.2, 106.5, 225.6)

# SURA YA TATU

# KIKAO KIKUU

### A. Kazi na Uratibishaji wa Kikao Kikuu

**300.** Kikao Kikuu ndicho chenye uwezo wa juu zaidi wa mafundisho ya imani, kutunga sheria, na mamlaka ya kuchagua katika Kanisa la Mnazareti kikifuata maagizo na mwongozo wa Katiba ya Kanisa. (25-25.8)

**300.1.** Kikao Kikuu kitasimamiwa na wasimamizi wakuu. (25.5, 307.3)

**300.2.** Kikao Kikuu kitachagua viongozi wake wengine na kujiratibu chenyewe kwa kusudi la kutekeleza shughuli. (25.6)

**300.3**. **Kanuni za Utengamano:** Kulingana na sheria inayotumika, Kanuni za Kushirikishwa na Sheria za uongozi ulioko katika *Kitabu cha Mwongozo*, mikutano na shughuli za Kanisa la Mnazareti katika mtaa, wilaya, na kanisa kuu, pamoja na kamati zake, itaongozwa na kusimamiwa kulingana na utaratibu wa bunge ulioandikwa katika toleo la sasa la kitabu cha *Kanuni za Utengamano za Robert.* (34)

## B. Ushirika wa Kikao Kikuu

**301.** Kikao Kikuu kitakuwa na idadi sawa ya wajumbe wahudumu na waumini kutoka katika kila wilaya ya Kiwango cha 3, msimamizi wa wilaya anayetumika kama mmoja wa wajumbe makasisi, wajumbe wengine makasisi waliosalia, na wajumbe wote waumini waliochaguliwa na vikao vya wilaya; wasimamizi wakuu waliotunukiwa heshima na waliostaafu; wasimamizi wakuu wanaohudumu; rais wa Umisheni wa Mnazareti wa Kimataifa Ulimwenguni; mwenyekiti wa Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa Ulimwenguni; Kanisa la Mnazareti, wakiwemo wakuu na wakurugenzi walio na wajibu wa kimataifa na kutoa ripoti kwa wajumbe wa Halmashauri Kuu; nusu ya viongozi wa majimbo wa Halmashauri ya Elimu ya Kimataifa kutoka kwa kila jimbo watakuwa washirika wa kupiga kura, na nusu nyingine itakuwa ya washirika wasiopiga kura, na idadi na hatua ya uchaguzi ikiamuliwa na Halmashauri ya Elimu ya Kimataifa; na mmishenari mmoja mjumbe wa Halmashauri Kuu aliyetumwa kutoka kwa kila jimbo ambaye amechaguliwa na wamishenari wa Halmashauri Kuu waliotumwa wataotumika katika jimbo hilo. Iwapo hakutakuwa na uchaguzi wa namna hiyo, mwakilishi wa wamishenari atachaguliwa na Kamati ya Umisheni na Uinjilisti ya Dunia.

**301.1.** Kila wilaya ya Kiwango cha 3 itakuwa na haki ya kuwakilishwa katika Kikao Kikuu na: makasisi wawili waliopewa na waumini wawili wanaohudumu kwa kanisa lililo na washirika 6,000 au washirika kamili wa kanisa wasiozidi idadi hiyo, na kasisi mmoja anayehudumu na muumini mmoja kwa washirika kamili wanaofuata 4,000, na kwa kila ongezeko la washirika kamili 5,000. "Kasisi anayehudumu" atakuwa ni pamoja na wazee na mashemasi. (Tazama ufafanuzi hapa chini.)

| Idadi ya Washirika Kamili | Idadi ya Wajumbe |
|---|---|
| 0-6,000 | 4 (waumini 2, wahudumu 2) |
| 6,001-10,000 | 6 (waumini 3, wahudumu 3) |
| 10,001-15,000 | 8 (waumini 4, wahudumu 4) |
| 15,001-20,000 | 10 (waumini 5, wahudumu 5) |
| 20,001-25,000 | 12 (waumini 6, wahudumu 6) |
| 25,001-30,000 | 14 (waumini 7, wahudumu 7) |
| 30,001-35,000 | 16 (waumini 8, wahudumu 8) |
| 35,001-40,000 | 18 (waumini 9, wahudumu 9) |

(Kwa kila idadi ya washirika 5,000 juu ya washirika 40,000, kutakuwa na muumini mjumbe mmoja na mhudumu mjumbe mmoja)

**301.2.** Kila wilaya ya Kiwango cha 2 itakuwa na haki ya kuwakilishwa na mjumbe mmoja muumini na mjumbe mmoja mhudumu katika Kikao Kikuu. Mjumbe mhudumu atakuwa ni msimamizi wa wilaya. Mjumbe mmoja wa kubadilishana atachaguliwa kwa kila mjumbe.

**301.3.** Wilaya ya Kiwango cha 1 itakuwa na haki ya kuwakilishwa na mjumbe mmoja asiyepiga kura katika Kikao Kikuu. Msimamizi wa wilaya atakuwa mjumbe huyo, mradi tu ushirika wake utakuwa katika wilaya hiyo. Ikiwa ushirika wa msimamizi wa wilaya hauko katika wilaya hiyo, mjumbe wa kubadilishana naye, ambaye ushirika wake uko katika wilaya hiyo atachaguliwa.

**301.4.** Haki ya mjumbe mhudumu aliyechaguliwa kwenda kwa Kikao Kikuu kuwakilisha kikao cha wilaya inayomchagua itaondolewa ikiwa atakubali kuchukua wadhifa mpya wa kiuhuduma katika wilaya nyingine, au ikiwa mjumbe huyo aliyechaguliwa ataacha kuhudumu katika Kanisa la Mnazareti kabla ya mkutano wa Kikao Kikuu. Mhudumu ambaye amestaafu rasmi hawezi kuteuliwa kuwa mjumbe katika mkutano wa Kikao Kikuu.

**301.5.** Haki ya mjumbe muumini ya kuwakilisha kikao cha wilaya iliyomchagua katika Kikao Kikuu itaondolewa ikiwa atahamisha ushirika wake kwa kanisa lingine la mtaa lililoko katika wilaya nyingine kabla ya mkutano wa Kikao Kikuu.

### C. Mahali na Wakati wa Mkutano wa Kikao Kikuu

**302**. Kikao Kikuu kitakutana mwezi wa sita, kila baada ya miaka minne, wakati na mahali palipoamuliwa na Tume ya Kikao Kikuu ambayo washirika wake watakuwa ni wasimamizi wakuu na idadi sawa ya watu wengine ambao wamechaguliwa na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu. Tume ya Wazimamizi Wakuu itakuwa na uwezo, kukitokea jambo la dharura, kubadilisha mahali na wakati wa mkutano wa Kikao Kikuu.

**302.1.** Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu ikishauriana na Kamati ya Watendaji wa Halmashauri Kuu inaidhinishwa, iwapo ni sawa, kuchagua sehemu kwa wakati mmoja ya Kikao Kikuu. Kupiga kutoka sehemu ya wakati mmoja kutatambuliwa kama kupiga kura kwa rasmi pamoja na kura za wajumbe wa katika sehemu ya mtaa.

**302.2.** Kikao Kikuu kitafunguliwa kwa ibada ya siku ya kujitoa kumcha Mungu na uhuishaji. Matayarisho yatafanywa ili kuwe na utengemano na uangalifu katika kutekelezwa kwa shughuli za Kikao hicho na ibada kama hizo mwisho wa ibada hiyo kama itakavyoagizwa. Kikao Kikuu kitaamua wakati wa kuahirishwa kwa mikutano yake. (25.3)

### D. Vikao Maalum vya Kikao Kikuu

**303.** Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu, au wengi wao, kwa idhini iliyoandikwa ya theluthi-mbili za wasimamizi wote wa wilaya, itakuwa na mamlaka na uwezo wa kuitisha mkutano maalum wa wajumbe wa Kikao Kikuu kukiwa na jambo la dharura, mahali na wakati wa kikao hicho utaamuliwa na wasimamizi wakuu na tume iliyochaguliwa na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu.

**303.1.** Iwapo kutakuwa na mkutano maalum wa Kikao Kikuu, wajumbe na wale waliokuwa wa kubadilishana nao waliohudhuria kikao kikuu kilichopita, au wale waliochaguliwa kihalali kuchukua nafasi zao, ndiyo watakaotumika kama wajumbe na wabadilishanaji katika mkutano maalum wa Kikao Kikuu.

### E. Kamati ya Matayarisho ya Kikao Kikuu

**304**. Katibu mkuu, mtunza hazina mkuu, na watu wengine watatu walioteuliwa na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu mwaka mmoja kabla ya mkutano wa Kikao Kikuu ndio watakaokuwa washirika wa Kamati ya Matarayisho ya Kikao Kikuu.

**304.1.** Kamati ya Matayarisho ya Kikao Kikuu itakuwa na mamlaka ya kupanga mipango yote inayohitajika, na kuingia katika mikataba inayohusiana na Kikao Kikuu.

**304.2.** Kamati ya Matayarisho ya Kikao Kikuu pamoja na wasimamizi wakuu watatayarisha ratiba ya Kikao Kikuu, ambayo itakuwa pamoja jambo la kusisitizwa kwa kila hitaji kuu; ibada ya Tume; na ibada za kidini; ambazo zitaambatana na idhini ya Kikao Kikuu.

## F. Shughuli za Kikao Kikuu

**305.** Shughuli za Kikao Kikuu, kufuatana na kifungu cha 25.8 cha Katiba ya Kanisa, zitakuwa ni:

**305.1.** Kurejesha, kupitia kwa Kamati yake ya Marejeo, maazimio, mapendekezo, na kutekeleza mambo ya kisheria kutoka kwenye tume zilizoteuliwa na ripoti za kamati maalum pamoja na hati nyingine kwa kamati za kudumu au maalum zinazoshughulikia mambo ya kisheria za kikao, au kwa mkutano wa jimbo ili zichunguzwe kabla ya kuwasilishwa kwa kikao. Kamati ya Marejeo inaweza tu kuwasilisha mambo ya kisheria yanayohusu jimbo au majimbo kwa wajumbe wa Kikao Kikuu kutoka kwenye jimbo au majimbo hayo ili wachukue hatua zinazohitajika. Mabadiliko ambayo yanahusu mambo yaliyoko katika *Kitabu cha Mwongozo* lazima yatekelezwe na wajumbe wote wa Kikao Kikuu.

**305.2.** Kuchagua, kwa theluthi-mbili za kura ya washirika wake walioko na wanapiga kura, wasimamizi wakuu sita ambao watakuwa katika ofisi hadi siku 30 zitakazofuata kuahirishwa kwa Kikao Kikuu kitakachofuata na hadi waandamizi wao watakapochaguliwa na kuhitimishwa;

a. Kwanza, kutakuwa na kura ya "Ndiyo" au "La" kwa wasimamizi wakuu wanaotumika.
b. Nafasi zilizobaki wazi baada ya hatua ya kupiga kura kukamilika kwa wasimamizi wote wakuu wanaotumika kwa sasa zitajazwa kwa kura zitakazofuatia hadi uchaguzi wao ukamilike.

Ikitokea kwamba mtu asiyestahili kuchaguliwa chini ya kifungu hiki atapata kura wakati wa uchaguzi wa kwanza, jina lake litaondolewa katika karatasi ya kura na ripoti ya kura iliyopigwa kwanza itakuwa na taarifa hii: "Jina moja au zaidi limeondolewa kwa sababu ya kutostahili kuwa katika ofisi hii."

Hakuna kasisi yeyote atakayehesabiwa kuwa anastahili katika ofisi ya msimamizi mkuu ambaye wakati mmoja hati yake ya kuhitimu ilitwaliwa kwa sababu za kinidhamu. Hakuna mtu atakayechaguliwa katika ofisi ya msimamizi mkuu ikiwa hajafikia umri wa miaka 35 au ametimiza umri wa miaka 68. (25.4, 307.16, 900)

**305.3.** Kuchagua msimamizi mkuu kutunukiwa heshima ya kuhifadhi jina la msimamizi mkuu baada ya kustaafu ikiwa inafaa, mradi tu awe aliacha kazi kwa sababu za kiafya au amepewa hali ya kustaafu.

Inaeleweka kwamba kuchaguliwa kwake kwa heshima hiyo kutadumu wakati wote wa uhai wake. (314.1)

**305.4.** Kwa kuwekwa katika uhusiano wa kustaafu, msimamizi mkuu ambaye ameomba uhusiano kama huo, au ambaye, kwa uamuzi wa Kikao Kikuu, hawezi kuendelea na kazi kwa sababu ya ulemavu wa mwili, au kuondolewa stahili ambalo litamzuia mtu huyo kushughulikia kikamilifu wajibu wa msimamizi mkuu; na mradi tu msimamizi awe ametumika katika ofisi ya msimamizi mkuu kwa kipindi cha mwaka mmoja. Msimamizi mkuu akiomba uhusiano wa kustaafu kabla ya wakati wa Kikao Kikuu, maombi hayo yanaweza kukubaliwa na Halmashauri Kuu wakati wa mkutano wa kawaida baada ya kupendekezwa na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu. (314.1)

**305.5.** Kuweka kiwango kinachofaa cha malipo ya kustaafu kwa kila msimamizi mkuu aliyestaafu.

**305.6**. Kuchagua Halmashauri Kuu, kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 332.1-333.4, itakayotumika hadi wakati wa kuahirishwa kwa mkutano utakaofuata wa Kikao Kikuu, na hadi waandamizi wao watakapochaguliwa na kuhitimishwa. (331, 901)

**305.7**. Kuchagua Mahakama Kuu ya Rufani, ambayo itakuwa na makasisi watano, watakaotumika hadi wakati wa kuahirishwa kwa Kikao Kikuu kitakachofuata na hadi waandamizi wao watakapochaguliwa na kuhitimishwa. Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu itateua mwenyekiti na katibu wa mahakama hiyo. (25.7, 611, 902)

**305.8.** Kufanya jambo lingine lolote, kufuatana na Maandiko Matakatifu, ambapo hekima itatoa mwongozo wa shughuli kuu za Kanisa la Mnazareti na hali takatifu ya Kristo, kuambatana na Katiba ya Kanisa. (25.8)

## G. Wasimamizi Wakuu

**306.** Kazi ya wasimamizi wakuu ni kutoa uongozi wa kimitume na maono ya kiroho kwa:

- kupeana maelezo ya misheni kwa ufasaha
- kuleta maono
- kuweka wahudumu wakfu
- kueneza mwambatano wa thiolojia, na
- kutoa mamlaka na usimamizi mkuu wa utawala kanisa lote kwa jumla.

**307. Kazi na mamlaka ya wasimamizi wakuu ni kama ifuatavyo:**

**307.1**. Kuwa na usimamizi wa jumla wa Kanisa la Mnazareti, kulingana na sheria na maagizo yaliyokubaliwa na Kikao Kikuu.

**307.2.** Kutumika kama washirika wa Kikao Kikuu kwa ajili ya wadhifa wao. (301)

**307.3.** Kusimamia Kikao Kikuu na mikutano ya Halmashauri Kuu ya Kanisa la Mnazareti. (300.1, 335.3)

**307.4**. Kuwa na mamlaka ya kipekee ya kuweka wakfu, au kuteua wengine kuwekwa wakfu, wale ambao wameteuliwa kwa utaratibu kuwa makasisi au mashemasi. (320, 538.5-538.6)

**307.5**. Kusimamia kila kikao cha wilaya kama vile ilivyopangwa na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu. Msimamizi mkuu anaweza kuteua kasisi wa kutumika kama mwenyekiti. (202, 214)

**307.6.** Msimamizi mkuu anayesimamia mkutano wa kikao cha wilaya, msimamizi wa wilaya, na Halmashauri ya Wilaya, wakikubaliana na wajumbe wa makanisa ya mtaa, watateua wachungaji kwa ajili ya makanisa ya mtaa ambayo hayajaita wachungaji. (218.1)

**307.7.** Wasimamizi wakuu wanaweza kuteua wasimamizi wa wilaya katika wilaya ambazo ofisi ya msimamizi wa wilaya inakuwa wazi kabla ya mkutano ufuatao wa kikao cha wilaya, baada ya kushauriana na Kamati ya Halmashauri ya Wilaya. Kufuatana na kifungu cha 208, makasisi wote waliohitimu wanaweza kuchaguliwa, wakiwa ni pamoja na wale wa kikao. (209, 239)

**307.8.** Iwapo msimamizi wa wilaya anayetumika atapatwa na shida itakayomfanya asiweze kutumika kwa muda, msimamizi mkuu anayesimamia eneo hilo, akishauriana na Halmashauri ya Wilaya, anaweza kuteua kasisi aliyehitimu kutumika kama msimamizi wa wilaya wa muda. Hali hiyo ya kutowezeshwa kwake itaamuliwa na msimamizi mkuu wa eneo hilo na Halmashauri ya Wilaya. (209.2)

**307.9**. Msimamizi mkuu wa eneo anaweza kupendekeza kwa Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu kwamba Kiwango cha 3 wilaya kitangazwe kuwa katika shida. (200.2, 322)

**307.10.** Msimamizi mkuu wa eneo anaweza kusimamia mkutano wa mwaka, au mkutano maalum wa kanisa la mtaa, au amteue mwakilishi wa kusimamia. (113.5)

**307.11** Hakuna msimamizi mkuu atakayekuwa mshirika wa kupiga kura wa halmashauri yoyote ya Kanisa la Mnazareti, mbali na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu, ila awe ameidhinishwa na sheria ambazo ziko za halmashauri hiyo. (307.12)

**307.12.** Msimamizi mkuu hatakuwa na ofisi ingine katika kanisa atakapokuwa akitumika kama msimamizi mkuu. (307.11)

**307.13.** Vitendo vyote rasmi vya msimamizi mkuu kulingana na kupitiwa tena na kurudiwa tena vitaangaliwa na Kikao Kikuu.

**307.14**. Kitendo chochote cha msimamizi mkuu kinaweza kubatilishwa kwa kura ya kukubali bila kupingwa ya washirika waliobakia wa Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu.

**307.15.** Ofisi ya msimamizi mkuu yeyote inaweza kutangazwa kuwa wazi, kwa sababu fulani, kwa kura ya kukubali bila kupingwa ya washirika wengine wa Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu, ikikubaliwa na theluthi-mbili za kura ya Halmashauri Kuu.

**307.16.** Msimamizi mkuu, aliyechaguliwa na Kikao Kikuu, atatumika hadi siku 30 baada ya kuahirishwa kwa Kikao Kikuu kitakachofuata na hadi waandamizi wao watakapochaguliwa na kuhitimishwa. (305.2)

## H. Wasimamizi Wakuu Waliotunukiwa Heshima na Waliostaafu

**314.** Wasimamizi wakuu wote waliotunukiwa heshima ya kuhifadhi jina la msimamizi mkuu na wale waliostaafu watakuwa washirika wa Kikao Kikuu kwa ajili ya wadhifa wao. (301)

**314.1.** Msimamizi mkuu ambaye amestaafu, au amepigiwa kura ya kutunukiwa heshima ya kuhifadhi jina la msimamizi mkuu, hatakuwa mshirika wa Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu. Hata hivyo, ikiwa msimamizi mkuu anayetumika atazuiwa kufanya kazi kwa ajili ya ugonjwa, kulazwa hospitali, au jambo jingine la dharura, Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu ina mamlaka ya kumwita msimamizi mkuu yeyote aliyestaafu kufanya kazi kwa muda. (305.3-305.5, 900.1)

## I. Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu.

**315.** Wasimamizi wakuu wataratibu kama halmashauri na kupanga na kugawa kwa washirika kazi ambayo watakuwa na mamlaka ya usimamizi juu yake.

**316. Nafasi Wazi.** Ikiwa kutatokea nafasi katika Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu, kabla ya sehemu za mkutano wa Kikao Kikuu, swala la kuitisha uchaguzi ili kujaza nafasi hiyo litaamuliwa na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu. Uamuzi wa halmashauri hiyo utakapopokewa, katibu mkuu atajulisha mara moja washirika wote wa Halmashauri Kuu. Uchaguzi utakapoitishwa, washirika wa Halmashauri Kuu watachagua, kwa theluthi-mbili ya kura, kasisi wa Kanisa la Mnazareti kujaza nafasi hiyo na kutekeleza kazi ya msimamizi mkuu hadi siku 30 kuambatana na kuahirishwa kwa Kikao Kikuu kitakachofuata, na hadi mwandamizi atakapochaguliwa na kuhitimishwa. (25.4, 305.2)

**316.1.** Katibu mkuu atatuma ripoti ya matokeo ya kura kwa Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu, ambayo itatangaza matokeo ya kura.

**317. Kazi ya Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu** itakuwa ni:

**317.1.** Kuwezesha kuwepo kwa usimamizi, uongozi, na kutia moyo kwa kanisa lote, pamoja na kuangazia kunakofaa kwa uongozi na thiolojia ya wilaya zote, vituo, na wilaya za Kanisa la Mnazareti kote ulimwenguni.

**317.2.** Kupendekeza, ikishauriana na mkurugenzi wa Tawi la Umisheni wa Dunia, na wakurugenzi wa uongozi wa kitaifa na/au wakurugenzi wa jimbo, mabadiliko katika kazi au wajibu wa maeneo hayo ikiidhinishwa na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu na Halmashauri Kuu.

**317.3.** Kuwa na mamlaka ya kwanza kulingana na sera na mipango ya kanisa la Kikristo, na ushauri wa Halmashauri Kuu, kamati zake, na halmashauri zote za Kanisa la Mnazareti juu ya mambo mengine. Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu itafanya mapendekezo ambayo yataonekana ya busara kwa Halmashauri Kuu na kwa kamati. Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu itaruhusu au kupinga uchaguzi wote uliofanywa na Kamati ya Misheni ya Dunia kwa Halmashauri Kuu kwa kuteuliwa kama wamishenari.

**317.4.** Kufanya kazi pamoja na Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu, kuleta jina moja au zaidi kwa Halmashauri Kuu kwa uchaguzi wa katibu mkuu na mtunza hazina mkuu.

**317.5.** Kutangaza kuwa wazi kwa theluthi-mbili za kura ofisi ya katibu mkuu, mtunza hazina mkuu, mkurugenzi wa idara.

**317.6.** Kujaza nafasi ambazo zinaweza kuwa wazi katika ushirika wa Mahakama Kuu ya Rufani kabla ya mkutano wa Kikao Kikuu, na kuchagua mwenyekiti na katibu wa mahakama hiyo. (305.7, 612, 902)

**317.7.** Kujaza nafasi ambazo zinaweza kuwa wazi katika tume au kamati yoyote kabla ya mkutano wa Kikao Kikuu au Halmashauri Kuu.

**317.8.** Kuteua wasimamizi wakuu watakaotumika kama washauri wa vyuo vyote vya elimu ya juu vilivyo na uhusiano na Halmashauri ya Elimu ya Kimataifa. (905)

**317.9.** Kupanga, wakiwa pamoja na Idara ya Huduma za Mhudumu, mafundisho ya kuongozwa kwa wahudumu wale wanaotumika katika huduma, waumini na wahudumu waliopewa vyeti. (529-530)

**317.10.** Kupanga, kuhifadhi na kuendeleza Hazina ya Uinjilisti wa Ulimwengu ni kazi ya utume wa kanisa ulimwenguni. Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu na Halmashauri Kuu wamepewa mamlaka na uwezo wa kuanzisha malengo ya hazina na majukumu ya Hazina ya Uinjilisti kwa matumizi ya makanisa ya mtaa. (32.5, 130, 335.7)

**317.11**. Kuidhinisha kwa maandishi kurudishwa kwa hati za kuhitimu za kasisi au shemasi kama inavyohitajika. (539.11, 540.8, 540.12)

**318.** Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu ndio itakayokuwa mamlaka ya kufafanua sheria na mafundisho ya Kanisa la Mnazareti, na maana pamoja na uzito wa maagizo yote ya *Kitabu cha Mwongozo*, kwa makubaliano na rufani ya Kikao Kikuu.

**319.** Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu itachunguza na kupitisha mipango ya makao ya wilaya. Mipango hiyo haitatekelezwa hadi itakapoidhinishwa kwa maandishi na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu. (225.12)

**320.** Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu itakuwa na uhuru wa kuamua katika kuweka wakfu watu waliotalikiana. (307.4, 533.3, 534.3)

**321.** Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu inaweza kutangaza nafasi wazi kwa sababu fulani ofisi ya msimamizi wa wilaya yoyote ya Kiwango cha 2 au wilaya ya Kiwango cha 1 ikipendekezwa na msimamizi mkuu wa eneo la wilaya hiyo na inaweza kutangaza kuwa wazi ofisi ya msimamizi wa wilaya ya Kiwango cha 3 kwa theluthi-mbili ya kura za Kamati ya Halmashauri ya Wilaya. (2019.1, 239)

**322.** Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu inaweza kuidhinisha kwamba Kiwango cha 3 cha wilaya kitangazwe kuwa katika mzozo. (200.2, 307.9)

**323.** Baada ya kila Kikao kikuu, *Kitabu cha Mwongozo* cha Kanisa la Mnazareti kilichosahihishwa kinafaa kutafsiriwa katika lugha zote zinazohitajika wakati Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu itatangaza tarehe rasmi ya kukitafsiri katika lugha hizo.

**324.** Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu itakuwa na mamlaka ya kufanya jambo lingine lolote katika utumishi kwa Kanisa la Mnazareti, ambalo halikutajwa, kulingana na hekima yake, lisilodhuru utaratibu wa kanisa, chini ya maagizo ya Katiba ya Kanisa.

### J. Katibu Mkuu.

**325.** Katibu mkuu, aliyechaguliwa na Halmashauri Kuu kama ilivyopitishwa katika Kanuni za Sheria za Halmashauri Kuu, atatumika hadi kuahirishwa kwa Kikao Kikuu kitakachofuata, na hadi mwandamizi wake atakapochaguliwa na kuhitimishwa, au hadi atakapoondolewa kulingana na kifungu cha 317.5. (900.2)

**325.1.** Katibu Mkuu atakuwa mshirika wa Kikao Kikuu kwa ajili ya wadhifa wake. (301)

**325.2.** Ikiwa wakati wa kipindi cha muda katika Halmashauri Kuu kutakuwa na nafasi katika ofisi ya katibu mkuu, nafasi hiyo itajazwa na

Halmashauri Kuu, kufuatia uteuzi utakaofanywa kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 317.4. (335.21)

**325.3.** Katibu Mkuu atakuwa chini ya Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu na Halmashauri Kuu.

**326. Kazi ya katibu mkuu** ni:

**326.1.** Kutumika kama katibu wa Kanisa la Mnazareti kwa ajili ya wadhifa wake, pamoja na Halmashauri Kuu, na Kikao Kikuu na ataweka rikodi na kuhifadhi jarida la mikutano yao. (331.2)

**326.2.** Kuandika kwa usahihi na kuhifadhi tarakimu za Kanisa la Mnazareti.

**326.3**. Kuhifadhi hati zote za Kikao Kikuu, na kuzikabidhi mara moja kwa atakayechukua nafasi yake.

**326.4.** Kuhifadhi rekodi zote na uamzi wote uliofikiwa na Mahakama Kuu ya Rufani. (614)

**326.5.** Kuhifadhi na kuweka katika mpangilio maalum hati zote za kuhitimu zilizowasilishwa, kusalimishwa au kutolewa au za kujiuzulu za wahudumu na kuzirudisha ikiwa tu agizo halisi linalofaa limetolewa na kikao cha wilaya ambayo ilizituma. (539-539.3, 539.8)

**326.6**. Kukagua ramani za tarakimu ya wilaya. (220.3)

**326.7.** Kutunza kumbukumbu za watu ambao wamepewa hati za kuhudumu za wilaya.

**326.8.** Kuweka tayari taarifa za vipindi vya Kikao Kikuu kwa wajumbe.

**326.9.** Kuweka tayari tafsiri ya sasa ya *Kitabu cha Mwongozo*.

**326.10.** Fanya kwa uaminifu chochote kinachohitajika kwa kutimiza majukumu ya ofisi.

**327.** Katibu mkuu atakuwa mtunzaji wa udhamini wa hati zote za kisheria za kanisa kuu.

**327.1**. Katibu mkuu ana mamlaka ya kukusanya mambo ya historia yote inayohusiana na kuinuka na maendeleo ya dhehebu, na atakuwa mlinzi wa rekodi na mambo hayo.

**327.2.** Katibu mkuu amepewa mamlaka ya kukusanya maandiko yote ya kihistoria yanayohusu kuanza na kustawi kwa dhehebu/ kanisa, na ndiye atakayekuwa mtunzaji wa maandiko hayo.

**328**. Katibu mkuu, pamoja na wasimamizi wakuu, kabla ya kufunguliwa kwa mkutano wa Kikao Kikuu, atatayarisha fomu zote zitakazohitajika, hii ikiwa ni pamoja na Kanuni za Utengamano *"Kitabu cha Mwongozo"* kwa ufupi ili ifanyiwe marekebisho, na vitu vingine vitakavyohitajika kwa kazi ya Kikao Kikuu. Gharama ya matayarisho hayo italipwa kutoka katika hazina ya gharama za Kikao Kikuu.

**328.1**. Katibu mkuu anaweza kuwa na wasaidizi katika kazi yake kadiri watakavyochaguliwa na Kikao Kikuu, na ikiwa ni katikati ya mikutano ya Kikao Kikuu, halmashauri ya wasimamizi wakuu inaweza kuteua.

## K. Mweka Hazina Mkuu.

**329**. Mweka hazina mkuu, aliyechaguliwa na Halmashauri Kuu kama ilivyopitishwa na Kanuni za Halmashauri Kuu, atatumika hadi kuahirishwa kwa Kikao Kikuu kifuatacho, na hadi mwandamizi wake atakapochaguliwa na kuhitimishwa au hadi atakapoondolewa kulingana na kifungu cha 317.5 (900.3)

**329.1.** Mweka hazina atakuwa mshirika wa Kikao Kikuu kwa ajili ya wadhifa wake. (301)

**329.2.** Mweka hazina mkuu atakuwa chini ya msimamizi mkuu anayesimamia ofisi ya Fedha katika Makao Makuu, Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu, na Halmashauri Kuu.

**330. Kazi za mweka hazina mkuu ni:**

**330.1.** Kuwa mtunzaji wa fedha zote za mahitaji makuu ya Kanisa la Mnazareti.

**330.2.** Kupokea, na kulipa fedha za Kamati ya Usimamizi na Fedha Ulimwenguni, Kamati ya Elimu na Maendeleo ya Wahudumu Ulimwenguni, Kamati ya Misheni wa Dunia, na fedha zingine za Halmashauri Kuu, au kwa idara zake zozote; hazina ya wasimamizi wakuu; hazina ya matumizi ya dharura; hazina ya matumizi ya Kikao Kikuu; hazina za hisani za kanisa; hazina za Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa Ulimwenguni; na hazina ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa Ulimwenguni. (331.3.)

**330.3.** Kuweka dhamana ya kuhakikisha kufanya kazi kwa uaminifu, katika kampuni inayoweza kutegemewa ya dhamana, kiasi kizuri na cha kutosha cha pesa, kama itakavyoagizwa na Halmashauri Kuu.

**330.4.** Kutoa ripoti ya fedha kwa halmashauri na matawi ambayo anatunza pesa zao, kama itakavyohitajika nao.

**330.5.** Kutoa ripoti ya mwaka kwa Halmashauri Kuu ya pesa zote za Kanisa la Mnazareti, hii ikiwa ni pamoja na kuweka akiba itakayoleta faida. (335.12)

**330.6.** Kulinda pesa zinazolipwa kwa mwaka zilizowekwa akiba katika raslimali (nyumba au shamba) kwa hati za bima na kuhakikisha kwamba malipo ya hati hizo yanalipwa kabla ya wakati wake kupita.

## L. Halmashauri Kuu

**331**. Kanisa la Mnazareti ni shirika lisiloleta faida la kidini na kufadhili ambalo limeandikishwa chini ya sheria za jimbo la Missouri, Kansas City, Marekani. Halmashauri Kuu itakuwa na washirika ambao watachaguliwa kwa kura za siri na Kikao Kikuu kutoka kati ya watu walioteuliwa kulingana na kifungu cha 332.1-333.5. Ili kuchaguliwa kuwa mshirika wa Halmashauri Kuu kama mwakilishi wa jimbo la kanisa, mtu ni lazima awe mkazi wa jimbo hilo na pia awe mshirika wa kanisa la mtaa ambalo liko katika jimbo hilo. (305.6, 334)

**331.1.** Hakuna atakayestahili kuchaguliwa katika Halmashauri Kuu au kuendelea kuwa mshirika wa halmashauri hiyo ikiwa ameajiriwa na Halmashauri Kuu, au ameajiriwa na tawi au shirika lolote la elimu ambalo linapokea msaada wa kifedha kutoka kwa Kanisa la Mnazareti ikiwa ni pamoja na watu kutoka katika wilaya au mashirika mengine yanayopokea msaada wa kifedha wa kuendesha shughuli zao kutoka kanisa kuu pia hawatastahili kuchaguliwa.

**331.2**. Katibu mkuu atakuwa katibu wa Halmashauri Kuu kwa ajili ya wadhifa wake wa Kanisa la Mnazareti, ikiwa ni pamoja na Halmashauri Kuu.

**331.3**. Mtunza hazina mkuu atakuwa mtunza hazina wa Kanisa la Mnazareti kwa ajili ya wadhifa wake, ikiwa ni pamoja na Halmashauri Kuu na pia idara za Kanisa la Mnazareti lote. (330.2)

**332. Uteuzi wa washirika wa Halmashauri Kuu** utafanywa kama ilivyoandikwa hapa chini:

**332.1.** Baada ya wajumbe wa Kikao Kikuu kuchaguliwa, wajumbe wa kila wilaya ya Kiwango cha 3 watakutana kuchagua wale watakaoteuliwa kwa uchaguzi wa ushirika wa Halmashauri Kuu kwa njia ifuatayo. Kila wilaya ya Kiwango cha 3 inaweza kuwasilisha majina ya makasisi wawili wanaohudumu na waumini wawili. Mkusanyiko wa jamii yenye tamaduni nyingi ya wilaya inayoteua inafaa kuzingatiwa katika kuchagua majina ya wale watakaoteuliwa. Kwa majimbo kama hayo yaliyo na Baraza la Halmashauri ya Jimbo, ambayo yanaweza kupunguza idadi ya majina kwa majina matatu ya kila mshirika ambaye mkutano unahitaji kupigia kura, baadaye majina yatatumwa mara moja kwa ofisi ya katibu mkuu ili kuwekwa kwenye kura za siri kwa ajili ya kuwasilishwa kwa wajumbe wa Kikao Kikuu kutoka kwa kila jimbo. (205.23)

**332.2.** Kutoka katika orodha ya watu waliopendekezwa, wajumbe wa Kikao Kikuu kutoka katika kila jimbo watateua washirika kwa Kikao Kikuu kama ifuatavyo:

Kila jimbo lenye washirika kamili 100,000 au washirika kamili wachache litateua kasisi mmoja anayehudumu na muumini mmoja; kila jimbo lenye washirika kamili wanaozidi 100,000 hadi kufikia 200,000 litateua makasisi wawili wanaohudumu, msimamizi mmoja wa wilaya, mchungaji au muinjilisti mmoja, na waumini wawili; na muumini mmoja zaidi na kasisi mmoja zaidi kwa majimbo ya washirika kamili waliozidi 200,000 kulingana na maelezo yafuatayo:

Katika majimbo ambayo idadi ya ushirika wake imezidi washirika kamili 200,000, kasisi mmoja atakuwa mchungaji au muinjilisti; mwingine atakuwa msimamizi wa wilaya; na huyo mhudumu mwingine anaweza kuwa yeyote kati ya hao waliotajwa.

Hakuna wilaya itakayokuwa na zaidi ya washirika wawili katika Halmashauri Kuu, na hakuna jimbo litakalokuwa na zaidi ya washirika sita (isipokuwa wawakilishi wa mashirika na washirika wa Umisheni wa Mnazareti wa Kimataifa na Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa. Iwapo zaidi ya watu wawili walioteuliwa kutoka katika wilaya kwenye jimbo, wale ambao kwenye wilaya ingine watapata kura zaidi ya wale walioteuliwa kutoka katika jimbo. Katika kila jimbo, muumini au waumini, mchungaji au muinjilisti, na/au msimamizi wa wilaya ambao watapata idadi kubwa zaidi ya kura katika kundi lao watateuliwa kwenye Kikao Kikuu kwa zaidi ya kura za wingi zilizopigwa. Katika majimbo makubwa ambapo washirika sita watahitajika kuchaguliwa, muumini na kasisi atakayepata idadi kubwa ya kura inayofuata ile ya kwanza ndiye atakayekuwa mteule wa ziada. Baraza la Halmashauri ya Jimbo ikiamua kwamba yawezekana wengi wa wajumbe walioteuliwa watazuiliwa kuhudhuria Kikao Kikuu, mkutano wa jimbo unaopiga kura unaweza kufanyika kupitia njia ya mtandao miezi sita kabla ya mwanzo wa Kikao Kikuu. Hatua yenyewe ambayo uteuzi huu wa mtandao wa washirika wa Halmashauri Kuu kwa Kikao Kikuu utaendelea utapendekezwa na Baraza la Halmashauri ya Jimbo na kutumwa kwa ofisi ya Katibu Mkuu kwa kuidhinishwa kabla kutekelezwa. (305.6, 901)

**332.3.** Halmashauri ya Elimu ya Kimataifa (HEK) itateua kwenda kwenye Kikao Kikuu watu wanne kutoka vyuo vya elimu, makasisi wawili waliopewa kazi na waumini wawili. Kikao Kikuu kitachagua wawakilishi wawili, kasisi mmoja anayetumika na muumini mmoja kwa Halmashauri Kuu. (331.1.)

**332.4.** Baraza Kuu la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa litateua kwenye Kikao Kikuu mwenyekiti wa Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti la Kimaitafa wa Dunia. Iwapo mwenyekiti mpya wa Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa

alieychaguliwa hataweza kuhudumu kwa Kikao Kikuu, Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti la Kimataifa litateua mshirika mmoja kutoka kwa Baraza hilo. (343.4)

**332.5.** Baraza Kuu la Misheni ya Mnazareti wa Kimataifa Ulimwenguni litamteua kwenye Kikao Kikuu mshirika mmoja wa Baraza la Misheni ya Mnazareti wa Kimataifa Ulimwenguni. Kikao Kikuu kitachagua mwakilishi mmoja wa Halmashauri Kuu. (344.3)

**332.6.** Msimamizi wa jimbo wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa na mkurugenzi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa Ulimwenguni watateua mtu mmoja kwenye Kikao Kikuu. Kikao Kikuu kitachagua mwakilishi mmoja wa Halmashauri Kuu.

**333. Uchaguzi wa Halmashauri Kuu utakuwa kama ifuatavyo:**

**333.1.** Kila mteule aliyewasilishwa na majimbo mbalimbali atachaguliwa na Kikao Kikuu kwa wingi wa kura za “Ndiyo” zitakazopigwa kwa siri.

**333.2.** Kutoka katika wateule waliowasilishwa na Halmashauri ya Elimu ya Kimataifa, Kikao Kikuu kitachagua wawili, ambao mmoja wao atakuwa kasisi na mwingine atakuwa muumini.

**333.3.** Kutoka katika wateule waliowasilishwa na Baraza Kuu la Huduma ya Vijana wa Mnazareti la Kimataifa la Dunia, Kikao Kikuu kitachagua kwa wingi wa kura za siri za “ndiyo”. (343.4, 903)

**333.4.** Kutoka katika wateule waliowasilishwa na Baraza Kuu la Misheni ya Mnazareti Ulimwenguni, Kikao Kikuu kitachagua kwa wingi wa kura za siri za “ndiyo”. (344.3, 904)

**333.5.** Kutoka katika wateule waliowakilishwa na msimamizi wa jimbo wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa na mkurugenzi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa Ulimwenguni, Kikao Kikuu kitachagua kwa wingi wa kura za siri za “ndiyo”. (332.6)

**334.** Washirika wa Halmashauri Kuu watakuwa katika ofisi hadi kuahirishwa kwa Kikao Kikuu kitakachofuata na hadi waandamizi wao watakapochaguliwa na kuhitimishwa. Ikiwa mshirika wa Halmashauri Kuu atahamisha ushirika wake wa kanisa au makao yake kutoka katika jimbo analowakilisha, au ikiwa mhudumu atabadilisha aina ya huduma ambayo alichaguliwa kufanya, au ikiwa mhudumu hatakuwa amepewa kazi, au ikiwa muumini ataomba na kupokea hati ya wilaya ya kuhudumu, ushirika wake utakomeshwa mara moja. Nafasi iliyoachwa itajazwa bila kukawia. (331)

**334.1**. **Nafasi zinazobaki wazi katika ushirika wa Halmashauri Kuu**, na pia katika kamati ambazo ziko, zitajazwa kwa uteuzi uliofanywa na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu, ambao watawasilisha kwa katibu mkuu, majina ya watu wawili wanaostahili ambao kutoka kwao kwa ajili ya uwakilishi wa jimbo, Halmashauri za Wilaya katika jimbo ambalo nafasi imetokea, zitachagua mmoja wao kwa wingi wa kura zitakazopigwa, kila Halmashauri ya Wilaya ya Kiwango cha 2 na Kiwango cha 3 ikiwa na mamlaka ya kura moja. Kwa wawakilishi wa elimu, wateule watawasilishwa kwa Halmashauri Kuu ili wachague mmoja kwa wingi wa kura. Kwa uwakilishi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, wateule wao watawasilishwa kwa Baraza Kuu ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ili lichague mmoja kwa wingi wa kura. Kwa uwakilishi wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa, wateule watawasilishwa kutoka katika Kamati Kuu ya Baraza Kuu la Misheni ya Mnazareti la Kimataifa wakishauriana na msimamizi mkuu anayehusika, na kwa idhini ya Halmashauri ya Wasimamizi Kuu kwa Baraza Kuu la Misheni ya Mnazareti la Kimataifa ili lichague mmoja kwa wingi wa kura. Kwa uwakilishi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa, wateule watawasilishwa kwenye Halmashauri Kuu ili wachague mmoja kwa wingi wa kura. (332.3-332.6)

**335. Kazi ya Halmashauri Kuu.** Halmashauri Kuu itatumika kama halmashauri ya wakurugenzi wa Kanisa la Mnazareti lote na litakuwa na mamlaka kulingana na sera na mipango ya makanisa yasiokuwa na washirika. Halmashauri Kuu itatia moyo na kutarajia halmahsauri zote za kitaifa, jimbo, wilaya, na za kanisa la mtaa kutekeleza utume wa Kanisa la Mnazareti, ambao ni kueneza utakatifu wa Kikristo kulingana na mwongozo uliotokana na Wesley wa kuwafanya wanafunzi kama Kristo katika mataifa, na kuwezesha kuendelezwa kwa kanisa la kimataifa katika kila taifa na/au jimbo. Halmashauri Kuu itaendeleza na kustawisha hali ya kifedha na vifaa vya kamati zote za Kanisa la Mnazareti, kulingana na maagizo yatakayotolewa na Kikao Kikuu. Itaunganisha na kusawazisha, na kuweka pamoja mipango na shughuli za kamati zilizoko ili utaratibu unaofungamana wa uongozi uanzishwe katika shughuli zote za Kanisa la Mnazareti. Itakuwa na mamlaka ya kuagiza kukaguliwa kwa vitabu vya pesa za idara zote na mashirika yanayohusiana na Kanisa la Mnazareti, na itaongoza kazi na shughuli za utawala wa Kanisa la Mnazareti, pamoja na idara na mashirika yote yanayohusiana rasmi na Kanisa la Mnazareti. Idara hizi na mashirika, zitazingatia ushauri na mapendekezo yanayotelwa na Halmashauri Kuu.

**335.1.** Halmashauri Kuu itakuwa na mamlaka ya kununua, kumiliki, kushikilia, kusimamia, kuweka rehani, kuuza, kuwasilisha na kutoa msaada, au kupata, kuzuia na kugawa mali ya watu binafsi, iliyouziwa, iliyochuma, iliyorithiwa, iliyopewa kama msaada, au iliyowasilishwa kwa Kanisa la Mnazareti, kwa kusudi lolote linalolingana na sheria, na kutekeleza udhamini huo; kukopa na kukopesha pesa kwa kusudi la Kanisa la Mnazareti.

**335.2.** Halmashauri Kuu itajaza nafasi itakayotokea katika Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu kulingana na vifungu vya 316 na 305.2.

**335.3.** Halmashauri Kuu itakutana kabla au mara tu baada ya kuahirishwa kwa Kikao Kikuu na itajiandaa kwa kuchagua viongozi wake, kamati zake, na washirika kwa kamati zake kama inavyohitajika na Nakala za Usajiri na sheria, kutumika kwa kipindi cha miaka minne na hadi waandamizi wao watakapochaguliwa na kuhitimishwa. Wasimamizi Wakuu watakaosimamia mikutano ya Halmashauri Kuu.

**335.4. Mikutano.** Halmashauri Kuu itakutana kwa Kikao angalau mara tatu katikati ya Vikao Vikuu, wakati na mahali palipopendekezwa na sheria ya halmashauri hiyo au kwa saa, tarahe, na sehemu iliyokubaliwa kwa azimio la pamoja katika mkutano wa kawaida au mkutano maalum kwa manufaa ya Halmashauri Kuu na kamati zake.

**335.5. Mikutano maalum** ya Halmashauri Kuu inaweza kuitishwa na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu, kiongozi, au katibu.

**335.6. Idara ya Fedha ya Uinjilisti wa Ulimwengu.** Kila Kanisa la Mnazareti la mtaa ni sehemu ya jitihada ya ulimwengu ya “kuwafanya watu katika mataifa kuwa wanafunzi wa Kristo.” Idara ya Fedha ya Uinjilisti wa Ulimwengu itatumika na kanisa kwa msaada, kazi ya kukarabati, na kuendeleza misheni kuu na shughuli zinazohusiana na misheni. Bajeti ya mwaka ya kanisa kuu itakuwa kulingana na utoaji, pamoja na misaada kutoka kwenye idara na sehemu za msaada za kanisa kuu, na kuangazia maelezo ya fedha ya mweka hazina mkuu. Mara kwa mara, Halmashauri Kuu, itasimamia kiasi cha pesa zitakazogawa kutoka kwenye Idara ya Fedha ya Uinjilisti wa Ulimwengu kwa kila idara na fedha. Mgawanyo huo ukiwa umekubalika, utatolewa kwa Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu kwa kuzingatiwa, maoni, au marekebisho kabla ya idhini ya mwisho kutoka kwa Halmashauri Kuu.

**335.7.** Halmashauri Kuu na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu wana mamlaka na uwezo wa kuanzisha malengo ya kifedha na majukumu ya Idara ya Fedha za Uinjilisti wa Ulimwengu kwa makanisa ya mtaa. (130, 317.10)

**335.8.** Halmashauri Kuu itakuwa na mamlaka ya kuongeza au kupunguza kiasi kilichoombwa na idara yoyote au hazina. Bidhaa za fedha zilizokubaliwa na Kikao Kikuu zitatumwa kwa Halmashauri Kuu, ambayo atawainisha kusawazisha pamoja na hali ya uchumi ilivyo mgawanyo wa mwaka wa chuo chochote au tawi la kanisa, katika kuhifadhi kujitoa kwa fedha zote za kanisa kuu.

**335.9.** Halmashauri Kuu itaidhinisha kiasi kilichotengwa kutoka katika Hazina ya Uinjilisti wa Ulimwengu kwa Seminari ya Thiolojia ya Mnazareti (Marekani) na Chuo cha Biblia cha Mnazareti (Marekani) kama itakavyoonekana kuwa inafaa kulingana na pesa zinazoweza kupatikana.

**335.10.** Kila mwaka, Halmashauri Kuu itachunguza na kufanya marekebisho yanayofaa katika mishahara na fadhili zinazohusika za wasimamizi wakuu kabla ya mikutano ya Kikao Kikuu.

**335.11**. **Taarifa**. Halmashauri Kuu, katika mkutano wake wa kawaida, itapokea ripoti kamili za shughuli za matawi kwa mwaka uliopita, hii ikiwa ni pamoja na ripoti ya fedha. Kila tawi pia litawasilisha pendekezo la makadirio ya matumizi kwa mwaka unaofuata.

**335.12.** Mtunza hazina mkuu atawasilisha kila mwaka kwa Halmashauri Kuu ripoti kamili ya mapato na matumizi ya pesa zote alizokuwa akitunza kwa mwaka uliopita, ikijumuisha pesa zinazodhaminiwa na raslimali pamoja na pesa ya udhamini na uwekezaji, pamoja na taarifa kamili ya matumizi yaliyopendekezwa ya mwaka unaofuata ya pesa ambazo hazikuhusishwa katika makadirio ya matawi ya Kanisa la Mnazareti. Mtunza Hazina mkuu atatekeleza wajibu wake kwa uaminifu chini ya mamlaka ya Halmashauri Kuu. (330.5)

**335.13**. Halmashauri Kuu itakutana kabla au mara tu baada ya kumalizika kwa mkutano wa Kikao Kikuu na itachagua katibu mkuu na mtunza hazina mkuu kama vile ilivyopeanwa katika Kanuni za Halmashauri Kuu, ambao watatumika katika ofisi hizo hadi kuahirishwa kwa Kikao Kikuu kitakachofuata na hadi waandamizi wao watakapochaguliwa na kuhitimishwa.

**335.14.** Washirika wa Halmashauri Kuu wanaowakilisha majimbo ya Marekani watachagua Halmashauri ya Marekani ya Malipo ya Kustaafu na Fadhili, ambayo itakuwa na mshirika mmoja kutoka katika kila jimbo la Marekani na mshirika mmoja maalum. Uteuzi utawasilishwa na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu kama ilivyoagizwa katika Kanuni za Halmashauri ya Malipo ya Kustaafu na Fadhili ya Marekani. (337)

**335.15**. Halmashauri Kuu itachagua msimamizi wa Shirika la Uchapishaji la Mnazareti baada kila Kikao Kikuu, ambaye atatumika hadi

kuhairishwa kwa Kikao Kikuu kitakachofuata na hadi mwaandamizi wao atakapochaguliwa na kuhitimishwa.

**335.16**. Jambo la ajenda la Halmashauri Kuu linaloathiri jimbo/taifa fulani litapelekwa baada ya kuidhinishwa na Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu, kwa washirika wa Halmashauri Kuu wa mkutano wa jimbo au taifa lililotajwa katika mkusanyiko.

**335.17**. Halmashauri Kuu itaweka au kuelekeza, kwa njia inayofaa, tume au kamati iliyoidhinishwa na Kikao Kikuu au Halmashauri Kuu kwa tawi au matawi, au kwa halmashauri yote, na kuipangia kazi, wajibu wake, na makadirio ya matumizi.

**335.18. Wakurugenzi wa Matawi.** Halmashauri Kuu itachagua mkurugenzi wa tawi ya Kanisa la Mnazareti kufuatana na utaratibu uliowekwa katika Kanuni za Halmashauri Kuu na *Sera za Halmashauri Kuu za Kitabu cha Mwongozo*, kutumika hadi mwisho wa Kikao Kikuu kitakachofuata na hadi waandamizi wao watakapochaguliwa na kuhitimishwa, isipokuwa wawe wameondolewa katika ofisi. (317.5.)

**335.19. Wakurugenzi wa matawi hayo watateuliwa kulingana na utaratibu ufuataao:** Ikiwa kuna mkurugenzi anayetumika, Kamati ya Uteuzi inaweza kupendekeza kura ya "ndiyo" au "la", ama iwasilishe majina ya wateule kadha. Kutafutwa kwa watu wenye uwezo wa kufanya kazi hiyo kutatekelezwa na kamati ya kutafuta kama ilivyoelezwa na Kanuni za Halmashauri Kuu. Kamati hii italeta majina mawili au zaidi kwa Kamati ya Uteuzi pamoja na sababu za kupendekezwa kwao.

Kamati ya Uteuzi, ambayo itakuwa na wasimamizi wakuu sita na Kamati ya Kuajiri kutoka katika idara mbalimblai, itawasilisha jina moja au zaidi kwa Halmashauri Kuu kwa uchaguzi utakaokubaliwa na Kanuni ya Halmashauri Kuu.

**335.20**. **Mishahara ya Viongozi Wakuu.** Halmashauri Kuu itaanzisha na kuweka utaratibu wa "kukadiria utendaji" na usimamizi wa mishahara ambao utahusisha mkurugenzi wa idara na wakurugenzi wa huduma au utumishi ulio na maelezo ya mshahara yanayotambua usawa wa wajibu na kustahili. Halmashauri Kuu itachunguza upya na kuidhinisha kila mwaka mishahara ya wakurugenzi wa idara, msimamizi wa Shirika la Uchapishaji la Mnazareti, na viongozi wengine ambao wanaweza kuidhinishwa na kuchaguliwa na Halmashauri Kuu.

**335.21**. Halmashauri Kuu, wakati wa kipindi cha mpito kabla ya mkutano wa Kikao Kikuu na/au Halmashauri Kuu, kwa uteuzi kama ilivyowekwa katika Kanuni za Halmashauri Kuu na kifungu cha 317.4, inaweza kujaza nafasi yoyote ya kazi inayoweza kutokea katika ofisi

zilizoorodheshwa katika kifungu 335.13. na kifungu cha 335.18, na ofisi yoyote kuu iliyoundwa na Kikao Kikuu, Halmashauri Kuu, au kamati zao zilizochaguliwa.

**336**. **Kustaafu** kwa viongozi wote na mkurugenzi mwingine yeyote aliyeorodheshwa katika kifungu cha 335.13 na 335.18, na kiongozi mwingine yeyote wa tawi aliyeajiriwa na Kikao Kikuu au tume zake zilizochaguliwa au Halmashauri Kuu na matawi yake, kutatekelezwa wakati wa mkutano wa Halmashauri Kuu baada ya wao kufikia umri wa miaka 70. Kukitokea nafasi za kazi, nafasi hizo zitajazwa kulingana na utaratibu uliowekwa katika *Kitabu cha Mwongozo.*

## M. MIPANGO YA MALIPO YA KUSTAAFU

**337.** Kutakuwepo na halmashauri ya malipo ya kustaafu, au idara yenye mamlaka, ya kushughulikia yenye wajibu kwa kila mpango wa malipo ya kustaafu unaohusiana na kanisa. Mpango wa malipo ya kustaafu unaweza kuwepo katika kiwango cha dhehebu, wilaya, wilaya moja au zaidi, kitaifa, jimbo mmoja au zaidi kama itakavyohitajika. (335.14)

**337.1.** Halmashauri Kuu itaanzisha na kuendeleza maongozi yaliyopendekezwa ambayo yana manufaa kwa mipango yote ya malipo ya kustaafu ya ulimwengu. Halmashauri Kuu haitatoa hakikisho kwamba mpango wowote wa malipo ya kustaafu hautapata hasara ama kupungua thamani. Halmashauri Kuu pia haitatoa hakikisho la malipo ya pesa zozote ambazo zitahitaji kulipwa kwa mtu yeyote kutoka katika mpango wowote wa malipo ya kustaafu, na haitapaswa kudaiwa ikiwa mpango wowote wa malipo ya kustaafu utapata hasara au kupungua thamani. (32.5)

**337.2.** Mipango yote ya malipo ya kustaafu, itawasilisha ripoti ya mwaka kwa halmashauri kuu kupitia kwa Kamati ya Kimataifa ya Malipo ya Kustaafu na Ufadhili katika hati na utaratibu unaotakikana.

## N. Wasaidizi wa Kanisa la Mnazareti Wanaohusishwa

**338.** Mashirika ya usaidizi wa Kanisa la Mnazareti yataanzishwa na kusimamiwa kulingana na kanuni zifuatazo:

a. Mshirika Mmoja
   i. Mshirika Mmoja wa shirika la wasaidizi la Marekani lazima awe "Kanisa lote la Mnazareti."
b. Halmashauri ya Ushirika wa Wakurugenzi
   i. Muundo: Kila shirika litaamua idadi inayohitajika ya wakurugenzi kulingana na mahitaji na kusudi lake.
      1. Mkurugenzi mmoja wa Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu ni mshirika kwa ajili ya wadhifa wake.

2. Mfanyakazi mmoja wa kiwango cha juu wa kanisa kuu aliyeteuliwa na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu.

ii. Wakurugenzi wote ni lazima wateuliwe na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu kwa kushirikiana na wakurugenzi wengine wa Shirika.

iii. Wakurugenzi wote ni lazima wateuliwe na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu wanaofanya kazi kwa niaba ya Mshirika Mmoja. Watakuwa katika ofisi hiyo hadi waandamizi wao watakapochaguliwa na kuhitimishwa.

iv. Kuondolewa: Mkurugenzi yeyote mmoja au zaidi anaweza kuondolewa kwa sababu au bila sababu, wakati wowote, kwa kura za Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu wanaofanya kazi kwa niaba ya Mshirika Mmoja wakati wa mkutano wowote maalum ulioitwa kwa kusudi hilo.

c. Maafisa na Watendaji Wakuu: Idadi na vyeo vya maafisa itaamuliwa na kila shirika kulingana na kanuni zao.

d. Mikutano ya Shirika.

i. Mikutano ya Mshirika Mmoja utafanyika tarehe na sehemu iliyotengwa mara kwa mara na Mshirika Mmoja wa (Kanisa Lote la Mnazareti).

ii. Mikutano ya Wakurugenzi itafanyika sehemu iliyotengwa na Shirika

e. Wakuu wa Shirika: Wanachaguliwa na kuondolewa kulingana na kanuni za usaidizi.

f. Mwaka wa Fedha: Wasaidizi wote watapokea kitambulisho cha mwaka wa fedha wa Kanisa lote la Mnazareti.

g. Kuvunjwa: Katika kuvunjwa kwa Shirika, mali yote itahamishwa kwa Mshirika Mmoja.

h. Kanuni za Ushirikishaji na Sheria

i. Wasaidizi wanaweza kuanzishwa kwa theluthi-mbili za kura ya Halmashauri Kuu ya Mshirika Mmoja. Kanuni za Ushirikishaji na Sheria ziko Chini ya idhini ya Halmashauri Kuu na Mshirika Mmoja.

ii. Marekebisho yanapendekezwa na theluthi mbili za kura ya Halmashauri ya Wakurugenzi wa Shirika na wako chini ya idhini ya Halmashauri Kuu ya Mshirika Mmoja.

## O. SHIRIKA LA UCHAPISHAJI LA MNAZARETI

**339.** Misheni ya Shirika la Uchapishaji la Mnazareti, ni kuchapisha au kutoa, kueneza, kumiliki, kuwa na hati, na kusimamia uchapishaji wote

kwa manufaa ya Kanisa la Mnazareti na masoko mengine ya Kikristo sawa na misheni ya Kanisa. Ili kulinda na kusimamia mali ya mawasiliano yanayotumika na Kanisa la Mnazareti na washirika wake, Kanisa la Mnazareti linakabidhi majukumu haya kwa Shirika la Uchapishaji la Mnazareti.

## P. Kamati Kuu ya Hatua za Kikristo

**340.** Kufuatia mkutano wa Kikao Kikuu, Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu itateua **Kamati Kuu ya Hatua za Kikristo,** mmoja wao atakuwa katibu mkuu, ambaye atatoa ripoti ya kazi ya kamati hiyo kwa Halmashauri Kuu.

**Kazi za Kamati Kuu ya Hatua za Kikristo zitakuwa ni:**

**340.1**. Kuwapa waumini wetu habari muhimu za kuwafaa kuhusu pombe na ulevi, sigara na tumbaku, madawa ya kulevya, na kamari na mambo ya maadili na yanahusu mahusiano kuambatana na imani ya kanisa, na kusambaza ujumbe katika mawasiliano ya kikanisa.

**340.2.** Kusisitiza utakatifu wa ndoa na utakatifu wa jamii ya Kikristo na kuangazia matatizo na uovu unaosababisha talaka. Hasa, kamati inafaa kusisitiza mpango wa kibiblia wa ndoa kama agano la maisha la milele, la kuvunjwa tu kwa kifo.

**340.3**. Kuwapa moyo watu wetu wanaotumika katika uongozi wa vyama vinavyosisitiza umuhimu wa kuwa na kiasi na mashirika mengine kama hayo yanayopigania haki ya raia kuishi kwa ustaarabu.

**340.4.** Kuwajulisha waumini wetu kuhusu kuadhimisha Siku ya Bwana, vyama vinavyoshikamana na kiapo cha siri, starehe ambazo ni kinyume cha maadili ya Kikristo, mambo mengine ya anasa za kidunia. (29.1)

**340.5.** Kusaidia na kuipa moyo kila wilaya kuanzisha Kamati ya Hatua za Kikristo; na kuipa kila kamati ya wilaya habari na vifaa vya mambo ya uadilifu ili vipelekwe kwa makanisa ya mtaa kwa hatua zifaazo.

**340.6.** Kufuatilia vile mambo ya uadilifu yenye umuhimu wa kitaifa na kimataifa yanavyoendelea na kutoa maoni ya kibiblia kwa vyama vinavyohusika ili yafikiriwe.

## Q. Kamati ya Maslahi ya Muinjilisti Aliyeitwa na Mungu

**341.** Kamati ya kushughulikia maslahi ya Muinjilisti mwenye Mwito wa Mungu itakuwa na msimamizi wa uhuishaji, ambaye atakuwa mwenyekiti wa kamati hiyo kwa ajili ya wadhifa wake, pamoja na makasisi wainjilisti wa kudumu wanne na mchungaji mmoja. Mkurugenzi wa ofisi ya Marekani na Canada, kwa kushirikiana na msimamizi wa uhuishaji atapeana orodha ya wateuzi ya kamati kwa Wasimamizi wa Halmashauri Kuu kwa

kuidhinishwa na uteuzi. Kamati au mwakilishi wake atawahoji waliopewa utume ambao wamependekezwa na vikao vyao vya wilaya kuwa “makasisi wainjilisti wa kudumu”. Pia itachunguza upya hali ya uinjilisti unaofanywa sehemu mbalimbali katika Kanisa la Mnazareti na kutoa mapendekezo kuhusu uhuishaji na wainjilisti kwa idara zinazohusika za Halmashauri Kuu. Nafasi zitakazopatikana zitajazwa kwa uteuzi kutoka kwa Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu kutoka kwa mapendekezo yaliyopokelewa kutoka mkurugenzi wa ofisi ya Marekani au Canada, kwa kushirikiana na msimamizi wa uhuishaji. (317.7, 510.3)

### R. Kamati ya Halmashauri ya Masomo ya Kimataifa

**342.** Baada ya Kikao Kikuu wakurugenzi wa Maendeleo ya Watumishi ya Ulimwengu, wakishirikiana na wasimamizi wa jimbo wa elimu, watatoa orodha ya wateuzi wa kuhudumu kwa Kamati ya Halmashauri ya Masomo Mbalimbali ya Kimataifa (KHMK). Wateuzi kwenye kamati wanaweza kuwa ni pamoja na wawakilishi wa kichungaji, uongozi, kielemu, na waumini. Utunzi wa Kamati ya Halmashauri ya Masomo Mbalimbali ya Kimataifa unafaa kuwakilishia kanisa la ulimwengu. Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu itateua Kamati ya Halmashauri ya Masomo ya Kimataifa kutumika kwa kipindi cha miaka minne.

Kamati ya Halmashauri ya Masomo ya Kimataifa itakutana kwa kipindi cha muda usiopungua mara moja kila miaka miwili katika sehemu inayoamuliwa na mkurugenzi wa Maendeleo ya Watumishi Ulimwenguni (529.1-529.2, 529.5)

### S. Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa

**343**. Huduma ya Vijana wa Mnazareti ulimwenguni inaongozwa chini ya msaada wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, chini ya Mkataba wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, na mamlaka ya msimamizi mkuu wa eneo la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na Halmashauri Kuu. Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa Ulimwenguni imeundwa na washirika, makundi ya mtaa na utaratibu wa wilaya, wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ulimwenguni kote. Huduma hii ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa Ulimwenguni inasimamiwa na Mkataba wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na Mpango wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa Ulimwenguni uliondhinishwa na Kikao Kikuu.

**343.1.** Kutakuwa na Kongamano baada ya kila miaka minne la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ambalo litakutana wakati ulipangwa

na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu, likishiriana na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti la Kimataifa Ulimwenguni. Kongamano hili la miaka minne litajumuisha washirika kama vile walivyotajwa katika Mpango wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa Ulimwenguni (810).

**343.2**. Kongomano hilo litachagua mwenyekiti wa Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti la Kimataifa Ulimwenguni. Naibu wa mwenyekiti wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti la Kimataifa Ulimwenguni atachaguliwa na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti la Kimataifa Ulimwenguni katika mkutano wake wa kwanza wakati Kikao Kikuu. Mwenyekiti wa Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti la Kimataifa Ulimwenguni na naibu wake watakuwa washirika wa Baraza la Huduma ya Vijana wa kanisa la Mnazareti wa Kimataifa kwa ajili ya wadhifa wao na watahudumu bila msharaha.

**343.3.** Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa Ulimwenguni itajumuisha mwenyekiti, naibu wake, na mwakilishi kutoka kila jimbo kama alivyochaguliwa na Mpango wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti la Kimataifa Ulimwenguni. Mkurugenzi wa Huduma ya Vijana wa kanisa la Mnazareti wa Kimataifa atahudumu kwenye baraza kama mshirika kwa ajili ya wadhifa wake. Baraza litawajibika kwa Halmashauri Kuu kupitia Kamati ya Misheni ya Ulimwenguni, na kwa msimamizi mkuu wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, na litajiongoza chini ya mamlaka ya katiba ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na Mpango wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti wa Kimataifa Ulimwenguni. Washirika wa Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti la Kimataifa Ulimwenguni watakuwa katika ofisi hiyo hadi kukamilika kwa Kikao Kikuu kinatakachofuata, wakati waandamizi wake watakapochaguliwa na kuhitimishwa. (810)

**343.4.** Huduma Kuu ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa (NYI) itawakilishwa katika Halmashauri Kuu ya Kanisa la Mnazareti na mwenyekiti wa Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti la Kimataifa Ulimwenguni aliyechaguliwa na Kikao Kikuu kutoka kwa uteuzi uliofanywa na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti la Kimataifa Ulimwenguni. (332.4, 333.3)

**343.5**. Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa Ulimwenguni itawakilishwa katika Kikao Kikuu na mwenyekiti wa Baraza la Huduma ya Vijana ya Kimataifa katika mwisho wa kipindi chake. (301)

## T. Baraza la Ulimwenguni la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa Ulimwenguni

**344.** Baraza la Ulimwenguni la Misheni wa Mnazareti Ulimwenguni litajumuisha mwenyekiti mkuu, mkurugenzi mkuu, na idadi ya washirika iliyotajwa na kuchaguilwa kulingana na Katiba ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa Ulimwenguni.

**344.1.** Baraza la Ulimwenguni litaongozwa na Katiba ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa. Baraza la Ulimwenguni litatoa ripoti kwa Kamati ya Misheni Ulimwenguni ya Halmashauri Kuu. (811)

**344.2. Uteuzi na Uchaguzi wa Mkurugenzi wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa Ulimwenguni.** Kamati kuu ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa ulimwenguni na msimamizi mkuu wa eneo watatunda kamati utafutaji ya kutambua wanafunzi wanaostahili kwenye cheo cha Mkurugenzi wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa Ulimwenguni. Majina mawili wanafunzi wanaostahili yatatolewa kwa Kamati ya Misheni ya Ulimwenguni ya Halmashauri Kuu.

Kamati ya Misheni ya Ulimwenguni ya Halmashauri Kuu pamoja na msimamizi mkuu wa eneo watayachunguza majina yaliyotolewa na kuidhinisha hadi majina mawili kwa kuchaguliwa na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu.

Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu itachagua mkurugenzi wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa Ulimwenguni kwa njia ya kura za siri kutokana na majina yaliyotolewa na Kamati ya Misheni Ulimwenguni ya Halmashauri Kuu.

Mkurugenzi wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa ulimwenguni atakuwa mshirika kwa ajili ya wadhifa wake wa Baraza la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa Ulimwenguni na mshirika wa wafanyakazi wa Misheni ya Ulimwenguni.

**344.3.** Jumuiya ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa itawakilishwa katika Halmashauri Kuu na mshirika mmoja aliyechaguliwa na Kikao Kikuu kutoka katika uteuzi uliofanywa na Baraza Kuu la Jumuiya ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa Ulimwenguni. (332.5, 333.4)

**344.4.** Kutakuwa na Kongamano la kila baada ya Miaka Minne utakaofanyika chini ya uongozi wa Baraza la Misheni ya Mnazareti la Kimataifa Ulimwenguni mara tu baada ya mkutano wa Kikao Kikuu. Kongamano hili litachagua Baraza Kuu Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa Ulimwenguni kulingana na Katiba. Kongamano hilo pia litachagua kiongozi mkuu, ambaye atakuwa mshirika wa Baraza Kuu la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa Ulimwenguni kwa ajili ya wadhifa wake. (811)

## U. Halmashauri za Kitaifa

**345.** Baada ya kupendekezwa na Wasimamizi wa Halmashauri Kuu, halmashauri ya kitaifa itaanzishwa mahali itakapohitajika ili kuwezesha kutimilizwa kwa umisheni na mikakati ya kanisa kataka taifa hilo. Halmashauri ya kitaifa itakuwa na mamlaka kama vile itakavyoongezwa halmashauri ya kitaifa na mkurugenzi wa jimbo na Halmashauri ya Wilaya ya taifa ya Kiwango cha 3, kama kutakuwa na yoyote na kwa kushirikiana na wasimamizi wakuu katika eneo la jimbo, na wilaya za taifa hilo, kutenda kazi kwa niaba ya kanisa katika kutimiza mikakati ya jimbo. Inaweza, wakati inahitajika na mkurugenzi wa jimbo, kwa kushirikiana na msimamizi mkuu wa eneo la jimbo, kuwa mamlaka ya kisheria yaliyoandikishwa ya Kanisa la Mnazareti katika taifa hilo. Wakati itaonekana kutokuwa na hitaji la kutimizwa kwa misheni au hitaji la rasmi, halmashauri ya kitaifa inaweza kuvunjwa na Wasimamizi wa Halmashauri Kuu.

Ushirika na mundo wa kila halmashauri ya kitaifa utakuwa katika hali ya kuidhinishwa na Wasimamizi wa Halmashauri Kuu.

Nakala ya kanuni ya kuratibu au kushirikishwa kwa halmashauri kama hiyo itahifadhiwa mara moja na katibu mkuu. Kanuni hizo zitawekwa katika hifadhi ya hivi karibuni kwa kuweka katika jalada mabadiliko yoyote na katibu mkuu. Shughuli zilizoendeshwa na halmashauri ya kitaifa kulingana na kuwezeshwa kwa misheni na mikakati ya Kanisa zitaongozwa kwa kushirikiana na mkurugenzi wa jimbo. Taarifa za mikutano ya mwaka na mikutano maalum ya halmashauri ya kitaifa itachunguzwa na Baraza la Halmashauri ya Jimbo, kabla ya kupelekwa kwa katibu mkuu kwa ukaguzi na mapendekezo kama inavyohitajika na Halmashauri Kuu. (32.5)

## V. Jimbo

**346. Chanzo na Kusudi.** Katika kustawi kwa kanisa kote ulimwenguni, kumetokea mkusanyiko wa wilaya kadha zilizoratibiwa katika sehemu za kijiografia zinazotambuliwa kama majimbo. Majimbo haya ni mkusanyiko wa wilaya zilizo chini ya utawala mkuu wa Kanisa la Mnazareti na ni sehemu na utamaduni unaotambulika zinaweza kuundwa katika jimbo la utawala kwa hatua ya Halmashauri Kuu na kuidhinishwa na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu.

**346.1. Maongozi ya Jimbo.** Katika kuambatana na utaratibu wa uongozi wa mwelekeo usiohitilafiana, Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu inaweza, ikihitajika, na kwa kushauriana na Baraza la Halmashauri ya Jimbo, kuandaa usimamizi wa kijimbo kulingana na mahitaji fulani, matatizo yanayotambuliwa, hali halisi iliyoko na utamaduni tofauti na

kiwango cha elimu katika sehemu zao za kijiografia za dunia. Katika hali kama hizo, Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu itatayarisha maongozi ambayo yatakumbatia kujitoa kusikoweza kujadiliwa, yatakayokuwa ni pamoja na Kanuni za Imani, kukubaliana na mafundisho ya utakatifu na mtindo wa maisha, na kutegemeza juhudi zetu za umishenari.

**346.2. Wajibu. Wajibu mkuu wa majimbo ni:**

1. Kutekeleza utume wa Kanisa la Mnazareti kupitia sehemu za uanzilishi, wilaya, na mashirika yake;
2. Kustawisha ufahamu wa jimbo, ushirika na njia za kutimiza Tume Kuu, kuleta pamoja wawakilishi wa wilaya na mashirika baada ya muda fulani kwa kupanga, maombi, na kutiana moyo;
3. Kuteua watu kwenda kwa Kikao Kikuu na Kongamano Kuu katika uchaguzi wa washirika katika Halmashauri Kuu;
4. Kulingana na Kitabu cha Mwongozo, kuanzisha na kudumisha, shule na vyuo au mashirika mengine;
5. Kuruhusiwa kuandika na kuchunguza watu wanaostahili kwa kazi ya umishenari katika jimbo kulingana na maongozi (346.3)
6. Kupanga mikutano ya Baraza la Ushauri la Jimbo, na mikutano ya mashauri ya jimbo
7. Kusaidia Halmashauri ya Kitaifa kama vile ilivyopitishwa katika Vifungu vya 345 na 346.3.

**346.3. Baraza la Ushauri la Jimbo (BUJ).** Jimbo linaweza kuwa na Baraza la Ushauri la Jimbo ambalo wajibu wake utakuwa kumsaidia mkurugenzi wa jimbo katika upangaji wa maendeleo ya jimbo, kukagua na kupendekeza kuidhinishwa au kutoidhinishwa kwa taarifa ya maazimio ya halmashauri za taifa kabla ya kupelekwa kwa katibu mkuu, kuorodhesha na kuchunguza wanaostahili kwa huduma ya umishenari ili wapendekezwe kwenye Halmashauri Kuu katika uteuzi wa Dunia, na kupokea ripoti kutoka kwa mkurugenzi wa jimbo, wakurugenzi wa maeneo ya kanisa, wasimamizi wa huduma.

Ushirika wa Baraza la Ushauri wa Jimbo utakuwa mwepesi ili uweze kuunda Baraza la Ushauri wa Jimbo kulingana na mahitaji, ustawi na matarajio ya majimbo yanayohusika. Wakurugenzi wa jimbo watapendekeza idadi ya washirika wa Baraza la Ushauri la Jimbo kwa mkurugenzi wa Misheni ya Dunia na msimamizi mkuu wa eneo kwa kuidhinishwa. Wasimamizi wakuu wa eneo watakuwa washirika kwa ajili ya wadhifa wao wa jimbo, wakurugenzi wa Misheni ya Dunia na wakurugenzi wa jimbo ambao watahudumu kama wenyeviti. Waajiriwa wanaowajibika kwa Misheni ya Dunia hawatakuwa wanafunzi wanaostahili katika uchaguzi wa Baraza la Ushauri la Jimbo bali watahudumu kama

wasaidizi. Washirika wa Baraza la Ushauri la Jimbo watachaguliwa kwa kura ya siri na washirika wa jimbo katika Kikao Kikuu. Baraza la Ushauri la Jimbo litajaza nafasi yoyote katikati ya Kikao Kikuu.

Mkurugenzi wa jimbo, kwa kushauriana na Baraza la Ushauri la Jimbo anaweza kuita mkutano wa jimbo au mkutano wa uinjilisti wa eneo. (32.5)

**346.4. Mkurugenzi wa Jimbo.** Jimbo linaweza kuwa na mkurugenzi aliyechaguliwa na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu kwa kushirikiana na mkurugenzi wa Misheni ya Dunia, na kuidhinishwa na Halmashauri Kuu, ili kufanya kazi kufuatana na maongozi na desturi za Kanisa la Mnazareti akitoa uongozi kwa wilaya, makanisa, na mashirika ya jimbo katika kutimiza utume, mipango ya ustawi, na kutekeleza maazimio ya kanisa.

Kila mkurugenzi wa jimbo atawajibika kiusimamizi kwa Misheni ya Dunia, Halmashauri Kuu, na kwa mambo ya kisheria na mamlaka, atawajibika kwa Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu.

**346.5.** Msimamizi wa Mipango ya Eneo. Wakati itahitajika, mkurugenzi wa jimbo anaweza kuanzisha muundo wa eneo katika jimbo, na kupendekeza kwa mkurugenzi wa Umisheni wa Ulimwenguni uteuzi wa wasimamizi wa Mipango ya eneo kulingana na *Maongozi ya Misheni ya Dunia na Maelekezo ya Kitabu cha Mwongozo*. Msimamizi wa mipango ya eneo atawajibika kwa mkurugenzi wa jimbo.

**346.6**. **Kamati ya Ushauri ya Masomo ya Juu ya Jimbo.** Kamati ya Ushauri ya Masomo ya Juu ya Jimbo (KUMJJ) itaundwa na msimamizi wa elimu wa jimbo, ambaye anaweza kuwa mwenyekiti wa kamati hiyo kwa ajili ya wadhifa wake, pamoja na wawakilishi walioteuliwa kwa kushauriana na mkurugenzi wa jimbo. Washirika wa Kamati hii watawakilisha sehemu zote zinazohusika na elimu ya Kikristo (k.m. wachungaji, watawala, waelimishaji na waumini) katika jimbo.

**346.7. Wajibu wa Kamati ya Ushauri ya Masomo ya Juu ya Jimbo. Majukumu ya msingi ya Kamati ya Ushauri ya Masomo ya Juu ya Jimbo yatakuwa ni:**

1. Kuanzisha *Kitabu cha Jimbo cha maelezo ya Ustawi wa Kihuduma*, kinachoeleza kiwango cha chini cha elimu kwa ajili ya kuwekwa wakfu katika jimbo. *Kitabu cha Jimbo cha maelezo ya Ustawi wa Kihuduma*, ni lazima kiambatane na viwango vya chini vilivyo katika *Kitabu cha Mwongozo* na kufafanuliwa katika *Kitabu cha Viwango vya Kimataifa vya maelezo ya Ustawi wa Kihuduma;*
2. Kuanzisha njia mbalimbali kwa ajili ya mipangilio ya elimu ya utumishi katika jimbo, kuhakikisha kwamba mipangilio hiyo inafikia

viwango vya chini vya Kamati ya Elimu ya Jimbo (KEJ) na Kamati ya Ushauri wa Elimu ya Kimataifa;

3. Kushirikiana na watoa elimu wa jimbo kwa kutafsiri viwango hivi katika mipangilio ya elimu;
4. Kupitia mipangilio ya elimu ya kitumishi iliyotolewa ili kulinganisha na *Kitabu cha Jimbo cha viwango vya elimu na kile cha viwango vya elimu cha Kimataifa.*
5. Kupeleka mipangilio ya jimbo ya elilmu ya kitumishi kwa Kamati ya Ushauri wa Elimu ya Kimataifa ili ikubaliwe na kuidhinishwa.

SURA YA NNE
## ELIMU YA JUU

# KANISA NA HALMASHAURI YA ELIMU YA CHUO/CHUO KIKUU CHA MNAZARETI ULIMWENGUNI CHA USHIRIKA WA ELIMU WA KIMATAIFA

# I. KANISA NA CHUO/CHUO KIKUU

**400.** Kanisa la Mnazareti, tangu lianzishwe, limekuwa likitilia mkazo umuhimu wa elimu ya juu. Kanisa hupatia vyuo/vyuo vikuu wanafunzi, usimamizi na uongozi mwelekevu, na msaada wa kifedha na wa kiroho. Chuo/chuo kikuu huelimisha vijana wa kanisa na wengi wa watu wake wazima, na kuwaongoza ili waweze kukomaa kiroho, kuwa na manufaa kwa kanisa, na kutuma watumishi wa Kristo ulimwenguni wenye ufahamu na upendo. Chuo/chuo kikuu, ingawa si kanisa la mtaa, ni sehemu muhimu ya kanisa; ni dhihirisho la kanisa.

Kanisa la Mnazareti linaamini katika thamani na heshima ya maisha ya mwanadamu na haja ya kuwa na mazingira ambayo watu wanaweza kuokolewa na kuimarishwa kiroho, kielimu, na kimwili, "waliotakaswa, wa kumfaa Bwana, na wametengenezwa kwa kila kazi iliyo njema" (2 Timotheo 2:21). Kazi ya msingi ya shughuli na dhihirisho la utamaduni wa kanisa la mtaa-uinjilisti, elimu ya dini, huduma za huruma, na ibada-huonyesha upendo wa kanisa kwa Mungu na kuhusika na watu.

Katika kiwango cha kanisa la mtaa, elimu ya Kikristo ya vijana na watu wazima katika viwango tofauti vya kukua kwa mwanadamu, huimarisha uwezo wa injili. Makanisa yanaweza kushirikisha katika shabaha na kazi zao ratiba ya elimu ya chekechea/mipangilio ya kielimu ya shule katika viwango vyovyote au vyote, kuanzia shule ya chekechea, hadi shule ya upili. Katika kiwango cha kanisa kwa jumla, kazi ya kihistoria ya kutoa elimu ya juu, na mafunzo ya kutayarisha watumishi wa kanisa kwa huduma ya Mungu itaendelezwa. Mahali popote ambapo vyuo kama hivyo vinaendeshwa, vitaendesha shughuli zake kulingana na filosofia na thiolojia ya Kanisa la Mnazareti kama ilivyoagizwa na Kikao Kikuu na kuelezwa katika *Kitabu cha Mwongozo.*

**400.1. Taarifa ya Utume wa Elimu.** Elimu katika Kanisa la Mnazareti, yenye misingi ya kibiblia na thiolojia ya mfumo wa utakatifu ulioenezwa na Wesley na inayowajibika kwa kusudi lililotajwa la dhehebu, inalenga kuwaongoza wale wanaotazamia elimu katika kukubali, kukuza, na katika kudhihirisha kwa kanisa na ulimwengu, ufahamu wa Kikristo wa maisha ya kijamii na kibinafsi. Zaidi ya hayo, vyuo kama hivyo vya elimu ya juu vitajitahidi kuwa na utaratibu wa elimu, kutoa mafunzo muhimu, na ushahidi wa mafanikio ya usomi ambao utawatayarisha wanaohitimu kufanya kazi kwa ustadi katika wajibu watakaochagua.

**400.2**. Idhini ya Kikao Kikuu, kwa pendekezo la Halmashauri ya Kimataifa ya Elimu, inahitajika kabla ya kuanzisha vyuo vya elimu vinavyotoa shahada.

Idhini ya kustawisha au kubadilisha kiwango cha chuo kinachoendelea inaweza kutolewa na Halmashauri Kuu kwa pendekezo la Halmashauri ya Kimataifa ya Elimu.

Hakuna kanisa la mtaa au muungano wa makanisa, au watu wanaowakilisha kanisa la mtaa au kundi la makanisa, linaloweza kuanzisha au kudhamini shule inayopita kiwango cha upili au chuo cha kutayarisha wanafunzi kihuduma kwa niaba ya kanisa, isipokuwa kwa pendekezo la Halmashauri ya Elimu ya Kimataifa.

## II. SHIRIKA LA ELIMU LA MNAZARETI ULIMWENGUNI

**401.** Kutakuwa na Shirika la Elimu ya Mnazareti Ulimwenguni ambalo litajumuisha mwenyekiti, mkuu wa chuo, kasisi, au mkurugenzi (au mwakilishi wake aliyeteuliwa) wa kila Halmashauri ya Elimu ya Kimataifa ya chuo kilicho chini ya Kanisa la Mnazareti, wasimamizi wa elimu wa jimbo, kamishna wa elimu, mkurugenzi wa Misheni ya Dunia, na msimamizi mkuu wa eneo na Halmashauri ya Elimu ya Kimataifa.

## III. HALMASHAURI YA ELIMU YA KIMATAIFA

**402.** Halmashauri ya Elimu ya Kimataifa itakuwa wakili wa kanisa katika taasisi za elimu katika Kanisa la Mnazareti.

Halmashauri hii itakuwa na washirika kumi na mbil: washirika nane waliochaguliwa na Halmashauri Kuu, pamoja na washirika hawa kwa ajili ya wadhifa wao: wawakilishi wawili wa elimu kwenye Halmashauri Kuu, mkurugenzi wa Misheni ya Dunia, mkurugenzi wa Ustawi wa Watumishi Duniani na kamishna wa elimu. Kamati ya Uteuzi inayojumuisha kamishna wa elimu, mkurugenzi wa Misheni ya Dunia, wawakilishi wawili wa elimu kwenye Halmashauri Kuu, na wasimamizi wakuu wa eneo wa Halmashauri ya Elimu ya Kimataifa na Misheni ya Dunia itawakilisha wateuzi nane walioidhinishwa na Wasimamizi wa Halmashauri Kuu kwa Halmashauri Kuu ili kuchaguliwa.

Katika juhudi ya kuhakikisha uwakilishi mkubwa katika kanisa lote, Kamati ya Uteuzi itatoa wateuzi kama ifuatavyo: msimamizi mmoja wa jimbo wa elimu; waumini watatu; makasisi wawili waliopewa wajibu kutoka kwa majimbo ya Misheni ya Dunia ambapo hakuna msimamizi wa elimu ambaye ameteuliwa; wateuzi wawili. Hakuna jimbo la Misheni ya Dunia ambalo litakuwa na zaidi ya mshirika mmoja aliyechaguliwa kwenye Halmashauri ya Elimu ya Kimataifa hadi kila jimbo litakapowakilishwa.

Katika hatua yote ya uteuzi na uchaguzi, mwangaza utatolewa kwa uchaguzi wa watu walio na maono ya tamaduni mbalimbali na/au ujuzi wa waelimishaji.

**Wajibu wa Halmashauri ya Elimu ya Kimataifa** ni:

**402.1.** Kuhakikisha kwamba vyuo viko chini ya usimamizi wa kisheria wa halmashauri zao za utawala ambazo katiba zake na sheria zitapaswa kuambatana na mkataba au kanuni za usajili na ambazo zitalingana na mwongozo ulioelezwa katika *Kitabu cha Mwongozo cha Kanisa la Mnazareti.*

**402.2.** Kuhakikisha kwamba washirika wa halmashauri za utawala za taasisi za Mnazareti watakuwa washirika wa Kanisa la Mnazareti walio katika msimamo mzuri. Watapaswa kuwa wanakubaliana kabisa na Kanuni za Imani, ikiwa ni pamoja na mafundisho ya utakaso kamili na jinsi Kanisa la Mnazareti linavyotumika kama ilivyoelezwa katika *Kitabu cha Mwongozo*. Kadiri inavyowezekana, ushirika wa halmashauri za usimamizi wa vyuo vya elimu ya juu utakuwa wa idadi sawa ya waumini na wahudumu.

**402.3.** Kupokea pesa zitakazochangwa kwa kusudi la kielimu kwa njia ya ruzuku, urithi, na michango, na itatoa pendekezo kila mwaka la mgawo wa pesa hizo kwa kila chuo/chuo kikuu cha elimu kulingana na maongozi yaliyokubaliwa na Halmashauri Kuu. Taasisi hazitaendelea kupewa msaada ikiwa viwango vyao vya elimu, mipango ya utaratibu na ripoti za fedha hazipelekwi kwa Halmashauri ya Kimataifa ya Elimu.

**402.4**. Kupokea na kushughulikia ipasavyo taarifa ya mwaka kutoka kwa kamishna wa elimu inayoeleza kwa ufupi habari ifuatayo kutoka kwa Halmashauri ya Kimataifa ya taasisi za Elimu: (1) ripoti za tarakimu za mwaka, (2) ripoti ya mwaka ya ukaguzi wa fedha, na (3) makadirio ya bajeti ya mwaka unaofuata.

**402.5.** Kupendekeza na kutoa msaada na uwakili, ingawa wajibu wake kwa taasisi ni ushauri, kwa Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu na Halmashauri Kuu.

**402.6.** Kutumikia kanisa katika mambo yanayohusiana na taasisi za elimu vya kanisa la Mnazareti ili kuimarisha uelewano kati ya taasisi hizo na kanisa,

**402.7**. Kuwasilisha shughuli zake na mapendekezo kwa kamati inayofaa ya Halmashauri Kuu.

**403.** Katiba zote za taasisi na kanuni lazima zijumuishe kanuni inayohusu kubalitilishwa na kuondoelewa kwa mali inayoonyesha kwamba Kanisa la Mnazareti litapokea mali kama hiyo ili kutumiwa kwa ajili ya huduma za elimu ya kanisa.

# SEHEMU YA TANO

## HUDUMA NA UTUMISHI WA KIKRISTO

MWITO WA KUHITIMU WA MHUDUMU

VIWANGO VYA MAJUKUMU YA HUDUMA

ELIMU YA HUDUMA YA MTUMISHI

HATI NA SHERIA ZA KIHUDUMA

## I. MWITO NA KUHITIMU KWA MHUDUMU

**500.** Kanisa la Mnazareti linatambua kwamba waumini wote wameitwa kuwahudumia watu wote.

Pia tunatambua kwamba Kristo anawaita baadhi ya wanaume na wanawake huduma maalum na ya hadhara hata wakati Aliwachagua na kuwaweka wakfu mitume Wake 12. Wakati kanisa, kwa kuangaziwa na Roho Mtakatifu, linatambua mwito kama huo wa kiungu, kanisa linaidhinisha na kumsaidia mtu huyo kuingia katika huduma ya maisha.

**501. Thiolojia ya Huduma ya Wanawake.** Kanisa la Mnazareti linaunga mkono hali ya wanawake kutumia vipawa vyao vya kiroho ambavyo walipewa na Mungu ndani ya kanisa na kuthibitisha haki ya kihistoria ya wanawake kuchaguliwa na kuteuliwa kwa kiwango cha uongozi ndani ya Kanisa la Mnazareti, ikiwa ni pamoja na ofisi za kasisi na shemasi.

Kusudi la kazi ya Kristo ya ukombozi ni kuweka huru viumbe vya Mungu kutokana na laana ya Kuanguka. Wale walio "ndani ya Kristo" ni viumbe vipya (2 Wakorintho 5:17). Katika jamii ya ukombozi, hakuna mwanadamu anayestahili kuchukuliwa kwa kiwango cha chini kwa misingi ya hali yake, rangi, au jinsia (Wagalatia 3:26-28). Kukubali ukweli dhahiri ulioundwa na maagizo ya Paulo kwa Timotheo (1 Timotheo 2:11-12) na kwa kanisa la Korintho (1 Wakorintho 14:33-34), tunaamini kutafsiri vifungu hivi kama kuzuia jukumu za wanawake katika huduma zenye mzozo mkali na vifungu maalum vya maandiko ambavyo vinapendekeza kuhusika kwa wanawake katika majukumu ya uongozi wa kiroho (Yoeli 2:28-29; Matendo ya Mitume 2:17-18; 21:8-9; Warumi 16:1, 3, 7; Wafilipi 4:2-4), na kupinga roho na mafundisho ya kitamaduni ya utakatifu wa Wesley. Mwishowe, hazikubaliani na tabia za Mungu anayewakilishwa kupitia kwa Maandiko, hasa kama ilivyofunuliwwa katika utu wa Yesu Kristo.

**502**. Thiolojia ya kuwekwa Wakfu. Wakati tunathibitisha maandiko yanayohusu ukuhani wa ulimwengu na huduma ya waumini wote, kuwekwa wakfu kunaonyesha imani ya kibiblia kuwa Mungu huita na kuwapa vipawa baadhi ya wanaume na wanawake kwa ajili ya uongozi wa kihuduma kanisani. Kuwekwa wakfu ni tendo la kuthibitishwa, la mamlaka ya Kanisa, ambalo linatambua na kuthibitisha mwito wa Mungu kwa uongozi wa kihuduma kama mawakili na watangazaji wa injili na Kanisa la Yesu Kristo. Kwa hali hiyo, kuwekwa wakfu ni ushahidi kwa Kanisa la Ulimwengu na dunia yote kuwa mhusika huyu ana ushuhuda wa maisha ya utakatifu, anamiliki vipawa na neema za huduma ya watu wote, na ana kiu

ya maarifa, hasa ya Neno la Mungu, na ana uwezo wa kuwasilisha mafundisho yanayofaa.

(Matendo ya Mitume 13:1-3; 20:28: Warumi 1:1-2; 1 Timotheo 4:11-16; 5:22; 2 Timotheo 1:6-7)

**502.1.** Kanisa la Mnazareti linategemea sana kuhitimu kiroho, sifa, na tabia za maisha ya wahudumu Wake. (538.17)

**502.2**. Mhudumu wa injili wa Kanisa la Mnazareti anastahili kuwa na amani na Mungu kupitia Bwana wetu Yesu Kristo, na kutakaswa kamili kwa kubatizwa na au kujazwa na Roho Mtakatifu. Mhudumu huyo anafaa kuwa na upendo wa ndani kwa wale wasioamini, akiamini kwamba wanapotea, na mwito wa kutangaza wokovu.

**502.3**. Mhudumu anastahili kuwa mfano mwema kwa kanisa: anafika kwa wakati, mwangalifu, mwadilifu, mwaminifu, katika usafi, wa kuelewa, mvumilivu, wa utu wema, mwenye upendo, na ukweli kwa nguvu za Mungu (2 Wakorintho 6:6-7).

**502.4.** Mhudumu ni lazima pia awe na ufahamu mzito wa umuhimu wa waumini kuwa wakamilifu na kuendeleza neema za Kikristo katika maisha ya kawaida, kwamba "upendo wao uzidi kuwa mwingi sana, katika hekima na ufahamu wote." (Wafilipi 1:9). Mtu ambaye atahudumu katika Kanisa la Mnazareti lazima awe na shukrani kubwa ya wokovu na maadili ya Kikristo.

**502.5.** Mhudumu anapaswa kuitikia fursa za kuandaa wahudumu wa siku za usoni na kukuza mwito wa huduma

**502.6.** Mhudumu ni lazima awe na karama na neema, kwa ajili ya huduma. Ni lazima awe na kiu ya maarifa, hasa ya Neno la Mungu, na lazima awe na hekima ya kufanya maamuzi, uwezo wa kuelewa vizuri, na maoni dhahiri yanayohusu mpango wa wokovu kama ilivyoelezwa katika Maandiko. Watakatifu wataimarishwa na wenye dhambi watageuzwa kupitia huduma yake. Zaidi, mhudumu wa injili katika Kanisa la Mnazareti anapaswa awe mfano katika maombi.

## II. NAMNA ZA HUDUMA NA WAJIBU WAKE

### A. Huduma ya Waumini Washirika

**503.** Wakristo wote wanapaswa kujihesabu kama wahudumu wa Kristo na kutafuta kujua mapenzi ya Mungu kuhusu njia zinazofaa za kutumika. (500)

**503.1**. Kanisa la Mnazareti linatambua huduma ya waumini washirika. Pia kanisa linatambua kwamba mshirika anaweza kutumikia kanisa katika viwango mbalimbali. (Waefeso 4:11-12) Kanisa linatambua majukumu yafuatayo ya utumishi ambapo kikao cha wilaya kinaweza kumweka muumini mshirika: mchungaji, muinjilisti, mmishenari, mwalimu, kiongozi-msimamizi, kasisi wa jeshi au gereza, na utumishi maalum. Mafunzo ya muumini mara nyingi yanahitajika, au yanatakikana pakubwa, ili kutimiza viwango vyao. (605.3)

**503.2. Mhudumu Muumini.** Mshirika yeyote wa Kanisa la Mnazareti ambaye anahisi kuitwa kuhudumu kama mwanzishaji wa kanisa, mchungaji wa taaluma mbalimbali, mwalimu, muinjilisti muumini muinjilisti wa nyimbo ambaye ni muumini, mhudumu wa uwakili, mhudumu wa kazi ya kanisa, na/au huduma zingine zinazohitajika kwa niaba ya kanisa, lakini ambaye kwa sasa anahisi kuwa na mwito maalum wa kuwa kasisi, anaweza kutafuata masomo yanayoelekeza kwa huduma ya muumini.

**503.3**. Halmashauri ya kanisa la mtaa, kwa kupendekeza na mchungaji, mwanzo watamchunguza na kumuidhinisha mhudumu muumini kwa uzoefu wake binafsi wa wokovu, kuhusika kwake kamili katika huduma za kanisa, na maarifa yake ya kazi ya kanisa.

**503.4**. Halmashauri ya kanisa la mtaa inaweza kumpa mhudumu muumini anayehusika hati iliyowekwa sahihi na mchungaji na katibu wa halmashauri ya kanisa.

**503.5**. Hati hiyo ya muumini mhudumu inaweza kutolewa upya kila mwaka na halmashauri ya kanisa kwa pendekezo la mchungaji, ikiwa muumini mhudumu amekamilisha aghalau masomo mawili katika kiwango cha elimu ya muumini mhudumu kama ilivyopitishwa na Mafunzo ya Kuendelea ya Muumini. Muumini mhudumu ataripoti kila mwaka kwa halmashauri ya kanisa.

**503.6**. Kwa muumini mhudumu anayetumika kwa agizo la wilaya kama mwanzilishi wa kanisa, mchungaji wa mpito, mchungaji anayefanya kazi nyingine, na/au huduma zingine maalum, baada ya kukamilisha mafunzo yanayohitajika, hati ya muumini mhudumu inaweza kutolewa upya na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya, ikiwa imesainiwa na msimamizi wa wilaya na katibu wa Halmashauri ya Wilaya. Hati ya muumini mhudumu inaweza kutolewa upya kila mwaka na Halmashauri ya Wilaya kwa pendekezo la msimamizi wa wilaya.

**503.7.** Muumini mhudumu anayetumika nje ya kanisa la mtaa ambalo yeye ni mshirika atakuwa chini ya uteuzi na usimamizi wa msimamizi wa wilaya na Halmashauri ya Wilaya, na atatoa ripoti kwao kila mwaka.

Wakati kazi ya wilaya itakapomalizika, taarifa itapelekwa kwa kanisa la mtaa ambalo muumini mhudumu ana ushirika kwa na kutoa ripoti.

**503.8.** Baada ya kukamilisha kiwango cha Kwanza cha masomo ya wahudumu, muumini mhudumu ataendelea na mafunzo maalum yanayoambatana na huduma aliyochagua kupitia ofisi ya Mafunzo ya Muumini ya Kuendelea.

**503.9**. Muumini mhudumu hana kibali cha kusimamia kuadhimisha kwa sakramenti za ubatizo na Meza ya Bwana, na hataweza kuadhimisha sherehe za ndoa.

## B. Huduma ya Watumishi

**504.** Kanisa la Mnazareti linatambua mwito mmoja tu wa huduma ya kuhubiri, ule wa kasisi. Pia linatambua kwamba mshirika wa ukasisi anaweza kutumikia kanisa katika viwango mbalimbali. (Waefeso 4:11-12) Kanisa linatambua viwango vifuatavyo vya utumishi ambavyo kikao cha wilaya kinaweza kumweka kasisi, shemasi, au, ikiwa hali ilivyo itaruhusu, mhudumu aliyepewa hati kuwa: mchungaji, muinjilisti, mmishenari, mwalimu, kiongozi-msimamizi, kasisi wa jeshi au gereza na utumishi maalum. Mafundisho ya utumishi na kuwekwa wakfu mara nyingi yanahitajika, au kutamaniwa, kutimiza viwango hivi kama "wahudumu wasaidizi". *Kitabu cha Maelezo ya Ustawi wa Kihuduma* kipeana mwongozo wa kila kiwango cha huduma ambayo itasaidia halmashauri za wilaya katika kutambua kuhitimu kunachohitajika kwa kuthibitishwa kuwa mhudumu msaidizi. Ni wale tu wahudumu wasaidizi ambao watakuwa washirika wa kupiga kura wa kikao cha wilaya.

**504.1.** Watu wote waliopewa kazi ya huduma fulani watatoa ripoti kila mwaka kwa kikao cha wilaya kilichowapa huduma hiyo.

**504.2**. Watu wote waliopewa kazi ya huduma fulani wanaweza kuomba na kupata hati ya namna ya utumishi wao kila mwaka kutoka kwa kikao cha wilaya kilichowapa huduma hiyo, iliyotiwa sahihi na msimamizi wa wilaya na katibu wa wilaya.

**504.3**. Watu wote waliopewa namna fulani ya huduma, wakiwekwa katika orodha ya walemavu na daktari wa matibabu aliyeidhinishwa, wanaweza kuhesabiwa kama "walemavu katika huduma."

## III. MAJUKUMU YA HUDUMA

**505.** Majukumu ya huduma yako kama ifuatavyo:

**506. Kiongozi-msimamizi.** Kiongozi-msimamizi ni kasisi au shemasi ambaye amechaguliwa na Kikao Kikuu kama kiongozi mkuu; au mhudumu

aliyechaguliwa au kuajiriwa ili kutumika katika kanisa kwa jumla. Kiongozi-msimamizi anaweza kuwa pia kasisi, ni kasisi au shemasi ambaye amechaguliwa na Kikao Kikuu kama kiongozi mkuu; au kasisi, shemasi, ama mhudumu aliyechaguliwa na kikao cha wilaya kuwa msimamizi wa wilaya; au mhudumu aliyechaguliwa au kuajiriwa katika kazi yake ya msingi katika utumishi wa wilaya. Mtu kama huyo ni mhudumu aliyepewa kazi.

**507. Kasisi wa Jeshi au Gereza.** Kasisi wa jeshi ni mhudumu aliyewekwa wakfu ambaye anahisi mwongozo wa Mungu wa huduma maalum katika jeshi, shirika au kiwanda. Wahudumu wote wanaotafuta kuhudumu katika huduma ya jeshi wanaweza kuidhinishwa na msimamizi wao wa wilaya. Kasisi aliyewekwa wakfu anayetumika katika huduma ya jeshi kama kazi yake ya msingi atakuwa mhudumu msaidizi, na atatoa taarifa kila mwaka kwa kikao cha wilaya na kutilia maanani uongozi na ushauri wa msimamizi wa wilaya na Halmashauri ya Wilaya. Kasisi huyo wa jeshi anaweza kupokea washirika wa ushirika katika Kanisa la Mnazareti kwa kushauriana rasmi na Kanisa la Mnazareti lililoratibiwa, kuadhimisha sakramenti kufuatana na *Kitabu cha Mwongozo,* kupeana utunzaji wa kichungaji, kuwafariji wanaohuzunika, kuonya na kutima moyo na kutafuta kwa njia zote kubadilishwa kwa wenye dhambi, kutakaswa kwa waumini, na kuwajenga watu wa Mungu katika imani takatifu. (519, 538.9, 538.13)

**508. Shemasi wa Kike.** Mwanamke ambaye ni mshirika wa Kanisa la Mnazareti na anaamini kwamba anaongozwa kiuungu kuhusika katika huduma ya kuwatumikia wagonjwa na wahitaji, kuwafariji wenye huzuni, na kufanya kazi nyingine za ukarimu wa Kikristo, na ambaye ameonyesha ushahidi katika maisha yake wa uwezo, neema, na wema, na ambaye katika miaka iliyotangulia mwaka 1985 alikuwa shemasi wa kike aliyepewa hati ama aliyewekwa wakfu kama shemasi wa kike ataendelea katika hali kama hiyo. Hata hivyo, wale wanawake walioitwa katika huduma kamili lakini hawakuitwa kuhubiri watakamilisha matakwa ya kutawazwa kama shemasi. Wanawake wanaotaka hati ya huduma za rehema wanaweza kujitahidi kukamilisha matakwa yanayohitajika kwa muumini mhudumu. (113.9, 503.2-503.9)

**509. Muelimishaji.** Muelimishaji ni kasisi, shemasi, au mhudumu aliyepewa hati ambaye ameajiriwa kutumika kwenye kazi ya usimamizi au katika taasisi mojawapo ya mashirika ya kielimu ya Kanisa la Mnazareti. Wilaya inayohusika itamuorodhesha mtu huyo kama muelimishaji wa kazi aliyopewa.

**510. Muinjilisti.** Kasisi au mhudumu aliyepewa hati ambaye ni muinjilisti ni yule aliyejitoa kusafiri na kuhubiri injili, na ambaye ameidhinishwa na kanisa kuendeleza uhuisho na kueneza injili ya Yesu Kristo katika nchi. Kanisa la Mnazareti linatambua viwango vitatu vya uinjilisti ambavyo kikao cha wilaya kinaweza kuwapa wahudumu: muinjilisti aliyesajiliwa, muinjilisti aliyetumwa, na muinjilisti anayejitoa kwa uinjilisti kama kazi yake. Muinjilisti anayetoa wakati wake kwa uinjilisti nje ya kanisa lake la mtaa kama kazi yake ya msingi, na ambaye hana uhusiano wa kustaafu na kanisa, au mojawapo wa idara zake au mashirika yake, atahesabiwa kama mhudumu aliyepewa kazi.

**510.1.** Muinjilisti aliyesajiliwa ni kasisi, au mhudumu aliyepewa hati, ambaye ameonyesha nia ya kutoa wakati wake kwa ajili ya uinjilisti kama huduma yake ya msingi. Kusajiliwa huko kutakuwa kwa muda wa mwaka mmoja. Kusajiliwa upya na vikao vifuatavyo vya wilaya kutategemea hali au kiwango na kiasi cha kazi ya uinjilisti iliyofanywa na muinjilisti huyo katika mwaka ulioutangulia mkutano wa kikao cha wilaya.

**510.2.** Muinjilisti aliyetumwa ni kasisi ambaye ametimiza matakwa yote ya muinjilisti aliyesajiliwa kwa muda wa miaka miwili mfululizo. Utume huo utakuwa kwa kipindi cha mwaka mmoja, na unaweza kutolewa upya kwa yule anayetimiza matakwa yanayohitajika na vikao vya wilaya vitakavyofuata.

**510.3.** Muinjilisti aliyejitoa kwa uinjilisti kama kazi yake ni kasisi ambaye ametimiza matakwa ya muinjilisti aliyetumwa kwa kipindi cha miaka 4 kamili mfululizo na miaka inayofuata mara tu kabla ya kutuma maombi ya kuwa katika kiwango cha muinjilisti aliyejitoa kwa huduma ya uinjilisti kama kazi yake, na amependekezwa na Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya au Halmashauri ya Huduma ya Wilaya na kuidhinishwa na Kamati Inayohusika na Maslahi ya Muinjilisti aliyeitwa na Mungu, na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu. Huduma ya uinjilisti wa kiwango hiki itaendelea hadi wakati muinjilisti anayehusika atakosa kutimiza matakwa ya muinjilisti aliyetumwa, au hadi atakapofikia wakati wa kustaafu. (231.2, 536)

**510.4.** Kujichunguza kibinafsi kwa kawaida na ukaguzi kama ule wa uhusiano wa kiuchungaji na kanisa utatekelezwa na muinjilisti akiwa pamoja na msimamizi wa wilaya angalau kila baada ya miaka 4 kufuatia kupewa wadhifa huo. Msimamizi wa wilaya atakuwa na wajibu wa kupanga na kutekeleza kikao cha ukaguzi. Kikao hicho kitapangwa kwa kushauriana na muinjilisti anayehusika. Baada ya kukamilisha ukaguzi huo, taarifa ya matokeo yake itapelekwa kwa Kamati Inayohusika na

Maslahi ya muinjilisti aliyeitwa na Mungu ili achunguzwe matakwa ya kuhitimu kwa muinjilisti huyo kwa kuidhinishwa upya. (211.21)

**510.5.** Kasisi au mhudumu aliyepewa hati ambaye ana uhusiano wa kustaafu na kanisa au mojawapo ya idara zake, na anataka kufanya kazi ya kihuduma kwa njia ya mikutano ya uhuisho au uinjilisti, anaweza kupewa hati ya "utumishi wa muinjilisti aliyestaafu." Hati kama hiyo, ambayo itakuwa kwa kipindi cha mwaka mmoja, itapigiwa kura na kikao cha wilaya ikipendekezwa na msimamizi wa wilaya, na inaweza kutolewa upya na vikao vya wilaya vitakavyofuata kulingana na kazi halisi ya uinjilisti itakayokuwa imefanywa katika mwaka uliotangulia kikao hicho cha wilaya.

**510.6.** Kasisi au mhudumu aliyepewa hati anayetaka kuingia katika huduma ya uinjilisti katikati ya vikao vya wilaya anaweza kutambuliwa na kamati kuu ya Huduma za Uinjilisti kwa pendekezo la msimamizi wa wilaya. Kusajiliwa au utume wa muinjilisti utapigiwa kura na kikao cha wilaya kwa pendekezo la msimamizi wa wilaya.

**510.7.** Maongozi na utaratibu wa kutolewa kwa vyeti vya uinjilisti utakuwa katika *Kitabu cha Maelezo ya Ustawi wa Kihuduma*

**511. Mhudumu wa Elimu ya Kikristo.** Mhudumu aliyepewa hati, aliyeajiriwa katika kiwango cha kihuduma katika mradi wa elimu ya Kikristo ya kanisa la mtaa anaweza kupewa kazi ya kuhudumu kama mhudumu wa elimu ya Kikristo.

**511.1**. Mtu ambaye, kabla ya miaka iliyotangulia mwaka wa 1985, alikuwa na hati au utume wa mhudumu wa elimu ya Kikristo, ataendelea kuwa katika msimamo mwema wa kanisa. Hata hivyo, wale wanaotaka kuanza kufuata matakwa ya huduma ya elimu ya Kikristo wanaweza kukamilisha matakwa ya kuwekwa wakfu kama shemasi kama hati yao ya huduma hii.

**512. Mhudumu wa Muziki.** Mshirika wa Kanisa la Mnazareti anayehisi kwamba ameitwa kwa huduma ya muziki anaweza kupewa utume wa mhudumu wa muziki na kikao cha wilaya kwa mwaka mmoja, mradi mtu huyo:

1. awe amependekezwa kwa kazi hiyo na halmashauri ya kanisa la mtaa ambalo yeye ni mshirika;
2. ataonyesha ushahidi wa neema, vipawa na kuwa na manufaa;
3. amekuwa na ujuzi wa muda usiopungua mwaka mmoja katika huduma za muziki;
4. awe ametimiza muda usiopungua mwaka mmoja wa mafunzo ya sauti za nyimbo chini ya mwalimu aliyehitimu na anaendelea na

utaratibu wa mafunzo yanayohitajika ya muziki au amekwisha kamilisha mafundisho hayo;

5. awe anajishughulisha mara kwa mara kama mhudumu wa muziki;
6. awe amekwisha hojiwa na kuchaguliwa kwa makini, chini ya uongozi wa kikao cha wilaya ambayo mtu huyo ana ushirika wa kanisa, kuhusu kuhitimu kwake kielimu na kiroho, kama anastahili na kufaa kwa kazi hiyo. (205.10)

**512.1.** Ni watu kama hao tu ambao wanadumisha kuajiriwa kwao katika huduma hii kwa wakati wao wote kama kazi yao na wajibu waliopewa, na wana hati za kuhitimu kama wahudumu, watakaohesabiwa kama wahudumu waliopewa wajibu.

**513. Mmishenari.** Mmishenari ni mtumishi au muumini anayehudumu chini ya usimamizi wa Misheni ya Ulimwengu. Mmishenari aliyeteuliwa na aliyepata hati ya kuhitimu kama mhudumu atahesabiwa kama mhudumu aliyepewa wajibu.

**514. Mchungaji.** Mchungaji ni kasisi au mhudumu aliyepewa cheti (hati ya kasisi) ambaye, chini ya mwito wa Mungu na watu Wake, anasimamia kanisa la mtaa. Mchungaji wa kanisa la mtaa ni mchungaji aliyepewa wajibu. (115, 213, 533.4)

**515.** Shughuli za msingi za mchungaji ni:

**515.1**. Kuomba.

**515.2**. Kuhubiri Neno.

**515.3.** Kuandaa watakatifu kwa kazi ya huduma.

**515.4.** Kuadhimisha sakramenti ya Meza ya Bwana na Ubatizo. Meza ya Bwana inafaa kuadhimishwa angalau mara moja baada ya miezi minne. Wachungaji wanahimizwa kuadhimisha tendo hili la neema mara kwa mara. Mhudumu mwenye cheti ambaye hajatimiza kwa ukamilifu matakwa ya kifungu cha 532.7 atapanga huduma hii pamoja na kasisi. Mhudumu aliyepewa cheti cha mtaa hatakuwa na ruhusa ya kuadhimisha sakramenti ya ubatizo au Meza ya Bwana. Kuangaziwa kwake kunafaa kutolewa kwa sababu ya kueneza Meza ya Bwana kwa watu wa nyumbani wasioenda kanisani, chini ya usimamizi wa mchungaji. (531.7, 700)

**515.5.** Kuwatunza watu kwa kuwatembelea, hasa wagonjwa na wenye mahitaji.

**515.6.** Kuwafariji wale wenye huzuni.

**515.7.** Kukaripia, kukemea, na kutia moyo, kwa uvumilivu wote wa usahihi wa mafunzo ya imani.

**515.8**. Kutafuta, kwa njia zote, kuokolewa kwa wenye dhambi, utakaso kamili kwa waumini, na kujengwa au kuimarishwa kwa watu wa Mungu katika imani takatifu (19)

**515.9.** Kupeana utunzaji unaohitajika kwa mambo yanayohusu kuhalalishwa kwa ndoa. Wachungaji watasimamia utakatifu wa ndoa ya Kikristo kupitia uangalifu wa makini kwa hali yao ya ndoa, kupitia njia zote za mawasiliano, kupitia kuwahudumia wengine, na kupitia ushauri wa ndoa kabla kuonana na kuhalalisha sherehe za ndoa. (538.19)

**515.10.** Kuimarisha mwito ambao watu huhisi wa huduma za Kikristo, na kuwafundisha watu kama hao wanapohisi mwito huo.

**515.11**. Kutimiza matarajio ya Mungu na Kanisa kwa kipindi cha mafunzo ya muda mrefu. (538.18)

**515.12.** Kulinda mwito wake kupitia miaka ya huduma, kuwa na maisha ya ibada binafsi ambayo yatainua nafsi yake kiroho, na, kama ameolewa, alinde uadilifu na bidii yake ya uhusiano huo wa ndoa.

**516.** Shughuli za kiutawala za mchungaji ni:

**516.1**. Kupokea watu kama washirika wa kanisa la mtaa kufuatana na kifungu cha 107 na 107.1.

**516.2.** Kuwa mwangalizi wa idara zote za kanisa la mtaa analohudumia.

**516.3**. Kuteua walimu wa Shule ya Jumapili/makundi ya kujisomea Biblia/makundi madogo kulingana na 145.8.

**516.4**. Kusomea washiriki Katiba ya Kanisa la Mnazareti na Kanuni Maalum ya Matendo ya Kikristo yaliyo katika vifungu vya 1-21, 28-33, vyote vikiwa pamoja, kila mwaka, au kuchapisha sehemu hiyo ya *Kitabu cha Mwongozo* na kuigawanya kwa washirika wa kanisa. (114)

**516.5.** Kusimamia kutayarishwa kwa taarifa zote za tarakimu kutoka kwa idara zote za kanisa la mtaa, na kuziwasilisha taarifa kama hizo mara moja kupitia kwa katibu hadi kwa kikao cha wilaya. (114.1)

**516.6.** Kutoa uongozi kwa ratiba za uinjilisti, elimu, kuabudu Mungu, na ustawi wa kanisa la mtaa, kulingana na wilaya na malengo na ratiba ya kuendeleza kanisa.

**516.7.** Kutoa taarifa kwenye mkutano wa mwaka wa kanisa, ikiwa ni pamoja na taarifa ya hali ya kanisa la mtaa na idara zake, na mukhtasari wa sehemu zenye mahitaji ya baadaye ya mafunzo na/au ustawi.

**516.8**. Kuteua kamati ya uchunguzi ya washirika watatu wa kanisa iwapo kutatokea mashtaka dhidi ya mshirika wa kanisa. (605)

**516.9**. Kuhakikisha kwamba pesa zote za Hazina ya Uinjilisti wa Ulimwengu zilizochangwa kupitia kwa jumuiya ya Huduma ya NMI zimepelekwa mara moja kwa mtunza hazina mkuu; na kwamba pesa zote za Hazina ya Huduma ya Wilaya zimepelekwa mara moja kwa mtunza hazina wa wilaya. (136.2)

**516.10.** Kuteua kwa halmashauri ya kanisa watu wote ambao ni waajiriwa wa kulipwa wa kanisa la mtaa, na kuwa msimamizi wao. (159.1-159.3)

**516.11.** Kutia sahihi, pamoja na katibu wa kanisa, hati zote za viwanja na nyumba, amana, kurudishwa kwa amana, mikataba, na hati nyingine za kisheria ambazo hazikutajwa katika *Kitabu cha Mwongozo.* (102.3, 103-104.3)

**516.12.** Kumjulisha mchungaji wa kanisa lililoko karibu wakati mshirika au rafiki wa kanisa la mtaa au mojawapo wa idara zake anapohamia mahali pengine katika wilaya hiyo ambapo uhusiano wa maana na kanisa la awali hauwezi kupendelewa, na kumpa anwani ya mshirika au rafiki huyo.

**516.13**. Kupanga na kuchanga pamoja na halmashauri ya kanisa, fedha za malengo ya makanisa yote zilizopewa kanisa la mtaa, ikiwa ni pamoja na Hazina ya Uinjilisti wa Ulimwengu, na malengo ya magawio ya yoyote yaliyoanzishwa na halmashauri za jimbo ay za kimataifa. (32.2, 130, 153)

**516.14.** Mchungaji anaweza, akiombwa na mshirika, kutoa uhamisho wa mshirika wa kanisa, Hati ya Sifa, au barua ya kumweka huru. (111-111.1, 112.2, 815-818)

**516.15.** Mchungaji atakuwa, kwa ajili ya wadhifa wake, msimamizi wa kanisa la mtaa, mwenyekiti wa halmashauri ya kanisa, mshirika wa halmashauri zote na kamati zote zilizochaguliwa na zinazostawi za kanisa analotumikia. Mchungaji anaweza kufikia kumbukumbu zote za kanisa la mtaa. (127, 145, 150, 151, 152.1)

**517**. Mchungaji atakuwa na haki ya kutoa maoni yake katika uteuzi wa viongozi wote wa idara zote za kanisa la mtaa, na katika shirika lolote la Mnazareti la ulezi wa watoto/shule (za awali mpaka sekondari).

**518.** Mchungaji na washirika wa karibu wa familia yake hawaruhusiwi kuliwekea kanisa jukumu la kifedha, kutumia pesa, kuhesabu pesa, au kuzuia kufikia kwa hazina ya fedha ya kanisa. Halmashauri ya kanisa au mkutano wa kanisa unaweza, kwa wingi wa kura, kuomba hatua ya kipekee kutoka kwa Halmashauri ya Wilaya na msimamizi wa wilaya. Kama msimamizi wa wilaya na wengi wa Halmashauri ya Wilaya wataidhinisha hali hiyo ya kipekee, msimamizi wa wilaya atatoa idhini iliyoandikwa ya ombi kwa katibu wa halmashauri ya wilaya, ambaye ataandika kumbukumbu ya hatua katika hifadhi za kanisa. Washirika wa karibu wa familia watajumuisha mke au mume wa mchungaji, watoto, dada au ndugu, au wazazi wa mchungaji. (129.1, 129.21-129.22)

**519.** Mchungaji daima ataonyesha heshima inayostahili kwa ushauri wa pamoja kutoka kwa msimamizi wa wilaya, na Halmashauri ya Wilaya. (225.2, 538.2)

**520.** Ikiwa mhudumu aliyepewa hati au aliyewekwa wakfu anayewasilisha vitambulisho vyake vya kuhitimu kutoka kwa dhehebu lingine, atatoa maombi yake ya kuwa mshirika wa kanisa la mtaa kabla ya wakati wa mkutano wa kikao cha wilaya, mchungaji anaweza kukataa maombi hayo hadi kwanza awe amepokea pendekezo la kufanya hivyo kutoka kwa Halmashauri ya Wilaya. (107, 228)

**521.** Kwa ajili ya kuwa katika huduma ya uchungaji, mchungaji atakuwa mtiifu kwa kikao cha wilaya, ambacho atatoa taarifa ya kila mwaka kwa kikao hicho pamoja na ushuhuda mfupi kuhusu maisha yake mwenyewe ya Kikristo. (205.3, 532.8, 538.9)

**522.** Mchungaji atakuwa mshirika wa kanisa ambalo yeye anahudumia mara tu atakapoanza huduma yake katika kanisa hilo; au ikiwa kuna kanisa zaidi ya moja chini yake, atakuwa mshirika wa kanisa atakalolichagua yeye mwenyewe. (538.8)

**523**. **Utumishi wa Uchungaji** unajumuisha huduma ya mchungaji au mchungaji msaidizi, ambaye anaweza kuwa na ujuzi maalum katika sehemu za huduma zinazotambuliwa na kuidhinishwa na vituo vinavyofaa vya usimamizi, hati na kukubaliwa. Kasisi aliyeitwa katika kiwango chochote kati ya viwango hivi vya uchungaji vinavyohusiana na kanisa anaweza kufikiriwa kama mhudumu alipewa wajibu.

**524**. **Mchungaji wa mpito.** Msimamizi wa wilaya atakuwa na uwezo wa kuteua mchungaji wa mpito, ambaye atatumika chini ya kanuni zifuatazo:

1. Mchungaji wa mpito anaweza kuwa mshirika Mnazareni ambaye ni kasisi anayetumika katika kazi nyingine, mhudumu wa mtaa au muumini mhudumu wa Kanisa la Mnazareti, mhudumu ambaye yuko katika utaratibu wa kuhama kutoka katika dhehebu lingine, au mhudumu ambaye ni wa dhehebu lingine.
2. Mchungaji wa mpito atateuliwa kwa muda ili kujaza nafasi ya mchungaji katika madhabahu na kutoa huduma ya kiroho, lakini hatakuwa na mamlaka ya kuadhimisha sakramenti au kufungisha ndoa isipokuwa awe alikuwa na mamlaka hayo hapo awali au ameyapata kwa sababu nyingine, na hatatekeleza wajibu wa mchungaji mbali na toa taarifa, isipokuwa awe amepata mamlaka ya kufanya hivyo kutoka kwa msimamizi wa wilaya.
3. Ushirika wa kanisa wa mchungaji wa mpito hautahamishwa katika kanisa analohudumia.

4. Mchungaji wa mpito atakuwa mshirika asiyepiga kura wa kikao cha wilaya isipokuwa akiwa ni mshirika anayepiga kura kwa sababu ya haki nyingine.
5. Mchungaji wa mpito anaweza kuondolewa au kubadilishwa wakati wowote na msimamizi wa wilaya.

**525. Mchungaji wa Ushirika Kushirikishwa kama Mzazi.** Mzee aliyewekwa wakfu au mhudumu aliyepewa hati na wilaya anayeongoza Ushirika wa Kushirikishwa kama Mzazi (UKM) atakuwa mhudumu msaidizi na anaweza kupewa kazi na wilaya kama "mchungaji wa Ushirika wa Kushirikishwa kama Mzazi"

**526. Mchungaji wa Muda.** Mzee aliyewekwa wakfu anaweza kuidhinishwa na kikao cha wilaya kama msimamizi wa wilaya wa muda (MWM) na kupendekezwa na msimamizi wa wilaya na Halmashauri ya Wilaya, na atatumika atakapoitwa na msimamizi wa wilaya na halmashauri ya kanisa. (212.1)

**527. Muinjilisti wa Nyimbo.** Muinjilisti wa nyimbo ni mshirika wa Kanisa la Mnazareti ambaye kusudi lake ni kujitolea kutumia sehemu kubwa ya wakati wake kwa huduma ya uinjilisti kupitia muziki. Muinjilisti ambaye ana hati za mhudumu na ambaye anahusika kamili katika huduma na ambaye wajibu wake ni uinjilisti, na ambaye haendelezi uhusiano wa kustaafu na kanisa au mojawapo wa idara au mashirika yake, atakuwa mhudumu aliye na wajibu

**527.1.** Mwongozo na utaratibu wa kupatiwa hati ya wajibu wa muinjilisti wa nyimbo unapatikana katika *"Kitabu cha Maelezo ya Ustawi wa Kihuduma"*

**528. Utumishi Maalum.** Mtumishi ambaye ana utumishi ambao haukupangwa atateuliwa kama mtumishi maalum, ikiwa utumishi huo utaidhinishwa na kikao cha wilaya, na ataorodheshwa na wilaya kama mhudumu aliye na wajibu. Watu waliopewa utumishi maalum watahitajika kuendeleza uhusiano na Kanisa la Mnazareti na watatoa taarifa kila mwaka katika maandishi kwa Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya na Halmashauri ya Hati za Wahudumu ya Wilaya au kwa Halmashauri ya Wahudumu ya Wilaya, jinsi uhusiano wao unavyondelea na Kanisa la Mnazareti.

**528.1**. Mtumishi aliyeajiriwa kazi ya kihuduma kama kiongozi katika shirika linalohusiana na kanisa ambalo linatumikia kanisa, au aliyeidhinishwa, baada ya kukaguliwa kwa makini na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya na kikao chake cha wilaya kutumika katika shirika la kielimu, kiinjilisti, au kimishenari ambalo halihusiani moja kwa moja na kanisa, anaweza kuteuliwa kwa utumishi maalum chini ya kifungu cha 538.13.

**528.2** Mtumishi aliye na wajibu wa muda mfupi au yuko katika likizo ya kutokuwa kazini anaweza kuteuliwa kwa huduma maalum na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya, baada ya kupendekezwa na msimamizi mkuu.

## IV. ELIMU KWA WAHUDUMU

### A. Misingi ya Elimu kwa Mhudumu Aliyewekwa Wakfu

**529.** Elimu ya kihuduma imeandaliwa ili kuwasaidia wahudumu walioitwa na Mungu ambao utumishi wao ni muhimu katika kupanua na kueneza ujumbe wa utakatifu katika sehemu mpya zilizo na nafasi ya uinjilisti. Tunatambua umuhimu wa kuelewa vyema kusudi la utume wetu "mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, kulingana na agizo la kwa Kanisa Lake katika Mathayo 28:19-20. Sehemu kubwa ya kujiandaa huko kimsingi itakuwa ni elimu ya thiolojia na ya kibiblia katika sifa yake, itakayoelekeza kuwekwa wakfu katika huduma ya Kanisa la Mnazareti. Halmashauri ya Mafunzo ya Kihuduma ya Wilaya itaamua mahali pa elimu na itafuatiliza jinsi gani kila mwanafunzi anavyoendelea katika utaratibu wa elimu anayojifunza ili kujiandaa kwa huduma.

**529.1.** Kanisa la Mnazareti linatayarisha vyuo vya elimu na ratiba tofauti katika sehemu mbalimbali za ulimwengu. Vifaa vilivyoko katika sehemu zingine za ulimwengu vinaruhusu kustawishwa kwa ratiba zaidi ya moja ili kutimizwa kwa misingi ya kielimu kwa huduma. Kila mwanafunzi anatarajiwa kutumia fursa ya mafunzo yanayofaa ambayo yanatolewa na Kanisa katika sehemu ya ulimwengu. Mahali pasipowezekana, Kanisa litatumia kila njia inayowezekana kumtayarisha kila mtu aliyeitwa na Mungu kwa huduma ya Kanisa. Wanafunzi wanaweza kutumia mfumo wa mafunzo yanayofaa, yaliyoelekezwa na kusimamiwa na Halmashauri ya Mafunzo ya Kihuduma ya Wilaya, au ratiba moja iliyoundwa na kutolewa na shirika la elimu ya juu la Mnazareti. Kila maelezo ya mafunzo yanayofaa yanastahili kuchukua viwango vilivyo sawa vya jumla kama vile ilivyoelezewa katika *Kitabu cha Kimataifa juu ya Viwango vya Kuendelea vya Maelezo ya Ustawi wa Kihuduma* na *Kitabu cha Maelezo ya Ustawi wa Kihuduma cha jimbo.*

**529.2.** Wakati mhudumu aliyepewa hati amekamilisha mfumo wa mafunzo unaohitajika kwa ufasaha, mtoaji wa elimu atapeana cheti cha kukamilika kwa mhudumu aliyepewa hati. Mhudumu aliyepewa hati atawasilisha cheti cha kukamilika kwa Halmashauri ya Mafunzo ya Kihuduma ya Wilaya inayohusika kukubaliwa kwa mapendekezo kwa

kikao cha wilaya kwa ajili ya kuhitimu kutoka kwa mfumo wa mafunzo yanatahitajika.

**529.3. Sehemu za Utaratibu wa Jumla wa Kujiandaa Kihuduma.** Ingawa utaratibu wa elimu mara nyingi unachukuliwa kuwa ni mipango ya masomo na yale yanayofundishwa wazo lake ni kubwa zaidi ya hayo. Tabia za anayefundisha, uhusiano wa wanafunzi na mwalimu, mazingira ya mafunzo, na ujuzi wa wanafunzi unaunganishwa na utaratibu wa masomo ili kuufanya uwe kamili. Hata hivyo, utaratibu wa kujiandaa kihuduma utajumuisha masomo machache ya maandalizi ya misingi ya kielimu kwa huduma. Tofauti za kiutamaduni na aina mbalimbali ya vifaa vya kielimu kutahitaji maelezo tofauti ya aina tofauti za utaratibu wa mafunzo. Hata hivyo, taratibu zote za kuandaa misingi ya kielimu kwa huduma ya ukasisi ambazo zinahitaji kuidhinishwa na Maendeleo ya Kasisi Ulimwenguni ni lazima zizingatiwe kwa makini hali ya masomo yale yatakayofundishwa, hali yake, msaada wake, na mazingira yake. Kusudi la kuwa na masomo yanayofaa ni kuhakikisha kwamba masomo yote yanajumuisha sehemu nne katika viwango mbalimbali na kwamba viwango hivyo vitawasaidia wahudumu kutimiza maneno ya utume wa Kanisa la Mnazareti kama vile ilivyokubaliwa na Halmashauri ya Wasimamizi Kuu kama inavyofuata:

"Utume wa Kanisa la Mnazareti ni kuwafanya mataifa yote kuwa wanafunzi"

"Lengo la msingi la Kanisa la Mnazareti ni kuendeleza Ufalme wa Mungu kwa kuhifadhi na kueneza utakatifu wa Kikristo kama ilivyoelezwa katika Maandiko"

"Shabaha muhimu za Kanisa la Mnazareti ni 'ushirika mtakatifu wa Kikristo, kuokolewa kwa wenye dhambi, utakaso kamili wa waumini, kujengwa kwao katika utakatifu, unyoofu na nguvu zilizodhihirika katika Kanisa la kale la Agano Jipya, pamoja na kuhubiriwa Injili kwa kila kiumbe'" (19).

Utaratibu wa mafunzo umeelezwa katika mgawo ufuatao:

- *Yaliyomo* – Ufahamu wa yaliyomo katika Agano la Kale na Agano Jipya, thiolojia ya imani ya Kikristo, historia na misheni ya Kanisa ni muhimu kwa huduma. Ufahamu wa jinsi ya kutafsiri Maandiko, mafundisho ya utakatifu, na utofauti wetu wa Kiwesley, na historia na maongozi ya Kanisa la Mnazareti ni lazima yajumuishwe katika utaratibu wa mafunzo.
- *Ustadi* – Uwezo wa kuwasiliana kwa maneno na maandishi; usimamizi na uongozi; fedha (pesa); na kuwaza kiutafiti pia ni muhimu kwa huduma. Pamoja na elimu ya kawaida inayohusiana na sehemu hizo, masomo ya kuimarisha kuhubiri, kutunza kiuchungaji, na kushauri, ibada, uinjilisti wenye matokeo, elimu ya Kikristo,

pamoja na usimamizi wa kanisa ni lazima ujumuishwe katika mafunzo kwa wahudumu wa kanisa.

- *Sifa/tabia* – Kukua kibinafsi katika sifa au tabia, maadili, hali ya kiroho, uhusiano wa kibinafsi na kijamii ni muhimu kwa huduma. Masomo yanayohusiana na sehemu za maadili ya Kikristo, kujenga kiroho, ustawi wa binadamu, nafsi ya mhudumu, ndoa na jamii yanapaswa kuwa sehemu ya mafunzo ya mhudumu.
- *Yanayodhihirisha maana* – Mhudumu ni lazima afahamu historia, mazingira ya kijamii na utamaduni wa sehemu kanisa linapohudumu, maoni na hali ya sasa ya wakazi wake. Masomo yanayohusiana na elimu ya mambo ya binadamu, hasa mapokeo, dini na desturi za watu, mambo ya jumuiya ya watu, mawasiliano ya tamaduni tofauti, na misheni ni lazima yawe katika utaratibu wa mafunzo kwa wahudumu.

**529.4.** Matayarisho kwa huduma ya ukasisi yaliyofanyika katika shule zisizo za Mnazareti au chini ya usimamizi usio wa Mnazareti yatachunguzwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mafunzo wa Kihuduma kuambatana na utaratibu wa matakwa ya masomo ulioelezwa katika *Kitabu cha Maelezo ya Ustawi wa Kihuduma* kilichotayarishwa na jimbo/kundi la lugha

**529.5.** Masomo yote, matakwa ya kielimu, na kanuni rasmi za uongozi zitaorodheshwa katika Kitabu cha Ustawi wa Kihuduma kilichotayarishwa na jimbo/kundi la lugha likishirikiana na Huduma ya Ustawi ya Uchungaji Ulimwenguni. *Kitabu hiki cha Ustawi wa Kihuduma* cha jimbo na masahihisho yatakayohitajika, kitaidhinishwa na Kamati ya Ushauri wa Utaratibu wa Mafunzo na kukubaliwa na Huduma ya Ustawi ya Uchungaji Ulimwenguni, Halmashauri Kuu, na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu. *Kitabu cha Ustawi wa Kihuduma* kitakuwa na makubaliano na *Kitabu cha Mwongozo na Kitabu cha Kimataifa cha Ustawi wa Viwango vya Maelezo ya Ustawi wa Kihuduma*, kinachotolewa na Huduma za Uchungaji kwa kushirikiana na Kamati ya Ushauri wa Mafunzo ya Kimataifa. Kamati ya Ushauri wa Mafunzo ya Kimataifa inateuliwa na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu.

**529.6.** Mara tu mhudumu anapotimiza matarajio ya misingi ya kielimu kwa huduma, ataendelea na utaratibu wa kujifunza katika maisha yake yote ili kuimarisha na kukuza huduma ambayo Mungu alimuitia. Matarajio yanayohitajika ni masaa 20 ya kujifunza maisha yake yote kila mwaka au kiasi kama hicho kilichowekwa na jimbo/kundi la lugha na kuelezwa katika Kitabu cha Ustawi wa Kihuduma cha jimbo. Makasisi wote wanaohudumu na wasiohudumu na watatoa ripoti ya vile wanavyoendelea katika mpango

huo kama sehemu ya taarifa yao kwenye kikao cha wilaya. Taarifa hizo za nanma mhudumu anavyoendelea na mafunzo zitatumiwa katika ukaguzi wa uchungaji na katika utaratibu wa kumwita mchungaji. *Kitabu cha Maelezo ya Ustawi wa Kihuduma* cha jimbo/kundi la lugha kitakuwa na maelezo ya jinsi ya ripoti hizo zitakavyotayarishwa na kuandikwa katika vyeti vya kufuzu.

**529.7**. Kukosa kukamilisha matarajio ya kujifunza ya maisha yote kwa zaidi ya miaka miwili inayofuata yatasababisha kasisi kukutana na Halmashauri ya Wilaya ya Mafunzo ya Kihuduma katika mkutano wao wa mara kwa mara. Halmashauri ya Wilaya ya Mafunzo ya Kihuduma itatoa mwongozo kwa mhudumu wa kukamilisha mafunzo ya maisha yanayohitajika. (115, 123, 515.11, 538.18)

## B. Marekebisho ya Kitamaduni ya Misingi ya Elimu kwa Huduma ya Kuwekwa Wakfu

**530.** Mukhtadha wa tamaduni tofauti ulimwenguni kote husababisha utaratibu mmoja kutofaa katika sehemu zote za dunia. Kila jimbo la ulimwenguni litatayarisha matarajio maalum ya utaratibu, likitoa misingi ya elimu kwa huduma katika njia ambayo inaonyesha raslimali na matarajio ya sehemu hiyo ya dunia. Idhini ya Kamati ya Ushauri wa Mafunzo ya Kimataifa, Halmashauri Kuu, na Halmalshauri ya Wasimamizi Wakuu itahitajika kabla ya kuanzisha ratiba iliyoundwa kulingana na jimbo. Hata ndani ya majimbo ya ulimwengu kuna matarajio mbalimbali ya kitamaduni na raslimali. Kwa sababu ya hiyo, umakini wa kitamaduni na uthabiti utabainisha mahitaji ya kijimbo kwa ajili ya misingi ya elimu kwa huduma, ambayo yataongozwa na kusimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mafunzo Kihuduma. Marekebisho ya kitamaduni ya kila ratiba ya jimbo ya kutoa misingi ya elimu kwa huduma yataidhinishwa na Ustawi wa Mhudumu wa Dunia na Kamati ya Ushauri wa Masomo ya Kimataifa katika kushauriana na msimamizi wa elimu wa jimbo. (529.5)

**530.1** Masomo yanayohitajika kujifunza, pamoja na utaratibu unaohitajika kuhusu kukamilishwa kwao kwa wale wanaotafuta hati ya ukasisi na ushemasi au kupata hati kama ya muinjilisti wa nyimbo na muumini mhudumu, yanapatikana katika *Kitabu cha Maelezo ya Ustawi wa Kihuduma cha jimbo.*

**530.2.** Masomo yote yanayohitajika kujifunza yatasimamiwa na *Kitabu cha Maelezo ya Ustawi wa Kihuduma* cha jimbo. (529.2-529.3, 529.5)

# V. HATI ZA KUHITIMU NA KANUNI ZA KIHUDUMA

## A. Mhudumu wa Mtaa

**531.** Mhudumu wa mtaa ni muumini wa Kanisa la Mnazareti ambaye halmashauri ya kanisa la mtaa imempa hati ya huduma, chini ya maagizo ya mchungaji, na kadri nafasi inavyopatikana, hivyo hutoa nafasi ya maonyesho, kuajiriwa, na kustawishwa kwa vipawa vya kihuduma na mazoezi yake. Kwa njia hiyo anaingia katika hatua ya mafunzo ya kuendelea maisha yote.

**531.1**. Mshirika yeyote wa Kanisa la Mnazareti anayehisi mwito wa Mungu kuhubiri au kuendelea na huduma kwa maisha yake kupitia kwa kanisa anaweza kupewa hati kama mhudumu wa mtaa kwa mwaka mmoja na halmashauri ya kanisa la mtaa ambalo lina kasisi anayehudumu kama mchungaji, kwa pendekezo la mchungaji; au na halmashauri ya kanisa la mtaa lisilo na kasisi anayehudumu kama mchungaji ikiwa utoaji wa hati umependekezwa na mchungaji na kuidhinishwa na msimamizi wa wilaya. Anayetaka hati ya huduma ni lazima kwanza achunguzwe kuhusiana na ujuzi wake wa wokovu, ufahamu wa mafundisho ya Biblia, na utaratibu wa kanisa; pia ni lazima aonyeshe kwa vitendo kwamba mwito wake una neema, vipawa na manufaa. Atapitia uchunguzi wa maisha yake unaosimamiwa na kanisa la mtaa. Mhudumu wa mtaa atatoa taarifa kwa kanisa la mtaa wakati wa mkutano wake wa mwaka. (113.9, 129.12, 211.12)

**531.2.** Halmashauri ya kanisa itatoa hati kwa kila mhudumu wa mtaa iliyotiwa sahihi na mchungaji pamoja na katibu wa halmashauri ya kanisa. Mahali ambapo kanisa linahudumiwa na mchungaji ambaye hana hati ya wilaya, mtu huyo anaweza kupewa hati ya mhudumu wa mtaa, au kutolewa upya kwa hati hiyo, na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya kufuatia pendekezo la msimamizi wa wilaya. (211.12, 225.13)

**531.3.** Hati ya mhudumu wa mtaa inaweza kutolewa upya na halmashauri ya kanisa la mtaa likiwa na kasisi anayehudumu kama mchungaji, kwa pendekezo la mchungaji; au na halmashauri ya kanisa la mtaa lisilo na kasisi, anayetumika kama mchungaji, mradi kutolewa upya kwa hati hiyo kuwe kumependekezwa na mchungaji na kuidhinishwa na msimamizi wa wilaya. (129.12, 2211.12)

**531.4.** Wahudumu wa mtaa watahudhuria masomo yanayohitajika ya wahudumu chini ya uongozi wa Halmashauri ya Mafunzo ya Kihuduma ya Wilaya. Hati ya mhudumu wa mtaa haiwezi kutolewa upya baada ya miaka miwili bila ya idhini iliyoandikwa ya msimamizi wa wilaya ikiwa

mhudumu wa mtaa hajakamilisha angalau masomo mawili ya mafunzo yanayohitajika kwa wahudumu.

**531.5.** Mhudumu wa mtaa, akiwa ametumika katika nafasi hiyo kwa kipindi cha muda usiopungua mwaka mmoja, na amekamilisha masomo inavyostahili masomo, anaweza kupendekezwa na halmashauri ya kanisa kwa kikao cha wilaya ili apewe hati ya wilaya; lakini, iwapo hatakubaliwa, ataendelea na wadhifa wake wa kwanza kwa kanisa la mtaa. (129.12, 529, 532.1)

**531.6.** Mhudumu wa mtaa ambaye ameteuliwa kama mchungaji wa mpito ni lazima aidhinishwe na Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu, iwapo ataendelea na huduma hiyo baada ya mkutano wa kikao cha wilaya utakaofuatia kuteuliwa kwake. (212, 231.5, 524)

**531.7.** Mhudumu wa mtaa haruhusiwi kusimamia kuadhimishwa kwa sakramenti ya ubatizo na Meza ya Bwana, wala kufungisha ndoa. (212, 231.5, 524)

### B. Mhudumu Aliyepewa Hati

**532.** Mhudumu aliyepewa hati ni yule ambaye mwito wake wa kuhudumu na vipawa vyake vimetambuliwa na kikao cha wilaya kwa kupewa hati ya kuhudumu. Kikao cha wilaya kinamuidhinisha na kumteua mhudumu kwa fursa kubwa zaidi ya kuhudumu na kwa haki zaidi na kuwajibika kuliko zile za mhudumu wa mtaa, kama hatua ya kuweza kuwekwa wakfu kama kasisi au shemasi. Hati ya kuhudumu ya wilaya itakuwa pamoja na taarifa ya kuonyesha ikiwa mhudumu anajiandaa kwa kuwekwa wakfu kama kasisi au shemasi au mwenye hati ya wilaya isioyoelekeza kwa kuwekwa wakfu. (532.7)

**532.1.** Wakati washirika wa Kanisa la Mnazareti wanakubali mwito wa maisha wa huduma, wanaweza kupewa hati kama wahuduma na kikao cha wilaya mradi wawe:

1. wapewa hati ya mhudumu wa mtaa kwa mwaka mmoja;
2. wamekamilisha robo ya masomo yanayohitajika kwa wahudumu, na wanaweza kuonyesha shukrani, ufahamu, na matumizi ya *Kitabu cha Mwongozo* na historia ya Kanisa la Mnazareti, na imani ya utakatifu, kwa kukamilisha kamili sehemu zinazohusiana za masomo yanayohitajika;
3. wamependekezwa kufanya kazi hiyo na halmashauri ya kanisa la mtaa ambalo wao ni washirika, na pendekezo hilo liambatanishwe na Maombi ya Kutaka Hati ya Kuhudumu;
4. wameonyesha ushahidi wa neema, vipawa na manufaa;

5. wamechunguzwa kwa makini, chini ya uongozi wa kikao cha wilaya ambayo ushirika wa kanisa lao uko, kuhusu maisha yao ya kiroho, elimu, na mambo mengine yanayofaa kwa kazi hiyo ikiwa ni pamoja na uchunguzi wa kina unaofaa kama vile ilivyoamuliwa na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya;
6. wameweka ahadi ya kuendelea na masomo ambayo yameelezwa kwa ajili ya wahudumu walio na hati na wanaotaka kuwekwa wakfu;
7. iwapo walikuwa na vizuizi vyovyote ambavyo vilikuwa vimewekwa na kikao cha wilaya, viondolewe kwa maandishi na msimamizi wa wilaya na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya ambayo vizuizi hivyo vilikuwa vimewekwa; na kwamba hali ya uhusiano wao wa ndoa haiwafanyi wawe hawastahili kupata hati ya wilaya na kuwekwa wakfu; na
8. iwapo kulitokea talaka, pendekezo la Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya pamoja na hati za kuthibitisha ukweli wa jambo hilo zitapelekwa kwa Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu, ambayo inaweza kuondoa kizuizi hicho ili aweze kupata hati au kuwekwa wakfu.

Mhudumu anaweza kuwa amekamilisha kiasi sawa cha robo ya masomo yanayohitajika katika Kanisa la Mnazareti. Hali ya kukubaliwa ya mahitaji haya inaweza kufanywa na Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya au Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya mradi mtahiniwa anachunga kanisa lililoratibiwa na ameandikishwa katika ratiba masomo iliyoidhinishwa, na mradi mtahiniwa anatimiza kiasi cha masomo yanayohijika na *Kitabu cha Mwongozo* kila mwaka ili kufanywa upya kwa hati, na mradi msimamizi wa wilaya ameidhinisha makubaliano.

Katika hali ambayo uchunguzi utaonyesha tabia za uhalifu kabla ya wokovu wa mtu, jambo hili lisitafsiriwe na Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya au Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya kama kumtenga anayeomba hati kutoka kwa huduma ya kupewa hati, isipokuwa chini ya maelezo ya kifungu cha 540.9. (129.14, 207.6, 531.5)

**532.2.** Wahudumu wengine waliopewa vyeti kutoka madhehebu mengine ya kiinjili, ambao wangependa kujiunga na Kanisa la Mnazareti, wanaweza kupewa hati ya kuhudumu na kikao cha wilaya, mradi tu walete vitambulisho walivyokuwa wamepewa na madhehebu ambayo kwanza walikuwa washirika wake; na pia itawabidi wawe:

1. wamekamilisha robo ya masomo yanayohitajika kwa wahudumu, na wanaweza kuonyesha shukrani, ufahamu, na matumizi ya *Kitabu cha Mwongozo* na historia ya Kanisa la Mnazareti, na imani ya utakatifu,

kwa kukamilisha kamili sehemu zinazohusiana za masomo yanayohitajika;
2. wamependekezwa na halmashauri ya Kanisa la mtaa la Mnazareti ambalo wao ni washirika wake;
3. wawe wameonyesha ushahidi wa neema, vipawa na manufaa;
4. wamechunguzwa kwa makini chini ya uongozi wa kikao cha wilaya juu ya maisha yao ya kiroho, elimu yao, na uwezo wao wa kazi ya aina hiyo;
5. wameahidi kuanza mara moja masomo ambayo yanatakiwa kwa wahudumu waliopewa hati na wale wanaotaka kuwekwa wakfu;
6. wamekuwa na sifa zisizostahili, ambazo zinaweza kuwa zimewekwa wazi na kikao cha wilaya au zinazokaribiana, wametolewa kwa maelezo ya maandishi na msimamizi wa wilaya au msaidizi wake na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya au ofisi inayolingana ya wilaya ambayo sifa zisizostahili ziliwekwa wazi; na mradi tu baadaye kwamba uhusiano wao wa ndoa hautawafanya wakose hati ya wilaya; na;
7. iwapo kulitokea pendekezo la Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya pamoja na hati za kuthibitisha ukweli wa jambo hilo zitapelekwa kwa Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu, ambayo inaweza kuondoa kizuizi hicho ili aweze kupata hati au kuwekwa wakfu. (532.1)

**532.3.** Hati ya Mhudumu itamalizika mwisho wa mkutano wa kikao cha wilaya. Inaweza kutolewa upya kwa kura za kikao cha wilaya, mradi:
1. mtu anayetaka hati yake itolewe upya atatuma maombi kwa kikao cha wilaya, akiwa amejaza fomu ya maombi kwa uangalifu; na
2. mtu huyo awe amemaliza inavyostahili masomo mawili; na
3. mtu huyo awe amependekezwa kupewa upya hati ya kuhudumu na halmashauri ya kanisa la mtaa ambalo yeye ni mshirika, baada ya kuteuliwa na mchungaji.

Hata hivyo, iwapo hatakuwa amekamilisha masomo yanayotakiwa, hati inaweza tu kutolewa upya na kikao cha wilaya ikiwa ataeleza kwa maandishi sababu ya kushindwa kwake kutimiza matakwa hayo. Maelezo hayo ni lazima yairidhishe Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya au Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya na kuidhinishwa na msimamizi mkuu wa sehemu hiyo. Kikao cha wilaya kinaweza, kwa sababu fulani au kikiona ni vyema, kukataa kutoa upya hati ya mhudumu.

Wahudumu waliopewa hati ya wilaya ambao wamehitimu kutoka katika mafunzo na amewekwa katika uhusiano wa kustaafu na kikao cha wilaya,

wanaweza, kwa pendekezo la Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya, kupewa upya hati ya kuhudumu bila kujaza Fomu ya Maombi ya Hati ya Mhudumu. (205.4)

**532.4.** Ili wahitimu kuwekwa wakfu, wahusika ni lazima wakamilishe inavyohitajika utaratibu wa mafunzo kwa wahudumu katika kipindi cha miaka kumi tangu walipopewa hati ya wilaya mara ya kwanza. Kuepushwa kwa matakwa hayo, kwa sababu ya mambo yasiyo ya kawaida, ni lazima ipendekezwe kwa kikao cha wilaya, ikiambatana na muda wa mwisho wa kutimiza matakwa hayo, na Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya, na litahitaji kuidhinishwa na msimamizi mkuu wa sehemu hiyo.

Mhudumu mwenye hati ambaye hafuatilii kuwekwa wakfu au ambaye amekataliwa kwa kushindwa kumaliza mafunzo katika kipindi kilichowekwa, anaweza kupewa upya hati ya wilaya kwa pendekezo la Halmashauri na Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya au Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya ya Wahudumu. Pendekezo hili linaambatana na mhudumu akiwa amehitimu kutoka kwa masomo yanayohitajika ya mwaka uliopita.

**532.5.** Kwa wahudumu waliopewa hati ambao wanatumika kama wachungaji, pendekezo la kupewa hati upya litatolewa na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya. Kwa wahudumu wa mtaa ambao wanatumika kama wachungaji, pendekezo la kupewa hati ya kuhudumu itafanywa na Halmashauri ya Wilaya. (225.13)

**532.6.** Msimamizi mkuu wa sehemu hiyo atatoa kwa kila mhudumu aliyepewa hati, hati ya kuhudumu, iliyotiwa sahihi na mzimamizi mkuu wa sehemu hiyo, msimamizi wa wilaya, na katibu wa wilaya.

**532.7.** Wahudumu waliopewa hati watapewa mamlaka ya kuhubiri neno na/au kutumia vipawa vyao na neema katika huduma mbalimbali za Mwili wa Kristo. Zaidi ya yote, mradi tu watumike katika huduma walizopewa ambazo zinatambuliwa na wilaya ambazo ushirika wao wa kihuduma uko hapo, wahudumu waliopewa hati watapewa pia mamlaka ya kuadhimisha sakramenti ya ubatizo na Meza ya Bwana katika makongamano yao, na kufunganisha ndoa mahali ambapo sheria ya nchi inaruhusu. (511-512, 515, 515.4, 523, 532.8, 533-533.2, 534.2, 700, 701, 705)

**532.8.** Wahudumu wote waliopewa hati watakuwa na ushirika wao wa kihuduma katika kikao cha wilaya kwa wilaya ambayo ushirika wao wa kanisa upo, na watatoa taarifa kila mwaka kwa mwili huu. Ripoti zinaweza kutolewa kwenye fomu inayofaa ya mwaka au Fomu ya Maombi ya Wilaya kwa Hati ya Mhudumu kama inafanywa upya. (201, 205.3, 521)

**532.9.** Iwapo mhudumu aliyepewa hati amejiunga na ushirika au huduma ya dhehebu lingine kando Kanisa la Mnazareti au kujiunga na kujihusisha katika huduma ingine ya Kikristo bila idhini ya Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya yake au bila idhini iliyoandikwa ya Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu, au ataondolewa mara moja kutoka kwa huduma na ushirika wa Kanisa la Mnazareti. Kwa kumbukumbu, kikao cha wilaya kitaweka kumbukumbu ya maneno yafuatayo: "Ameondolewa kutoka katika ushirika na huduma ya Kanisa la Mnazareti kwa kujiunga na dhehebu lingine." (107, 112)

## C. Shemasi

**533.** Shemasi ni mhudumu ambaye kuitwa kwake na Mungu katika huduma ya Kikristo, vipawa na manufaa ya huduma hiyo vimeonekana na kuendelezwa kwa masomo yanayohitajiwa na ujuzi, ambaye ametengwa kwa huduma ya Kristo kwa kupigiwa kura na kikao cha wilaya na kwa tendo takatifu la kuwekwa wakfu, na ambaye amepewa mamlaka kutenda aina fulani za huduma ya Kikristo.

**533.1.** Shemasi hashuhudii kuwa na mwito maalum wa kuhubiri. Kanisa linatambua, kwa kufuata Maandiko na ujuzi, kwamba Mungu anawaita watu kwa huduma za maisha ambao si wahubiri, na kuamini kwamba watu wanaoitwa kwa huduma hizi ni lazima watambuliwe na kukubaliwa na kanisa na lazima wafikie mambo yanayohitajika na wapewe majukumu yaliyowekwa na kanisa. Huu ni utaratibu wa kudumu wa huduma.

**533.2.** Shemasi ni lazima atimize matakwa ya utaratibu wa elimu, aonyeshe vipawa na neema inayofaa, na pia atambuliwe na kukubaliwa na kanisa. Shemasi atapewa mamlaka ya kuadhimisha sakramenti ya ubatizo na Meza ya Bwana, na kufungisha ndoa mahali sheria ya nchi inaruhusu, na kwa wakati fulani kuongoza ibada na kuhubiri. Inaeleweka kwamba Bwana na kanisa wanaweza kutumia vipawa vya mtu na neema yake katika huduma mbalimbali. Kama ishara ya utumishi katika huduma katika Mwili wa Kristo, shemasi pia anaweza kutumia vipawa na majukumu yake nje ya mashirika au idara za kanisa. (515.4, 515.9)

**533.3.** Kasisi anaweza kutangaza mwito wa Mungu kwa huduma hii. Mtu huyo anaweza kuwa na hati ya wilaya, na amekuwa na hati wakati mmoja kwa miaka isiyopungua mitatu ikifuatana. Zaidi, mtu huyo amependekezwa kwa kufanywa upya kwa hati ya wilaya na halmashauri ya kanisa ya kanisa la mtaa ambalo ushirika wake uko pale au na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya. Zaidi mtu huyo:

1. ametimiza matakwa yote ya kanisa hilo,

2. amekamilisha masomo yanayotahitajika yaliyopendekezwa kwa wahudumu waliopewa hati na watahiniwa wa kuwekwa wakfu kama kasisi, na
3. amefikiwa kwa makini na kupendekezwa na Halmashauri ya Hati ya Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya au Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya kwa kikao kikuu.

Mtu huyo anaweza kuchaguliwa kwa utaratibu wa shemasi na theluthi mbili za kura ya kikao kikuu; mradi awe amekuwa mhudumu kwa wadhifa wake kwa miaka isiyopungua mitatu ikifuatana; na mradi zaidi awe mtu ambaye anahuduma kwa wakati huu katika huduma aliyopewa. Kwa jukumu ambalo ni la muda mfupi, itatakiwa kueleweka kwamba kutahitajika kuwa na ongezeko la miaka inayofuatana katika huduma, kulingana na kiwango cha kuhusika katika huduma ya kanisa la mtaa, na kwamba ushuhuda wao na utumishi unadhihirisha kwmaba mwito wao kwa huduma ni wa kwanza kwa majukumu mengine yote. Zaidi, sifa zozote zisizohitimu ambazo zinaweza kuwa zimethibitishwa na kikao cha wilaya ziwe zimeondolewa kwa maandisi na msimamizi wa wilaya na Halmashauri ya Wilaya ya wilaya iliyotajwa; na mradi zaidi kwamba uhusiano wake wa ndoa hautamzuia kuwekwa wakfu. 205.6, 320, 529)

**533.4.** Iwapo katika kuendeleza huduma yake, shemasi aliyewekwa wakfu atapata mwito wa kujiunga na huduma ya kuhubiri, anaweza kuwekwa wakfu kuwa kasisi baada ya kukamilisha mahitaji hayo na kurudisha hati za ushemasi.

### D. Kasisi

**534.** Kasisi ni mhudumu ambaye mwito wake wa Mungu wa kuhubiri, vipawa na manufaa yake yamedhihirika na kuendelezwa kwa masomo yanayofaa na ujuzi, na ambaye ameteuliwa kwa huduma ya Kristo kupitia kwa kanisa lake kwa kura ya kikao cha wilaya, na kwa utaratibu wa kutawazwa, na kwa hivyo ana idhini kamili ya kuendesha shughuli zote za huduma ya Kikristo.

**534.1.** Tunatambua namna moja tu ya huduma ya kuhubiri - ile ya kasisi. Hii ni namna ya huduma ya kudumu katika kanisa. Kasisi anapaswa kuongoza vyema kanisani, kuhubiri Neno, kuadhimisha sakramenti ya ubatizo na Meza ya Bwana, na kuhalalisha ndoa, yote katika jina, na chini ya Yesu Kristo, Mkuu wa Kanisa. (31, 514-515.3, 515.4, 515.9, 538.15)

**534.2.** Kanisa linatarajia kwamba mtu aliyeitwa kwa kazi hii rasmi ya huduma anapaswa kuwa wakili wa Neno na kujitoa nguvu zake na maisha yake katika kulitangaza.

**534.3.** Kasisi hutangaza mwito wa Mungu kwa huduma hii. Mtu huyo anaweza kuwa na hati ya wilaya kwa wakati wa sasa, na amekuwa kwa wakati mmoja na hati kwa miaka isiyopungua mitatu mfululizo. Zaidi, mtu huyo amependekezwa kupewa upya hati ya wilaya na halmashauri ya kanisa ya kanisa la mtaa ambalo ushirika wake uko au na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya. Zaidi ya mtu huyo:

1. ametimiza matakwa yote ya kanisa kwa ajili hiyo,
2. amekamilisha masomo yanayotakiwa kwa mhudumu aliyepewa hati na anayetaka kuwekwa wakfu kama kasisi, na
3. ambaye amependekezwa na kuelezewa na Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya au Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya ya kikao cha wilaya.

Mtu huyo anaweza kuchaguliwa kwenye wadhifa wa kasisi kwa theluthi mbili ya kura za kikao cha wilaya. Ili kuweza kuchaguliwa kwa uchaguzi, mtu huyo lazima awe alikuwa na kazi ya kuhudumu kwa miaka isiyopungua mitatu mfululizo, na mtu huyo awe anahudumu katika huduma aliyopewa. Kwa kazi ya muda mfaupi, inastahili kueleweka kwamba kutakuwa na ongezeko la miaka mfululizo ya wakati wa utumishi, kulingana na kiwango cha kuhusika katika huduma ya kanisa la mtaa, na kwamba ushuhuda wao na utumishi zinathihirisha kwamba mwito wao wa huduma ni wa kwanza juu ya shughuli zingine zote. Zaidi, sifa yoyote isiyofaa ambayo inaweza kudhihirishwa na kikao cha wilaya lazima iondolewe kwa maandishi na msimamizi wa wilaya na Halmashauri ya Ushauri Wilaya wa wilaya ambayo sifa isiyofaa ilidhihirishwa kabla ya mhudumu kukubaliwa kwa uchaguzi wa utaratibu wa ukasisi. Zaidi, uhusiano wa mtu huyo wa ndoa usiwe kizuizi cha kuwekwa wakfu. (205.6, 320, 529)

### E. Kutambuliwa kwa Hati za Kuhitimu

**535.** Wahudumu waliowekwa wakfu kutoka katika madhehebu mengine, wanaotaka kujiunga na Kanisa la Mnazareti na wanaowasilisha hati zao za kuwekwa wakfu, pengine kuwekwa wakfu kwao kunaweza kutambuliwa na kikao cha wilaya, baada ya kufanyiwa uchunguzi na Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya kuhusiana na tabia yao, ujuzi wao, na mafundisho ya kidini, mradi wawe

1. wamedhihirisha shukrani, maonyesho na matumizi ya *Kitabu cha Mwongozo* na historia ya Kanisa la Mnazareti na imani ya utakatifu kwa kukamilisha vilivyo sehemu zinazohusiana na masomo yanayohitajika;

2. wajaze na kupeleka kwa kikao cha wilaya fomu ya Maswali kwa watu wanaotaka Kuwekwa Wakfu na wale wanaotaka Hati zao Zitambuliwe; na
3. wametimiza masharti yote yanayotakiwa kwa wanaotaka kuwekwa wakfu kama ilivyoelezwa katika vifungu vya 533-533.3 au 534-534.3; na
4. mradi zaidi kwamba mtu huyo awe anatumika katika huduma aliyopewa. (205.7, 228, 529, 532.2)

**535.1.** Msimamizi mkuu anayehusika atatoa hati ya kutambuliwa kwa kasisi aliyetambuliwa iliyotiwa sahihi na yeye mwenyewe, msimamizi wa wilaya na katibu wa wilaya. (538.6)

**535.2.** Wakati hati ya mhudumu kutoka kanisa lingine itakapotambuliwa, hati hiyo itarudishwa kwa mhudumu huyo ikiwa imeandikwa au kupigwa muhuri ulioandikwa kama ifuatavyo:

Imekubaliwa na Kikao cha Wilaya ya (jina la wilaya) ______________ ya Kanisa la Mnazareti tarehe ____________, mwezi wa_______ mwaka wa ________ kama msingi wa hati mpya ya kuhitimu.

__________________________, Msimamizi Mkuu
__________________________, Msimamizi wa Wilaya
__________________________, Katibu wa Wilaya

## F. Mhudumu Aliyestaafu

**536.** Mhudumu aliyestaafu ni yule ambaye amewekwa katika uhusiano wa kustaafu na kikao cha wilaya ambayo ushirika wake kiuhuduma upo, kwa pendekezo la Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya. Mabadiliko yoyote katika uhusiano huo ni lazima yakubaliwe na Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya au Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya.

**536.1.** Kustaafu hakuwezi kumfanya mtu aache kabisa kazi ya kihuduma au kusababisha kuondolewa katika ushirika wa kikao cha wilaya. Mhudumu ambaye alikuwa akitumika katika 'wajibu" wakati wa kutuma ombi la uhusiano wa kustaafu au katika umri wa kawaida wa kustaafu anaweza kuwekwa katika uhusiano wa "mstaafu aliye na wajibu". Mhudumu "mstaafu aliye na wajibu" ni mshirika wa kikao cha wilaya. Hata hivyo, mhudumu ambaye "hakuwa na wajibu" katika aidha hali zilizo hapo juu anaweza kustaafu akiwa na uhusiano wa "mstaafu asiye na wajibu". Mhudumu "mstaafu asiye na wajibu" si mshirika wa kikao cha wilaya (201, 538.9)

**536.2.** Wahudumu walistaafu (walio na wajibu na wasio na wajibu) bado wako na wajibu wa kutoa taarifa kila mwaka kwa kikao cha wilaya.

Kwa wahudumu waliostaafu ambao hawawezi kutoa taarifa kwa ajili ya upungufu fulani kuliko wanavyoweza, kikao cha wilaya kinaweza, kwa pendekezo la Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya, kuwapa hali ya "kumradhi" mhudumu huyo, hivyo ataendelea kutimiza majukumu ya kutoa taarifa kila mwaka. (538.9)

## G. Kuhama kwa Wahudumu

**537.** Iwapo kasisi aliyepewa hati anapenda kuhamia wilaya nyingine, kuhamishwa kwa ushirika wa kihuduma kunaweza kukubaliwa kwa kura ya kikao cha wilaya, au Halmashauri ya Wilaya katika muda wa vikao, yeye ni mshirika. Uhamisho huo unaweza kupokelewa na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya kabla ya kukutana kwa kikao cha wilaya, na kumpa mhudumu huyo haki zote na manufaa ya ushirika katika wilaya ambayo inampokea kwa idhini ya mwisho ya Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya na kikao cha wilaya. (205.8-205.9, 226, 231.9-231.10)

**537.1.** Uhamisho wa mhudumu aliyepewa hati utakuwa halali tu iwapo kumbukumbu ya matokeo ya mitihani aliyofanya ya masomo ya wahudumu waliopewa hati, iliyothibitishwa na katibu wa Halmashauri ya Mafunzo ya Wahudumu ya Wilaya ya kikao cha wilaya kinachotoa hati, imetumwa kwa katibu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafunzo ya Wahudumu wa wilaya mhudumu anakohamia. Katibu wa Halmashauri ya Mafunzo ya Wahudumu ya Wilaya ambayo mhudumu anahamia atamjulisha katibu wa wilaya hiyo kuhusu kupokelewa kwa kumbukumbu hizo za matokeo ya mitihani aliyofanya mhudumu anayehamia katika wilaya hiyo. Mhudumu anayehama atahakikisha kwamba kumbukumbu hizo zimefika katika wilaya anayohamia. (233.1- 233.2)

**537.2.** Kikao cha wilaya kinachopokea hati ya uhamisho kitajulisha kikao cha wilaya kilichotoa uhamisho huo kuhusu kupokelewa kwa ushirika wa mtu aliyehama. Hadi uhamisho huo utakapopokelewa kwa kura na kikao cha wilaya inayompokea mhudumu anayehama, mhudumu huyo ataendelea kuwa mshirika wa wilaya iliyotoa uhamisho. Uhamisho kama huo utakuwa halali tu hadi mwisho wa kikao cha wilaya kitakachofuata tarehe ya kutolewa kwa uhamisho katika wilaya iliyohamiwa. (205.8, 226, 231.10)

## H. Maagizo ya Jumla

**538. Maelezo** yafuatayo yanahusu maagizo ya jumla kwa wahudumu wa Kanisa la Mnazareti:

**Washirika Wahudumu**–Wazee, mashemasi, wahudumu waliopewa hati. (530, 531, 532)

**Washirika Waumini**–Washiriki wa Kanisa la Mnazareti ambao si watumishi.

**Mwenye juhudi**–Mshirika mhudumu anayetimiza kazi aliyopewa.

**Aliyepewa Wajibu**-Mhudumu aliyepewa hati, aliye na jukumu ambalo limetajwa kwenye orodha ya wahudumu katika kifungu cha 505-528.

**Mstaafu Aliye na Wajibu-**Mhudumu mstaafu ambaye alipewa wajibu wakati aliomba kustaafu.

**Mstaafu Asiye na Wajibu**-Mhudumu ambaye hakupewa kazi ombi lake la kustaafu lilitolewa.

**Ratiba ya Wahuduma-**Majina ya wahuduma wa wilaya, waliopewa hati na waliowekwa wakfu, ambao msimamo wao wa kuhudumu ni mzuri na ambao hawajarudisha hati zao kwa katibu mkuu kwa kuhifadhiwa.

**Msimamo Mzuri-**Mhudumu asiye na mashtaka ya kusuluhishwa ambayo yanasubiri na ambaye hajachuliwa nidhamu.

**Kuondolewa-**Tendo linalochukuliwa na kikao cha wilaya kuondoa kwenye Ratiba ya Wahudumu majina ya wahudumu ambao wamehifadhi, wamejiuzulu, au wamekabidhi hati zao au hati zao zimesimamishwa au kubatilishwa.

**Kutiwa Nidhamu**-Hali ya mhudumu ambaye amepumzishwa, kazi yote au kiasi cha kazi, haki, fursa, na majukumu ya kuwa mhudumu kwa njia ya nidhamu.

**Kusimamishwa**-Matendo zaidi ya nidhamu, isiyokuwa pamoja na hati, ambayo mhudumu anapumzishwa kwa muda mfupi kutoka kuwa na haki, fursa, na majukumu ya kuwa mhudumu hadi hali yake ya kurudishwa kwa majukumu ikubaliwe.

**Kuondoshwa kabisa**-Hali ya mhudumu ambaye hati yake imebatilishwa na ambaye ameondolewa kwa ushirika wa Kanisa la Mnazareti.

**Hati Zilizohifadhiwa-**hati za mhudumu aliye katika msimamo mzuri ambaye, kwa sababu ya kutohusika kamili katika huduma, ameacha haki, fursa, na majukumu ya kuwa mhudumu kwa kuhifadhi hati yake kwa katibu mkuu. Mtu ambaye amehifadhi hati yake atabaki mhudumu na kuwa na haki, fursa, na majukumbu ya kuwa mhudumu aliyerudishwa kulingana na kifungu cha 539.10. (539, 539.1)

**Hati Zilizosalimishwa**-Hali ya hati ya mhudumu ambaye kwa sababu ya tendo baya, mashtaka, kukiri makosa, hatua iliyochukuliwa na halmashauri ya nidhamu, au hatua ya kujitolea kwa hiari kwa sababu zilizotajwa hapa mbali na kuhusika kamili katika huduma amepumzishwa kutoka kwa haki, fursa, na majukumu ya kuwa mhudumu. Mtu ambaye hati zake zimesalimishwa ni mhudumu aliye chini ya nidhamu. Haki, fursa, na majukumu ya kuwa mhudumu inaweza kurudishiwa mtu huyo baada ya kurejesha msimamo mzuri na amerudisha hati zake za huduma.

**Kujiuzulu kwa Hati-**Hali ya hati ya mhudumu anayeacha haki, fursa, na majukumu ya kuwa mhudumu ili kuwa muumini mshirika wa kanisa. Mhudumu asiye katika msimamo mzuri anaweza kuacha hati yake baada ya idhini kutoka kwa Halmashauri ya Wilaya. (539.1, 539.5)

**Kubatilishwa kwa Hati-**Hali ya hati ya mhudumu ambaye ameondolewa kutoka kwa huduma na ushirika wa Kanisa la Mnazareti. Jina la mhudumu ambaye hati yake imebatilishwa litaondolewa kutoka kwa Ratiba ya Wahudumu.

**Kurudishwa kwa Hati za Huduma**-Tendo linaloambatana na kurejeshwa kwa haki, fursa, na majukumu ya kuwa mhudumu wa mhuduma ambaye hati yake imehifadhiwa, imesimamishwa, imerudishwa, amejiusulu, au kubatilishwa.

**Kurudishiwa Hati ya utumishi-**Hatua ya kumsaidia mhudumu aliyepumzishwa, kujitolea au kwa njia ingine, haki, fursa, na majukumu ya kuwa mhudumu, na mke au mume wake na familia katika urejesho wa afya na utimilifu. Juhudi za kurejeshwa zinafaa kuchukuliwa kibinafsi kwa hatua ya kuamua kama kurudishwa kwa hati kwa mhuduma kunafaa na kukubalika.

**Kurejeshewa Hati za Utumishi-**Kutoa haki, fursa, na majukumu ya kuwa mhudumu kwa mhudumu ambaye hati yake ilihifadhiwa, ilisimamishwa, ilirudishwa, alijiuzulu, au ilibatilishwa, kwa masharti ya kurejeshwa katika msimamo mzuri na idhini zinazohitajika.

**Tuhuma**-Waraka ulioandikwa na kutiwa sahihi na angalau washirika wawili wa Kanisa la Mnazareti wakimshtaki mshirika wa Kanisa la Mnazareti juu ya mienendo inayoashiria mshirika kuwekwa chini ya nidhamu kulingana na *Kitabu cha Mwongozo.*

**Maarifa**-Kutambua ukweli uliojifunza kutokana na hisia.

**Taarifa**-Ukweli uliojifunza kutoka kwa wengine.

**Imani**-Hitimisho lililofikiwa kwa imani njema katika misingi ya maarifa na taarifa.

**Kamati ya Uchunguzi**-Ni kamati iliyoteuliwa kulingana na Kitabu cha Mwongozo kukusanya taarifa kuhusiana na tuhuma au tabia zilizokuwa zinatuhumiwa.

**Mashtaka**-Waraka ulioandikwa unaoeleza hasa tabia ya mshirika wa Kanisa la Mnazareti ambayo imethibitishwa kuwa na msingi wa nidhamu chini ya masharti ya *Kitabu cha Mwongozo*.

**538.1.** Mtumishi atakuwa chini ya nidhamu kama mara kwa mara ataendeleza shughuli binafsi za kanisa na kundi la dini ingine bila idhini iliyoandikwa ya Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya ya kikao cha wilaya ambacho yeyé anahudumu kama mshirika, na idhini iliyoandikwa ya Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu. (538.13, 606.1)

**538.2**. Mtumishi aliyepewa hati ataonyesha heshima kwa ushauri wa msimamizi wa wilaya na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya. (519)

**538.3**. Madai yoyote ya kushiriki kwa mtumishi aliyepewa hati, na/au wanaomtegemea katika mpango au hazina ambayo kanisa linayo linaweza kuwa nayo kwa wakati wa huu au baadaye kwa kusaidia walemavu au wahudumu wazee yatategemea huduma ya mara kwa mara, shughuli zilizotolewa na mhudumu kama mchungaji msaidizi, au muinjilisti au jukumu lingine lolote linalotambuliwa, chini ya idhini ya kikao cha wilaya. Amri hii itawashirikisha washiriki wote wanaotumika wakati wote na pia wanaotumika kwa muda mfupi.

**538.4.** Mhudumu aliyepewa hati anayetumika kama mchungaji au mchungaji msaidizi wa Kanisa la Mnazareti atakuwa mshirika anayepiga kura wa kikao cha wilaya. (201)

**538.5.** Mtu aliyechaguliwa kwenye wadhifa wa kasisi au utaratibu wa shemasi atawekwa wakfu kwa kuwekewa mikono na msimamizi mkuu na wahudumu waliowekwa wakfu wakifuata utaratibu unaofaa, chini ya uongozi wa msimamizi mkuu (307.4)

**538.6.** Msimamizi mkuu aliye na mamlaka atatoa hati ya kuwekwa wakfu kwa mtu aliyewekwa wakfu iliyotiwa sahihi na msimamizi mkuu aliye na mamlaka, msimamizi wa wilaya, na katibu wa wilaya. (535.1)

**538.7.** Iwapo hati ya kasisi au shemasi itakuwa imepotea, imepasuliwa au imeharibiwa, nakala ya hati hiyo inaweza kutolewa kufuatia pendekezo la Halmashauri ya Wilaya. Pendekezo hilo litatolewa moja kwa moja kwa msimamizi mkuu aliye na mamlaka. Na iwapo atakubali, nakala ya hati hiyo itatolewa na katibu mkuu. Nyuma ya hati hiyo, nambari ya awali itatambuliwa pamoja na neno NAKALA. Iwapo msimamizi mkuu, msimamizi wa wilaya, na katibu mkuu aliyetia sahihi hati ya awali hayupo, msimamizi mkuu aliye na mamlaka, msimamizi wa wilaya, na katibu wa wilaya iliyoomba nakala ya hati hiyo wataweka sahihi katika hati hiyo.

Kwa upande wa nyuma wataweka maneno yafuatayo, yakiwa yameandikwa kwa mkono au kupigwa chapa, au yote mawili kuandikwa na kupigwa chapa, na kutiwa sahihi na msimamizi mkuu aliye na mamlaka, msimamizi wa wilaya, na katibu wa wilaya.

Hati hii imetolewa kuchukua nafasi ya hati ya zamani ya kuwekwa wakfu iliyotolewa kwa (jina la mhudumu) tarehe _________ (mwezi wa), (mwaka wa), na (jina la shirika lililoweka wakfu) ambaye aliwekwa wakfu tarehe _________ na hati yake ya awali ilitiwa sahihi na ________ pamoja na ________ (imepotea, imepasuliwa, imeharibiwa)

_________________, Msimamizi Mkuu
_________________, Msimamizi wa Wilaya
_________________, Katibu wa Wilaya

**538.8.** Watumishi wote (walio na wajibu na wasio na wajibu) watakuwa washirika kamili wa Kanisa la mtaa la Mnazareti ambapo watahudhuria ibada kwa uaminifu, kutoa zaka, na kuhusika katika huduma za kanisa. Matarajio ya matakwa haya yanaweza kutolewa tu kwa idhini ya Halmashauri ya Msimamizi wa Wilaya. Mtumishi yeyote asiyekuwa na ushirika katika Kanisa la Mnazareti kwenye wilaya iliyo na hati yake na ambaye hajapewa idhini atakuwa chini ya nidhambu kwa idhini ya Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya. (522, 538.10)

**538.9.** Makasisi wote na mashemasi watakuwa na ushirika wa kihuduma katika kikao cha wilaya ambazo ushirika wao wa kanisa uko na watakuwa wakitoa taarifa kila mwaka kwenye kikao hicho. Kasisi yeyote au shemasi ambaye kwa muda wa miaka miwili mfululizo hatatoa taarifa katika kikao cha wilaya yake, ikiwa ni yeye binafsi au kwa barua, kikao cha wilaya kikiamua, atakoma kuwa mshirika wake. (201, 205.3, 521, 536.1)

**538.10**. Mtumishi yeyote aliyewekwa wakfu anayejiunga na kanisa au dhehebu lingine ambalo si la Kanisa la Mnazareti, au huduma za Kikristo, atakomesha ushirika wake katika Kanisa la Mnazareti utakoma isipokuwa apate idhini kutoka kwa Halmashauri ya Wilaya ya kikao cha wilaya ambayo ushirika wake wa huduma uko. Kikao cha wilaya kutokana na sababu hiyo kitaandika katika kumbukumbu ya mkutano wake maneno yafuatayo: “Ametolewa katika ushirika wa Kanisa la Mnazareti kwa ajili ya kujiunga na dhehebu lingine.” (107, 112)

**538.11.** Mtumishi yeyote aliyewekwa wakfu anayejiondoa au aliyefukuzwa kutoka kwa ushirika wa kanisa la mtaa wakati hayuko katika msimamo mzuri anaweza kujiunga tena na Kanisa la Mnazareti kwa idhini ya Halmashauri ya Wilaya ya kikao cha wilaya ambayo alijiondoa au

aliachishwa ushirika. Halmashauri ya Wilaya inaweza kumpa idhini kwa masharti kwamba mhudumu aliyekuweko ataendelea kuwa mshirika muumini wa kanisa au, kwa kuidhinishwa na msimamizi wa wilaya na msimamizi mkuu wa eneo, kwamba mhudumu aliyekuwepo atakubaliwa tena kama mhudumu chini ya nidhamu akiwa amethibitisha kujitoa kwake katika kuhusika kamili na kila wakati katika hatua ya urejesho. (539.6)

**538.12.** Kasisi au shemasi ambaye jina lake limetolewa kwenye Ratiba ya Wahudumu ya kikao cha wilaya na ambaye hajahifadhi hati zake hatatambuliwa katika wilaya nyingine yoyote bila kupata idhini iliyoandikwa ya kikao cha wilaya kutoka kwenye Ratiba ya Wahudumu ambayo jina lake limeondolewa, isipokuwa litolewe. Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya inaweza kuchukua hatua kwa ombi la kuhamishwa la usimamizi kati ya wilaya. (538.11)

**538.13.** Mtumishi ni lazima awe na idhini iliyoandikwa kila mwaka ya Halmashauri ya Wilaya ili kufanya yafuatayo:

- Kuendeleza shughuli za kipee za kanisa kila mara bila usimamizi wa Kanisa la Mnazareti, au
- Kuendeleza misheni za binafsi au shughuli za kanisa zisizoidhinishwa, au
- Kuungana na kundi la wafanyakazi wa kanisa binafsi au kundi lingine la dini, huduma ya Kikristo, au dhehebu.

Mtumishi yeyote akikosa kutimiza matakwa haya, anaweza kwa pendekezo la theluthi mbili za kura ya ushirika wote wa Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya au Halmashauri kwa Wahudumu ya Wilaya, na hatua ya kikao cha wilaya, kufukuzwa kutoka kwa ushirika na huduma ya Kanisa la Mnazareti. Uamuzi wa mwisho iwapo shughuli yoyote inaunda “misheni ya kipekee” au “shughuli za kanisa zisizoidhinishwa” zitabaki na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu. (112-112.1, 532.9)

**538.14**. Kabla ya kutoa idhini kwa mhudumu ya kuhusika katika shughuli za kipekee za kanisa, Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya lazima iombe idhini iliyoandikwa ya Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu wakati kuhusika huko ni kwa wilaya zaidi ya moja, au wilaya ingine mbali na ile ambayo iliyo na ushirika wa kihuduma wa mhudumu.

Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu itajulisha Halmashauri ya Wilaya inayohusika kwamba ombi la idhini hiyo bado halijashughulikiwa.

**538.15**. Mhudumu aliyepewa wajibu anaweza kuanzisha kanisa la mtaa akiwa amepewa idhini ya kufanya hivyo na msimamizi wa wilaya au

msimamizi mkuu wa eneo. Taarifa rasmi za kuratibiwa zitahifadhiwa katika ofisi ya Katibu Mkuu na msimamizi wa wilaya. (100, 211.1)

**538.16**. Ushirika katika kikao utakuwa kwa mchungaji au huduma zingine zilizopewa wadhifa ambaye anatumika kamili na anaendeleza kuajiriwa kwake katika huduma kama hizo kama mwito wake wa kwanza katika moja ya majukumu ya kihudumu ya wadhifa iliyoelezewa katika vifungu vya 505-528.

**538.17**. Taarifa iliyoonyeshwa kwa mhudumu wakati wa ushauri, maoni, au maelekezo ya kiroho itawekwa kwa siri ya ndani, na haitaonyeshwa bila kumjulisha mtu anayehusika isipokuwa ikihitajika na sheria.

Wakati itawezekana na iwezekane hivi karibuni, mhudumu anafaa kuweka wazi zile hali ambazo kwa siri zinaweza kuleta uvunjaji:

1. Wakati kuna tishio la wazi na linaloonekana la madhara kwa mtu binafsi au wengine.
2. Wakati kuna shaka ya matusi au kutengwa kunakoendelezwa kwa mtoto, mtu mlemavu, mzee, au watu wengine wadhaifu kama ilivyoelezwa na sheria ya nchi. Si jukumu la anayetoa taarifa kuhakikisha ukweli wa taarifa au kuchunguza maelezo ya taarifa, bali kutoa tu taarifa ya shaka kwa mamlaka inayohusika. Mtoto anaelezewa kama mwanadamu yeyote aliye chini ya miaka 18, isipokuwa umri wa wengi ulipatikana baadaye chini ya sheria za nyumbani za mji au nchi ya watu.
3. Katika hali ya sheria wakati mtu yuko chini ya amri ya mahakama ili kutoa ushahidi. Wahudumu wanafaa kulinda hifadhi za yaliyomo ya sehemu, ikiwa ni pamoja na hifadhi zilizowekwa wazi zilizotolewa na ujumbe uliopokewa.

Maarifa ambayo yanatokea kutoka kwa wataalamu yanaweza kutumiwa katika mafundisho, maandishi, mahubiri, au maonyesho mengine ya wazi wakati ule tu hatua zimechukuliwa kuweka usalama kamili wa kitambulisho cha mtu na uhakika wa kuwekwa wazi.

Wakati wa kumshauri mtoto, ikiwa mhudumu atagundua kuna vitisho vikali kwa maslahi ya mtoto na kwamba mawasiliano ya ujumbe wa siri kwa mzazi au msimamizi halali vinafaa afya ya mtoto na usalama wake, mhudumu anafaa kutoa ujumbe unahitajika ili kulinda afya na usalama wa mtoto.

**538.18**. Makasisi na wahudumu wote wanatarajiwa kuhusika katika masaa 20 ya masomo ya maisha ya mwaka, ambayo yatapeanwa na Halmashauri ya Mafunzo ya Wahudumu ya Wilaya. (529.6)

**538.19**. Mhudumu anaweza kuadhimisha ndoa kwa wale tu ambao wamehitimu kwa ushauri mwangalifu, na ambao wako na misingi ya kibiblia ya ndoa.

Ndoa ya kibiblia ziko tu katika uhusiano unaohusu mwanaume mmoja na mwanamke mmoja. (31, 515.9)

**538.20**. Kila wilaya inafaa kuwa na mpango kamili ulioandikwa na kuchunguzwa kila mwaka ili kuongoza bidii katika kutoa majibu ya wakati, huruma, na yaliyofahamika kwa wahuduma wanaohusika kwa mwelekeo wa kutokuwa mhudumu, kwa familia na kwa kongamano zinazohusika. Mpango wa wilaya utaambatana na mielekeo ya *Kitabu cha Mwongozo* na utajumuisha maelezo ya kuanzisha na kuhifadhi taarifa za ukweli na hali ya mabadiliko katika msimamo wa mhudumu yeyote ambaye ataomba kuhusika katika kuendeleza haki, fursa, na majukumu ya kuwa mhudumu. Hifadhi hizi zitajumuisha mawasiliano yote na hatua rasmi zinazohusiana na hali ya mhudumu anayehusika na majina na tarehe za ya uteuzi wa wale watu waliochaguliwa kwa kundi la urejesho kama vile itakavyoelezewa kulingana na kifungu cha 540.1. (225.5)

## I. Kuhifadhi, Kusimamishwa, Kujiuzulu au Kuondolewa katika Huduma

**539.** Katibu mkuu anaruhusiwa kupokea na kuweka kwa usalama hati za wahudumu walio katika msimam mzuri ambao, kwa sababu ya kutoshiriki kikamilifu katika huduma kwa kipindi fulani, wanataka hati hizo zihifadhiwe. Wakati huo wa kuhifadhi hati, Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya ya kikao cha wilaya cha mhudumu itathibitisha kwa katibu mkuu kwamba hati hazijahifadhiwa kwa sababu ya kuepuka nidhamu. Kuhifadhi kwa hati hakutamzuia mhudumu kuwa chini ya nidhamu kama mhudumu. Wahudumu ambao hati zao zimehifadhiwa na katibu mkuu zinaweza kurudishwa. (539.10)

**539.1.** Mtumishi aliye katika msimamo mzuri ambaye hajapewa hatua ya kustaafu na ambaye amebaki bila majukumu kwa miaka minne au zaidi ikifuatana anachululiwa kutohusika kama mhudumu na anahitajika kuhifadhi hati yake. Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya itaarifu kikao cha wilaya "hati ya (kasisi au shemasi anayehusika) imehifadhiwa na Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu." Hatua hii itachukuliwa kuwa bila madhara kwa mhusika. Mtu huyo ambaye amehifadhi hati yake anaweza kurudishiwa. (539.10)

**539.2**. Wakati mhudumu aliyewekwa wakfu katika msimamo mzuri anaacha shughuli zake za huduma ili kufuatilia mwito au wito mbali na kuwa mhudumu katika Kanisa la Mnazareti, anaweza kujiuzulu kutoka kwa

haki, fursa na majukumu ya kuwa mhudumu. Kikao cha wilaya, ambacho anahudumu, kitapokea hati na kuiweka katika ulinzi wa katibu mkuu. Taarifa iliyo katika mukhtasari wa kikao utaonyesha kwamba "alitolewa kwenye Ratiba ya Wahudumu, akiwa amejiuzulu kutoka kwa kazi yake." Mhudumu ambaye anajiuzulu basi anaweza kurudishiwa hati yake. (539.11)

**539.3**. Mhudumu aliyewekwa wakfu ambaye hajastaafu anaacha kutumika kikamilifu kama mhudumu na kuchukua ajira ya muda mrefu, baada ya miaka miwili anaweza kuombwa na Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya au Halmashauri ya Wahudumu ya Wilaya kujiuzulu kutokana na kuwa mhudumu au ahifadhi hati yake na katibu mkuu. Kipindi hiki cha miaka miwili kitaanza wakati wa kikao cha wilaya mara tu baada ya kukomeshwa kwa shughuli kama mhudumu. Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya au Halmashauri ya Mhudumu ya Wilaya itatoa taarifa ya hatua ya kikao cha wilaya. Hatua hiyo itachukuliwa kuwa bila madhara kwa mhusika.

**539.4**. Haki, fursa, na majukumu ya mhudumu inaweza kusimamishwa na jina lake likaondolewa kwenye Orodha ya Wahudumu kama atabadilisha makao kutoka kwenye anwani ya awali bila kutoa anwani mpya ya rekodi kwa Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya au Halmashauri ya Huduma ya Wilaya kwa mwaka mmoja, akikosa kutoa taarifa ya mwaka kama inavyohitajika katika vifungu vya 532.8.na 538.9. Hatua kama hiyo ya kusimamisha itakuwa ni jukumu la Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya au Halmashauri ya Huduma ya Wilaya.

**539.5**. Mtumishi ambaye anapokea Cheti cha Kupendekezwa kutoka kwa kanisa lake la mtaa na amejiunga na Kanisa lingine la Mnazareti wakati wa kikao kingine cha wilaya, au anayekiri kwa maandishi kwamba amejiondoa kutoka kwa Kanisa la Mnazareti, au yule anayejiunga na dhehebu lingine aidha kama mshiriki au mhudumu, na ambaye hajajiuzulu kutoka kwa hati yake ya kihuduma, anaweza kufukuzwa kutoka kwa huduma ya Kanisa la Mnazareti kwa amri ya kikao cha wilaya baada na mapendekezo kutoka kwa Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya au Halmashauri ya Huduma ya Wilaya na jina lake litaondolewa kwa Orodha ya Wahudumu na kazi ya ushirika wa kanisa la mtaa. (111.1, 815)

**539.6.** Mtumishi hayuko katika mwenendo mzuri anaweza kujiuzulu na kukabidhi hati zake za huduma kwa idhini ya Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya. (540)

**539.7.** Mtumishi aliyepewa hati anaweza kuondolewa katika huduma ya Kanisa la Mnazareti kama ilivyoelezewa katika vifungu vya 539.5 na 540.10, au kupitia hatua ya nidhamu kulingana na vifungu vya 606-609.

**539.8.** Wakati kasisi au shemasi ameondolewa katika huduma, hati za mhudumu zitapelekwa kwa katibu mkuu ili zihifadhiwe kwa maagizo ya kikao cha wilaya ambapo kasisi au shemasi alikuwa mshirika wakati huo ama wakati aliondolewa. 326.5).

**539.9.** Wachungaji na halmashauri za makanisa ya mtaa, na wengine ambao wanachukua majukumu katika kanisa hawatamhusisha mtumishi ambaye hayuko katika msimamo mzuri katika jukumu lolote la kihuduma au nafasi yoyote ya kihuduma au mamlaka (kama vile kuongoza ibada, kufundisha darasa la Shule ya Jumapili, au kuongoza mafunzo ya Biblia au kundi ndogo) hadi mwenendo wake mzuri urudishwe. Kukataliwa kwa kupigwa marufuku kutahitaji idhini iliyoandikwa ya msimamizi wa wilaya ambayo mhudumu anahudumu wakati anapumzishwa kutoka kwa haki, fursa, na majukumu yake ya kuwa mhudumu, na msimamizi mkuu anayehusika wa eneo hilo. (540.4)

**539.10. Kurudishwa kwa Hati Zilizohifadhiwa**. Wakati kasisi au shemasi aliye katika mwenendo mzuri amehifadhi hati yake, hati hiyo inaweza, kwa wakati wowote ambapo kasisi au shemasi aliye katika mwenendo mzuri, kurudishwa kwa kasisi au shemasi baada ya amri kutoka kwa kikao cha wilaya ambayo ilihifadhi hati, mradi kwamba kurudishwa kwa hati kutapendekezwa na msimamizi wa wilaya na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya. Katika vikao vya wilaya, Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya inaweza kupiga kura kuidhinisha kurudishwa kwa hati zilizohifadhiwa za mhudumu.

**539.11**. **Kurudishwa kwa Hati ya Kujiuzulu au Kukataliwa.** Kasisi au shemasi ambaye, akiwa mhudumu katika mwenendo mzuri, atajiuzulu kutoka kwa kazi yake ya huduma au ambaye hati ya ilikataliwa baada ya kujiunga na kanisa lingine, dhehebu, au huduma, anaweza kurudishiwa hati yake na kikao cha wilaya baada ya kutoa fomu ya Maswali ya Kuwekwa Wakfu/Kutambuliwa, akithibitisha maagano ya huduma, akichunguzwa na kupendekezwa ianvyostahili na Halmashauri ya Hati ya Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya au Halmashauri ya Huduma ya Wilaya, na baada ya idhini ya msimamizi wa wilaya na msimamizi mkuu wa eneo. (539.2)

**539.12.** Cheti cha kuwekwa wakfu cha aliyeaga dunia ambaye hati yake ilihifadhiwa na ambaye alikuwa katika msimamo mzuri wakati wa kifo chake, kinaweza kupelekewa familia ya mhudumu baada ya ombi lililoandikwa kwa katibu mkuu na idhini ya msimamizi mkuu wa wilaya ambayo hifadhi hiyo iliwekwa.

**539.13**. **Utengano/Talaka.** Katika muda wa masaa 48 wa kutoa ombi la talaka au kuvunja/utengano wa halali wa ndoa wa mhudumu na mke au mume wake kwa madhumuni ya kuacha kuacha kuishi pamoja, mhudumu (a) atawasiliana na msimamizi wa wilaya, akimjulisha msimamizi huyo juu ya hatua hiyo aliyochukua; (b) akubali kukutana na msimamizi wa wilaya na mshirika wa Halmashauri ya Wilaya baada ya maafikiano ya mahali na wakati, au iwapo hakutakuwa na maafikiano ya wakati na mahali pa kukutana, watakutana wakati na mahali palipochaguliwa na msimamizi wa wilaya; (c) ataeleza (katika mkutano uliotajwa katika sehemu ya "b" hapa juu, hali ya hatua iliyochukuliwa, ataeleza ugomvi wa ndoa, na ataeleza misingi ya kibiblia ya uthibitishaji wa sababu za mhudumu kuruhusiwa kuendelea kama mhudumu aliye katika msimamo mzuri. Iwapo mhudumu hatakubaliana na sehemu zilizo hapa juu, kukosa kukubaliana huku kutasababisha nidhamu, Wahudumu wote wawe wanahudumu kamili, wasiouhudumu kamili, au walistaafu, walio na majukumu na wasio na majukumu, wako chini ya maongozi haya, na ni lazima waonyeshe heshima kwa ushauri wa umoja wa msimamizi wa wilaya na Halmashauri ya Wilaya. Hakuna mhudumu aliye hai au mwenye wajibu ataendelea katika huduma bila kura ya kumthibitisha ya Halmashauri ya Wilaya.

## J. Kurudishwa kwa Wahudumu Katika Ushirika na Msimamo wa Kanisa

**540.** Kanisa la Mnazareti linatambua jukumu lake la kueneza tumaini na uponyaji wa neema ya Mungu inayokomboa na kufanya upya kwa mhudumu yeyote ambaye, kwa kusalimisha hati, kujitoelea au pengine, amepumzishwa kwa haki, fursa na majukumu yake ya kuwa mhudumu kwa sababu ya kukosa kutimiza wajibu wa mhudumu. Kanisa pia linakubali wajibu wake wa kuwaalika mke na mume na familia, kongamano, na jamii ya mhudumu katika kukumbatiwa upendo wa Mungu wa kujali. Kwa sababu hii, hatua inayoelekeza kurejesha mhudumu kwa msimamo mzuri kutaendelezwa katika hatua mbili za kipekee:

1. Kurudishwa hati. Bila kuangalia ukubwa wa mwenendo mbaya wa mhudumu, uwezekano wa karibu wa kurudishwa kwa utumishi wake wa kihuduma, au kuitika kwake kwa mwanzo kwa neema na msaada unaoenezwa, kurudishwa kwa hali ya mhudumu (kiroho na kwa njia zingine) na ule wa mke na mume wake na familia kulingana na vifungu vya 540.1-540.7. Kurudishwa huku kunafaa kuwa kwa lengo moja la hatua hii.
2. Kurejeshewa hati. Kurejeshewa hati kwa msimamo mzuri wa mhudumu na mapendekezo ya kurudishiwa hati yake kutafikirwa

katika hatua tofauti kutoka na kufuatia bidii ya kutafuata kurudishwa kwa afya na wema wa mhudumu na mke au mume wake na familia. (540.6-540.12)

**540.1 Uteuzi wa Kundi la Kurudishiwa Hati.** Wakati mienendo mibaya ya mtumishi inadhirihika wazi, hatua ya kuingilia kati inayofaa na ya huruma ni muhimu sana kwa ajili ya mhudumu na mke au mume wake na familia yake, kongamano, na jamii. Kwa vile maendeleo kama hayo hayatarajiwi kirahisi, uchaguzi wa mapema na matayarisho ya watu waliohitimu, kwa mhudumu na muumini, ili kuanzisha kurudishwa ni jambo muhimu kwa mpango wa matokeo ya wilaya. Watu hawa watafaa kuteuliwa na msimamizi wa wilaya akishikiriana na Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya. Hali ya mwenendo mbaya wa mhudumu ikitokea, watu hawa, wanaofanya kazi kama kundi la kurudishwa kwa mhudumu, watatumwa na msimamizi wa wilaya mara moja inavyohitajika na kulingana na mpango wa wilaya. Kundi la kurudishwa lililotumwa litakuwa na watu wasiopungua watatu. (211.20, 225.5, 540)

**540.2**. **Kazi ya Kundi la Kurudishiwa Hati.** Kundi la kurudishiwa hati lina wajibu wa kuanzisha kurudishiwa hati kwa afya na wema wa mhudumu na mke au mume wa mhudumu pamoja na familia yake. Si wajibu au mamlaka ya kuamua kama haki, fursa, na majukumu ya kuwa mtumishi yatarejeshewa mhudumu. Ikiwezekana kama hali inaruhusu, kazi ya kundi la kurudishiwa hati inajumuisha:

1. kueneza usalama kwa mke au mume wa mhudumu pamoja na familia yake na pia kwa mhudumu;
2. kutoa uwazi kwa mhudumu na mke au mume wake juu ya hatua na madhumuni ya kurudishiwa hati;
3. kusimamia bidii ya pamoja ya mhudumu, wilaya, na kongamano lolote linalohusika katika kuweka mpango wa kushughulikia hali ya fedha, nyumba, matibabu, hisia, kiroho, na mahitaji mengine ambayo yanaweza kutokea kwa kuyashughulikia kwa haraka katika hali ambayo mwenendo usiofaa uko wazi;
4. kuanzisha mpango ulioidhinishwa na wilaya, ukiwa ni pamoja na kutoa taarifa kila mara kwa bidii yake na kwa hali ya hatua ya mhudumu na mke au mume wake na familia katika kurudishiwa afya na wema wake;
5. kuwasilisha kwa mhudumu na mke au mume wake, kwa msimamizi wa wilaya, na kwa halmashauri inayofaa ya wilaya wakati itahukumu kazi iko karibu kukamilika au kazi hiyo imefika kiwango ambacho kinaweza kutarajiwa;

6. kutoa kwa Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya au Halmashauri ya Huduma ya Wilaya au kamati iliyoteuliwa inayosimamia maamuzi ya kurejeshewa hati, baada ya maombi ya mhudumu kwa ajili ya kurejeshewa haki, fursa, na majukumu ya kuwa mhudumu, mapendekezo yake iwapo uamuzi wa kurejeshwa kwa mhudumu katika msimamo mzuri unafaa. (540.8)

**540.3**. Katika hali ambayo mhudumu aliye chini ya nidhamu hataitikia hatua ya kurudishwa, bidii ya uadilifu inafaa kutolewa kuahirishwa kwa kurudishwa kwa mke au mume wa mhudumu na familia yake wakati ambapo kutafuta kumhusisha kamili au kumhusisha tena mhudumu katika kurudishwa. Baada ya kuchunguza bidii ya kurudishwa na kwa heshima ya wema wa mke au mume na familia ya mhudumu, msimamizi wa wilaya anaweza kusimamisha, kuhitimisha, au kwa njia ingine kubadilisha bidii za kurudishwa.

Katika hali ambayo wilaya haitateua kundi la kurudishwa au kundi la kurudishwa lililoteuliwa likose kutimiza majukumu kwa siku zisizopungua 180 kutoka tarehe mhudumu aliwekwa chini ya nidhamu, mhudumu aliye chini ya nidhamu anaweza kuomba Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu kuhamishia kwa wilaya ingine jukumu la bidii zilizoanzishwa juu ya kurudishwa kwake na hatua inayochukuliwa kufuatia ombi lake, kama kuna, kurejeshwa kwa msimamo mzuri na kurejeshewa haki, fursa, na majukumu ya kuwa mhudumu. Maoni haya pia yako kwa mhudumu anayehusika iwapo wilaya itashindwa kutoa jibu kwa ombi la kumrejesha katika msimamo mzuri. (540-540.2, 540-540.12)

**540.4**. Mhudumu mshirika ambaye hayuko katika msimamo mzuri hatakuwa na kazi yoyote ya usimamizi au mamlaka katika kanisa au katika ibada zake kama: kuhubiri, kuongoza ibada, kufundisha darasa la Shule ya Jumapili, kuongoza mafunzo ya Biblia au kundi ndogo. Mhudumu huyo anaweza kutumika tu katika majukumu haya au apewa jukumu lingine la huduma baada ya pendekezo lililokubaliwa la kundi la kurudishwa lililoteuliwa na wilaya ambalo lilipewa mhudumu na kibali kutoka kwa Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya, Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Wahudumu ya Wilaya au Halmashauri ya Huduma ya Wilaya, msimamizi wa wilaya, na msimamizi mkuu wa eneo. Pendekezo linalofaa linaonyesha bidii ya kwamba mtu na mke au mume wake na familia yake wamefanya hatua ya kutosha katika hatua ya kurudishwa ya kumruhusu tena mtu huyo kuwa wa utumishi katika nafasi ya usimamizi au mamlaka. Idhini ya kutumika katika nafasi ya usimamizi au mamlaka inaweza kutolewa na au bila pingamizi na inaweza kuondolewa na msimamizi wa wilaya katika kushauriana na kundi la kurudishwa. (606.1-606.2, 606.5, 606.11-606.12)

**540.5**. Baada ya ombi kutolewa na mhudumu chini ya nidhamu kwa ajili ya kurejeshwa katika msimamo mzuri kama ilivyotolewa katika kifungu cha 540.6, kundi la kurudisha linaweza kupendekeza kwa msimamizi wa wilaya na halmashauri ya wilaya inayohusika au kamati iliyoteuliwa kwamba ombi likubaliwe kulingana na maelezo ya kifungu cha 540.8; au, kwamba mhudumu aendelee na hatua ya kurudishwa kwa muda zaidi na wakati fulani kabla ya kutuma ombi tena.

Katika hali ambapo kundi la kurudishwa limekamilisha bidii yake na mhudumu aliye chini ya nidhamu hatatuma ombi la kurejeshwa kwa msimamo mzuri, mhudumu atabaki chini ya nidhamu isipokuwa hatua ichukuliwe 1) kumwondoa mhudumu kutoka kwa ushirika na huduma ya Kanisa la Mnazareti; au 2) kutoa idhini kwa mhudumu kujiuzulu kwa hati yake na kuwa mshirika muumini wa kanisa. Katika hali ya kujiuzulu kwa hati na mhudumu ambaye amekuwa chini ya nidhamu ambapo kuna thibitisho la kurudishwa kunakotosha na kunaridhisha, ulinzi utatolewa kutambua ipasavyo na kusherehekea hatua hiyo. (539.5, 540.10)

**540.6**. **Maombi ya Kurejeshwa katika Msimamo Mzuri.** Mhudumu akiwa amepumzishwa kutoka kuwa na haki, fursa, na majukumu ya kuwa mhudumu anaweza kutuma ombi la kurejeshwa katika msimamo mzuri na kurudisha kwa hati yake chini ya matakwa yanayowezekana ya kifungu cha 540.7. Ombi kama hilo lazima litumwe kwa msimamizi wa wilaya angalau miezi sita kabla ya mkutano unaofuata uliopangwa wa kikao cha wilaya na lazima likubaliane na mpango wa wilaya ulioidhinishwa kwa siku 30.

**540.7.** Mhudumu anaweza kutuma ombi la kurejeshwa kwa msimamo mzuri na kurudishwa kwa hati yake mradi kundi la kurudishwa lililopewa wajibu kwa mhudumu lisaidie vile inavyofaa ombi hilo na kutoa ushahidi kwamba mhudumu ahusike kikamilifu na kwa uthabiti angalau kwa muda wa miaka miwili katika hatua ya kurudishwa chini ya usimamizi. Mhudumu ambaye, katika kuhukumu kwake, amejitahidi kuhusika kikamilifu na kwa uthabiti kwa miaka isiyopungua minne katika hatua ya kurudishwa kama hii anaweza kutuma ombi la urejesho kwa msimamo mzuri na au bila kuungwa mkono kwa ombi na kundi la kurudishwa.

Wakati mhudumu aliye chini ya nidhamu ametafuta kuhusika katika kurudishwa akiwa nje, kiasi cha muda kitakachohitajika kabla ya kutuma ombi la kurejeshwa kwa msimamo mzuri kitaanza na mkutano rasmi uliokuwepo mwanzoni mwa mhudumu pamoja na kundi la kurudishwa au siku 60 baada ya tarehe ya kundi la kurudishwa kupewa wajibu kwa mhudumu. Katika hali ambazo mhudumu aliahirisha au alihitilafiana na kuhusika katika hatua ya kurudishwa, msimamizi wa wilaya akishauriana na kundi la kurudishwa ataamua iwapo kiasi cha muda kinachohitajika

kabla ya maombi ya kurejeshwa kwa msimamo mzuri kimekamilishwa. (538, 540.3)

**540.8. Majibu kwa Maombi ya Kurejeshwa kwa Msimamo Mzuri.** Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Mhudumu ya Wilaya, au kamati yake iliyoteuliwa na msimamizi wa wilaya, itatilia maanani maombi ya kurejeshwa kwa msimamo mzuri yaliyopokelewa na msimamizi mkuu, na:

1. kuthibitisha kwamba maombi hayo ni halali, na yamefikia ratiba zote za kutumwa;
2. kuomba na kutathmini pendekezo la kundi la kurudishwa;
3. kumhoji mhudumu anayetafuta kurejeshwa kwa msimamo mzuri na watu wengine wowote ambao wana uwezekano wa kuhojiwa;
4. kuamua iwapo kupendekeza haki, fursa, na majukumu ya kuwa mhudumu yarejeshewe kwa mhudumu na hati yake kurudishwa.

Wakati maombi yametumwa angalau siku 180 mbele ya kikao kitakachofuta cha wilaya, kuzingatiwa kwa ombi kutakamilishwa na kupendekezwa kufanywe na msimamizi wa wilaya kabla ya kikao cha wilaya. Pendekezo la kurejeshwa kwa haki, fursa na majukumu ya mhudumu kuwa mhudumu ambaye hati yake imesalimishwa kwa sababu ya mienendo mibaya ya kimapenzi litahitaji idhini ya theluthi mbili ya Halmashauri ya Ushauri ya Wilaya. Pendekezo linafaa litumwe kwa Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu kwa kipindi cha mwaka mmoja wa tarehe ya ombi la hivi karibuni la mhudumu la kurejeshwa kwa msimamo mzuri. Makubaliano kwa muda wowote uliotolewa katika kifungu hiki lazima idhini iliyoandikwa mwanzo kwa msimamizi mkuu wa eneo. (540.2, 540.3, 540.6, 540.7, 540.12)

**540.9**. Mtu aliye na hatia ya mienendo mibaya ya kimapenzi yanayohusisha watoto hatarejeshwa kwa msimamo mzuri kama mhudumu au aruhusiwe kuwa na hati yoyote ya kihuduma, kutumika katika nafasi yoyote ya jukumu la au huduma ya watoto, au achaguliwe au kuteuliwa katika kazi ya uongozi katika kanisa la mtaa. Mtoto anaelezewa kama mwanadamu yeyote aliye chini ya umri wa miaka 18, isipokuwa umri wa wengi imekuja baadaye chini ya sheria za kinyumbani taifa au nchi. (129.30, 600, 606.1-606.2, 606.5, 606.11-606.12, 916)

**540.10**. Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Mhudumu ya Wilaya au kamati yake, baada ya kuangazia ombi la kurejeshwa kwa msimamo mzuri lililotumwa kwa muda ulioruhusiwa, inaweza kupendekeza kwa msimamizi wa wilaya na halmashauri za wilaya zinazohusika moja ya mambo yafuatayo:

1. kwamba mhudumu arejeshwe katika msimamo mzuri na hati yake irudishwe;

2. kwamba mhudumu aendelee katika hatua ya kurushwa kwa muda fulani uliotengwa kabla ya kutuma ombi tena la kurejeshwa katika msimamo mzuri;
3. kwamba muda wa kurudishwa uongozwe na mpango wa kurudishwa uangaliwe tena (kama vile kuchunguza kuhusika kwake tena katika huduma, kuweka kundi jipya la kurudishwa, au kuzungumzia mambo ya binafsi, ndoa, au familia);
4. kwamba mhudumu aendelee chini ya nidhamu'
5. kwamba mhudumu asirudishwe katika msimamo mzuri, bali thibitisho la kurudishwa likubaliwe vinavyofaa na kusherehekewa, na ruhusa itolewa kwa mhudumu ajiuzulu kutoka kwa hati;
6. kwamba mhudumu aondolewe kutoka kwa ushirika na huduma ya Kanisa la Mnazareti. (539.5, 540.7, 540.12)

**540.11**. Iwapo maombi mawili ya kurejeshwa na mhudumu aliye chini ya nidhamu yatakataliwa, ombi linaweza kutolewa na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu kuhamisha jukumu la kurudishwa na kurejeshwa kunakowezekana katika msimamo mzuri kwa mhudumu anayehusika hadi wilaya ingine ambayo ombi hilo linaweza kukubaliwa. Kama ombi la tatu la kurejeshwa katika msimamo mzuri na kurejeshewa haki, fursa, na majukumu ya kuwa mhudumu litakataliwa, mhudumu anaweza kuwa muumini baada ya idhini ya Halmashauri ya Wilaya. (538.13, 539.6)

**540.12**. Kurejeshwa kwa Hati, Fursa na Majukumu ya kuwa Mhudumu. Mhudumu ambaye amepoteza msimamo mzuri na ambaye maombi yake ya kurejeshwa katika msimamo mzuri yamesababisha pendekezo la kurejeshwa kwa hati, fursa, na majukumu ya kuwa mhudumu, anaweza kurejeshwa katika msimamo mzuri na hati yake kurudishwa kwa hatua zifuatazo pekee:

1. idhini ya msimamizi wa wilaya;
2. idhini ya Halmashauri ya Wilaya ya Hati za Kuhitimu kwa Mhudumu au Halmashauri ya Huduma;
3. theluthi mbili za idhini ya Halmashauri ya Wilaya;
4. idhini ya Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu; na
5. idhini ya kikao kikuu ambacho msimamo mzuri ulipotezwa. (606.1-606.2, 606.5, 606.11-606.12)

SEHEMU YA SABA

# UTARATIBU WA UTEKELEZAJI WA NIDHAMU

UCHUNGUZI WA UWEZEKANO WA KUWEPO KWA TENDO BAYA NA NIDHAMU YA KANISA

KUCHUKUA HATUA KUNAPOKUWA NA UWEZEKANO WA TENDO BAYA

KUCHUKUA HATUA KWA TENDO BAYA LA MTU MWENYE MAMLAKA AU WADHIFA WA KUAMINIWA

NIDHAMU YENYE UBISHI YA MHUDUMU

KANUNI YA UTARATIBU

MAHAKAMA YA WILAYA YA RUFANI

MAHAKAMA KUU YA RUFANI

MAHAKAMA YA JIMBO YA RUFANI

HAKIKISHO LA HAKI

## I. UCHUNGUZI WA UWEZEKANO WA KUWEPO KWA TENDO BAYA NA NIDHAMU YA KANISA

**600**. Kusudi la nidhamu ya kanisa ni kuhifadhi heshima ya kanisa, kulinda wasio na hatia wasidhuriwe, kulinda uwezo wa ushuhuda wa kanisa, kuonya na kurekebisha wasiojali, kuleta wenye hatia katika wokovu, kurejesha katika utumishi wale waliorekebishwa, na kulinda sifa na vifaa au mali ya kanisa. Washirika wa kanisa wanaovunja Agano la Sifa ya Kikristo au Agano la Maadili ya Kikristo, au wale kwa makusudi na mara kwa mara wanavunja maagano yao ya ushirika, wanapaswa kuchukuliwa hatua kwa upole na kwa uaminifu, kulingana na kiasi cha ubaya wa makosa yao. Utakatifu wa moyo na maisha ikiwa ni kiwango cha Agano Jipya, Kanisa la Mnazareti linasisitiza huduma safi na linawahitaji wale wanaotumia jina lake kama wahudumu wawe na mafundisho sahihi ya ukristo na maisha matakatifu. Kwa hivyo kusudi la nidhamu si kuadhibu au kupatiliza makosa kwa mhudumu bali ni kutimiza malengo haya. Jitihada ya uhusiano imara na inayoendelea kwa knaisa pia ni kazi ya hatua ya nidhamu.

## II. KUCHUKUA HATUA KUNAPOKUWA NA UWEZEKANO WA TENDO BAYA

**601.** Kuchukua hatua ni muhimu wakati wowote mtu aliye na mamlaka ya kufanya hivyo anapopata habari zinazomfanya mtu mwenye akili timamu kuamini kwamba zinaweza kuwa sahihi. Zaidi kuchukua hatua ni muhimu wakati habari ambayo inaweza kumfanya mtu mwenye busara aamini kwamba madhara yanaweza kuingia kanisani, kwa wale wanaoshukiwa kuwa wametenda jambo baya, au kwa mtu yeyote kwa sababu ya tendo baya lililofanywa na mtu aliye katika nafasi ya kuheshimwa au mamlaka Kanisani.

**601.1.** Wakati mtu asiye na mamlaka ya kuchukua hatua kwa niaba ya kanisa anapata habari zinazoweza kumfanya mtu mwenye busara kuamini kwamba zinaweza kuwa sahihi na ambazo zinaweza kumsababisha mtu mwenye busara aamini kwamba tendo baya linaweza kuwa limetendwa na mtu mwenye mamlaka au mwenye wadhifa wa kuheshimiwa katika kanisa, mtu mwenye habari hizo atamjulisha mwakilishi wa kanisa aliye na mamlaka ya kuchukua hatua juu ya tendo hilo.

**601.2**. Mtu aliye na mamlaka ya kuchukua hatua anakuwa na bidii ya nafasi iliyo katika kanisa dhidi ya mtu au watu ambao wanashukiwa kuwa wamehusika na tendo baya atajulikana kama ifuatavyo:

| *Mtu anayeshukiwa* | *Mwenye mamlaka ya kuchukua hatua* |
|---|---|
| Mtu *a*siye mshiriki | Mchungaji wa kanisa ambalo tendo baya limefanyika |
| Mshiriki wa kanisa | Mchungaji wa kanisa ambalo anashiriki. |
| Mtumishi wa Kanisa | Msimamizi wa wilaya ambayo mhudumu huyo anayeshukiwa anahudumu, au mchungaji wa kanisa la mtaa lililomuajiri. |
| Msimamizi wa wilaya | Msimamizi mkuu anayesimamia wilaya hiyo. |
| Mkurugenzi wa Jimbo hilo | Msimamzi mkuu anayesimamia Jimbo |
| Msimamizi wa Eneo Asiyetajwa | Msimamizi Mkuu wa eneo Katibu mkuu mtendaji. |

Mtu aliye na mamlaka ya kuchukua hatua anaweza pia katika wakati unaofaa kuwajulisha watu wanaohusika katika uongozi wa wilaya, eneo, jimbo, na/au ulimwenguni kote juu ya mashtaka. Mtu aliye na mamlaka ya kuchukua hatua anaweza kutumia msaada wa watu wengine katika kutafuta ukweli au kuchukua hatua inayohitajika.

**601.3.** Ikiwa hakuna mashtaka yaliyotolewa, kusudi la uchunguzi litaamuliwa kama kuna hatua inayohitaji kuchukuliwa kuzuia madhara au kupunguza kiasi cha madhara ambayo yalifanyika awali. Katika hali ambayo mtu mwenye busara anaamini kwamba hakuna hatua zaidi inayohitaji kuchukuliwa kuzuia au kupunguza kiasi cha madhara, hakuna uchunguzi utakaoendelea isipokuwa shtaka likihifadhiwa. Ukweli uliogunduliwa wakati wa uchunguzi unaweza kutumiwa kama msingi wa shtaka lolote.

## III. KUCHUKUA HATUA KWA TENDO BAYA LA MTU MWENYE MAMLAKA AU WADHIFA WA KUAMINIWA

**602.** Wakati wowote mtu aliyeruhusiwa kuchukua hatua anapopata ukweli unaoonyesha kwamba watu wasio na hatia huenda wakawa wamepata madhara kwa ajili ya tendo baya na mtu mwenye mamlaka au wadhifa wa kuaminiwa, hatua itachukuliwa itakayofanya kanisa kuchukua hatua inayofaa ya kinidhamu. Hatua kama hiyo itakuwa ya kutafuta kuzuia

madhara zaidi yasitokee kwa watu hao wasio na hatia, kutafuta kuchukua hatua za kukabiliana na mahitaji ya waathirika, mshtakiwa na wengine ambao wamepata madhara kwa sababu ya matokeo ya tendo hilo baya. Uzito unapaswa kuwekwa kwa mahitaji ya mume au ya mke na familia ya mshtakiwa. Hatua hiyo pia itatafuta kushughulikia mahitaji ya kanisa la mtaa, wilaya na kanisa kuu yanayohusiana na uhusiano wao na wengine, kulindwa na madhara zaidi pamoja na heshima ya kanisa.

Wale wanaochukua hatua kwa niaba ya kanisa wanapaswa kufahamu kwamba chochote wanachosema na kufanya kinaweza kuwa na madhara ya kisheria. Jukumu la kanisa la kuchukua hatua linatokana na kuhusika kwake kwa maadili ya Kikristo. Hakuna mtu yeyote aliye na mamlaka ya kulitwika kanisa jukumu la kifedha bila ruhusa ya halmashauri au kamati ya kanisa, au kutwika wilaya jukumu kama hilo bila ruhusa ya Halmashauri ya Wilaya. Mtu ambaye hana uhakika wa hatua inayofaa kuchukuliwa anapaswa kutafuta ushauri kutoka kwa mtu aliyehitimu kwa jambo hilo.

**602.1**. Katika kila kanisa la mtaa, ni muhimu kwa halmashauri ya kanisa kutoa mwongozo wa hatua inayofaa kuchukuliwa shida inapotokea; hata hivyo huenda wakati mwingine ikahitajika kuchukua hatua kabla ya kufanyika kwa mkutano wa halmashauri ya kanisa. Ni muhimu kwa kila kanisa la mtaa kuwa na mpango wa kuchukua hatua za dharura.

**602.2.** Kwa kila wilaya jukumu la kimsingi la kukabiliana na mzozo litakuwa chini ya Halmashauri ya Wilaya; hata hivyo, ni muhimu kwa kila wilaya kuwa na mpango wa kuchukua hatua za dharura ikiwa/iwapo itahitajika. Mpango huo unaweza kuwa ni pamoja na kuteuliwa na Halmashauri ya Wilaya kwa kamati maalum ya kuchukua hatua inayohitajika inayojumuisha watu wenye utaalamu maalum kama vile washauri, mawakili, na watenda kazi katika jamii, na wale waliohitimu katika mawasiliano yanayohusiana na hatua inayohitaji kuchukuliwa.

**603. Kusuluhisha Mambo ya Nidhamu na Mapatano Kanisani.** Mabishano ni sehemu ya maisha, hata ndani ya kanisa. Hata hivyo, mabishano haya yanapokuwa mzozo ambao unawagawanya washirika au kuhitilafiana na ushirika wa kanisa, hatua isiyo ya rasmi ya ufahamu inafaa kuwa kabla ya hatua ya rasmi ya kukubaliana. Yaweza kuwa hatua isiyo rasmi au iliyo rasmi, lengo linafaa kuwa kukubaliana au mapatano.

**603.1.** Hatua Isiyo Rasmi: Wakati mzozo unatokea kanisani, kipindi cha ufahamu na ushauri kinafaa kutafutwa kwa matamanio ya kuishi kwa amani na watu. Watu wote wanaohusika wanatiwa moyo kulikabidhi jambo hilo kwa Bwana katika maombi, na hata hivyo hatua yote izamishwe katika maombi. Watu walio katika mzozo wanafaa kuendelae kila mmoja kwa unyenyekevu kwa matumaini ya mapatano.

**603.2**. Hatua Rasmi: Kama hatua hii haitawezekana, watu hawa wanaweza kuamua kuhamia kwenye hatua rasmi ya mapatano. Jambo hili linafaa kuamuliwa na kundi la kuwakilisha la watu waliokomaa na wasiokuwa na ubaguzi ndani ya kanisa. Kama kosa litaonekana, kundi hili linaweza kupendekeza hatua inayofaa kama vile ilivyoelezwa katika kifungu cha 604.

**604**. **Kusuluhisha Mambo ya Nidhamu kwa Mapatano**. Utaratibu wa kinidhamu ulioelezwa katika Kitabu cha Mwongozo unakusudiwa kutoa hatua inayofaa ya kusuluhisha mashtaka ya tendo baya wakati kuna ubishi kutoka kwa mshtakiwa. Katika hali nyingi, ni sawa kusuluhisha mambo ya nidhamu kwa kukubaliana au kwa mapatano. Juhudi ya kusuluhisha mambo ya kinidhamu kwa kukubaliana inatiwa moyo na inafaa kufuatwa kadri invyowezekana.

**604.1**. Mambo yoyote yaliyo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Nidhamu ya Mtaa yanaweza kusuluhishwa kwa makubaliano yaliyoandikwa kati ya mshtakiwa na mchungaji ikiwa imeidhinishwa na halmashauri ya kanisa na msimamizi wa wilaya. Masharti ya makubaliano kama hayo yatakuwa na uwezo sawa na hatua ya makubaliano kama hayo yatakuwa na uwezo sawa na hatua ya Halmashauri ya Nidhamu ya Mtaa.

**604.2.** Mambo yoyote yaliyo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Nidhamu ya Wilaya yanaweza kusuluhishwa kwa makubaliano yaliyoandikwa kati ya mshtakiwa na msimamizi wa wilaya ikiwa makubaliano hayo yameidhinishwa na Halmashauri ya Wilaya na msimamizi mkuu anayesimamia wilaya. Masharti ya makubaliano kama hayo yatakuwa na uwezo sawa na hatua ya Halmashauri ya Nidhamu ya Wilaya.

## IV. NIDHAMU YENYE UBISHI YA MUUMINI

**605.** Ikiwa mshirika ameshtakiwa kwa tendo la kinyume la maadili ya kikristo, mashtaka kama hayo yanapaswa kuwekwa katika maandishi na kuwekwa sahihi na washirika wasiopungua wawili ambao wamekuwa wakihudhuria ibada kwa uaminifu kwa muda usiopungua miezi sita. Mchungaji atateua kamati ya uchunguzi yenye washirika watatu wa kanisa la mtaa linalohusika, kwa idhini ya msimamizi wa wilaya. Kamati hiyo itatoa taarifa iliyoandikwa ya matokeo ya uchunguzi wake. Taarifa hiyo ni lazima iwekwe sahihi na wengi na ipelekwe kuhifadhiwa na halmashauri ya kanisa.

Baada ya uchunguzi na kufuatiliwa kwake, washirika wowote wawili walio katika msimamo mzuri katika kanisa la mtaa wanaweza kuweka sahihi kwenye hati za mashtaka kabla ya kupelekwa kwenye halmashauri

ya kanisa. Halmashauri ya kanisa ikipata taarifa hiyo itateuwa, chini ya idhini ya msimamizi wa wilaya, Halmashauri ya Nidhamu ya Mtaa ya washirika watano, ambao hawana upendeleo na wenye uwezo wa kusikiliza na kuamua kesi kwa njia ya haki na bila upendeleo. Ikiwa kwa maoni ya msimamizi wa wilaya, haiwezekani kuteuwa washirika watano kutoka katika kanisa la mtaa linalohusika kwa sababu ya ukubwa wake, hali ya mashtaka, au hali ya ushawishi wa mshtakiwa, msimamizi wa wilaya akishauriana na mchungaji anaweza kuteuwa washiriki watano kutoka kwa makanisa mengine katika wilaya hiyo kuunda Halmashauri ya Nidhamu. Halmashauri hiyo itaketi haraka iwezekanavyo kufanya uamuzi juu ya mambo yanayohusika. Baada ya kusikiliza maelezo ya mashahidi na kuchunguza ushahidi uliotolewa, Halmashauri ya Nidhamu aidha itamuondolea hatia au itamuadhibu, kulingana na vile ushahidi unavyoonyesha kuwa inastahili. Uamuzi utakaofikiwa ni lazima uwe umekubaliwa na washiriki wote walioko katika Halmashauri ya Nidhamu. Adhabu inaweza kuwa kukemea, kuonya, kusimamishwa au kuondolewa kutoka katika ushirika wa kanisa. (516.8)

**605.1.** Rufaa ya kupinga uamuzi wa Halmashauri ya Nidhamu ya Mtaa inaweza kupelekwa kwa Mahakama ya Rufaa ya Wilaya katika kipindi cha siku 30 na mshtakiwa au halmashauri ya kanisa.

**605.2.** Mshirika akiondolewa katika ushirika wa kanisa la mtaa na Halmashauri ya Nidhamu ya Mtaa, anaweza kujiunga tena na Kanisa la Mnazareti katika wilaya hiyo ikiwa tu ameruhusiwa na Halmashauri ya Wilaya. Ikiwa kibali kama hicho kitatolewa, atapokelewa katika ushirika wa kanisa la mtaa akitumia hati iliyokubaliwa ya kupokewa kwa washiriki kanisani. (21, 28-33, 112.1-112.4, 704)

**605.3.** Washirika wanaohudumu katika majukumu ya uongozi wanaheshimika katika kiwango cha juu. Wakati tendo baya linatokea, uzito wake unakuwa mkubwa zaidi. Mtu aliye na hatia ya tendo baya ya kimapenzi linahusu watoto hastahili kuruhusiwa kuhudumu katika nafasi yoyote ya jukumu la au huduma ya watoto, au kuchaguliwa au kuteuliwa katika wadhifa wowote wa uongozi katika kanisa la mtaa. Mtoto anaelezwa kama mwanadamu yeyote aliye chini ya umri wa miaka 18, isipokuwa umri wa wengi uliopatikana baadaya chini ya sheria ya jamii ya taifa au nchi. (503.1)

## V. NIDHAMU YENYE UBISHI YA MHUDUMU

**606**. Kuendelea na uwezo wa Kanisa la Mnazareti kunategemea sana sifa za kiroho, tabia na hali ya maisha ya wahudumu wake. Wahudumu wana mwito wa hali ya juu na wanatenda kazi kama watu waliopakwa

mafuta ambao kanisa limewapa wadhifa wa kuaminika. Wanakubali kuitwa kwao wakijua kwamba watatakiwa kuwa na kiwango cha juu cha maadili na wale wanaowahudumia. Kwa sababu ya matarajio ya juu yaliyowekwa kwao, wahudumu na huduma yao wako katika hali ya uwazi zaidi kwa mashtaka yoyote ya kinidhamu. Kwa hivyo inabidi wahudumu kutumia taratibu zifuatazo pamoja na hekima ya kibiblia na ukomavu unaostahili watu wa Mungu.

**606.1.** Ikiwa mtumishi atashtakiwa kuwa vitendo vyake haviambatani na mhudumu, au anafundisha mafundisho ambayo hayalingani na mafundisho ya Kanisa la Mnazareti, mashtaka kama hayo yatatolewa kwa maandishi na yatatiwa sahihi na washiriki wasiopungua wawili wa Kanisa la Mnazareti ambao wakati huo watakuwa na msimamo mzuri. Mashtaka ya uzinzi au uasherati hayawezi kutiwa sahihi na mtu yeyote anayehusika na kosa linalodaiwa. Mashtaka yaliyoandikwa ni lazima yapelekwe kwa msimamizi wa wilaya ambaye atayawakilisha mashtaka hayo kwa Halmashauri ya Wilaya ambayo mshtakiwa ana ushirika wa huduma. Mashtaka hayo yatakuwa sehemu ya taarifa zitakazotolewa katika kesi hiyo.

Halmashauri ya Wilaya itampelekea mshtakiwa ilani iliyoandikwa haraka iwezekanavyo kwa njia yoyote ambayo inatoa ilani yenyewe. Wakati ilani yenyewe haitakuwa mwafaka, ilani inaweza kutolewa kwa hali ambayo ni ya kitamaduni kwa kutumika kama ilani ya kisheria katika sehemu hiyo. Mshtakiwa pamoja na wakili wake watakuwa na haki ya kuchunguza mashtaka na kupata nakala ya mashtaka hayo haraka iwezekananvyo ikihitajika. (540.4, 540.9.540.12)

**606.2** Sahihi ya mtu juu ya mashtaka dhidi ya mhudumu itakuwa thibitisho ya aliyeweka sahihi hiyo kuwa, kadri ya ufahamu wake, taarifa zilizotolewa ni za haki, na ya kwamba mashtaka yamesimama katika msingi wa ukweli. (540.4, 540.12)

**606.3** Mashtaka yalioandikiwa yanahifadhiwa na msimamizi wa wilaya yamewakilishwa kwa Halmashauri ya Wilaya, Halmashauri ya Wilaya itateua kamati ya makasisi watatu au zaidi kuchunguza ukweli na hali inayohusiana na mashtaka hayo na kutoa taarifa iliyoandikwa na kutiwa sahihi na wengi wa kamati hiyo. Ikiwa baada ya kuchunguza taarifa ya kamati hiyo, itaonekana kwamba kuna sababu za kutosha kwa mashtaka yaliyotolewa, sababu hizo zitaorodheshwa na kutiwa sahihi na makasisi wowote wawili waliowekwa wakfu. Halmashauri ya Wilaya itampelekea mshtakiwa ilani ya mashtaka hayo kwa njia yoyote inayotoa ilani yenyewe. Wakati ilani hiyo haina uhakika, ilani inaweza kutolewa katika hali ambayo ni ya kitamaduni kwa kutumika kama ilani za sheria katika sehemu hiyo.

Mshtakiwa pamoja na wakili wake watakuwa na haki ya kuchunguza mashtaka na jinsi yalivyoandikwa na kupata nakala ya mashtaka hayo mara tu wanapohitajika kujibu mashtaka hayo. Hakuna mshtakiwa yeyote atakayehitajika kujibu mashtaka ambayo hajajulishwa kulingana na utaratibu uliolezwa hapa. (225.3)

**606.4**. Ikiwa, baada ya uchunguzi itaonekana kuwa mashtaka dhidi ya mhudumu hayana ukweli kamili na kwamba yameeleweka vibaya, mashtaka yatatolewa kwa wale waliotia sahihi kwenye hati ya mashtaka ili hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yao.

**606.5.** Ikiwa mashtaka yaliyotolewa yamethibitishwa, Halmashauri ya Wilaya itateua makasisi watano na waumini wasiopungua wawili kadri wilaya itakavyoshauri ili kusikiliza kesi hiyo na kuamua juu ya masuala yanayohusika; watu hao waliotajwa watatengeneza Halmashauri ya Wilaya ya Nidhamu ambayo itasikiliza na kuamua kesi kulingana na sheria za kanisa. Hakuna kiongozi wa wilaya atakayehudumu kama mshtaki au msaidizi wa mshtaki katika kesi inayohusu kasisi au mhudumu aliyepewa hati. Halmashauri hii ya Nidhamu itakuwa na mamlaka ya kutetea haki ya mshtakiwa na kumuondolea mashtaka yanayodaiwa au kutoa adhabu kwa mshtakiwa akipatikana na hatia kulingana na kosa lililotendwa. Adhabu itakayotolewa inaweza kuwa kutakiwa kutubu, kuungama, kutoa fidia, kutengwa, kutolewa pendekezo la kufutwa kwa hati yake ya huduma, kufukuzwa au kuondolewa katika huduma au ushirika wa kanisa au vyote viwili, kukemewa hadharani au faraghani, au adhabu nyingine inayostahili ikiwa ni pamoja na kuahirisha adhabu wakati wa kujirekebisha ambao hauzidi mwaka mmoja. (225.4, 540.4, 540.12, 606.11-606.12)

**606.6.** Ikiwa aidha mshtakiwa au Halmashauri ya Wilaya itaomba hivyo, Halmashauri ya Nidhamu itakuwa Halmashauri ya Nidhamu ya Jimbo. Halmashauri ya jimbo itakayoshughulikia kila kesi itateuliwa na msimamizi mkuu mwenye mamlaka katika wilaya ambayo mhudumu aliyeshtakiwa ni mshiriki

**606.7.** Imeagizwa kwamba hakuna hatua yoyote ya kinidhamu itakayochukuliwa dhidi ya mmishenari katika wilaya ya kiwango cha kwanza.

**606.8** Uamuzi wa Halmashauri ya Nidhamu ni lazima ukubaliwe na wote, na ni lazima uwe umeandikwa na kutiwa sahihi na wajumbe wote wa halmashauri hiyo, na ni lazima uonyeshe kama mshtakiwa 'alipatikana na hatia' au 'hakupatikana na hatia' kwa kila shtaka na taarifa iliyotolewa dhidi yake.

**606.9.** Kusikilizwa kwa kesi yoyote na Halmashauri ya Nidhamu kama ilivyoelezwa hapa kutafanyika ndani ya wilaya ambayo mashtaka

yametolewa, mahali ambapo patachaguliwa na halmashauri itakayosikiliza mashtaka hayo.

**606.10.** Utaratibu wa kusikiliza kesi yoyote utakuwa kulingana na Kanuni za Utaratibu zilizoelezwa baada ya kifungu hiki. (225.3-225.4, 538.13, 609)

**606.11.** Mhudumu akishtakiwa kwa kitendo kisichostahili kutendwa na mhudumu na akubali kuwa ana hatia, au akiri kuwa na hatia bila ya kushtakiwa, Halmashauri ya Wilaya inaweza kukadiria mojawapo ya adhabu zilizotajwa katika kifungu cha 606.5. (540.4, 540.12)

**606.12.** Mhudumu akishtakiwa kuwa ana mwenendo usiostahili mhudumu, na akubali kuwa ana hatia au akiri kuwa na hatia kabla kuletwa mbele ya Halmashauri ya Nidhamu, Halmashauri ya Wilaya inaweza kukadiria mojawapo ya adhabu zilizoelezwa katika kifungu cha 606.5. (540.4, 540.12)

**607.** Kufuatia uamuzi wa Halmashauri ya Nidhamu, mshtakiwa, Halmashauri ya Wilaya, au wale waliotia sahihi mashtaka watakuwa na haki ya kukata rufani katika Mahakama Kuu ya Rufani. Rufani itaanza katika kipindi cha siku 30 baada ya uamuzi, na mahakama ya rufani itachunguza upya hati zote za kesi hiyo na hatua zote zilizochukuliwa. Ikiwa mahakama itagundua kosa lolote linalosababisha mtu yeyote asitendewe haki, itasahihisha kosa hilo kwa kuamuru kesi hiyo isikilizwe upya kwa njia ambayo itampa haki mtu aliyeadhiriwa na vikao au uamuzi uliotangulia.

**608.** Ikiwa uamuzi wa Halmashauri ya Nidhamu unaathiri mhudumu aliyeshtakiwa na uamuzi huo umeagiza mhudumu huyo atengwe na huduma ya kanisa au kufutwa kwa hati ya huduma, mhudumu aliyeshtakiwa ataacha mara moja kujihusisha na shughuli zote za huduma; na ikiwa atakataa kufanya hivyo atapoteza haki yake ya kukata rufani.

**608.1.** Ikiwa uamuzi wa Halmashauri ya Nidhamu umeagiza kutengwa na kufutwa kwa hati ya huduma na mhudumu aliyeshtakiwa anataka kukata rufani, atapeleka hati yake iliyoandikwa kama mhudumu kwa katibu wa mahakama ambayo itasikiliza rufani, wakati wa kupeleka ilani ya kutaka kukata rufani, hati yake iliyoandikwa kama mhudumu, na haki yake ya kukata rufani itakuwa ni sharti iambatane na matakwa ya kifungu hiki. Hati ya huduma ikipelekwa kwa njia hiyo, itawekwa salama na katibu anayehusika mpaka kesi imalizike. Kesi ikimalizika hati hiyo itarudishiwa mhudumu au itafutwa, kama vile mahakama itakavyoamuru.

**608.2.** Rufani katika Mahakama Kuu ya Rufani zinaweza kukatwa na mshtakiwa, au Halmashauri ya Nidhamu, kupinga uamuzi wa Mahakama ya Rufani ya Jimbo. Rufani hizo zitapelekwa katika mahakama hiyo kwa

kutumia kanuni na utaratibu unaotumiwa wakati wa kukata rufani zingine katika Mahakama Kuu ya Rufani.

## VI. KANUNI ZA UTARATIBU

**609**. Mahakama Kuu ya Rufani itatayarisha Kanuni za Utaratibu zilizo sawa zitakazotumiwa katika kesi zote zilizo mbele ya halmashauri za nidhamu na mahakama za rufani. Kanuni hizo zikishakubaliwa na kuchapishwa, zitakuwa ndiyo mamlaka ya mwisho katika utaratibu wa kisheria. Kanuni za Utaratibu zilizochapishwa zitagawanywa na katibu mkuu. Mabadiliko au masahihisho kwa kanuni kama hizo yanaweza kukubaliwa na Mahakama Kuu ya Rufani wakati wowote, na zitakapokubaliwa na kuchapishwa, zitaanza kutumika na kuwa mamlaka katika kesi zote. Hatua zozote zitakazochukuliwa baada ya hapo katika kesi yoyote zitakuwa kulingana na mabadiliko au masahihisho kama hayo. (606.1)

## VII. MAHAKAMA YA RUFANI YA WILAYA

**610.** Kila wilaya iliyoratibiwa itakuwa na Mahakama ya Wilaya ya Rufani yenye washirika wawili na makasisi watatu, akiwemo msimamizi wa wilaya, waliochaguliwa na kikao cha wilaya kulingana na kifungu cha 205.22. Mahakama hii itasikiliza rufani za washirika wa kanisa zinazohusu hatua yoyote ya halmashauri ya kanisa ya nidhamu. Ilani ya rufani ni lazima ipelekwe kwa maandishi katika kipindi cha siku 30 baada ya hatua hiyo au baada ya mtaka rufani kupata habari kuhusu hatua hiyo. Ilani hiyo itapelekwa kwa Mahakama ya Wilaya ya Rufani au kwa mojawapo wa wajumbe wake, na nakala ya ilani hiyo itapelekwa kwa mchungaji na kwa katibu wa halmashauri ya kanisa linalohusika. (205.22)

**610.1.** Mahakama ya wilaya ya Rufani itakuwa na mamlaka ya kusikiliza na kuamua rufani zote za washiriki au makanisa zilizoletwa kupinga uamuzi au hatua ya halmashauri ya Nidhamu iliyoteuliwa kumuadhibu mshiriki.

## VIII. MAHAKAMA KUU YA RUFANI

**611.** Kikao Kikuu kitachagua makasisi watano waliopewa wajibu watakaotumika kama wajumbe wa Mahakama Kuu ya Rufani kwa kipindi cha miaka minne, au hadi waandamizi wao watakapochaguliwa na kuhitimishwa. Mahakama hii itakuwa na mamlaka kama ifuatavyo:

**611.1.** Kusikiliza na kuamua rufani zote zitakazotokana na kitendo au uamuzi wa Halmashauri yoyote ya Wilaya ya Nidhamu au Mahakama ya

Jimbo ya Rufani. Rufani kama hizo zikishaamuliwa na mahakama hiyo, uamuzi huo utakubaliwa na utakuwa wa mwisho. (305.7)

**612.** Nafasi za kazi ambazo zinaweza kutokea katika Mahakama Kuu ya Rufani kabla ya mkutano utakaofuata wa Kikao Kikuu zitajazwa kwa uteuzi wa Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu. (317.6)

**613.** Malipo na gharama za matumizi ya wajumbe wa Mahakama Kuu ya Rufani yatakuwa sawa na yale ya wajumbe wa Halmashauri Kuu ya kanisa, wakati wajumbe wa mahakama hiyo wanapokuwa katika shughuli rasmi za mahakama, na malipo hayo yatalipwa na mtunza hazina mkuu.

**614**. Katibu mkuu ndiye atakayehifadhi kumbukumbu na taarifa zote za maamuzi ya Mahakama Kuu ya Rufani. (326.4)

## IX. MAHAKAMA YA JIMBO YA RUFANI

**615.** Kutapaswa kuwepo na Mahakama ya Jimbo ya Rufani katika kila jimbo. Kila Mahakama ya Jimbo ya Rufani itakuwa na makasisi watano au zaidi waliopewa wajibu ambao wamechaguliwa na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu baada ya kila mkutano wa Kikao Kikuu. Nafasi za kazi zitajazwa na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu. Kanuni za Utaratibu zitakazotumiwa na Mahakama ya Jimbo ya Rufani zitakuwa sawa na zile zitakazotumiwa na Mahakama Kuu ya Rufani, zilizoelezwa katika Kitabu cha mwongozo na Utekelezaji wa Nidhamu. Kundi la watu watano litahitajika kwa kutoa rufani itakayopelekwa mahakamani.

## X. HAKIKISHO LA HAKI

**616**. Haki ya kusikilizwa kwa makini na bila upendeleo kwa mashtaka yaliyotolewa dhidi ya mhudumu au mshiriki haitaondolewa au kuhairishwa bila sababu. Mashtaka yaliyoandikwa yatasikilizwa haraka iwezekanavyo ili kumuondolea hatia yule asiye na hatia na kumuadhibu mwenye hatia. Kila mshtakiwa atachukuliwa kuwa bila hatia hadi athibitishwe kuwa na hatia. Na kwa kila shtaka na dai, upande wa mashtaka utakuwa na jukumu la kuthibitisha hakika na bila mashaka yoyote kuwa mshtakiwa ana hatia.

**616.1.** Gharama ya kutayarisha kumbukumbu ya kesi ya mhudumu, ikiwa ni pamoja na ushahidi wote uliotolewa wakati wa kusikilizwa kwa kesi, kwa kusudi la kutaka rufani katika Mahakama Kuu ya Rufani, italipwa na wilaya ambayo kesi hiyo ilisikilizwa na hatua ya kinidhamu ikachukuliwa. Kila mhudumu atakayekata rufani atakuwa na haki ya kujitetea kwa maneno na pia kwa taarifa zilizoandikwa, lakini haki hiyo inaweza kutotumiwa na mshtakiwa akiomba hivyo kwa maandishi.

Gharama ya kutayarisha kumbukumbu ya kesi ya mshirika, ikiwa ni pamoja na ushahidi wote uliotolewa wakati wa kusikilizwa kwa kesi, kwa

kusudi la kutaka rufani katika Mahakama Kuu ya Rufani, italipwa na wilaya ambayo kesi hiyo ilisikilizwa na hatua ya kinidhamu ikachukuliwa. Kila mshirika atakayekata rufani atakuwa na haki ya kujitetea kwa maneno na pia kwa taarifa zilizoandikwa, lakini haki hiyo inaweza kutotumiwa na mshtakiwa akiomba hivyo kwa maandishi.

**616.2.** Mahakama ya juu ya mhudumu kutaka kukata rufani ni Mahakama Kuu ya Rufani, na mahakama kuu ya mshiriki kutaka rufani ni Mahakama ya Wilaya ya Rufani.

**616.3.** Mhudumu au mshiriki ambaye ameshtakiwa kwa kitendo kibaya au kwenda kinyume cha maagizo ya *Kitabu cha Mwongozo cha* kanisa na ambaye mashtaka yametayarishwa dhidi yake, atakuwa na haki ya kukutana na washtaki wake uso kwa uso na kuwahoji mashahidi wa upande wa mashtaka.

**616.4.** Ushuhuda wa shahidi yeyote mbele ya Halmashauri ya Nidhamu hautapokelewa au kufikiriwa katika ushahidi ikiwa ushuhuda huo haukutolewa kwa kiapo au hakikisho thabiti.

**616.5.** Mhudumu au mshiriki anayeletwa mbele ya Halmashauri ya Nidhamu kujibu mashtaka atakuwa na haki wakati wote ya kuwakilishwa na wakili au mtetezi wa chaguo lake, mradi tu mtetezi huyo awe ni mshiriki mwenye sifa nzuri katika Kanisa la Mnazareti. Mshiriki yeyote wa kanisa lililoratibiwa kwa utaratibu uliowekwa ambaye hakuna mashtaka yaliyoandikwa yameletwa dhidi yake atahesabiwa kuwa mwenye sifa nzuri.

**616.6.** Mhudumu au mshiriki hatahitajika kujibu mashtaka ya kitendo chochote kilichotokea zaidi ya miaka mitano kabla ya mashtaka hayo, na hakuna ushahidi wowote utakokubaliwa katika kesi yoyote unaohusu mambo yoyote yaliyotokea zaidi ya miaka mitano kabla ya mashtaka hayo kuletwa dhidi yake. Hata hivyo, iwapo mtu aliyedhurika na kitendo kama hicho alikuwa chini ya miaka 18 au alikuwa hana akili timamu za kuweza kuleta mashtaka dhidi ya mshtakiwa, kizuizi hicho cha miaka mitano hakitaanza kutumika hadi mlalamikaji atakapotimiza umri wa miaka 18 au amepata akili timamu. Ikiwa ni mashtaka ya kumnajisi mtoto mdogo, hakuna muda utakaowekwa wa kuzuia mashtaka kuletwa dhidi ya mshtakiwa. Mtoto mdogo anaelezewa kama mwanadamu yeyote aliye chini ya miaka 18, isipokuwa umri wa wengi utapatikana baadaye chini ya sheria ya taifa au nchi ya nyumbani.

Ikiwa mhudumu atapatikana na hatia katika mahakama iliyoundwa kulingana na sheria, atakabidhi hati zake kwa msimamizi wa wilaya. Kwa ombi la mhudumu huyo, na ikiwa Halmashauri ya Nidhamu haikuhusishwa, Halmashauri ya Wilaya itachunguza kesi hiyo na hukumu

iliyotolewa, na inaweza kurudisha hati hizo ikiwa itaonekana inafaa kufanya hivyo.

**616.7.** Mhudumu au mshiriki hatashtakiwa mara mbili kwa kosa moja. Hata hivyo, haitachukuliwa kuwa mtu huyo ameshtakiwa mara mbili kwa kesi yoyote ambayo mahakama ya rufani itagundua kuwa kosa lilitendeka wakati wa kusikilizwa kwa kesi hiyo mara ya kwanza mbele ya Halmashauri ya Nidhamu.

## SEHEMU YA VIII

# SAKRAMENTI NA TARATIBU

### MEZA YA BWANA UBATIZO WA WAUMINI

### UBATIZO WA WATOTO WACHANGA AU WATOTO WADOGO

### KUWEKWA WAKFU WATOTO WACHANGA AU KUWAPOKEA WATOTO WADOGO KATIKA USHIRIKA WA KANISA

### NDOA IBADA YA MAZISHI

### KUTAWAZWA KWA VIONGOZI WA KANISA

### KURATIBIWA KWA KANISA LA MTAA

## I. SAKRAMENTI YA UBATIZO

## 700. MEZA YA BWANA

Kuadhimishwa kwa meza ya Bwana kunaweza kutanguliwa na mahubiri yanayofaa na kusomwa kwa maandiko haya: 1 Wakorintho 11:23-29; Luka 22:14-20; au maandiko mengineyo. Halafu kasisi atatoa mwaliko ufuatao:

Ushirika Mtakatifu, ulioanzishwa na Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo ni sakramenti, ambayo inatangaza maisha Yake, Mateso Yake, kifo Chake cha dhabihu, na ufufuo, na tumaini la kuja Kwake tena. Unaonyesha kifo cha Bwana hadi kurudi Kwake.

Ushirika huu ni njia ya neema ambayo Kristo anawakilishwa na Roho. Unapaswa kupokelewa kwa heshima ya kuzingatiwa na shukrani kwa kazi ya Kristo.

Wale wote wanaotubu kwa kweli, wakizikana dhambi zao, na kuamini katika Kristo kwa ajili ya wokovu wanakaribishwa kushiriki katika kifo na ufufuo wa Kristo. Tunakaribia Meza ili tufanywe upya katika maisha na wokovu na kufanywa kuwa kitu kimoja na Roho

Katika umoja na Kanisa, tunakiri imani yetu: Kristo amekufa, Kristo amefufuka, Kristo atarudi tena. Na hivyo tunaomba:

Kasisi anaweza kufanya maombi ya toba na kujitoa, na kumaliza kwa sala ya kutakasa kama ifuatayo:

Mungu Mtakatifu,

Tumekusanyika hapa kwenye hii, meza yako, katika jina la Mwana, wako Yesu Kristo, ambaye kwa Roho Wako alipakwa mafuta kuhubiri habari njema kwa maskini, kuwatangazia mateka

uhuru wao, kuwafungua wanaodhulumiwa. Kristo aliwaponya wagonjwa, aliwalisha wenye njaa, alikula na wenye dhambi, na akaanzisha agano jipya ya msamaha wa dhambi. Tunaishi katika tumaini la kurudi Kwake tena.

Usiku ule aliotolewa, alitwaa mkate mkate, naye akiisha kushukuru, akaumega, akawapa wanafunzi Wake, na akasema: "Huu ndio mwili wangu unaotolewa kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu."

Na vivi hivi baada ya kula, Akakitwaa kikombe akiisha kushukuru, akawapa wanafunzi Wake, na akasema: "Kunyweni nyote. Hii ni damu yangu ya agano, jipya, iliyomwagika kwa ajili ya ondoleo la dhambi. Fanyeni hivyo kwa ukumbusho wangu." Katika jina la Yesu Kristo Bwana wetu. Amina.

(Mathayo 26:27-29, Luka 22:19)

Kwa hiyo, twaja kwako pamoja tukiwa Mwili wa Kristo tunajitoa kwako katika sifa na shukrani. Tumwagie Roho wako Mtakatifu na pia umwage juu ya sadaka hizi. Zifanye kwa nguvu za Roho mtakatifu wako kuwa kwetu mwili na damu ya Kristo, ili tuwe kielelezo ulimwenguni kwa ajili ya Mwili wa Kristo, uliokombolewa na damu Yake.

Kwa njia ya Roho wako utufanye tuwe kitu kimoja katika Kristo, kitu kimoja kwa kila mmoja wetu, na kitu kimoja na huduma ya Kristo ulimwenguni kote, hadi Kristo atakaporudi kwa ushindi wa mwisho. Katika jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, Amina.

Na sasa, kama vile Mwokozi wetu Yesu Kristo alivyotufundisha, na tuombe: (Hapa kusanyiko linaweza kuomba Sala la Bwana)

Baba yetu, uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako na uje, mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo riziki yetu. Utusamehe deni zetu, kama na sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu. Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu. Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina.

Kabla ya kuchukua mkate, kasisi aseme:

Mwili wa Bwana Yesu Kristo uliovunjwa unatufanya tusiwe na mawaa, hadi uzima ya milele. Kuleni mkate huu kwa kumkumbuka Kristo aliyetufia na tuwe na shukrani.

Kabla ya kuchukua kikombe kasisi aseme:

Damu ya Bwana wetu Yesu Kristo, iliyomwagika kwa ajili yenu, inatufanya tusiwe na mawaa, hadi uzima wa milele. Kunyweni kwa kukumbuka kwamba alikufa kwa ajili yetu, na tuwe na shukrani.

Baada ya watu wote kuchukua, mhudumu anaweza kufanya maombi ya shukrani ya kuhitimisha na kujitoa. (29.5, 515.5, 532.7, 533.2, 534.1)

KUMBUKA: Ni divai tu isiyo na chachu ndiyo inapaswa kutumiwa kwa sakramenti ya Meza ya Bwana.

## 701. UBATIZO WA WAUMINI

WAPENDWA: Ubatizo wa Kikristo ni sakramenti ya ishara ya kuamini katika kifo na ufufuo wa Yesu Kristo na kushirikishwa katika Mwili wa Wake, Kanisa. Ni njia ya neema ya kutangaza Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi.

Mtume Paulo anatangaza kwamba wale wote waliobatizwa katika Yesu Kristo wamebatizwa katika kifo Chake. Tunazikwa Naye kupitia katika ubatizo ili kwamba kama vile Kristo alifufuka kutoka katika wafu, nasi pia tunafufuliwa na kutembea katika upya wa maisha. Kama vile tulivyounganishwa Naye katika kifo Chake, tutaunganishwa pia Naye katika ufufuo Wake.

Imani ya Kikristo, ambayo kwake unakuja kubatizwa, inathibitishwa na Imani ya Mitume ambayo tunakiri:

Mhudumu anaongoza kongamano katika kuthibitisha kukiri kwa imani.

“Tunaamini katika Mungu Baba Mwenyezi, Muumba wa mbingu na nchi;

“Na katika Yesu Kristo, Mwanawe wa Pekee, Bwana wetu; ambaye aliposwa na Roho Mtakatifu, alizaliwa na Bikira Mariamu, aliteseka chini ya Pilato, alisulibiwa, akafa, na akazikwa; Alishuka kuzimu; siku ya tatu Alifufuka tena kutoka kwa wafu; Alipaa mbinguni, na ameketi mkono wa kuume wa Mungu Baba Mwenyezi; kutoka hapo Atakuja kuhukumu walio hai na wafu.

"Tunaamini katika Roho Mtakatifu, Kanisa Takatifu la Yesu Kristo, ushirika wa wateule, msamaha wa dhambi, ufufuo wa mwili, na uzima wa milele."

Je, utabatizwa katika imani hii?

*Jibu*: Nakubali.

"Unakiri kwamba Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi, na unaamini kwamba Alikuokoa?

*Jibu*: Ndio naamini.

Kama mshirika wa Kanisa la Yesu Kristo, je, utamfuata siku zote za maisha yako, ukikua katika neema na upendo wa Mungu na jirani?

*Jibu*: Nakubali kwa msaada kwa Mungu.

Mhudumu, baada ya kutaja majina yote ya anayebatizwa na kutumia fomu i~~i~~nayohitajika ya ubatizo-kunyunyiziwa, kumwagiwa, na kuzamishwa atasema:

________________, Nakubatiza katika jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina."

## 702. UBATIZO WA WATOTO WACHANGA AU WADOGO

*Wakati wadhamini watakapowasili pamoja na mtoto au watoto wao mbele ya kasisi, kasisi atasema:*

WAPENDWA: Sakramenti ya ubatizo ni ishara na hakikisho la agano jipya la neema. Ingawa hatuamini kwamba uabatizo huleta neema ya Mungu ya kuzaliwa mara ya pili, tunaamini kwamba ubatizo wa Kikristo unadhihirisha kukubaliwa na Mungu kwa mtoto huyu mdogo katika jamii ya imani ya Kikristo kwa misingi ya neema tangulizi. Inatazamia kukiri kwake binafsi kwa imani katika Yesu Kristo.

Kwa kumwasilisha mtoto huyu katika ubatizo mnathibitisha imani yenu ya Kikristo na kwamba nia yenu kuwa mtamuongoza katika maisha yake ya mwanzo ili amjue Yesu kama Mwokozi. Hadi wakati huo utakapofika ni jukumu lenu kumfundisha, mara tu atakapoweza kujifunza, namna na madhumuni ya sakramenti hii takatifu; kuilinda elimu yake ili asipotoshwe; kuongoza miguu yake mahali patakatifu; kumzuia kutokana na marafiki waovu na tabia mbaya; na kwa uwezo wenu wote, kumlea katika malezi na mausia ya Bwana wetu Yesu Kristo.

Je, mnakubali kufanya hayo yote kwa msaada wake Mwenyezi Mungu? Kama ndiyo, jibu, “Nakubali.”

*Mhudumu atawaomba wazazi au walezi kumpa mtoto jina; na atambatiza akirudia majina sahihi na kusema:*

______________Nakubatiza katika jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu. Amina.

*Mchungaji*: Ubatizo unathibitisha kukubalika kwa mtoto huyu katika jamii ya imani ya Kikristo. Sasa ninawauliza, waumini; je, mnakubali kwa Mwili wa Kristo kuwasaidia na kuwahimiza wazazi hawa wanapojitahidi kutimiza jukumu lao kwa mtoto huyu na kusaidia kwa kumlea kwa ukuaji wa kiroho?

*Jibu*: Nakubali.

Mhudumu anaweza kufanya maombi au anaweza kutumia maombi bila kujiandaa.

Baba yetu uliye mbinguni, kwa unyenyekevu tunaomba kwamba umtunze huyu mtoto katika mapenzi yako. Umjaze neema yako ya mbinguni, kutokana na majaribu ya ujana; muongoze katika kumjua Kristo kama Mwokozi; msaidie akuwe katika hekima na kimo na katika fadhili za Mungu na mwanadamu, na kustahimili katika imani hadi mwisho. Waimarishe wazazi wake ili wampe malezi ya upendo, ushauri wa busara na mfano mtakatifu ili waweze kutimiza wajibu wao kwa mtoto huyu na kwako. Katika jina la Yesu Kristo Mwokozi wetu. Amina.

# II. UTARATIBU

## 703. KUWEKA WAKFU WATOTO WACHANGA AU WADOGO

*Wakati wazazi au walezi wamefika pamoja na mtoto (au watoto) mhudumu atasema.*

"Ndipo akaletewa watoto wadogo ili aweke mikono yake juu yao na kuwaombea; wanafunzi wake wakawakemea. Lakini Yesu akasema, 'Waacheni watoto wadogo waje kwangu; wala msiwazuie; kwa maana walio mfano wa hao, ufalme wa mbinguni ni wao." (Mathayo 19:13-14).

Katika kumwasilisha mtoto huyu hapa ili awekwe wakfu, mnadhihirisha imani yenu katika imani ya Kikristo lakini pia mnatamani kwamba aweze kujua mapema mapenzi ya Mungu, aweze kuishi na kufa akiwa Mkristo, na kufikia baraka za milele mbinguni.

Ili kufikia kusudi hili takatifu, ni wajibu wenu kama wazazi (au walezi), kumfundisha kumcha Bwana mapema, kushughulikia elimu yake, ili asipotoshwe; kumuongoza katika utakatifu; kumzuia kutokana na marafiki wabaya na tabia mbaya; kuongoza mawazo yake ya ujana kwa Maandiko Matakatifu, na miguu yake mahali patakatifu; kumzuia na ushirikiano na tabia mbaya; na, na kwa uwezo wenu wote, kumlea katika malezi na mausia ya Bwana.

Je, mnakubali kufanya hayo yote kwa usaidizi wa Mungu? Kama ndiyo, *jibu*. "Nakubali".

*Mchungaji:* Sasa nawauliza ninyi waumini: Je, mnakubali kujitoa kama Mwili wa Kristo kuwasaidia na kuwahimiza wazazi hawa wanapojitahili kutimiza wajibu wao kwa mtoto huyu na kumsaidia katika malezi yake ili akue na kufikia upeo wa kiroho?

*Jibu*: Ndiyo twakubali.

*Mchungaji:* Baba yetu uliye mbinguni, tunakukabidhi _______________ (*jina la mtoto)* katika jina la Baba, na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Amina.

Hatimaye mhudumu anaweza kuomba maombi yafuatayo au anaweza kutumia maombi yake binafsi.

Baba yetu uliye mbinguni, kwa unyenyekevu tunakuomba umtunze mtoto huyu katika mapenzi yako. Umjaze neema yako ya mbinguni, umlinde vyema katika hatari za utotoni; umkomboe kutokana na majaribu ya ujana; umwongoze katika kumjua Kristo kama Mwokozi; msaidie akue katika hekima na kimo, na apate kibali kwa Mungu na kwa watu, na kustahimili hadi mwisho. Waimarishe wazazi wake kwa malezi ya upendo, ushauri wa busara na mfano mtakatifu ili waweze kutimiza wajibu wao kwa mtoto na kwako katika jina la Yesu Kristo Mwokozi wetu. Amina.

## 704. KUPOKEA RASMI WASHIRIKA WA KANISA.

*Inatarajiwa kwamba washirika wanaotarajiwa wamekiri imani ya Kikristo na wameelekezwa katika imani na desturi za Kanisa la Mnazareti. Wanaweza kuja mbele ya ya madhabahu ya kanisa na mchungaji atawahutubia kama ifuatavyo:*

WAPENDWA: Heshima na baraka ambazo tunazo katika kushirikiana pamoja katika kanisa la Yesu Kristo ni takatifu na za thamani kubwa. Kuna ushirika mtakatifu ambao hauwezi kupatikana mahali pengine ila kutoka kwa familia ya Mungu.

Kuna utunzaji wa kimungu wa wachungaji pamoja na mafundisho ya Neno na kuhimiza katika ibada ya ushirika. Na kuna ushirikiano katika huduma, ambao unatimiza yale ambayo hayangeweza kufanywa.

*Leo tunathibitisha tena imani na desturi za kanisa,

Tunamwamini Mungu mmoja-Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.

*Tunaamini kwamba mwanadamu amezaliwa katika dhambi; na kwamba anahitaji msamaha wa dhambi kupitia kwa Kristo na kuzaliwa mara ya pili kwa Roho Mtakatifu; na kwamba baada ya hayo kuna kazi nyingine muhimu ya kusafishwa kwa moyo au utakaso kamili kwa njia ya kujazwa na Roho Mtakatifu, na kwamba kwa kila moja ya kazi hizi za neema Roho Mtakatifu hushuhudia.*

*Tunaamini kwamba Bwana wetu Yesu Kristo atarudi, waliokufa watafufuliwa, na watu wote watasimama mbele ya hukumu ya mwisho ili kupata malipo au adhabu.*

*KUMBUKA: Mhudumu anaweza kutumia Taarifa ifuatayo Iliyokubaliwa ya Imani ya (kifungu cha 20 cha Manual) kama mbadala.

Leo tunathibitisha tena Taarifa Iliyokubalika ya Imani ya Kanisa la Mnazareti:

*Kwamba kuna Mungu mmoja-Baba, Mwana na Roho Mtakatifu; kwamba Maandiko ya Agano la Kale na Agano Jipya, yaliyoandikwa kwa pumzi kamili, yana ukweli wote unaohitajika kwa imani na maisha ya Kikristo; kwamba wanadamu wanazaliwa wakiwa na asili ya dhambi, na kwa hivyo, wana mvuto unaomwelekeza kwenye uovu na unaoendelea; kwamba wale waliokataa kutubu mwisho wao ni kupotea milele bila tumaini; kwamba upatanisho kupitia kwa Yesu Kristo ni kwa wanadamu wote; na kwamba yeyote anayetubu na kumwamini Bwana Yesu Kristo anahesabiwa haki na kuhuishwa kiroho na kuokolewa kutoka katika utawala wa dhambi; kwamba waumini wanapaswa kutakaswa kikamilifu, kufuatia kuhuishwa kiroho, kupitia imani katika Bwana Yesu Kristo; kwamba Roho Mtakatifu hushuhudia kuzaliwa upya na pia utakaso kamili wa waumini; kwamba Bwana wetu atarudi, wafu watafufuliwa, na hukumu ya mwisho itafanyika (Vifungu vya Manual vya 20.1-20.8)*

Je, unaamini ukweli huu wote kwa moyo mkunjufu? Kama ndiyo, jibu, “Naamini”.

Je, unamkiri Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wako, na unaamini kwamba anakuokoa sasa?

*Jibu:* Nakubali kwa imani.

Kwa kutaka kujiunga na Kanisa la Mnazareti, unaahidi kwamba unajitolea kumpenda Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote, kwa akili yako yote na kwa nguvu zako zote na kumpenda jirani kama unavyojipenda kama vile ilivyoelezwa katika Agano la Maadili ya Kikristo na Mienendo? Je, unajitolea katika utume wa Mungu kama vile ulivyoelezewa katika kanuni, ushirika, na kazi za Kanisa la Mnazareti? Je, utaunga mkono mafundisho ya Kanisa la Mnazareti na kutia bidii, kwa msaada wa Mungu, kukua katika ufahamu na desturi za Kanisa la Mnazareti katika njia ambayo inaimarisha ushuhuda wa kanisa? Je, utajitahili katika njia yote kumtukuza Mungu, kwa kutembea katika unyenyekevu, kuwa na mazungumzo ya kimungu, na ibada takatifu; kwa kujitolea na mali yako; na kuhusika kwa uaminifu katika njia ya neema? Je, utamfuata Yesu Kristo siku za maisha yako zote, ukiepuka na uovu, na kutafuta kwa uadilifu kukamilisha utakaso wa moyo na maisha katika kumwogopa Bwana?

*Jibu*: Nakubali.

*Mhudumu hatimaye atamwambia mtu au atawaambia watu:*

Ninakukaribisha (au nawakaribisha) katika Kanisa la Mnazareti na ushirika wake mtakatifu wa kusanyiko hili la mtaa pamoja na manufaa na majukumu yake. Na kiongozi Mkuu wa Kanisa akubariki na kukuhifadhi, na kukuwezesha kuwa mtiifu katika kazi zote nzuri, ili maisha yako na ushuhuda wako uwe mkamilifu katika

ulinzi wa maskini na wanaodhulumiwa na katika kuwaongoza wengine kwa Kristo.

**705. NDOA**

Katika kutambua mafundisho tofauti ya dunia na tamaduni kuhusu ndoa, Kanisa la Mnazareti linapendekeza kanuni zifuatazo:

- Usawa kati ya mume na mke
- Uhusiano wa agano unaoangazia uhusiano wa agano kati ya Kristo na kanisa Lake
- Matumizi ya lugha ambayo ni halali na ya heshima. Utaratibu huu hauondoi au kubalidilisha matakwa ya sheria ya nchi yoyote.

Sherehe inayofuata inatolewa kama raslimali.

Katika siku na wakati uliowekwa wa kufunganisha ndoa, watu wale watakaofunga ndoa-baada ya kukaguliwa kulingana na sheria, na kushauriwa ipasavyo na kuongozwa na mhudumu-watasimama pamoja mbele ya kasisi, mume upande wa kuume na mke upande wa kushoto wakimwangalia mhudumu, na mhudumu atatoa maelezo yafuatayo mbele ya kusanyiko kama ifuatavyo:

WAPENDWA: Tumekusanyika hapa pamoja mbele za Mungu na mbele ya mashahidi hawa, kuwaunganisha pamoja mwanamume huyu (Jina la Bwana arusi) na mwanamke huyu ((Jina la Bibi arusi) katika ndoa takatifu, ambayo ni ya hali ya heshima, iliyoagizwa na Mungu katika bustani la Edeni, ikidhihirisha umoja wa kimiujiza kati ya Kristo na kanisa Lake. Hali hii takatifu iliyotukuzwa na Mungu na kutakaswa na uwepo Wake na mwujiza wa kwanza aliotenda, katika Kana ya Galilaya, na mwandishi wa Waebrania akasema kuwa inastahili kuheshimiwa miongoni mwa watu wote. Kwa hivyo ni

muhimu hali hii ya ndoa isingiwe bila ushauri, heshima, busara, na kwa kumcha Mungu.

Katika hali hii takatifu ambayo watu hawa wanakuja kuunganishwa pamoja.

*Akiwahutubia wale wanaofunga ndoa, kasisi atasema:*

(Majina ya maarusi)___________ na ____________, ninawauliza na kuwaagiza ninyi wakati huu mnaposimama mbele za Mungu, mkumbuke kwamba ndoa ni uhusiano wa kudumu kati ya mwanamume na mwanamke. Ni mapenzi ya Mungu kwamba ndoa yenu itakuwa ya milele, na kwamba kifo pekee ndicho kitakachowatenganisha.

Ikiwa viapo mtakavyofanya leo vitadumishwa bila kuvunjwa, na ikiwa mtatafuta tu kujua na kutenda mapenzi ya Mungu, maisha yenu yatabarikiwa na nyumba yenu itakuwa na amani tele siku zote za maisha yenu.

*Baada ya maagizo hayo, mhudumu atamwambia mwanamume:*

(Jina la mwanamume)_______________, Je, utamkubali mwanamke huyu kuwa mke wako wa ndoa, mkaishi pamoja baada ya agizo hili la Mungu katika utakatifu wa ndoa? Je, utampenda, na kumtunza, na kumheshimu pamoja na kumfurahisha na kumfariji, na kuwa pamoja naye wakati wa magonjwa na wakati wa uzima? Je, utawaepuka wengine wote na kuwa naye pekee wakati wote mtakapokuwa hai?

*Jibu:* Ndiyo, nakubali

*Kisha atamwambia mwanamke:*

(Jina la Mwanamke) _______________, Je, utamkubali mwanamume huyu kuwa mume wako wa ndoa, mkaishi pamoja baada ya agizo hili la Mungu katika utakatifu wa ndoa? Je, utampenda, na kumtunza, na kumheshimu pamoja na kumfurahisha na kumfariji, na kuwa pamoja naye wakati wa magonjwa na wakati wa uzima? Je, utawaepuka wengine wote na kuwa naye pekee wakati wote mtakapokuwa hai?

*Jibu*: Ndiyo, nakubali.

*Kisha mhudumu atauliza:*

Je, ninyi kama (wazazi wa bibi arusi na bwana arusi, washirika wa familia, na/au washirika wa familia ya Mungu) mtawapa hawa maarusi msaada na baraka zenu?

*Jibu* (kutoka kwa wazazi wa bibi arusi na bwana arusi, washirika wa familia, na/au washirika wa familia ya Mungu): Ndiyo tunakubali.

*Wakiwa wanatazamana na wameshikana mikono, maarusi watabadilishana maagano yafuatayo:*

Mwanaume atafuatisha maneno ya kasisi:

Mimi (Jina la mwanamume) ____________, ninakubali na kukuchukua (Jina la mwanamke) ______________, uwe mke wangu wa ndoa, kuwa nawe kuanzia leo na kuendelea, kwa mema na mabaya, kwa utajiri na umaskini, katika ugonjwa na katika uzima, nitakupenda na kukutunza, hadi kifo kitakapotutenganisha, kulingana na agizo takatifu la Mungu; na kwa imani yangu ninaahidi.

*Bibi arusi naye pia atafuatisha maneno ya kasisi:*

Mimi (Jina la mwanamke) ___________ nakuchukua (Jina la mwanamume) ____________, uwe mume wangu wa ndoa, kuwa nawe kuanzia leo na kuendelea kwa mema na mabaya, kwa utajiri na umaskini, katika ugonjwa na katika uzima, nitakupenda na kumtunza, hadi kifo kitakapotutenganisha, kulingana na agizo takatifu la Mungu na kwa imani yangu ninaahidi.

*Kama ikihitajika, sherehe ya kuvishana pete inaweza kufanyika wakati huu. Mhudumu atapokea pete kutoka kwa msimamizi wa bwana-arusi na kisha atampa bwana-arusi. Wakati bwana-arusi anamvalisha bibi-arusi pete, atasema maneno haya baada ya mhudumu:*

Ninakupa pete hii kama ishara ya upendo wangu kwako na kama ahadi ya uaminifu wangu katika ndoa yetu."

*Marudio ya sherehe ya pili ya pete.*

*Maarusi hatimaye watapiga magoti mhudumu atakapoomba maombi yafuatayo, au atatumia maombi yake mwenyewe:*

Ee Mungu Uishiye Milele, Muumba na Mhifadhi wa vyote, Mpaji wa neema ya kiroho, Mwenye uzima wa milele, tuma baraka Zako juu ya hawa watumishi Wako, (Jina la Bwana-arusi) na (Jina la Bibi-arusi, ambao tunawabariki sasa kwa jina lako; ili waweze kutekeleza na kudumisha agano walilofanya kati yao wakati huu na waweze kubaki katika upendo na amani pamoja, katika jina la Yesu Kristo Bwana wetu. Amina.

*Baada ya hayo, mhudumu atasema:*

Kwa vile mwanamume huyu na mwanamke huyu wamekubali kuishi pamoja katika ndoa takatifu, na wameshuhudia mbele za

Mungu na umati huu, na wamekubaliana kwa kushikana mikono, natangaza kwamba kuanzia sasa wao ni mke na mume katika jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Wale ambao Mungu amewaunganisha pamoja mwanadamu asije akawatenganisha. Amina.

*Baadaye Mhudumu atawabariki kwa maneno haya:*

Mungu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, awabariki, awahifadhi, na awatunze; Bwana wa rehema awakirimie fadhili zake na awajaze na neema za kiroho. Mwishi pamoja katika maisha haya hapa ulimwenguni kwa njia ambayo katika ulimwengu ujao mtapata uzima wa milele.

Baada ya wote kushirikishwa, kasisi anaweza kufanya maombi ya kurudisha shukrani kwa mwenyezi Mungu. (532.7, 533.2, 534.1, 538.19)

## 706. IBADA YA MAZISHI

WAPENDWA: Tumekusanyika hapa leo kutoa heshima zetu za mwisho kwa mpendwa na rafiki yetu aliyetuaga. Kwenu ninyi mnaoomboleza kifo cha mpendwa wenu, tunawapa pole sana. Hebu tushirikiane pamoja katika Neno la Mungu ambalo hutuliza mioyo na kuleta faraja wakati kama huu wa huzuni.

"Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu; niamininі na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu" (Yohana 14:1-3).

"Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi; naye kila aishiye na kuniamini hatakufa kabisa hata milele" [Yohana 11:25-26]

SALA (*kwa maneno ya mhudumu mwenyewe au kwa maneno yafuatayo*):

Mwenyezi Mungu, Baba yetu uliye Mbinguni, twaja mahali hapa patakatifu na huzuni, tukitambua kutegemea kwetu Kwao. Twajua kwamba unatupenda na unaweza kubadili giza la mauti kuwa nuru ya asubuhi. Tusaidie sasa kukungojea kwa unyenyekevu na kwa mioyo ya uvumilivu.

Wewe ndiye Kimbilio na Nguvu zetu, Mungu wetu, wewe uliye Faraja wakati wa shida. Tujalie rehema Yako kwa wingi. Wale wanaomboleza leo wapate faraja na uponyaji wa kiroho katika

neema Yako inayodumisha. Tunaomba haya yote kwa unyenyekevu katika jina la Bwana wetu Yesu Kristo. Amina.

WIMBO AU PAMBIO WIMBO MAALUM

SEHEMU YA MAANDIKO MATAKATIFU:

"Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo! Katika rehema zake nyingi alituzaa mara ya pili ili tupate tumaini lenye uzima kwa kufufuka kwa Yesu Kristo katika wafu, tupate na urithi usioharibika, usio na uchafu, usionyauka. Urithi uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu, nanyi mnalindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya imani hata mpate wokovu ulio tayari kufunuliwa wakati wa mwisho. Mnafurahi sana wakati huo, ijapokuwa sasa kwa kitambo kidogo, ikiwa ni lazima, mmehuzunishwa kwa majaribu ya namna mbali mbali; ili kwamba kujaribiwa kwa imani yenu, ambayo ina thamani kuu kuliko dhahabu ipoteayo, ijapokuwa hiyo hujaribiwa kwa moto, kuonekana kuwakwenye sifa na utukufu na heshima, katika kufunuliwa kwake Yesu Kristo. Naye mwampenda, ijapokuwa hamkumwona; ambaye ijapokuwa hamwoni sasa, mnamwamini; na kufarahi sana, kwa furaha isiyoneneka, yenye utukufu, katika kuupokea mwisho wa imani yenu, yaani, wokovu wa roho zenu" (1 Petro 1:3-9)

(Vifungu vingine ambavyo vinaweza kutumiwa ni: Mathayo 5:3-4, 6, 8; Zaburi 27:3-5, 11, 13-14; 46:1-6, 10-11)

UJUMBE/MAHUBIRI

WIMBO AU PAMBIO MAALUM

MAOMBI YA KUFUNGA

* * *

**KANDO YA KABURI**

*Baada ya waombolezaji kukusanyika pamoja, mhudumu anaweza kusoma baadhi au vifungu vyote vya maandiko matakatifu kama ifuatavyo:*

"Lakini mimi najua ya kuwa mteteaji wangu yu hai, na ya kuwa hatimaye atasimama juu ya nchi, na baada ya ngozi yangu kuharibiwa hivi, lakini, pasipokuwa na mwili wangu nitamwona Mungu; nami nitamwona mimi nafsi yangu, na macho yangu yatamtazama, wala si mwingine" (Ayubu 19:25-27).

"Angalieni, nawaambia nyinyi siri, hatutalala sote, lakini sote tutabadilika, kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho; maana parapanda italia, na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika…

"Basi huu uharibikao utakapovaa kutokuharibika, na huu wa kufa utakapova kutokufa, hapo ndipo litakapokuwa lile neno lililoandikiwa, Mauti imemezwa kwa kushind. Ku wapi, ewe mauti; kushind kwako? U wapi, ewe mauti, uchungu wako? Unchungu wa mauti ni dhambi, na nguvu za dhambi ni torai. Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo.

"Basi ndugu zangu wapendwa, mwimarike, msitikisike, mkazidi sana kutenda kazi ya Bwana siku zote, kwa kuwa mwajua ya kwamba taabu yenu siyo bure katika Bwana." (1 Wakorintho 15:51-52, 54-58)

“Naikasikia sauti kutoka mbinguni ikisema, andika, Heri wafu wafao katika Bwana tangu sasa, naam, asema Roho, wapate kupumzika baada ya taabu zao; kwa kuwa matendo yao yafuatana nao.” (Ufunuo wa Yohana 14:13)

*Baada ya kusoma maandiko hayo, kasisi atasoma mojawapo ya taarifa hizi za mazishi:*

*Kwa Muumini:*

Kwa vile roho ya mpendwa wetu aliyetuaga imerudi kwa Mungu, ambaye aliyetoa, tunauweka mwili wake katika kaburi tukiwa na tumaini la ufufuo wake kutoka kwa wafu na uzima mpya katika ulimwengu ujao kwa imani katika Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye atatupatia miili mipya ya utukufu kama mwili wake. “Wamebarikiwa wale wanaokufa katika Bwana”.

*Kwa asiye Muumini:*

Tumekuja kuuzika mwili huu wa rafiki yetu aliyetuaga ili urudi katika udongo ambako ulitoka. Roho yake tunaiacha kwa Mungu, kwa maana yeye ni hakimu mwenye huruma nyingi, atafanya kama ipasavyo. Nasi tuliobaki tujitoe upya kumcha na kumpenda Mungu, ili tuweze kuigia katika ufalme wa mbinguni.

*Kwa Mtoto:*

Kwa hakika na dhana dhahiri ya ufufuo kwa uzima wa milele kupitia Bwana wetu Yesu Kristo, tunauzika mwili wa mtoto huyu kaburini. Na Yesu alivyowachukua watoto mikononi mwake na akawabariki akisema, “Kama hawa ndio ufalme wa mbinguni”.

*SALA:*

Baba yetu wa mbinguni, Mungu mwenye rehema yote, tunakutazamia wakati huu wa uchungu na machozi. Wafariji hawa wapendwa ambao wana mioyo mizito na huzuni. Uwe pamoja nao, uwalinde na uwaongoze katika siku zijazo. Wakubalie Bwana ili waweze kupenda na kukutumikia na kupokea ahadi zako katika dunia ijayo.

“Basi, Mungu wa amani, ambaye alimleta tena kutoka kwa wafu mchungaji mkuu wa kondoo, kwa damu ya agano la milele, yeye Bwana wetu Yesu, awafanye ninyi kuwa wakamilifu katika kila tendo jema, mpate kuyafanya mapenzi yake; naye akifanya ndani yetu lipendezalo mbele zake, kwa Yesu Kristo; utukufu una yeye milele. Amina” (Waebrania 13:20-21)

## 707. KUTAWAZWA KWA VIONGOZI WA KANISA

*Baada ya wimbo ufaao, mhudumu asome majina na wadhifa wa viongozi watakaotazwa. Hawa wanaweza kuja mbele na kusimama karibu na madhabahu ya kanisa, wakimwangalia kasisi. Hati ya agano itolewe kwa kila mmoja wao. Kasisi au padre au mchungaji atasema:*

Kwa kutambua njia ya Mungu ya kuwateua watumishi fulani kwa sehemu zinazojulikana na utumishi wa Kikristo, tunajua wakati huu wa kutawazwa kwa viongozi hawa (na/au waalimu) ambao wamechaguliwa watumike katika kanisa yetu mwaka unaofuata. Ebu basi tusome j maagizo ya Mungu kwetu kutoka katika neno lake takatifu.

"Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyohai, takatifu ya kupendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana wala msifuate namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanya upya nia zenu, mpate kujua, hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza na ukamilifu" (Warumi 12:1-2)

''Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiya na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli.'' (2 Timotheo 2 :15).

"Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za mioyoni mwenu". (Wakolosai 3:16)

"Mwanafunzi na amshirikishe mkufunzi wake katika mema yote". (Wagalatia 6:6).

Sasa tunakuja kwa wakati huu muhimu ambapo mwasimama madhabahuni kuchukua jukumu la kutumikia kanisa na Huduma ya Mnazareti ya Misheni ya Kimataifa, Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, na Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa. Mwaombwa kuangalia wadhifa mnaochukua sasa kama nafasi muhimu ya kazi ya Bwana na mpate furaha na baraka za kiroho katika kutekeleza majukumu yenu.

Yenu si kazi rahisi kwa sababu kuendelea kwa kanisa na hatima ya mioyo yote si katika mikono yenu. Maendeleo ya tabia za Kikristo yamo mikononi mwenu au ni jukumu lenu na kuwaongoza wale ambao hawajaokoka kumfikia Yesu Kristo ndilo jukumu lenu kubwa. Mungu awajalie hekima na uwezo mtakapokuwa mkifanya kazi yake kwa utukufu wake.

Mmepewa kadi iliyo na ahadi. Tutasema kwa pamoja na tunayofanya hivyo, tuifanye iwe ahadi ya kibinafsi.

## AGANO LA WATUMISHI WA KANISA

Kwa kuzingatia imani ambayo kanisa limeweka kwangu kwa kunichagua kuendesha kazi ninayochukua sasa au wadhifa ninaochukua sasa, naahidi:

Kudumisha viwango vya juu vya maisha ya Kikristo na mfano kufuatana na ufahamu na viwango vya Kanisa la Mnazareti.

Kukuza ujuzi wangu wa kibinafsi wa Kikristo kwa kutenga kila siku muda wa maombi na kusoma biblia.

Kuwa daima katika Shule ya Jumapili, kuhudhuria ibada kila Jumapili na ibada za mahubiri ya jioni ya Jumapili, na maombi ya katikati ya juma bila kukosa ila tu pale ambapo hali itanizuia.

Kuhudhuria kwa uaminifu mikutano yote ya halmashauri mbali mbali, mabaraza, au kamati ambazo nimekuwa mshirika ama nitakazopewa jukumu juu yake.

Kumjulisha kiongozi wangu mkuu iwapo sitaweza kuhudhuria muda uliopendekezwa au sitaweza kutimiza jukumu langu katika huduma hii wakati fulani.

Kusoma kwa upana nakala dhehebu, na vitabu vinginevyo na fasihi itakayonisaidia kutekeleza wajibu wangu katika uongozi wangu au katika kazi yangu.

Kujiendeleza na ujuzi wangu kwa kushiriki katika kazi za kawaida jinsi ambavyo nafasi itakavyopatikana.

Kujitahidi kuwaongoza watu kwa Yesu Kristo kwa kuonyesha bidii katika mambo ya wengine ya kiroho na kwa kuhudhuria na kusaidia mikutano yote ya uinjilisti katika kanisa.

Mhudumu kisha atato maombi mwafaka na wimbo ulioteuliwa unaweza kuimbwa na baadaye atasema:

Baada ya kuahidi pamoja mioyo na mikono yenu kutoa kwa kazi ya kanisa katika majukumu yetu hapa, basi mimi nawatawaza katika nafasi mbali mbali ambazo mmechaguliwa kuanza au mmeteuliwa. Sasa nyinyi mu sehemu moja muhimu mno ya ushirika na maongozi ya kanisa hili. Hivyo basi mumekuwa mfano wa bustani ya Bwana.

*Mhudumu atawauliza waumini kusimama na atawambia ifuatavyo:*

Mmesikia ahadi na agano ambalo limefanywa na viongozi wenu wa mwaka ujao. Sasa nawaagiza, kama waumini kuwa waumini katika msaada wenu kwao mizigo ambayo tumetwika ni mizito na itahitaji usaidizi na maombi yenu nyote basi muwe watu wa kuelewa shida zao na wavumilivu kwa udahifu wao. Toeni usaidizi kwa moyo mkunjufu mnapoombwa ili tunapofanya kazi pamoja, kanisa letu laweza kuwa chombo muhimu katika kuwavuta wapotevu kwa Kristo.

*Mhudumu kisha anaweza kuongoza maombi ya kufunga au awaambie kongamano kurudia Sala la Bwana kwa pamoja.*

## 708. URATIBISHAJI WA KANISA LA MTAA

*Msimamizi wa Wilaya:* Wapendwa katika Kristo, tumekusanyika katika Siku hii ya Bwana kwa lengo maalum ya kuratibu rasmi (jina la kanisa) Kanisa la Mnazareti. Hakika ninyi tayari ni kanisa lakini leo katika uhai wa kusanyiko hili mnasonga kwa kiwango kipya mnapokumbatia haki, nafasi, na majukumu ya kongamano lililoratibiwa kulingana na Katiba na kanuni za Kanisa la Mnazareti.

Kwa niaba ya familia ya Wanazareti ulimwenguni, ninawapongeza kwa maono yenu, imani yenu, na kazi yenu ya uadilifu kama vile mmefanya kazi pamoja bega kwa bega na moyo mmoja kuwa jamii yenye imani ambayo inaishi kama kielelezo halisi cha ufalme wa Mungu ulimwenguni. Kwa tendo hili la kuratibiwa, mnatangazi nia yenu kushiriki pamoja na familia ya ulimwengu ya Wanazareni katika kutimiza misheni yetu moja: “kuwafanya wanafunzi katika mataifa.”

Misingi mitatu ya muhimu inatuongoza katika utume huu:

Sisi ni watu Wakristo. Tunasimama na Wakristo popote pale kukiri imani ya kihistoria ya Utatu Mtakatifu, na thamani  kwa kina na urithi wetu wa kipekee wa utamaduni wa utakatifu wa Wesley. Tunatazamia Biblia kama inavyomtangaza Kristo kwetu, na “mambo yote yaliyo muhimu kwa ajili ya wokovu wetu”.

Sisi ni watu Watakatifu. Tunaamini kwamba neema ya Mungu inatoa sio msamaha wa dhambi tu bali pia kusafishwa kwa mioyo

kwa imani. Kwa tendo hili la neema ya Roho Mtakatifu, tunatakaswa na kutiwa nguvu za kuishi maisha ya Kikristo ulimwenguni.

Sisi ni watu wa Utume. Tunaamini Mungu ametuita kushiriki katika utume wa kifalme wa upatanisho. Tunafanya hilo kwa kuhubiri injili, kwa mateno ya huruma na haki na kwa kufanya wafuasi wa Kristo kufuata njia za Yesu.

*Msimamizi wa Wilaya kwa mchungaji:* Mchungaji, unaweza sasa kuwasilisha watu ambao watakuwa washirika hai wa (jina la kanisa) Kanisa Mnazareti

*Mchungaji:* (jina la msimamizi wa wilaya), ni heshima yangu kuwasilisha kwako washirika walio hai wa kanisa hili. Ninawaleta kwako kama ndugu wa kike na kiume katika Kristo waliojitoa kutimiza utume wetu wa pamoja kama washirika wa Kanisa la Mnazareti.

*(Mchungaji atasoma majina au kutambulsiha kila mshirika au jamii)*

*Msimamizi wa Wilaya*: Ndugu wa kike na wa Kiume, nawaomba sasa mthibitishe viapo vyenu vya ushirika.

Je, mnakubali Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi, na mnaamini kwamba Anawaokoa sasa?

*Jibu:* Ninakubali kwa imani.

Je, mnathibitisha kuamini Taarifa Iliyokubaliwa ya Imani ya Kanisa la Mnazareti?

*Jibu*: Ninakubali.

Je, mnaweka agano la kujitoa katika ushirika na kazi ya Mungu kwa kuungana na Kanisa la Mnazareti kama ilivyo katika Agano la Maadili ya Kikristo na Agano la Tabia ya Kikristo? Je, mtajitahidi katika njia zote kumtukuza Mungu kwa kwenda kwa unyenyekevu, kunena kwa wema, na huduma takatifu; kwa kujitoa kwa matoleo yenu; kwa mahudhurio ya uaminifu juu ya njia ya neema; na, kujitenga na maovu yote, mtatafuta kwa kweli kukamilisha utakatifu wa moyo na maisha katika heshima ya Bwana?

*Jibu*: Nakubali

*Msimamizi wa Wilaya:* Kwa hivyo, kwa mamlaka niliyopewa kama msimamizi wa wilaya (jina la wilaya) ya Kanisa la Mnazareti, ninatangaza kuratibiwa rasmi kwa (jina la kanisa) Kanisa la Mnazareti. Karibuni katika familia ya Wanazareti ulimwenguni. Na Bwana kwa neema yake kubwa awawezeshe kila siku na vitu vyote vizuri vya kutenda mapenzi yake. Na amani ya Kristo iwe nanyi.

## 709. KUWEKA KANISA WAKFU

*Mhudumu*: Baada ya kufanikishwa na mkono wa Bwana na kuwezeshwa kwa neema na uwezo wake kulimaliza jengo hili kwa utukufu Wake, sasa twasimama mbele zake na kuliweka jengo hili wakfu kwa matumizi na kazi ya ufalme wake.

Kwa utukufu wa Mungu Baba yetu ambaye kwake ndiko kipaji chema na bora zaidi hutoka, kwa heshima ya Yesu Kristo Bwana na Mwokozi wetu; na kwa utukufu wa Roho Mtakatifu, ambaye ndiye Chanzo cha nuru, uzima na nguvu zetu-Mtakasaji wetu.

*Waumini:* Sasa kwa furaha na shukrani twalitoa jengo hili kwa unyenyekevu.

*Mhudumu*: Kwa ukumbusho wa wale wote ambao wamependa na kutumikia kanisa hii kwa kuweka urithi ambao tunafurahia sasa na ambao ni sehemu mojawapo ya Ushindi wa Kanisa,

*Waumini:* Kwa shukrani sasa twatoa sehemu hii teule, (jengo la elimu, ukumbi wa ushirika, na kadhalika.)

*Mhudumu:* Kwa ibada ya maombi na wimbo, kwa kuhubiriwa kwa Neno, kwa mafundisho ya Maandiko, na kwa ushirika wa watakatifu,

*Waumini:* Kwa dhati twalitoa kiheshima jengo hili la Mungu.

*Mhudumu*: Kwa faraja ya wale wote wanaolia, kwa kuwastawisha wanyonge, kwa msaada wa wale wote wanaojaribiwa, na kwa kutoa matumaini na ujasiri kwa wale wote wanaokuja kati ya kuta hizi.

*Waumini:* Twaweka wakfu mahali hapa pa ushirika na maombi.

*Mhudumu:* Kwa kushiriki katika habari njema ya wokovu kutoka dhambini, kwa kueneza utakatifu wa maandiko, kwa kutoa maagizo katika haki, na kwa utumishi kwa watu wetu.

*Waumini:* Twaliweka jengo hili wakfu kwa heshima.

*Wote:* Kwa sauti moja: Sisi, kama wafanyakazi pamoja na Mungu, sasa twaungana mikono yetu na mioyo yetu na kujitoa upya kwa makusudi ya juu na takatifu ambayo jengo hili limetengewa.. Tunaahidi kujitolea kwa uaminifu usimamizi na uaminifu na utumishi mwema hadi mwisho na kwamba katika mahali hapa jina la Bwana litatukuzwa na ufalme Wake utaendelezwa katika Yesu Kristo Bwana wetu. Amina.

## SEHEMU YA TISA

# MKATABA NA MIPANGO YA HUDUMA/KATIBA/ SHERIA

### HUDUMA YA VIJANA WA MNAZARETI WA KIMATAIFA

### HUDUMA YA MISHENI YA MNAZARETI YA KIMATAIFA

### HUDUMA ZA SHULE YA JUMAPILI NA UANAFUNZI ZA KIMATAIFA

## I. HUDUMA YA VIJANA WA MNAZARETI WA KIMATAIFA

## 810. MKATABA WA HUDUMA YA VIJANA WA MNAZARETI YA KIMATAIFA

*"Mtu awaye yote asiudharau ujana wako, bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi na mwenendo, na katika upendo na imani na usafi" 1 Timotheo 4:12*

**810.1 Misheni Yetu**

Misheni ya huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ni kuita kizazi chetu kwa maisha ya mwenendo wa Kristo.

**810.2 Washirika Wetu**

Ushirika katika Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa unajumlisha watu wote wanaohusika katika huduma ya Vijana wa Mnazareti ambao wamechagua kukumbatia maono na thamani zetu zilizoelezewa.

**810.3 Maono Yetu**

Kanisa la Mnazareti linaamini kwamba vijana ni sehemu ndogo ya Kanisa. Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ipo ili kuwaongoza vijana katika uhusiano wa maisha marefu na Yesu Kristo na kurahisisha kukua kwao kama wanafunzi wa huduma ya Kikristo.

**810.4 Thamani Zetu**

1. Tunawathamini Vijana … wa muhimu katika ufalme wa Mungu.
2. Tunathamini Biblia . . . Ukweli wa Mungu usiobadilika wa maisha yetu.
3. Tunathamini Maombi . . . mawasiliano ya muhimu sana na Baba yetu wa mbinguni.
4. Tunathamini Kanisa . . . jamii takatifu ya imani ulimwenguni, yenye tamaduni tofauti bali moja katika Kristo.
5. Tunathamini Ibada . . . mkutano wa mabadiliko ya maisha na Mungu wa undani.
6. Tunathamini ***Uanafunzi*** . . . mtindo wa maisha wa kuwa (kama)Kristo.

7. Tunathamini *Jamii* . . . kujenga uhusiano ambao unasaidia kutuunganisha pamoja na kutuunganisha na Mungu.
8. Tunathamani ***Huduma*** . . . Kueneza neema ya Mungu kwa ulimwengu.
9. Tunathamini ***Ushuhuda*** . . . kushiriki upendo wa Mungu kwa maneno na matendo.
10. Tunathamini ***Utakatifu*** . . . kazi ya neema ambayo Mungu, kuptia kwa kufanya kazi ya Roho Wake Mtakatifu, anatuwezesha tuishi tukimwakilisha Kristo kwa kuwa sisi ni nani na katika kila jambo tunalofanya.

Thamani hizi ni maeneno muhimu sana ya maisha matakatifu na yanafaa kudhihirishwa katika maisha na Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa katika kila kiwango cha kanisa. (Tafadhali rejelea kanuni ya Imani katika *Kitabu cha Mwongozo cha Kanisa la Mnazareti* kwa maelezo zaidi juu ya thamani hizi.) Katika kuangazia thamani hizo, tunakubali kanuni zifuatazo za Uongozi.

**810.5 Kanuni Zetu za Uongozi**

1. ***Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ipo kwa ajili ya vijana.***
   Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ipo kwa kuwavutia, kuwaandaa, na kuwawezesha vijana kwa ajili ya huduma katika ufalme wa Mungu na kurahisisha mwunganiko wao katika Kanisa la Mnazareti.
2. ***Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa huangazia Kristo.***
   Kristo ndiye sehemu kuu ya kuwa sisi ni nani, Neno la Mungu chanzo cha mamlaka ya yote tunayofanya, na utakatifu mtindo wetu wa maisha.
3. ***Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa imejengwa juu ya huduma ya vijana katika kanisa la mtaa.***
   Huduma imara kwa vijana katika kanisa la mtaa ni muhimu kwa ajili ya afya na msisimko wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa. Uhusiano na huduma za mwili wa mwanadamu zinaunda msingi wa huduma ya vijana ya wa Mnazareti, ikiongoza vijana kwa ukomavu wa kiroho ndani ya Kristo.
4. ***Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa huwajenga na kuwashauri viongozi.***

Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa hutoa nafasi kwa viongozi wanaoibuka ili kujenga na kutumia vipawa vyao ndani ya mazingira ya malezi na usaidizi, wakihakikisha uongozi wenye nguvu wa Kanisa la Mnazareti. Mafundisho ya uongozi, kuwajibika, na utathmini wa utaratibu na mabadiliko ya huduma ni vifaa muhimu vya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.

5. ***Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa inawezeshwa kuongoza.***
   Huduma ya vijana inayohusika inahitajika kwamba jukumu la huduma na uamuzi uliopangwa uwe na uongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na halmashauri inayotawala iliyoidhinishwa kwa kila kiwango. Hali ya kuwa nayo na kumiliki, tamaa ya huduma, na kutumika katika kufanya uamuzi ni vipengele muhimu vya kuwawezesha vijana wadogo kupitia Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.
6. ***Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa hukumbatia umoja na tofauti ndani ya Kristo.***
   Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa imejitoa katika kuelewa na kusherehekea/kukubali tofauti na utofauti katika lugha, rangi, kabila, tamaduni, kiwango cha uhusiano wa kiuchumu, na jinsia. Tofauti zetu hazidhoofishi umoja bali zinaongeza uwezo na bidii yetu. Kushiriki habari njema za Yesu Kristo katika njia tofauti za kitamadauni lazima kila wakati iwe kipaumbele cha juu.
7. ***Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa huunda mtandao na ushirikiano.***
   Hali ya ushirikiano inaainisha uhusiano wetu kwa kila kiwango cha Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa. Kueneza kazi ndani ya kanisa huongeza ujenzi na usambazaji wa vijana wadogo kwa ajili ya huduma; Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa uhusika vikamilifu katika jitihada za ushirikiano kama huo.

### 810.6 Muundo wa Huduma Yetu

Mkataba wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti wa Kimataifa hutoa msingi wa kuandaa, kupanga, na kufanya huduma ya vijana kwa kila kiwango cha Kanisa la Mnazareti. Mipango ya huduma ya viwango inatolewa kwamba vikundi vya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa vya mtaa, wilaya na eneo vinahimizwa kurekebisha kwa wajibu wa huduma ya vijana

mahitaji katika hali yao ya huduma. Mipango ya huduma kwa kila kiwango lazima iwe uthabiti na Mkataba wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti wa Kimataifa na *Kitabu cha Mwongozo cha Kanisa la Mnazareti.*

**810.7 Masahihisho**

Mkataba wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa inaweza kusahihishwa kupitia azimio iliyokubaliwa na Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa Ulimwenguni, kulingana na Mpango wa Huduma Ulimwenguni.

## A. KIELELEZO CHA MPANGO WA HUDUMA YA MTAA

**Huduma**

**810.100 Uinjilisti**

Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa hujenga na kutekeleza huduma tofauti zinazoendelea na mikutano maalum ya kuwafikia vijana kwa ajili ya Kristo.

**810.101 Uanafunzi**

Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa hujenga na kuendeleza huduma tofauti zinazoendelea na mikutano maalum ya kulea na kuwaweka vijana kukabili changamtoto na kupevuka kama wanafunzi wa Kristo, kaktika kujitoa kwa binafsi, ibada, ushirika, huduma na kuwaleta wengine kwa Kristo.

**810.102 Ujenzi wa Viongozi**

Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa hujenga na kuendeleza huduma tofauti zinazoendelea na mikutano maalum ya kushauri na kujenga vijana kuwa viongozi kwa ajili ya Kristo na kanisa Lake.

**Marudio**

**810.103 Utoaji**

1. Mpango wa huduma ya mtaa hutoa muundo wa kiwango maandilizi, kazi, na uongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa katika kiwango cha mtaa. Kikundi cha Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa cha mtaa kinaweza kukubali mpango kulingana na mahitaji ya huduma ya vijana ya mtaa, kufuata na Mkataba wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na *Kitabu cha Mwongozo* cha Kanisa la Mnazareti.

2. Sehemu yoyote ambayo haijafikiwa na mpango huu wa huduma iko chini ya mamlaka ya Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la mtaa.

**810.104 Hatua**

1. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti la Kimataifa huanzisha na kutangaza hatua ya kurekebisha na kurudia mpango wa huduma ya mtaa na ni lazima waidhinishe marudio yaliyopendekezwa kabla ya kuletwa kwenye mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa mwaka.
2. Marudio yaliyopendekezwa kwa mapngo wa huduma wa mtaa ni lazima ugawanyishwe kwa washirika wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kabla ya mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa mwaka.
3. Marudio ni lazima yaidhinishwe na theluji mbili za wingi wa kura za washirika wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ambao wako na wanapiga kura katika mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa mwaka na wamejitoa kwa idhini ya halmashauri ya kanisa.
4. Mabadiliko yote katika mpango wa huduma ya mtaa huwa yenye kufaa kabla ya siku 30 kufuatia mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa mwaka. Mpango uliorekebishwa ni lazima utumwe katika utaratibu ulioandikwa kabla ya kukubaliwa.

**Ushirika na Mtazamo wa Huduma**

**810.105 Uteuzi na Wajibu**

1. Ushirika wa mtaa wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ni wa wale wanaojishirikisha na kundi la Huduma ya Vijana wa Mnazareti la Kimataifa kwa kuhusika kaktika huduma zake na kujiunga na kundi la mtaa.
2. Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya mtaa inahifadhi orodha ya washirika wote wanaoshiriki kikamilifu.
3. Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya Mtaa inawajibika kwa washirika wake, halmashauri ya kanisa la mtaa, na mchungaji.
4. Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa inatoa ripoti ya kila mwezi kwa halmashauri ya kanisa na kwa mkutano wa kanisa wa mwaka.

**810.106. Mtazamo wa Huduma**

1. Mtazamo wa huduma wa tamaduni ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa mtaa ni kwa vijana wa umri wa miaka 12 na zaidi, wanafunzi wa chuo kikuu, na watu wazima.
2. Kwa makusudi ya kuwakilisha na kupanga, baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la mtaa huanzisha migawanyo ya umri kulingana na mahitaji ya huduma ya vijana ya mtaa.

**Uongozi**

**810.107 Viongozi**

1. Viongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa mtaa ni kiongozi na hadi watu watatu wanaochaguliwa na mkutano wa Hudumua ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa mwaka kwa kupewa majukumu ya hudumaku kulingana na mahitaji ya kanisa la mtaa. Maafisa hawa hutumika kwa Kamati Kuu.
2. Viongozi wa Hudumua ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa mtaa lazima wawe washirika wa kanisa la mtaa ambao wanahudumu kwa huduma yao ya Hudumua ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, wawe watendaji katika huduma ya vijana ya mtaa, na ni viongozi mfano wa binafsi na huduma.
3. Katika makanisa yasiyo na huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa iliyoratibiwa, mchungaji, akiwa na idhini ya halmashauri ya kanisa, anaweza kumteua kiongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ili kanisa liweze kuanza kufawafikia vijana kwa ajili ya Kristo na katika kukutana na mahitaji yao ya kukua kiroho.

**810.108 Uteuzi**

1. Viongozi wanateuliwa kila mwaka na washirika wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa mtaa katika mkutano wa mwaka na kutumika hadi waandimizi wao wanateuliwa na kuchukua majukumu ya huduma.
2. Kamati teule huteuwa viongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa. Kamati Teule inachaguliwa na wachungaji na inajumlisha washirika wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, na pia mchungaji na kiongozi wa vijana. Wateule wote ni lazima waidhinishwe na mchungaji na halmashauri ya kanisa. Watu walioteuliwa kama kiongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa mtaa lazima awe amefikia umri wao wa miaka 15 wakati wa kuteuliwa.

3. Viongozi wanateuliwa kwa wingi wa kura za washirika wa NYI walio kwenye mkutano wa NYI wa mwaka. Wakati kuna mteuliwa mmoja wa nafasi, kura ya siri ya "ndio" au "la" inatumika, kwa idhini ya theluji-mbili ya kura. Ni wale tu pia ambao ni washirika wa Kanisa la Mnazareti la Mtaa ambao wanaweza kupiga kura ya kiongozi wa huduma ya vijana..
4. Afisa aliye madarakarni anaweza kuteuliwa tena na kura ya "ndio" au "la" wakati kura kama hiyo imependekezwa na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kwa kamati teule, ikiidhinishwa na mchungaji na halmashauri ya kanisa, na kuidhinishwa kwa theluji-mbili ya kura za mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa mwaka.
5. Nafasi ya wazi inatokea wakati ofisa anahamisha ushirika wake kutoka kwa kanisa, anajiuzulu, au anaondolewa kutoka kwa ofisi na theluji-mbili ya kura za baraza kwa sababu ya kutotekeleza majukumu au tabia isiyofaa. Iwapo nafasi itatokea kati ya maafisa, Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa hujaza nafasi hiyo kwa theluji-mbil za kura kama kuna mteuliwa mmoja au na wingi wa kura kama wateuliwa ni wawili au zaidi. Iwapo nafasi itatokea katika ofisi ya kiongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, mchungaji, mchungaji wa vijana, au ya kiongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa au ya wasaidizi wake wa mkutano wa kuachaguliwa.

**810.109 Majukumu**

1. Majukumu ya kiongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa yanajumlisha:
   a. Kuongoza Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kuweka maono ya huduma ya vijana katika kanisa.
   b. Kurahisisha ujenzi wa huduma ya vijana na kufanya kazi na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ili kufafanua mtazamo wa huduma kulingana na matahiji ya vijana wao.
   c. Kuhudumu kwenye halmashauri ya kanisa na kutoa ripoti ya kila mwezi kwa halmashauri. Halmashauri ya kanisa la mtaa inaweza kuanzisha kabla ya uteuzi wa mwaka kiwango cha umri cha kiongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kuhudumu kwenye halmashauri ya wilaya; kiongozi akiwa wa umri wa chini, mwakilishi mwingine wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kwenye halmashauri ya kanisa anaweza

kuchaguliwa na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, chini ya idhini ya halmashauri.

d. Kutoa ripoti ya mwaka ya huduma na fedha kwa mkutano wa mwaka wa kanisa.
e. Kupendekeza bajeti ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya mtaa, kama ilivyoidhinishwa na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, kwa halmashauri ya kanisa.
f. Kuhudumu kama mshirika wa Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa ili kusimamia Shule ya Jumapili ya Vijana/masomo ya Biblia/vikundi vidogo katika kanisa.
g. Kufanya kazi pamoja na kiongozi wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa katika kuendeleza sisitizo la misheni kwa vijana.
h. Kuhudumu kama mjumbe kwenye Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya na Kikao cha Wilaya. Iwapo kiongozi hataweza kuhudhuria, mwakilishi aliyechaguliwa na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na kuidhinishwa na mchungaji na halmashauri ya kanisa anaweza kutoa mwakilishi mwingine badala yake.

2. Majukumu ya maafisa wengine wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa yanajumlisha:
   a. Kuwajenga na kuwatengea kazi viongozi kwa huduma mbali mbali za Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa za mtaa.
   b. Kuwa mfano mwema na mwongozo mwema wa kiroho kwa vijana nje na ndani ya kanisa.
   c. Kuamua na kutoa vyeo na majukumu ya huduma za vijana kulingana na mahitaji ya kanisa la mtaa.
   d. Kugawa majukumu yafuatayo kuhakikisha kuwajibika na utimilifu:
      (1) Kuweka rekodi iliyo sahihi ya mikutano yote ya Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na kushughulikia mambo yote ya mawasiliano ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya mtaa
      (2) Kugawa, kupokea, na kuweka rekodi za fedha ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kulingana na sera ya halmashauri ya kanisa.
      (3) Kukusanya ripoti ya fedha ya mwaka ya pesa zote zilizochangwa na kugawanywa ili kuitoa kwa mkutano wa kanisa wa mwaka.
      (4) Kufanya kazi pamoja na kiongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ili kuunda bajeti ya mwaka ya

kuwakilisha kwa baraza na kwa halmashauri ya kanisa ili kuidhinishwa.

e. Kushirikiana na kiongozi katika kila njia inayowezekana karahisisha huduma ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya mtaa.
f. Kutekeleza huduma zingine kama vile zilizvyopeanwa na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.

**810.110 Wafanyakazi Wanaolipwa**

1. Wakati mchungaji wa vijana ameajiriwa kanisani, mchungaji, akiwasiliana na halmashauri ya kanisa na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, anampa mchungaji wa vijana jukumu la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa. Katika hali hii, mchungaji wa vijana anatekeleza baadhi majukumu ambayo yangepewa kiongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa mtaa. Hata hivyo, umuhimu wa kiongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa hubaki, katika kutoa uongozi wa kawaida, kusaidia, na kuwasilisha huduma ya vijana ya mtaa. Mchungaji, mchungaji wa vijana na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wanafanya kazi pamoja kufafauna wajibu na majukumu ya vyeo viwili na jinsi wanafanya kazi pamoja kwa manufa ya huduma ya vijana ya kanisa.
2. Mchungaji wa vijana anaweza kukosa kuhudumu kama kiongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.
3. Mchungaji wa vijana hutumika kama afisa asiye rasmi kwenye Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, Kamati Kuu, na Kamati Teule ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.
4. Mchungaji wa vijana anaweza kuhudumu kama msaidizi wa mchungaji kwa majukumu yanayohusiana na Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.
5. Kama kanisa lina wafanyakazi wengi wa kulipwa ambao wanahudumia makundi tofauti ya umri maalum ndani ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, inaweza kutengeneza maafisa wa kila kikundi cha umri chini ya uongozi wa wafanyakazi na kuamua kutoka kwa hao maafisa jinsi Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa inafaa kuwakilishwa kwenye halmashauri ya kanisa.

**Baraza**

**810.111 Uteuzi**

1. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la mtaa limetungwa na maafisa wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, wengine wamechaguliwa au washirika wa vijana walioteuliwa kwa upana na viongozi wa huduma kama vile inavyostahili, na mchungaji na wa vijana, ambaye analeta maono ya huduma ya vijana ya mtaa.
2. Washirika wa Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ni lazima wawe washirika wa Vijana wa Mnazareti wa Kimataifa wa mtaa. Ushirika wa kanisa wa mtaa unahimiziwa kwa bidii na washirika wa Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wanatarajiwa kuwa washirika wa kanisa.

**810.112 Uteuzi**

1. Kamati teule ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa huteuwa washirika wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa watakaochaguliwa na baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti la Kimataifa.
2. Ushirika wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti wa Kimataifa hatimaye huteuwa washirika wa Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kutoka kwa uteuzi uliotolewa na wingi wa kura kwenye mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa mwaka.
3. Nafasi hutokea wakati mshirika wa baraza anahamisha ushirika wake ktuoka kwa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya mtaa, anajiuzulu, au anaondolewa ofisini na theluji-mbili ya wingi wa kura ya baraza kwa sababu ya kutotekeleza jukumu au tabia isiyofaa. Nafasi inapotokea kati ya washirika wa baraza, Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa hujaza nafasi hiyo kwa theluji-mbili ya wingi wa kura kama kuna mteuliwa mmoja au na wingi wa kura kama kuna wateuliwa wawili au zaidi.

**810.113 Majukumu**

1. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa linawajibika kwa kupanga na kutekeleza huduma yote ya vijana ndani ya kanisa la mtaa na, kupitia kwa maafisa wake na wasimamizi, linaanzisha na kusimamia huduma na shughuli za kuwafikia vijana wadogo kwa ajili ya Kristo na kuitika kwa mahitaji yao ya kiroho, kufuatana na uongozi wa kanisa la mtaa.

2. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa hueleza mtazamo wa huduma wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya mtaa kulingana na mahitaji ya huduma ya vijana ya mtaa, na kujenga na kupeana vichwa na maelezo ya kazi kwa wasimamizi wa huduma.
3. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa hupeana uongozi kwa eneo la vijana wa Shule ya Jumapili/mafunzo ya Biblia/vikundi vidogo kwa kuendeleza ukuaji katika uandikishaji na mahudhurio ya vijana, kuteuwa na kupeana mafundisho ya Shule ya Jumapili kwa vijana/masomo ya Biblia/vikundi vidogo vya walimu na viongozi, na likipendekeza mitaala na raslimali ya kutumia, kwa kushirikiana na Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa.
4. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa hushirikiana na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya katika kuendeleza wilaya, jimbo, na huduma za Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa za ulimwenguni kwa vijana wa kanisa.
5. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa huanzisha na kuwasilisha hatua ya kupeana upitiaji kwa mpango wa huduma ya mtaa.

**810.114 Kamati**

1. Kamati Kuu ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa inajumlisha maafisa wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa walioteuliwa na mchungaji au mchungaji wa vijana. Kamati Kuu inaweza kuongoza shughuli za Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa mahali inahitajika. Mambo yote ya Kamati Kuu yanawasilishwa kwa washirika waliobaki wa baraza na wanajitoa kwa idhini ya baraza lote kwenye mkutano wao unaofuata.
2. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa linaweza kuanzisha huduma maalum au kamati ya migawanyo ya umri kulingana na mahitaji ya huduma ya vijana.

**810.115 Wafanyakazi Wanaolipwa**

1. Mchungaji hupeana majukumu ya mchungaji wa vijana kwa kushauriana na halmashauri ya kanisa na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.
2. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na mchungaji wa vijana hufanya kazi kwa kushirikiana na kuelewana na kila mmoja.
3. Kama kanisa linalo wafanyakazi wengi wa kulipwa ambao wanahudumia migawanyo maalum ya umri ndani ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, linaweza kujenga mabaraza zingine za

Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa au kamati za kila moja ya migawanyo hii ya umri chini ya uongozi wa wafanyakazi. Kanisa linaweza kuamua iwapo baraza linalosimamia vikungu tofauti linatumika.

**Mikutano**

**810.116 Mikutano ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya Mtaa**

1. Mikutano mbali mbali ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya mtaa husaidia kutoa huduma yenye kufaa ya vijana.
2. Kikundi cha mtaa cha Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa uhusika katika mikutano ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya wilaya, jimbo, na mikusanyiko ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa uliwenguni ambayo baadaye huongeza huduma ya vijana kanisani.

**810.117 Mikutano Huduma ya Vijana wa Mnazreti ya Kimataifa**

1. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa hukutana mara kwa mara kutimiza misheni na maono ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.
2. Mikutano ya baraza inaweza kupangwa au kuitiwa na kiongozi au mchungaji.

**810.118 Mkutano wa Mwaka**

1. Mkutano wa mwaka wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya mtaa kufanywa kati ya siku sitini ya Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya na katika kuelewana na *Kitabu cha Mwongozo cha Kanisa la Mnazareti*.
2. Viongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na washirika wa baraza na wajumbe kwenye Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya wanateuliwa na mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa mwaka.
3. Mpango wa huduma ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya mtaa unaweza kupitiwa tena na theluji-mbili ya wingi wa kura kwenye mktauno wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa mwaka

## B. KIELELEZO CHA MPANGO WA HUDUMA YA WILAYA

**Huduma**

**810.200 Uinjilisti**

Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya Wilaya hujenga na kutekeleza huduma tofauti zinazoendelea na mikutano maalum ya kuwafikiwa vijana kwa ajili ya Kristo.

**810.201 Uanafunzi**

Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya Wilaya hujenga na kuendeleza huduma tofauti zinazoendelea na mkutano maalum ya kulea na kuwaweka vijana changamoto kuku kama wanafunzi wa Kristo, katika kujitoa kwa binafsi, ibada, ushirika, huduma na kuwaongoza wengine kwa Kristo.

**810.202 Ujenzi wa Viongozi**

Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya Wilaya hujenga na kuendeleza huduma tofauti zinazoendelea na mkutano maalum ya kushauri na kujenga vijana kuwa viongozi kwa ajili ya Kristo na kanisa Lake.

**Marudio**

**810.203 Utoaji**

1. Kielelezo cha mpango wa huduma ya wilaya hutoa mundo wa kiwango cha maandilizi, kazi, na uongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa katika kiwango cha wilaya. Huduma ya Vijana ya Kimataifa ya Wilaya inaweza kukubali na kurudia mpango kulingana na mahitaji ya huduma ya vijana ya wilaya, kufuatana na Katiba ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na *Kitabu cha Mwongozo cha Kanisa la Mnazareti*.
2. Sehemu yoyote ambayo haijafikiwa na mpango huu wa huduma iko chini ya mamlaka ya Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya.

**810.204 Hatua**

1. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya huanzisha na kutanagaza hatua ya kurekebisha na kurudia mpango wa huduma wa wilaya, na waidhinishe marudio yaliyopendekezwa kabla ya

kuletwa kwenye Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya.

2. Marudio yaliyopendekezwa kwa mpango wa huduma wa wilaya ni lazima yagawanyishwe katika hali ya maandishi kwa vikundi vya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa vya mtaa kabla ya Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya.
3. Ni lazima marudio yaidhinishwe na theluji-mbili za wingi wa kura za wajumbe na washirika ambao wako na wanapiga kura katika Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya na wamejitoa kwa idhin ya msimamizi wa wilaya na Halmashauri ya Wilaya.
4. Mabadiliko yote katika mpango wa huduma ya wilaya huwa yenye kufaa kabla ya siku 60 kufuatia Mkutano. Hati iliyorekebishwa ni lazima igawanywe katika hali ya maandishi kabla ya kukubaliwa.

**Ushirika na Mtazamo wa Huduma**

**810.205 Uteuzi na Wajibu**

1. Vikundi vyote vya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa vya mtaa na washirika wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ndani ya mipaka ya wilaya huunda Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya wilaya.
2. Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya wilaya kinawajibika kwa ushirika wake, kwa msimamizi wa wilaya, na kwa Halmashauri ya Wilaya.
3. Huduma ya vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya wilaya inatoa taarifai kila mwaka kwa Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya na Kikao cha Wilaya kupitia kiongozi/mwenyekiti wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya.

**810.206 Mtazamo wa Huduma**

1. Mtazamo wa huduma ya tamaduni ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ni kwa vijana wa umri wa miaka 12 na zaidi, wanafunzi wa chuo kikuu, na watu wazima. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya linaweza kubadilisha mtazamo wa huduma kama vile inavyotakikana, kwa idhini ya msimamizi wa wilaya na Halmashauri ya Wilaya.
2. Kwa makusudi ya kuwakilisha na kupanga, Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya huanzisha migawanyo ya umri kulingana na mahitaji ya huduma ya vijana katika wilaya.

## Uongozi

### 810.207 Viongozi

1. Viongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya ni kiongozi, katibu wa kiongozi, karani, na mweka hazina.
2. Viongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya ni lazima wawe washirika wa Kanisa la Mnazareti la mtaa ndani ya mipaka ya wilaya wakati wa kuteuliwa kwao, wawe wahusika watendaji katika huduma ya vijana ya mtaa na ya wilaya, na wachukuliwe kama viongozi katika mfano wa binafsi na huduma.
3. Viongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya hutumika bila mshahara. Fedha zinazotumika kwa matumizi ya maafisa wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya zimetengwa kama sehemu ya bajeti ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya wilaya.
4. Ikiwa wilaya haitakuwa na Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa iliyoratibiwa (Mkutano wa Huduma ya vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya), msimamizi wa wilaya anaweza kumteuwa kiongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya ili makanisa ya mtaa yaweze kusaidiwa katika kuwafikia vijana kwa ajili ya Kristo na katika kukutana na mahitaji yao ya kukua kiroho.

### 810.208 Uteuzi

1. Viongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya wanateuliwa na Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya kutumika kwa muda wa mwaka mmoja, kuanzia kufungwa kwa mkutano hadi waandimizi wao watakapoteuliwa na kuchukua majukumu ya huduma. Katika kupendekezwa kwa Kamati Teule ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya wilaya na kuidhinishwa na msimamizi wa wilaya, afisa anaweza kuteuliwa kwa muda wa miaka miwili.
2. Kamati Teule ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya wilaya huteuwa maafisa wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya. Kamati teule inachaguliwa na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya na inajumlisha angalau washirika wanne wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya, na pia inajumlisha msimamizi wa wilaya na kiongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya. Wateule wote ni lazima waidhinishwe na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya na msimamizi wa wilaya.

3. Viongozi hatimaye wanateuliwa kwa kura ya siri na wingi wa kura katika Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa mwaka. Wakati kuna mteuliwa mmoja wa nafasi, kura ya siri ya "ndio" au "La" inatumika, kwa idhini ya theluji-mbili za kura. Ikiwa itapendekezwa na kamati teule, mkutano unaweza kupiga kura ili kuruhusu Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya kuteuwa katibu na mweka hazina wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya.
4. Viongozi aliye madarakani anaweza kuteuliwa tena na kura ya "ndio" au "hapana" wakati kura kama hiyo imependekezwa na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya, kwa idhini ya msimamizi wa wilaya na kuidhinishwa na theluji-mbili ya wingi wa kura za Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya.
5. Nafasi inatokea wakati afisa anahamisha ushirika wake kutoka kwa wilaya, anajiuzulu, au anaondolewa kutoka kwa ofisi na theluji-mbili ya wingi wa kura za baraza kwa sababu ya kutotekeleza kazi au tabia isiyofaa. Iwapo nafasi itatokea katika ofisi ya kiongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya wilaya, katibu wa kiongozi atachukua majukumu ya kiongozi hadi Mkutano mwingine wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya. Iwapo nafasi itatokea miongoni mwa maafisa wengine, Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya hujaza nafasi kwa theluji-mbili za wingi wa kura ikiwa kuna mteuliwa mmoja au na wingi wa kura ikiwa kuna wateuliwa wawili au zaidi.

**810.209 Majukumu**

1. Majukumu ya kiongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya wilaya yanajumlisha:
    a. Kuwa kiongozi na msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya, kufanya kazi kwa kushirikiana na Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na uongozi wa wilaya.
    b. Kuongoza Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya kuweka maono ya huduma ya vijana kwenye wilaya.
    c. Kurahisisha ujenzi wa huduma ya vijana kwenye wilaya na kufanya kazi pamoja na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya ili kufafanua mtazamo wa huduma ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya wilaya kulingana na mahitaji.

   d. Kuongoza Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya.
   e. Kutia moyo ujenzi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa katika kila kanisa la mtaa ndani ya wilaya.
   f. Kuwasilisha maslahi ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kwenye halmashauri ya zote za wilaya zinazofaa na kamati.
   g. Kutoa ripoti ya mwaka kwa Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya na kwa Mkutano wa Wilaya.
   h. Kutoa bajeti ya mwaka kwa Kamati ya Fedha ya Wilaya (au ofisi ianyotakikana ya wilaya) na kwa Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya ili kuidhinishwa.
   i. Kuwa mjumbe kwa sababu ya wadhifa wake kwenye Mkutano wa Kikao cha Wilaya.
   j. Kuwa mjumbe kwenye Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa. Ikiwa kiongozi hataweza kuhudhuria, mwakilishi aliyeteuliwa na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya na kuidhinishwa na msimamizi wa wilaya na halmashauri ya wilaya anaweza kutoa mwakilishi mwingine.
   k. Kuwa mjumbe wa Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo, ikiwa amechaguliwa na mpango wa huduma wa jimbo.
2. Majukumu ya katibu wa kiongozi yanajumlisha:
   a. Kushirikiana na kiongozi katika namna inayowezekana kutekeleza huduma ya vijana kikamilifu kwenye wilaya
   b. Kutekeleza kazi ya kiongozi wakati hayuko.
   c. Kutekeleza kazi zingine kama vile zilizotolewa na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya na Mkutano.
   d. Iwapo kutakuwa na nafasi katika ofisi ya kiongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya wilaya, ikitimiza kazi za kiongozi hadi mwandamizi wake atapochaguliwa na kuajiriwa.
3. Majukumu ya katibu yanajumlisha:
   a. Kuweka kumbukumbu sahihi ya majadiliano ya Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya Wilaya, ya Kamati Kuu, na ya Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya.
   b. Kushughulikia shuhguli zote za mawasiliano za Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa za wilaya.

c. Kujulisha ofisi ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ulimwenguni na kiongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo majina ya anuani za viongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa tofauti na wasimamizi wa huduma mara tu wamechaguliwa.
d. Kutekeleza kazi zingine ambazo zimeagizwa na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya na Mkutano.

4. Majukumu ya mweka hazina yanajumlisha:
    a. Kulipa, kupokea, na kuweka kumbukumbui ya fedha za Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya wilaya.
    b. Kukusanya taarifa ya fedha ya mwaka ya pesa zote zilizochangwa na kulipwa na kukabidhi kwenye Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya wa mwaka.
    c. Kufanya kazi pamoja na kiongozi ili kuunda bajeti ya kuwakilisha kwa halmashauri zinazofaa.
5. Majukumu mengine yanaweza kutolewa kwa viongozi kulingana mahitaji ya huduma ya vijana ya wilaya.

**810.210 Wafanyakazi Wanaolipwa**

1. Wakati wilaya inaajiri mchungaji wa vijana, msimamizi wa wilaya, akishirikiana na Halmashauri ya Wilaya na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya, wanapeana jukumu za Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa za wilaya kwa mchungaji wa vijana. Katika hali hiyo, mchungaji wa vijana wa wilaya anatekeleza baadhi ya kazi zilizopeanwa kwa kiongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya. Hata hivyo, umuhimu wa kiongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya hubaki, katika kupeana uongozi ulioongezwa, msaada, na msimamizi wa wilaya wanafanya kazi pamoja kufafanua kazi na majukumu ya nafasi mbili na jinsi zinafanya pamoja kwa manufaa ya huduma ya vijana ya wilaya.
2. Mchungaji wa vijana anaweza kuhudumu kama kiongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya.
3. Mchungaji wa vijana wa wilaya hudumu kama afisa wa zamu kwenye Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya, Kamati Kuu, na kwa Kamati Teule ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.
4. Mchungaji wa vijana wa wilaya anaweza kutumika kama msaidizi wa msimamizi wa wilaya kwa majukumu yanayohusiana na Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.

**Baraza**

## 810.211 Uteuzi

1. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya linajumlisha maafisa wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya, wateuliwa wengine au washirika wa vijana waliochaguliwa na viongozi wa huduma kama vile inavyotakikana na baraza, na msimamizi wa wilaya na mchungaji wa wilaya.
2. Ni washirika tu wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ambao ni washirika wa Kanisa la Mnazareti kwa wilaya ambao watatumika kama washirika wa Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya.

## 810.212 Uchaguzi

1. Kamati Teule ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya wilaya huteuwa washirika wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya ili kuchaguliwa kwa Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya.
2. Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya kisha huchagua washirika wa Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya kutoka kwa wateule waliopeanwa na wingi wa kura.
3. Nafasi iapopatikana wakati mshirika wa baraza anahamisha ushirika wake kutoka kwa wilaya, anajiuzulu, au anaondolewa kwa ofisi na baraza na theluji-mbili ya wingi wa kura kwa sababu ya kutotekeleza majukumu au tabia isiyofaa. Nafasi inapopatikana miongoni mwa washirika wa baraza, Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya hujaza nafasi kwa theluji-mbili za wingi wa kura kama kuna mteule mmoja au na wingi wa kura kama kuna wateule wawili au zaidi.
4. Kamati teule inaweza kutoa mamlaka kwa Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya kuteuwa wasimamizi wa huduma ya wilaya.

## 810.213 Majukumu

1. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya linawajibika kwa kupanga na kuandaa huduma yote ya vijana ndani ya wilaya na, kupitia kwa maafisa na wasimamizi wake, kuanzisha na kusimamia huduma na shughuli za kuwafikia vijana kwa ajili ya Kristo

na kuitikia kwa mahitaji yao ya ukuaji wa kiroho, kufuatana na uongozi wa wilaya.

2. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya hueleza mtazamo wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya kulingana na mahitaji ya huduma ya wilaya na kuendeleza na kupeana vichwa na majukumu kwa wasimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya.
3. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya hutia moyo na kujenga makanisa ya mtaa kwenye wilaya kwa ajili ya huduma imara ya vijana.
4. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya hutoa uongozi kwa sehemu ya vijana wa Shule ya Jumapili ya Wilaya/masomo ya Biblia/vikundi vidogo kwa kuendeleza ukuaji katika kujiunga na mahudhurio ya vijana na kwa kutoa mafundisho kwa walimu wa Shule ya Jumapili wa vijana na Halmashauri ya Huduma ya Uanafunzi ya Kimataifa.
5. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya huendeleza huduma za Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa za jimbo za Kimataifa na ratiba ya vikundi vya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya mtaa.
6. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya hutengeneza mapendekezo kwa Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya kuhusu Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa. Mkutano unaweza kurudia mapendekezo haya kabla ya kukubaliwa.
7. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa huanzisha na kuwasilisha hatua ya kusahihisha mpango wa huduma wa wilaya.

**810.214 Kamati**

1. Kamati kuu ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa inajumlisha maafisa wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya waliochaguliwa na msimamizi wa wilaya na/au mchungaji wa vijana wa wilaya. Ikiwa karani na mweka hazina atakuwa mshirika aliyechaguliwa na baraza, baraza linaweza kuteuwa kwa kura ya wengi washirka wengine wawiliw wa Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya Kutumika kwenye Kamati Kuu. Shughuli zote za Kamati Kuu zinawasilishwa kwa washirika waliobaki wa baraza na walio chini ya idhini ya baraza lote katika mkutano wake mwingine.

2. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya linaweza kuanzisha huduma maalum au mgawanyo wa umri wa kamti kulingana na mahitaji ya huduma ya vijana ya wilaya.

**810.215 Huduma ya Vijana wa Mnazareti wa Kimataifa ya Eneo**

1. Katika kushirikiana na uongozi wa wilaya, Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya linaweza kutoa amri kwa maeneo tofauti ndani ya mundo uliopo wa wilaya kuandaa viongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ili kusimamia na kupanua huduma za Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kwenye wilaya.
2. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la eneo linaweza kuundwa ili kuwa na jukumu la huduma maalum na shughuli kwenye eneo.
3. Kiongozi au mwakilishi kutoka kila eneo anaweza kutumika kwenye Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya, ikiwa ametajwa na Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya.

**810.216 Wafanyakazi Wanaolipwa**

1. Msimamizi wa wilaya hugawa majukumu ya wachungaji wa vijana wa wilaya, kwa kushauriana na Halmashauri ya Wilaya na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya.
2. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya na mchungaji wa vijana wanafanya kazi kwa kushirikiana kwa amani na kila mmoja.

**Mikutano**

**810.217 Mikutano ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya Wilaya**

1. Mikutano tofauti ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya wilaya husaidia kutoa huduma imara ya vijana.
2. Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya wilaya pia hutia moyo na kuongeza Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya mtaa kwa kukutana na vikundi vya NYI vya mtaa kwenye wilaya yote ili kuwatafuta kwa ajili ya huduma imara.
3. Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya wilaya uhusika katika mikutano ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya jimbo na ya kimataifa ambayo baadaye huongeza huduma imara ya vijana walayani kote.

### 810.218 Mikutano ya Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti la Kimataifa ya Wilaya

1. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya hukutana mara kwa mara kutimiza misheni na maono ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya wilaya
2. Mikutano ya baraza inaweza kupangwa au kuitwa na kiongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya au msimamizi wa wilaya.

### 810.219 Mkutano wa mwaka wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya

1. Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya wa mwaka hutoa sehemu ya kuhimiza na ratiba ya kuinua huduma ya vijana kwenye wilaya. Taarifa zitapokelewa, uongozi unateuliwa, na jukumu la kutunga sheria inayohusu kazi za Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa inashughuilkiwa kwenye Mkutano. Wajumbe wa Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa pia huteuliwa kufuatana na Mpango wa Huduma ya Dunia ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifaå.
2. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya hupanga na kusimamia Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya, kwa kushirikiana na msimamizi wa wilaya. Mkutano huitishwa wakati na hali ambapo pamechaguliwa na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya, kwa idhini ya msimamizi wa wilaya kwa siku tisini na Mkutano wa Wilaya.
3. Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya unajumisha washirika wa Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya, msimamizi wa wilaya, wachungaji wa mtaa, wahudumu wengine waliowekwa wakfu wa wilaya ambao uhusika katika huduma ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, na wajumbe wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa mtaa.
4. Wajumbe wote wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya lazima wawe washirika wa Kanisa la Mnazareti ambalo wanawakilisha.
5. Hesabu ya wajumbe wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa kila kanisa wanathibitishwa na idadi ya Mkutano wa Wilaya. Uongozo wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya hitia moyo makanisa ya mtaa kufanya mipango inayofaa kwa ajili ya gharama ya wajumbe wanaohudhuria Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya.

6. Ujumbe wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa mtaa kwa Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya wa makanisa ukiwa wa washirika wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa 30 au wachache unajumlisha:
    a. Mchungaji na mchungaji wa vijana au wafanyakazi wachungaji wanaolipwa ambao wanahusika katika huduma ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.
    b. Kiongozi mpya wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa aliyeteuliwa.
    c. Hadi wajumbe wanne walioteuliwa, na angalau nusu yake wakiwa ndani ya mtazamo wa huduma ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya wilaya iliyoanzishwa.
    d. Makanisa ya mtaa yanaweza kuongeza wajumbe wengine zaidi kwa kila washirika 30 wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa mtaa waliofuatana na/au sehemu za mwisho za wale washirika 30 (yaani, washirika 16-29)
7. Mchungaji wa kanisa lolote la mtaa au msimamizi wa Kituo cha Huduma ya Mnazareti ya Huruma ambaye hana Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa iliyoratibiwa anaweza kumteuwa mjumbe mmoja.

| Idadi ya washirika | Idadi ya wajumbe* | Idadi ya washirika | Idadi ya wajumbe* |
|---|---|---|---|
| 5-45 | 4 | 136-165 | 8 |
| 46-74 | 5 | 166-195 | 9 |
| 76-105 | 6 | 196-225 | 10 |
| 106-135 | 7 | 226-255 | 11 |

*Hesabu ya wajumbe walioteuliwa kutoka kwa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya mtaa haijumlishi wajumbe (kiongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, mchungaji, mchungaji wa vijana, washirika wa Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya kutoka kanisa la mtaa, n.k.) kwa ajili ya wadhifa wao.

## C. KIELELEZO CHA MPANGO WA HUDUMA YA JIMBO

### Huduma

### 810.300 Uinjilisti

Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya jimbo hujenga na kufanya huduma mbali mbali zinazoendelea na matukio maalum ili kuwafikia vijana kwa ajil ya Kristo.

**810.301 Uanafunzi**

Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya jimbo hujenga na kufanya huduma mbali mbali zinazoendelea na matukio maalum ya kulea na kuwatia changamoto vijana ili kukua kama wanafunzi wa Kristo katika kujitoa kwa binafsi, ibada, ushirika, huduma, na kuwaongoza wengine kwa Kristo.

**810.302 Ujenzi wa Viongozi**

Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya jimbo hujenga na kufanya huduma mbali mbali zinazoendelea na matukio maalum ya kuwashauri na kuwajenga vijana kuwa viongozi wa Kristo na kanisa Lake.

**Marudio**

**810.303 Utoaji**

1. Kielelezo cha mpango wa huduma ya jimbo hutoa muundo wa kiwango kwa ajili ya mpango, kazi, na uongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kwa kiwango cha jimbo. Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya jimbo kinaweza kurekebisha na kurudia mapngo kulingana na mahitaji ya huduma ya vijana katika jimbo, inayokubaliana na Mkataba wa Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na *Kitabu cha Mwongozo* cha Kanisa la Mnazareti.
2. Sehemu yoyote ambayo haijafikiwa na mpango wa huduma iko chini ya mamlaka ya Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya Wilaya.

**810.304 Hatua**

1. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo, katika kushirikiana na jimbo, huanzisha na kuweka wazi hatua ya kurekebisha na kurudia mpango wa huduma ya jimbo na ni lazima liidhinishe marudio yaliyopendekezwa kabla ya kuletwa kwa Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Jimbo.
2. Marudio yaliyopendekezwa kwa mapngo wa huduma ya jimbo ni lazima yagawanyishwe katika mundo ulioandikwa kwa vikundi vya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa vya wilaya kabla ya Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Jimbo katika Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.

3. Marudio ni lazima yaidhinishwe na theluji-mbili ya wingi wa kura za wajumbe wote na washirika waliohudhuria na kupiga kura katika Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Jimbo na wako chini ya idhini ya msimamizi wa jimbo na Baraza la Halmashauri ya Jimbo (mahali inatakikana).
4. Mabadiliko yote ya mpango wa huduma ya jimbo huwa kamili kabla ya siku 90 kufuatia Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa. Maandishi ya marudia ni lazima yagawanywe kwa muundo ulioandikwa kabla ya kuchukuliwa.

**Ushirika na Mtazamo wa Huduma**

**810.305 Uteuzi na Wajibu**

1. Vikundi vyote vya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa vya mtaa, Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa za wilaya, na washirika wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ndani ya mipaka ya jimbo huunda Huduma ya Vijana ya Kimataifa ya jimbo.
2. Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya jimbo kinawajibika kwa ushirika wake, msimamizi wa jimbo, msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ulimwenguni, baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la jimbo, na kwa Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.
3. Taarifa ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya jimbo kwa Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kwa msingi wa kila mwaka.

**810.306 Mtazamo wa Huduma**

1. Mtazamo wa huduma wa kitamaduni wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo ni wa vijana wa umri wa miaka 12 na zaidi, wanafunzi wa chuo kikuu, na vijana wazima. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo linaweza kubadilisha mtazamo wa huduma kama vile inavyohitajika, kwa idhini ya wilaya kwenye jimbo na, mahali inahitajika, msimamizi wa jimbo.
2. Kwa makusudi ya kuwasilisha na kuandaa, Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo huanzisha migawanyo ya umri kulingana na mahitaji ya huduma ya vijana kwenye jimbo.

**Uongozi**

**810.307 Viongozi**

1. Viongozi wa Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Jimbo ni mwenyekiti, naibu wa mwenyekiti, na katibu. Maafisa hawa na msimamizi wa vijana wa jimbo wanatumika kama Kamati Kuu.
2. Viongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Jimbo ni lazima waishi na kuwa na ushirika katika Kanisa la Mnazareti ndani ya mipaka ya jimbo wakati wa kuchaguliwa kwao, wawe watendaji katika huduma ya vijana, na kuchukuliwa kama viongozi katika mfano wao binafsi na huduma.
3. Viongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Jimbo hutumika bila mshahara. Fedha zinazotumika kwa matumizi ya utawala ya maafisa wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo zinatengwa kama sehemu ya fedha za jimbo.

**810.308 Uteuzi**

1. Viongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Jimbo wanateuliwa na Mkutano wa Ulimwenguni wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Jimbo katika mkutano maalum wakati wa Mkutano wa Ulimwenguni wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti wa Kimataifa. Maafisa wa jimbo hutumika kuanzia mwisho wa Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa hadi mwisho wa Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa unaofuata.
2. Kamati Teule ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya jimbo huteuwa maafisa wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo. Kamati teule inachaguliwa na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo na inajumlisha angalau washirika wanne wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo, ikihusisha mwenyekiti wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo na msimamizi wa jimbo. Angalau majina mawili yanatumwa kwa Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Jimbo kwa kila nafasi. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na msimamizi wa jimbo lazima aidhinishe wateuliwa wote.
3. Mwenyekiti wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo anayetumika ambaye anaweza kuchaguliwa kwa kipindi cha pili anaweza kuteuliwa tena kwa kura ya "ndio" au "la", wakati kuteuliwa huko kupependekezwa na theluthi-mbili za kura ya siri ya Mkutano wa

Jimbo wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo wakati wa Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.

4. Nafasi inatokea wakati afisa amehamisha ushirika wake wa jimbo, anajiuzulu, au ameondolewa kwa ofisi kwa theluji-mbili za wingi wa kura za Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa za Jimbo kwa sababu ya kutotekeleza majukumu au tabia isiyofaa. Nafasi ikitokea miongoni mwa maafisa, Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo hujaza nafasi kwa theluji-mbili za wingi wa kura ikiwa kuna mteuliwa mmoja au kwa wingi wa kura ikiwa kuna wateuliwa wawili au zaid. Katika hali ya nafasi kama hiyo katika ofisi ya mwenyekiti wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo, jimbo huchagua kiongozi mpya kufuatana na Mpango wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.

**810.309 Majukumu**

1. Majukumu ya mwenyekiti wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo yanajumlisha:
    a. Kuwa kiongozi na msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo, wakifanya kazi kwa kushirikiana na uongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa kimataifa na wa jimbo.
    b. Kusimamia Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo kusimamia maono ya huduma ya vijana kwenye jimbo.
    c. Kurahisisha ujenzi wa huduma ya vijana kwenye jimbo na kufanya kazi na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo kueleza mtazamo wa huduma wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo kulingana na mahitaji.
    d. Kuongoza kwenye Mkutano wa Jimbo wakati wa Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.
    e. Kuhimiza ujenzi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kwa kila wilaya au uwanda ndani ya jimbo.
    f. Kuwasilisha maslahi ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya jimbo kwenye halmashauri ya jimbo inayofaa na kamati na, wakati inahitajika, kwa kamati kadhaa za jimbo.
    g. Kutoa taarifa ya mwaka kwa Baraza la Jimbo la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, msimamizi wa jimbo na Baraza la Ushauri la Jimbo (mahali inahitajika), na Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.

h. Kupendekeza bajeti ya mwaka ya Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo na Ofisi ya Jimbo (mahali inahitajika).
i. Kutumika kama mjumbe kwenye Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.
j. Kutumika kama mawasiliano katikati ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya jimbo na taasisi za Mnazareti za elimu ya juu kwenye jimbo kuendeleza mawasiliano, ushirikiano, na uhusiano wa huduma.

2. Majukumu ya maafisa wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo yanajumlisha:
   a. Kujenga na kugawa viongozi kwa huduma tofauti za Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa za jimbo.
   b. Kueleza na kutoa maelekezoa na majukumu ya huduma ya vijana kulingana na mahitaji ya jimbo.
   c. Kugawa majukumu yafuatayo kuhakikisha kuwajibika na kuimarika:
      (1) Kuweka kumbukumbui sahihi ya mikutano yote ya Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo na kushughulikia mawasiliano yote ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya jimbo.
      (2) Kulipa, kupokea, na kuweka kumbukumbui ya fedha za Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa za jimbo, kulingana na será za Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, Halmashauri Kuu, na será za ofisi ya jimbo.
      (3) Kusaidia mwenyekiti katika kukusanya taarifa za fedha za mwaka za pesa zote zilizochangishwa na kulipwa ili kutuma kwa Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na sehemu zingine zinazohitajika.
      (4) Kufanya kazi pamoja na mwenyekiti ili kuunda bajeti ya mwaka ya kuwasilisha katika Baraza la Jimbo Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na msimamizi wa jimbo (mahali inahitajika) kwa kuidhinishwa.
      (5) Kueleza Ofisi ya Dunia ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na ofisi ya jimbo (mahali inahitajika) majina na anuani za maafisa tofauti wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo na wasimamizi wa huduma mara baada ya uteuzi au uchaguzi.
   d. Kushirikiana na mwenyekiti katika njia zote zinazowezakana ili

kurahisisha huduma ya vijana ya jimbo.

e. Kutekeleza huduma zingine kama vile zilivyopeanwa na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo au Mkutano wa Jimbo.

**810.310 Wafanyakazi wa Kulipwa**

1. Wakati jimbo linaajiri msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo, msimamizi wa jimbo, kwa kushirikiana na Halmashauri ya Baraza la Jimbo na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo, hugawa majukumu ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya jimbo kwa msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo. Katika hali hiyo, msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo anaweza kutekeleza baadhi ya majukumu ambayo yamepewa mwenyekiti wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo. Hata hivyo, umuhimu wa mwenyekiti wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo bado unaendelea, katika kupeana uongozi zaidi, msaada, na uwakilishi wa huduma ya vijana wa jimbo. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo na msimamizi wa jimbo hufanya kazi pamoja ili kueleza kazi na majukumu ya nafasi mbili jinsi zinafanya kazi pamoja kwa manufaa ya huduma ya vijana ya jimbo.
2. Msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo anaweza kukosa kuhudumu kama mwenyekiti wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo.
3. Msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo hutumika kama afisa wa zamu kwenye Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo, kwa Kamati Kuu, na kwa Kamati Teule ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya Jimbo.
4. Msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo anaweza kuhudumu kama msaidizi msimamizi wa jimbo kwa majukumu yanayohusiana na Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.

**Baraza**

**810.311 Uteuzi**

1. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo linajumlisha maafisa wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo na wateule wengine au washirika vijana waliochaguliwa na

viongozi wa huduma kama inavyohitajika na baraza, na, mahali inahitajika, msimamizi wa jibmo na/au msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo.

2. Ni wale tu washirika wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ambao ni washirika wa Kanisa la Mnazareti katika jimbo ambao wanaweza kutumika kama washirika wa Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Jimbo.
3. Wakati ikihitajika, wawakilishi wa chuo cha Mnazareti wanaowajibika kwa huduma za kushiriki na Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya jimbo wanaweza pia kutumika kwenye Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo.

**810.312 Uteuzi**

1. Kamati Teule ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya jimbo huteuwa washirika wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo watakaoteuliwa kwa Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa jimbo.
2. Mkutano wa Jimbo kwenye Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa hatimaye huchagua kwa wingi wa kura washirika wa Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Jimbo kutoka kwa wateule waliopeanwa. Mkutano wa Jimbo unaweza kutoa idhini kwa Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo kuteua wasimamizi wa huduma ya jimbo.
3. Nafasi inapotokea wakati mshirika amehamisha ushirika wake kutoka kwa jimbo, amejiuzulu, au ameondolewa kwa ofisi na theluji-mbili za wingi wa kura za baraza kwa asababu kutotekeleza majukumu au tabia isiyofaa. Ikiwa nafasi kama hiyo itatokea miongoni mwa washirika wa baraza waliteuliwa na kuchaguliwa na baraza, Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo hujaza nafasi hiyo kwa theluji-mbili za wingi wa kura ikiwa kuna mteule mmoja au kwa wingi wa kura ikiwa kuna wateule wawili au zaidi. Ikiwa nafasi itatotkea miongoni mwa washirika wanaowakilisha wilaya kwenye jimbo, nafasi hiyo inajazwa kulingana na mpango wa huduma wa wilaya.

**810.313 Majukumu**

1. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo linawajibika kwa kupanga na kuandaa huduma kamili ya vijana ndani ya jimbo na, kupitia kwa maafisa wake na wasimamizi, huanzisha na kusimamia huduma na shuhguli za kuwafikia vijana kwa ajili ya Kristo na kuitika kwa mahitaji ya kukua kiroho, kufuata na na uongozi wa

jimbo.

2. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo hueleza mtazamo wa huduma wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo kulingana na mahitaji ya huduma ya vijana ya jimbo, na kujenga na kupeana vichwa na majukumu ya wasimamizi wa huduma ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya jimbo.
3. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo uhimiza na kuandaa wilaya katika jimbo lote kwa ajili ya huduma imara ya vijana.
4. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la jimbo hutoa uongozi kwa vijana wa eneo wa Shule ya Jumapili/Masomo ya Biblia/vikundi vidogo vya jimbo kwa kuendeleza ukuaji katika kujiandikisha na kuhudhuria kwa vijana na kutoa mafundisho ya Shule ya Jumapili ya Vijana/Masomo ya Biblia/vikundi vidogo vya walimu na viongozi kwa kushirikiana na Huduma ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi ya Kimataifa.
5. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo huendeleza Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa za kimataifa na ratiba kwa uongozi wa jimbo.
6. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo husimamia matumizi ya fedha yaliyotolewa kwa jimbo kwa njia ya matukio ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na ushirikiano.
7. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo hutoa mapendekezo kwa Mkutano wa Jimbo wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa katika Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kuhusu huduma ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa. Baraza hilo pia litateuwa hadi watu wawili kuwa wajumbe wa jimbo kama washirika wa Kamati ya Uamuzi kwenye Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, kuhusiana na Mpango wa Huduma wa Kimataifa.
8. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo hufanya kazi kwa kushauriana na msimamizi wa jimbo kuchagua mwakilishi mmoja kutumika kwenye Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Dunia.
9. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo huanzisha na kuwasilisha hatua ya kubadilisha mpango wa huduma wa jimbo.

**810.314 Kamati**

1. Kamati Kuu ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa inajumlisha maafisa wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo walioteuliwa na msimamizi wa jimbo na/au msimamizi wa vijana wa jimbo. Kamati Kuu inaweza kuongoza shughuli za Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo wakati imeshindikana au imekosa kuwezekana kuongoza baraza lote. Shughuli zote za Kamati Kuu zinawasilishwa kwa washirika waliobaki wa baraza na wako chini ya idhini ya baraza lote katika mkutano wao unaofuata.
2. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo linewaza kuanzisha kamati maalum za huduma kulingana na mahitaji ya huduma ya vijana ya jimbo.
3. Katika nchi ambapo kuna wilaya kadhaa, jimbo linaweza kuandaa uongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa taifa kusimamia na kurahisisha huduma ya vijana katika nchi hiyo.

**810.315 Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa katika Eneo**

1. Mahali ikihitajika na kwa kushirikiana na uongozi wa kanisa la jimbo, Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo linaweza kuandaa uongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kwenye eneo tofauti ndani ya mundo ambao upo wa jimbo, ili kusimamia na kueneza Huduma za Vijana wa Mnazareti za Kimataifa katika jimbo lote.
2. Baraza la eneo la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa linaweza kuundwa ili kuwa na jukumu za huduma maalum na shughuli za eneo.
3. Mwakilishi kutoka kwa kila eneo anaweza kuhudumu kwenye Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo, ikiwa imekubaliwa na Mkutano wa Jimbo.

**810.316 Wafanyakazi Wanaolipwa**

1. Msimamizi wa jimbo hugawa majukumu ya msimamizi wa NYI wa jimbo, kwa kushauriana na Halmashauri ya Baraza la Jimbo na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo.
2. Baraza la Jimbo la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo hufanya kazi kwa kushirikiana na kuelewana na kila mmoja.

**Mikutano**

### 810.317 Mikutano ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya Jimbo

1. Mikutano mbalimbali ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya jimbo husaidia kutoa huduma imara kwa vijana kwenye jimbo.
2. Huduma ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya jimbo pia uhimiza na kuendeleza huduma za Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa za wilaya kwa kukutana na vikundi vya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa vya wilaya katika jimbo lote ili kuwatafuta kwa ajili ya huduma imara.
3. Huduma ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya jimbo uhusika katika mikutano ya dunia ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ambayo baadaye huongeza huduma imara za vijana kwenye jimbo lote.

### 810.318 Mikutano ya Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti wa Kimataifa ya Jimbo

1. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo hukutana mara kwa mara kutimiza misheni na maono ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya jimbo.
2. Mikutano ya baraza inaweza kupangwa au kuitwa na mwenyekiti wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo, msimamizi wa jimbo, msimamizi wa vijana wa jimbo, mkurugenzi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa kimataifa.

### 810.319. Mikutano ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya Jimbo

1. Mkutano wa Jimbo Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa huitishwa wakati wa Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa. Mkutano huo hutoa sehemu za kuhimiza na ratiba ya kuinua huduma ya vijana katika jimbo lote. Ripoti zinapokelewa, uongozi unateuliwa, na shughuli za kutunga sheria zinazohusiana na kazi ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kwenye jimbo zinaendelea katika mkutano.
2. Baraza la Jimbo Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, kwa kushirikiana na Baraza la dunia Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, hupanga na kusimamia Mikutano ya Jimbo ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.
3. Mikutano ya Jimbo Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa

inajumlisha washirika wa Baraza la Jimbo la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, msimamizi wa jimbo, na wajumbe kutoka kwa jimbo kwenda kwa Mkutano wa Dunia ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ambao wamechaguliwa, ikithibitishwa na Mpango wa Huduma wa Kimataifa.

4. Mkutano huitishwa wakati wa Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wakati na mahali palipotengwa na msimamizi wa dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa. Wakati imeidhinishwa na Baraza la Jimbo Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, msimamizi wa jimbo, na Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, mkutano unaweza kuitishwa kwa njia ya posta au ya umeme kwa miezi sita kabla ya Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ili kuongoza shughuli za jimbo za Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wakati hali inazuia wengi wa wajumbe waliochaguliwa kuhudhuria Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.

## D. KIELELEZO CHA MPANGO WA HUDUMA WA KIMATAIFA

### Huduma

**810.400 Uinjilisti**

Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa katika kiwango cha kimataifa hujenga na kufanya huduma mbalimbali zinazoendelea na matukio maalum ili kuwafikia vijana kwa ajili ya Kristo.

**810.401. Uanafunzi**

Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa katika kiwango cha kimataifa hujenga na kufanya huduma mbali mbali zinazoendelea na matukio maalum ya kulea na kuwatia changamoto vijana ili kukua kama wanafunzi wa Kristo katika kujitoa kwa binafsi, ibada, ushirika, huduma, na kuwaongoza wengine kwa Kristo.

**810.402. Kujengwa kwa Uongozi**

Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa katika kiwango cha kimataifa hujenga na kufanya huduma mbali mbali zinazoendelea na matukio maalum kuwashauri na kuwajenga vijana kuwa viongozi wa Kristo na kanisa Lake.

**Marudio**

**810.403 Utoaji**

1. Mkataba wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na Mpango wa Huduma wa Dunia hutoa muundo kwa ajili ya mpango, kazi, na uongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kwa kiwango cha kimataifa. Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Kimataifa unaweza kurekebisha Mkataba wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na Mpango wa Huduma wa Kimataifa kulingana na mahitaji ya huduma ya vijana ulimwenguni kote kupitia maazimio yaliyopeanwa. Marekebisho yote ya mpango wa Huduma wa Kimataifa ni lazima yakubaliane na Katiba ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na *Kitabu cha Mwongozo* cha Kanisa la Mnazareti.
2. Sehemu yoyote ambayo haijafikiwa Katiba ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa au na mpango wa Huduma wa Kimataifa iko chini ya mamlaka ya Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.

**810.404 Hatua**

1. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, kwa kushirikiana na msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, huanzisha na kuweka wazi hatua ya kurekebisha Mpango Huduma wa Kimataifa na Mkataba wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kupitia maazimio yaliyopeanwa.
2. Baraza lolote la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Wilaya, Baraza lolote la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo, Baraza lolote la Kimataifa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, au angalau wajumbe sita wanasimamiwa kwenda kwenye Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wanaweza kutoa maazimio haya. Maazimio ni lazima yawe katika muundo mzuri wa azimio na kupokelewa kwa tarehe ya mwisho iliyotolewa.
3. Ofisi ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ni lazima ipokee maazimio yote angalau siku thelathini kabla ya mkutano wa mwaka wa Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa katika mwaka wa Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.

4. Maazimio ni lazima yatumwe katika hali ya maandishi kwa wajumbe wa Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Kimataifa kabla ya Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.
5. Maazimio yanachukuliwa kwanza na Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na Kamati ya Maazimio ya Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Kimataifa, yanaundwa na wajumbe wawili wa Baraza la Jimbo la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa waliochaguliwa na kutoka kwa kila jimbo la Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa. Maazimio ambayo yatapokea kura za wengi za sehemu yoyote kupendekeza idhini yao hatimaye yanachukuliwa na Mkutano.
6. Maazimio ni lazima yaidhinishwe na theluji-mbili za kura za wajumbe waote ambao wako na wanapiga kura katika Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.
7. Mabadiliko yote yaliyoidhinishwa katika Mkataba wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na Mpango wa Huduma ya Vijana wa Kimataifa huwa kamili kabla ya siku 90 kufuatia Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Kimataifa. Maandishi ya marudio ni lazima yagawanywe kwa muundo uliondikwa kabla ya kuchukuliwa.

**Ushirika na Mtazamo wa Huduma**

**810.405 Uteuzi na Wajibu**

1. Vikundi vyote vya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa vya huduma za wilaya, eneo na za jimbo, na washirika wao wanajumlisha Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa .
2. Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya dunia inawajibika kwa ushirika, msimamizi mkuu anayewajibika wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, msimamizi wa misheni wa dunia, Halmashauri Kuu, na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu.
3. Huduma ya Vijana wa Mnazaeti ya Kimataifa ya dunia inatoa taarifa kila mwaka kwa Halmashauri Kuu na kwa Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Kimataifa na Kikao Kikuu cha Kanisa la Mnazareti.
4. Msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa anawajibika kwa usimamizi wote na kusimamia ujenzi wa huduma ya vijana ya Kanisa la Mnazareti kupitia kwa Huduma ya Vijana wa

Mnazareti ya Kimataifa.

5. Viongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ulimwenguni kote wanafanya kazi pamoja na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Kimataifa kwa kuandaa huduma ya vijana ulimwenguni kwa ajili ya Kanisa la Mnazareti.

**810.406 Mtazamo wa Huduma**

1. Mtazamo wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ni wa vijana wa umri wa miaka 12 na zaidi, wanafunzi wa chuo kikuu, na vijana wazima. Jimbo, eneo, wilaya, na mabaraza ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya mtaa zinaweza kubalidisha mtazamo wa huduma kama vile inavyohitajika, kufuatana na mpango wa huduma wa kiwango hicho.
2. Kwa makusudi ya kuwasiliana na kuandaa, Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa katika kiwango cha kimataifa huanzisha migawanyo tatu – vijana wadogo, vijana wakubwa, na vijana wazima wa chuo.

**Uongozi**

**810.407. Viongozi**

1. Viongozi walioteuliwa wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ya kimataifa ni mwenyekiti wa baraza na katibu wa mwenyekiti.
2. Hakuna anayeweza kuteuliwa kama mwenyekiti wa Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ambaye ni mwajiriwa wa Kanisa la Mnazareti, akiwemo au vituo vinavyojumlisha vyuo vya elimu ambavyo vinapokea msaada kidogo wa fedha kutoka kwa Kanisa la Mnazareti. Watu kutoka kwa wilaya au vituo vingine ambavyo vinapokea fedha za kufanya kazi kutoka kwa kanisa kuu pia hawawezi kuchaguliwa.
3. Viongozi wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa lazima wawe washirika wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Kanisa la Mnazareti, watendaji wahusika katika huduma ya vijana, na wawe viongozi katika mfano binafsi na huduma, na washirika wa Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.
4. Viongozi wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa hutumika bila mshahara. Fedha zinazotumika kwa matumizi ya utawala ya maafisa ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa

kimataifa zimetengwa kama sehemu ya bajeti ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.

5. Kiongozi wa dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa anaweza kutumika katika nafasi yake kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja.

**810.408 Uteuzi**

1. Mwenyekiti wa baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa anateuliwa na kura za wingi katika Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na atatumika hadi mwisho wa Kikao Kikuu kitakachofuata au hadi mwaandimizi wake atakapoteuliwa.
2. Kila jimbo linachagua jina moja la mwenyekiti wa baraza la dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kutoka kwa mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo wa Mkutano dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.
3. Katibu wa mwenyekiti wa Huduma ya Dunia ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa anateuliwa na Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa katika mkutano wa kwanza wakati au kufuatia Kikao Kikuu na atatumika hadi mwisho wa Kikao Kikuu kitakachofuatia au hadi mwandamizi wake atakapoteuliwa.
4. Nafasi inatokea katika nafasi ya mwenyekiti wa Huduma ya dunia ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa au naibu wa mwenyekiti wakati mwenyekiti au naibu wa mwenyekiti anajiuzulu ofisini au anaondolewa kutoka kwa ofisi na theluji-mbili ya wingi wa kura za Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kwa sababu ya kutotekeleza kazi au tabia isiyofaa. Katika hali ya nafasi miongoni mwa maafisa, Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa litateuwa mtu mwingine.

**810.409 Majukumu**

1. Majukumu ya mwenyekiti wa Baraza la dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa yanajumlisha:
   a. Kuongoza katika mikutano ya shughuli za Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na mikutano ya Dunia ya Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.
   b. Kuwakilisha Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kama mshirika wa Halmashauri Kuu na kama mjumbe wa Kikao Kikuu.
   c. Kutekeleza majukumu mengine kama vile yalivyotolewa na Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na

Mkutano.

2. Majukumu ya naibu wa mwenyekiti wa Huduma ya dunia ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa yanajumlisha:
   a. Kushirikiana na mwenyekiti wa baraza la dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa katika kila njia inayowezekana kutekeleza huduma ya vijana vikamilifu ulimwenguni.
   b. Kuhakikisha rekodi sahihi ya hatua zote za Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti wa Kimataifa na mikutano yote ya Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa imewekwa kwa kutolewa kwenye Halmashauri Kuu kupitia Kamati ya Huduma Inayotumika ya Kimataifa na Mkutano Mkuu.
   c. Kuongoza Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti la Kimataifa, kutoa wawakilishi tofauti kwenye halmashauri yoyote au baraza, na kutimiza majukumu yoyote yaliyopeanwa kwa kutokuwepo kwa mwenyekiti wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa Kimataifa.
   d. Kutekeleza majukumu mengine kama vile yalivyopeanwa na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na Mkutano.

**810.410 Wafanyakazi Wanaolipwa**

1. Msimamizi mkuu anayewajibika wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na Halmashauri Kuu hugawa majukumu ya Huduma ya dunia ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kwa msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa. Msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa yuko chini ya usimamizi wa Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu.
2. Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu huteua msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kufuatana na utaratibu wa uteuzi wa Halmashauri Kuu.
3. Nafasi ikitokea katika cheo, inajazwa kulingana na utaratibu ufuatao:
   a. Msimamizi mkuu anayewajibika huteua msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, kwa kushirikiana na Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu.
   b. Kura ya siri kisha inawakilishwa kwa Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kwa kuidhinishwa na wingi wa kura na inakuwa chini ya utaratibu wa uteuzi wa Halmashauri Kuu.

4. Baada ya kuteuliwa na msimamizi mkuu wa eneo anayewajibika na Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, msimamizi aliye madarakani wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa anaidhinishwa na wingi wa kura za Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wakati wa mkutano wake wa kwanza uliopangwa kufuatia Kikao Kikuu, na anakuwa chini ya utaratibu wa uteuzi wa Halmashauri Kuu.
5. Msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa anaweza kuhudumu kama afisa wa dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa aliyeteuliwa.
6. Msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa uhudumu kama ofisa kwenye Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kwa wadhifa wake, kwa Kamati Kuu, baraza zote za jimbo, na kamati zingine za Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa za kimataifa vile alivyoteuliwa.

**Baraza**

**810.411 Utunzi**

1. Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa linajumlisha wasimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, mwenyekiti wa baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa kimataifa, na mwakilishi kutoka kwa kila jimbo ulimwenguni, ambaye amechaguliwa kulingana na mpango wa huduma wa kila jimbo ambao umekubaliwa.
2. Watu wengine ambao wamechaguliwa kama inavyotakikana na Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wanaweza kuteuliwa kutumika kama washirika wasiopiga kura wa baraza.
3. Washirika wote wa Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa lazima wawe washirika wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Kanisa la Mnazareti.

**810.412 Majukumu**

1. Baraza la Dunia Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, kwa kushirikiana na msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na wafanyakazi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, huanzisha ratiba ya Huduma ya Dunia ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na kupeana mwongozo na msaada kwa ujenzi wa raslimali za huduma ya vijana ya viwango vyote vya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, kwa idhini ya msimamizi mkuu

anayewajibika kwa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na Halmashauri Kuu. Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa imeundwa kuwafikia vijana kwa ajili ya Kristo na kuitika kwa mahitaji yao ya ukuaji wa kiroho; inarahisisishwa kupitia kwa msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na uongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa katika ulimwengu wote.

2. Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa hupeana kikao kwa msaada na ujenzi wenye kufaa wa ratiba za huduma za vijana, matukio, na raslimali kwa kiwango cha jimbo, kulingana na misheni na maono ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.
3. Baraza la Dunia Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa hupeana njia kwa uwakilishi wa viwango vya jimbo, eneo, wilaya, na mtaa vya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na washirika wa baraza kwa wafanyakazi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa. Washirika wa baraza huwakilisha pia Huduma ya dunia Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kwa kuanzisha mawasiliano na jimbo lao, eneo, wilaya, na makanisa ya mtaa kwa niaba ya Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na ofisi ya Dunia ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.
4. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Kimataifa husaidia katika kupanga na kusimamia Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Kimataifa.
5. Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa hupeana maoni kwa eneo la vijana wa Shule ya Jumapili/Masomo ya Biblia/vikundi vidogo na kusaidia kuendeleza ukuaji katika kujiandikisha na kuhudhuria kwa vijana na mafundisho ya vijana ya Shule ya Jumapili/Masomo ya Biblia/vikundi vidogo vya walimu na viongoi wa kimataifa, kwa kushirikiana na Huduma ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi ya Kimataifa.
6. Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa hurudia tena bajeti ya mwaka na matumizi ya ofisi ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa iliyopeanwa kupitia kwa Halmashauri Kuu.
7. Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa huongoza na kurudia katika matumizi ya fedha zilizopeanwa kupitia kwa shughuli za Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na ushirika kwa idhini ya msimamizi mkuu anayewajibika.

**810.413 Kamati**

1. Kamati Kuu inajumlisha maafisa wa Huduma ya Dunia ya Vijana wa

Mnazareti ya Kimataifa, msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa. Kamati Kuu inaweza kuongoza shughuli za Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wakati haitendi kazi au haiwezekani kuita baraza lote. Shughuli zote za Kamati Kuu zinawasilishwa kwa washirika waliobaki wa baraza na walio chini ya idhini ya baraza lote katika mkutano unaofuata.

2. Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa linaweza kuanzisha kamati za huduma maalum kama inavyohitajika kwa kuendeleza kazi yake.

**810.414 Wafanyakazi wa Kulipwa**

1. Msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa anawajibika kwa kusimamia Wasimamizi wa Misheni wa Kimataifa na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu. Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Kimataifa linaweza kupendekeza marudio ya majukumu haya kwa msimamizi mkuu anayewajibika wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.
2. Msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, kwa kushirikiana na Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, hugawa majukumu ya wafanyakazi wa kulipwa wa Ofisi ya Huduma ya dunia ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.
3. Msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa hataweza kutumika kama mwenyekiti wa baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.

**Mikutano**

**810.415 Mikutano ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa**

1. Ili kutoa huduma yenye kufaa kwa vijana, Huduma ya dunia ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa inaweza kuhusisha mikutano mbali mbali ya ibada, mafundisho, mafunzo, ushirika, na uinjilisti. Uongozi wa Huduma ya Dunia ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa hufanya kazi pamoja na jimbo, eneo, wilaya, na uongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa mtaa kupanga huduma ya kimataifa, inayohusiana na vikundi maalum, na inayoelekezwa kwa majimbo mengi, ili huduma ya vijana katika Kanisa la Mnazareti iweze kuwa yenye kufaa.
2. Viongozi wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na wafanyakazi uhusika vikamilifu na Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kwa kila kiwango kama raslimali ya huduma yenye kufaa.

**810.416 Mikutano ya Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti la Kimataifa**

1. Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa hukutana kila mwaka kuendeleza misheni na maono ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa. Mkutano hupangwa kufuatana na mkutano wa mwaka wa Halmashauri Kuu.
2. Maafisa wa dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa au wasimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wanaweza kuita mikutano maalum inavyohitajika, kwa kushirikiana na msimamizi mkuu anayewajibika wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.

**810.417 Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti wa Kimataifa**

1. Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa hupeana sehemu ya kutia moyo na ratiba ya kuendeleza huduma ya vijana ulimwenguni kote. Ripoti zinapokelewa, uongozi unateuliwa, na biashara za utawala zinazohusiana na kazi ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa zinashughulikiwa kwenye Mkutano wa Dunia Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.
2. Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu huweka muda wa Mkutano na wakati inaanza, kutoka kwa mapendekezo ya Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kwa Kamati ya Mpango wa Mkutano Mkuu. Maafisa wa dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na wasimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa husimamia mkutano, kwa msaada wa Baraza la Dunia la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.
3. Wajumbe wote wa Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ni lazima wawe washirika wa Kanisa la Mnazareti ni wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na wana miaka 12 na zaidi wakati wa Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa. Kwa kuongezea, kila mjumbe wa wilaya wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ni lazima awe mshirika na kuishi kwenye wilaya ambayo wanawakilisha wakati wa mkutano.
4. Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa unajumlisha Baraza la Dunia Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, maafisa wakuu wa jimbo walioteuliwa (wasiozidi watatu), wasimamizi wa jimbo, wa eneo, wa taifa, na wasimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya, na wajumbe wa

Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kama vile inavyohitajika:

a. Wilaya zilizo na washirika wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa 1,000 au wachache wanaweza kutuma wajumbe wafuatao.
   (1) Kiongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya anayetumika wakati wa Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa;
   (2) Mjumbe mmoja wa wahuduma anayehusika katika uongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ambaye ni mzee aliyeteuliwa, shemasi, au mhudumu wa wilaya aliyepewa hati;
   (3) Mjumbe mmoja mshirika aliye na umri zaidi ya miaka 23 wakati wa Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ambaye ni mhusika katika uongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na
   (4) Mjumbe mmoja wa vijana katikati ya miaka 12 na 23 wakati wa Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ambaye ni mhusika katika Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.

b. Kwa kuongezea, wilaya inaweza kutuma mjumbe mwingine wa huduma, mjumbe mhudumu, na mjumbe wa vijana kati ya miaka 12 na 23 wakati wa Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, kwa kila washirika 1,500 wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa au/na sehemu kubwa ya mwisho ya washirika 1,500 (washirika 751-1,499).

c. Kipimo cha ujumbe wa wilaya kinalingana na taarifa ya ushirika wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya kwa ajili ya kalenda Kikao cha Wilaya katika mwaka wa kalenda papo hapo kabla ya Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.

d. Wajumbe wote wa wilaya wanahitajika kuchaguliwa kwa kura ya siri na wingi wa kura katika sehemu ya Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya kati ya miezi 18 na Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa au miezi 24 katika maeneo ambayo viza au matayarisho makubwa yanahitajika. Wajumbe wengine tofauti wanaweza kuteuliwa baada ya wajumbe walioteuliwa kwenye kura nyingine ya siri kutoka kwa wateule waliobaki kwa kura nyingi, na mpokezi wa kwanza, mpokezi wa pili, mpokezi wa tatu, n.k., waliochaguliwa na hesabu ya kura zilizopokelewa. Wajumbe na wapokezi ni lazima wateuliwe kufikia tarahe 31 Machi ya mwaka wa Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa.

e. Ofisi ya kiongozi/mwenyekiti ya mwanafunzi wa kila chuo cha Mnazareti, chuo, na shule ya thiolojia, inaweza pia kutumika kama mjumbe, kama mwakilishi wa ushirika wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa pamoja na taasisi yake. Iwapo hataweza kutumika au kuhudhuria, mwakilishi aliyechaguliwa na utawala wa mwanafunzi anaweza kupeana uwakilishi mwingine wa upokezi.

5. Katika hali ambayo wilaya bila Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa iliyoratibiwa (bila Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya), uwakilishi wa Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa unaweza kujumlisha mjumbe mmoja wa umri wa ushirika wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa ukiwa umechaguliwa na Kikao cha Wilaya. Kama mjumbe atajiondoa kabla ya mkutano. Halmashauri ya Wilaya inaweza kumteuwa mjumbe mwingine aliyehitimu.
6. Kikao cha Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa kinawekwa ili kuwezesha wajumbe wote walioteuliwa kuhusika katika kupiga kura za Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa. Kupiga huku kwa kura kunaweza kufanyika kwa utaratibu wa kupiga kura ulioanzishwa na Kamati ya Mkutano Shughuli.
7. Mkutano wa kila jimbo unafanyika wakati wa Mkutano wa Dunia wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na unajumlisha Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa la Jimbo, msimamizi wa jimbo na msimamizi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo, na wajumbe wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya waliochaguliwa kutoka kwa jimbo hilo.

| Idadi ya Washirika | Idadi ya Wajumbe* | Idadi ya Washirika | Idadi ya Wajumbe* |
|---|---|---|---|
| 4-1750 | 3 | 4751-6250 | 12 |
| 1751-3250 | 6 | 6251-7750 | 15 |
| 3251-4750 | 9 | 7751-9250 | 18 |

*Hesabu ya wajumbe walioteuliwa kutoka kwa NYI ya wilaya haijumlishi wajumbe kwa ajili ya wadhifa wao (kiongozi/mwenyekiti wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya, viongozi/wenyeviti wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo na wasimamizi, na viongozi wa kimataifa, n.k.)

## II. MISHENI YA MNAZARETI YA KIMATAIFA (MMK)

## 811. KATIBA YA MISHENI YA MNAZARETI YA KIMATAIFA

### NAKALA YA KWANZA. Jina

Jina la huduma hii litakuwa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa ya Kanisa la Mnazareti.

### NAKALA YA PILI. Kusudi

Kusudi la huduma hii litakuwa ni kushirikisha Kanisa la Mnazareti katika misheni kupitia (1) maombi, (2) kutoa, (3) kuelimisha, na (4) kuhusisha watoto na vijana.

### NAKALA YA TATU. Muundo

**Sehemu ya Kwanza. Mtaa**

Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa ya mtaa itakuwa jumuiya ya kanisa la mtaa na itafanya kazi kwa kushirikiana na mchungaji na halmashauri ya kanisa kupitia Baraza la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa la mtaa.

**Sehemu ya Pili. Wilaya**

Viongozi wanaounda Baraza la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa la wilaya watafanya kazi kwa kushirikiana na msimamizi wa wilaya, halmashauri ya wilaya, na viongozi wengine wanaohusimama na wilaya.

Huduma zote za Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa za mtaa zilizo ndani ya mipaka ya wilaya zitaunda Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa ya wilaya.

**Sehemu ya Tatu. Dunia**

Viongozi wanaounda Baraza la Dunia la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa watafanya kazi kwa kushirikiana na Ofisi ya Misheni wa Dunia, Kamati ya Misheni ya Dunia ya Halmashauri Kuu, na wasimamizi wakuu wanaowajibika.

Huduma zote za Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa za wilaya na za mtaa zitakuwa na Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa ya Dunia.

## Nakala ya Nne. Ushirika

### Sehemu 1. Washirika

Mtu yeyote ambaye ni mshirika wa Kanisa la Mnazareti na anaunga mkono kusudi la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa anaweza kuwa mshirika wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa katika kanisa hilo la mtaa.

Kupiga kura na kuwa na ofisi itakuwa ya washirika walio na umri wa miaka 15 na zaidi, isipokuwa kwa vikundi vya watoto na vijana.

Kama haijatangazwa katika katiba, marejeleo ya "washirika" inamaanisha washirika wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa ambao ni washirika wa kanisa.

### Sehemu ya 2. Washirika

Mtu yeyote ambaye ni mshirika wa Kanisa la Mnazareti na anaunga mkono kusudi la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa anaweza kuwa mshirika wa jumuiya ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa.

## Nakala ya Tano. Baraza na Maafisa

### Sehemu ya 1. Baraza la Mtaa

#### A. Kusudi

Baraza la mtaa litaendeleza kusudi la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa la kuhamasisha Kanisa la Mnazareti katika kupitia 1) maombi, 2) kutoa, 3) kuelimisha, na 4) kuhusisha watoto na vijana.

#### B. Utunzi

1. Baraza la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa litakuwa na kiongozi na hesabu ya maafisa na/au washirika wa baraza kama ilivyokubaliwa na kiongozi na mchungaji anayeongoza, kulinagana na mahitaji na kipimo cha kanisa.
2. Baraza la mtaa linaweza kuwa na kamati kuu iliyo na kiongozi, mchungaji anayeongoza (kwa ajili ya wadhifa wake), na washirika wengine wawili au zaidi kama ilivyoamuliwa na baraza Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa mtaa.
3. Washirika wa baraza walioongezwa wanaweza kuwajibika kwa sehemu maalum ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa ikiwa ni pamoja na maombi, kutoa, kuelimisha, na kuhusisha watoto na vijana.
4. Mshirika wa baraza anaweza kuwa na zaidi ya cheo kimoja lakini atakuwa na kura moja peke yake.

5. Mshirika yeyote wa baraza la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa la wilaya anatakuwa mshirika wa baraza la mtaa kwa wadhifa wake kwa idhini ya baraza la mtaa.

**C. Uchaguzi, Uteuzi, Uteuzi na Nafasi**

Baraza la mtaa linaweza kuamua hitaji la kutumia kamati teule, mbali na kamati teule ya kanisa, kama sehemu ya hatua ya kutambuliwa kwa watahiniwa wanaostahili kwa uteuzi kwa baraza la mtaa. Kama kamati teule itatumika, basi kamati teule itateuliwa na kiongozi kwa makubaliano na baraza la mtaa.

1. Kiongozi
   a. Baraza la mtaa katika nafasi katika mwisho wa mwaka wa kanisa linaweza kupendekeza majina kwa kamati teule kwa uteuzi wa ofisi ya kiongozi, chini ya idhini ya halmashauri ya kanisa.
   b. Kiongozi atateuliwa au kuteuliwa tena na wingi wa kura za siri za washirika ambao wako na wanapiga kura kwa kipindi cha kutumika wa mwaka mmoja au miaka miwili ya kanisa. Baraza la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa na mchungaji watapendekeza muda wa kipindi cha kutumika.
   c. Mtu aliye madarakani anaweza kuteuliwa tena kwa kura ya siri ya ndio/la wakati uteuzi kama huo umependekezwa na baraza la mtaa na kuidhinishwa na mchungaji au halmashauri ya kanisa.
   d. Kwa upande mwingine, katika kanisa ambalo bado halijaratibiwa, limeratibiwa kwa miaka isiyopungua mitano, au lina ushirika usiopungua washirika 35, kiongozi anawewa kuchaguliwa na mchungaji kwa mazungumzo, na idhini ya, halmashauri ya kanisa.
2. Baraza
   a. Kwa kupendekezwa kwa kiongozi anayetumika kwas asa na kwa makubaliana na mchungaji anayeongoza, baraza la mtaa mbali na kiongozi linaweza kuteuliwa na kura za wingi za ushirika wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa au kwa mkutano wa mwaka wa kanisa, au kuteuliwa na kiongozi na mchungaji kwa idhini ya halmashauri ya kanisa.
   b. Muda wa kutumika utakuwa mwaka mmoja au miaka miwili, au hadi waandamizi wao watapoteuliwa au watapochaguliwa, kwa mapendekezo ya baraza la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa au, kwa kukosa kuweko kwa baraza, halmashauri ya kanisa na mchungaji.

c. Viongozi hawa wataanza kutumika siku ya kwanza ya mwaka mpya wa kanisa baada ya uteuzi.
d. Ikiwa kanisa lina mweka hazina mmoja ambaye anawajibika kwa hazina ya kanisa ikijumlisha pesa za Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa mtu huyo atakuwa mweka hazina wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa na mshirika wa baraza la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa la mtaa kwa wadhifa wake na haki zote na fursa, isipokuwa imebadilishwa na baraza la mtaa.

3. Wajumbe wa Mkutano wa Wilaya
   a. Wajumbe na watu tofauti watateuliwa kwa kura ya siri kwenye mkutano wa mwaka kwa wingi wa kura.
   b. Ikiwa uteuzi hautawezekana au kuonekana, uteuzi unaweza kufanywa na baraza la mtaa, au kwa kukosa kwa baraza, halmashauri ya kanisa, kwa wingi wa kura. Rejelea Nakala ya 6, Sehemu ya 3.A.3. kwa kuamua hesabu ya wajumbe.
4. Nafasi
   a. Kiongozi: Baraza la mtaa linaweza kupendekeza majina kwa halmashauri ya kanisa ambao watateuwa jina moja au majina zaidi. Uteuzi utafanywa kwa kura ya siri kwa wingi wa kura za washirika wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa kwenye mkutano ulioitwa kulingana na maelezo ya *Kitabu cha Mwongozo*. Aidha, mahali ambapo hakuna baraza la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa, halmashauri ya kanisa itajaza nafasi kwa uteuzi wa kura za wingi.
   b. Washirika wengine wa baraza: Baraza la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa, au katika kukosa kuwa kwa halmashauri ya kanisa, litajaza nafasi yoyote kwa uteuzi.

## D. Kazi za Washirika wa Baraza

1. Kiongozi
   a. Kusimamia kazi ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa katika kanisa la mtaa.
   b. Kuongoza katika mikutano yote ya kawaida na mikutano maalum ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa.
   c. Kugawa kazi kwa washirika wa baraza kama inavyohitajika mara kwa mara.
   d. Kutumika kama mshirika wa halmashauri ya kanisa kwa wadhifa wake, Halmashuri Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi, mkutano wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya, na kikao cha wilaya.

e. Kazi zingine ni kama vile zimeorodheshwa katika maelezo ya kazi.
f. Katika hali ambayo mke au mume wa kiongozi wa mtaa ni mshirika wa halmashauri ya kanisa, au mke au mume wa mchungaji wa kanisa, kama kiongozi wa mtaa atachagua kutohudumu katika halmashauri ya kanisa, mwakilishi wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa aliyeamuliwa na baraza la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa ana haki ya kutumika kwenye halmashauri ya kanisa katika nafasi ya kiongozi pamoja na haki na fursa zote.

2. Kamati Kuu
   a. Huendesha shughuli katikati ya mikutano ya baraza.

**Sehemu ya 2. Baraza la Wilaya**

**A. Kusudi**

Baraza la wilaya litaendeleza kusudi la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa la kuhamasisha Kanisa la Mnazareti katika misheni kupitia 1) Maombi, 2) Kutoa, 3) Kuelimisha, na 4) Kuhusisha watoto na vijana ndani ya wilaya.

**B. Utunzi**

1. Katika kiwango cha 3 ya wilaya, baraza litakuwa na maafisa wanne: kiongozi, naibu wa kiongozi, katibu, na mweka hazina (maafisa wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa), pamoja na washirika watatu au zaidi kulingana na mahitaji na ukubwa wa wilaya.
2. Mshirika wa barasa anaweza kuwa na nafasi aidi ya moja lakini awe na kura moja.
3. Kamati kuu itakuwa na kiongozi na maafisa wengine wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa. Kama itahitajika, angalau washirika watatu wa baraza wanaweza kuteuliwa au kuchaguliwa na baraza la wilaya kutumika kwenye kamati kuu kwa kipindi cha utumishi wa mwaka mmoja mkutano na hadi waandamizi wao watapoteuliwa. Msimamizi wa wilaya anatakuwa mshirika wa kamati kuu kwa wadhifa wake.
4. Kwa sehemu mpya, kiwango cha 1, na kiwango cha 3 cha wilaya, rejelea Sehemu ya 2.C.3 hapo chini.

**C. Uchaguzi, Uteuzi, Uteuzi na Nafasi**

1. Uchaguzi: Baraza litachaguliwa na kamati isiyokuwa na washirika chini ya watano (5) wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa.

Wateuliwa wote watakuwa washirika wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa wa Kanisa la Mnazareti la mtaa kwenye wilaya ambayo wanatumika.

a. Kamati kuu ya wilaya itachagua kamati teule na kuamua hesabu ya washirika wa baraza watakaoteuliwa.
b. Msimamizi wa wilaya atatumika kama mwenyekiti wa kamati kwa kuteuliwa kwa kiongozi wa wilaya. Baada ya idhini ya msimamizi wa wilaya, kiongozi wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya atatumika kama mwenyekiti wa kamati teule ya uteuzi zingine.

2. Uteuzi: Kiongozi na angalau washirika wengine wanne wa baraza, watateuliwa kwa kura ya siri katika mkutano wa wilaya wa mwaka. Washirika watatu walioongezwa watakuwa naibu wa kiongozi, katibu, na mweka hazina. Kipindi cha kutumika kitakuwa mwaka mmoja au miaka miwili ya mkutano kama vile itaamuliwa na baraza la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa la wilaya kwa idhini ya msimamizi wa wilaya au hadi waandamizi wao watakapoteuliwa. Katika hali ya uteuzi wa kiongozi mpya, kiongozi mpya atajaza nafasi ya ofisi kati ya siku 30 za mwisho wa mkutano wa wilaya. Mwaka wa mkutano utaanzia mwisho wa mkutano wa wilaya hadi mwisho wa mkutano wa wilaya utakaofuata. Washirika hawa wanne wa baraza wataunda kamati kuu ya baraza. Washirika wengine watatu au zaidi wa baraza wanaweza kuteuliwa au kuchaguliwa ili kutumika kwenye kamati kuu na baraza la wilaya.

   a. Kiongozi
      1) Kamati kuu itatoa angalau jina moja au zaidi la ofisi ya kiongozi isipokuwa wakati wa kuteuwa kiongozi anayehudumu kwa kipindi kingine.
      2) Wateule wanaohudumu wanaweza kuteuliwa na kura ya siri ya ndio/la wakati wa uteuzi kama huo umependekezwa na baraza la wilaya na kuidhinishwa na msimamizi wa wilaya.
      3) Kiongozi atateuliwa na theluji-mbili za kura za washirika ambao wako na kupiga kura katika hali ambapo jina moja linawakilishwa kwa nafasi ya kiongozi au na wingi wa kura wakati kuna angalau watainiwa wawili walioteuliwa kuwa kiongozi. Muda wa kutumika utakuwa mwaka mmoja au miaka miwili ya mkutano au hadi mwandamizi awe ameteuliwa. Baraza la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa la wilaya na msimamizi wa wilaya watapendekeza muda wa kipindi cha huduma.

4) Kwa muungano wa wilaya mbili, kiongozi wawili wa wilaya wanaohudumu wanaweza kutumika kama kiongozi wasaidizi. Kiongozi wasaidizi wanaweza kuteuliwa na mkutano wa wilaya hadi kamati kuu ya wilaya ikishirikiana na halmashauri ya wilaya wataamua kuwa inapendekeza kuteua kiongozi mmoja wa wilaya. Viongozi wasaidizi wataongoza kwa idhini. Katika hali ya kutokubaliana ambako hakuweza kusuluhishwa, suala hilo litaaumuliwa na kura ya kamati kuu ya wilaya. Kiongozi msaidizi mmoja pekee atawakilisha Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa ya wilaya katika kikao cha wilaya, kamati za wilaya, na Mkutano wa Dunia wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa na ataamuliwa na kamati kuu ya wilaya.

b. Naibu wa kiongozi atateuliwa kwa kura ya siri katika moja ya njia zifuatazo:
   1) Kamati kuu itatoa jina moja au zaidi za ofisi ya naibu wa kiongozi isipokuwa wakati baraza la wilaya kwa idhini ya msimamizi wa wilaya itapendekeza kura ya ndio au la ya mhudumu anayesimama kwa kipindi kingine; au
   2) Kwa baraza lote na nafasi maalum za baraza kuamuliwa na baraza.
   3) Kwenye wilaya ambayo ina kiongozi wasaidizi, hakuna haja ya naibu wa kiongozi.

c. Katibu au mweka hazina atateuliwa kwa kura ya siri na:
   1) Kamati teuzi itapeana jina moja au zaidi za ofisi ya katibu na mweka hazina isipokuwa wakati baraza la wilaya kwa idhini ya msimamizi wa wilaya itapendekeza kura ya ndio au la ya mhudumu anayesimama kwa kipindi kingine; au
   2) Kama wilaya mweka hazina mmoja ambaye anawajibika kwa fedha za wilaya pamoja na pesa za Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa, mtu huyo atakuwa mweka hazina wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa kama mshirika wa baraza la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa la wilaya kwa wadhifa wake na haki na fursa zote, isipokuwa imependekezwa na baraza la wilaya.

d. Washirika wa kuongezwa wa baraza: Washirika wengine wa baraza, wakiwa ni pamoja na kiongozi, naibu wa kiongozi, katibu, na mweka hazina, wanaweza kuteuliwa kwa kura ya siri kwa mwaka mmoja au miwili ya mkutano na majukumu ya

kuamuliwa na baraza. Kamati teule na msimamizi wa wilaya watapendekeza muda wa kipindi cha huduma cha mwaka mmoja au miwili ya mkutano. Kwa upande mwingine, washirika wengine wa baraza wanaweza kuchaguliwa na kamati kuu au baraza la wilaya kwa haki na fursa zote.

e. Kamati za mwakilishi wa vijana zinaweza kuombwa kutoka kwa Huduma ya Vijana wa Mnazareti cha Kimataifa.

3. Sehemu mpya ya Wilaya, Kiwango cha 1, na Kiwango cha 2 cha Wilaya: Katika sehemu mpya, kiwango cha 1, na kiwango cha 2 cha wilaya, kiongozi wa wilaya anaweza kuteuliwa na Mkutano wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa wa Wilaya au, mahali ambapo hakuna mkutano, msimamizi wa wilaya atamchagua kiongozi wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya ambaye ataendeleza kusudi la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa kwenye wilaya. Kiongozi anaweza kutumika peke yake au anaweza kushauriana na msimamizi wa wilaya kuchagua washirika wengine wa kanisa wa wilaya ili kusaidia rasi kwa kutumika kama baraza la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa.
4. Nafasi
   a. Kiongozi: Kamati kuu itateuwa jina moja au mbili. Uteuzi utakuwa kwa kura ya siri na wingi wa kura za baraza la wilaya ambayo iko na inapiga kura. Mtu aliyeteuliwa atatumika hadi kufungwa kwa mkutano wa wilaya utakaofuata au hadi mwandamizi wake atakapoteuliwa.
   b. Washirika wengine baraza: Kamati kuu au baraza la wilaya litajaza nafasi yoyote kwa uteuzi. Washirika wapya wa baraza walioteuliwa watahudumu hadi kufungwa kwa mkutano mwingine wa wilaya.
   c. Mweka hazina wa muungano: Kama wilaya nayo mweka hazina wa muungano, nafasi hiyo itajazwa na halmashauri ya wilaya.

**D. Majukumu ya Washirika wa Baraza.**

1. Kiongozi
   a. Husimamia na kurahisisha baraza la wilaya kuhakikisha matokeo ya kusudi la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa kwenye wilaya.
   b. Huongoza mikutano yote ya baraza la wilaya, kamati kuu, na mkutano wa wilaya.
   c. Hutayarisha bajeti ya mwaka ya kuidhinishwa na Kamati ya Fedha ya Wilaya.

d. Hutoa ripoti iliyoandikwa kwa mkutano wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya na kwa mwakilishi wa jimbo wa Baraza la Dunia la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa.
e. Hutoa kazi kwa washirika wengine wa kama itakavyohitajika mara kwa mara.
f. Hutumika kama mshirika wa kamati ya wilaya kwa wadhifa wake kama vile ilivyorejelewa katika *Kitabu cha Mwongozo* kifungu cha 239.

2. Naibu wa Kiongozi
   a. Hutekeleza kazi zote za kiongozi wakati kiongozi hayuko ofisini.
   b. Uhudumu katika sehemu zingine kama vile zilivyopewa na Baraza la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa la wilaya.
   c. Hutekeleza kazi zingine zilizoelezwa katika kitengo cha majukumu au kazi ambayo inaweza kupeanwa na kiongozi wa wilaya kama inavyohitajika mara kwa mara.
3. Katibu
   a. Huandika rekodi ya mawasiliano yote ya shughuli za mikutano.
   b. Hutoa usaidizi na msaada wakati anaombwa na kiongozi wa:
      1) Kutuma fomu za ripoti kila mwaka kwa kiongozi wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa wa mtaa.
      2) Hukusanya rekodi za takwimu na kutoa ripoti ya mwaka kwa kiongozi wa wilaya, msimamizi wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa, mwakilishi wa Baraza la Dunia, na mahali inahitajikia kwa msimamizi wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa wa jimbo wa majibo ya Misheni ya Kimataifa.
   c. Hutekeleza kazi zingine kama vile ilivyoelezwa katika maelezo ya kazi au ile inayoweza kupeanwa na kiongozi wa wilaya kama inavyohitajika mara kwa mara.
4. Mweka hazina
   a. Huweka hesabu sahihi ya fedha zote zilizochangwa na kutumiwa.
   b. Hutoa fedha kwa waweka hazina waliochaguliwa kwa wakati unaofaa.
   c. Hutoa maelezo ya ripoti zilizoorodheshwa kwa baraza la wilaya na kutayarisha ripoti ya mwaka kwa ajili ya mkutano wa wilaya.
   d. Hupanga pamoja na wafanyakazi wa wilaya ukaguzi wa fedha wa mwaka wa vitabu vya mweka hazina wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya.

e. Hutekeleza kazi zingine kama ilivyoelezwa katika maelezo ya kazi au ile inaweza kupeanzwa na kiongozi wa wilaya kama inavyohitajika mara kwa mara.

5. Kamati Kuu
   a. Huchagua washirika wengine wa baraza la wilaya na, kama inavyohitajika, hujaza nafasi kwenye baraza.
   b. Huendesha shuguli kati ya mikutano ya wilaya.
   c. Huteua jina moja au zaidi ya kiongozi kama nafasi itapatikana kati ya mikutano ya mwaka.
6. Washirika Wengine wa Baraza
   a. Hutekeleza kazi kama walivyoombwa na kiongozi wa wilaya na baraza la wilaya.

**Sehemu ya 3. Baraza la Dunia**

**A. Kusudi**

Baraza la Dunia la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa litaendeleza kusudi la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa la kuendesha Kanisa la Mnazareti katika misheni kupitia 1) maombi, 2) kutoa 3) kuelimisha, na 4) kuhusisha watot na vijana katika dhehebu lote kutumia mtandao wa majimbo, maeneo, wilaya, na makanisa ya mtaa ndani ya dhehebu.

**B. Utunzi**

1. Baraza la Dunia la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa litakuwa na kiongozi wa dunia wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa, mzimamizi wa dunia wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa, mwakilishi mmoja kutoka kila jimbo katika Kanisa la Mnazareti, na msimamizi wa Misheni ya Kimataifa.
2. Kamati kuu ya Dunia ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa itakuwa na kiongozi wa dunia wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa, msimamizi wa dunia wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa, naibu wa kiongozi wa dunia wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa, katibu wa dunia wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa, mshirika mmoja wa baraza, na msimimamizi wa Misheni ya Kimataifa.

**C. Uchaguzi, Uteuzi, na Nafasi**

1. Uchaguzi na Uteuzi wa Dunia wa Msimamizi wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa
   a. Kamati kuu ya Dunia ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa na msimamizi mkuu wa eneo wataunda kamati ya uvumbuzi ya kutambua watahiniwa waliohitimu kwa nafasi ya msimamizi wa

Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa. Hadi majina mawili ya watahiniwa wanaohitimu yatapeanwa kwa Kamati ya Misheni ya Kimataifa ya Halmashauri Kuu.

b. Kamati ya Misheni ya Dunia ya Halmashauri Kuu pamoja na msimamizi mkuu wa eneo watachukua majina yaliyopeanwa na kuratibu hadi majina mawili ya uteuzi na Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu.

c. Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu itateua msimamizi wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa wa kimataifa kwa kura ya siri kutoka kwa majina yaliyopeanwa kwake na Kamati ya Misheni ya Dunia ya Halmalshauri Kuu.

2. Uchaguzi na Uteuzi wa Kiongozi wa Dunia wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa

a. Kamati ya uteuzi itakuwa na watu 6, 7, au 8 na kusimamiwa na msimamizi wa dunia wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa. Kamati itakuwa na mwakilishi wa washirika wa baraza na mwakilishi wa washirika wasiokuwa wa baraza wa Misheni ya Dunia ya Mnazareti ya Kimataifa na atachaguliwa na kamati kuu.

b. Kamati itapeana jina moja au majina mawili ya uteuzi kama kiongozi wa kimataifa. Wateuliwa wataidhinishwa na Msimamizi wa Halmashauri ya Kuu. Wateuliwa hawatakuwa waajiriwa wa Halmashauri Kuu.

c. Kutoka kwa hawa wateuliwa Mkutano wa Dunia wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa utateuwa kiongozi wa dunia wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa kwa wingi wa kura za siri wakati kuna wateuliwa wawili au zaidi wa uongozi na theluji-mbili za kura wakati kuna mteuliwa mmoja.

d. Kiongozi wa dunia atatumika kwa kipindi cha miaka minne kuanzia kufungwa kwa Kikao Kikuu hadi mwisho wa Kikao Kikuu kitakachofuata au hadi mwandamizi wake atakapoteuliwa.

e. Kiongozi wa kimataifa atahudumu kwa vipindi vitatu vya huduma mfululizo. Kipindi cha huduma kitakuwa miaka minne. Kama mtu ameteuliwa kujaza nafasi katika ofisi ya kiongozi ya kimataifa, mtu huyo pia anaweza kutumika kwa vipindi vitatu mfululizo.

**3. Uchaguzi na Uteuzi wa Washirika wa Baraza la Dunia**

a. Kila Baraza la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa la wilaya linaweza kutoa au kupendekeza jina moja au majina mawili

kwenye Ofisi ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa ya Kimataifa kutoka kwa jimbo lake kama mwakilishi wa jimbo wa kura ya siri ya kuteuliwa.

1) Watu hawa watakuwa wakaazi na washirika wa Kanisa la Mnazareti katika jimbo ambalo watawakilisha.
2) Nafasi hii hairuhusu mtu yeyote ambaye makao yake ya nyumbani yako karibu na mipyaka ya jimbo kutoka sehemu ya ushirika wa kanisa lake.
3) Waajiriwa wa Halmashauri Kuu hawataweza kuchaguliwa.

b. Kutoka katika majina haya kwenye kura ya siri ya uteuzi, kila jimbo la mkutano katika Mkutano wa Dunia wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa litachagua kwa kura ya siri wateule wawili. Wale wawili watakaokuwa na hesabu ya juu ya kura watatangazwa kuwa wateule; hata hivyo, wateule hao wawili hawatatoka wilaya moja. Kama itafanyika hivyo, mtu aliye na kura za juu wa pili anabadilishwa na mtu mwingine aliye na hesabu ya juu ya kura kutoka kwa wilaya tofauti.

c. Jimbo la mkutano hatimaye litateuwa mtu mmoja kwa wingi wa kura kuwakilisha jimbo kwenye Baraza la Kimataifa.

d. Washirika wa Baraza watahudumu kwa kipindi cha mika minne kuanzia kufungwa kwa Kikao Kikuu hadi kufungwa kwa Kikao Kikuu kitakachofuata au hadi waandamizi wao watakapochaguliwa.

e. Kipindi cha kuhudumu kitakuwa cha muda wa vipindi vitatu mfululizo. Kipindi kitakuwa miaka minne. Kama mtu ameteuliwa kujaza nafasi ya mshirika wa Baraza la Kimataifa, mtu huyo pia anaruhusiwa kuhudumu kwa muda wa vipindi vitatu mfululizo. Mtu anaweza kuteuliwa kuhudumu tena baada ya kutumika angalau kwa kipindi kimoja mfululizo.

4. Uchaguzi na Uteuzi wa Kamati Kuu ya Dunia ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa

   a. Baraza la Dunia la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa katika mkutano wake wa kwanza, ambao unaweza kufanyika kabla kufungwa kwa Kikao Kikuu, litachagua na kuteuwa naibu wa kiongozi, katibu, na mshirika mwingine mmoja zaidi wa kamati kuu ya Dunia ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa.

   **b.** Uteuzi utakuwa kwa kura ya sir iza wingi za wale watakaokuwepo na kupiga kura.

5. Uchaguzi na Uteuzi wa Mwakilishi wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa kwenye Halmashauri Kuu

a. Baraza la Dunia la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa litateuwa mshirika mmoja wa wa baraza kuwakilisha Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa kwenye Halmashauri Kuu ya Kanisa la Mnazareti.
b. Kikao Kikuu kitateuwa mwakilishi wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa kwa kura ya siri ya wengi.

**6. Nafasi**

a. Kama nafasi itatokea katika ofisi ya kiongozi wa dunia wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa kati ya Mkutano wa Dunia wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa, kiongozi mpya wa kimataifa atateuliwa kwa theluji-mbili za kura za Baraza la Kimataifa kutoka kwa wateuliwa waliochaguliwa na kamati kuu kwa kushirikiana na msimamizi mkuu wa eneo Mtu huyo atatekeleza kazi ya kiongozi wa kimataifa hadi kufungwa kwa Kikao Kikuu kitakachofuata. Swala la kufanya uteuzi wa kujaza nafasi litaamuliwa na Baraza ya Kimataifa kwa kushirikiana na msimamizi mkuu wa eneo.
b. Kama nafasi itatokea katika kamati kuu ya Dunia ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa kati ya Mikutano ya Dunia ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa, Baraza la Kimataifa litateuwa mtu mmoja au zaidi. Nafasi itajazwa na wingi wa kura za siri za Baraza ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa.
c. Kama nafasi itatokea katika Baraza la Dunia la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa kati ya Mikutano ya Kimataifa, kila kamati kuu ya wilaya kwenye jimbo linalohusika itaomba kupeana mteule mmoja kutoka kwenye jimbo hadi kwa kamati kuu ya Dunia ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa. Kutoka kwa majina haya, kamati kuu itawasilisha majina mawili kama wateuliwa. Nafasi hatimaye itajazwa kwa wingi wa kura za viongozi wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya kwenye jimbo. Swala la kufanya uteuzi wa kujaza nafasi litaamuliwa na kamati kuu ya Dunia ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa kwa kushauriana na msimamizi mkuu wa eneo.
d. Kama nafasi itatokea katika ofisi ya msimamizi wa dunia wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa, hatua iyo hiyo itafuatwa kwa uchaguzi na uteuzi wa msimamizi wa kimataifa (tazama Nakala ya V, Sehemu ya 3.C.1.).
e. Kama nafasi itatokea katika uwakilishi wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa kwenye Halmashauri Kuu, kamati kuu ya Dunia ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa itatoa mteule mmoja

baada ya kushauriana na msimamizi mkuu wa eneo na idhini ya Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu. Baraza la Dunia la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa litateuwa mwakilishi wa Halmashauri Kuu kwa wingi wa kura.

**D. Majukumu**

1. Kiongozi wa Dunia
    a. Huongoza katika mikutano ya Baraza la Kimataifa, kamati kuu, na Mkutano wa Dunia wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa.
    b. Uhudumu kama mshirika wa Kikao Kikuu kwa wadhifa wake.
    c. Hutoa majukumu kwa washirika wengine wa baraza kama vile itahitajika mara kwa mara.
    d. Hutekeleza majukumu mengine katika maelezo ya kazi.
2. Naibu wa Kiongozi
    a. Hutekeleza majukumu ya kiongozi wakati kiongozi hayuko.
    b. Hutekeleza majukumu kama ilivyoelezwa katika maelezo ya kazi au ambayo yanaweza kupeanwa na kiongozi wa kimataifa kama inavyohitajika mara kwa mara.
3. Kamati Kuu: Huendesha shughuli kati ya mikutano ya baraza.
4. Washirika wa Baraza la Dunia
    a. Hushirikiana na kiongozi wa dunia wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa na msimamizi wa dunia wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa katika kuendeleza kusudi la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa.
    b. Huendeleza Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa katika jimbo analowakilisha.
    c. Hutoa ripoti ya kazi ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa katika jimbo kwa kila mkutano wa Baraza la Dunia la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa.
    d. Hutenda kwenye sheria zilizotungwa na kupitishwa na Kikao Kikuu kinachofaa kwa mwakilishi wa jimbo.
    e. Hutekeleza majukumu kama ilivyoelezwa katika maelezo ya kazi au kama anavyoweza kupewa na kiongozi wa kimataifa mara kwa mara.
5. Msimamizi wa Dunia
    a. Hutumika kama afisa mkuu wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa.
    b. Huinua matamanio ya misheni ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa katika wilaya zote ulimwenguni katika kushirikiana na Baraza la Kimataifa.

c. Hufafanua Kitabu cha Maelezo na Katiba ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa.
d. Huongoza wafanyakazi na shughuli za ofisi ya Dunia za Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa.
e. Uhudumu kama mwenyekiti mhariri wa chapa zote za Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa.
f. Huandaa fedha ya mwaka na ripoti ya takwimu kwa Baraza la Dunia, Kamati ya Misheni ya Dunia, na Halmashauri Kuu.
g. Pamoja na kiongozi wa kimataifa, huongoza mpango na ratiba ya Mkutano wa Dunia kwa kushirikiana na Baraza la Dunia.
h. Hutayarisha ripoti ya Mkutano wa Dunia, ya kifedha na takwimu, kwa mukhtasari mfupi kupitia Ofisi ya Misheni ya Dunia kwa ajili ya Kikao Kikuu.
i. Hutumika kama mshirika wa Kikao Kikuu kwa wadhifa wake.
j. Hutekeleza majukumu mengine kama yalivyoelezwa katika maelezo ya kazi.

## Nakala ya VI. Mikutano

### Sehemu ya 1. Mikutano na Mawasiliano ya Mtandao.

**A. Mikutano**

Mikutano yote ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa, baraza, kamati, kamati ndogo, na vikosi maalum itapewa mamlaka ya kukutana kupitia mikutano ya simu au kupitia mawasiliano mengine ya mitandao kama washirika wote wataweza kusikia kila mmoja kwa wakati mmoja na kuhusika katika mikutano.

B. **Mawasiliano**

Isipokuwa washirika watataka njia ingine, mawasiliano yote yanayohitajika ya Katiba hii yanaweza kutumia kwa njia ya mtandao.

### Sehemu ya 2. Shughuli za Mtaa na Mikutano

**A. Shughuli Zinazoendelea**

1. Kutakuwa na shughuli za kawaida, misheni inayoendelea ya ujumbe wa misheni, kutiwa moyo, na maombi yanayofanyika kala mwezi.
2. Shughuli zinaweza kuchukua muundo wa mikutano, huduma za misheni, wanenaji wa misheni, masomo ya misheni, shughuli na matukio ya misheni, muda wa misheni, sisitizo za Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa, n.k.

3. Mchungaji, kiongozi wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa, na baraza watafanya kazi kwa kushirikiana katika kupanga elimu ya misheni na kuhusika kwa kanisa la mtaa.
4. Katika uanzishaji wa kanisa na aina ya kanisa la misheni, kiongozi wa wilaya aliyechaguliwa wa kongamano anahimizwa kuhakikisha elimu ya misheni na kuhusika kwa kongamano la mtaa.

**B. Mkutano wa Mwaka**

1. Mkutano wa mwaka utafanyika kwa wakati usiozidi siku 30 kabla ya mkutano wa wilaya.
2. Kupiga kura na uchaguzi wa baraza la mtaa utakuwa wa kipimo cha washirika wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa ambao wako na umri wa miaka 15 au zaidi.

**C. Mikutano ya Baraza**

Baraza la mtaa litakutana mara nne kwa mwaka kupanga, kutoa ripoti, kutathmini, kueleza, kutia moyo, na kutekeleza kazi ya mpangilio wa mtaa. Zaidi, mikutano maalum inaweza kupangwa na kiongozi. Washirika wengi wa baraza watakuwa na watu wengi.

**Sehemu ya 3. Mikutano ya Wilaya**

A. **Mkutano**

1. Kutakuwa na mkutano wa mwaka wa wilaya wa kutoa ripoti, kuomba, kueleza, kutia moyo, kuwakilisha mpango, na kuendeleza shughuli zinazohusu chama.
2. Muda na mahali pa mkutano utaamuliwa na baraza la wilaya kwa kushauriana na msimamizi wa wilaya.
3. Ushirika
   a. Ni washirika wa wilaya husika pekee ndio wataruhusiwa kuhudumu kama washirika kwa wadhifa wao au wajumbe walioteuliwa.
   b. Washirka wa mkutano kwa wadhifa wao watakuwa baraza la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa la wilaya, msimamizi wa wilaya, wahudumu wote waliopewa wajibu na wahudumu washirika wanaolipwa mshahara wa makanisa ya mtaa; washirika waumini wa halmashauri ya wilaya; kiongozi wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa wa mtaa wa mwaka wa kikao ambacho kimekamilika hivi punde na kiongozi mpya wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa walioteuliwa au naibu wapya wa kiongozi walioteuliwa kama kiongozi mpya aliyeteuliwa hawezi kuhudhuria; mshirika wa Baraza la Dunia la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa; wahudumu waliopewa

wajibu ambao wamestaafu; wamishenari waliostaafu, wamishenari walio kwenye kazi ya likizo nyumbani; na wamishenari wateule; na kiongozi wowote wa hapo awali wa wilaya ambao wamehifadhi ushirika wao kwenye wilaya.

c. Wajumbe walioteuliwa kutoka kwa kila kanisa la mtaa au misheni ya aina ya kanisa watakuwa washirika wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa (umri wa miaka 15 au zaidi). Hesabu ya wajumbe walioteuliwa italingana na kanuni ifuatayo: wajumbe wawili kutoka kwa kila Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa ya mtaa ya washirika 25 au wachache, na mjumbe mmoja zaidi wa kila washirika 25 walioongezwa au sehemu kuu inayohusika. Ushirika utalingana na ushirika wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa ulioripotiwa katika mkutano wa mwaka wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa wa mtaa wakati uteuzi utakuwa unafanyika.

4. Wajumbe watakaokuwepo watahusisha watu wengi.

**B. Baraza**

Baraza la wilaya litakutana angalau mara mbili kwa mwaka kutekeleza shughuli katika muda wa mikutano ya wilaya. Zaidi, mikutano maalum inaweza kupangwa na kiongozi. Washirika wengi wa baraza watahusisha watu wengi.

**Sehemu ya 4. Mikutano ya Kimataifa**

A. **Mkutano**

1. Kutakuwa na Mkutano wa Dunia wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa papo hapo kutangulia Kikao Kikuu kutoa ripoti, kuomba, kueleza, kutia moyo, kuwakilisha mipango, na kusimamia shughuli zinazohusu chama. Wengi wa wajumbe waliojiandikisha watajumlisha watu wengi.
2. Muda na mahali pa Mkutano utaamuliwa na Barara za Kimataifa kwa kushauriana na msimamizi mkuu wa eneo. Baraza la Kimataifa litaidhinisha sehemu zote rasmi.
3. Ushirika

   a. Washirika wa Mkutano wa Dunia kwa wadhifa wao watakuwa washirika wa Baraza la Dunia; kiongozi wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya bila kuangalia hali ya uratibu wa wilaya, au katika hali ambayo kiongozi wa wilaya hataweza kuhudhuria, naibu wa kiongozi wa wilaya anaweza kuruhusiwa kuwakilisha wilaya kwa haki na fursa zote.

b. Wajumbe na wapokezi kwenye Mkutano wa Dunia watateuliwa kwa kura ya siri katika mkutano wa wilaya. Wapokezi wanaweza kuteuliwa kwenye kura tofauti ya siri au kwa mapendekezo ya baraza la wilaya kwenye kura iyo hiyo ya siri kama wajumbe. Wajumbe na wapokezi wanaweza wanaweza kuchaguliwa kwa kura za wengi na kura ya siri kwa kuidhinishwa na theluji-mbili za kura za mkutano wa wilaya kwa mapendekezo ya baraza la wilaya. (Tazama sehemu ya 3.c. kwa uamuzi wa hesabu ya wajumbe na muda wa uchaguzi).

c. Wajumbe walioteuliwa kwenye Mkutano wa Dunia wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa watalinganishwa na mtindo ufuatao: wajumbe wawili kutoka kila awamu ya 3 na awamu ya 2 ya wilaya ya washirika 1,000 au chini yake, isipokuwa washiriki, na mjumbe mwingine mmoja kwa kila washirika walioongezwa 700 au sehemu kuu inayohusika. Ushirika utalinganishwa na ushirika wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa ulioripotiwa katika mkutano wa wilaya wakati uteuzi utakuwa unafanyika. Kamati teule ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa itateuwa wajumbe. (Tazama *Kitabu cha Mwongozo* kifungu cha 200.2 kwa ufafanuzi wa awamu za wilaya.) Baraza la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa la wilaya litaamua hesabu ya wapokezi ambao mkutano wa wilaya utachagua.

d. Mjumbe mmoja mmishenari wa kimataifa aliyeagizwa wa kila jimbo la Misheni ya Kimataifa la wamishenari 50 au chini yake wa kimataifa walioagizwa, au wajumbe wamishenari wa kimataifa walioagizwa kwa kila jimbo la wamishenari walioagizwa wa kimataifa 51 au zaidi watateuliwa na kuchaguliwa kutoka na wamishenari walioagizwa wa kimataifa waliopewa wajibu wanaotumika katika jimbo hilo kwa kura ya siri iliyotolewa kwa ofisi ya msimamizi wa dunia wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa. Kura ya kwanza ya siri itakuwa kura ya siri iliyoteuliwa ya kuamua angalau majina mawili ya uchaguzi kwa wingi wa kura ya siri.

e. Wajumbe watahitajika kuchaguliwa kwa kura ya siri na mkutano wa wilaya kati ya miezi 16 ya Mkutano wa Kimataifa au kati ya miezi 24 katika sehemu ambazo vyeti vya kusafiri au matayarisho yasiyotarajiwa yanahitajika.

f. Mjumbe yeyote aliyechaguliwa atakuwa anaishi wakati wa Mkutano wa Kimataifa kwenye wilaya ambapo ana ushirika wakati wa uchaguzi. Kama mjumbe yeyote aliyechaguliwa

atahama kutoka kwa wilaya, nafasi ya kuwakilisha wilaya zamani inapotea. Nafasi hii haihusu mtu yeyote ambaye makazi yake yako tu karibu na mipaka ya wilaya kutoka sehemu ya ushirika wa kanisa.

g. Katika hali ambayo kiongozi wa wilaya, naibu wa kiongozi wa wilaya, mjumbe aliyechaguliwa, mjumbe mpokezi aliyechaguliwa, au wajumbe wapokezi waliochaguliwa hawataweza kuhudhuria Mkutano wa Kimataifa na jambo hili litambuliwe baada ya mkutano wa mwisho wa wilaya kabla ya Mkutano wa Kimataifa, basi wajumbe wengine wapokezi wanaweza kuteuliwa na baraza la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa la wilaya, au katika hali ambayo hakuna baraza la wilaya, kiongozi wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya kwa idhini ya msimamizi wa wilaya.

**B. Mikutano wa Baraza**

Baraza la Dunia Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa litakutana kila mwaka wakati wa kipindi cha miaka minne ya kuendeleza shughuli zinazohusu mpango. Wengi wa washirika wa baraza katika ofisi watajumlisha watu wengi.

## Nakala ya VII. Fedha

### Sehemu ya 1. Zilizochangishwa na Kanisa la Mtaa

### A. Fedha za Uinjilisti wa Ulimwengu

1. Fedha zote zilizochangishwa na Fedha za Uinjilisti wa Ulimwengu (FUU) zitatumwa kwa mweka hazina mkuu.
2. Fedha za Uinjilisti wa Ulimwenguni zinachangishwa kulingana na mtindo ufuatao: kila kanisa litachangisha asilimia 5.5 ya fedha yao.
3. Makanisa yanaweza kuomba hisani ya Fedha za Uinjilisti wa Ulimwengu kupitia njia tofauti, kama vile Ahadi ya Imani, Matoleo ya Pasaka na ya Shukrani, matoleo ya kawaida ya Fedha za Uinjilisti wa Ulimwengu, matoleo ya Maombi na ya maombi ya Kufunga.

### B. Matoleo ya Misheni Yaliyoidhinishwa

c. Nafasi itatolewa ya kutoa Matoleo ya Misheni Yaliyoidhinishwa juu ya matoleo ya Fedha za Uinjilisti wa Ulimwengu.

d. Matoleo ya Misheni yaliyoidhinishwa na yaliyoongezwa yanaweza kuidhinishwa na kuhalalishwa na kuidhinishwa na Kituo cha Huduma ya Mnazareti cha Kimataifa.

e. Baraza la Fedha za Uinjilisti wa Ulimwengu la Kimataifa litahalalisha Matoleo yote ya Misheni Yaliyoidhinishwa ambayo yameendelezwa na kuchangishwa kupitia Fedha za Uinjilisti wa Ulimwengu kwa kiwango cha kimataifa.

**C. Fedha Zilizotengwa**

Hakuna sehemu ya Fedha za Uinjilisti wa Ulimwengu na Mateleo ya Misheni Yaliyoidhinishwa yaliyochangishwa na kanisa la mtaa au kanisa la wilaya yatatumiwa kwa kusudi lolote la mtaa au la wilaya au sababu zingine zozote mbali na misheni ya Mnazareti.

**D. Matumizi ya Mtaa**

Halmashauri ya kanisa la mtaa itahakikisha bajeti inayofaa kwa matumizi ya Fedha za Uinjilisti wa Ulimwengu katika kanisa la mtaa, ikijumlisha kuangaziwa kurudisha malipo yaliyotumiwa ya uongozi wa mtaa.

**Sehemu ya 2. Zilizochangishwa na Wilaya**

Kamati ya Fedha ya Wilaya itahakikisha kwamba bajeti inayofaa inaendelea kwa matumizi ya Fedha za Uinjilisti wa Ulimwengu kwenye wilaya, ikijumlisha kuangaziwa kurudishwa kwa malipo yaliyotumiwa ya uongozi wa wilaya.

**Sehemu ya 3. Malipo**

Huduma ya Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa itakuwa huduma ya upendo kwa kanisa. Hakuna mshahara utalipwa kwa kiwango chochote-cha mtaa, wilaya, kimataifa, isipokuwa kwa msimamizi wa kimataifa, ambaye ameajiriwa na Kanisa la Mnazareti.

Malipo ya kutosha yatatolewa kwa matumizi ya washirika wa baraza katika viwango vyote vya mtaa, wilaya, na kimataifa.

## Nakala ya VIII. Sera na Utaratibu

Baraza la Fedha za Uinjilisti wa Ulimwengu la Kimataifa litaanzisha sera zingine na utaratibu wa Fedha za Uinjilisti wa Ulimwengu zitakazowekwa katika Kitabu cha Maelezo cha Fedha za Uinjilisti wa Ulimwengu pamoja na Katiba yake.

## Nakala ya IX. Mamlaka ya Bungeni

Sheria zinazohusishwa katika toleo la Kanuni za Utengamano za Robert Lililoboreshwa, wakati haziko katika mzozo na shria zinazotakikana, Nakala ya Ushirikishaji ya Kanisa la Mnazareti, Katiba ya Fedha za Uinjilisti wa Ulimwengu, na sheria zingine zozote za utaratibu ambao Fedha za Uinjilisti wa Ulimwengu inaweza kupendekeza, itatawala mpangilio.

**Nakala ya X Marekebisho**

Katiba ya Fedha za Uinjilisti wa Ulimwengu inaweza kurekebishwa na theluji-mbili za kura za washirika ambao wako na wanapiga kura katika Mkutano wa Kimataifa wa Misheni za Mnazareti ya Kimataifa.

# SURA YA TATU

# HUDUMA ZA SHULE YA JUMAPILI NA UANAFUNZI ZA KIMATAIFA

## 812. SHERIA ZA HUDUMA ZA SHULE YA JUMAPILI NA UANAFUNZI ZA KIMATAIFA

### MAELEZOYAMISHENI

Misheni ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi ya Kimataifa (HSJUK) nikutekeleza Agizo Kuu kwa watoto, vijana, na watu wazima katika kutayarisha muda wa maisha wakuwafanya wanafunzi wa Kristo katika mataifa.

### KUSUDI

Kusudi la Huduma ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa ni:

A. Kuwa watu wa maombi, kuhusika katika Neno, kuwafanya wanafunzi wawe kama Kristo.
B. Kujenga uhusiano wa makusudi na watu wasiofikiwa hadi wawe kama wanafunzi wa Kristo na kuwafanya wanafunzi kama Kristo.
C. Kufundisha Neno la Mungu kwa watoto, vijana na watu wazima ili waweze kuokolewa, watakaswe kabisa, na kukomaa katika ujuzi wa Kikristo ambao unaleta matokeo ya huruma, uinjilisti, elimu ya Kikristo, na kufanya wanafunzi.
D. Kuhimiza kila mtu kujihusisha kwa uaminifu katika huduma ya uanafunzi kama vile Shule ya Jumapili/mafunzo ya Biblia, vikundi vidogo, na huduma zingine za kuwafanya wanafunzi.

### NAKALA YA 1 USHIRIKA WA HUDUMA ZA SHULE YA JUMAPILI NA UANAFUNZI ZA KIMATAIFA

**Orodha ya Walioandikishwa**

Kila kanisa la mtaa linapaswa kujitwika jukumu la kuwafikia watu wote wasiookoka katika jamii. Kila huduma ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa itakuwa na orodha ya walioandikishwa. Orodha ya walioandikishwa itajumuisha kila mtu ambaye jina lake na mawasiliano/kufuatilia kwa ujumbe inapatikana. Mara tu mtu anapoongezwa kwenye orodha ya walioandikishwa, kanisa la mtaa

linafaa kufanya bidii ya kumhudumia yule mtu anapoletwa katika ushirika wa kanisa hilo. Walimu/viongozi wa kila huduma watasimamia mawasiliano ya kawaida na muungano kati ya washirika wa kundi na wale walio kwenye orodha ya walioandikishwa.

Jumla ya watu wote walio kwenye orodha ya walioandikishwa ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa itaripotiwa katika Ripoti ya Mchungaji ya kila Mwaka (RMM). Orodha ya walioandikishwa inajumlisha vikundi vyote vya umri vya Shule ya Jumapili, mikutano ya uanafunzi, mafunzo ya Biblia, na huduma zote za Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa.

**SEHEMU YA 1.** Wahusikakatika huduma zifuatazo watajumlishwa kwenye orodha ya walioandikishwa:

a. Orodha ya watoto wachanga: Watoto wenye umri wa chini ya miaka minne ambao, pamoja na wazazi wao, hawahudhurii huduma yoyote ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa wanaweza kuandikishwa kwenye Orodha ya Walioandikishwa kama Orodha ya Watoto wachanga.
b. Idara ya Nyumbani: Mtu yeyote ambaye kwa sababu za ulemavu wa mwili au hali ya kazi yake hawezi kuhudhuria huduma ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa anaweza kuandikishwa kwenye orodha ya walioandikishwa.
c. Makao ya Uuguzi/Kituo cha Ahueni/Makao ya kutunza Wagonjwa, n.k.: Mkazi yeyote katika moja ya makao haya ambaye anahusika katika mafundisho ya kawaida ya mtaala ulioidhinishwa.
d. Kanisa la Misheni Ambalo Halijaratibiwa: Kundi lolote linalodhaminiwa na kanisa la mtaa au wilaya ambayo wanakutana kila juma angalau kwa nusu saa kujifunza kanuni za kibiblia na/au mtaala ulioidhinishwa na lengo la kuwa Kanisa la Mnazareti la mtaa lililoratibiwa.
e. Malezi ya Watoto/Shule: Kundi lolote la wanafunzi katika malezi ya watoto/shule ya Mnazareti (uzazi wa pili) inayodhaminiwa/kuendelezwa na Kanisa la Mnazareti la mtaa.
f. Vituo vya Ujenzi wa Watoto (VUW): Vinavyodhaminiwa/ kuendelezwa na Kanisa la Mnazareti la mtaa.

**SEHEMU YA 2.** Kuondolewa kwa Majina

Kuondolewa kwa Majina kunafaa kufanywa tu kwa idhini ya mchungaji wakati mtu huyo:

a. amehama mjini.
b. anajiunga na darasa lingine la Shule ya Jumapili, kundi la ufuasi, au kanisa.
c. hasa anapo omba jina lake kuondolewa.
d. anapofariki.

## NAKALA YA II. MAHUDHURIO YA SHULE YA JUMAPILI NA UANAFUNZI WA KIMATAIFA

Kusudi la kuhesabu na kutoa ripoti ya mahudhurio ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa katika kanisa la mtaa ni kupima (kunakofaa zaidi kwa juhudi ya kanisa hilo katika kuwafanya wanafunzi wa Kristo. Juhudi zote za Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa zinapaswa kumwelekeza mtu kuwa mwanafunzi wa Kristo, mshirika wa kanisa, na yule anayemuandaa mwanafunzi.

Mahudhurio ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa yanajumlisha sehemu za Shule ya Jumapili na Vikundi vya uanafunzi. Viwango hivi vitahesabiwa kila juma kwa kanisa la mtaa kulingana na uongozi uliyoorodheshwa hapa chini na katika Nakala ya 1, Sehemu ya 1 hapo juu.

Ofisi ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa ya jimbo inahitaji kutoa ripoti za Orodha ya Walioandikishwa na kiasi cha kila juma cha mahudhurio ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa kutoka kila wilaya ili kukusanya rekodi iliyo sahihi ya ukuaji wa Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa katika madhehebu kila mwaka.

**SEHEMU YA 1**. Maelezo na Ripoti

Mahudhurio ya Vikundi vyote vya uanafunzi vitaelezwa kama watu waliohusika katika mafundisho ya Biblia na matumizi ya kanuni za Biblia za kuwa kama Kristo.

a. Kwa makanisa mengi, hesabu ya Shule ya Jumapili/sehemu za mafundisho ya Biblia iliyofanywa itakuwa 52 na itaripotiwa. Halmashauri ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa ya Wilaya, kwa kushauriana na msimamizi wa wilaya, wataamua mambo ya kipekee yanayostahili na kuripotiwa kwa mara kwa mara.
b. Kanisa la mtaa lililo na zaidi ya aina moja ya kundi la huduma la uanafunzi linapaswa kuweka pamoja hesabu ya kila juma ya mahudhurio na kutoa ripoti ya kiasi kimoja cha mwaka katika Ripoti ya Mchungaji ya kila Mwaka.

c. Kwa vile huduma za uanafuzni zinaweza kuanza au kuisha wakati wowote katika mwaka wa kanisa, kiwango cha kila mwaka kinapaswa kuamuliwa kwa kugawanyisha hesabu iliyowekwa pamoja na hesabu ya majuma ambayo huduma ziliendelezwa.

## NAKALA YA III. HALMASHAURI YA SDMI YA MTAA

Majukumu ya Halmashauri ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa ya mtaa yanaelezwa katika *Kitabu cha Mwongozo* kifungu cha 145-145.10 na yanajumlisha:

1. Kufanya kazi pamoja na mchungaji na halmashauri ya kanisa la mtaa kuendeleza/kupanga Halmashauri ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa.
2. Kufanya kazi pamoja na mchungaji kujenga na kuanzisha mpango mwafaka wa uanafunzi katika kanisa la mtaa ambao unaambatana na mikakati/malengo na unaokubaliana na maono ya wilaya na misheni ya Kanisa la Mnazareti.
3. Kufanya utafiti, kuunda, kutengeneza mtaala unaokubaliana na thiolojia na misheni ya Kanisa la Mnazareti iliyoandaliwa na uchapishaji wa madhumuni ya Kanisa la Mnazareti, kusimamia na kufuatilia: ratiba ya mafundisho ya uanafunzi wa kukusudia, kuinua kanisa, kufundisha wafanyakazi wa huduma wanaohusika katika vikundi vya umri wote wa huduma, na miradi maalum.
4. Kufanya uvumbuzi na kutoa ripoti katika mkutano wa mwaka wa elimu inayoendelea ya kanisa la mtaa na huduma/miradi ya uanafunzi wakichunguza wazi wazi matokeo yake.
5. Kuidhinisha mtaala unaombatana na thiolojia na misheni/miradi/raslimali ya Kanisa la Mnazareti ambao huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa za mtaa zinaweza kutumia.

## NAKALA YA IV. MADARASA NA IDARA ZA SHULE YA JUMAPILI

**SEHEMU YA 1**. Shule ya Jumapili itagawanywa katika madarasa ya watoto na vijana kwa misingi ya umri au kiwango cha shule. Kwa watu wazima madarasa yanafaa kulingana na masomo yanayowavutia, misheni, kichwa, n.k. Mahali yanapohitajika, madarasa ya pamoja yanaweza kuangaziwa.

**SEHEMU YA 2.** Wakati hesabu ya madarasa kati ya umri wa vikundi vya watoto, vijana, au watu wazima yanapoongezeka, umakini utapewa kiwango cha mpango wa umri na usimamizi ukiteuliwa na Halmashauri ya SDMI ya mtaa.

**SEHEMU YA 3**. Kazi ya msimamizi wa idara itaamuliwa na Halmashauri ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa ya mtaa. Majukumu yaliyopendekezwa yameorodheshwa katika kitabu cha mwongozo cha Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa.

## NAKALA YA V. WALIMU NA VIONGOZI WA HUDUMA ZA SHULE YA JUMAPILI NA UANAFUNZI WA KIMATAIFA

**SEHEMU YA 1**. Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa zinajumlisha Shule ya Jumapili ya umri wote, vikundi vidogo, huduma za ndoa, huduma za wanaume, huduma za wanawake, huduma za watoto, Shule za Biblia za likizo, matamanio ya vikund, n.k. Wasimamizi wa huduma/idara na walimu/viongozi watachaguliwa kila mwaka kulingana na *Kitabu cha Mwongozo* 145.8.

**SEHEMU YA 2**. Halmashauri ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa, kwa kushauriana na mchungaji, inaweza kutangaza nafasi ya afisa au mwalimu/kiongozi kuwa wazi ikiwa imeonekana kukosa kufuata kanuni, tabia isiyohitajika au kutotekeleza jukumu.

**SEHEMU YA 3.** Walimu/viongozi wote na wabadilishanaji watapaswa kuwa watu wa maombi, wanaojihusisha na Neno, na kwa makusudi kuwa na kuwafanya wanafunzi wa Kristo.

## NAKALA YA VI. MAJUKUMU YA KIONGOZI HUDUMA ZA SHULE YA JUMAPILI NA UANAFUNZI WA KIMATAIFA

**SEHEMU YA 1**. Msimamizi wa Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa wa mtaa atateuliwa kila mwaka kulingana na *Kitabu cha Mwongozo* 113.10-113.11 na 127. Majukumu ya msimamizi wa Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa yatakuwa:

a. Kusimamia Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa chini ya uongozi wa mchungaji.

b. Kupanga mikutano ya mara kwa mara ya viongozi na walimu wa huduma.
c. Kutoa nafasi za mafundisho kwa walimu na viongozi ambao wako
d. Kila mwaka kuvumbua, kuendeleza, na kuanzisha pamoja na Halmashauri ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa mkakati wa uanafunzi wa kuwafikia walio kwenye Orodha ya Walioandikishwa.
e. Kutoa takwimu ya ripoti ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa mara kwa mara kwa eneo linalohusika, wilaya, au ofisi ya kiwanda.
f. Kuhimiza mahudhurio katika mtaa, eneo, wilaya, kiwanda jimbo, na shughuli za Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa za kimataifa.

**SEHEMU YA 2.** Kazi ya wakurugenzi wa makundi ya rika imefafanuliwa katika *Kitabu cha Mwongozo* 147.1-147.9 na 148.2.

**SEHEMU YA 3.** Halmashauri ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa itateuwa mtu wa kuhifadhi rekodi za Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa. Mtu huyo ataweka rekodi sahihi za Shule yote ya Jumapili za Orodha ya Waliandikishwa, mahudhurio, wageni, na takwimu zingine kama itakavyohitajika na huduma ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa.

**SEHEMU YA 4.** Mahali inahitajika, Halmashauri ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa itateuwa mweka hazina wa kuweka hesabu sahihi za fedha zote zilizokusanywa na Shule ya Jumapili kila juma na kuagiza ugawaji kulingana na maagizo ya Halmashauri. Ripoti ya kila mwezi itatolewa kwa msimamizi wa Shule ya Jumapili.

**SEHEMU YA 5.** Mitaala yote na raslimali zingine zilizotumiwa na Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa zitaidhinishwa na Halmashauri ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa au msimamizi wa Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa au mchungaji.

## NAKALA YA VII. UONGOZI NA UANGALIZI WA WA SHULE YA JUMAPILI NA UANAFUNZI WA KIMATAIFA

**SEHEMU YA 1**. Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa iko chini ya ulinzi wa mchungaji, inawajibika kwa halmashauri ya kanisa la mtaa, chini ya uangalizi wote wa Halmashauri ya Shule ya Jumapili na

Uanafunzi wa Kimataifa na uongozi wa karibu wa msimamizi na wakurugenzi wa makundi ya rika.

**SEHEMU YA 2**. Ikiwa kanisa ambalo limeajiri mkurugenzi wa elimu ya Kikristo litataka kwamba mtu atimize majukumu ya msimamizi wa Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa, kanisa linapaswa kumteuwa mshirika mwingine wa kawaida wa kuwakilisha Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa kwenye halmashauri ya kanisa la mtaa kama mshirika anayepiga. Tunahimiza juhudi zote zinazowezekana zifanywe za kufundisha na kuwaelimisha viongozi wa kawaida wa mtaa kwa uongozi katika Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa.

**SEHEMU YA 3.** Wakati mchungaji/kiongozi/mkurugenzi wa watoto, vijana, watu wazima ameajiriwa na kanisa, mchungaji, kwa kushauriana na halmashauri ya kanisa, Halmashauri ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa, na/au Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, anapewa jukumu la huduma za watoto, vijana, au watu wazima kwa kiwango cha umri wa mwajiriwa. Katika hali hiyo, mwajiriwa anayehudumia huduma za watoto, vijana, au watu wazima anatekeleza baadhi ya kazi alizopewa mkurugenzi wa Huduma za Watoto za mtaa (HW), kiongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, au mkurugenzi wa Huduma za Watu Wazima (WW). Hata hivyo, jukumu la mkurugenzi wa Huduma za Watoto, kiongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa, au mkurugenzi wa Huduma za Watu Wazima zinabaki kutoa uongozi wa ushirika wa kawaida ulio muhimu, usaidizi na uwakilishi wa huduma za kundi la rika la mtaa. Mchungaji na mwajiriwa wa huduma ya kundi la rika anashauriana na Halmashauri ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa na Baraza la Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa kueleza majukumu na kazi za nafasi tatu za kawaida.

## NAKALA YA VIII. MIKUTANO YA SHULE YA JUMAPILI NA UANAFUNZI WA KIMATAIFA

**SEHEMU YA 1.** Mikutano ya Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa ya Wilaya

Ni muhimu kwamba kila wilaya ipange Mkutano wa Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa kila mwaka ilikutia moyo, kuhimiza, na kutoa ripoti za shughuli na uteuzi. Kuendelezwa Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa na kundi dogo la huduma za kuwafanya

wanafunzi inafaa kuambatana na kila mkutano.

a. Washirika wa Mkutano wa Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa ya Wilaya kwa wadhifa wao watakuwa: msimamizi wa wilaya; wachungaji wote, makasisi wanaohudumu, wahudumu wenye vyeti wanaohudumu, makasisi wanaohudumu waliostaafu, washirika washiriki wanaohudumu, mwenyekiti wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa wilaya; wakurugenzi wa Huduma za Watoto na Huduma za Watu Wazima; kiongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya; kiongozi wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa wa wilaya; wasimamizi wote wa Shule ya Jumapili na Uanafunzi wa Kimataifa wa mtaa; wakurugenzi wa Huduma ya Watoto na Huduma za Watu Wazima wa mtaa, kiongozi wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa wa mtaa; washirika walioteuliwa wa Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa ya Wilaya; washirika wa kawaida wa Halmashauri ya Wilaya; na walimu wowote wa Mnazareti walioajiriwa wa elimu ya Kikristo na ushirika kwa wilaya hiyo; na maafisa wa kiwanda, wa jimbo na wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa ya kimataifa.
b. Katika kuongezea kwa orodha ya wajumbe hapo juu, kila kanisa la mtaa katika mkutano wa mwaka litateuwa wajumbe zaidi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa kwenye Mkutano. Hesabu hii itakuwa asilimia 25 ya hesabu ya maafisa, walimu, na viongozi wa huduma za Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa za mtaa. Kama wajumbe walioteuliwa hawataweza kuhudhuria mkutano, wajumbe wa kubadilishana watatengwa kulingana utaratibu wa kura zilizopokelewa.
c. Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa ya Wilaya itachagua kamati ya uteuzi ya kuchagua mara mbili idadi ya wateule kwa nafasi zilizochaguliwa za mwenyekiti wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa wilaya na washirika watatu walioteuliwa wa Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa ya Wilaya, ambao hatimaye watateuliwa kwa wingi wa kura kwenye Mkutano wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa Wilaya. Wateule hawa lazima wawe washirika wa Kanisa la Mnazareti, wanaohusika kamili katika moja ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa, na watafaa kuchaguliwa kutoka kwa vikundi tofauti vya rika (watoto, vijana na

walimu/wafanyakazi wa watu wazima).

d. Wajumbe katika Mkutano wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa Wilaya wanaweza kuteuwa mwenyekiti wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa wilaya (*Kitabu cha Mwongozo* kifungu cha 242) na washirika watatu walioteuliwa wa Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa ya Wilaya na wajumbe kwenye Mkutano wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa Kimataifa.

**SEHEMU YA 2. Mkutano wa SDMI wa Kimataifa**

Katika kuhusiana na Kikao cha Wilaya, Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa itatazama Mkutano wa Kimataifa na wajumbe kutoka sehemu moja au zaidi ulimwenguni. Wajumbe walioteuliwa (na wageni) watakutana kwa makusudi ya kutia moyo, kuhimiza, na kufunza ili kutunza na kuendeleza ushirikiano katika kutimiza misheni ya kusudi la Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi ya Kimataifa.

Mkutano wa Kimataifa pia utajumlisha mikutano ya jimbo inayojumuisha Baraza la Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa la Jimbo, mkurugenzi wa jimbo, msimamizi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa jimbo, na wajumbe wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa ya wilaya walioteuliwa kutoka kwa jimbo hilo. Mikutano itakutana kwa makusudi ya kuteuwa mteule wa kuchukuliwa wa kuhudumu kama mwakilishi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa kwenye Halmashauri ya Wilaya. Baraza la Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa la Kimataifa na mkurugenzi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa Kimataifa hatimaye atachagua jina moja kutoka kwa wale walioteuliwa na kupeana jina hilo kwenye Kikao Kikuu kwa kuidhinishwa (*Kitabu cha Mwongozo* kifungu cha 332.6)

a. Wajumbe walioandikishwa kwenye Mkutano wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa Kimataifa kwa wadhifa wao watakuwa: wasimamizi wa wilaya, wenyeviti wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa wilaya, wakurugenzi wa Huduma za Watoto wa wilaya na Huduma za Watu Wazima wa wilaya; wasimamizi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa jimbo, wasimamizi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa eneo, wasimamisi

wa Huduma za Watoto na Huduma za Watu Wazima wa jimbo; na wakurugenzi na wafanykazi wa kuajiriwa wa ofisi ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa ya kimataifa. Zaidi, walimu wa elimu ya Kikristo katika vituo vya Mnazareti, vyuo, na seminari wanaweza kuhudhuria kama wajumbe.

b. Katika kuongeza kwa wajumbe kwa ajili ya wadhifa wao, kila wilaya inapaswa kuchagua wajumbe wengine wanne au idadi sawa kwa asilimia kumi ya makanisa yaliyoratibiwa katika wilaya, ile iliyo kubwa.

c. Miongozo ifuatayo inapaswa kufuatwa wakati wa uchaguzi wa wajumbe katika Mkutano wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa Kimataifa:

   1. Kamati ya Uteuzi itakuwa na msimamizi wa wilaya, mwenyekiti wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa wilaya, na angalau watu wengine watatu waliochaguliwa na Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa ya Wilaya. Watachagua mara tatu idadi ya wateuliwa watakaochaguliwa.
   2. Mkutano wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa Wilaya utachagua idadi sawa ya wajumbe nawapokezi wanaowakilisha huduma mbalimbali za Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa (ikihusisha walimu/wafanyakazi wa vijana). Wale waliochaguliwa wanapaswa kuhusika kikamilifu katika sehemu husika ambazo wamechaguliwa. Idadi ya wapokezi waliochaguliwa inapaswa kuhusisha maafisa wa wilaya kwa wadhifa wao. Watu hawatachaguliwa ambao watahudumu kama wajumbe kwenye Mkutano wa Misheni ya Mnazareti wa Kimataifa kwa sababu mikutano mitatu inafanyika kwa wakati mmoja.
   3. Wajumbe watachaguliwa kwa kura ya sirika katika Mkutano wa Wilaya wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa katika kipindi cha miezi 16 cha mkutano cha Kikao Kikuu au katika kipindi cha miezi 24 katika sehemu ambapo vyeti vya usafiri au matayarisho ya siyo tarajiwa yana hitajika.
   4. Kadiri inavyo wezeka na, chagua idadi sawa ya washirika na makasisi-yaani asilimia 50 wawe washirika na asilimia 50 wawe wahudumu kikamilifu, makasisi, mashemasi, au wahudumu waliopewa vyeti. Wakati idadi hailingani, mwakilishi atayeongezwa atakuwa mshirika.
   5. Viongozi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za

Kimataifa ya Wilaya walioteuliwa kabla ya na wanashikilia ofisi wakati wa Mkutano wa Kimataifa watakuwa washirika wa mkutano kwa wadhifa wao.

6. Wajumbe wote waliochaguliwa na wanaohudhuria Mkutano wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa Wilaya watakuwa na haki ya kupiga kura kwa wawakilishi wa Mkutano wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa Kimataifa.
7. Kupiga kura za wengi kutatosha katika uchaguzi.
8. Ikiwawajumbe waliochaguliwa hawawezi kuhudhuria Mkutano wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa Kimataifa, wajumbe wapokezi watapewa nafasi kwa utaratibu wa kura zilizopokewa., wajumbe wapo kezi watapewa nafasi kwa utaratibuwa kura zilizopokewa.
9. Wakati wa kuhudhuria Mkutano wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa Kimataifa, kila mjumbe atakaa na kuwamshirika wa Kanisa la Mnazareti kwenye wilaya ambayo alichaguliwa kuwakilisha.
10. Wajumbe ambao watahudhuria mkutano wanapaswa kuwa na msaada wa kifedha kutoka kwa wilaya inayolingana kwa gharama zilizotolewa kutoka kwa wajumbe wa Mkutano wa wilaya ya Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa na Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa.
11. Kama uchaguzi wa wajumbe kwa Mkutano wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa Kimataifa hautafanyika katika Mkutano wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa Wilaya, wajumbe watachaguliwa katika Kikao cha Wilaya.

## NAKALA YA IX. BARAZA LA SDMI LA KIMATAIFA

**SEHEMU YA 1.** Kusudi

Kuendeleza ratiba yote ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa kwa kufanya kazi na viongozi wa jimbo, kiwanda, wilaya, na Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa ya mtaa katika kuunganisha mikakati ya kimataifa kwa kuwafanya wanafunzi kunakofaa.

**SEHEMU YA 2.** Utunzi

a. Baraza la Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa la Kimataifa likutana angalau kila mwaka, aidha binafsi

au kupitia mitandao, na litakuwa na msimamizi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa jimbo kutoka kila Misheni ya Kimataifa ya jimbo na msimamizi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa Kimataifa, ambaye ataongoza mkutano.

b. Wasimamizi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa jimbo watachaguliwa na msimamizi wa jimbo anayehusika kwa kushauriana na mkurugenzi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa Kimataifa.

**SEHEMU YA 3**. Kazi za wasimamizi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa jimbo itakuwa ni:

a. Kuwakilisha na kuongoza makusudi ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa kwenye jimbo lao.
b. Kutoa maono na kutia moyo inayohusiana kuanzisha mikakati na vifaa vinavyoambatana na maono ya jimbo kwa kanisa.
c. Kufanya utafiti, kuunda, kuendeleza, kusimamia, na kufuatilia kuanzishwa kwa mafunzo ya maendeleo ya uongozi wa ufuasi wa kukusudia wa jimbo, kiwanda, na kuendeleza kwa kanisa la wilaya, kuunganisha huduma zote za kanisa kwa jukumu la kufanya wanafunzi wa Kristo.
d. Kuhudhuria na kutoa ripoti katika mkutano wa mwaka wa Baraza la Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa Kimataifa.
e. Kuleta pamoja wateuliwa kwa uwakilishi wa Halmashauri Kuu ya Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa, waliochaguliwa na mkutano wao wa jimbo, kwa Baraza la Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa la Kimataifa. Baraza litawakilisha jina moja kwa Kikao Kikuu kwa uteuzi kama mwakilishi wa Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa wa Halmashauri Kuu *(Kitabu cha Mwongozo* kifungu cha 332.6).

## NAKALA YA X. MAREKEBISHO YA HUDUMA ZA SHULE YA JUMAPILI NA UANAFUNZI ZA KIMATAIFA

Sheria hizi zinaweza kurekebishwa kwa kura za wengi za Halmashauri Kuu ambao wako na wanapiga kura.

# SEHEMU YA KUMI

# FOMU

SURA YA KWANZA

KANISA LA MTAA

KIKAO CHA WILAYA

HATI ZA MASHTAKA

## I. KANISA LA MTAA

**KUMBUKA: Fomu ifuatayo inaweza kutayarishwa na kutumiwa na kanisa la mtaa kama vile itakavyohitajika**

### 813. Cheti cha Mhudumu wa Mtaa

CHETI HIKI KINATHIBITISHA kwamba _______________ amepewa cheti kama Mhudumu wa Mtaa katika Kanisa la Mnazareti kwa mwaka mmoja, ili mradi roho na mwenendo wake uko kama inavyostahili injili ya Kristo, na kwamba mafundisho yake yanalingana na imani ya Maandiko Matakatifu kama inavyokubaliwa na Kanisa lililotajwa hapa.

Kwa Amri ya Halmashauri ya Kanisa Mnazareti la __________ (jina la Kanisa)

Imetolewa _________________ (jina la mahali), tarehe __________ mwezi wa ____________ mwaka wa _________

______________________________________________

Mwenyekiti

______________________________________________

Katibu

### 814. Pendekezo la Kikao cha Wilaya

(itakamilishwa kila mwaka kwa wahudumu waliopewa cheti cha_wilaya *(Weka alama kwenye halmashauri itakayohitajika)*

- ☐ Halmashauri ya Kanisa la Mnazareti la __________________________
- ☐ Halmashauri ya Wilaya ya (*Kitabu cha Mwongozo* 225.13) inapendekeza ____________________________kwa (Halmashauri ya Hati za Kuhitimu za Wahudumu) katika Kikao cha Wilaya kwa:
  - ☐ **Cheti cha Mhudumu cha Wilaya**
  - ☐ **Kufanywa upya kwa Cheti cha Mhudumu cha Wilaya**
  - ☐ **Kufanywa upya kwa Cheti cha Shemasi**
  - ☐ **Kufanywa upya kwa Cheti cha Mkurugenzi wa Elimu ya Kikristo**
    **Kuthibitishwa kwa Kazi ya Mhudumu** (*Kitabu cha Mwongozo* 503-528)
- ☐ **Mhudumu wa Elimu ya Kikristo (MEK)** (wahudumu walioajiriwa na shule ya kanisa la mtaa)
- ☐ **Elimu (ELI)** (aliyeajiriwa kuhudumu kwa usimamizi wa waajiriwa au sehemu moja ya taasisi za kielimu za Kanisa la Mnazareti)

- ☐ **Muinjilisti, Aliyeandikishwa (MA)** (amejitolea kusafiri na kufundisha injili kama huduma yake ya msingi, akiendeleza ufufuo na kuhubiri injili nje ya nchi)
- ☐ **Majukumu Makuu, Mmishenari** (aliyeteuliwa) na Halmashauri Kuu kupitia Kamati ya Misheni ya Kimataifa kuhudumia kanisa)
- ☐ **Majukumu Makuu, Mengine** (ya aliyeteuliwa au kuajiriwa kuhudumu katika Kanisa Kuu)
- ☐ **Mchungaji -**
- ☐ **Huduma ya Kiuchungaji ya Muda Mrefu**
- ☐ **Huduma ya Kiuchungaji ya Muda Mfupi** (mchungaji msaidizi, akitekeleza huduma ya kichungaji kwa kushirikiana na kanisa, katika sehemu maalum za huduma zilizotambuliwa na kuidhinishwa na usimamizi unaofaa, na uwakili uliopewa cheti na idhini)
- ☐ **Muinjilisti wa Nyimbo, Aliyesajiliwa** (anatoa sehemu kubwa ya wakati wake kwa huduma ya uinjilisti kupitia muziki kama kazi yake ya msingi)
- ☐ **Huduma Maalum/Madhehebu ya Kutegemeana** (katika huduma iliyo hai katika hali isipokuwa imetolewa, ambayo ni lazima iidhinishwe na kikao cha wilaya baada ya kupendekezwa na Halmashauri ya Wilaya. Watu waliopewa Huduma Maalum wanahitajika kuhifadhi uhusiano na Kanisa la Mnazareti na litatoa katika maandishi kwa Halmashauri ya Wilaya kila mwaka, hali ya muungano wao unaoendeleza na Kanisa la Mnazareti.)
- ☐ **Mwanafunzi**
- ☐ **Asiyepewa wajibu**

Rejea matakwa yatayohitajika ya kuwekwa wakfu (*Kitabu cha Mwongozo* 533.3, 534.3) na pia hatua za kuhalalishwa kwa uhusiano, iwe ya kulipwa au kutolipwa. (*Kitabu cha Mwongozo* 159-159.3) Jambo hili ni muhimu kwa kuanzisha na kuhifadhi historia ya huduma ya mtahiniwa.

Ikiwa Jukumu la Huduma lililopeanwala Huduma ya Kiuchungaji ya Muda Mrefu au Huduma ya Kiuchungaji ya Muda Mfupi limependekezwa kwa mwaka unaofuata, je, lina idhini iliyoandikwa ya msimamizi wa wilaya iliyopokelewa (129.27; 159-159.2)?

☐ Ndiyo ☐La

________________________________________

________________________________________

Ikiwa cheo kando na "Mwanafunzi" au "Asiyepewa Wajibu" kama vile ilivyoonyeshwa hapo juu, kinaeleza uhusiano wa rasmi ambao upo na mtahiniwa, kama ilivyoidhinishwa na halmashauri ya kanisa na msimamizi wa wilaya.

______________________________________________________________

______________________________________________________________

Tunathibitisha kwamba ____________________________ametimiza mahitaji yote ya maombi kama haya.
Kwa kura ya Halmashauri hii ______________ (tarehe), na kwa kupokea barua ya ruhusa kutoka kwa msimamizi wa wilaya hii _____________________(tarehe).

______________________________________________________________
Mwenyekiti

______________________________________________________________
Katibu

Aliyewakilisha ☐ Ripotiwa ☐ Tabia______________

KUMBUKA: Tafadhali weka alama yote ya pendekezo la cheti na pendekezo la thibitisho la kazi ya mhudumu binafsi.

## 815. Cheti cha Sifa

Cheti hiki kinathibitisha kwamba ________________________ ni mshirika wa Kanisa la Mnazareti liloko ____________________ na imependekezwa kwa uaminifu wa Kikristo kwa wale ambao cheti hiki kimewasilishwa kwao.

______________________________________________________________
Mchungaji

Tarehe ______________________, ______________(mwaka)

KUMBUKA: Wakati mtu anapopewa cheti cha sifa, ushirika wake unakoma mara moja katika kanisa la mtaa linalotoa cheti hicho. (111.1)

## 816. Barua ya Kuwekwa Huru

Cheti hiki kinathibitisha kwamba _______________________ hadi tarehe ya barua hii alikuwa mshirika wa Kanisa la Mnazareti liloko _______________________________ na kwa ombi lake, anapewa barua hii ya kumweka huru.

______________________________________________________________
Mchungaji

Tarehe ____________________________, ____________(mwaka)

TAZAMA: Ushirika unamalizika mara moja baada ya kutolewa kwa barua hii ya kuwekwa huru. (112.2)

### 817. Uhamisho wa Ushirika

Cheti hiki kinathibitisha kwamba _________________________ ni mshirika wa Kanisa la Mnazareti lililoko ___________________ na kwa ombi lake, amehamishiwa katika Kanisa la Mnazareti lililoko ____________________ katika Wilaya ya ______________________.

Wakati wa kupokelewa kwa uhamisho huu kutakapothibitishwa katika kanisa la mtaa linalompokea, ushirika wake katika kanisa la mtaa alikotokea, utafikia kikomo.

______________________________________________________________

Mchungaji

______________________________________________________________

Anwani

Tarehe _________________________, _____________(mwaka)

TAZAMA: Barua ya uhamisho inakubalika kwa miezi mitatu tu baada ya kutolewa (111)

### 818. Kukubaliwa kwa Uhamisho

Hii inathibitisha kwamba __________________________________ amepokelewa katika ushirika na Kanisa la Mnazareti lililoko __________________ tarehe _____________________ mwezi wa _________________, mwaka wa ______________________.

______________________________________________________________

Mchungaji

______________________________________________________________

Anwani

## II. KIKAO CHA WILAYA

**819.** Fomu rasmi ya wilaya inawezwa kuchukuliwa kutoka kwa Katibu Mkuu, 17001, Prairie Star Parkway, Lenexa, KS 66220, Marekani

## III. IDHINI YA KUTHIBITISHWA

### Sehemu ya 1. Katika Majaribio ya Ushirika wa Kanisa

### Sehemu ya 2. Katika Majaribio ya Kasisi

### Sehemu ya 3. Katika Majaribio ya Mhudumu Aliyepewa Cheti

820. Idhini ya kuthibitishwa inaweza kuchukuliwa kutoka kwa Katibu Mkuu, 17001, Prairie Star Parkway, Lenexa, KS 66220, Marekeni

**SEHEMU YA KUMI NA MOJA**

# NYONGEZA

VIONGOZI WAKUU

HALMASHAURI YA MABARAZA YA USIMAMIZI,
NA VYUO VYA ELIMU

MAONGOZI YA USIMAMIZI

MAMBO YA KISASA KUHUSU UADILIFU NA JAMII

SURA YA KWANZA

## I. VIONGOZI WAKUU

### 900. Wasimamizi Wakuu

Eugenio R. Duarte
David W. Graves
David A. Busic
Gustavo A. Crocker
Filimao M. Chambo
Carla D. Sunberg

### 900.1. Wasimamizi Wakuu Waliotunukiwa Heshima na Waliostaafu

Eugene L. Stowe, Ametunukiwa Heshima
Jerald D. Johnson, Ametunukiwa heshima
Donald D. Owens, Ametunukiwa heshima
Jim L. Bond, Ametunukiwa heshima
W. Talmadge Johnson, Ametunukiwa heshima
James H. Diehl, Ametunukiwa heshima
Paul G. Cunningham, Ametunukiwa heshima
Nina G. Gunter, Ametunukiwa heshima
Jesse C. Middendorf, Ametunukiwa heshima
Stan A. Toler, Ametunukiwa heshima
Jerry D. Porter, Ametunukiwa heshima
J. K. Warrick, Ametunukiwa heshima

### 900.2. Katibu Mkuu

David P. Wilson

### 900.3. Mtunza Hazina Mkuu

Keith B. Cox

KITUO CHA HUDUMA CHA KIMATAIFA
CHA KANISA LA MNAZARETI
17001 PRAIRIE STAR PARKWAY
LENEXA, KS 66220, MAREKANI

# II. HALMASHAURI, MABARAZA YA USIMAMIZI, NA VYUO VYA ELIMU

## 901. Halmashauri Kuu

WASHIRIKA KWA MAJIMBO YA KANISA

| Kasisi | Muumini |
|---|---|
| | ***Jimbo la Afrika*** |
| Arsenio Jeremias Manjate | Sibongile Gumedze |
| Solomon Ndlovu | Benjamin Langa |
| Stanley Ushe | Angela M. Pereira B. D. V. Moreno |
| | ***Jimbo la Asia Pacific*** |
| Kafoa Muaror | Leonila Domen |
| Min-Gyoo Shin | Joung Won Lee |
| | ***Jimbo la Canada*** |
| D. Ian Fitzpatrick | David W. Falk |
| | ***Jimbo la Marekani ya Kati*** |
| Ron Blake | Judy H. Owens |
| | ***Jimbo la Marekani ya Kati ya Mashariki*** |
| D. Geoffrey Kunselman | Carson Castleman |
| | ***Jimbo la Marekani ya Mashariki*** |
| Samuel Vassel | Larry Bollinger |
| | ***Jimbo la Eurasia*** |
| Sanjay Gawali | David Day |
| David Montgomery | Vinay Gawali |
| Mary Schaar | Christoph Nick |
| | ***Jimbo la Mesoamerika*** |
| Elias Betanzos | Carmen L. Checo de Acosta |
| Walliere Pierre | Abraham Fernandez Gamez |
| Antonie St. Louis | Plinio E. Urizar Garcia |

***Jimbo la Marekani ya Kaskazini ya Kati***

Jim Bond
Larry McIntire

***Jimbo la Marekani ya Kaskazini-Magharibi***

Randall J. Craker
Joel K. Pearsall

***Jimbo la Marekani ya Kusini***

Adalberto Herrera Cuello
Galdina Arrais
Fernando Oliveira
Jacob Rivera Medina
Amadeu Teixeira
Emerson Natal

***Jimbo la Marekani ya Kusini ya Kati***

Terry C. Rowland
Cheryl Crouch

***Jimbo la Marekani ya Kusini-Mashariki***

Larry D. Dennis
Michael T. Johnson
Dwight M. Gunter II
Dennis Moore

***Jimbo la Marekani ya Kusini-Magharibi***

Ron Benefiel
Daniel Spaite

***Elimu***

John Bowling
Bob Brower

***Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa***

Philip Weatherill

***Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa***

Adiel Teixeira

***Huduma za Shule ya Jumapili na Uanafunzi za Kimataifa***

Milon Patwary

**902. Mahakama Kuu ya Rufani**

Hans-Gunter Mohn, *Mwenyekiti*
Janine Metcalf, Katibu
D. Ian Fitzpatrick
Donna Wilson
Brian Powell

**903. Baraza Kuu la Kimataifa la Huduma ya Vijana wa Mnazareti**

Gary Hartke, *Mkurugenzi mkuu wa NYI*
Adiel Teixeira, *Mwenyekiti wa Baraza la NYI*
Ronald Miller, Jimbo la Afrika
Janary Suyat de Godoy, Jimbo la Asia Pacific
Diego Lopez, Jimbo la Eurasia
Milton Gay, Jimbo la Mesoamerika
Christiano Malta, Jimbo la Marekani ya Kusini
Justin Pickard, Jimbo la Marekani/Canada

**904. Baraza Kuu la Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa**

Lola Brickey, *Mkurugenzi Mkuu*
Philip Weatherill, *Kiongozi*
Dawid De Koker, Jimbo la Afrika
Pauline Sheppard, Jimbo la Asia-Pacific
Penny Ure, Jimbo la Canada
Carla Lovett, Jimbo la Marekani ya Kati
Kathy Pelley, Jimbo la Marekani Mashariki ya Kati
Sharon Kessler, Jimbo la Marekani Mashariki
Cathy Tarrant, Jimbo la Eurasia
Blanca Campos, Jimbo la Mesoamerika
Rhonda Rhoades, Jimbo la Marekani ya Kaskazini ya Kati
Debra Voelker, Jimbo la Marekani ya Kaskazini-Magharibi
Antonio Carlos, Jimbo la Marekani ya Kusini
Mary Runion, Jimbo la Marekani ya Kusini ya Kati
Teresa Hodge, Jimbo la Kusini-Mashariki
Martha Lundquiest, Jimbo la Marekani ya Kusini-Magharibi
Verne Ward, Mkurugenzi wa Misheni ya Kimataifa
Msimamizi Mkuu wa Eneo (Mshauri)

**905. Vyuo vya Mnazareti vya Elimu ya Juu Baraza la Kimataifa la Elimu ya Juu**

BARAZA LA KIMATAIFA LA ELIMU YA JUU

***Jimbo la Afrika***

Chuo Kikuu cha Mnazareti cha Afrika
Nairobi, Kenya-Kikihudumia Afrika Mashariki
Chuo cha Biblia cha Mnazareti cha Afrika Mashariki
Nairobi, Kenya-Kikihudumia eneo la Afrika Mashariki

Chuo cha Thiolojia cha Mnazareti
    Honeydew, Afrika Kusini-Kikihudumia eneo la Kusini mwa Afrika
Chuo cha Thiolojia cha Mnazareti cha Afrika ya Kati
    Malawi, Afrika ya Kati-Kikihudumia eneo la Kusini-Mashariki
Taasisi ya Thiolojia ya Mnazareti
    Ikihudumia maeneo ya vya Kati na Magharibi
Seminario Nazareno em Mozambique
    Maputo, Mozambique-Ikihudumia maeneo ya Lusophone
Chuo Kikuu cha Mnazareti cha Kusini mwa Afrika
    Manzini, Swazilanda-Kikihudumia Kusini mwa Afrika

***Jimbo la Asia-Pacific***

Seminari ya Thiolojia ya Mnazareti Asia-Pacific
    Rizal, Philippines
Chuo cha Thiolojia cha Mnazareti Indonesia
    Yogyakarta, Indonesia
Seminari ya Thiolojia ya Mnazareti Japan
    Tokyo, Japan
Chuo Kikuu cha Mnazareti cha Korea
    Choong Nam, Korea
Chuo cha Biblia cha Mnazareti Melanesia
    Mount Hagen, papua New Guinea
Chuo cha Walimu cha Mnazareti Melanesia
    Mount Hagen, Papua New Guinea
Chuo cha Uuguzi cha Mnazareti
    Mount Hagen, Papua New Guinea
Chuo cha Thiolojia cha Mnazareti
    Thornlands, Queensland, Australia
Chuo cha Biblia cha Mnazareti Philippine
    Baguio City, Phillipines
Chuo cha Thiolojia cha Mnazareti cha Pacific Kusini
    Suva, Fiji
Chuo cha Biblia cha Mnazareti Kusini-Mashariki mwa Asia
    Bangkok, Thailand
Chuo cha Thiolojia cha Mnazareti Taiwan
    Peitou, Taiwan
Chuo cha Biblia cha Mnazareti Visayan
    Cebu City, Philippines

### *Jimbo la Eurasia*

Chuo cha Biblia cha Mnazareti cha Mediterranean Mashariki
Karak, Jordan-Kikihudumia Mediterranean Mashariki
Chuo cha Mnazareti cha Uropa
Kikihudumia maeneo ya Uropa na Eurasia
Chuo cha Mafundisho ya Wauguzi cha Mnazareti
Washim, Maharashtra, India
Chuo cha Thiolojia cha Mnazareti-Manchester
Manchester, England
Chuo cha Biblia cha Mnazareti Asia Kusini
Bangalore, India-Kikihudumia India na Asia Kusini

### *Jimbo la Mesoamerika*

Chuo cha Mnazareti cha Caribbean
Santa Cruz, Trinidad-Kikihudumia English, Dutch na French Antilles
Instituto Biblico Nazareno
Coban, Alta Verapaz, Guatemala-Kikihudumia Magharibi mwa Guatemala
Seminaire Theologique Nazareen d'Haiti
Petion-Vile, Haiti-Kikihudumia nchi ya Haiti
Seminario Nazareno de las Americas
San Jose, Costa Rica-Kikihudumia Latin Amerika na eneo la Kati
Seminario Nazareno Dominicano
Santo Domingo, Serikali ya Dominican-Ikihudumia Serikali ya nchi ya Dominican
Semianario Nazareno Mexicano
Mexico City D.F, Mexico-Ikihudumia maeneo yaMagharibi na Kusini ya Mexico
Seminario Teologico Nazareno Cubano
La Lisa, La Habana, Cuba-Ikihudumia nchi ya Cuba

### *Jimbo la Amerika ya Kusini*

Faculdade Nazarena do Brasil
Sao Paulo, Brazil-Ikihudumia nchi ya Brazil
Seminario Biblico Nazareno Chile
Santiago, Chile-Ikihudumia nchi ya Chile
Seminario Nazareno Boliviano
La Paz, Bolivia-Ikihudumia chini ya Bolivya
Seminario Teologico Nazareno del Cono Sur
Buenos Aires, Argentina-Ikihudumia eneo la cha Cone Kusini
Seminario Teologico Nazareno de Peru

Chiclayo, Peru-Ikihudumia nchi ya Peru
Seminario Teologico Nazareno do Brasil
Sao Paulo, Brazil-Ikihudumia nchi ya Brazil
Seminario Teologico Nazareno Sudemericano
Quto, Ecuador-Ikihudumia Kiwanda cha Andean Magharibi

***Jimbo la Marekani/Canada***

Chuo Kikuu cha Ambrose
Calgary, alberta, Canada
Chuo cha Mnazareti cha Mashariki
Quincy, Massachusetts, Marekani
Chuo Kikuu cha Mnazareti cha MidAmerica
Olathe, Kansas, Marekani
Chuo Kikuu cha Mnazareti cha Mount Vernon
Mount Vernon, Ohio, USA
Chuo cha Biblia cha Mnazareti
Lenexa, Kansas, USA
Seminari ya Thiolojia ya Mnazareti
Kansas city, Missouri, USA
Chuo Kikuu cha Mnazareti cha Kaskazini-Magharibi
Nampa, Idaho, USA Olive
Chuo Kikuu cha Mnazareti cha Olivet
Bourbonnais, Illinois, USA
Chuo Kikuu cha Mnazareti cha Point Loma
San Diego, California, USA
Chuo Kikuu cha Mnazareti mwa Kusini
Bethani, Oklahoma, USD
Chuo Kikuu cha Mnazareti Trevecca
Nashville, Tennessee, USA

## III. MAELEKEZO YA USIMAMIZI

**906. Ruzuku.** Halmashauri Kuu na mashirika ya kanisa yamekatazwa kutumia pesa zinazolipwa kila mwaka kama ruzuku hadi ruzuku hizo zitakapokuwa mali yao halali kisheria baada ya kifo cha aliyetoa ruzuku hizo. Ruzuku za namna hiyo zitawekwa akiba kwa makini katika hazina au raslimali yenye faida ambayo inakubaliwa kama hazina ya udhamini na mahakama za nchi. (2017)

**907. Deni**. Hakuna shirika ambalo linaweza kukubaliwa kuwa na deni kwa kuweka ahadi ya kulipa.

**908. Vyama vya Biblia.**

**1. Vyama vya Biblia Vilivyoidhinishwa**. Kanisa la Mnazareti linaweka mkazo maalum katika Biblia kama ufunuo ulioandikwa wa Mungu, na tunaamini kwamba ndiyo njia yenye uwezo wa kuleta wafuasi wapya kwa Yesu Kristo, na kwa sababu kuna haja inayoongozeka ya nakala zaidi za Maandiko; kwa hivyo Inaazimiwa,

Kwanza, Kwamba Kikao Kikuu kinaeleza kuridhishwa kwake kwa dhati na kinashiriki katika maono ya kazi ya Muungano wa Vyama vya Biblia kote ulimwenguni.

Pili, Kwamba tunakubali kuadhimishwa kwa siku ya Jumapili ya Biblia Duniani, na kuelekeza mawazo katika siku hii kuwa sehemu muhimu ambayo maandiko matakatifu huwa nayo katika maisha ya wale walio Wakristo.

**2. Matoleo Kwa Vyama vya Biblia**

*Imeazimiwa,* Kwamba Kanisa la Mnazareti litenge Jumapili ya pili ya Desemba kila mwaka kuwa siku muhimu ya kutoa sadaka kwa Chama cha Biblia cha kila taifa. Chama cha Biblia kilichochaguliwa kitakuwa washirika (washiriki au kamili), wa ushirika wa ulimwengu wote wa Chama cha Biblia cha Umoja au pasipokuwepo mshirika wa chama, Chama kingine cha Biblia kilichotengwa na wilaya; pia kwamba juhudi maalum zitafanywa kuhakikisha kwamba makanisa yetu yote yanashiriki katika utoaji kama huo wa sadaka. Makanisa yote yanapaswa kushauriana na ofisi ya wilaya kwa maagizo kuhusu namna ya kutuma mchango wao kwa Chama cha Biblia cha nchi yao kinachohusika. (2017)

**909. Azimio la Kuhariri Kitabu cha Mwongozo.** Na iwe imeazimiwa, Kwamba Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu iteuwe na kuruhusu Kamati ya Uhariri wa *Kitabu cha Mwongozo* kupatanisha taarifa zinazohitajika ambazo zinaweza kutokea katika kumbukumbu za maazimio ya Kikao Kikuu cha 29 kuhusiana na mabadiliko katika Manual; na pia kufanya mabadiliko ya kiuhariri katika toleo la sasa la *Kitabu cha Mwongozo* kwa njia ambayo itasahihisha lugha bila kubadilisha maana; na pia kufanya mabadiliko ya kiuhariri katika nakala ya jambo lililokubaliwa hivi karibuni kama itakavyohitajika katika kusahihisha lugha bila kubadilisha maana.

Pia imeazimiwa kwamba usimamizi wa tafsiri zote za  utakuwa ni wajibu wa kamati ya Uhariri wa *Kitabu cha Mwongozo* (2017)

**910. Marudio ya Nyongeza ya Kitabu cha Mwongozo**. Kitu chochote kilichobaki katika Sehemu za 3 na ya 4 za Nyongeza (vifungu vya 906-933) kwa muda wa miaka 12 bila kufikiriwa upya kitapelekwa  na Kamati ya Marejeo kwa kamati inayohusika ya Kikao Kikuu kwa kufikiria kama azimio kwa Kikao Kikuu. (2013)

**911. Muda wa Kamati**. Kamati yoyote maalum iliyoundwa kwa kusudi lolote, isipokuwa iwe imeelezwa vingine, itakoma kuwepo wakati wa Kikao Kikuu. (2017)

**912. Shughuli za Kikao Kikuu**
(Kutoka katika Sheria za Utaratibu za Kikao Kikuu cha mwaka 2017)

## MAAZIMIO NA MAOMBI

**Sheria ya 14. Kuwasilisha Maazimio kwa Kikao Kikuu**. Vikao vya wilaya, kamati iliyopewa mamlaka na kikao cha wilaya, mabaraza ya jimbo, Halmashauri Kuu au idara zozote zinazotambuliwa, halmashauri au tume rasmi za kanisa lote, au Mkutano wa Misheni ya Mnazareti ya Kimataifa Ulimwenguni, Mkutano wa Huduma ya Vijana wa Mnazareti ya Kimataifa Ulimwenguni, washirika watano wa Kikao Kikuu, wanaweza kuwasilisha maazimio na maombi ili yafikiriwe na Kikao Kikuu kulingana na kanuni zifuatazo:

*a.* Maazimio na maombi yatachapishwa au kuandikwa kupitia mashine kwenye fomu rasmi iliyotolewa na katibu mkuu.
*b.* Kila azimio au ombi lililowasilishwa litapaswa kuwa na kiini pamoja na jina la wajumbe au kundi ambalo linawasilisha jambo hilo.
*c.* Mazimio yote ambayo yanahitajika hatua ambazo zinahitaji matumizi lazima yajumulishe kiwango cha gharama ya kukamilisha hatua.
*d.* Mapendekezo ya mabadiliko katika Kitabu cha Mwongozo ya kanisa lazima yawasilishwe kwa maandishi na yataonyesha kifungu na sehemu ya Manual itakayohusika na mabadiliko yanayotakiwa, ikiwa yatakubaliwa.
*e.* Maazimio au maombi hayo yatawasilishwa kwa katibu mkuu **kufikia tarehe moja mwezi wa Desemba** kabla ya kukutana kwa kikao ili yawekwe nambari na kutumwa kwa Kamati ya Marejeo kwa maelekezo kulingana na Kanuni ya 24 na Kitabu cha Mwongozo 305.1.
*f.* Maazimio yoyote ambayo si vifaa vya Manual lazima yaelezwe ni taasisi gani inayowajibika utunzaji sheria.

